# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## KIMEANDIKWA NA SHEIKH JA'FAR SUBHANI

### KIMETAFSIRIWA NA MUSABBAH SHAABANI MAPINDA

**KIMETOLEWA NA AHLUL BAYT ASSEMBLY OF TANZANIA**
Dar es Salaam - Tanzania

### MUHTASARI

Afrika ya Mashariki imefaidi mazingira ya amani sana kiasi cha karne mbili zilizopita. Watu wa imani na itikadi zote waliishi pamoja kwa upendo na mapenzi. Kila mmoja akishiriki kwenye shughuli za mwenzake za kijamii na za Kidini. Ukiangalia kwenye Jumuiya za Kiislamu, wote wakihudhuria kwenye Misikiti ya kila mmoja, waliungana pamoja katika Maulidi na hafla za Muharram, na kupanua ushirikiano wao katika miradi ya kila mmoja. Kama Rais Mstaafu Alhaji Ali Hassan Mwinyi alivyosema katika hotuba moja ya hadhara; "Misikiti mingi ya Waislamu wa (Madhehebu ya) Shafi'i iliyoko Zanzibar na Pemba ilijengwa na kutolewa na Shia Ithna-ashariyya" Hatimaye Wahhabi walianza Tabligh (Mahubiri) yao hapa. Badala ya kujaribu kuwaleta mapagani au wasio waislamu kwenye boma ya Uislamu, nia yao kabisa ilikuwa na bado inakaziwa katika kuwabadilisha Mashafii wawe Mawahabi. Kwa lengo hili, hujifanya kama wao ni Masunni, na kuchanganyika pamoja na Masunni. Mawahabi hao wamepanda mbegu ya fitina na chuki kati ya Madhehebu mbali mbali za Kiislamu, na hususan kati ya Sunni na Shia. Wanazungumza dhidi ya Shia, na kusambaza vitabu na vijitabu (vya mambo ya dini) dhidi ya itikadi ya Shia ambavyo vimejaa mambo ya uwongo na uzushi. Kishawishi chao kiko wazi, kwa kuwatenganisha Masunni na Mashia, wakitumaini kupata urahisi wa kuingia katika jamii ya Sunni na Misikiti yao, ingawaje tumaini hili lingali bado kukamilishwa katika Tanzania.

Hebu tuangalie katika mzizi wa uovu wa kampeni hii. Huenda hapo nyuma katika mwaka 1979, ambapo Mapinduzi ya Ki-Islamu yalipotokea katika nchi ya Iran, na watawala wa Kiwahaabi wa Saudia walihadharishwa vikali mno, hata kabla ya tukio la Mapinduzi ya Kiislamu, wakati Ayatullah al-'uzma al-Khomeini (r.a.) akiwa bado Najaf (Iraq). Waziri wa mambo ya nchi za nje wa Saudi Arabia, akizungumza katika hadhara moja ya Waarabu, aliuonya ulimwengu wa Waarabu kwamba kama Khomeini ataruhusiwa kuendeleza harakati zake kutoka Iraq kama hapo nyuma, sio tu kwamba utawala wa Shaha utaangushwa, lakini, hali katika eneo lote vile vile itakuwa imetibuliwa. Hivyo wakaishinikiza Iraq kuweka vikwazo juu ya Khomeini kwa hofu ya kwamba, kama juhudi zake zitafanikiwa katika Iran, zitatingisha tawala zao wenyewe zisizo imara. Haikushangaza kwamba mara tu Mapinduzi ya Kiislamu yalipoimarika nchini Iran, hawa Wahhabi wakuanza propoganda kali yenye chuki dhidi ya Khomeini, dhidi ya Iran na dhidi ya Ushia. Kalamu za kukodisha zikuanza mchakato kutoa vitabu, makala na vijitabu (vya mambo ya dini) dhidi ya Shia. Shia waliitwa Makafiri, na pengine mtu angeuliza: Kama ni Makafiri, basi kwa nini wanapewa viza kwa ajili ya Hija na Umra? Wairani waliitwa Majus (Waabudu Moto) kwa nini? Kwa sababu kabla ya kuja kwa Uislamu

waliabudu moto. Kwa hoja hii nasi hatuna haki ya kuwaita Wahhabi Mushrikuna? Kwa sababu kabla ya kuja kwa Uislamu wata wa Najd walikuwa wakiabudu Masanamu.

Baadhi ya waajiriwa wao wa ngazi za juu walikuwa ni (marehemu) Ihsan Ilahi Zaheer wa Pakistan, na Manzoor Ahmad Nu'mani na Abul Hasan Ali Nadwi wa India. Sauti itokayo kwenye vinywa vyao ni katika watakiwayo na mabwana zao kuyasema, na jambia la uzayuni lilichovywa kwenye damu ya waislamu linatumika kama kalamu yao. Kitabu kinachoandikwa dhidi ya Shia na watumwa hawa, kwa miezi michache tu kinatarujumiwa katika lugha zote kubwa za ulimwengu wa Kiislamu; na hufanywa kipatikane kila mahali, kadhalika husambazwa bure miongoni mwa Mahujaji: Nimeandika majibu kwa kitabu kimoja kama hicho, ambacho kilichapishwa katika mwaka 1994 nchini Tanzania na Marekani kwa jina la "Wahhabi's Fitna Exposed". Kimevunja habari za uwongo wao wote na masingizio yasiyo na msingi dhidi ya Shia. Tarjuma yake ya Kiswahili (Fitina za Wahhabi Zafichuliwa) imechapishwa na Bilal Muslim Mission of Tanzania, Dar es Salaam.

Bado inahisiwa haja ya kuweko kitabu katika sehemu hizi za ulimwengu ambacho kitaangalia katika mawazo yote na mafundisho ya Uwahhabi na kushughulika nayo katika mwanga wa Qur'an na Hadithi, ili kufichua uwongo na itikadi yao na mtizamo wao juu ya vita vitakatifu vya Kiislamu. Ahlul-Bayt (a.s) Assembly of Tanzania, ina furaha kutoa kitabu kama hiki kwa wata wazungumzao Kiswahili. Nimechagua kwa ajili ya madhumuni haya kitabu (kitwacho) "Al-Wahhabiyah Fil-Mizan" kilichoandikwa na Mwanachuoni mashuhuri wa dini na mtunzi, aitwaye Shaykh Ja'far Subhani, Profesa wa Chuo cha dini Qum (Iran). Kitabu hiki kwa hakika (bila kupendelea) kinaangalia katika hoja zote zilizotolewa na Wahhabi na kutahini kusihi kwake kutoka kwenye Qur'an na Sunnah.

Shaykh Musabbah Shaabani Mapinda, wa Dar-es-Salaam kwa ushauri wangu amefanya tarjuma ya kitabu hiki kutoka Kiarabu kwenda kwenye Kiswahili, kinachoitwa "Uchunguzi juu ya Uwahhabi". Nimekikagua kwa utaratibu ili kuhakikisha kwamba mafuhumu ya Kiarabu kwa uaminifu na ukweli yametolewa kwenda kwenye Kiswahili. Hiki ni kitabu cha kwanza cha "Ahlul-Bayt (a.s) Assembly of Tanzania", na nina fahari kwa kushirikishwa katika kila hatua. Namuomba Allah Subhanahu Wa Ta'ala atoe malipo yake kwa Mtunzi, mtarjumi na wale wote ambao wamesaidia katika kuchapishwa kwake kwa njia yoyote ile. Wa Ma Tawfeeq Illa Billah

Syed Saeed Akhtar Rizvi
Mwenyekiti,
Ahlul-Bayt (A.S.) Assembly
P.O. Box 75215,
Dar- es- Salaam, Tanzania

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## UTANGULIZI WA CHAPA YA KWANZA

### KUHUSU MAWAHABI NA ITIKADI ZAO

Shukurani zote Anastahiki Mwenyezi Mungu ambaye ni Mtangu na hapana kitu kilichokuwepo kabla yake, naye ndiye wa mwisho hapana baada yake chochote. Na yeye ni dhahiri hapana kilicho dhahiri kuliko yeye, naye ni batin hapana kilicho Batin kuliko yeye. Na Sala na Salamu zimshukie Mtume wake na mbora wa viumbe wake ambaye alimtuma katika kipindi ambacho watu walikuwa ndani ya upotevu wakihangaika na wamezama ndani ya Fitna, na wametekwa na matamanio yao na wamepotoshwa na ujeuri na akili zao zimepotoshwa na Ujahili uliopita kiasi, wakihangaika katika mambo yaliyovurugika na balaa linalotokana na ujinga, basi Mtume **[s.a.w.w]** akatoa nasaha kwa upeo, akaitengeneza njia na akalingania kwa hekima na mawaidha mazuri.

Mwenyezi Mungu alimtuma kuitimiza ahadi yake na kukamilisha Utume wake. Alichukua ahadi yake toka kwa Manabii na alama zilikuwa Mashuhuri na mazazi yake yalikuwa matukufu hali ya kuwa walimwengu katika zama hizo wakiwa na mila tofauti tofauti, na fikra mbali mbali na ni vikundi vingi wakiwemo wanaomshabihisha Mwenyezi Mungu kwa viumbe wake au walikuwa wakifanya kufuru na shiriki katika jina lake au wakimuabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu. Basi Mwenyezi Mungu akawaongoa kupitia kwa Mtume **[s.a.w.w]** kutoka kwenye upotovu na akawaokoa kutokana na ujinga kwa njia yake na ni nguzo ya dini yake. Na Rehma za (Mwenyezi Mungu) zimshukie Mtume na kizazi chake (watu) ambao ndiyo wa ndani wake na ni tegemeo la dini yake na ni chombo cha elimu yake, na ni rejea ya hekima zake na ni hazina ya vitabu vyake.

Kwao wao Mwenyezi Mungu aliimarisha dini yake, na ni watu ambao Mwenyezi Mungu amewaondoshea uchafu na kuwatakasa mno. Na (Pia) ziwashukie Masahaba wake ambao waliisoma Qur'an na wakazitumia hukmu zake na wakazizingatia faradhi kisha wakazisimamisha. Waliihuyisha Sunna na kuuwa Bid'a, walilinganiwa kwenye jihadi wakaitika, na walimuamini kiongozi wao (ambaye ni Mtume **[s.a.w.w]**, kisha wakamfuata. Wamekutana na Mwenyezi Mungu na akawalipa ujira wao, na amewapa makazi ya amani baada ya khofu waliyokuwa nayo, waliendelea katika njia ya Dini na wakaifuata haki, Rehma ziwashukie daima milele muda wote wa kudumu mbingu na ardhi. Amma baad, bila shaka umma wa Kiislamu tangu mwanzoni umeshikamana juu ya Tauhudi katika nyanja zake mbali mbali, ukaafikiana juu ya kuipwekesha dhati ya Mwenyezi Mungu na kwamba, yeye ni mmoja hana mshirika wake na ni mpweke hana mfano. Kama ambavyo umeafikiana ya kwamba, yeye ni uumba na hapana muumba asiyekuwa yeye. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Je, kuna muumba asiyekuwa Mwenyezi Mungu" Qur'an, 35:3.

Na Amesema tena: "Waambie, Mwenyezi Mungu ndiye muumba wa kila kitu" Qur'an, 13:16.

Vile vile umekubaliana juu ya Tauhidi yake katika Rububiya yake na kwamba hapana Mola wala mwenye kusimamiya (mambo yao) asiyekuwa yeye. Amesema Mwenyezi Mungu: Yeye ndiye anayesimamia mambo yote

hakuna muombezi ila baada ya idnini yake, huyo ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu basi muabuduni yeye, Je, hamna kumbukumbu? Pia wamekubaliana kempwekesha Mwenyezi Mungu katika Ibada na kwamba, yeye Mwenyezi Mungu ndiye Mola ambaye anastahiki kuabudiwa na hukuna wa kuabudiwa asiyekuwa Yeye. Mwenyezi Mungu Amesema:

قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْا إِلَىٰ كَلِمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَّا نَعْبُدَ إِلَّا اللَّـهَ وَلَا نُ شْرِكَ بِهِ شَيْئًا
وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّـهِ فَإِن تَوَلَّوْا فَقُولُوا اشْهَدُوا بِأَنَّا مُسْلِمُونَ ﴿٦٤﴾

"Waambie, Enyi mliopewa Kitabu, njooni kwenye neno lililo sawa kati yetu na ninyi ya kwamba, tusimuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu, na wala tusimshirikishe na chochote, wala baadhi yeta tusiwafanye kuwa waungu badala ya Mwenyezi Mungu". Qur 'an, 3:64.

Bali hizi ndizo nukta ambazo zenye kuafikiana baina ya sheria zote za mbinguni, na yote haya yanaonekana kuwa ni miongoni mwa mambo ya kipekee kwa baadhi ya wafuasi wa sheria zilizopita. Basi mtazamo uliyo kinyume na misingi hii ni miongoni mwa vitendo vya uchafuzi na kupotosha vinavyotokana na wanachuoni, Watawa na Makasisi (wao).

## MAWAHABI NA MSIMAMO WAO KWA UNDANI KATIKA QADHIYYAH ZA TAUHID

Cha ajabu, (na midhali uhai utona maajabu zaidi) in kwamba, Uwahabi unatokana na fikia ya Sheikh mpotofu aitwaye Ibn Taimiyyah ambaye ametuarifisha maana ya Tauhidi katika kitabu chake aliposema: "Hakika Mwenyezi Mungu yuko juu ya mbingu yake kwenye arshi yake, yuko juu ya viumbe wake".[1] Na amesema tena: "Mola wete hushuka mpaka kwenye mbingu ya dunia kila siku inapobakia theluthi ya mwisho ya usiku kisha husema; Nani ataniomba (saa hizi) nami nitamkubalia (maombi yake) nani ataniomba nami nitampa, ni nani atanitaka msamaha nami nitamsamehe".[2] Haya ndiyo maarifa ya mtu huyo (Ibn Taimiyyah) na huku ndiko kumtakasa kwake Mwenyezi Mungu Mtukufu na (yote haya aliyoyasema) inajulisha wazi kabisa kuwa yeye anaitakidi kuwa Mwenyezi Mungu anao mwili na anapatikana upande fulani. Na (huyu Ibn Taimiyyah) amesema hayo kutokana na kung'ang'ania kwake dhahiri ya aya na hadithi za Mtume bila ya kuzitafiti kwa undani aya zilizokuja kuhusu maudhui hiyo, na bila ya kufanya uhakiki katika isnadi za hadithi na madhumuni yake.

Basi iwapo haya ndiyo maoni ya mwalimu (wa Mawahabi) basi itakuwaje hali ya watu wanaoramba vikombe vyake na wanakaa katika meza zake kama kina Ibn Al-Qayyim na Muhammad bin Abdul-Wahhab. Na cha ajabu ni kwamba, hawa nao wanataka wawe ni waalimu wa Tauhidi na walinganiaji wa Tauhid. Na Mwenyezi Mungu amrehemu mshairi aliyesema: "Katika maajabu ya duniani ni kwamba, mwenye ugonjwa wa manjano anadai kuwa ni mganga na mwenye macho mabovu awe mwenye kutengeneza dawa ya macho na kipofu awe mnajimu, na msomaji wetu wa Qur'an awe Mturuki na Khatibu wetu awe Muhindi, basi njooni tulie na tupige vifuajuu ya Uislamu, (Tuulilie kwa msiba uliyoufika). Hii ndiyo itikadi ya jamaa hawa kuhusu Mwenyezi Mungu, basi iwapo tutataka

1. Maj-mu'a 'Tur-Rasailil-Kubra, cha Ibn Taimiyyah, Al-A'qidatul-Wasitiyah uk. 401.
2. Rejea iliyotangulia uk. 309.

kuzipima fikra hizi, basi tunawajibika kulinganisha kati ya maelezo hayo na yale yaliyopokelewa kutoka kwa Maimamu wa nyumba ya Mtume **[s.a.w.w]** kuhusu makusudio hayo (ya Tauhid), kisha tuone ni lipi kati ya makundi haya mawili lenye haki ya kufuatwa.

Je, ni yule amsifuye Mwenyezi Mungu kwamba, yeye ana mwili na anakaa upande fulani na kuteremka mpaka mbingu ya dunia, (ndiye wa kufuatwa) au yule amsifuye Mwenyezi Mungu kwa kusema: "Shukurani zote anastahiki Mwenyezi Mungu ambaye hawafikii kikamilifu sifa zake wenye kuzisema, wala hawazidhibiti neema zake wenye kuhesabu, na wala hawatekelezi ipasavyo haki yake wenye kujitahidi, Mwenyezi Mungu ambaye fikra hazimfikii hate ziende umbali kiasi gani, wala akili hazimfikii japo ziende ndani kiasi gani, ambaye sifa zake hazina mpaka, wala hakuna maneno yatakayoeleza sifa zake kikamilifu. Na yeye hana wakati uliohesabiwa wala muda uliopangwa, mwenye kumsifu Mwenyezi Mungu kwa mujibu wa fikra zake atakuwa kamfanyia mwenza, na mwenye kumfanyia mwenza atakuwa kanifanya wawili na mwenye kumfanya wawili basi atakuwa kamgawa. Na mwenye kumgawa hakumjua, na asiyemjua atamuashiria na mwenye kumuashiria atakuwa kamuwekea mipaka, na mwenye kumuwekea mipaka atakuwa kamfanya kuwa zaidi ya mmoja, na atakayeuliza yuko katika kitu gani, basi yeye atakuwa kamuweka ndani ya kitu, na atakayemuuliza kuwa yuko juu ya kitu gani, basi yeye atapafanya mahala pengine pote kuwa Mwenyezi Mungu hayupo. Yeye yupo lakini si kwamba hapo kabla hakuwepo. Yupo pamoja na kila kitu, lakini si kwa kuambatana naye yu mbali na kila kitu lakini si kwa kuondoka.[1]

(Ndugu msomaji), utakapolinganisha yale yaliyonakiliwa kutoka kwa As-Habul-Hadithi kuhusu Tauhidi ya Mwenyezi Mungu na kumtakasa kwake utastaajabu, kwani Imam Al-Ash-Ari amenakili toka kwao kwamba, maana ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika kuomba ni kuwa: Maovu ya waja anayaumba Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuwa matendo ya waja anayeyaumba ni Mwenyezi Mungu na waja hawawezi kufanya chochote.[2] Bila shaka ibn Taimiyyah na wale walioko kama yeye wanajisifu wenyewe kuwa ni Ahlul-hadithi na wanaitafsiri Tauhidi inayohusu kuumba kwa maana hii. Basi Je, baada ya hali hii itawezekanaje kwao (kina ibn Taimiyyah) kumtakasa Mwenyezi Mungu kutokana na dhulma na ujeuri na kuvuka mipaka. Basi iwapo Mwenyezi Mungu ndiye anayeumba maovu ya waja, na waja hao wakawa hawana walichokifanya katika maovu hayo, si kwa uwezo wao wala kwa kuiga basi ni kwa nini Mwenyezi Mungu awaadhibu? Je, hali hii siyo miongoni mwa kauli za msemaji fulani aliposema: "Amefanya makosa mwingine nami ninaadhbiwa."

Nawe unatambua kwamba Tauhid inayohusu kuumba haimaanishi kama walivyoileza Ahlul-Hadithi, na kabla na baada yao (waliyasema kama hayo) Jabriyyah na ibn Taimiyyah na wafuasi wake. Bali maana yake ni kwamba: Muumba mwenye kujitosheleza na mtendaji asiyehitaji kitu chochote ni yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu. Lakini wako watendaji wanaotenda kwa idhini yake na wanaumba kwa amri yake na husimama na kukaa kwa uwezo

1. Nahjul-Balagha Khutba ya Kwanza.
2. Maqa'latul-Islamiyyin uk. 321.

wake na nguvu zake, hivyo basi mtu analo jukumu lake kutokana na matendo yake na kazi zake: "Kila nafsi itafungika kwa yale iliyoyatenda". Qur'an, 74:38.

## WANACHUONI WA KIWAHABI WANAJIPENDEKEZA KWA WATAWALA

Tunaona kwamba wanachuoni wa Kiwahabi nchini Saudia na sehemu zingine wanajipendekeza kwa watawala na Makhalifa wajeuri, wanajaribu kuyatakasa matendo ya dhulma ya watawala hao na msimamo wao wakijeuri, na wanajitahidi kutoa kibali cha kisheria kwa kila kinachotokana na watawala wao na wenye mamlaka juu yao (mtawala huyo) awe mwema au muovu. Na hilo siyo jambo la ajabu (kwao) kwani wao (Mawahabi) ndiyo wanaoona kuwa kusali nyuma ya kila Imam mwema au muovu sala inasihi, na kuwaombea wema viongozi wa Waislamu ni faradhi, na kuwapinga wanapopotoka ni haramu.[1] Wanaichukuliaje kauli ya Mtume wa Mwenyezi Mungu [s.w.t] kama alivyoinakili toka kwake mjukuu wake Husein bin Ali [a.s] "Abu-Shuhadaa" pale aliposema: "Enyi watu, hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu [s.w.t] amesema; mtu yeyote atakayemuona mtawala muovu anayehalalisha haramu ya Mwenyezi Mungu, mwenye kutengua ahadi ya Mwenyezi Mungu, mwenye kwenda kinyume cha Sunna ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, anawatendea uovu na uadui waja wa Mwenyezi Mungu, kisha mtu huyo akaacha kumkataza kwa kitendo au kauli, basi Mwenyezi Mungu atakuwa na haki ya kumuingiza motoni mtu huyo." [2][6] Hebu niambie kweli, ni ipi baina ya kauli mbili na ni ipi baina ya njia mbili inayotokana na Uislamu halisi na inaonyesha picha ya nadharia ya Uislamu halisi?

Mwenyezi Mungu amesema: "Wala msiwategemee (mkawa pamoja nao) wale wanaodhulumu usije kukupateni moto." Qur'an, 11:113.

## MAPINDUZI YA KIISLAMU NA HUJUMA ZA KIWAHABI

Kwa hakika Mapinduzi ya Kiislamu nchini Iran yameleta mshituko mkubwa katika ghuba, na kuzisononesha tawala zote zilizoko sehemu hiyo na hasa hasa zile zinazohusiana na mataifa makubwa na kuyategemea kwa kila hali, na kwa upande mwingine madola hayo ya kikoloni yanazitegemea nchi hizo na miongoni mwa tawala hizi ni ule utawala wa Kiwahabi unaotawala nchi kubwa miongoni mwa nchi za Kiislamu, nchi ambayo inasifika kwa utajiri mkubwa wa asili na inufaika kwa hali maalum ya kijiografia. Basi ukoloni mbaya na vibaraka wake na watendaji wake wakiongozwa na waliaganiaji wa Kiwahabi wamekusudia kupinga mapinduzi ya Kiislamu na kimbunga chake kwa njia mbali mbali, miongoni mwa upinzani huo ni kuzusha wasi wasi ndani yake na kuwasha mioto ya vita dhidi yake na kulazimisha vikwazo vya kiuchumi dhidi ya mapinduzi hayo. Na njama zote hizi za upinzani dhidi ya mapinduzi ziliposhindwa, wakakusudia kuleta picha mbaya ya utamaduni wa mapinduzi an kuondosha Mafhumu yake na kuuzushia uongo na kuupakazia uzushi ili kuwazuia watu

1. Maqa'latul-Islamiyyin uk 322 (na hii ni Itikadi ya As-habul-hadith na ibn Taiymiyyah na wafuasi wake katika kundi hili.)
2. Tarikh at-Tabari Juz. 4 Uk. 304 (matukio ya mwaka wa sitini na moja).

kufuata muongozo wake na kumfuata kiongozi wa mapinduzi hayo. Kwa hakika njama hii ya kiadui dhidi ya utamaduni wa mapinduzi ya Kiislamu, inabainika katika mambo yafuatayo:

1. Kueneza matangazo na magazeti aina nyingi katika nchi mbali mbali za ulimwengu ili kuzungumzia dhidi ya mapinduzi na kufanya ushawishi dhidi yake na kuonyesha sura mbaya ya utamaduni wake halisi.

2. Kuchapisha vijitabu na vitabu vingi mno kuhusu utamaduni huo kwa kupitia mikono ya watu na waandishi ambao wameuza nafsi zao na hawajali isipokuwa mlo wao na pengine vyeo vyao vya kidunia, wakiongozwa na yule muongo mkubwa ih-Sa'an ilahi dhahiri[1] ambaye ni miongoni mwa watu wanaopata mali nyingi kutoka Saudia. Mtu huyu amesimama kidete kwa nguvu zake zote na kwa kila kile ambacho Suudia inakitoa ili kutoa picha mbaya ya taaluma ya mapinduzi miongoni mwa Waislamu.

Na huyu Bwana ni masikini kwa kila kitu hata katika madai yake kuwa anayafahamu madhhebu ya Shia Imamiyyah, basi anachanganya na kuvuruga na wala hapambanui baina ya Asili na Far-i. Wala baina ya Aqida na Riwaya, na anatoa ushahidi kwa kutumia riwaya kuwa eti ndiyo madhhebu ya Shia (yalivyo). Yapo mengi zaidi ya hayo, katika uongo wake na uzushi wake na natija mbovu atoazo, hivyo basi sisi tutahusika naye mahala pengine ndani ya kitabu pekee.

3. Kuyaeneza Madhhebu ya Kiwahabi miongoni mwa vijana katika Eneo hilo kwa njia mbali mbali huku wakibainisha wazi kuwa Mawahabi ndiyo Waislamu na kwamba wao ndiyo wanaompwekesha Mwenyezi Mungu na ndiyo wanaoitumia Qur'an na sunna kwa usahihi, na wasiyokuwa wao wako mbali mno na hayo. Basi kwa ajili hiyo tumeweka risala hiyo kuyabainisha madhhebu ya Kiwahabi, na kuweka bayana ndani yake upeo wa yale wayasemayo Mawahabi na upeo wa kuwa kwao mbali na Qur'an na Sunna na sera ya Waislamu.

Mwisho, tunatoa ushauri kwa wanachuoni wa Kiislamu walioko ulimwenguni kwanza, na pili kwa waandishi wa Kiwahabi, wasimamie kuitisha mkutano wa Ulimwengu wa Kiislamu, mkutano ambao utawakusanya wanachuoni wa Kiislamu kutoka vikundi vyote vya Kiislamu ili kuyachambua Mas-ala haya kwa mujibu wa Qur'an na Sunna na kuyasambaza matokeo ya mkutano huo kwa Waislamu wote ili haki iwabainikie kwa uwazi na ifuatwe, na iliyo haki ndiyo yenye haki mno kufuatwa, na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuwafikisha na ndiye msaidizi. Jaafar Subhani

Qum Takatifu

1/Mfunguo Tano/1405

1. Sasa hivi ni marehemu.

1

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## UTANGULIZI WA CHAPA YA PILl

### HAJA YA KUWEKO MKUTANO WA KIISLAMU WA ULIMWENGU ILI KUIDURUSU TAUHIDI NA SHIRKI

Bila shaka Al-Kaaba ndiyo nyumba ya mwanzo iliyojengwa kwa ajili ya ibada ya Mwenyezi Mungu na humo apwekeshwe yeye Mwenyezi Mungu, na kwa hakika misingi yake ilidhoofika kabla ya zama za Nabii Nuh [a.s], na kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu inatueleza juu ya jambo hilo.

إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِي بِبَكَّةَ مُبَارَكًا وَهُدًى لِّلْعَالَمِينَ ﴿٩٦﴾

"Kwa yakini nyumba ya mwanzo iliyowekwa kwa ajili ya watu (kufanya Ibada) ni ile iliyoko katika jangwa takatifu (Makka) lenye kubarikiwa na muna uongofu kwa walimwengu." Qur'an, 3:96.

Na kwa kweli Al-Kaaba (baada ya kujengwa) ilichakaa kwa sababu ya tufani (zilizokuwa zikitokea), jambo ambalo lilipelekea kubomoka jengo lake na kuvunjika kuta zake, na alipokuja Nabii Ibrahim [a.s] akalijenga jengo lake kama anavyotufahamisha Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema:

وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْمَاعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا إِنَّكَ أَنتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٢٧﴾

Na kumbukeni Ibrahim na Ismail walipo inyanyua misingi ya ile Nyumba wakaomba: Ewe Mola Mlezi wetu! Tutakabalie! Hakika Wewe ndiye Msikizi Mjuzi." Qur'an, 2:127.

Na baada ya Ibrahim [a.s] kuisimamisha misingi yake na kuijenga AI-Kaaba alielekeza mwito maalum kwa amri ya Mwenyezi Mungu na Wahyi wake kwa kila mwenye kumpwekesha Mwenyezi Mungu ili aizuru nyumba hii na akahiji. Mwenvezi Mungu anasema: "Watangazie watu habari ya Hijja". Qur'an, 22:27.

Na Mwenyezi Mungu ameifanya nyumba yake hiyo tukufu, kuwa ni kituo cha mkusanyiko wa waumini na ni nyumba ya amani kwa wenye kumpwekesha, basi inapasa mtu yeyote asihisi hofu awapo hapo wala asiogope hatari yoyote wala dhulma, kama kauli ya Mwenyezi Mungu inavyojulisha.

وَإِذْ جَعَلْنَا الْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمْنًا ﴿١٢٥﴾

"Na kumbukeni tulipoifanya nyumba (AI-Kaaba) pawe ni mahala panapoendewa na watu na pawe pa amani". Qur 'an, 2:125. Pia 28:57.

Hiyo ni kwa kuwa Mwenyezi Mungu ameifanya ziyara ya kuzuru nyumba yake iwe ni dhamana ya kuendelea kwa maisha ya waumini, na imekuwa kusimamisha maadhimisho ya Hijja ni jambo linaloleta amani kwa maisha ya mtu mmoja mmoja na jamii, pia kwa maisha ya kimaada na ya kiroho kwa waumini. Mwenyezi Mungu ameifanya Al-Kaaba (ambayo ni) nyumba takatifu kuwa tengenezo la (maisha ya) watu. Qur'an, 5:97.

Kwa majibu wa aya hii Tukufu Imam As-Sadiq [a.s] anasema: "Dini itaendelea kuwa imara muda wote Al-Kaaba itapokuwa imesimama."[1] Kwa hakika ubora wa kuizuru nyumba Tukufu ya Mwenyezi Mungu ni mwingi mno kuliko tunavyoweza kuuzungumzia ndani ya utangulizi huu, lakini kitu tunachopenda kukiashiria ni yale mazingira iliyonayo Al-Kaaba leo hii, mazingira ambayo yameifanya iwe mikononi mwa watu ambao wao wanajiona kuwa ni watumishi wa miji miwili mitakatifu, na wanajifakharisha kwa jambo hilo. Nasi kufuatana na ubora ambao Mwenyezi Mungu ameihusisha nao Al-Kaaba, tunajiuliza mambo mawili muhimu.

Kwanza: Je, hivi leo hii maadhimisho ya hija yanazingatiwa kuwa ni tengenezo (litakalowarekebisha) watu sasa hivi? Je, kuizuru Al-Kaaba na kukusanyika pembezoni mwake Waislamu zaidi ya milioni mbili kumeleta amani kwenye maisha ya kimaada na ya kiroho kwa Waislamu na kuwadhaminia kuendelea kwa amani hiyo maishani mwao? Kama kweli ndivyo, basi hebu tuulizaneni, ni msimu upi miongoni mwa misimu ya hija za kila mwaka Makhatibu wa Makka na Madina walipata kuzungumzia masuala ya maisha ya Waislamu?

Na je, mambo ya Waislamu na matatizo yao yalipata kuwasilishwa katika uwanja wa majadiliano na kuyatafutia ufumbuzi katika mikusanyiko hii mikubwa? Basi ni lini watumishi hao wa Haramain (Makka na Madina) na Makhatibu wao walipata kuyasuluhisha mambo ya Waislama na matatizo yao? Na ili iwe kama mfano kuhusu mazingira ya kuhuzunisha ambayo Al-Kaaba inakabiliana nayo, ninaeleza kisa kifuatacho. Mwaka 1396 A.H. nilibahatika kuizuru nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu na nikafanya umra pamoja na kundi la watu waliohifadhi Qur'an, ili kushiriki mashindano ya kuhifadhi Qur'an. Na katika siko hizo (Tulipokuwa Makka) idhaa mbali mbali na vyombo vya habari vilikuwa vikitangaza uvamizi wa Israel huko kusini mwa Lebanon na vitendo vyake vya kishenzi ilivyokuwa ikivifanya dhidi ya Wapalestina na wengineo.

Na katika siku ya Ijumaa tulifika kwenye kituo cha kuhifadhisha Qur'an kilichopo ubavuni mwa msikiti mtukufu wa Makka, na baada ya kumalizika kikao cha mashindano ya Qur'an paliadhiniwa na hivyo wakati wa Sala ukawa umeingia, na Khatibu akapanda kwenye mimbari ili kutoa khutba. Mimi nilikuwa nikidhnai kwamba, Khutibu huyu huenda atahutubia kuhusu tukio lililotawala katika kipindi hicho (nalo ni lile la uvamizi kusini mwa Lebanon na wajibu wa Waislamu kusimama dhidi ya vita hivi vya Kizayoni vya kupanua mipaka yake) lakini mara dhana yangu nzuri ilibadilika na kuwa yakini mbaya, kwani Khatibu huyu alianza kuzungumzia unadhifu na namna ulivyosisitizwa na athari zake nzuri na (alizungumzia) adabu zinazohusu msikiti na Sala ya Ijumaa na mengine kama hayo na wala hakutamka japokuwa neno moja kuhusu tukio lilokuwepo katika kipindi hicho.

Kuna mtu fulani alikuwa amekaa pembeni yangu ambaye alikuwa Mmisri miongoni mwa "Ikh-Wanil-Muslimina" waliokimbia kutoka Misri na kwenda Hijaz, basi mimi nikamwambia, hivi kweli khutba hii ilikuwa

1. Wasailus-Shia, juz. 8 uk 14.

inaafikiana na mazingira wanayoishi Waislamu leo hii? Na kwa kuwa mtu huyu alikuwa mtu wa haki alishirikiana nami katika masikitiko na huzuni.

Inaonyesha wazi kwamba khutba za sala ya Ijumaa zote huwa zinafanyiwa sensa na uchunguzi kabla ya kusomwa, na serikali ya Saudia ndiyo inayowaelekeza Makhatibu kile watakiwacho kukisema ili wasije wakayavuka maelekezo hayo. Basi hakuti katika khutba hizo maelezo yoyote juu ya ukoloni na vitimbi vyake dhidi ya Uislamu wala maneno yanayohusu maadui wa Uislamu na hali za Waislamu.... Amma kuwazungumzia Mashia na "Majusi" hilo linazungumzwa kwa mapana yote kwa kiwango cha kumridhisha shetani. Na kwa hakika baada ya mapinduzi (ya Kiislamu) nchini Iran, kilitolewa Kitabu kiitwacho, "Wajaa Daurul-Majus" yaani umefika wakati wa majusi.[1]

Baada ya maelezo yaliyotangulia, Je, inafaa kusemwa kwamba, watawala wa Najdi na Hijazi ni wattumishi wa Haram ya Mwenyezi Mungu na walinzi wa nyumba ya Mwenyezi Mungu?!

Na je, Hivi katika zamn zao (Watawala hawa) Al-Kaaba imekuwa ni tengenezo kwa ulimwengu wa Kiislamu? Ya Pili: Je, Haram ya Mwenyezi Mungu ni nyumba ya utuliva na amani siku hizi? Kwa hakika Qur'an Tukufu inaizingatia Al-Kaaba na viunga vyake kuwa ni Haram ambavyo ni mahala pa Mwenyezi Mungu penye amani. Mwenyezi Mungu Anasema: "Na yeyote atakayeingia Makka atakuwa katika amani." Qur'an, 3:97.

Bila shaka Nabii Ibrahim ambaye ndiye baba wa Waislamu wote, alimuomba Mola wake aifanye Haram (ya Makka) kuwa hi mahali pa salama na amani. Mwenyezi Mungu amesema Akimnukuu Ibrahim: "Ewe Mola wangu ufanye mji huu kuwa mahali pa amani" Qur'an, 14:35.

Na sasa hebu tujiulize: Je, Watumishi hao wa Haramaini hivi wao kweli ndiyo walinzi wa sheria hii ya Mwenyezi Mungu? Je, Waislamu pamoja na Khitilafu zao za Madh-hebu wanao uhuru wa kutatua mambo yao ya kisiasa na kubadilishana mitazamo yao hapo kivenye Al-Kaaba Tukufu? Hivi Waislamu waliokusanyika kwenye Al-Kaaba wanaweza kutangaza matatizo yao na kujulishana wao kwa wao hali zao na mambo yanayowakabili? Je, Mambo ndivyo yalivyo, au ni kwamba uhuru wa kusema na kutoa maoni unatolewa kwa madh-hebu ya Hanbal peke yake tu miongoni mwa Madhehebu ya Kiislamu?! Na wala hakuna ruhusa ya kutoa fikara na maarifa ya juu katika Uislamu isipokuwa zile fikra dhaifu za Ibn Taymiyah na Ibn AI-Qayyim na zaidi ya hapo ni fikra za Muhammad Ibn Abdil-Wahab!! Na wala hakuna kizungumzwacho katika khutba za Ijumaa na nyinginezo kuhusu maudhui yoyote ya Uislamu isipokuwa ni kuzuru makaburi na kuharamisha hafla za maulidi ya Mtume **[s.a.w.w]** na kuharamisha kuwaheshimu Mawalii wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, eti kama kwamba Uislamu umedhibitiwa katika maudhui hizi peke vake!!

Na yeyote mwenye kuzikhalifu fikra zao hizo batili, basi malipo yake ni kumhukumu kuwa ni kafiri na ni mshirikina, na kwamba inajuzu kumshutumu na kumpiga na kumlaani, hivyo basi ni kafiri tena mshirikina na mengineyo. Je, hii ndiyo maana ya "Haraman Aminan" (Yaani Nyumba Tukufu ya Amani) na je, hivi tutakuwa tuko kinyume cha ukweli ulivyo

1. Watu waliokuwa wakiabudu moto.

iwapo tutasema kwamba leo hii Al-Kaaba inakanyagwa na nyayo za Mawahabi? Bila shake fikra Kiwahabi imesimama juu ya msingi wa kuyakufurisha Madh-hebu na vikundi vya Kiislamu na kupanda mbegu ya utengano miongoni mwa Waislamu, na kuharibu heshima ya Uislamu na mafunzo yake bora na kuondosha athari za Utume, na (pia Uwahabi umesimama juu ya msingi wa) kufanya mapatano na kujipendekeza kwa kila waovu na watawala wachafu na waovu mpaka hata (wanajipendekeza) kwa Yazid bin Muawiyah!! Nao Makhatibu na waandishi ambao wanatumiwa na Masultani wa Kiwahabi, hao siyo Makhatibu (Safi) isipokuwa ni waajiriwa wa Pilato na wawaidhi wa Masultani, hawasemi wala hawaandiki ila kile wanachokitamani mabwana zao wa Kiwahabi wasiyoijuwa Dini. Ewe msomaji Mtukufu, huenda ukatuona sisi labda tumezidi mao katika kuwalezea (Mawahabi) na tumejitenga mbali na ukweli na uadilifu katika maelezo tuliyoyaeleza juu ya kundi hili.

Lakini ili usiendelee kuwa na mashaka na wala usitutuhumu kuvuka mipaka katika maelezo, basi sisi tunaweka mbele ya macho yako picha ya Jalada la kimoja kati ya vitabu ambavyo vimechapishwa na Serikali ya Saudia na kuvigawa kwa wingi, na kitabu hiki kinahusu kumtukuza na kumheshimu mtu ambaye jeshi Iake liliipiga Al-Kaaba kwa mizinga, na kuhalalisha kila kilicho haramu katika mji wa Mtume wa Mwenyezi Mungu [s.w.t] kwa jeshi lake kuukalia siko tatu kamili likipora mali na kuwavunjia watu heshima zao na kuwauwa! Na utaona kwa macho yako pameandikwa juu ya jalada kwamba Wizara ya Elimu katika Serikali ya Kiwahabi ndiyo iliyobeba jukumu la kuchapa na kusambaza kitabu hiki kilichobatili. Baada ya maelezo hayo.... tunsema kwamba: Katika nchi ya Hijazi kuna uhuru usiyo na mpaka na wakati huo huo kuna ukandamizaji usiyo na mpaka.

Ama uhuru usiyo na mpaka ni ule walionao Mawahabi na washirika wao miongoni mwa wanaokula fadhila zao, kwani vitabu na vijitabu vilivyojazwa maandiko yanayowasifia madhalimu na kuwatukuza mafasiki wa Kibanu Umayyah na Bani Abbasi vinachapishwa na kusambazwa bila kikwazo cho chote au Sharti yoyote, bali serikali inachangia kuvichapisha kuvisambaza. Ama shinikizo na ugandamizaji na unyanyasaji na vizuwizi na kupiga marufuku kuko kwenye vitabu vinavyozungumzia Uislamu kama ulivyo shuka toka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na vinavyozungumzia Ah-lul-Bait ambao Mwenyezi Mungu amewalinganisha na Qur'an na akaiteremsha Qur'an ndani ya nyumba zao na akawatakasa mno kutokana na uchafu.

Naam... bila shaka kila kitabu kianchoingia Hijazi (Saudi Arabia) ni lazima kichunguzwe na kufanyiwa utafiti na wala hakiruhusiwi kuingia nchini humo mpaka kwanza Wizara ya habari itoe ruhusa!! Kwa hakika mwaka uliopita, ambao ni mwaka wa 1404 A.H. mimi nilikwenda hija na kuyazuru maziyara matukufu likiwemo la Mtume **[s.a.w.w]** na kizazi chake kitukufu [a.s] huko Madina. Basi katika uwanja wa ndege wa Madina nilikuwa na nakala kumi za kitabu kiitwacho "Mas-dar Al-Wujud". Ambacho kinachambua dalili za kimaumbile na za kiakili juu ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Na lengo la kuzichukua nakala hizo katika nchi hiyo ilikuwa ni kushirikiana kueneza Tauhid na kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba, mtu anayehusika na mambo ya vitabu katika uwanja wa ndenge aliamuru nakala hizo zizuwiwe na zisisambazwe mpaka hapo itakapotolewa hukumu nyingine. Na baada ya yeye kukipitia kitabu hiki kwa haraka haraka aliniambia: "Japokuwa kitabu hiki ni chenye faida na ni kizuri lakini ni lazima kukipeleka kwenye wizara ya habari nawe utakichukua kutoka kwao. Naama hii ndiyo maana ya kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo: "Nchi yenye Amani"!!!?

## NENO "SHIRKI" LITAKUKUTA KILA UPANDE

Bila shaka kabisa miongoni mwa maneno ambayo ni rahisi na yanatumika katika nchi ya Saudia ni neno "Shirki", na tuhuma hii huelekezwa kwa wanachuoni wengi na watu wenye heshima katika Uislamu! Utakapokutana na watu idara ya "Al-Amri Bil Maaruf Wannahyi Anil Munkar neno utakalolisikia kila wakati ni hili neno baya na mfano wa hili, kama kwamba ndani ya kamusi zao hakuna maneno mengine isipokuwa maneno haya mabaya yenye kuchukiza tena machafu na ni kana kwamba hawana jingine la maana isipokuwa kuelekeza tuhuma hii ya shirki kwa kuwatuhumu (vibaya) wageni wa Mwenyezi Mungu na mahujaji wa nyumba Tukufu ya Mwenyezi Mungu!! Wakati nikiandika utangulizi huu kimenifikia kitabu kiitwacho, "As-hiatu-wa At-Tashayuu" kilichotungwa na Mpakistani mwenye chuki ambaye ni miongoni mwa wanaofadhiliwa na Mawahabi, jina lake ni Ihsan Ilahi Dharir, na kimechapishwa Saudia. Na ndani yake anazitupa tuhuma na uzushi dhidi ya Ushia, na anadai kwamba yeye anaeleza kutokana na vitabu vyao na rejea zao.

Kwa mfano, utaona katika ukurasa wa ishirini wa kitabu hicho, anataja neno la Al-Marhum Al-Ustadh Mheshimiwa Sheikh Muhammad Husein Al-Mudhaffar, kisha analisherehesha kufuatana na vile apendavyo na namna inavyompelekea nafsi yake inayoamrisha uovu. Katika maelezo yafuatayo tunaweka mbele yako Ewe msomaji Mutukufu neno hilo pamoja na sherehe ya Wahabi huyu ili uone mwenyewe ni vipi Mawahabi waliofilisika kwa dalili wanavyotegemea maneno ya tuhuma na uzushi na uongo dhidi ya Shia. Marhum Al-Mudhaffar anasema: "Fakanatid-Daawatu Littashayui Liabil-Hasan Alayhis Salaam Min Sahibir-Risalat Salallahu Alayhi Waalihi Wasallama Tamshi Minhu Janban Lijanbin Maad-dawat Lish-Shahadatayn." Tafsiri Yake: Mwito kutoka kwa Mtume **[s.a.w.w]** kumfuata Abul-Hasan Ali [a.s] ulikuwa ukienda sambamba na mwito wa Shahada mbili. Na maana ya maneno yake haya ni kwamba: Ushia haukuzalikana kutokana na hali ya kimazingira wala siyo Madh-hebu yaliyoanzishwa baadaye, bali ni Mah-hebu ya asili ambayo chanzo chake kinaanzia kwa Mwenyewe Mtume Muhammad **[s.a.w.w]**, kwani Mtume alikuwa akilingania wau juu ya Uimamu wa Amirul-Muuminina Ali [a.s] sambamba na wito Wa Shahada mbili.

Kisha Wahabi huyu muovu anayawekea Taaliq maneno ya Sheikh Mudhaffar na anasema: Hakika Mtume (kwa mujibu wa madai ya Mudhaffar) alikuwa akimfanya Ali kuwa ni mshirika wake katika Unabii wake na ujumbe wake"!! Iwapo Mwandishi huyu siyo mtumwa wa matamanio yake na chuki na mwenye kufadhiliwa na Mawahabi, na iwapo ni mchunguzi wa misingi ya itikadi za Kiislamu za Kishia na misingi Tabari, nasi kwa sasa hivi hatuna lengo la kufanya ufafanuzi katika maudhui

hii, lakini tunataja mfano wa jambo hilo: Ndani ya Kitabu "As-hiatu-wa At-Tashayuu" uk. 49 mtungaji anatuhumu Ushia kwamba umepokea fikra zake kutoka kwa Abdallah bin Sabaa aliyezalikana kutoka kwa Myahudi wa Yemen, na anavyoitakidi Tabari kwamba (Abdallah bin Sabaa) alidhihirisha Uislamu na kuficha Uyahudi na mapenzi yake kwa Imam Ali aliyafanya kuwa ni kifuniko cha kueneza fikra zake.

Jambo hili hatutalitafiti kwa wakati huu. Basi utamona mwandishi huyu wa Kiwahabi anategemea mambo aliyoyapokea Tabari kuhusu uzushi huu, Amma Sanad za riwaya ambayo Tabari anaieleza ni kama ifutavyo neon kwa neon:"Aliniandikia As-Sariyyu kutoka kwa Shuaib, kutoka kwa Seif, kutoka Atiyyah naye toka kwa Yazid Al-Faq-Asi: Abdullah bin Sabaa alikuwa Myahudi katika watu wa Sanaa...." (Vile vile ameipokea riwaya hii Ibn Khaladun Al-Magharibi na Ibn Kathir Ash-Shami na walio mfano wa Tabari miongoni mwa maadui wa Ahlul-Bait. Sasa hivi tunaiweka riwaya hii kwenye meza ya uchunguzi wa uhakiki ili tuone, je, inajuzu kuitegemea riwaya ya wapokezi hawa amboa majina yao yametajwa hapa au haifi? Kwa mtazamo wa haraka ndani ya vitabu vya elimu ya rijali (ambavyo vimeandikwa na wanachuoni wa Kisunni) vitatutosheleza kufahamu hali zaa wapokezi hawa.

Hebu Tazama uhakika wenyewe:

1. As-Sari sawa sawa akiwa ni As-Sari ibn Ismail Al-Kufi au As-Sari lbn A'sim aliyekufa mwaka 258 kila mmoja wao ni miongoni mwa waongo na wazushi.[1]

2. Shuaib ibn Ibrahim Al-Kufi: Maj-hul (Hatambulikani hali yake).[2]

"Hakika huyu ni ndugu yangu na ni wasii wangu na ni khalifa wangu kwenu, basi msikilizeni na mumtii.[3]

Kutokana na ukweli huu wa kihistoria Mashia wanasema kwamba, tangu siku hiyo aliyoamrishwa Mtume **[s.a.w.w]** kulingania Tauhidi na Utume, aliamuriwa pia katika siku hiyo kulingania Uimamu wa Ali [a.s] na ukhalifa wake baada yake, basi mwito wa imani na Utume umeambatanishwa na mwito na kuamini Uimamu. Je, inasihi kusemwa kwamba Mashia wanaitakidi kuwa Ali [a.s] alikuwa mshirika wa Mtume katika Utume?" Na Je, mwito wa Ukhalifa wa Imam Ali [a.s] baada ya Mtume **[s.a.w.w]** kufariki maana yake ni mwito wa Unabii?

## MAKOSA KATIKA VITABU VYA MASUNNI

Naam bila shaka upungufu na kosa lililoko katika vitabu vya Masunni na hasa Mawahabi linarudi kwenye mambo mawili:

Jambo la Kwanza: Ni kukosa kwao maarifa mengi ya kutosha kuhusu madhehebu ya haki, na upungufu huu walionao hauhusu zama zetu hizi tu, bali unarudi hadi kwenye karne zilizopita katika historia, na huenda sababu ya jambo hilo ni ile hali iliyokuwa ikitendwa na serikali za watu wa

---

1. Tahdhibut-Tahdhib cha Ibn Hajar, Juz. 3, uk. 46, Tarikh al-Khatib, Juz. 1, uk. 193, Mizanul-Itidal, Juz. 1, uk.37, Lisanul Mizan, Juz. 3, uk. 13.

2. Mizanul-Itidal, Juz. 1, uk. 447, Lisanul-Mizan, Juz.3, uk. 145.

3. Rejea za hadithi hii zimetajwa ndani ya vitabu vya wanahistoria na wanahadithi na wafasiri wa Qur'an, na ni hadithi maarufu kwao kwa jina la (Yaumul-Indhar na Badu'd-dawah) yaani mwaanzo wa da'awah na miongoni mwa walioipokea ni Tabari katika Tarikh yake. Juz. 2, uk. 63, chapa ya Misri.

Jahannam yaani Banu Umayyah na wengineo katika kuwakandamiza na kuwanyima uhuru Mashia na kutokuwapa nafasi ya kubainisha itikadi zao za haki katika Mahfali na mikusanyiko ya Kielimu, ili watu waufahamu Ushia kutoka katika vinywa vya viongozi wake wasipotoshwe na uzushi wa maadui zake. Kwa hakika historia inatuthibitishia kwamba, Madh-hebu yote yalikuwa yanauhuru wa kutoa maoni na kubainisha itikadi (zao) isipokuwa haya Madh-hebu ya haki yalikuwa yamezuwiliwa kufanya hivyo.. Naam, upepo wa uhuru kwa Mashia ulivuma katika baadhi ya nyakati ambazo hazikutosheleza kulithibitisha lengo hili.

Na kwa hali yoyote ile, kutokuyafahamu Madh-hebu ya Ushia (na wakati mwingine chuki) imekuwa ndiyo sababu ya kutengenezwa uongo na uzushi huu na kuvijaza vitabu uzushi na kuichafua shabaha ya Madh-hebu haya ya haki. Na kwa hakika Ahmad Amin wa Misri, mwandishi wa kitabu kiitwacho "Fajrul-Islam" amekiri jambo hili baada ya kutawanya kitabu chake hicho kilichojaa uongo na uzushi dhidi ya Shia, kisha akauzuru mji wa Najaf baadhi ya wanachuoni wakamlaumu kuhusiana na kupotosha kwake na uzushi wake dhidi ya Shia, na udhuru wake mkubwa aliokuwa nao ilikuwa ni kutokuujua Ushia na uchache wa rejea. Jambo La Pili: Ni kuharibika kwa utaratibu wa masomo katika vyuo vya Kisunni na kubadilishwa kwa vitabu vyenye maarifa kwa undani kama vile "Kitabul-Mawaqifi na Sharhul Maqasid" (Na badala yake vikawekwa) vitabu vya kiwango cha chini visivyokuwa na uchunguzi wa kina, na jambo hilo limepelekea kushuka kwa kiwango chakufikiri na utunzi na kutoweka fikra za uchunguzi wa kina kiasi kwamba hakuna katika nchi nyingi za Kiislamu anayeweza kuvisomesha vyema vitabu hivi viwili ambavyo vimeandikwa katika karne ya nane Hijiriyyah.

Kwa sababu hii basi, siyo jambo la ajabu kumuona "Ihsan Ilahi Dhahir" kwa mfano anatangatanga hajui anachokifanya kwani hatenganishi baina ya mwito wa Uimamu na mwito wa Utume, na anaandika kitabu juu ya madh-hebu katika historia na kuvitawanya kwa kusaidiwa na mali zinazotokana na petroli ambaye inaporwa na serikali ya uvamizi ya Kiwahabi ndani ya Hijazi, na hili linafanyika hali ya kuwa inafahamika kwamba mwandishi huyu hafahamu misingi ya itikadi ya Kishia.

## UCHACHE WA KUFIKIRI KWA UNDANI

Tangu zaidi ya miaka mia moja iliyopita, vita ya kifikra dhidi ya Uislamu ikiwa inawasha moto wake, na mataifa ya magharibi na mashariki yakisaidiana na vibaraka wao walioko katika nchi za Kiislamu yanafanya juhudi zao za upeo mkubwa ili kuinagamiza dini hii tukufu na kuchafua shabaha yake, haipiti wiki au mwezi isipokuwa hutolewa kitabu dhidi ya dini tukufu ya KiisIamu. Katika hali hii yenye majonzi, hivi kweli inafaa kwa Saudia kukusanya nguvu zake na uwezo wake na matoleo yake yote ili kuupiga vita Ushia peke yake tu?!! Na kana kwamba katika ulimwengu wa Kiislamu hakuna tatizo jingine isipokuwa Ushia?!! Hata hivyo, lau vijitabu hivyo vingekuwa vinazungumza juu ya msingi wa mantiq na dalili tusingevipinga kwani mantiq inakubalika kwa wanachuoni wa Kishia, kwani wao huikubali au kuipinga kwa mantiq na hoja, lakini kwa bahati mbaya sana vijitabu vyao vingi utaviona vimejaa uongo, uzushi, makosa na uzandiki dhidi ya Mashia na dhidi ya wanachuoni wao wema (r.a).

Bali utaona katika baadhi ya vitaba hivyo kuwa, havikuepukana na kumtweza na kumkosea Adabu Imamul-Muta-Qina na Amirul-Muuminina Bwana wetu na kiongozi wetu Ali [a.s]. Hebu chukua mfano wa hilo katika kitabu, "Ashiatu WatTashayyuu" tulichokiashiria hapo kabla, hicho ni mfano ulio wazi miongoni mwa vijitabu vyenye kupotoka, kwani utamuona mtunzi (Akinakili kutoka kwa Tabari, Ibn Kathir, Ibn Khaladun na wengineo miongoni mwa maadui wa haki) anauona Ushia kuwa ni (Dhehebu) lililozalikana kutokana na fikra ya Abdallah Bin Sabaa ambaye ni Myahudi, kisha anatolea Ushahidi aliouandika Ahmad Amin wa Misri (ndani ya kitaba kiitwacho Fajrul-Islam) dhidi ya Shia, kisha anakamilisha safari yake kutolea ushahidi makala za mustashriqin Mayahudi na Wakristo "Dauzi" na "Mul-Aer" na "Wilhazen".

Lakini hataji chochote kutoka katika vitaba vya Mashia, basi je, hii ndiyo Insaaf (Usawa)!? Hakika wanachuoni wa Kishia wa hapo mwanzo kama vile Sheikh Saduq aliyefariki mwaka 381 A.H. na Sheikh Mufid aliyefariki mwaka 413 A.H. na wengineo, bila shaka waliziandika Aqida (Itikadi) za Kishia na kuzitawanya kwa watu nazo ni nyingi mno ndani ya maktaba na zinatoa picha ya asili ya Aqida za Kishia, basi ni vipi hazitegemei katika kuzinakili? Je, Siyo kwamba "'Wenye nyumba ndiyo wajuao zaidi kilichomo ndani yake"?! Je, Ahmad Amin wa Misri ambaye haujui Ushia na hautambui kama alivyokiri yeye mwenyewe ndiye ayajuaye madhehebu ya haki kuliko wanachuoni wake wema? Na utamuona mwandishi huyu muovu wa Kiwahabi anajaribu kujitakasa makosa aliyoyafanya dhidi ya Mashia kwa kutegemea vitabu vya maadui zao anasema: "Kwa hakika vitabu hivi (yaani vitabu vya itikadi za Kishia) ni vitabu vya propaganda za Kishia ama kwa itikadi yao halisi haikutajwa ndani ya vitabu hivi!!!

Na baya zaidi kuliko hilo ni kwamba, yeye anaileta hadithi iliyoko ndani ya 'Biharul-Anwaar" na Al-n-Waarun-Nu'maniyyah na kuizingatia kuwa ni dalili ya itiqadi ya Mashia, huku akijua kwamba hapana shaka kuwa kuna hadithi dhaifu ndani ya vitabu vya Kisunni na Kishia, hili sote tunalijua, na kutaja hadithi moja haiwi ndiyo dalili juu ya itikadi ya watu fulani (kwa namna yoyote ile) kwani wako wapokezi wengine ni dhaifu na waongo na ni Majhul hawatambulikani hali zao". Basi haiwezekani kuitegemea hadithi ila baada ya kuihakiki katika sanadi yake na wapokezi wake. Sisi tunamuuliza Wahabi huyu mwenye kuajiriwa na wengineo mfano wake miongoni mwa wanaofadhiliwa: Je, hivi kila kilichokuja katika Tarikhut-Tabari kinazingatiwa kuwa ni sahihi bila ya shaka au ni kwamba kuyategemea hayo aliyoyaleta kunategemea uhakiki katika Isnadi yake?! Hakika katika mambo yasiyokuwa na shaka ndani yake, ni kuwemo kwa wapokezi waongo wa wazushi ndani ya riwaya za yake, basi Taaliq hiyo mbovu isingetoka kwake na wala asingemkosoa Sheikh Mudhafar ambaye ni mwanachuoni mkubwa. Kishia sisi tunasema, ikiwa mwito wa Uimamu wa Ali [a.s] unazingatiwa kuwa ni shirki au ni kuushirikisha na utume, basi Qur'an imetangulia kulisema hilo, kwani imetoa mwito kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Ulul-Amri katika Siyaqi moja. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu "Mtiini Mwenyezi Mungu na mumtii Mtume na Ulul-Amri miongoni mwenu." Qur'an, 4:5.

Basi kwa mujibu wa maoni ya mwandishi huyu wa Kiwahabi, ni kwamba mjumbe wa Mwenyezi Mungu [s.w.t] badala ya kulingania Tauhidi alilingania shirki na Aqida ya miungu wawili kwani aliambatanisha baina ya kuwatii Ulul Amri na kumtii Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwani neno Ulul Amri kwa namna yoyote ile tutakayolifasiri bila shaka litamuingiza Imam Ali [a.s] (Katika maana hiyo), bali yeye anastahiki zaidi kuliko wengine. Wanahistoria na wanachuoni wa Tafsiri na hadithi wameeleza kwamba iliposhuka kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo: "Na Uwaone Jamaa zako wa karibu" Qur'an 26:214.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu [s.w.t] aliwaita jamaa zake wa karibu (nduguze, na wazee wake) kwenye karamu ya chakula nyumbani kwake, kasha akawatangazia habari ya Unabii wake na Utume wake na baada ya hapo akasema: "Ni nani kati yenu atakayenisaidia juu ya jambo hili kwa sharti awe ndugu yangu na wasii wangu na Khalifa wangu kwenu"? Basi hapana yeyote aliyesimama isipokua Imam Ali [a.s] akasema, "Mimi Ewe Mjumbe wa Mwenezi Mungu." Mtume **[s.a.w.w]** alikariri maneno yake hayo mara ya pili na ya tatu ili awape fursa ya kuchukua uthibitisho..... Na hakuna yeyote aliyejibu isipokuwa Amir-ul-Muuminina Ali [a.s] basi Mtume akasema:

3. Seif Ibn Umar: Anasimulia hadithi za uongo na kuzinasibisha kwa wapokezi waaminifu.[1]

4. Yazid Al-Faq-Asii: Maj-hul kabisa (Hatambulikani hali yake kabisa) jina lake halikutajwa popote ndani ya vitabu vya "Rijal" (yaani vitabu vinavyochunguza hali za wapokezi wa hadithi).

Na inafaa kusema kwamba, Tabari anasimulia ndani ya juzuu Ia tatu, la nne na la tano katika Tarikh yake tokea mwaka wa kumi na moja A.H. mpaka mwaka wa thelathini na saba A.H. na miaka hii ni kipindi cha utawala wa Abubakr na Umar na Uthman na riwaya zote hizo zimepokelewa kutoka kwa watu hawa watano tu!! Na matokeo yake Tabari amezua matukio mengi miongoni mwa hayo na akayaeleza kama vile ipendavyo nafsi yake!! Basi Je, hii inasihi na Je, inajuzu kuzitegemea riwaya kama hizi?! Na kinacholeta mshangao zaidi ni kwamba, riwaya za watu hawa watano ziko katika juzuu ya tatu na ya nne na ya tano tu ndani ya Tarikh Tabari, amma majuzuu mengine huwezi kuona majina yao yanatajwa wala riwaya itokayo kwao isipokuwa riwaya moja tu ndani ya juzuu ya kumi!! Basi Je, Ujuzi wa Tarikh (Historia) alionao "Sari" na "Seif bin Umar" ulikuwa umedhibitiwa katika kipindi hiki peke yake tu, na ulikuwa unahusika na mambo ya Madh-heb peke yake?!!

Naam, yeyote mwenye kuzichunguza kwa undani riwaya za watu hawa watano atafahamu wazi kwamba riwaya hizo ni uzushi wa mtu mmoja, na kwamba ndani yake kulikuwa na lengo makhsusi. Ni mushkeli kufikiria kuwa Tabari hakufahamu jambo hili, basi ni kwa nini Tabari ametaja yote haya? Jawabu lake ni kwamba: Bila shaka hiyo ni hali ya kupenda na chuki vitu ambavyo humpofua mtu na kumfanya awe kiziwi! Na kinachohuzunisha zaidi ni kwamba kundi la wanahistoria waliokuja baada ya Tabari wakanakili toka kwake na wakafuata nyayo zake na wakazileta

1. Mizanul-Itidal, juz. 1, uk. 438, Tahdhib-but-Tahdhib. juz. 4, uk. 295.

riwaya hizi za uzushi na uongo ndani ya vitabu vyao vya historia bila ya uchunguzi wowote juu ya kusihi kwake na watu waliozisimulia na sanadi zake, wakidhani kwamba kila anachokisimulia Tabari ndiyo hasa tukio halisi na ndiyo ukweli ulivyo. Iangalie Tarikh ya Ibn Asakir na Al-kamil ya Ibn Al-Athir, na Al-Bidayatu Wan-Nihayah ya Ibn Kathir na Tarikh ya Ibn Khaladun na nyinginezo utaona usahihi wa maneno yetu.

Hali ni hiyo hiyo kwani vitabu vya Tarikh vya sasa hivi havikusalimika na uzushi huu mbaya na Ikhtilafu inayochukiza. Lakini kwa bahati nzuri watu wa Sanadi ndani ya riwaya zilizomo katika Tarikh ya Tabari wametajwa, na hilo ni miongoni mwa mambo ambayo yanatoa nafasi ya kufahamu riwaya sahihi na kuilinganisha na riwaya dhaifu au iliyozushwa kama tulivyokuletea mfano mmoja unaoeleza jambo hilo. Na sasa tunarudia mazungumzo juu ya Kitabu "As-Shiatu Wa At-Tashayyuu" na tunasema: "Kwa hakika kitabu kinachotegemea rejea ambazo riwaya zake ni za uzushi na wapokezi wa riwaya hizo ni waongo tena wazushi, basi kitabu hiki kitakuwa hakimiliki japo thamani ndogo, nasi sasa hivi tuko katika zama za usomi na uchunguzi.

Basi Je, hivi itasihi kwa kundi kubwa la Kiislamu Ienye hadhi kubwa katika elimu za Kiislamu na kuhuisha Sunna Tukufu ya Mtume **[s.a.w.w]** ambalo liko mstari wa mbele kuwapiga wavamizi wa Ki'Israeli, hivi kweli ni sahihi kundi hilo linasibishwe kwa Myahudi asiyejulikana kwa kutegemea Tarikh potofu ambazo umekwisha thibiti uongo wa wapokezi wake?

2

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## KIASI CHENYE MAKOSA

Tunakwenda sambamba na mwandishi huyu wa Kiwahabi katika kitabu chake kisichokuwa na maana, na tunamuona anamkosoa Imam Ali ibn Abi-Talib [a] kwa njia ya kutaka kufahamu na kuuliza sababu za kufanya haraka kumuuzulu Muawiyah mara tu Imam Ali [a.s] alipotawalia (Ukhalifa) na anajiuliza anasema: Kwa nini, kwa nini? Bila shaka kilichompelekea kupinga ni kule kumlinganisha kwake Imam Ali [a.s] na watawala wenye kujali maslahi ambao hawafikiri isipokua maslahi yao binafsi na kuyatanguliza kuliko hukumu za sheria na wajibu aliowajibisha Mwenyezi Mungu, bali huupinda upande wa sheria kwa lengo la kulinda uongozi na utawala wao, basi kwa mujibu wao "lengo lao in kujisafishia wasiIa." Fikra hii potofu ndiyo iliyomfanya mwandishi huyo wa Kiwahabi ampinge kiongozi wa wachamungu Ali [a.s] kwa njia ya kuuliza na kutaka kufahamu. Naam, lau Imam Ali [a.s] angekuwa kama watawala wengine wanaojali maslahi yao, basi upinzani wa Wahabi huyu ungekuja hapa na angetakiwa awaache watu wapotofu na mafasid kama vile Muawiyah na mfano wake waendelee kuwatawala Waislamu kama zipendavyo nafsi zao za kishetani, lakini Imam Ali [a.s] siyo kiongozi wa aina hiyo ya watawala hao sivyo kabisa.

Kwa hakika ni kiongozi mwenye Ikhlas, kwani anasema Imam Ali [a.s] akimjibu Mughira ibn Shu'bah na walio kama Mughira "Mimi sitaki Mwenyezi Mungu anione ni mwenye kuwafanya wanaopotosha kuwa ni wasaidizi (wangu)".[1] Ewe msomaji mpendwa: Mpaka hapa tunafupisha maneno, na tunachokitarajia ni kwamba jibu hili la haraka tulilolileta limekuwekea wazi msimamo wa huyu Wahabi mwenye chuki dhidi ya kizazi cha Mtume Muhammad **[s.a.w.w]** na wafuasi wao na (na vile vile limekuwekea wazi) kufilisika kwake (Wahabi huyu) katika maarifa ya Dini na Itikadi za haki za Kiislamu na kukosea kwake na upotofu wake alioufanya kwa makusudi na riwaya zake za nongo. Nao wanachuoni wa dini na wanachuoni wa sheria ya haki watazishughulikia hujuma hizi mbaya za Kiwahabi, nasi tunataraji hivi karibuni apendapo Mwenyezi Mungu, litatolewa jawabu thabiti dhidi ya uzushi wa Wahabi huyu mpotofu mwenye kupotosha.

### MWITO WA KUFANYIKA KONGAMANO LA KIISLAMU

Kwa hakika ni muhimu sana kufanyika kongamano la Kiislamu ambalo ndani yake yatatatuliwa Masail yenye Khitilafu kwa mujibu wa muongozo wa kielimu na Mantiq na dalili, kwani wakati huu wa sasa ziko khitilafu kubwa mbili ambazo ni Uwahabi na madhehebu mengine ya Kiislamu juu ya Tauhidi na shirki, basi Je, kwa lengo la kukurubiana pande hizi mbili si inafaa kufanya mkutano wa kielimu ambao Masail haya yataaridhiwa katika meza ya uchunguzi na uhakiki kwa lengo Ia kuondoa batili na kuithibitisha haki, kwani huenda ikachomoza nuru ya kuonyesha njia kwa

1. Kitabu Waqiatis-Sifin uk. 58 Chapa ya Misri.

wanaobabaika? Inabidi kongamano hili lifanyike kwa msingi wa kutatua tatizo na siyo propaganda tu, na lisichukuliwe kama vile ni jambo Ia propaganda ya Serikali fulani.

Na ili jambo hili lipate kukamilika kama inavyotakiwa, inapasa kuchunga sharti zifuatazo:

1. Mwito huo utolewe kwa wanafikra wa Kiislamu kutoka katika Madhehebu mbali mbali za Kiislamu ambao wanawakilisha Madhehebu hayo na wanafahamika khasa kuwa wao ni wanachuoni na ni wafikra wa dhehebu hilo (wanaloliwakilisha), na wasipelekewe mwito huu wanachuoni wa Pilato wa Saudia peke yao ambao wanapatikana India, Pakistani na Misri iliyodhulumiwa.

2. Na zaidi ya wawakilishi wa Madhehebu manne, ni lazima mwito huu utolewe kwa wanachuoni na wanafikra wa Shia Ithna-Asheriyyah na dhehebu la Zaydiyyah ili mkutano huo unenekane kwa muono wa pamoja na ujumla wa Waislamu wote.

3. Ni lazima utolewe uhuru kamili kwa wajumbe wa mkutano ili kila mmoja miongoni mwao aweze kujadili juu ya Masail yatakayokuwa yamearidhiwa kwenye uwanja (wa majadiliano), na awe na haki ya kuzitetea kwa uhuru fikra zake na itikadi zake, pia kongamano hilo lijiepushe na kila kitu kinachoharibu heshima ya wajumbe wake, miongoni mwa maneno ya matusi na dharau ambayo leo hii yameenea katika miji ya Saudia.

4. Na ni lazima idara inayoendesha kongamano isifungamane na upande wowote, na bora zaidi iwe imeundwa kutokana na Madh-hebu tofauti tofauti yanayoshiriki kwenye kongamano.

5. Utafiti wote unaofanyika kwenye kongamano usambazwe (kama ulivyo) bila ya mabadiliko yoyote ndani yake na utumwe kwenye vituo (vyuo) vya Elimu ulimwenguni ili wanaopenda kujua matokeo ya kongamano hilo wausome. Aina hii ya kongamano na kwa kuchunga sharti hizi, tunataraji Masail mengi mbali mbali yatatatuliwa, na kile kiini cha mafahamiano kitathibitika na maelewano baina ya Waislamu yatapatikana.

## LENGO LA KITABU HIKI

Katika kitabu lilki tumejaribu kuchukua Masail ya msingi ambayo kuna hitilafu ndani yake baina ya Mawahabi na Madh-hebu mengine ya Kiislamu, na kuyatolea hukumu kwa mujibu wa Qur'an Tukufu na Sunna Tukufu ili tufahamu rai ya Uislamu katika Masail hayo. Na kitabu hiki siyo pekee ambacho tulichoandika kuhusu maudhui hizi, bali kimetanguliwa na vitabu vitatu na kila kimoja miongoni mwa hivyo kimebeba jukumu Ia kuchunguza na kuhakiki baadhi ya Masail haya, na vitabu hivyo ni:

1. Mafahimul-Qur'an: Na ndani yake kuna uchunguzi mpana juu ya Tauhidi katika ibada ndani ya juzuu ya kwanza ya kitabu hicho kutoka ukurasa wa 378 hadi 528, nayo ni mkusanyiko wa mihadhara iliyotolewa katika hauza ya elmu katika mji mtakatifu wa Qum, na akaiandika kwa kalamu Sheikh Jaafar al-Hadi na ikachapishwa nchini Iran na Lebanon.

2. At-Tawasul-Bil-Auliya: Ni uchunguzi unaohusu kujuzu kutawassal kwa Maimamu watakatifu (Amani iwashukie) na kutawassal kwa Mawalii wema wa Mwenyezi Mungu, na mas-ala haya ni miongoni mwa mas-ala muhimu ambayo Mawahabi wanaeneza Shub-ha (Utata) juu yake.

3. At-Tauhid Wash-Shirki Fil-Qur'anil-Karimu: Kwa hakika (ndani ya Kitabu hiki) nimejaribu kujihusisha na Mas-ail ya Tauhidi na shirki, na nimelitatua tatizo hili ambalo limekishughulisha kikundi hiki cha Mawahabi kwa muda wote wa karne mbili na nusu, na kimechapishwa katika nchi nyingi za ulimwengu.

Na mihadhara hii (iliyomo kitabuni humu) ni uchunguzi wa mara ya nne ambao tunautoa kwa ulimwengu wa Kiislamu, na tunawaita Mawahabi walioko Riyadhi na katika Haram mbili Tukufu na waandishi walioajiriwa na Mawahabi ambao wanaandika kwa Maslahi yao, waikubali haki wala usiwadanganye upinzani wa kijinga na wazinyenyekee dalili, na iwapo hawatakubali isipokuwa (kuendelea na) uadui na kupinga haki, basi sisi tunawapa changa moto ya kukijibu kitabu hiki kwa jawabu madhubuti linalokubalika, linalotegemea mantiki na siyo (jibu la) udanganyifu na uzushi. Na, Mawahabi wanalazimika kuwaacha huru Waislamu katika Haram mbili tukufu watende mambo yao matukufu ya dini, na wasiwakabili kwa uovu ndani ya Haram ya amani ya Mwenyezi Mungu na waache propaganda za Kiwahabi ambazo haziongezi chochote ndani ya Waislamu isipokuwa utengano, fitna na bughudha. "Bila shaka huu ni ukumbusho, basi yeyote atakaye na aishike njia kwenda kwa Mola wake". Jaafar Subhani

Chuo cha Elimu - Qum Tukufu

26 / Mfunguo Mosi /1406 A.H.

## VIDOKEZO JUU YA MAISHA YA MUASISI WA UWAHABI

Madhehebu ya Kiwahabi yanahusishwa kwa Sheikh Muhammad bin Abdul-Wahabi kuwa ndiyo muanzilishi wake. Madhehebu ya Sheikh huyu yameitwa "Wahabiyya" kwa munasaba wa jina lababa yake aliyekuwa akiitwa "Abdul-Wahabi". Ama sababu zilizofanya Madhehebu ya Kiwahabi yasiitwe "Muhammadiyya" kwa munasaba wa jina la muanzilishi wake, ni kama wasemavyo baadhi ya Wanachuoni kwamba, palifanywa tahadhari ya kuepusha kufanana baina ya hao wafuasi wa Kiwahabi na Waislamu wengine ambao ni wafuasi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (Muhammad bin Abdillahi).[1] Sheikh Muhammad bin Abdul-Wahab alizaliwa mwaka 1115 A.H. katika mji wa Uyainah ambao ni miongoni mwa miji ya Najdi; na mzazi wake alikuwa kadhi wa hapo Uyainah. Tangu utotoni, Muhammad bin Abdul-Wahab alikuwa na shauku sana ya kusoma vitabu vya tafsiri, hadithi na mambo ya ambaye alikuwa ni miongoni mwa wanachuoni wa Kihanbal. Na tangu akiwa kijana, Muhammad bin Abdul-Wahabi alikuwa akiyakosoa mambo mengi ya Dini waliyokuwa wakiyatenda watu wa Najdi.

Sheikh huyu hakutosheka na Najdi peke yake katika upinzani wake huo, bali alivuka mipaka hadi Madina alikokwenda wakati akitoka Hija na kuendelea kusambaza upinzani huo. Kwa hakika hapo Madina, alikuwa akiwakemea wata waliokuwa wakitawasal kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu [s.w.t] kwenye kaburi lake tukufu. Baadaye alirejea Najdi na hatimaye akaenda Basra kwa lengo la kwenda Shamu. Alipokuwa Basra alianza kuwakemea watu na kuwakataza wasitende mambo yao ya dini, wenyeji wa Basra walipoiona hali hii, wakamtimua na kumfukuzilia mbali kutoka katika mji wao. Muhammad bin Abdul-Wahabi akakimbia na

1. Dairatul-Maarif Fil QarniI-Ish-riin cha Farid Wujdi, Juz 10 uk 871.

kuelekea katika mji wa Az-Zubair. Wakati akiwa njiani kuelekea Az-Zubair, Muhammad bin Abdul-Wahabi alichoka sana kutokana na mwendo wasafari hiyo, hivyo basi joto kali la jua lilimsababishia kiu kali kiasi cha kukaribia kufa; (Afadhali angekufa). Kwa bahati mtu mmoja kutoka Az-Zubair alimuona akamhurumia hasa kwa kuwa mavazi aliyokuwa amevaa yalikuwa ni mavazi ya watu wa dini basi mtu huyo akamnywesha maji Muhammad bin Abdul-Wahab; na akampandisha kwenye kipando chake na kumfikisha mjini.

Makusudio ya Muhammad bin Abdul-Wahabi ilikuwa ni kwenda mpaka Shamu, lakini kutokana na kukosa kwake chakula na mali ya kuweza kumudu safari hiyo, alisafiri mpaka Al-Ahsaa; kisha akaenda Huraimala ambao ni mji katika miji ya Najdi, na huo ulikuwa ni mwaka 1139 A.H. Katika mwaka huo huo, baba yake alihama kutoka Uyainah akaenda Huraimala. Hapo Muhammad bin Abdul-Wahabi akaungana na mzazi wake na akaendelea kusoma kwake. Katika kipindi hicho hicho, yeye aliendelea kueneza upinzani wake dhidi ya ibada mbali mbali za kidini katika nchi ya Najdi, jambo ambalo lilisababisha machafuko na kutokuelewana baina yake na baba yake kwa upande mmoja, na baina yake na watu wa Najdi kwa upande wa pili. Hali hii ya vurugu na kutoelewana iliendelea hadi mwaka 1153 alipofariki baba yake.[1] Kufariki kwa baba yake kulimpa nafasi nzuri Muhammad bin Abdul-Wahabi kutangaza wazi wazi itikadi zake za pekee. Alitembea huku na kule kueneza Aqida yake potofu, akawa anawakemea watu kutenda matendo ya dini, na kuwataka wajiunge katika kundi lake na wawe chini ya uongozi wake. Baadhi ya watu walihadaika na mwenendo wake, na wengine walimpinga.

Pamoja na hali hii, mambo yake yalijulikana wazi kwa watu wa mji wa Huraimala, na baada ya muda Muhammad bin AbdulWahabi alifunga safari kurudi Uyainah mahala alipozaliwa. Wakati huu Athumani bin Hamad alikuwa ndiyo mtawala wa hapo Uyainah, na alimpokea Muhammad bin Abdul-Wahabi na akamkaribisha kwa wema. Muhammad bin Abdul-Wahabi na mtawala huyo wa Uyainah walifanya makubaliano ya kila mmoja kumlinda mwenzake; ili mmoja wao awe na nguvu za kisheria na mwingine awe na nguvu za utekelezaji wa maamuzi yanayoamuliwa.

Kwa hiyo basi mtawala wa Uyainah akawa anamsaidia Muhammad bin Abdul-Wahabi kutekeleza malengo yake kwa kutumia nguvu za kiutawala, naye Muhammad bin Abdul-Wahabi humsaidia mtawala huyo kwa kutoa fatwa zinazowataka watu wamtii mtawala huyo na kuzifuata amri zake. Habari zilimfikia mtawala wa Al-Ahsaa kwamba, Muhammad bin Abdul-Wahabi anawalingania watu kwenye rai zake na uzushi wake, na pia kwamba mtawala wa Uyainah ndiye anayempa nguvu ya kufanya hayo. Mtawala huyu wa Al-Ahsaa alimwandikia barua kiongozi wa Uyainah kumuonya kwa kumsaidia kwake Muhammad bin Abdul-Wahabi. Barua hiyo alipoisoma, akamwita Muhammad bin Abdul-Wahabi na kumfahamisha kuwa yeye hatomsaidia tena.

Muhammad bin Abdul-Wahabi akamwambia mtawala wa Uyainah, "Iau ungenisaidia katika mwito wangu huu, ungeitawala Najdi yote". Mtawala

1. Tarikh AI-Alusi, uk. 111 - 113.

huyo alikataa rai hiyo na akamuamuni Muhammad bin Abdul-Wahabi aondoke hapo Uyainah. Hivyo basi Muhammad bin Abdul-Wahabi akafukuzwa kutoka Uyainah hali ya kuwa mwenye kufedheheka. Tukio hili la kufukuzwa kwa Muhammad bin Abdul-Wahabi lilitokea mwaka 1160 A.H. na aliondoka hapo Uyainah akaelekea Dir'iyyah, mji ambao ulikuwa mashuhuri miongoni mwa miji ya Najdi. Mtawala wa hapo alikuwa in Muhammad bin Saud ambaye ndiye babu mkuu wa kizazi cha Saud (wafalme wa Saudi Arabia). Muhammad bin Abdul-Wahabi alipofika hapo, akatembelewa na mtawala huyo na akakirimiwa vizuri na kuahidiwa kutendewa mema. Naye kwa upande wake alimpa bishara mtawala huyo kwamba, ataitawala miji yote ya Najdi. Hivyo ndivyo yalivyotimia maafikiano ya wawili hawa, katika kutekeleza maovu yao dhidi ya Uislamu.

Ukweli ulivyo kuhusu watu wa Dir'iyya ni kwamba, watu hawa walikuwa ni masikini mno mpaka kipindi alichofika Muhammad bin Abdul-Wahabi na kufanya mapatano ya kusaidiana baina yake na Muhammad bin Saud. Anasema Ibn Bishri An-Najdi kama alivyopokea kutoka kwake Al-Alusi: "Watu wa Dir'iyya zama hizo (kabla ya kufika huko Muhammad bin Abdul-Wahab) walikuwa katika dhiki na taabu ya maisha, kwa hakika nilipata kushuhudia dhiki yao ya maisha hapo mwanzoni, na kisha baadaye katika utawala wa Suud, niliwaona wakaazi wale wale wa Dir'iyya wakiwa na mali nyingi na silaha zilizorembeshwa kwa dhahabu na fedha. Pia nikawaona wakiwa na farasi wazuri, vyombo vizuri na mavazi ya fahari na mambo mengine ambayo ni katika kuonyesha kuwa hali yao ya utajiri sasa imekuwa bora kiasi cha kushindwa kutaja kila kitu kwa ubainifu. "Wakati fulani niliona katika kipindi cha mkusanyiko mkubwa wa watu wa Ad-Dir'iyya (siku ya soko) makundi ya wanaume wakiwa upande mmoja, na makundi ya wanawake yakiwa upande mwingine. Basi katika makundi haya niliona vitu mbali mbali ikiwemo dhahabu, fedha, silaha, ngamia, mbuzi, farasi na mavazi ya fahari pamoja na vitu vingine vingi visivyoweza kutajwa kutokana na wingi wake, isitoshe uwingi wa watu waliokuwepo hapo ulikuwa unatazamika hadi upeo wa macho.

Nami nilikuwa nazisikia sauti za wauzaji na wanunuzi zikivuma kama mvumo wa kundi Ia nyuki.[1] Sasa basi, utajiri huu mkubwa wa Ad-Dir'iyya umetokea wapi? Ibn Bishri An-Najdi hakufichua siri hii; lakini historia inaonyesha kuwa Muhammad bin Abdul-Wahab ndiye aliyekuwa akizipata mali hizo kwa kupitia mashambulizi yake ya kuvizia yeye na wafuasi wake dhidi ya miji ya Kiislamu ambayo ilikuwa ikipinga kukubaliana naye na kumtii. Hivyo basi, akawa anapora mali na milki ya miji hiyo na kuigawa kwa watu wa Ad-Dir'iyya. Katika kugawa mali alizozipora kutoka kwa waislamu waliokataa kumtii, Muhammad bin Abdul-Wahabi alikuwa akitumia njia ya pekee aliyojipangia, kwani ugawaji wake ulikuwa ni kwa namna apendavyo yeye. Wakati mwingine alikuwa akigawa mali hiyo baina ya watu wawili na watatu miongoni mwa wafuasi wake ijapokuwa mali hiyo ilikuwa nyingi. Ama mtawala wa Najdi yeye alikuwa akichukua fungu lake kwa ridhaa ya Muhammad Bin Abdul-Wahab mwenyewe.

1. Tarikh An-Najdi cha Al-Alusi, uk. 117 - 118.

Na katika mambo muhimu yanayoonyesha uasi wa Muhammad bin Abdul-Wahab, ni sera hii mbaya aliyowafanyia Waislamu waliokataa kutii matamanio yake na rai zake; akawa anawatendea nambo yanayostahiki kufanyiwa kafiri anayeupiga vita Uislamu. Bwana huyu alihalalisha mali za Waislamu ziporwe na heshima zao zivunjwe. Kwa kifupi, Muhammad bin Abdul-Wahabi alikuwa akilingania watu Tauhidi ya Mwenyezi Mungu, lakini Tauhidi aliyokuwa akiilingania yeye ilikuwa isiyo na maana sahihi; kwa sababu ilitokana naye mwenyewe, wala siyo ile Tauhidi inayolinganiwa katika Qur'an.

Ikawa yule anayekubali Tauhidi yake husalimika nafsi yake na mali yake, ama anayekataa basi huambiwa kuwa ni kafiri anayeupiga vita Uislamu, na kumwaga damu yake na kuchukua mali yake inatangazwa kuwa ni halali. Wafuasi wa Muhammad Abdul-Wahab wakawa wanazusha vita katika Najdi na nje ya Najdi, kama vile Yemen, Hijaz na sehemu za Syria na Iraq. Na kila mji waliyouteka, walikuwa wakiruhusu kufanya katika mji huo mambo yoyote wayapendayo; kiasi kwamba kila walipoweza kuiunganisha miji hiyo kwenye utawala wao waliiunganisha, na kama hawakuweza basi walitosheka na uporaji wa mali peke yake.[1]

Vile vile Muhammad ibn Abdul-Wahab alimuamuru kila aliyehadaika na wito wake huo wa Tauhidi potofu afike kwake na kula kiapo cha utii (Bai'ah); na yeyote atakayekataa ni lazima auawe na mali yake igawiwe. Na kwa sababu hii, aliwashambulia watu wa kijiji cha Al-Fusul kilicho pembezoni mwa Al-Ahsa, akawaua watu mia tatu na akapora mali zao.[2][19] Ulipofika mwaka 1206 A.H. Muhammad ibn Abdul-Wahab alifariki dunia lakini wafuasi wake waliendeleza uzushi wake na upotovu wake. Na ilipokuwa mwaka 1216 Wahabi Amir Suud aliandaa jeshi kubwa lipatalo watu elfu ishirini, wakafanya mashambulizi ya kinyama katika mji mtukufu wa Karbala nchini Iraq. Mji wa Karbala ni mji mtukufu tangu hapo zamani mpaka sasa, na unao umaarufu mkubwa na mapenzi kwa waumini, na watu haukusudia kwa ajili ya ziyara kutoka sehemu mbali mbali na mataifa tofauti tofauti wakiwemo Wairan, Waturuki, Waarabu na wengineo.

Majeshi hayo ya Kiwahabi, yaliuzingira mji huu mtukufu na kufanya mauaji mengi na kupora mali, kuubomoa na kufanya kila aina ya uovu. Kwa hakika Mawahabi kwa kuishambulia Karbala tukufu walitenda jinai kubwa na walileta msiba usio mfano, kwani waliwaua watu wapatao elfu tano au zaidi, mpaka yasemekana waliwauwa watu wapatao elfu ishirini. Baada ya Amir Suud kumaliza mashambulizi ya kivita dhidi ya wakazi wa mji wa Karbala, alielekea kwenye Haram Tukufu ya Imam Husein bin Ali [a.s], ambayo ilikuwa imejaa hazina mbali mbali nzuri na zawadi nyingi za thamani zilizotolewa na wafalme mbali mbali na Maamiri pamoja na watu wengine kwenye uwanja mtukufu wa Kaburi Ia Imam Husein [a.s] nazo akazipora.

Baada ya msiba huu unaoumiza roho, mji wa Karbala ulionekana wazi kuwa umekumbwa na huzuni kubwa na masikitiko kutokana na unyama uliofanywa na Mawahabi. Hali hii iliwatawanya washairi wengi wa

1. Jazira Al-Arab Fil-Qarnil-Ishriin, uk 341.
2. Tarikh AI-Mamlakatul Arabiyya As-Suudiyya, Juz. 1 uk. 51.

Kiislamu watunge Mashairi ya kuomboleza msiba ulioufika mji huu Mtukufu wa Karbala.[1] Siyo tu kwamba Mawahabi walitosheka na shambulio hilo la kwanza dhidi ya mji wa Karbala na viunga vyake, bali waliendelea kufanya mashambulizi mara kwa mara karibu muda wa miaka kumi na miwili. Pia Mawahabi walikuwa wakiushambulia mji Mtukufu wa Najaf na kufanya uporaji, na kama tulivyokwisha sema, shambulio la mwanzo dhidi ya Karbala lilikuwa mwaka 1216 A.H.

Waandishi wa Kishia wameafikiana kwamba, tukio hilo Ia mashambulizi dhidi ya mji wa Najaf lilifanyika siku ya kumbukumbu ya Ghadir ambayo Mtume **[s.a.w.w]** alimbainisha Imam Ali bin Abi Talib kuwa ndiyo Khalifa wake baada ya kuondoka kwake yeye Mtume **[s.a.w.w]**. Ili kuifahamu kumbukumbu ya Ghadir, rejea: Kitabu cha Al-Ghadir cha Al-Aminiy, Juz. 1. Anasema Marhum Al-Allamah As-Sayyid Jawad Al-'Amili kuhusu mauaji yaliyofanywa na Mawahabi huko Karbala na Najaf: "Hakika Mwenyezi Mungu kwa hisani yake na fadhila zake pia kwa baraka za Mtume Muhammad na kizazi chake amejalia kutimia kwa Juzuu hii ya kitabu, "Miftah Al-Karamah" "usiku wa manane kuamkia tarehe tisa ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani mwaka 1225 A.H. kwa mkono wa mwandishi wake..... (kazi hii ya kuandika kitabu hiki nimeifanya kutokana na ushawishi wa kimawazo pia kutokana na hali ya mambo kuharibika". Anaendelea kusema:

"Kwa hakika mabedui wenye imani za Kiwahabi kutoka Unaizah, (ambao wamekwisha toka katika Uislamu) waliuzingira mji mtukufu wa Najaf na kaburi la Imam Husein [a.s] katika Karbala, wakazifunga njia zote kisha wakawapora watu waliokuwa wakitoka kumzuru Imam Husein [a.s] katika ziyara ya nusu ya mwezi wa Shaaban, wakawaua watu wengi, na wengi waliouawa walikuwa Waajemi. Yawezekana idadi ya watu waliouawa ilikuwa mia moja na hamsini na pengine chini ya idadi hiyo kama inavyosemekana."[2]

Kwa ujumla, Tauhidi aliyokuwa akiilingania Muhammad ibn Abdul-Wahabi na kundi lake ilikuwa ni ile isemayo kwamba "Mwenyezi Mungu ana mwili wenye viungo na anapo mahala pake maalum (na walikuwa wanahalalisha damu na mali za wenye kupinga kauli yao hiyo)". Bwana Al-Alusi anasema kuhusu Tauhidi ya Mawahabi: "Mawahabi wanaziamini hadithi zisemwazo kuwa zimetoka kwa Mtume **[s.a.w.w]** kwamba, Mwenyezi Mungu hushuka hadi kwenye mbingu ya dunia kisha hauliza, "Je, kuna yeyote mwenye kutaka msamaha?"[3].

Al-Alusi anaendelea kusema: "Mawahabi wanaitakidi pia kwamba, Mwenyezi Mungu atakuja siku ya Qiyama kama alivyosema katika Qur'an "Waja'a Rabbuka Wal Malaku Saffan Saffa", na wanaammi kwamba Mwenyezi Mungu hujisogeza kwa viumbe vyake namna apendavyo kama alivyosema katika Qur'an: "Nasi tuko karibu mno na binadamu kuliko mshipa wa shingo yake".[4] Katika kitabu cha Ibn Taymiyyah kiitwacho "Ar-Radd AlalAkhnaiy", kana ushahidi ulio wazi kwamba, yeye Ibn Taymiyyah

1.Tarikh Karbala, Dr. Abdul Jawad.
2. Miftah al-Karamah, Juz. 7, uk. 653.
3. Tarikh Najd, uk. 90-91.
4. Sura al-Fajr, Aya 23, na Sura Qaf, Aya 16.

alikuwa akiitakidi hadithi zilizopokelewa kuhusu fadhila za kumzuru Mtume **[s.a.w.w]** kuwa ni za uzushi, na kwamba anyeitakidi kuwa mjumbe wa Mwenyezi Mungu yu hai baada ya kufariki kwake kwa uhai kama ule wa zama alipokuwa duniani, basi mtu huyo atakuwa katenda dhambi kubwa. Na hivi ndivyo anavyoitakidi Muhammad ibn Abdul-Wahabi na wafuasi wake; lakini hawa wamezidi mno kuliko Ibn Taimiyyah katika upotovu na kuvuruga. Itikadi hizo mbovu za Kiwahabi zimekuwa ni sababu ya kuwafanya watu wanaotafiti juu ya dini ya Kiislamu kwa kupitia vitabu vya Mawahabi, wauone Uislamu kuwa ni Dini isiyo ya maendeleo na wala haiwezi kutegemewa kukidhi mahitaji ya maisha ya watu katika nyakati zote.

Mmarekani mmoja aitwaye "Lutrub Studard" anasema: 'Walisimama katika misingi hiyo watu wengi wanaoukosoa Uislamu, wakayafanya Madh-hebu ya Uwahabi kuwa ni ushahidi wa maneno yao wakasema, 'Hakika Uislamu kwa asili yake na mazingira yake, haukubali mabadiliko kulingana na wakati, wala haukubali maendeleo na mabadiliko ya hali, na Uislamu hauwezi kuwa tumaini katika maisha".[1]

Inapasa kusemwa kwamba wanachuoni wa Madh-hebu ya Hanbal tangu hapo mwanzo walimpinga Muhammad ibn Abdul Wahab na kupitisha uamuzi kuwa yeye amepotea, na kwamba hizo itikadi zake siyo sahihi. Na mtu wa kwanza kumpinga Muhammad ibn Abdul-Wahabi na kutangaza vita dhidi yake, alikuwa ni baba yake, kisha ndugu yake aliyekuwa akiitwa Sheikh Suleiman, na wawili hawa walikuwa ni wanachuoni wa Kihanbal. Ama huyu Sheikh Suleiman yeye aliandika kitabu cha kuzipinga itikadi za Muhammad ibn Abdul-Wahabi kiitwacho "As-Sawaiqul-llahiyyah Fi Araddi Al-Wahabiyyah". Ndani ya kitabu hicho amezipinga itikadi potofu na uzushi wa nduguye. Mufti wa Kis-Shafi'i katika Makka, Ash-Shaykh Zaini Dahlan, anasema kama ifuatavyo:- "Mzazi wa Muhammad ibn Abdul-Wahab ambaye ni Sheikh Abdul-Wahab, alikuwa ni mtu mcha Mungu miongoni mwa wanachuoni, naye Sheikh Suleiman ambaye ni ndugu wa Muhammad ibn Abdul-Wahab vile vile alikuwa miongoni mwa wanachuoni. Kwa kuwa Sheikh Abdul-Wahab na Sheikh Suleiman, toka hapo mwanzo walikuwa wakizifahamu fikra potofu za Muhammad ibn Abdul-Wahab hasa pale alipokuwa akiendelea na masomo yake huko Madina, walikuwa wakimlaumu na kuwatahadharisha watu kutokana naye."[2].

Naye Abbas Al-'Aqqad Al-Misri anasema: "Mpinzani mkubwa wa Muhammad ibn Abdul-Wahab ni nduguye aliyekuwa akiitwa Sheikh Suleiman, ambaye ndiye mwandishi wa kitabu kiitwacho "As-Sawaiqul Ilahiyya". Sheikh Suleiman hakukubaliana kuwa nduguye (Muhammad ibn Abdul-Wahab) eti alikuwa amefikia daraja ya ijtihadi na akaweza kuifahamu Qur'an na Sunna. Na kwa maoni ya Sheikh Suleiman ni kwamba, zile bid'ah ambazo maimamu walikuwa wakiziona karne baada ya karne na hawamkufurishi mwenye kuzitenda, basi sisi hatuna haki ya kumkufurisha

1. Hadhir al-Islami, juz. 1, uk. 264.
2. Al-Futuhatul Islamiyya, Juz. 2, uk. 357.

mtu kwa sababu ya hizo bid'ah wala hatuwezi kuhalalisha vita dhidi ya watu wanaotenda matendo hayo.

Anasema tena Sheikh Suleiman: "Mambo haya yalikuwepo sika nyingi hata kabla ya Imam Ahmad ibn Hanbal katika zama za Maimamu wa Kiislamu, na wenye kuyapinga waliyapinga miongoni mwa maimamu hao, na yaliendelea kuwepo mpaka yakaenea katika miji yote ya Kiislamu. Na matendo yote haya ambayo ninyi Mawahabi mnawakufurisha watu kwa kuyatenda, haikupokewa kutoka kwa Maimamu wa Waislamu kwamba, wao walimkufurisha mtu kwa ajili hiyo, wala hawakusema eti watendao matendo haya wameritadi, na wala maimamu hao hawakuamuru kuwapiga vita watendao mambo haya, wala hawakuiita miii ya Waislamu kuwa ni miji ya shirki na vita kama msemavyo ninyi; bali ninyi mmezidi mno kiasi cha kumkufurisha hata mtu asiyewakufurisha watu watendao haya japokuwa yeye mwenyewe hakuyatenda".[1]

Ni wazi kabisa kwamba, Muhammad ibn Abdul-Wahab siyo mtu wa mwanzo kutoa hizo rai zake na fikra zake azitoazo, bali yule aliyemtangulia tangu karne nyingi zilizopita ambaye ni Ibn Taymiyyah al-Harrani pamoja na mwanafunzi wake aitwaye Ibnul-Qayyim Al-Jauziyyah, na wengineo kama hawa, fikra za wote hawa hazikuanzisha madhehebu kama alivyozusha jambo hilo mwana wa Abdul Wahab.

1. Al-Islam Fil-Qarnil-Ishriin, uk. 108-109.

3

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## IBNU TAYMIYYAH NI NANI?

Bwana huyu alikuwa hi miongoni mwa wanachuoni wa Kihanbal, na alifariki mwaka 728 A.H. Jina lake ni Abu'l-'Abbas Ahmad bin 'Abdul-Halim, anayejulikana sana kwa jina la Ibnu Taymiyyah. Kutokana na rai zake mbovu, na fikra zake zilizo kinyume na itikadi za Waislamu (pamoja na kuwepo tofauti ya kimadhehebu baina yao) Wanachuohi wa zama zake walikuwa wakimpinga na kutangaza vita dhidi yake, isitoshe walimhukumu kuwa hi fasiki (mharibifu wa Dini) na hasa pale alipoandika vitabu vinavyoeleza itikadi zake na akavisambaza miongonini mwa watu. Vita vya kidini dhidi ya Ibnu Taymiyyah vilikuwa katika pande mbili muhimu: Kwanza: Utunzi wa vitabu kupinga fikra zake potofu na kuzitengua kwa mujibu wa Qur'an na Sunna Tukufu ya Mtume **[s.a.w.w]**. Kwa mfano, tunataja baadhi ya vitabu vilivyotungwa na kutolewa dhidi ya Ibnu Taimiyyah:

1). Shifa's-Saqam Fi Ziyarati Qabril-Imam: kimeandikwa na Taqiyu'd Din Subaki.

2). Ad-Durrah Al-Mudiyyah Fi 'r-Raddi Ala Ibni Taimiyyah: kimeandikwa na mtunzi wa kile cha kwanza.

3). Al-Maqalatu'l-Mardiyyah: kimetungwa na Qadi'l-Qudat Al-Malikiyyah Taqiyu'd-Din Abi 'Abdillah Al-Akhnai.

4) Najmu'l-Muhtadi wa Rajmul-Muqtadi, kilichoandikwa na Fakhr bin Muhammad Al-Qurashi.

5). Daf'us'h-Shubhah, kimeandikwa na Taqiyu'd-Din Al-Hisni.

6). At-Tuhfatu'l-Mukhtarah Fi'r Raddi Ala Munkiri'z-Ziyarah, kimeandikwa na Taju'd-Din.

Hivi ni baadhi ya vitabu vilivyoandikwa dhidi ya itikadi na rai mbovu za lbn Taimiyyah, na vilidhihirisha ubovu wa itikadi hizo pamoja na ubaya wake.

Upande wa pili kuhusu vita dhidi ya Ibn Taimiyyah, ni hujuma dhidi yake zilizokuwa zikifanywa na wanachuoni wa zama zake, ikiwa na pamoja na kutoa Fatwa kuwa yeye Ibn Taimiyyah hi fasiki, na wakati mwingine walimhukumu kuwa ni kafiri, pia wakiwatahadharisha watu juu ya uzushi aliouzusha katika dini tukufu ya Kiislamu. Miongoni mwa Wanachuoni hao ni Qadi 'l-Qudat Al-Badru ibn Jama'ah wa Misri, yeye aliandikiwa suala kuhusu rai ya Ibn Taimiyyah juu ya kufanya ziyara ya kumzuru Mtume **[s.a.w.w]** kuwa haifai. Qadi huyu aliandika jawabu lifuatalo: "Kwa hakika kumzuru Mtume **[s.a.w.w]** ni jambo la Sunna iliyosisitizwa, na wanachuoni wameafikiana katika jambo hili; na yeyote anayeona kuwa kumzuru Mtume ni haramu, ni wajibu juu ya Wanachuoni kumkemea na kumkataza aondokane na mawazo ya aina hii; na iwapo hataachana na mawazo hayo, basi itakuwa ni lazima kumfunga na kumfedhehesha mbele za watu ili wasimfuate".

Qadi huyu wa Kishafi'i wa Misri siyo yeye peke yake aliyetoa Fatwa ya aina hii, bali Maqadhi wa Madhehebu ya Maliki na Hanbal nao walitoa Fatwa zinazofanana katika kuonyesha uovu wa Ibn Taimiyyah na

wakahukumu kuwa yeye ni mpotevu. Katika kutilia nguvu maelezo yaliyotangulia hivi punde, mwanachuoni aitwaye Adh-Dhahabi ambaye anazingatiwa kuwa miongoni mwa wanachuoni wakubwa katika Karne ya Nane Hijiriyya (alitunga vitabu vingi vya maana mno katika hadithi na wapokezi wa hadithi, na aliishi katika zama zile zile za Ibn Taimiyyah) alimuandikia Ibn Taimiyyah barua ya nasaha, akamkataza mambo yake hayo mabaya na alimfananisha (kutokana na uovu wake huo) kwa Al-Hajjaj Ath-Thaqafi katika uovu na upotevu wake.[1]

U'ipofikamwaka 728 Hijiriyya Ibn Taimiyyah alifariki katika gereza Ia Shamu, na mwanafunzi wake aitwaye Ibn Al-Qayyim akajaribu kuendeleza mwenendo wa mwalimu wake lakini hakufaulu. Jambo la kuhuzunisha sana ni kwamba, shetani aliutega mtego wake kwa mara nyingine alipokuja Muhammad ibn AbdulWahab, hali ya kuwa amezibeba fikra za Ibn Taimiyyah zilizokuwa zimetoweka, akaafikiana yeye na kizazi cha Wasaudi kwamba, kila mmoja amsaidie mwenziwe, mmoja ashike mambo ya utawala na mwingine ashike mambo ya dini. Basi kipindi hiki upotovu ukawa umerudi na kueneza mizizi yake katika nchi ya Najdi, hivyo basi Uwahabi ukaenea katika nchi hiyo mfano wa maradhi mabaya ya Kansa katika mwili.

Watu wengi walihadaika na wakuanzisha kundi lao; inasikitisha sana kusema kwamba walitumia nembo ya Tauhidi ili kuwaua watu wa Tauhidi, na walimwaga damu za Waislamu kwa madai ya kuwapiga vita washirikina. Maelfu ya watu, wanaume na wanawake, wakubwa kwa wadogo, walijitolea muhanga dhidi ya uzushi huu. Kwa hiyo mfarakano baina ya Waislamu ulipanuka; na likaongezeka dhehebu jipya kwenye madhehebu mengi ya Kiislamu yaliyokuwepo hapo kabla. Na msiba huu mkubwa ulifikia kilele chake wakati miji miwili mitukufu ya Makka na Madina ilipoangukia mikononi mwa kundi hili ovu Ia Kiwahabi. Hivyo basi, Mawahabi kutoka Najdi walijiimarisha kwa kupewa msaada na Serikali ya Uingereza ambayo kwa chuki yake dhidi ya Uislamu, sika zote ilikuwa ikikusudia kuigawa dola ya Kiislamu (iliyokuwa chini ya ukhalifa wa Kiturki), na kuifanya kuwa vijidola vidogo vidogo ambavyo vitatenganishwa na mipaka ya kijiografia. Mawahabi walikusudia kuondoa kumbukumbu zote za Kiislamu zilizokuwepo Makka na Madina, na kuyabomoa makaburi ya Mawalli wa Mwenyezi Mungu na kukiondolea heshima kizazi cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, pamoja na mambo mengine maovu na machafu (waliyoyatenda Mawahabi) ambayo hutetemesha nafsi ya Muislamu.

Baadhi ya wanahistoria wanasema: "Jambo la kwanza walilolifanya Mawahabi haraka haraka baada ya kuiteka Makka ni kuchukua na shoka na kuibomoa Mualla (makaburi ya Maqureish) ambapo palikuwa na qubba nyingi za watukufu wa Kiislamu. Miongoni mwa Maqubba hayo lilikuwa ni qubba la Sayyidina Abdul-Mutalib ambaye ni babu yake Mtume **[s.a.w.w]**, na qubba Ia Sayyidina Abu Talib (r.a.) ami yake Mtume, pia qubba la Bibi Khadija (r.a) mkewe Mtume **[s.a.w.w]**. Vile vile walibomoa jengo alimozaliwa Mtume **[s.a.w.w]**, na lile la Abubakr na mahala alipozaliwa Imam Ali [a.s], na wakabomoa Qubba la Zam-zam lililokuwa pembeni ya Al-Ka'bah; pia walifuatilia kila mahali zilipo kumbukumbu za watu wema

1. Takmilat As-Saif Asaqil, uk. 190.

wakazibomoa". "Wakati wakibomoa walikuwa wakiimba na kupiga ngoma na kuyashutumu makaburi... kiasi yasemekana kwamba baadhi yao walilikojolea kaburi la Bwana Mpendwa.....!![1]

Amesema mwanachuoni mkubwa aitwaye As-Sayyid Sadru'd-Din As-Sadr (Mwenyezi Mungu amrehemu) kwamba: "Naapa kwa 'umri wangu kwa hakika tukio la (kubomolewa makaburi ya) Baqii' huzifanya kuwa kongwe nyoyo za watoto wachanga." "Huenda (tukio hili) likawa ndiyo mwanzo wa kufikwa na misiba (mfululizo) ikiwa (waislamu) hawatazinduliwa kutoka katika usingizi (walionao)". "Je, hayuko Muislamu awezaye kuzichunga haki za Mtume, aliye kiongozi na muombezi wetu (kwa ajili ya Mwenyezi Mungu)?" Amesema msha'iri mwingine: "Wameangamia wajukuu wa Mayahudi (yaani kizazi cha Saudi) kwa matendo waliyoyatenda, hawakupata isipokuwa fedheha. Wameitweza heshima ya Mtume Muhammad kuhusu kizazi chake. Ole wao, watapata adhabu kali kwa kumuasi Mwenyezi Mungu mwenye nguvu. Wameyabomoa makaburi ya watu wema kutokana na chuki walizo nazo, kwa hakika wameangamia na wamemchukiza Mtume **[s.a.w.w]**." Kufuatia kauli yake Mtume **[s.a.w.w]** kwamba:

"Pindi bid'ah itakapodhihiri, basi ni wajibu kwa Mwanachuoni kudhihirisha elimu yake (kupingana kukemea bid'ah hizo) na iwapo hatafanya hivyo, basi laana ya Mwenyezi Mungu imshukie mwanachuoni huyo". Kwa hiyo basi wanachuoni wengi wa Kishia na wale wa Kisunni walijitokeza (kupinga na kukemea uzushi wa Kiwahabi), kama tulivyokwisha taja hapo kabla, waliandika vitabu na kuvitawanya ili kumfedhehesha mtu huyu (Muhammad ibn Abdul Wahabi) ambaye alikuja kutekeleza malengo ya Waingereza, akiwa amevaa ngozi ya kondoo; na walizifichua siri zake kwa kuidhihirisha asili yake pia walizipinga na kuzikemea fikra zake mbaya. Kitabu cha kwanza kutolewa dhidi ya Muhammad ibn Abdul Wahab ni "As-Sawa'iqul Ilahiyyah fi'r Raddi 'Al Wahabiyyah", kilichoandikwa na Sheikh Suleiman ambaye ni ndugu wa Muhammad Abdul Wahabi.

Kadhalika kwa upande wa Kishia, kitabu cha kwanza kutolewa dhidi ya Muhammad ibn Abdul-Wahabi ni "Man-haju 'r-Rashad" kilichoandikwa na mwanachuoni mkubwa aitwaye Sheikh Ja'far Kashif Al-Ghita' aliyefariki mwaka 1228 A.H. Sheikh Kashif Al-Ghita' alikiandika kitabu hiki kuwa ni jawabu la barua iliyotumwa kwake na mmoja wa Maamiri wa Kisuud katika wakati huo aliyekuwa akiitwa Abdul-'Aziz ibn Su'ud. Ndani ya kitabu hicho Sheikh Kashif Al-Ghita' ameudhihirisha wazi uwongo wa fikra za Muhammad ibn Abdul-Wahab, na amethibitisha ubatili (ubovu) wa fikra hizo kwa mujibu wa Qur'an na Sunna.

Kitabu hicho kilichapishwa katika mji mtukufu wa Najaf (Iraq) mwaka 1343. Baadaye ulifuatia ukosoaji na kukemea itikadi za Kiwahabi katika nyakati mbali mbali, na vikatolewa vitabu mfululizo kimoja baada ya kingine mpaka katika zama zetu hizi. Na wakati huu Mawahabi wamezielekeza hujuma zao zenye hatari kubwa dhidi ya Uislamu na Waislamu kwa kutumia mali zao nyingi ambazo kizazi cha Wasuud

1. Kashful Ir-tiyabi kama alivyonakili kwa Al-Jabrati.

kinazipata kutokana na mauzo ya mafuta ambayo faida yake yote hurejea kwenye kizazi hiki cha Wasuud peke yao. Watawala wavamizi wa Kisuud wametenga fungu kubwa Ia pesa zinazotokana na mauzo ya petroli kwa ajili ya kuyaeneza Madhehebu yao yaliyotoka Uingereza miongoni mwa Waislamu, na pia kuyaimarisha na kuyalinda madhehebu hayo. Lau isingekuwa mali hizi nyingi, madhehebu haya duni yaisingeweza kabisa kudumu mpaka wakati huu. Kwa hakika wakoloni ndani ya madhehebu haya wamekipata walichokuwa wanakitafuta, nao wameyatumia kuwa ndiyo njia bora ya kuleta mgawanyiko baina ya Waislamu na kuvunja umoja wao na kuwafanya wapigane wao kwa wao.

Na Madhehebu haya yametekeleza na kutimiza malengo ya wakoloni waovu wa Kiingereza, kwani utaona kuwa yamezusha ugomvi kati ya Waislamu; imekuwa Mwislamu huyu humuona Mwislamu yule kuwa ni fasiki na mwingine naye humkufurisha. La hawla wala Quwwata Illa Billahil 'Aliyyil 'Azim. Ewe msomaji mtukufu, kwa kweli tumekusudia katika kitabu hiki kuzichambua kwa utafiti wa kina itikadi za Kiwahabi, na tutafichua kiini chake mpaka ikudhihirikie kwamba itikadi za Waislamu zimetegemea Qur'an na Sunna tukufu, na kwamba itikadi za Kiwahabi zinakwenda kinyume cha Qur'an na Sunna ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]**, nasi tumetumia njia ya kufupisha maelezo lakini yanayoeleweka.

## MAWAHABI NA QADHIA YA KUJENGEA MAKABURI YA MAWALII

Kwa mujibu wa fikra ya Mawahabi, kujengea na kuimarisha majengo juu ya makaburi ya Manabii, Mawalii na Wachamungu ni miongoni mwa mambo yasiyoweza kuvumiliwa. Ibn Taimiyya na mwanafunzi wake Ibn Al-Qayyim, ni watu wa kwanza kutoa fatwa ya kuharamisha ujenzi huu na kwamba ni wajibu kuyabomoa majengo hayo. Ibn Al-Qayyim anasema: "Ni wajibu kuyabomoa majengo ambayo yamejengwa kwenye makaburi, na wala haifai kabisa kuyaacha japo siku moja kila itakapowezekana kuyabomoa na kuyaondoa."[1] Katika mwaka wa 1344 A.H., baada ya watawala wa kizazi Ili kufanikisha azma yao, watawala hawa waliwauliza maswali wanachuoni wa Madina kwa kuwataka wanachuoni hao watoc fatwa inayoharamisha kujengca makaburi, na pia kufanya kila mbinu kuutakasa msimamo wa watawala wa Kisuud mbele ya mtazamo wa Waislamu wengine, na hasa katika nchi ya Hijazi. Na hii ilitokana na ukweli kwamba, Waislamu wa Hijazi (nchi ambazo zimo Makka na Madina) walikuwa na msimamo kama Waislamu wengine ulimwenguni kuhusu jambo hili, na walikuwa wakiitakidi utukufu wa Mawalii wa Mwenyezi Mungu na kuwaheshumi, pia walikuwa wakikubali kuyajengea makaburi yao. Kwa hiyo 'Mawahabi wakajaribu kuingiza maovu yao kwa kulitumia vazi la Uislamu, ili wazuie shutma na lawama kutoka kwa Waislamu!!! Subhanallah!!!

Watawala wa Kisaud walimtuma Qadhi Mkuu wa Najdi Suleiman ibn Balhiid aende Madina ili akatake fatwa kwa wanachuoni wa Madina juu ya kujengea makaburi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu. Lakini ni lazima

1. Zaadul-Maad fil Hudaa Khairil-anam, uk. 661.

kueleza kwamba, maswali aliyoyauliza ibn Balhiid yalikuwa yanayo majibu ndani yake ambayo yanaafikiana na mtazamo halisi wa Kiwahabi. Hivyo basi wanachuoni hao hawakuwa na la kufanya ila kujibu kama maswali yenyewe yalivyo. Na wanachuoni hao wa Madina hawakuwa na ushujaa au ujasiri wa kuweza kuitangaza haki kwa kutoa fatwa iliyo sahihi, hasa kwa sababu ya wao kuwa ni watu ambao riziki zao walikuwa wakizipata kupitia milango ya watawala siku zote, na walikuwa wakifahamu tangu mwanzo kwamba, kutoa fatwa kinyume cha mtazamo wa watawala kutawasababishia kutuhumiwa kuwa ni makafiri na ni washirikina, na watahukumiwa kuuawa iwapo watakataa kutubia. Katika Mwezi wa Mfunguo Mosi Mwaka 1344 A.H., jarida liitwalo "Ummul Quraa" linalotolewa huko Makka, lilichapisha maswali na majibu kati ya Qadhi Ibn Balhiid na wanachuoni wa Madina.

Kwa hakika kuchapishwa kwa maswali hayo kulizusha zogo na kelele nyingi miongoni mwa Waislamu, Mashia na Masunni wote; kwani walikuwa wakifahamu wazi kwamba matokeo ya fatwa hii ambayo imetolewa chini ya maafikiano yenye vitisho, yatakuwa ni kubomoa Maquba na majengo yaliyojengwa kwenye makaburi ya viongozi wa Uislamu na watu watukufu katika Uislamu. Na hayo ndiyo yaliyotokea. Na baada tu ya fatwa hii kutolewa na hao wanachuoni wa Madina wapatao kumi na tano, na ikaenea fatwa hiyo katika nchi ya Hijazi, utawala wa Kiwahabi ulianza kuyabomoa makaburi ya kizazi cha Mtume wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]**, mnamo tarehe nane ya mfunguo mosi mwaka ule ule, na uliondosha kumbukumbu za kizazi cha nyumba ya Mtume **[s.a.w.w]** na Masahaba, pia walipora kila kilichokuwemo katika haram hivo tukufu yakiwemo mazulia ya thamani na vitu vingine vya thamani.

Kikundi hiki cha wakorofi kikaugeuza uwanja mtukufu wa Baqi' kuwa ardhi tupu yenye kuhuzunisha. Katika maelezo yafuatayo tutataja sehemu ya namna maswali yalivyoulizwa na lbn Balhiid; ili ufahamu ni namna gani muulizaji alivyoyatayarisha majibu katika masuali yake na utafahamu pia kwamba lengo halikuwa kuuliza na kutaka fatwa, bali ilikuwa ni kutaka kupatikane kuungwa mkono na kuupotosha mtazamo wa Waislamu wote, na pia kuziangamiza kumbukumbu za Unabii na Utume. Lau lengo lingekuwa ni kutaka fatwa ya kweli na kufahamu mtazamo wa uislamu, basi nini maana ya kuingiza majibu ndani ya maswali wakati wa kutaka fatwa hivo? Bali sisi tunadhani kwamba maswali na majibu yote yalikuwa yameandaliwa tangu hapo mwanzo katika karatasi maalum, kisha karatasi hiyo ilitumwa kwa hao wanachuoni wa Madina ili kutia saini tu.

Vinginevyo haiingii akilini kuwa, eti wanachuoni wa Madina kubadilisha muelekeo wa mtazamo wao ghafla na wakatoa fatwa kuharamisha kujengea kwenye makaburi na kuwa eti ni wajibu kuyabomoa, hali ya kuwa wakifahamu kwamba, wao na wazee wao waliyokwisha pita walikuwa wakilingania kuzihifadhi kumbukumbu za Mtume, na pia wakiyazuru majengo hayo matakatifu. Ibn Balhiid anasema katika maswali yake hayo: "Ni ipi kauli ya wanachuoni wa Madina (Mwenyezi Mungu na awazidishie fahamu na elimu) juu ya (uhalali) wa kujenga kwenye makaburi na kisha kuyafanya majengo hayo kuwa ni Misikiti, je jambo hili linafaa au hapana?" "Na iwapo haifai bali ni jambo linalokatazwa sana sana, basi je, ni wajibu kuyabomoa na kuzuia watu wasisalie mahala hapo au hapana?"

"Na kama jengo litakuwa kwenye ardhi iliyowekwa wakfu kama vile "Baqi", hali ya kuwa linazuia kuzika maiti mwingine katika nafasi iliyochukuliwa na jengo hilo, basi je kufanya hivyo itakuwa ni kupora sehemu hiyo, jambo ambalo ni wajibu kuliondosha kutokana na kuwa ni miongoni mwa dhulma dhidi ya wanaostahiki na kwamba itakuwa ni kuzuia haki yao au hapana?" Kwa kuwa maswali haya yaliulizwa hali ya kuwa wanachuoni hao wa Madina walikuwa chini ya vitisho, basi majibu yao kwa Sheikh Ibn Balhiid yakawa kama ituatavyo:

"Ama kujenga juu ya makaburi ni jambo ambalo limekatazwa kwa ijmai' kutokana na hadithi sahihi zilizokuja kukataza jambo hilo; na kwa hiyo basi wanachuoni wengi wametoa fatwa kuwa ni wajibu kuyabomoa majengo hayo wakitegemea hadithi ya Ali (r.a.) kwamba yeye alimwambia Abul-Hayyaaji, "Nakutuma kwa jambo ambalo Mtume wa Mwenyezi Mungu alinituma mimi nikalifanye, nalo ni kwamba usiliache sanamu lolote ila ulivunje, na wala usiache kaburi lolote lililonyanyuliwa ila ulisawazishe." Sheikh An-Najdi anasema katika makala iliyochapishwa na jarida la "Ummu'l-Quraa" katika toleo lake Ia Mwezi wa Mfunguo tisa Mwaka 1345 A.H. kwamba: "Hakika ku jenga maquba juu ya makaburi ya Mawalii ni jambo ambalo limekuwa likiendelea kuwepo tangu karne ya tano Hijiriyya." Naam: Hii ni baadhi ya mifano ya maneno ya Mawahabi kuhusu suala la kujenga juu ya makaburi. Na utaona kwamba mategemeo ya ushahidi wao katika kuharamisha kujengea makaburi ndani ya vitabu vyao na maandiko yao yako kwenye hoja mbili:

1. Wanadai kuna ijma'i ya wanachuoni wa Kiislamu juu ya kuharamisha jambo hilo.

2. Hadithi ya Abul-Hayyaaj aliyoipokea kwa Imam Ali [a.s], na zingine zinazofanana na hadithi hiyo.

Sasa hivi sisi tutazungumzia juu ya kujenga juu ya makaburi na kuyawekea paa na kusimamisha majengo kwenye makaburi hayo. Ama kuhusu suala la kuyazuru makaburi tutalizungumzia katika sehemu yake maalum "Mwenyezi Mungu apendapo". Kwa munasaba wa lile suala la kwanza (kuwa kuna ijma'i ya wanachuoni wa Kiislamu kuharamisha kujengea makaburi) tutalizungumzia katika vipengele vitatui:

1. Je, nini mtazamo wa Qur'an katika kujenga juu ya makaburi, naje, katika Qur'an jambo hili limebainishwa wazi?

2. Je, ni kweli kwamba umma wa Kiislamu umeafikiana juu ya uharamu wa kujenga juu ya makaburi? Au kujenga huku kumekuwa kukiendelea kuwepo katika

zama zote za Uislamu kuanzia wakati wa Mtume **[s.a.w.w]** na Masahaba?

3. Hadithi ya Abul-Hayyaaj inakusudia nini? Pia hadithi aliyopokea Jabir na Ummu Salamah na Na'im? Hadithi hizi ambazo Mawahabi wanatolea kama ushahidi wa mambo yao maovu.

## A: MTAZAMO WA QUR'AN KATIKA KUJENGA JUU YA MAKABURI

Qur'an haikuweka wazi hukumu ya kujenga juu ya makaburi; isipokuwa inawezekana kuifahamu hukumu yake kwa kupitia baadhi ya aya tukufu

ambazo zimelizungumzia jambo hili kiujumla. Hebu fuatilia ufafanuzi ufuatao:

## 1). KUJENGA JUU YA MAKABURI YA MAWALII NA KUVIHESHIMU VITU VITUKUFU VYA MWENYEZI MUNGU

Hakika Qur'an Tukufu inakichukulia kitendo cha kuheshimu mambo matukufu ya Mwenyezi Mungu kuwa ni dalili ya ucha Mungu (Utawa). Mwenyezi Mungu anasema:

ذَٰلِكَ وَمَن يُعَظِّمْ شَعَائِرَ اللَّـهِ فَإِنَّهَا مِن تَقْوَى الْقُلُوبِ ﴿٣٢﴾

"Na ye yote anayeziheshimu alama za Mwenyezi Mungu, basi kufanya hivyo ni miongoni mwa uchaji wa moyo." (Qur'an, 22:32).

Sasa tunajiuliza: Nini maana ya "taadhim sha'airillah?" Jawabu: "Sha'air" ni tamko la uwingi na umoja wake ni "Sha'irah", nalo lina maana ya dalili na alama, na wala haikuwa makusudio ya "Sha'air" katika aya hii kuwa ni alama zinazothibitisha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu, kwani ulimwengu wote ni dalili ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu. Mshairi mmoja anasema: "Katika kila kita kuna dalili inayojulisha kwamba Mwenyezi Mungu ni mmoja."

Kama ambavyo ni vema ifahamike kwamba hakuna ye yote anayesema kuwa, "kukiheshimu kila kita kilichoko ulimwenguni ni dalili ya ucha Mungu"; bali makusudio ni kuziheshimu dalili (alama) za dini ya Mwenyezi Mungu. Na maana hii ndiyo ambayo waisemayo wafasiri wa Qur'an katika aya hii kwamba, neno "Sha'airullah", maana yake ni vitambulisho vya dini ya Mwenyezi Mungu. Na iwapo "safa" na "Marwah" na pia ngamia anayepelekwa Mina kwa ajili ya kuchinjwa ni miongoni mwa alama za dini ya Mwenyezi Mungu, basi siyo kwa sababu nyingine bali ni kwa kuwa ni vitambulisho vya dini tukufu na mpenzi wa Mwenyezi Mungu Nabii Ibrahim [a.s]. Na iwapo Muzdalifah huitwa "Mash'ar" hiyo ni kwa sababu ipo miongoni mwa alama za dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu; na kwamba kusimama katika Mashar hiyo ni dalili za kumtii Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Vile vile Ibada za Hija zinapoitwa kuwa ni Sha'air; basi siyo kwa sababu nyingine isipokuwa ni kwa kuwa ni alama za tauhidi na za dini tukufu. Kwa kifupi ni kwamba, kila kile ambacho ni kitambulisho cha dini ya Mwenyezi Mungu, kukiheshimu ni katika mambo yanayomsogeza mtu katika ucha Mungu. Hivyo basi hakuna shaka kwamba Manabii na Mawalii wa Mwenyezi Mungu, wao ndiyo alama kubwa zaidi miongoni mwa alama za dini ya Mwenyezi Mungu, kwani wao walikuwa ndiyo njia bora ya kufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu na kuueneza miongoni mwa watu.

Hakika miongoni mwa mambo yenye kuthibiti kwa kila mtu aliyemuadilifu ni kwamba, kuwepo kwa Mtume **[s.a.w.w]** na Maimamu watukufa [a.s] ni katika alama na vitambulisho vya dini hii tukufu, kwa hiyo kuwaheshimu wao ni kumtukuza Mwenyezi Mungu, na ndiyo alama ya ucha Mungu. Na hapana shaka kwamba, kuhifadhi kumbukumbu zao na kuyahifadhi makaburi yao yasiondolewe, ni moja katika aina ya kuviheshimu vitambulisho vya dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na kwa maneno mengine, tunaweza kufahamu umihimu wa kuheshimu makaburi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu kwa kupitia nukta mbili zifuatazo:

**Kwanza**: Mawalii wa Mwenyezi Mungu hasa wale ambao waliuawa kwa ajili ya kueneza dini, wao ni vitambulisho vya Mwenyezi Mungu na ni alama za dini yake.

**Pili**: Kujenga juu ya makaburi yao ili kudumisha utajo wao na kuishi kwa kufuata mwenendo wao wa haki ni aina ya kuonyesha kuwaheshimu na kuwatukuza. Kwa msingi huu basi, ndiyo maana tunaona mataifa yote ulimwenguni yanatenga maeneo maalum kwa ajili ya makaburi ya watu wao mashuhuri wa kidini na kisiasa, ili kuzibakisha kumbukumbu zao zidumu kwa ajili ya wafuasi wao milele. Kwa hiyo inakuwa kana kwamba kuyahifadhi makaburi yao yasitoweke na kuharibiwa ni katika jumla ya kudumisha kumbukumbu zao na kuendelea kuwepo kwa fikra zao na miongozo yao. Ili kuufahamu vyema ukweli huu, hapana budi tuifanyie mazingatio aya ya 36 katika Surah Al-Haj: "Na ngamia, ngombe, mbuzi na kondoo (muwachinjao) tumekufanyieni kuwa ni katika alama za Mwenyezi Mungu".

Baadhi ya Mahujaji wa Nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu walikuwa wakienda hija pamoja na ngamia wao kutoka katika miji yao ili wanyama hao wapelekwe iliko Al-Kaaba - kwa madhumuni ya kuwachinja karibu na nyumba ya Mwenyezi Mungu, pia walikuwa wakiwavalisha makoja shingoni mwao ikiwa ni alama ya kutambulisha kwamba, mnyama huyo atapelekwa Makka kwa ajili ya kuchinjwa. Basi mnyama huyo huwa amewekwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, hawezi kuuzwa wala kununuliwa; na kitambulisho chake katika kundi la ngamia wengine hi huko kuvalishwa hilo koja. Kwa sababu hii basi, Mwenyezi Mungu amemzingatia mnyama wa aina hii kuwa ni miongoni mwa alama za Mwenyezi Mungu. Na kwa ajili hii, Uislamu umetoa hukumu ya kumheshimu mnyama huyu; hivyo basi haifai kumpanda; na ni wajibu kumkamilishia mahitaji ya chakula na kinywaji mpaka wakati wa kuchinjwa hapo karibu na Al-Kaaba.

Sasa basi, ikiwa ngamia huyu anapata heshima hii na utukufu huu kwa sababu tu amekuwa miongoni mwa alama za Mwenyezi Mungu Mtukufu, basi utasemaje juu ya Manabii na Maimamu watukufu? Je, Manabii na Maimamu watukufu [a.s] pamoja na wanachuoni na mashahidi ambao walivaa makoja ya utuinwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tangu hapo mwanzo, na walijitoa muhanga nafsi zao kuitumikia dini ya Mwenyezi Mungu, pia wakawa ni wawakilishi wa Mwenyezi Mungu katika kuwaongoza na kuwaongoza viumbe wake; basi kwa yote haya hawatazingatiwa kuwa ni miongoni mwa vitambulishovya dini ya Mwenyezi Mungu?

Je, hivi siyo jambo la wajibu kuwatukuza na kuwapa heshima inayowastahiki wakiwa hai na baada ya kufa kwao? Ikiwa Al-Kaaba, Safa na Marwah, Mina na Arafat (vitu ambavyo havina uhai, na ni mchanganyiko wa udongo na mawe tu vinazingatiwa kuwa ni alama za Mwenyezi Mungu, na vinastahiki heshima na utukufu unaonasibiana navyo kwa sababu tu ya kuwepo mafungamano ya vitu hivyo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, basi kwa nini Mawalii wa Mwenyezi Mungu ambao wao ndiyo watetezi wa dini ya Mwenyezi Mungu na walizieneza shari'ah zake wasiwe ni miongoni mwa alama za Mwenyezi Mungu? Basi sisi tunawataka Mawahabi waamue wenyewe kuhusu jambo hili, na tunawauliza maswali yafuatyo: Je, mnayo

mashaka yoyote au wasiwasi wowote kwamba Manabii na Mtume ni miongoni mwa alama za dini ya Mwenyezi Mungu? Je, nafsi zenu hazioni umuhimu na kuwatukuza na kudumisha utajo wao na kushikamana na mafundisho yao? Se, kujenga juu ya makaburi yao na kuvisafisha viwanja yalipo makaburi yao ni kuwatukuza na kuwaheshimu? Au kuyabomoa makaburi yao na kuvipuuza bila kuvisafisha viwanja walipozikwa na kuvitelekeza ndiyo kuwatukuza?!

### 2. KUWAPENDA AL-QURBAA

Kwa hakika Qur'an inatuamuru wazi wazi kuwapenda jamaa wa Mtume **[s.a.w.w]** na kushirikiana nao vizuri, na inasema:

قُل لَّا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِلَّا الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَىٰ ﴿٢٣﴾

"Waambie (ewe Mtume Wetu) sikuombeni malipo yoyote (katika kazi hii) isipokuwa muwapende jamaa (zangu), (42:23).

Kitu kinachoonekana wazi kwa ye yote yule ambaye Mwenyezi Mungu amemsemesha kwa usemi uliyomo katika aya hii ni kwamba, kujenga juu ya makaburi ya watu wa nyumba ya Mtume **[s.a.w.w]** ni moja katika aina za kuonyesha upendo kwao. Desturi hii (ya kujenga juu ya makaburi ya viongozi) ni yenye kufuatwa na mataifa yote katika ulimwengu, na wote wanaizingatia hali hii kuwa ni namna mojawapo ya upendo kwa huyo aliyezikwa kwenye kaburi hilo; na ndiyo maana utaona wanawazika viongozi wao wakubwa wa kisiasa na utaalamu mbali mbali katika makanisa na sehemu mashuhuri za kuzikia, na kisha wakapanda pembeni ya makaburi hayo aina tofauti za maua na miti.

### 3. KUJENGEA MAKABURI KATIKA NYUMATI LILIZOPITA

Baadhi ya aya tukufa za Qur'an zinatufahamisha kwamba, kuyaheshimu makaburi ya waumini ni jambo ambalo lilikuwa limeenea miongoni mwa nyumati zilizotangulia kabla Uislamu haujadhihiri. Kwa mfano, zilipokuwa zimeenea habari za As-habul kahfi (Watu wa Pangoni) miongoni mwa watu, na watu hao wakaenda kwenye hilo pango ili wakawaone hao As-habul Kahfi wenyewe, ilitokea tofauti na mabishano juu ya mahala pa maziko yao hao As-habul-Kahfi, na watu wakagawanyika makundi mawili. Kundi moja likasema: Jengeni jengo juu yao". Na kundi la pili likasema: "Bila shaka tutajenga Msikiti juu yao" Hapa utaona kwamba Qur'an Tukufu inatutajia rai hizi mbili bila ya kuzikosoa; kwa hali hiyo basi inawezekana kusema kwamba lau rai hizi mbili zingekuwa hazifai, bila shaka Qur'an ingezikosoa au ingesimulia kisa cha semi mbili hizi kwa kuzipinga na kuzikemea. Wafasiri wa Qur'an wanasema: "Mzozo kuhusu mahali walipozikwa As-habul-Kahfi, ulitokea baina ya waumini na makafiri ama makafiri wao walisema: "Jengeni jengo juu yao", na waumini nao walisema: "Tutajenga msikiti juu yao."

Ushindi waliupata waumini, kwani Mwenyezi Mungu anasema:

قَالَ الَّذِينَ غَلَبُوا عَلَىٰ أَمْرِهِمْ لَنَتَّخِذَنَّ عَلَيْهِم مَّسْجِدًا ﴿٢١﴾

"Wakasema wale walioshinda katika shauri lao, bila shaka tutajenga msikiti juu yao". (Qur'an, 18:21).

Msikiti ulijengwa na makaburi ya As-habul-Kahfi yakawa ni mahali panapotukuzwa na kuheshimiwa. Hali hii inatuonyesha kwamba lengo Ia

kujenga juu ya makaburi ya hao As-habul-Kahfi halikuwa jingine isipokuwa ni kuonyesha namna ya kuwatukuza Mawalii wa Mwenyezi Mungu. Ewe msomaji mpendwa, baada ya aya tatu za Qur'an zilizotangulia hapo kabla, ni dhahiri haiwezekani kuharamisha kujengea juu ya makaburi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu, wala hakuna karaha ya kutenda hilo kwa namna ye yote ile, isipokuwa kinachowezekana ni kulizingatia tendo la kujengea juu ya makaburi kuwa ni katika namna ya kuviheshimu vitambulisho vya dini ya Mwenyezi Mungu, na kwa kufanya hivyo ni katika kuonyesha wazi upendo wa jamaa ya Mtume **[s.a.w.w]**.

### 4. RUHUSA YA NYUMBA MAALUM

Bila shaka Mwenyezi Mungu ametoa ruhusa ya nyumba ambazo ndani yake litatajwa jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mwenyezi Mungu akasema:

فِي بُيُوتٍ أَذِنَ اللَّـهُ أَن تُرْفَعَ وَيُذْكَرَ فِيهَا اسْمُهُ يُسَبِّحُ لَهُ فِيهَا بِالْغُدُوِّ وَالْآصَالِ ﴿٣٦﴾ رِجَالٌ لَّا تُلْهِيهِمْ تِجَارَةٌ وَلَا بَيْعٌ عَن ذِكْرِ اللَّـهِ وَإِقَامِ الصَّلَاةِ وَإِيتَاءِ الزَّكَاةِ ﴿٣٧﴾

"Katika nyumba ambazo Mwenyezi Mungu ameamrisha litajwe humo jina lake, humtukuza humo asubuhi na jioni. Watu ambao hawashughulishwi na biashara ya kuuza na kununua (wakasahau) kumkumbuka Mwenyezi Mungu, na kushika Sala, na kutoa Zaka. (Qur'an, 24:36-37).

Katika aya hizi, ushahidi wa kufaa kujenga juu ya makaburi utakamilika kwa kubainisha mambo mawili: La kwanza: Nini makusudio ya neno Al-Buyut (nyumba) lililomo katika aya? La pili: Nini makusudio ya neno Ar-Raf'u pia lililoko katika aya? Kuhusu lile neno la kwanza, kinachokusudiwa katika neno "Al-Buyut" siyo Misikiti peke yake, isipokuwa muradi wake ni misikiti na sehemu ambazo hutajwa katika sehemu hizo jina Ia Mwenyezi Mungu, sawa sawa ikiwa ni misikiti au isiwe misikiti, kama vile nyumba za Manabii na Maimamu [a.s] na wacha Mungu ambao haiwashughulishi biashara ya kuuza na kununua kiasi cha kuwasahaulisha kumkumbuka Mwenyezi Mungu.

Basi nyumba hizi zitazingatiwa kuwa ni miongoni mwa makusudio yanayojitokeza katika aya hiyo tukufu. Bali inawezekana kabisa kusema kwamba makusudio ya "Al-Buyuut" siyo Misikiti, kwa sababu "Al-Bait" kwa maana ya nyumba, ni jengo ambalo Iimejengwa kwa kuta nne na juu yake kuna paa. Sasa basi ikiwa Al-Kaaba inaitwa kuwa ni nyumba ya Mwenyezi Mungu (Baitullahi), hakuna kinachosababisha iitwe hivyo ila ni kwa kuwa inalo paa. Qur'an kwa upande wake, inazingatia neno "Al-Bait" kwa maana ya nyumba yenye paa. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Na isingekuwa watu watakuwa kundi moja, bila shaka tungeliwafanyia wanaomkufuru (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa Rehema, majumba yao kuwa ni yenye mapaa ya fedha"..... (Qur'an, 43:44).

Kinachofahamika katika aya hii ni kwamba nyumba "Al-Bait" huwa haiepukani na paa. Na kwa kisheria inapendekezwa Misikiti isiwe na paa na ndiyo maana unanona msikiti Mtukufu wa Makka kwa juu uko wazi haukufunikwa na paa. Na kwa hali yoyote ile, makusudio ya "Al-Buyuut" ima yatakuwa na maana zaidi ya ile manna ya misikiti au manna yake isikusudie misikiti. Maelezo yaliyotangulia hivi punde yamelihusu lile

jambo la kwanza yaani nini makusudio ya neno "Al-Buyuut". Na ama lile la pili ambalo ni maana ya (Ar-Raf'u), hili linawezekana kuwa na manna mbili. Maana ya kwanza: Ni kuwa makusudio ya neno "Ar-Raf'u" (kuinua) ni kwa ile maana ya kimaada inayoonekana wazi wazi, maana ambayo huthibitika kwa kuweka msingi (wa jengo) na kusimamisha kuta na hatimaye jengo lenyewe kusimama kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

﴿وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْمَاعِيلُ ﴿١٢٧﴾

Na (kumbukeni pale) Ibrahimu alipoziinua kuta za nyumba na Isma'il. (Qur'an, 2:127).

Maana ya pili: Ni kuwa makusudio ya neno "Ar-Raf'u" ni kimaana (na wala siyo ya kimaada) kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu, "Na tulimuinua daraja ya juu kabisa, maana yake ni kuwa "Tulimpa daraja ya juu kabisa". Iwapo makusudio ya Ar-Raf'u yatakuwa ni kwa ile maana ya kwanza, basi itakuwa inajulisha wazi kabisa kwamba inafaa kuyajenga na kuyaimarisha majumba ya Manabii na Mawalii wa Mwenyezi Mungu, katika zama za uhai wao na baada ya kufa kwao. Na ni jambo linaloeleweka kwamba mahali alipozikwa Mtume **[s.a.w.w]** na mahali walimozikwa wengi wa Maimamu watukufu na Mawalii wa Mwenyezi Mungu ni katika majumba yao.

Hivyo basi, kuyajenga majumba haya na kuyahifadhi yasiharibiwe na kuondoka alama zake ni tendo linalofaa kwa mujibu wa nassi ya aya tukufu ya Qur'an; na zaidi ya hapo ni jambo lililopendekezwa litendwe. Na kama muradi wake neno Ar-Raf'u itakuwa ni ile ya kimaana tu yaani kutukuza (kuinua daraja, cheo) matokeo yake yatakuwa ni kupatikana ruhusa ya kuyaheshimu na kuyatakuza majumba hayo na kuyahifadhi na kuyaepusha kutokana na kila kile ambacho hakistahiki heshima yake. Na kwa hali yoyote, ile ruhusa iliyopo katika maana ya neno Ar-Raf'u, sawasawa kama itakuwa ni ile ya kimaada au ni ile ya kimaana tu, basi itakuwa haikupatikana ila kwa sababu ya kuwepo katika mahali hapo watu wema, ambao humtaja Mwenyezi Mungu Mtukufu asubuhi na jioni. Baada ya kuitaja aya hii na aya nyingine zinazofanana na hii, basi itakuwaje Mawahabi waone kuwa inafaa kuyabomoa majumba waliyokuwamo kizazi cha Mtume **[s.a.w.w]**, majumba ambayo yalikuwa ni mahala ambapo Malaika wa Mwenyezi Mungu walikuwa wakishuka na pia yalikuwa ni vituo vya kumtaja Mwenyezi Mungu na kueneza dini yake na hukumu zake?

Vipi itakuwa inafaa kwa Mawahabi kubomoa makaburi matukufu ambayo ndiyo mahala pa (kuonyesha) upendo wa nyoyo za mamilioni ya waumini ambao walikuwa wakiyazuru - wake kwa waume, asubuhi na jioni, na walikuwa wakimtaja Mwenyezi Mungu katika majumba hayo, kwa kuswali, kuomba na kumtakasa? Kwa nini basi Mawahabi wamefanya jeuri kwa kuyadharau majumba haya na kuyadhalilisha na kuyapuuza? Kwa nini wameyageuza yakawa hi mahala palipotengwa na kubaki pweke. Nyoyo za waumini wote huomboleza na kuhuzunika kutokana na kuyadharau na kuyadhalilisha majumba haya. Kwa nini? Tena kwa nini? Amepokea Al-Hafiz As-Suyuti kutoka kwa Anas ibn Malik na Buraidah kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** aliisoma kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu (isemayo) "Katika majumba ambayo Mwenyezi Mungu

ameamrisha zijengwe....." Basi alisimama mtu fulani akasema: "Ni nyumba gani hizi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?"

Mtume **[s.a.w.w]** akasema: "Ni nyumba za Mitume." Basi Abubakar akasimama na akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, na nyumba hii ni miongoni mwa hizo?" Na aliashiria nyumba ya Ali na Fatma [a.s]. Mtume **[s.a.w.w]** akasema: "Ndiyo; nayo ni bora mno kuliko zingine".

## B: UMMA WA KIISLAMU NA KUJENGA JUU YA MAKABURI

Uislamu ulipokuwa umeenea katika bara Arabu, na nuru yake ikaenea katika sehemu kubwa ya mashariki ya kati, makaburi ya Manabii yaliyokuwa yakifahamika yalikuwa yamejengewa na kuwekwa mapaa yaliyoyafunika. Baadhi ya makaburi hayo yalikuwa yana Maquba imara na kuna madharih mazuri, na baadhi yake yapo mpaka leo. Katika mji wa Makka yenyewe utaliona kaburi la Nabii Isma'il na mama yake, Hajirah, yapo katika mahala panapojulikana kama "Hijri Isma'il". Na kadhalika Kaburi Ia Nabii Daniel liko katika mji wa Shush nchini Iran. Na makaburi ya Manabii Hud, Saleh, Yunus, Dhulkifl [a.s] yako nchini Iraq. Vile vile kaburi la Nabii Ibrahim na makaburi ya wanawe kina Ishaq; Ya'qub na Yusuf [a.s] yako huko Baitul-Muqaddas (Jerusalem).

Na hapo kabla makaburi haya ya wana wa Ibrahim [a.s] yalikuwa Misri, na baadaye Nabii Musa [a.s] akaihamishia miili yao mitukufu huko Quds kwa amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na mpaka leo makaburi hayo bado yapo, na kila kaburi limejengwa imara na linajulikana wazi. Na kaburi la mama Hawa (mama wa wanaadamu) liko katika mji wa Jeddah ndani ya nchi ya Hijazi, kwa mujibu wa kauli iliyo mashuhuri; na umeitwa hivyo mji huu kutokana na kuwepo kwa kaburi la mama Hawa katika sehemu hiyo. Kaburi hili Ia mama Hawa hapo mwanzo alama zake zilikuwa zikionekana, lakini Mawahabi walipokwisha kuikalia nchi ya Hijazi waliziondosha alama zake na kufuta kabisa athari zake.

Makaburi yote haya tuliyoyataja yaliendelea kuwepo hata baada ya Waislamu kuiteka miji hiyo na waliyaona, lakini pamoja na hali hiyo hawakutenda tendo lolote la kupinga kuwepo kwa makaburi hayo na wala hawakuamrisha yabomolewe au kuharibiwa. Basi lau ingekuwa kujenga juu ya makaburi na kuwazika wafu katika makaburi yaliyojengwa na kuwekewa mapaa ni jambo lililoharamishwa katika Uislamu, lingekuwa ni jambo la lazima kwa Waislamu hao kabla ya kufanya chochote wayabomoe makaburi hayo ambayo yapo mpaka leo katika sehemu mbali mbali nchini Iraq, Jordan na Palestina.

Pia Waislamu hao wangezuia kujengwa upya makaburi hayo kila yanapoharibika muda wote. Lakini tunachokiona ni kuwa, Waislamu hao hawakuamuru yabomolewe, bali waliendelea kuyaimarisha na kuyahifadhi muda wote wa kipindi cha karne kumi na nne. Kwa hakika walikuwa wakifahamu kwa kupitia ufunuo wa kiakili kwamba, kuzilinda kumbukumbu za Manabii na kuzihifadhi ni miongoni mwa kuwaheshimu Manabii hao, na kwamba jambo hilo huwakuru - bisha kwa Mwenyezi Mungu na linawapatia malipo mema.

Ibn Taimiyya anasema ndani ya kitabu chake kiitwacho, As-siratul-Mustaqiim: "Quds ilipokuwa imeingia mikononi mwa Waislamu, makaburi ya Manabii yalikuwa yamo ndani ya majengo, lakini milango ya majengo

hayo ilikuwa imefungwa mpaka katika karne ya nne Hijriyya."[1] Kwa hiyo basi, lau kujengea makaburi ingekuwa ni haramu, pasingekuwa na sababu yoyote ya kuyaacha makaburi hayo kama yalivyokuwa na huku milango yake imefungwa; isipokuwa ingekuwa ni jambo la wajibu kuyabomoa mara moja, (Hata kama tukichukuwa usemi wa Ibn Taimiyya kwamba milango yake ilikuwa imefungwa mpaka karne ya nne, lakini kauli hii haina uthibitisho.) Kwa kifupi kuyabakisha majengo hayo na Maquba yaliyojengewa kwenye makaburi muda wote huu mbele ya macho ya wanachuoni na mafaqihi wa Kiislamu, ni dalili iliyo wazi ya ruhusa ya kuyajengea makaburi katika dini ya Kiislamu.

1. Kash-ful Irtiyab, uk. 384.

4

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## KUMBUKUMBU ZA KIISLAMU NI DALILI YA KUENDELEZA DINI

Hapana shaka kwamba kuhifadhi kumbukumbu za Manabii na hasa zile za Nabii Muhammad **[s.a.w.w]** pamoja na kaburi Ia Mtume **[s.a.w.w]** na makaburi ya wakeze, wanawe na masahaba wake, na vile vile nyumba walizokuwa wakiishi na misikiti walimokuwa wakisali, hapana shaka kabisa kwamba mambo haya yanazo faida nyingi na yanayo matokeo mazuri. Tunataja baadhi ya faida hizo kama ifuatavyo: Leo hii baada ya kupita karne ishirini tangu kuzaliwa Nabii 'Isa [a.s] yeye na mama yake na kitabu chake cha Injili pamoja na wale wafuasi wake maalum (Hawaariyyuun) kwa mtazamo wa watu wa magharibi wamegeuka kuwa kama masimulizi yasiyo na ukweli, na baadhi ya wataalamu wanatia shaka hata kuwa je, alikuwako mtu aitwaye Masih 'Isa au mama yake aitwaye Mariyam, au kitabu chake kiitwacho lnjili. Na habari za Nabii 'Isa [a.s] wanazichukulia kuwa ni mazungumzo tu yasiyo na ukweli na kwamba yanafanana na ngano za Laila Majnuun.

Basi kwa nini imekuwa hivyo? Hii ni kwa sababu hakuna athari yoyote inayoonekana kuhusu Nabii 'Isa [a.s]. Kwa mfano: Haifahamiki kabisa ni mahali gani Nabii 'Isa [a.s] alipozaliwa; na iko sehemu gani nyumba aliyokuwa akiishi, na hi mahali gani alipozikwa? (Kwa mujibu wa madai ya Wakristo kuwa Nabii 'Isa [a.s] aliuawa). Kwa upande wa kitabu chake kilichoteremshwa toka mbinguni, kitabu hiki kimeingiliwa na mikono ya watu waliokigeuza na kukibadilisha na kuzua mambo mbalimbali. Na hizi Injili nne zilizomo mikononi mwa watu hazina uhusiano wowote na Nabii 'Isa [a.s], na wala siyo ile Injili yake; bali hizo ni Injili za kina Matayo, Yohana, Marko na Luka.

Ndiyo maana basi, utaviona mwishoni mwake vinataja kisa cha kuuawa kwa Nabii 'Isa [a.s] na kuzikwa kwake. Basi ukweli halisi ulivyo ni kuwa, lnjili hizo zimeandikwa baada ya Nabii 'Isa [a.s] kutoweka. Na kwa msingi huu basi wengi wa watafiti na wachunguzi wanaitakidi kwamba, Injili hizi nne ni miongoni mwa vitabu vya mafunzo tu ambayo historia yake inaanzia karnye ya pili ya masihiya. Na lau kama vingekuwepo vitu muhimu vinavyomuhusu Nabii Isa [a.s] vimehifadhiwa, vingelikuwa ndiyo dalili madhubuti ya kuthibitisha kuwepo kwake, na maisha yake yalivyokuwa; na pia vingeonyesha utukufu wake, na wala kusingekuwa na nafasi ya kuzusha mashaka na maswali mengi toka kwa wataalam wenye mawazo potofu.

Ama kwa upande wa Waislamu, wao wanaukabili ulimwengu bila ya hofu na wanasema: "Enyi watu, kwa hakika kuna mtu kutoka katika ardhi ya Hijazi aliyetumwa kuja kuiongoza jamii ya wanadamu tangu miaka elfu moja na mia nne iliyopita, na ameuthibitisha ushindi wenye mafanikio katika jambo lake hilo (la dini) na hizi hapa kumbukumbu za maisha yake zimehifadhiwa kikamilifu katika miji ya Makka na Madina". Wanaendelea kusema: "Hii hapa ndiyo nyumba alimozaliwa na hili hapa ni pango la Hiraa mahala ambapo Wahyi na ufunuo vilimshukia, na huu ndiyo Msikiti wake ambamo alikuwa akisalisha ndani yake, na hii hapa ndiyo nyumba

alimozikwa na hizi ni nyumba za wanawe, wakeze, na jamaa zake, na makaburi haya ni ya kizazi chake na mawasii wake [a.s]."

Sasa basi, iwapo sisi tutaziondosha kumbukumbu hizi zinazojulisha kuwa Mtume **[s.a.w.w]** alikuweko, na takaondosha dalili zinazoashiria utukufu wake na ukweli wake, tutakuwa tayari tumeandaa njia kwa maadui wa UisIamu waseme yale wayatakayo dhidi yetu na Uislamu wetu. Kwa hakika kubomoa kumbukumbu za Mtume **[s.a.w.w]** na zile za watu watukufu wa nyumba yake, siyo tu ni kuwakosea wao na kuvunja heshima yao, bali ni kufanya uadui dhahiri dhidi ya Utume wenyewe kwa nafsi yake na Mtume **[s.a.w.w]** mwenyewe na vitambulisho vya dini aliyokuja nayo. Ujumbe wa dini ya Kiislamu ni ujumbe wa kudumu milele; na Uislamu utaendelea kuwa ndiyo dini pekee inayowafaa wanaadamu mpaka siku ya Kiyama; na vizazi vijavyo havina budi kukiri ukweli wake na kuamini utukufu wa ujumbe huu.

Na ili litimie lengo hili, ni lazima kuzihifadhi kumbukumbu za Mtume **[s.a.w.w]** ili tupige hatua mbele katika njia za kuendeleza dini hii na kuifanya ibakie milele kiasi ambacho asiwe na shaka mtu ye yote juu ya kuwepo kwa Nabii wa Uislamu **[s.a.w.w]** kama ambavyo watu wamefanya shaka kuhusu kuweko kwa Nabii 'Isa [a.s] (kutokana na kupotea kwa kumbukumbu zake). Waislamu (kwa upande wao) wamelipatia umuhimu mkubwa jambo la uwekaji kumbukumbu za Nabii Muhammad **[s.a.w.w]** ikiwemo sera zake na mwenendo wake kiasi kwamba wameyasajili katika historia mambo yake madogo madogo yanayohusiana na maisha yake na athari zake za kipekee.

Wameandika pia maelezo yanayohusu pete yake na viatu vyake, mswaki wake na upanga wake, deraya yake, mkuki wake na farasi wake, ngamia wake na hata mtumishi wake na mpaka wameandika visima alivyokunywa maji na ardhi aliyoitoa wakfu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. (Waislamu) wameandika pia aina ya chakula ambacho Mtume **[s.a.w.w]** alikuwa akikipenda na zaidi ya hayo wameandika hata namna ya kutembea kwake na kula kwake na kunywa kwake na pia namna ya ndevu zake zilivyokuwa na alivyokuwa akizipaka hina na mengineyo. Na baadhi yakumbukumbu hizo bado zimebakia mpaka katika siku zetu hizi.[1]

Na kila inaporejewa historia ya Uislamu na kuichunguza hali ya miji ya Kiislamu na kumbukumbu zilizomo, inadhihirika wazi kabisa kwamba, kujenga juu ya makaburi ili kuyahifadhi yasitoweke ni jambo lililokuwa likifanyika kwa Waislamu wote katika sehemu mbali mbali za miji mikubwa ya Kiislamu, na mpaka sasa yako madhariha yaliyowekwa kwenye makaburi ya Manabii na ya watu wachamungu kiasi kwamba Waislamu wanakwenda kufanya ziyara kwenye sehemu hizo na kuomba dua. Na Makaburi hayo yanahesabiwa (kuwa ni miongoni mwa kumbukumbu za kihistoria za Kiislamu. Vile vile katika sehemu hizo kuna waqfu nyingi zilizowekwa ambazo kipato chake hutumika katika kuimarisha hifadhi ya kumbukumbu hizo na kusafisha mazingira yake na mengineyo.

Ukweli ulivyo ni kwamba makaburi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu yalikuwa yamejengewa hata katika nchi ya Hijazi yenyewe, na kabla fitana

1. Tabaqat As-Sahaba cha lbn Saad: Juz. 1 uk. 360-503.

hii ya Mawahabi haijaingia na kuikalia Haram ya Makka na Madina pamoja na pembezoni mwake, kulikuwa na makaburi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu katika kila upande wa nchi ya Hijazi yamejengewa yakipata hadhi kutokana na kupewa heshima na Waislamu wote, na wala hapakuweko mwanachuoni yeyote aliyekemea kubakia kwa makaburi hayo au aliyepinga kujenga juu yake. Wala siyo kwamba nchi ya Iran peke yake ndiyo ambayo kunapatikana makaburi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu yaliyojengewa juu yake, bali hali hii imeenea katika nchi za Kiislamu, hasa hasa Misri, Syria, Iraq, Morocco, Tunisia na Jordan.

Katika miji hiyo kuna makaburi ya wanachuoni wakubwa wa Kiislamu yamejengewa, na Waislamu wanayatembelea kwa wingi na kusoma Qur'an wafikapo hapo, hasa Surah al-Fatiha na kumuomba Mwenyezi Mungu azipeleke thawabu za kisomo chao kwa roho za walioko kwenye makaburi hayo. Vile vile kwenye makaburi hayo wapo wafanyakazi wanaosimamia ulinzi, huduma, usafi na hifadhi ya sehemu hizo. Baada ya maelezo yaliyotangulia, itakuwaje ni haramu kuyajengea makaburi wakati desturi iliyokuwa ikifuatwa tangu mwanzo wa kuja Uislamu hadi leo inaendelea kutumika kitu ambacho wanachuoni wanakiita kuwa ndiyo sera ya Waislamu ambayo mizizi yake inakwenda hadi kuzifikia zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu, au zama za Maimamu watukufu wa nyumba ya Mtume **[s.a.w.w]**.

Kwa hakika sera hii imesimama kwenye msingi wa ruhusa ya kujenga juu ya makaburi; bali inathibitisha umuhimu na kupendekezwa kwa jambo hili; na halikupata kupingwa na upinzani wa aina yoyote muda wote wa kuwepo kwake kitu ambacho kinaonyesha kuwa linayo asili kwa Waislamu na linafaa wakati wote, na kwamba limekuwa katika sunna zenye kufuatwa kwa Waislamu. Mwandishi mmoja wa Kiwahabi anakiri uasili wa jambo hili alipoandika akasema: "Jambo hili limeenea katika miji na limeenea ulimwenguni mashariki na magharibi kiasi kwamba hapana mji katika miji ya Kiislamu isipokuwa yamo makaburi na maziyara, zaidi ya hapo misikiti mingi haikosi kuwa na kaburi na ziyara; na wala haingii katika akili ya mtu kabisa kwamba jambo hili ni baya, kiasi cha ubaya nilioutaja, na kisha wanachuoni wa Kiislamu wanyamaze kimya."[1]

Ni ajabu kwamba mwandishi huyu wa Kiwahabi anakiri kuwa sera ya Waislamu inao msimamo wa kujenga juu ya makaburi ya watu wacha Mungu na kuyatukuza, lakini utamuona kuwa hakuacha uovu wake na dhamira yake mbaya, na utamuona analiona jambo hili kuwa ni baya na anawalaumu wanachuoni kwa kukaa kwao kimya na anadai kwamba kimya cha wanachuoni hao wa kale kwa muda mrefu hakiwazuwii wanachuoni wa zama hizi kulikemea jambo hilo. Lakini jibu lake liko wazi mno. Basi ni vipi wanachuoni wanyamaze muda wote wa karne saba wasitamke chochote? Je, wote hawa katika karne hizo zilizopita walikuwa wakilinyamazia jambo baya na wakijizuwiya kulikataza kama anavyodai Wahabi huyu? Katika zama za Khalifa Omar bin Khattab Waislamu walipoiteka Bait-al-Muqaddas, ni kwa nini Omar hakuamrisha makaburi ya

1. Tat-hirul-iitikadi. uk. 17, Chapa ya Misri.

Manabii yaliyoko hapo yabomolewe? Basi je, enyi Mawahabi mwamuona Omar kwamba ni mwenye kukubaliana na washirikina?

### JAWABU LA WANACHUONI WA MADINA

Jambo la ajabu katika maudhui haya ya kujenga juu ya makaburi ni lile jawabu linalonasibishwa kuwa limetoka kwa wanachuoni wa Madina, waliposema: "Ama kujenga juu ya makaburi, ni jambo Iililokatazwa kwa ijma'i, na hii ni kutokana na hadithi sahihi zilizokuja kuzuwiya jambo hili, na kwa ajili hii wametoa fatwa wanachuoni wengi kuwa ni wajibu kuyabomoa". Lakini ni vipi madai ya Ijma'i yatasihi katika kuharamisha kujenga juu ya makaburi, wakati VVaislamu walimzika Mtume **[s.a.w.w]** katika nyumba aliyokuwa akikaa Bibi Aisha kisha baadaye wakawazika katika nyumba hiyo hiyo Abubakar na Omar; tena karibu kabisa na Mtume kwa nia ya kupata baraka, na hatimaye walijenga ukuta uliotenganisha, sehemu moja ikawa ni makazi ya Bibi Aisha na sehemu nyingine ikawa ni makaburi ya Mtume **[s.a.w.w]** na Abubakar na Omar.

Ilipokuwa ukuta huo wa kutenganisha sehemu hizo mbili ni mfupi, uliongezwa urefu katika zama za Abdallah bin Zubair, na kisha nyumba hii yenye makaburi haya ikawa hujengwa upya kila zama na karne zinavyopita kwa ujenzi wa kitaalam ulivyo katika kila zama. Na katika wakati wa utawala wa Banu Ummaya na Banu Abbas ujenzi wa kaburi Ia Mtume **[s.a.w.w]** ulipewa umuhimu na heshima kubwa na uliendelea kujengwa upya kwa mujibu wa utaalamu uliokuwepo katika zama zile. Jengo Ia mwisho lililojengewa kaburi tukufu la Mtume **[s.a.w.w]** ambalo mpaka leo lipo, ni lile lililojengwa wakati wa Sultan Abdul Hamid (wa Uturki) mwaka 1270 A.H. sawa na mwaka 1869 A.D., na ujenzi huu ulimalizika kwa muda wa miaka minne.

Ewe msomaji, unaweza kurejea kitabu kiitwacho Wafa'ul-wafa cha As-samhudi, kutoka ukurasa 383 hadi ukurasa 390 ili upate maelezo kwa urefu juu ya kujengewa kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** na kufanywa upya na kuimarishwa ujenzi wake katika historia ya Uislamu mpaka kufikia zama za huyu As-samhudi katika vitabu vya historia ya mji wa Madina.

### C. HADITHI YA ABUL-HAYYAJ

Hivi sasa umefika wakati wa kuichunguza hadithi wanayoitegemea Mawahabi kuharamisha kujenga juu ya makaburi. Kabla ya yote tunaitaja hadithi yenyewe kwa sanadi aliyoipokea Muslim katika kitabu chake. "Ametusimulia Yahya ibn Yahya, na Abubakar ibn Abi Shaiba na Zuhayr ibn Harb, Yahya ametusimulia; (na watu wawili wa mwisho wamesema): Ametusimulia Waki'i, amepokea kutoka kwa Sufyan, toka kwa Habib bin Abi Thabiti, naye kapokea kwa Abi Wa'il ambaye kapokea toka kwa Abil Hayyaj Al Asadi' amesema: "Ali ibn Abi Talib alimambia: Je, nikutume kwa jambo ambalo Mtume wa Mwenyezi Mungu alinituma kwamba, usiache sanamu yoyote ila uiondoshe wala kaburi lolote lile lililonyanyuka isipokuwa ulisawazishe".[1] Hadithi hii Mawahabi wameifanya kuwa ndiyo

1. (1) Sahih Muslim, juz. 3, Kitabul-Janaiz, uk. 612. (2) Sunan Tirmidhi, juz. 2. uk. 256, Babu Majaa fii taswiyatil-qubur. (3) Sunan an-nasaiy, juz. 4. uk. 88, Babu Taswiyatil-qubur.

dalili ya kuharamisha kujenga juu ya makaburi bila hata ya kufanya uchunguzi wowote kwa watu walioipokea na Sanadi yake.

### KUIJADILI HADITHI

Kwa ujumla tunapotaka kutoa ushahidi kwa kutumia hadithi ili tutoe hukmu miongoni mwa hukmu za Mwenyezi Mungu, hapana budi hadithi hiyo itimize masharti haya mawili:

1) Kusihi kwa Sanadi: Hii ikiwa na maana kwamba, wapokezi na watu wahusikao kwenye hadithi yenyewe katika kila ngazi wawe ni waaminifu kiasi ambacho iwezekane kuwategemea katika maneno yao.

2) Ushahidi wa hadithi: Maana yake ni kwamba, matamko na sentensi zilizomo katika hadithi hiyo ziwe zimetimia katika kuelekeza makusudio yetu kwenye hadithi hiyo, kiasi waweze kuifahamu na wengine wanaofahamu vizuri lugha iliyomo katika hadithi hiyo, na wazifahamu pia kanuni zake kama tunavyozifahamu sisi na waweze kutoa matokeo tunayoweza kuyatoa.

Na kwa bahati nzuri, hadithi ya Abul-Hayyaj imekosa sharti zote mbili na hasa ile ya pili, kwani hakuna mahusiano yoyote kabisa ya kujenga juu ya makaburi katika hadithi hiyo.

### UFAFANUZI WA MAMBO HAYA

(A) Ama upande wa Sanad, ndani ya hadithi hii wamo wapokezi ambao wanachuohi wa hadithi hawakuafikiana juu ya uaminifu wa wapokezi hao, tin hapa chini tunataja majina ya wapokezi waliomo katika hadithi hii ambao wanachuoni wa hadithi wamezikataa hadithi zao:

1) Waki'
2) Sufyan Ath-Thauri
3) Habib ibn Abi Thabit
4) Abu Wai'l Al-Asadi.

Wapokezi hawa wanne amewatia kasoro Al-Hafiz ibn Hajar Al-'Asqalani katika kitabu chake kiitwacho "Tahdhibut-Tahdhib, na amewataja kwa sifa ambazo zinaondoa uaminifu katika hadithi yao hii tuliyotaja hapo kabla na pia kwenye hadithi zao nyingine.

1. Kwa upande wa huyu Waki' anapokea Al-Hafiz Al- 'Asqalani kutoka kwa Ahmad bin Hanbal (Imam wa Madhhebu ya Kihambal) amesema: "Hakika Waki' amefanya makosa katika hadithi mia tano".[1] Anasema tena Al-'Asqalani akimnakili Muhammad bin Nasr Al-Marwazi "Waki' alikuwa akisimulia hadithi kwa mujibu wa maa'na yake' isitoshe hakuwa mtaalam wa lugha".[2]

2. Na kwa upande wa "Sufyan At-Thauri" AI-'Asqalani anasema kwa kumnakili ibn Mubarak: "Sufyan alikuwa akisimulia hadithi, basi mimi nikafika kwake na yeye alikuwa anafanyia Tadlis hadithi hiyo (kufanya udanganyifu katika hadithi), basi aliponiona aliona haya (kwa tendo lake hilo).[3]

---

1. Tah-dhibut-Tah-dhib. juz. 11, uk. 125.
2. Tah-dhibut-Tah-dhib. juz. 11, uk. 130.
3. Tah-dhibut-Tah-dhib. juz. 4, uk. 145.

Kitendo cha kudanganya katika hadithi kwa namna yo yote ile, kinajulisha kwamba yule msimulizi alikuwa hana tabia ya uadilifu na ukweli, kwa hiyo alikuwa akikifanya kitu kisicho cha kweli kionekane kuwa ni kweli, kama ilivyo maana ya tadlis katika lugha ya Kiarabu.

3. Ama huyu "Habib ibn Abi Thabit", Al-Asqalani ameandika akimnakili Abu Habbani: "Kwa hakika Habib: Alikuwa mdanganyifu."[1] Na ameandika Al-Asqalani akimnakili Qat-tan: "Hakika Habib siyo mtu wa kufuatwa."

4. Ama huyu Abu Wa'il, yeye alikuwa mpinzani wa Imam Ali [a.s] na ni miongoni mwa watu waliomfanyia uadui na kero Imam Ali [a.s].[2] Basi vipi atategemewa mtu kama huyo, wakati Mtume **[s.a.w.w]** amesema; "Ewe Ali, hatakupenda wewe isipokuwa mtu muumini, na hatakubughudhi isipokuwa mtu mnafiki".[3]

Na inafaa kusema kwamba mpokeaji wa hadithi ya Abul-Hayyaj hana hadithi hata moja katika sihahi zote sita isipokuwa hadithi hii tu tunayoizungumzia. Basi utasema nini kuhusu mtu ambaye hakusimulia ila Riwaya moja? Jambo hili kwa hakika linajulisha kwamba mtu huyu hakuwa mpokeaji wa hadithi, na kwa msingi huu basi kumtegemea katika hadithi yake ni jambo lenye mushkili. Ewe msomaji mpendwa, hii ndiyo Sanad ya hadithi ya AbulHayyaj; na umefahamu udhaifu wa wapokezi wake, na kwamba wanachuoni wa hadithi hawakuafiki ukweli wa wapokezi hao. Basi iwapo hadithi itakuwa imezungukwa na matatizo kama haya mengi haitawezekana kwa faqihi yeyote kuitegemea hadithi hiyo kwa ajili ya kufahamu hukmu ya shari'ah au kutoa fatwa. Ama utambulisho wa hadithi hi, hautaepukana na matatizo licha ya ile Sanad yenyewe, kwani ile nukta muhimu wanayoitolea ushahidi Mawahabi ni hii ifuatayo: "Walaa qabran mush-rifan illa Sawwaitahu".

Hapa ni lazima kutulia na kufanya mazingatio na uchunguzi kwenye maneno mawili:

1) Mushrifan

2) Sawwaitahu.

1. Tamko Al-Mushrif manna yake ni kitu kuwa juu na chenye

kunyanyuka. Amesema katika Munjid: Al-Mushrif minal-amakin: Al-aali Wal-mutilu ala Ghairih. Maana yake: Mahali Mush-rif, ni pale palipo juu na pamejitokeza kuliko mahali pengine. Naye mwenye Al-Qamus ambaye ni mpangaji bora wa utaratibu wa maana za matamko amesema: "As-Sharaf: Al-Uluwu, Waminal-Ibili Sanaamuhu".

Yaani As-Sharafuni kuwa juu; na likitumika kwa ngamia maana yake ni nundu yake". Kwa hiyo basi maana ya "Mushrif' ni kuwa kitu chenye muinuko (kutokeza); na hasa muinuko ulio katika umbile Ia nundu ya ngamia. Basi hapa niwajibu pamoja na kuzirejea dalili na qarina, tufanye uchambuzi kuhusu nini lengo la neno "Al-Mush-rif" lililoko katika hadithi tunaoizimgumzia.

2. Tamko "Sawwaitahu" maana yake ni, kukifanya kitu kuwa sawa (kukisawazisha) na kurekebisha kiwe sawa sawa. Sawwas-Shaia: Maana

---

1. Tah-dhibut-Tah-dhib. juz. 2, uk. 179.
2. Sharh Nahjul-Balagha ya Ibn Abil Hadid, juz. 9, uk. 99.
3. (1) Majma'uz-zawa'id, ya Al-Haithami, Juz. 9 uk 133. (2) At-Tirmidhi katika Sahihi yake, Juz. 2 uk 301. Muslim, katika Sahihi yake, (Mlango wa Imani).

yake amekifanya kiwe sawasawa; husemwa: Nimesawazisha kitu kilichopinda kikasawazika, (Nimekitengeneza sawasawa). Katika Qur'an tukufu kuna aya isemayo Al-ladhii Khalaqa Fasawwaa (Aliyeumba Akasawazisha). Surah Al-Aalaa,aya ya 2. Baada ya kuangalia maana ya maneno mawili tofuati, tunawajibika kufahamu nini makusudio ya maneno haya katika hadithi. Kwa hakika hadithi hii ina mielekeo miwili, na ni lazima kuchagua mmojawapo kwa mujibu wa maana zitumikazo kwenye maneno haya pamoja na dalili nyingine.

## MWELEKEO WA KWANZA

Ni kwamba Imam Ali [a.s] alimuamuru Abul-Hayyaj kuyabomoa makaburi yaliyoinuliwa na kuyasawazisha kabisa na ardhi. Lakini mwelekeo huu ambao ndio wanaoushikilia Mawahabi haukubaliki kutokana na sababu nyingi.

Ya Kwanza: Neno "At-Taswiyya" katika lugha ya Kiarabu halikuja kwa manna ya kubomoa; na lau makusudio yake hapa ingekuwa ni kubomoa basi ilitakiwa hadithi hiyo isemwe hivi: "Wala Qabran Illa Sawwaitahu bil ardhi" Yaani "Wala (usiache) kaburi ila ulisawazishe na ardhi". Lakini hadithi haikuja namna hiyo.

Ya Pill: Lau kama makusudio katika hadithi yangekuwa ni kubomoa, basi ni kwa nini hakutoa fatwa mwanachuoni ye yote wa Kiislamu kuyabomoa? Zaidi ya hapo ni kwamba, kulisawazisha kaburi na ardhi ni kinyume cha sunna ya Kiislamu na mapendekezo ya kisheria; kwani inapendekezwa na sheria kaburi linyanyake kuliko ardhi, na hii ndiyo fatwa waliyoitowa mafaqihi wote wa Kiislamu kwamba kaburi liinuke kutoka katika ardhi kiasi cha shibri moja. Katika kitabu cha Al-Fiqhu Alal-Madhaahibil-arba'ah (Fiqhi kwa mujibu wa madhehebu manne) kuna maelezo yafuatayo: "Ni Sunna kuinua udongo juu ya kaburi kiasi cha shibri moja".[1] Basi itapokuwa muelekeo huu wa kwanza haukubaliki itakuwa ni lazima kuifasiri hadithi hii kwa kutumia muelekeo wa pili ufuatao.

## MUELEKO WA PILl

Makusudio ya neno "Tas-wiyatu l-Qabri" itakuwa ni kulisawazisha kaburi likawa sawa kwa sawa kinyume na makaburi ambayo hujengwa kwa umbile Ia samaki au nundu ya ngamia. Kwa msingi huu hadithi itakuwa inakusudia kwamba, sehemu ya juu ya kaburi iwe imetandazwa sawa sawa, na haifai kuwa kama mgongo wa samaki au nundu ya ngamia, kama wafanyavyo baadhi ya Waislamu wa Madhehebu ya Kisunni. Maimamu wa Madhehebu ya Kisunni (isipokuwa Imam Shafi'i) wametoa fatwa kwamba inapendekezwa kulifanya kaburi kama nundu.[2] Na kwa ajili hii basi hadithi hii inathibitisha ukweli wa fatwa ya wanachuoni wa Kishia na Kishafi'i ambao wanasema kwamba, "Inapasa kulisawazisha kaburi na kuliinua kuliko ardhi". Muslim katika sahihi yake ameileta hadithi hii ya Abul-Hayyaj pamoja na hadithi nyingine (ambayo tutaitaja) kwenye Babul-Amri Bitas-wiyatil-Qabri, na vile vile At-Tir-midhi na An-Nasai katika Sunan zao wameileta hadithi hii kwenye hiyo hiyo Babul-Amri Bi Tas-Wiyatil-Qabri.

1. Al-Fiqhu Alal-Madhaahibil-arba'ah, juz. 1, uk.420.
2. Al-Fiqhu Alal-Madhaahibil-arba'ah, juz. 1, uk. 420.

Na makusudio ya Babul-Amri Bitas-wiyatil-Qabri ni (kujulisha) kwamba kaburi linatakiwa liwe ni lenye kusawazishwa, na lau ingekuwa makusudio ni kulisawazisha na ardhi basi ingekuwa lazima kuuita mlango huu kuwa ni "Babul-Amri bi TakhiriibilQuburi Wahadmiha" yaani mlango wa kuharibu na kubomoa makaburi. Manna tuliyoieleza juu ya neno Tas-wiyah lililo ndani ya hadithi ndiyo unayoweza kuikuta katika lugha ya Kiarabu, kwani neno Tas-wiyah linapotumika kwenye kitu kama kaburi, manna yake huwa ni kwamba, hilo kaburi lisawazishwe na siyo lilinganishwe na kitu kingine kama vile ardhi. Hebu tuangalie hadithi nyingine aliyoitaja Imam Muslim katika Sahihi yake, hadithi ambayo inayo madhumuni yale yale tuliyoyateuwa: "Kunnaa Maa Fadhaalah Ibn Ubaid Biardhir Ruum, Biraudasi, Fatuwufiyya Sahibun lana, Faamara Fadhaalah Ibn Ubaid Biqabrihi Fasuwwiya Thumma Qaala, Samitu Rasulallahi Ya'muru Bitas-wiyatiha". Maana Yake: Tulikuwa pamoja na Fadhaalah ibn Ubaid huko Ruum (katika sehemu iitwayo) Raudas; basi mwenzetu (mmoja) akafishwa; na Fadhaalah ibn Ubaid akaamuru lichimbwe kaburi lake (kisha tulipokwisha mzika) akalisawazisha halafu akasema: Nilimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akiamuru kuyasawazisha makaburi.[1].

Kwa kifupi ufunguo wa kuifahamu hadithi liii umejificha katika tamko Ia "Sawwaitahu", na ndani yake mna uwezekano wa kupatikana maana tatu. Pamoja na kuzifahamu dalili na Qarina hapana budi kuchagua maana moja tu. Maana hizo tatu ni hizi zifuatazo: Ya Kwanza: Maana yake iwe ni kuyabomoa majengo yaliyojengwa juu ya kaburi. Na maana hii ni batili kwa sababu makaburi yaliyokuwepo Madina zama hizo hayakuwa na maqubba au madharih. Ya Pili: Iwe maana ya "Tas-wiyah" ni kulisawazisha kaburi na ardhi. Maana hii pia haikubaliki kwa kuwa Sunna iliyothibiti inaamuru kuliinua kaburi kiasi cha shibri moja. Ya Tatu: Maana yake iwe ni kulisawazisha kaburi na kurekebisha (likae sawa) na wala isiwe kuliinua kama ngongo wa samaki au nundu ya ngamia. Na maana hii ndiyo maana inayokusudiwa. Kwa hiyo haina uhusiano na makusudio wanayoyatolea ushahidi Mawahabi. Sasa hivi ndugu msomaji, hebu muangalie Al-Allamah Annawawi ambaye ndiye aliyeandika Sharhi ya Sahihi Muslim na uone ni vipi alivyoisherehesha hadithi hiyo:

Anasema: "Innas-Sunnata Annal-Qabra la Yurfa'u Anil Ardhi Kathiran wala Yusannamu, bal Yurfau Nahwa Shibrin wayusattahu."[2] Maana Yake: Iliyo sunna ni kwamba, kaburi lisiinuliwe (muinuko) mkubwa kutoka ardhini bali liinuliwe kiasi cha shibri lizawazishwe. Katika ibara hii inadhihiri kwamba mshereheshaji wa Sahih Muslim amefahamu maana ile ile tuliyofahamu katika hadithi hii, kwamba Imam Ali [a.s] alimuusia Abul-Hayyaj kuyabadilisha makaburi yenye kunyanyaliwa mno au yale yenye maumbile kama mgongo wa samaki yasawazishwe na wala hakuamuru kuyasawazisha na ardhi. Na sisi katika kutoa maana hii ndani ya hadithi hii hatuko peke yetu bali amesema pia Al-Hafiz Al-Asqalani katika kitabu chake Irshaad as-sraari fi sharhi Sahihil-Bukhari. Baada ya yeye kutaja kwamba iliyo sunna katika kaburi ni kulisawazisha; na kwamba haifai

1. Sahihi Muslim, juz. 3 Kitabul Janaiz, uk. 61.
2. Sharhu Sahihi Muslim Lin-Nawai.

kuiacha sunna hii eti tu kwa sababu kufanya hivyo imekuwa ni alama ya marafidhi (anakusudia Mashia) kwani hakuna upinzani baina ya kusawazisha kaburi na hadithi ya Abul-Hayaj. Al-Hafiz Al-Asqalani anasema kama ifuatavyo:

"....Ni kwamba (katika hadithi hiyo) hapakukusudiwa kusawazishakaburi na ardhi bali alichokusudia ni kulisawazisha (yaani kuliweka sawa) na kwa hiyo tunakusanya maana za haadithi zote." Baada ya yote haya lau ingekuwa maana ya wasia wa Imam Ali [a.s] kwa Abul-Hayyaaj ni kubomoa maquba na majengo yaliyojengwa kwenye makaburi, basi ni kwa nini Imam [a.s] hakuamuru kuyabomoa maquba ambayo yalikuwa kwenye makaburi ya Manabii katika zama zake? Pamoja na kwamba inaeleweka kuwa yeye Imam Ali [a.s] alikuwa ndiyo mtawala wa nchi zote za Kiislamu na alikuwa akiyafahamu maquba yaliyojengwa kwenye makaburi ya Manabii huko Palestina, Syria, Iraq, Misri, Iran na Yemen, (lakini hakuyabomoa). Na tukiyafumbia macho maelezo yaliyotangulia hivi punde, na tukakadiria kwamba Imam Ali [a.s] alimuamuru Abul-Hayyaj kuyabomoa makaburi yaliyoinuliwa na ayasawazishe kabisa na ardhi, basi ndani ya hadithi hiyo hakuna kinachojulisha wajibu wa kubomoa majengo yaliyojengwa kwenye makaburi, kwa kuwa Imam Ali [a.s] alisema (iwapo tutakadiria kuwa hadithi hiyo imesihi):

"Wala Qabran illa Sawwaitahu" (wala kaburi ila ulisawazishe); na wala hakusema "wala Binaan Wala Qubbatan Illa Sawwaitahuma" (yaani wala jengo wala quba isipokuwa uyabomoe). Kwa kuwa uchunguzi wetu katika maudhui haya hauhusu kaburi lenyewe, bali majengo yaliyojengwa juu ya kaburi, kwa kuwa majengo haya yaliyoko kwenye makaburi waumini huwa wanapata kivuli kwa ajili ya kusoma Qur'an, dua na kusali, basije, katika sentensi hii (wala Qabran 1lla Sawwaitahu) kuna chochote kinachojulisha kuyabomoa majengo haya na kumbukumbu ambazo zinawasaidia wenye kuzuru makaburi hayo kufanya ibada na kuwakinga kutokana na joto au baridi?

### UWEZEKANO WA MAANA MBILI MWISHONI

Mwisho wa uchunguzi kuna maana mbili nyingine hatuwezi kuepuka kuzitaja ili kukamilisha maudhui hayo. Ya Kwanza: Ni kwamba hadithi hii (ya Abul-Hayyaj na nyinginezo zinazofanana) ni ishara ya yale yaliyokuwa yamezoweleka kwa baadhi ya nyumati zilizopita ikiwa ni pamoja na kuyafanya makaburi ya wachamungu kuwa ndiyo kibla chao wakayaelekea wakati wa ibada. Watu hao pia walikuwa wakiweka picha kwenye kaburi, kwa hiyo waliacha kuelekea kibla aliyowaamuru Mwenyezi Mungu wakati wa ibada na wakayaelekea makaburi hayo. Na kwa maana hii basi, haiwezekani kwa hadithi hii kuwa na uhusiano wowote na makaburi ya Waislamu, na wala haijapata kuonekana kwa Muislamu yeyote kuyaelekea makaburi katika swala au kuyasujudia; isipokuwa mwenendo wa Waislamu ni kuswali jirani ya makaburi bila ya kuwa yenyewe ndiyo kibla chao, bali nyuso zao zinaelekea upande iliko Al-Kaaba, nao husimamisha swala na kusoma kitabu cha Mwenyezi Mungu huku wakiwa karibu ya makaburi. Na kama Waislamu wanakwenda kuzuru makaburi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu, na wakatumia huko muda mrefu kufanya ibada ya Mwenyezi Mungu Mtukufu karibu na malazi hayo matukufu, basi si kwa jingine ila ni

kwa sababu ya utukufu uliyopatikana kwenye ardhi hizo kwa kuwepo watu watukufu waliozikwa mahali hapo.

Jambo hili ufafanuzi wake utakuja baadaye. Maana ya Pili: Ni kwamba, makusudio ya kauli ya Imam Ali [a.s] kwa Abul-Hayyaj aliposema: "Anlaa Tada'a Timthaalan Illa Tamastahu, Wala Qabran Mushrifan Illa Sawwaitahu", makusudio yake kusema "At-Timthal" ni mapicha na masanamu, na "Al-Qabr" ni makaburi ya washirikina ambayo yalikuwa yakienziwa na kuheshimiwa na wahusika. Kwa kifupi ni kwamba hadithi ya Abul-Hayyaj haina uhusiano wowote kabisa na kujenga juu ya makaburi, isipokuwa inahusu makaburi yaliyoinuliwa mno (kama ilivyoelezwa hapo kabla) au makaburi ya washirikina na masanamu. Maelezo yafuatayo tunataja fatwa ya Maimamu wa Madhehebu manne ya Kisunni kuhusu kujenga juu ya makaburi."

"Yukrahu An-yubnal-qabru Bibaytin au Qubatin au Madrasatin au Masjidin."[1] Maana Yake: Ni karaha kulijengea kaburi katika nyumba au Qubbah au chuo au msikiti. Basi maadamu Maimamu wa Madh-hebu nne za Kisunni wameafikiana kuwa ni karaha tu kuyajengea makaburi basi ni vipi Qadhi wa Najdi anathubutu kutoa fatwa ya uharamu wa kuyajengea? "Kwa hakika huu ni uzushi. Tena tunajua kwamba fatwa ya ukaraha wa kujenga juu ya makaburi haitegemei dalili sahihi yo yote, na hasa itapokuwa jengo hilo linamsaidia mwenye kuzuru hapo aweze kusimamisha mambo ya faradhi ya dini na kusoma Qur'an kwenye jengo hilo.

## D. HADITHI YA JABIR

Hadithi ya Jabir inafahamika kuwa ni miongoni mwa hadithi wanazozitegemea Mawahabi kuharamisha kujenga juu ya makaburi; na imepokewa hadithi hii katika Sihah na Sunan kwa matamko tofauti tofauti, na wanapatikana katika Sanadi zake zote na mapokezi yake wanapatikana watu wawili.

1. Ibnu Juraih
2. Abuz-Zubair.

Na ili kuthibitisha kusihi kwa hadithi hii itategemea kuzifahamu hali za wapokezi wake na watu wa Sanad yake. Katika maelezo yafuatayo tutaitaja hadithi hiyo kwa matamko mbali mbali tena tofauti: Imekuja katika Sahihi Muslim (Babun-Nahyi 'An Tajsisil-Qabri Wal-Bina'i Alaih) Hadithi ya Jabir iliyopokelewa kwa njia tatu na katika aina mbili:

1. Ametusimulia Abubakar ibn Abi Shaiba, ametusimulia Hafsu ibn Ghiyath, kutoka kwa Ibn Juraih, naye toka kwa Abuz-Zubair kutoka kwa Jabir, amesema: "Amekataza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kulipaka kaburi jasi (aina ya chokaa) na kulikalia na kujengea juu yake."

2. Amenisimulia Harun ibn Abdillah, ametusimulia Hajaaj ibn Muhammad, na amemsimulia Muhammad ibn Raafi', ametusimilia 'Abdur-Razzaq, wote hawa wamepokea toka kwa Ibn Juraih, amesema: Alinieleza Abuz-Zubair kwamba yeye alimsikia Jabir ibn Abdillah anasema, "Nilimsikia Mtume..... (kama ilivyo hadithi ya hapo awali).

3. Ametusimulia Yahya ibn Yahya, ametusimulia Isma'il ibn Ulayyah kutoka kwa Ayyub, naye toka kwa Abuz-Zubair toka kwa Jabir; amesema:

1. Al-Fiqhu Alal Madhahibi-l-arba'a, juz. 1, uk. 421.

Amekataza kuyapaka makaburi jasi.[1] Na imekuja katika Sahihi Tirmidhi hadithi moja na kwa njia moja (kwenye Babu Karahiyyati Taj-sisil-Quburi Wal-Kitabati Alaiha) kama ifuatavyo:

4. Ametusimulia 'Abdur-Rahman ibn Al-Aswad, ametueleza Muhammad ibn Rabi'ah, kiltoka kwa Ibn Juraih naye toka kwa Abuz-Zubair kutoka kwa Jabir; amesema: Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amekataza kuyapaka jasi makaburi na kuyaandika juu yake na kuyajenga juu yake na kutembea juu yake.

Kisha baada ya kuandika hadithi hii At-Tirmidhi anaeleza kwamba imepokewa kwa al-Hasan Al-Basri na Shafi'i, kuwa wao wametoa fatwa kuruhusu kuyapaka makaburi jasi.[2] Na katika Sahih Ibn Majah, imekuja (katika Babu Ma Ja'a fin-nahyi Anil-Bina'i Alal-Quburi Wataj-sisiha Wal-Kitabati 'alaiha) hadithi hii kwa njia mbili na aina mbili, nazo ni hizi zifuatazo:

5. Ametusimulia Azhar ibn Marwan na Muhammad ibn Ziyad, wamesema: Ametusimulia 'Abdul Warith kutoka kwa Ayyub naye toka kwa Abuz-Zubair naye toka kwa Jabir; amesema: "Amekataza Mtume wa Mwenyezi Mungn kuyapaka makaburi jasi."

6. Ametusimulia Abdallah ibn Said ametusimulia Hafsi kutoka kwa Ibn Juraih naye toka kwa Suleiman ibn Musa kutoka kwa Jabir, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu amekataza kuandikwa chochote juu ya kaburi".[3]

Na baada ya kuitaja hadithi hii As-Sindi aliyeisherehesha anaandika akimnukuu Al-Hakim An-Nishapuri kwamba hadithi hii ni sahihi lakini haifuatwi, kwani viongozi wa Uislamu mashariki ya dunia na magharibi yake sera yao imekuwa ni ya kuandika juu ya makaburi kizazi baada ya kizazi.

Na imekuja hadithi hii katika Sahih An-nasa'i (katika Babul-Bina'I Alal-Qabri) kwa njia mbili na kwa namna mbili zifuatazo:

7. Ametueleza Yusuf ibn Sa'id amesema: Ametusimulia Hajjaj kutoka kwa Ibn Juraih amesema, amenieleza Abuz-Zubair kwamba yeye alimsikia Jabir anasema: "Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amekataza kuyapaka makaburi jasi au kujenga juu yake au yeyote yule kuyakalia."

8. Ametueleza Imran ibn Musa amesema, ametusimulia 'AbdulWarith amesema, ametusimulia Ayyub kutoka kwa Abuz-Zubair nayr kutoka kwa Jabir amesema: "Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amekataza kuyapaka jasi makaburi.[4] Na hadithi ya Jabir imekuja katika Sunan Abi Dawuud (Juzuu ya tatu ukurasa 216), "Babul-Bina'I Alal-Qabr) kwa njia mbili na namna mbili zifuatazo:

9. Ametusimulia Ahmad ibn Hanbal, ametusimulia 'Abdur-Razzaq, ametusimulia Ibn Juraih, amenieleza Abuz-Zubair kwamba yeye amemsikia Jabir anasema, nimemsikia Mtume amekataza kukalia kaburi, na kupakwa jasi na kujenga juu yake."

---

1. Sahihi Muslim kitabul janaiz Juz. 3, uk. 62.
2. As-Sunan At-Tirmidhi Juz. 2 uk. 208 Chapa ya Maktabatus Salafiyyah.
3. Sahih Ibn Majah, juz. 1 kitabul-Janaiz uk. 473.
4. Sahih An Nasa'i juz. 4 uk. 87-88.

10. Ametusimulia Musaddad na Uthman bin Abi Shaibah amesema: Ametusimulia Hafsu ibn Ghiyath kutoka kwa lbn Juraih naye toka kwa Sulaiman ibn Musa na kutoka kwa Abuz-Zubair kutoka kwa Jabir amenisimulia hadithi hii (iliyotajwa kabla). Amesema Abu Daud: Amesema Uthman "au kuliongeza", na akaongeza Suleiman ibn Musa "au kuandikwa juu yake". Ama Ahmad ibn Hanbal (Imam wa madhehebu ya Kihanbal) yeye ameipokea hadithi hii katika Musnad yake kwa namna ifuatayo:

11. Imepokewa toka kwa 'Abdur-Razzaq naye kapokea kwa Ibn Juraih: Amenieleza Abuz-Zubair kwamba yeye amemsikia Jabir ibn Abdilahi anasema: Nimemsikia Mtume akikataza mtu kukalia kaburi na kulipaka jasi na kulijenga juu yake.[1] Haya ndiyo mapokezi yaliyopokelewa toka kwa Jabir kuhusu maudhui haya, na tumeitaja hadithi hii kwa mapokezi tofauti tofauti na Sanad zake mbali mbali. Sasa hivi umefika wakati wa kuitafiti na kuichunguza ndani yake ili tuone je, hadithi hii inafaa kutolea ushahidi au hapana?

## DALILI ZA UDHAIFU NDANI YA HADITHI HII

Hadithi hii ya Jabir ma mkusanyiko mkubwa wa nukta mbali mbali za udhaifu, kiasi kwamba nukta hizo zinaiangusha isiwezekane kuitolea hoja na kuizingatia, na haiwezekani kabisa kuitolea ushahidi kwa namna yoyote ile. Maelezo yafuatayo tutataja nukta za udhaifu uliyomo katika hadithi hii: Kwanza: Katika sanad zote za Hadithi hii yamo majina ya Ibn Juraih (Abdul-Malik ibn Abdul-Aziz ibn Juraih AI-Amawi) na Abuz-Zubair (Muhammad ibn Muslim Al-Asadi) kwa pamoja au likawepo Ia mmoja wao. Tutakapofahamu mazingira ya hawa wapokezi wawili na hali zao, basi hakutakuwa na sababu ya kutaka kuwafahamu wapokezi wengine waliomo katika hadithi hii, ambao baadhi yao hawatambuliki na wengine wanaosababisha hadithi hii iwe dhaifu. Katika kitabu kiitwacho Tahdhibut-Tahdhib cha Ibn Hajar Al-'Asqalani utasoma maoni ya wanachuoni wa Rijal (wanaotambua wapokezi wa hadithi) juu ya ibn Juraih kama ifuatavyo:

Yahya ibn Said aliulizwa kuhusu hadithi za Ibn Juraih, akasema: "Ni dhaifu;" akaambiwa: "Hata kama akisema kuwa amenieleza fulani?" Akasema, "Usihadaike; si lolote; zote ni dhaifu".[2] Naye Ahmad ibn Hanbal amesema: "Iwapo Ibn Juraih atasema kuwa fulani amesema na fulani amesema, nami nimeambiwa, basi haya yote ni uzushi". Maana yake ni kuwa hadithi zake hazitambuliwi au ni za uzushi.[3][51] Naye Malik ibn Anas amesema: kuwa Ibn Juraih alikuwa akisenya kuni usiku (akikusanya kila kitu bila kuchagua kilicho sahihi na kisicho sahihi kama msenya kuni asenyeaye usiku hawezi kuona ni zipi kuni na wepi nyoka). Ama Ad-Daruqutni yeye amesema: Jiepushe na tadlisi ya Ibn Juraih, kwani tadlisi yake hi mbaya sana, yeye alikuwa hafanyi tadlisi isipokuwa kwa yale aliyoyasikia toka kwa mtu Majruh. (Mpokezi ambaye ubaya wake umebainishwa).

1. Musnad Ahmad, juz. 3, uk. 295 na 332.
2. Tah-dhibut-Tah-dhib, juz. 6 uk. 406.
3. Tah-dhibut-Tah-dhib.

Ibnu Hibbaan amesema: "Ibn Juraih alikuwa akidanganya katika hadithi"[1] Ewe msomaji, nakuapia Mwenyezi Mungu, hivi kweli inafaa kuchukuwa mapokezi ya mtu huyu pamoja na kuwa wanachuoni wa hadithi wamemshutumu na kuonyesha unyonge wake? Na je, inafaa kuacha sera ya Waislamu ya kujenga juu ya makaburi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu na kuyaheshimu kwa kutegemea hadithi za mpokeaji huyu mdanganyifu? Na je, inafaa tuwashutumu Waislamu kwa ushirikina na ukafiri na upinzani kwa kuwa wanaupenda mwenendo wa Kiislamu na wanafuata sera ya watu wema waliopita ya kujenga juu ya makaburi na kuyazuru na kuyaheshimu? Maelezo haya yaliyopita ndiyo baadhi ya yalioandikwa kuhusu Ibn Juraih.

Ama Abuz-Zubair, msikilize lbn Hajar huyu hapa anataja kauli za wanachuoni wa Rijal wasemavyo: "Imepokewa kutoka kwa Abdullah ibn Ahmad ibn Hanbal, naye amepokea toka kwa babaye (Imam wa Kihanbal) naye toka kwa Ayyub kwamba yeye alikuwa akimfahamu Abuz-Zubair kuwa hi mpokezi dhaifu. Na imepokewa toka kwa Shu'bah kwamba, Abuz-Zubair alikuwa hawezi hata kuswali vizuri. Na imepokewa tena toka kwa Shu'bah amesema: Hapakuwepo katika dunia mtu nimpendaye mno kuliko yule ajaye kisha nikamuuliza habari za Abuz-Zubair; basi nilifika Makka nikawa napokea toka kwake, ghafla nikiwa nimekaa kwake alikuja mtu na akamuuliza swali fulani, basi alimjibu lakini alizusha uongo; basi mimi nikasema: "Ewe Abuz-Zubair, unamwambia uzushi mtu Mwislamu?" Akajibu:- "Hakika yeye amenikasirisha".

Nikasema: "Basi yeyote anayekukasirisha unamzushia? Basi kamwe sitapokea hadithi yoyote toka kwako". Na imepokewa toka kwa Warqaa amesema: "Nilimwambia Shu'bah, vipi mbona umeziacha hadithi za Abuz-Zubair"? Akasema: "Nilimuona akipima, na anapunguza kipimo". Ibn Abi Hatima amesema: "Nilimwuliza baba yangu kuhusu Abuz-Zubair; akasema: "Hadithi zake zinaandikwa lakini hazitolewi ushahidi." Anasema tena: Na nilimwuliza Abu-zar'ah kuhusu Abuz-Zubair. Akasema: "Watu wanapokea toka kwake". Nikasema: "Hadithi zake hutolewa ushahidi?"

Akasema: Hutolewa ushahidi hadithi za watu waaminifu. (Akiwa na maana kuwa Abuz-Zubair siyo mwaminifu.)[2] Naam! Ewe ndugu yangu ....... hii ndiyo hali ya Ibn Juraih na Abuz-Zubair; nao ndiyo miongoni mwa wapokezi wa hadithi ya Jabir katika Sanad zake zote. Basi, je inawezekana kutolea ushahdi hadithi ambayo ndani yake wamo wapokezi wawili hawa? Na hapo kabla ilitangulia ishara kwamba ndani ya Sanad za hadithi hii wamo wapokezi wanyonge zaidi ya Ibn Juraih na Abuz-Zubair, kama vile Abdur-Rahman ibn Aswad anayetuhumiwa kuwa ni mwongo tena mzushi. Basi je, inafaa kubomoa athari za watu wa nyumba ya Mtume [a.s] na athari za Masahaba na kuwanasibisha Waislamu kuwa wamepotea kwa muda wa karne zote kumi na nne kwa kutegemea hadithi hii dhaifu isiyokubalika? Nukta ya Pili: Hakika hadithi ya Jabir inamvurugano sana katika matamko na matni yake, na mvurugano huu unajulisha kuwa wapokezi wa hadithi hii walikuwa hawana uwezo wa kudhibiti na kufuatilia riwaya (mapokezi),

1. Tah-dhibut-Tah-dhib.
2. Tahdhibut Tahdhib, katika maelezo juu ya Abuz-Zubair.

pamoja kuwa na uwezo wa kudhibiti ni moja ya masharti anayotakiwa kuwa nayo Rawii (mpokeaji).

Kwa mvurugano uliyomo kwenye hadithi hii, uaminifu unakosekana, na pia imani na mategemeo ya hadithi hii vinaondoka. Hebu endelea kuona ufafanuzi zaidi katika kuitafiti hadithi hii: Hadithi hii ya Jabir imepokewa katika namna saba, pamoja na kuwa Mtume **[s.a.w.w]** aliitamka kwa tamko la aina moja tu. Angalia namna hizo saba zilivyo:

1. Amekataza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kulipaka kaburi jasi na kuliegemea. Hadithi Na. 1, 2 na 9.

2. Amekataza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kulipaka kaburi jasi. Hadithi Na. 5 na 8.

3. Amekataza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kulipaka kaburi jasi na kuliandika na kujenga juu yake na kutembea juu yake. Hadithi Na. 4.

4. Amekataza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kuandika juu ya kaburi. Hadithi Na. 6.

5. Amekataza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kukaa juu ya kaburi na kulipaka jasi na kulijenga na kuliandika juu yake. Hadithi Na. 10.

6. Amekataza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kukaa juu ya kaburi na kulipaka jasi na kujenga juu yake. Hadithi Na. 11.

Hapa iko tofauti baina ya hadithi hii na ile ya kwanza, kwani ile ya kwanza imekataza kuliegemea kaburi na hii inakataza kukaa juu ya kaburi.

7. Amekataza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kukaa juu ya kaburi na kulipaka jasi na kujengea juu yake na kuliongeza na kuliandika.

Tunaona katika sura hii kumeongezwa kwenye kukaa, kupaka jasi na kujenga kuna ziada ya kuliongeza kaburi na kuandika juu yake. Baada ya yote haya utaona kuna hitilafu katika matni za hadithi na sentensi zake, kwani katika namna ya kwanza anasema (Al-'itimadu) kuegemea, na ya tatu (Al-wat'u) kutembea, na ya tano na ya sita: (Al-qu'udu) kukaa. Hivyo basi hakuna uwezekano wa kuikubali hadithi hii na kuitegemea kwa mwanachuoni yeyote kutokana na mvurugano uliyomo.

Nukta ya Tatu: Hadithi hii iwapo itakadiriwa kuwa ni sahihi na kupuuza mvuragano uliyomo, haijulishi zaidi ya kuwa Mtume **[s.a.w.w]** alikataza kujenga juu ya makaburi, lakini haijulishi kuwa jambo hilo ni haramu kwani kukataza (Nah-yi) kumegawanyika vigao viwili: Kuna Nahyi Tahriim na Nahyi Karaha. Yaani kukataza kwa kuharamisha na kukataza kwa karaha. Na hiki kigawo cha pili kimekuja mara nyingi mno katika hadithi za Mtume **[s.a.w.w]** na Maimamu watukufu [a.s]. Ni kweli kwamba nahyi kwa asili yake inajulisha kuharamisha na tahriim ndiyo inayothibiti kwanza mpaka ije dalili ya kugeuza uharamu na kuwa karaha, lakini wanachuoni hawakufahamu katika hadithi hiyo isipokuwa karaha tu. Kwa mfano utamwona At-Tirmidhi ameitaja hadithi hiyo katika Sahihi yake chini ya anuani isemayo, "Karahiyyatu Taj-sisilqubur " (Ukaraha wa kupiga lipu makaburi.).

Na ushahidi uliyo wazi zaidi ni kuwa As-Sindi aliyesherehesha Sahih Ibn Majah amemnakili Al-Hakim An-Nishapuri amesema kwamba, "Hajalitumia katazo hili Mwislamu yeyote;" kwa hiyo hakulizingatia kuwa ni Nahyi Tahriim kwa dalili kuwa, sera ya Waislamu iko kwenye kuandika juu ya makaburi. Kingine ambacho ni ushahidi vile vile kuwa Nahyi hiyo ni

Nahyi karaha ni maafikiano ya madhehebu za Kiislamu kuwa inafaa kujenga juu ya kaburi isipokuwa ardhi iliyowekwa wakfu kisheria. Anasema mashereheshaji wa Sahih Muslim alipokuwa akifafanua hadithi hii: "Ama suala la kujenga juu ya kaburi, iwapo (ardhi) ni mali ya mjengaji basi ni karaha (kujenga) na kama ni (ardhi) ya wakfii basi ni haramu (kujenga).[1]

Katika mambo yasiyohitaji maelezo marefu ni kuwa kitu kinapokuwa karaha basi ukaraha wake huondoka kwa kuyazingatia baadhi ya mambo fulani muhimu. Kwa mfano: Ikiwa kujenga juu ya kaburi itakuwa ni sababu ya kuhifadhi asili ya Uislamu na kudhihirisha mapenzi kwa mwenye kaburi hilo ambaye Mwenyezi Mungu amefaradhisha kumpenda au kujenga huko kutakuwa ni sababu ya kuhifadhi athari za Uislamu au itafanya wakusanyike wenye kuzuru mahali hapo chini ya jengo hilo ili wasome Qur'an na kuswali na kusoma dua, basi moja kwa moja karaha hiyo itaondoka. Si hivyo tu bali jambo hilo litakuwa ni mustahab, lenye kupendekezwa kufanywa, na litakuwa katika mlango wa kuhuyisha desturi na urithi wa dini na ni kuimarisha mambo matukufu ya Kiislamu.

1. Sahih Muslim, Juz. 3 uk. 62 chapa ya Misri.

5

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## KUTOLEA USHAHIDI HADITHI ZINGINE MBILI

Kwa kukamilisha uchunguzi tunataja hadithi zingine mbili ambazo Mawahabi wanazitegemea katika maudhi haya: Amepokea lbn Majah katika Sahih yake kama ifuatavyo:

(1) Ametusimulia Muhammad ibn Yahya, ametusimulia Muhammad ibn Abdullah Ar-Riqashi ametusimulia Wahab ametusimulia Abdur-Rahman ibn Yazid ibn Jabir kutoka kwa Qasim ibn Mukhaimara, naye amepokea toka kwa Abu Sa'id: Hakika Mtume amekataza kujengwa juu ya kaburi.[1] Na anasimulia Ahmad ibn Hanbal, hadithi ingine kwa sanadi mbili ambazo ni kama ifuatavyo:

(2) Ametusimulia Hasan, ametusimulia Ibn Lahi'a, ametusimulia Buraida ibn Abii Habib, amepokea toka kwa Na'im kijana wa Ummu-Salama, naye kapokea kutoka kwa Ummu-Salama amesema: Amekataza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kujenga juu ya kaburi au kupakwa jasi.

Kuhusu hadithi ya kwanza, inatosha kuwa dhaifu kwa kuwa miongoni mwa wapokezi wake yumo mtu aitwaye "Wahab", ambaye hali yake haitambuliki; kwani kuna watu kumi na sababa kila mmoja wao jina lake ni "Wahab" ambao hawakupambanuliwa wala kufahamika yupi ni nani. Na kati yao wamo wazushi na waongo, na katika hadithi hii Wahab huyu hakutambulika kuwa ni yupi katika hao, kwa hiyo riwaya hii inaporomoka. Ama hadithi ya pili inaanguka kwa kuwepo Abdallah ibn Luhay'ah katika Sanad yake. Adh-Dhabi anasema kuhusu mtu huyu: lbn Mu'in anasema: "(Mtu huyu) ni mdhaifu haitolewi kwake hoja. Al-Humaydi anasema: "Imepokewa toka kwa Yahya bin Sa'idi kwamba yeye (Yahya bin Sa'id) alikuwa hamuoni kuwa ni kitu chochote.[2] Sisi hatutajadili Sanadi ya hadithi hizi mbili, bali tutatosheka na kuonyesha nukta moja muhimu nayo ni kuwa: Wanahistoria na wanahadithi na wanasira wameeleza kuwa mwili wa Mtume **[s.a.w.w]** umezikwa katika nyumba ya Bibi Aisha kwa maafikiano ya Masahaba. Na kuchaguliwa kwa nyumba ya Bibi Aisha kulitimia kwa kutegemea kauli yake Mtume **[s.a.w.w]** kwamba "Kila Nabii huzikwa pale alipofia".[3] Na sasa linakuja swali lifuatalo:

Ikiwa Mtume alikataza kujenga juu ya kaburi, basi vipi waliuzika mwili wake Mtukufu katika nyumba yenye paa, kisha wakajenga ukuta katikati ya nyumba hiyo na hivyo kulifanya kaburi tukufu la Mtume **[s.a.w.w]** kuwa ni jengo maalum wanalolikusudia waumini na Waislamu kulizuru? Katika mambo yanayochekesha ni kauli ya mwandishi mmoja wa Mawahabi wanaopinga ukweli anaposema: "Kilicho haramu ni kujenga juu ya kaburi na siyo kuzika ndani ya jengo, kwani walimzika Mtume ndani ya jengo na

1. Sahih Ibn Majah, Juz. 1, uk. 474.
2. Mizanul-I'tidal, juz. 3, uk. 476.
3. (1) Musnad Ahmad, juz. 1, uk. 72 (2) Sahih Tirmidhi, juz. 2, uk. 139 (3) Tabaqat Bin Saad, juz. 2, uk. 71 na vinginevyo.

hawakujenga chochote kwenye kaburi lake.[1] Mwandishi huyu amelazimika kuandika kauli hii ya kipumbavu kwa kuwa analiona kaburi la Mtume limejengewa jengo na Qubbah, na lau si hivyo angeharamisha pia kuzika ndani ya nyumba vile vile. Hebu mwangalie ni vipi alivyotoa fatwa kutoka katika nafsi yake bila ya kuangalia yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu ili ayaridhishe matamanio yake pamoja na mwelekeo wake potofu!!

Nasi tunamwuliza Wahabi huyu mpotovu, je, kilicho haramu ni kujenga juu ya kaburi tu lakini kubakisha jengo siyo haramu? Au ni kwamba jengo ni haramu kulijenga na kulibakisha? Ikiwa kilicho haramu ni jengo tu, sisi tunauliza ni kwa nini basi serekali ya mabavu ya Kisaudi kwa dhulma na uzushi ilizibomoa athari za Mtume na makaburi ya Maimamu watukufu [a.s] na makaburi ya Masahaba na ya watoto wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, pamoja na kuwa, kwenu ninyi Mawahabi kilicho haramu ni kujenga jengo tu, na wala siyo kulibakisha jengo lililokwisha jengwa? Zaidi ya haya, hukmu hii muitowayo iko kinyume na fatwa ya viongozi wenu waliotangulia kama vile Ibnul Qayyim Al-Jauziyya na Ibn Taimiyya, kwani anasema Ibnul Qayyim "Ni wajibu kuyabomoa maziyara yaliyojengwa kwenye makaburi na wala haifai kuyaacha yabakie hata siku moja baada ya kuwa na uwezo wa kuyabomoa.

Kwa msingi huu basi hawezi Wahabi huyu muovu kusema kuwa ni haramu kujenga tu, ili asije akawakhalifu waliomtangulia kuingia motoni, na wala hawezi kukwepa hukmu yao ya kuharamisha kujengea na kuyabakisha. Hapa linakuja swali lifuatalo: Ni kwa nini Waislamu waliuzika mwili wa Mtume **[s.a.w.w]** ndani ya jengo? Ni kweli kwamba hawakujenga jengo kwenye kaburi lake isipokuwa kule kuzikwa kwake hapo kulipelekea kaburi liwe ndani ya jengo lenye paa. Na utamwona Wahabi huyu muovu anajaribu kulikwepa swali hili na kutoa fatwa aonayo yeye badala ya vile alivyoteremshwa Mwenyezi Mungu - kama ilivyo kawaida yao Mawahabi. Eti anasema: "Kubakisha (jengo) kuliko haramu ni lile lililojenwa kwenye kaburi, ama ikiwa jengo ndilo lililo tangulia kaburi, basi kulibakisha siyo haramu." Angalia ni jinsi gani anatenganisha katika hukmu na kutoa fatwa aonavyo yeye ili ajitenge na msimamo wa Waislamu wa tangu zama hizo na anajaribu kuikwepa haki ambayo inampinga.

## KUPINGANA KWA SERA YA WAISLAMU NA MAWAHABI

Nukta hii ambayo maelezo yake yametangulia hapo kabla, siyo pekee ambayo inayoweka wazi kutofautiana kwa Mawahabi na sera ya Waislamu kwa muda wote wa karne kumi na nne. Bali tofauti zipo pia katika mambo mengine mengi mno. Kwa mfano: Mawahabi wanazingatia kuwa kutabaruku (kutaka baraka) kwenye athari za Mtume **[s.a.w.w]** ni haramu, wanakataza jambo hili kwa nguvu zote; wanasema "Hakika jiwe na udongo havinufaishi chochote." Lakini utawaona Waislamu wanasongamana kwenye Hajarul-Aswad (Jiwe jeusi, lililoko kwenye Al-Kaaba) ili walibusu na kuligusa ili wapate baraka kwalo, na wanasongamana kwenye Kiswa cha Al-Kaaba (nguo inayofunikwa al-Kaaba) ili wajipanguse kwacho, na kwenye Al-Kaaba, wanavibusu vitu hivyo na kuweka mashavu yao juu

1. Kitabu Riyadhil-Jannat kilichoandikwa na Muqbil ibn AI-Hadi Al-wadi/chapa ya Kuwait.

yake. Basi Waislamu wanabusu jiwe na udongo na wanatofautiana na Mawahabi ambao wanasema eti jiwe na udongo havisaidii kitu. Vile vile Mawahabi wanakataza kujenga msikiti karibu na Makaburi ya Mawalii, wakati ambapo katika kila nchi ya Kiislamu kunapatikana misikiti iliyojengwa karibu na maziyara, hata katika ardhi ya Uhudi, palikuwepo Msikiti uliokuwa karibu na kaburi Ia Sayyidina Hamza [r.a], lakini Mawahabi walipoikalia ardhi hiyo tukufu wakaubomoa Msikiti huo na kuifuta athari yake.

Sasa hivi utaona kaburi tukufu la Mtume **[s.a.w.w]** liko katikati ya Msikiti na Waislamu wanaswali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu katika pembe zake zote. Kwa hakika iko mifano mingi ya jambo hili duniani. Hebu ona tofauti kubwa iliyoko baina ya Mawahabi na mwendo wa Waislamu, kitu ambacho kinajulisha kujitenga kwa Uwahabi kutoka kwenye Uislamu na kujitenga kwa Mawahabi kutoka kwa Waislamu.

haramu." Angalia ni jinsi gani anatenganisha katika hukmu na kutoa fatwa aonavyo yeye ili ajitenge na msimamo wa Waislamu wa tangu zama hizo na anajaribu kuikwepa haki ambayo inampinga.

## KUZUA DALILI POTOFU KWA KUKWEPA KOSA

Mawahabi wametegemea kuzua hoja dhaifu zitakazowaruhusu kuyabomoa makaburi matukufu na maquba ya Maimamu watukufu [a.s] katika Baqii. Miongoni mwa hoja walizozizua kuhusu jambo hili ni kwamba: "Baqii ni ardhi iliyowekwa waqfu na ni wajibu itumike kwa lengo lililokusudiwa na huyo muwekaji wa waqfu, na ni wajibu kuondosha kila kitu kitakacholazimisha kuzuia matumizi ya lile lengo, na kujenga na kusimika nguzo na kuta katika ardhi hii ni jambo linalolazimisha kuzuia matumizi ya sehemu fulani ya Baqii, kwani ardhi ya Baqii ni waqfa kwa ajili ya kuzika wafu, na ukweli ni kwamba kusimika nguzo na kuta kwa ajili ya ujenzi kunaziba sehemu ya ardhi, kwani haiwezekani kuzika chini ya nguzo na kuta, na jambo hili linasababisha kuzuia matumizi ya lengo lililokusudiwa. Na kwa ajili hii basi ni wajibu kuondosha kila kitu kilichoko katika ardhi hii ya Baqii ikiwa ni pamoja na majengo ili iwezekane kuzika katika sehemu yote ya Baqii.

**Jibu Letu**: Hapana shaka kwamba aina ya ushahidi kama huu ni kutoa maamuzi bila kufikiri na ni kuukwepa ukweli halisi. Qadhi huyu wa Kiwahabi katika fatwa yake hiyo analenga kuondoa athari za watu wa nyumba ya Mtume **[s.a.w.w]** kwa hali yoyote iwayo japo atakuwa hana dalili lakini anaamuru zivunjwe kwa nguvu na uzushi ataouzua. Na dalili hii aliyoitoa haina chochote isipokuwa ni kuwahadaa Waislamu wa kawaida kuwa eti ametoa fatwa kwa mujibu wa hukmu aliyoiteremsha Mwenyezi Mungu, na ndiyo maana utamwona anauzingatia uwanja wa Baqii kuwa ni ardhi iliyowekwa waqfu kwa ajili ya kuzikia. Lakini dalili yao hii ni, kama zile dalili zao zingine, haifai kwa namna nyingi.

Ya Kwanza: Haikuja katika kitabu chochote miongoni mwa vitabu vya historia na hadithi habari yoyote inayoashiria kuwa ardhi ya Baqii iliwekwa waqfu, na hakuna mwana historia ye yote au mwanachuoni wa hadithi aliyebainisha jambo hili. Angalia katika vitabu vya historia hutaona chochote kuhusu kauli hiyo; bali inawezekana kabisa kwamba ardhi ya Baqii ilikuwa ni mahali palipoachwa kwa matumizi ya watu wote kwa jumla

kama ilivyo katika ardhi zingine za aina hii; na watu wa Madina walikuwa wanazika wafu wao hapo. Na kwa maelezo haya ni wazi kuwa ardhi ya Baqii asili yake ilikuwa ni mubah (halali) kwa watu wote ambayo ilikuwa inafaa kuitumia na watu kwa matumizi mbali mbali na kwa namna yoyote.

Katika zama hizo zilizopita watu walikuwa hawapupii kumiliki ardhi tupu isiyotumika, kwani hawakuwa na uwezo wa kujenga pote ila mahala padogo. Na kadhalika watu kuhamia mjini toka vijijini lilikuwa jambo ambalo halijaanza kutokea kwa wingi. Na hapakuweko mas'ala ya ardhi, wala tatizo la watu wanaojilimbikizia ardhi au taasisi. Kwa hiyo basi ardhi kubwa ilikuwa imeachwa bila kuwa na mwenye kuimiliki. Na ardhi namna hii ndiyo ile iitwayo katika sheria ya Kiislamu kuwa ni ardhi (Al-Mubahat na Al-Ardhil-Mawat Al-Bairah). Kwahiyo desturi hii iliendelea katika miji na vijiji kutenga maeneo kwa ajili ya kuzikia, au pengine mtu mmoja alimzika jamaa yake mahali fulani kisha na wengine nao wakafuatia kuzika hapo bila ya kuangalia kabisa kuwa ardhi hiyo ni waqfu.

Na hii ardhi ya Baqii haiwezi kutoka kwenye desturi hii, kwani katika Hijazi yote na mji wa Madina ardhi haikuwa ni yenye thamani. Na kutokana na kuwepo kwa ardhi isiyotumika kuuzungaka mji wa Madina, haikuwa haja kwa mtu yeyote kutenga ardhi yake ya kilimo na kuiweka waqfu kwa ajili ya kuzikia, kwani ardhi ya kilimo ilikuwa ni ndogo kinyume cha ardhi tupu isiyotumika hiyo ilikuwa ni kubwa na ni miongoni mwa ardhi iliyo halali/kwa asili yake kwa matumizi mbali mbali. lnafaa kusema kwamba historia pia inaunga mkono ukweli huu kama asemavyo As-Samhudi katika kitabu kiitwacho "Wafaul Wafa". "Mtu wa kwanza ambaye Mtume alimzika hapo Baqii ni Uthman bin Maz'uun na alipofariki Ibrahim mtoto wa Mtume **[s.a.w.w]**, Mtume aliamuru azikwe mahali alikozikwa Uthman bin Maz'uun. Basi watu wakapapenda hapo Baqii na wakaikata miti, kisha kila kabila likachagua upande wake, na kuanzia hapo kila kabila likafahamu yalipo makaburi yao.

Uwanja wa Baqii ulikuwa na miti mingi ya gharqad, alipofariki Uthman bin Maaz'un na kuzikwa hapo Baqii, miti hiyo ikakatwa."[1] Kutokana na maneno ya As-Samhudi inadhihiri kwamba ardhi ya Baqii ilikuwa imeachwa bila mwenye kuimiliki na iligawanywa vipande vipande baada ya kuzikwa hapo sahaba mmoja, na kikatengwa kila kipande kwa ajili ya kabila fulani miongoni mwa makabila ya nyumba za hapo Madina. Ama eti Baqii kuwa iliwekwa wakfu huwezi kuona habari yoyote katika historia kuhusu jambo la wakfu, isipokuwa kinachofahamika katika historia ni kuwa sehemu walipozikwa Maimamu watukufu [a.s] katika Baqii palikuwa na nyumba ya Aqil ibn Abi Talib, na kwamba miili hiyo mitukufu ya Maimamu [a.s] imezikwa kwenye nyumba ambayo inarudi katika milki ya Bani Hashim.

Anasema tena As-Samhudi: "Amezikwa Abbasi ibn Abdil-Muttalib mahala alikozikwa Fatma bint Asad bin Hashim, sehemu ambayo ndiyo yenye makaburi ya mwanzo ya Bani Hashim yaliyoko katika nyumba ya Aqil." Na anasema tena:

Imepokewa toka kwa Said bin Muhammad bin Jubair kwamba yeye aliliona kaburi la Ibrahim mtoto wa Mtume hapo Azzawara' nayo ni nyumba

---

1. Wafaul-wafa juz. 2 uk. 84.

ambayo baadaye ilikuwa ya Muhammad bin Zaid bin Ali .... Na kwamba Mtume alimzika Sa'd ibn Mua'adh pembeni mwa njia iliyo ubavuni mwa nyumba ya Miqidad ibn AlAswad.... nayo ndiyo nyumba iitwayo kuwa ni "Daru Ibn Aflah" mwishoni mwa Baqii na ilikuwa juu yake kuna Qubbah."[1] Sentensi hizi zote kwa jumla zinasisitiza kwamba ardhi ya Baqii haikuwa wakfu na kwamba miili mitukufu ya Maimamu [a.s] ilizikwa katika nyumba zao walizokuwa wakizimiliki wenyewe. Baada ya maelezo yaliyotangulia, je, kweli inafaa kuzibomoa athari za kizazi cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** na kuzisawazisha na ardhi eti kwa hoja kwamba hazikubaliani na wakfu?

Lau tukikubali kwa ajili ya majadiliano kwamba eti ardhi ya Baqii imewekwa wakfu, basi je kuna kitu cha kuthibitisha namna wakfu huo ulivyowekwa? Basi huenda aliyeweka wakfu aliruhusu kusimamisha majengo na maquba juu ya makaburi ya watu watukufu wataozikwa katika ardhi hiyo. Sisi hatujui ufafanuzi wa mambo haya, lakini tunachokifahamu ni kuwa Waislamu walijenga majengo na maquba kwenye makaburi hayo na tunawajibika kukichukuliwa kusihi kitendo hicho na kujiepusha na tuhuma na kukinasibisha kuwa ni kitendo cha maasi.

Na kwa msingi huu basi, kubomoa maquba matukufu na majengo yenye kuheshimiwa inazingatiwa kuwa ni haramu na ni kinyume kabisa cha hukmu ya sheria. Na huyu Qadhi Ibn Balhid na wafuasi wake walikuwa wanatambua vizuri kwamba fikra ya kuifanya Baqii kuwa ni wakfu ni dalili iliyoundwa. Na hata kama shetani asingewaundia dalili hii potofu, wangeendelea tu kuvunja athari za kizazi cha Mtume wa Mwenyezi Mungu bila kusita, kwa kuwa mara hii siyo mara yao ya kwanza kwa Mawahabi walioundwa na Waingereza, kubomoa athari za Utume na Uislamu, kwani mara yao ya kwanza ilikuwa mwaka 1221 A.H.-1801 A.D., wakati walipoikalia Madina kwa mara ya kwanza na wakayavunja majengo hayo na kumbukumbu hizo, kisha yalijengwa tena baada Mawahabi kufukuzwa kutoka Madina kutokana na nguvu za Dola ya Uthmaniyyah.

## KUJENGA MSIKITI KARIBU NA MAKABURI MATAKATIFU

Je, kujenga msikiti kwenye makaburi ya watu wema au karibu yake kunajuzu au hakujuzu? Na kama inajuzu basi nini maana ya hadithi iliyopokewa kwamba "Mtume **[s.a.w.w]** amewalaani Wayahudi na Wakristo kwa kuwa wao waliyafanya makaburi ya Manabii kuwa mahala pa ibada". Je, matokeo ya kujenga msikiti karibu ya makaburi ya Mawalii hakuwezi kuambatana na laana iliyokuja katika hadithi hii? Jawabu: Kwa hakika kujenga msikiti karibu na makaburi ya watu wema hakuna kizuizi kabisa, kwani jambo hili limo ndani ya misingi ya Kiislamu ya jumla inayoruhusu mambo kama haya. Hali hiyo ni kwa sababu lengo la kujenga misikiti katika sehemu hizo ni kumwabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu karibu na makazi ya mmoja wa vipenzi vyake na Mawalii wake wema ambao kwa kuzikwa kwao hapo wameifanya ardhi ya mahali hapo kupata baraka na utukufu.

Na kwa maneno mengine tunaweza kusema kuwa, lengo Ia kujenga misikiti katika shemu hizo ni kuhamasisha utekelezaji wa faradhi za kisheria na ibada mbali mbali kabla ya kuzuru kaburi lililopo hapo au baada ya

1. Wafaul-wafa juz. 2, uk. 96.

kulizuru. Kimsingi, kuzuru makaburi siyo haramu hata kwa hao Mawahabi, na hivyo hivyo kusimamisha sala kabla ya ziyara au baada yake. Basi kauli ya kuharamisha kujenga msikiti karibu ya makaburi ya watu wema, ili kumwabudu Mwenyezi Mungu na kutenda faradhi zake, haina maana yoyote. Mazingatio yanayopatikana katika kisa cha As-habul-Kahfi yanatudhihirishia kwamba kujenga msikiti karibu ya makaburi ni Sunna iliyokuwa ikifuatwa na watu wa nyumati na sheria zilizopita.

Nayo Qur'an tukufu inaiashiria Sunna hiyo bila ya kuikosa wala kuipinga. Hapo kabla yametangulia maelezo kuhusu As-habul-Kahfi, wakati habari zao zilipojulikana baada ya kupita miaka 309, na watu walihitilafiana ni heshima na takrima ya aina gani waliyostahiki kufanyiwa hao As-habul-Kahf. Basi watu wakagawanyika makundi mawili.

1 Kundi moja wakasema, "wajengeeni jengo" ili kudumisha utajao wao.

2. Na kundi la pili ambalo ndilo lililopata ushindi lilitaka ujengwe msikiti kwenye pango hilo ili mahala hapo pawe ni kituo kwa ajili ya ibada ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, karibu na makaburi ya watu ambao walikataa kumwabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu na wakatoka katika nchi yao wakikimbia ukafiri na kwenda kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kumtii. Wameafikiana wafasiri wa Qur'an ya kuwa rai ya kwanza kuhusu hawa As-habul-Kahfi ilikuwa ni ya washirikina, wakati ile ya pili ilikuwa ni rai ya waumini.[1]

Na kwa rai hii ya pili Qur'an tukufa inasema: "Wakasema wale walioshinda kwenye jambo lao, tutawajengea msikiti juu yao." Na yamekuja maelezo katika historia kwamba kutokeza na kujulikana habari zao kulikuwa ni katika wakati wa ushindi wa Tauhidi dhidi ya shirki, na viongozi wa ushirikina waliokuwa wakihimiza ibada ya masanamu katika zama hizo walikuwa wameshindwa, basi rai ya kujenga msikiti ilitokana na wanaomuamini Mwenyezi Mungu na kumpwekesha. Basi kama itakuwa kujenga msikiti kwenye makaburi ya watu wema au karibu yake ni alama ya ushirikina, basi ni kwa nini rai hii ilitokana na waumini? Na ni kwa nini Qur'an imetaja rai yao hii bila ya kuikosoa wala kuipinga? Je, hiyo siyo dalili kwamba jambo hilo linajuzu kufanywa? Na haiwezekani kabisa kwa Mwenyezi Mungu kuyataja maneno ya washirikina kisha akapita tu bila kukemea na kukosoa kwa jumla au kwa ufafanuzi. Hakika huku ni kukiri kwa Qur'an juu ya kusihi kwa rai ya waumini, na iwe iwavyo ni kwamba kukiri kwa Qur'an ni hoja ya kisheria kama ilivyothibiti katika elimu ya Usulul-fiqh (Misingi ya Sheria ya Dini).

Hali hii inatuonyesha kwamba mwendo wa waumini wenye kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika ulimwengu wote ulikuwa ukitenda jambo hili na lilikuwa likizingatiwa kuwa ni moja ya namna ya kuheshimu mwenye kaburi na kutaka baraka kwake. Ilikuwa ni bora kwa Mawahabi kuyalinganisha (kuyapima) mas'ala haya kwenye Qur'an kwanza, kisha watafiti huku na huko katika hadithi tukufu. Katika maelezo yafuatayo tutataja mategemeo ya Mawahabi katika kukataza kwao jambo hili, ili tuonyeshe udhaifu wa mashiko hayo na ubatili wake:

1. Tafsir Al-Kash-Shaaf ya Az-Zamakhshari, na Ghara'ibul-Qur'an ya An-Nishapuri na nyinginezo.

## DALILI ZA MAWAHABI KATIKA KUHARAMISHA KUJENGA MISIKITI KARIBU YA MAKABURI YA WATU WEMA

Mawahabi wametegemea hadithi nyingi katika kuharamisha kujenga msikiti kwenye makaburi ya watu wema. Hapa tunataja hadithi hizo pamoja na kuzijadili na kuzitafiti: Bukhari katika Sahihi yake ametaja hadithi mbili kwenye "Babu Karahatit-Tikhadhil-Masajid Alal-Qubuur"

1. Alipokufa Al-Hasan ibn Al-Hasan ibn Ali, mkewe aliweka Qubbah juu ya kaburi lake, likadumu kwa mwaka mmoja kisha likaondolewa, kisha walisikia sauti ikisema, "Je, wamekipata walichokuwa wamekikosa?" Mwingine akajibu, "Hapana, isipokuwa wamekata tamaa wakarudi."

2. "Mwenyezi Mungu amewalaani Mayahudi na Wakristo, waliyafanya makaburi ya Mitume yao kuwa ni misikiti." Bibi Aisha amesema: "Lau si hivyo, basi wangelidhihirisha kaburi lake (Mtume), lakini mimi ninahofu watalifanya kuwa msikiti.[1] Muslim naye ameitaja hadithi hii pamoja na kuwa kuna tofauti ndogo, na ametaja vile vile ibara ifuatayo: ".......Fahamuni kwamba, waliopita kabla yenu walikuwa wakiyafanya makaburi ya Mitume yao na watu wema kuwa misikiti; basi msiyafanye makaburi kuwa ni misikiti, hakika mimi nakukatazeni jambo hilo."[2]

4. Hakika Umu Habiba na Ummu Salama walilitaja Kanisa moja waliloliona huko Ethiopia ndani yake mna picha za Wajumbe wa Mwenyezi Mungu. Basi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema: "Watu hao walikuwa kama kuna mtu mwema miongoni mwao akufa hujenga juu ya kaburi lake msikiti na wakachora humo picha hizo; basi hao ni viumbe waovu mbele ya Mwenyezi Mungu siku ya Kiyama."[3] Naye An-Nasai anasimulia katika kitabu chake Sunan (Babut-Taghliz Fit-Tikhadhis-Surji Alal Qubur):

5. Imepokewa toka kwa Ibn Abbas: "Mtume amewalaani wanawake wanaozuru makaburi na wanaoyafanya kuwa misikiti na kuyawashia taa".[4] Na utamuona Ibn Taimiyyah ambaye anaitakidiwa kuwa ndiyo mwanzilishi wa itikadi hii potofu, na Muhammad ibn AbdilWahhab ambaye anakula makombo ya Ibn Taimiyyah anazitegemea hadithi hizi kuharamisha kujenga msikiti juu ya makaburi ya watu wema au karibu yake. Amesema Ibn Taimiyyah: "Wanachuoni wetu wanasema: Haijuzu kujenga msikiti juu ya makaburi".[5]

## KUZIHAKIKI MAANA ZA HADITHI HIZI

Sasa hivi ni lazima kuzihakiki na kuzifanyia mazingatio hadithi hizi, ili tufahamu usahihi wa maana zinazozijulisha. Kabla ya kufanya kitu chochote ni lazima tujue kama asili ya jumla kwamba, kama ilivyo aya ya Qur'an kufasiriwa na aya nyingine, basi ndivyo ilivyo katika hadithi moja kuifasiri nyingine, na kuiweka wazi kutokana na utatanishi. Mawababi wameshikilia dhahiri ya hadithi moja na wakatoa uharamu wa kujenga msikiti juu ya makaburi ya watu wema au karibu yake, wakati ambapo lau

---

1. (1)Sahih Bukhari, kitabul-Janaiz Juz. 2 uk. 111. (2) Suna An-Nasai Juz. 2 uk. 871 Kitabul Janaiz.
2. Sahih Muslim, Juz. 2, uk. 68.
3. Sahih Muslim kitabul-Masajid, Juz. 2 uk. 66.
4. As-Suna cha An-Nasaiyy, juz. 3, uk. 7 Chapa ya Mustafa Al-Halabiy Misri.
5. Ziyaratul-Qubur, uk. 106.

wangezikusanya (hadithi) mahala pamoja na kuzichambua wangefahamu alichokikusudia Mtume **[s.a.w.w]**. Mawahabi hawa, wamejifungia wenyewe mlango wa Ijtihadi, kitu ambacho kimewafanya wazifasiri hadithi nyingi kwa tafsiri ya makosa. Mimi nasema: Hadithi walizozishikilia Mawahabi kuharamisha kujenga Msikiti juu ya kaburi, zitakubalika tu iwapo Sanad zake zitakuwa sahihi na wapokezi wake watakapokuwa waaminifu. Kinyume cha hali hii, hadithi hizo hazitafaa kutolea ushahidi kabisa.

Kwa kuwa kuzungumzia Sanad ya kila hadithi itasababisha maneno kuwa marefu, basi tunafupisha mazungumzo kwa maelezo yaliyomo ndani ya hadithi hizo na tunasema: Hadithi ya kwanza ni ile isemayo "Alipokufa Al-Hasan bin Al-Hasan mkewe aliweka Qubbah kwenye kaburi lake....." Hadithi hii inapinga madhehebu ya Mawahabi, kwani ni dalili inayoruhusu kuweka vivuli na Qubbah juu ya kaburi, na Mawahabi wao wanaharamisha moja kwa moja kuweka kivuli sawa kikiwa cha Qubbah au jengo.

Basi hadithi hii inajulisha ruhusa ya kuweka kivuli na kujenga Qubbah juu ya kaburi, na lau jambo hilo lingekuwa haramu lisingefanywa na mke wa Hasan bin Hasan, kwani kitendo hicho kilifanyika mbele ya macho na masikio ya Tabiina na wanachuoni wa Madina. Na huenda aliweka Qubbah hilo kwa ajili ya kusoma Qur'an kwenye kaburi ajikinge na joto, baridi na mengineyo. Na ama kauli ya mpokeaji wa hadithi aliposema: (Wakaisikia sauti inasema.....) Inafanana na kauli ya mtu asiyemcha Mungu, kwani kauli hiyo ni moja ya aina za kufurahia msiba wa mwingine, na kufurahia msiba wa mwingine siyo miongoni mwa tabia za wachamungu, na mfano ni huo huo kwa yule mwingine anayedaiwa kuwa alijibu.

Kwa mwanamke yule kuweka Qubbah juu ya kaburi Ia mumewe haikuwa lengo ni kumfanya mume huyo arudi mpaka aambiwe kuwa amekata tamaa, bali lengo lilikuwa ni kwa ajili ya kusomea Qur'an na ibada nyinginezo. Kifupi, kauli ya huyo anayedaiwa kusema na yule mwingine aliyejibu siyo hoja ya kisheria, kwani kauli zao siyo Qur'an wala siyo Sunna tukufu ya Mtume wala maneno ya Ma'sum. Ama kwa upande wa zile hadithi zinazowalaani Wayahudi na Wakristo na kuwahadharisha Waislamu kufanana na Wayahudi na Wakristo sisi tunajibu kwa kusema: Kufahamu makusudio ya hadithi hizo kutategemea kufahamu waliyokuwa wakiyafanya Wayahudi na Wakristo kwenye makaburi ya Manabii wao na kwa ajili hiyo ndiyo maana Mtume **[s.a.w.w]** akakataza kufanya waliyokuwa wakiyafanya Wayahudi na Wakristo.

Tutakapofahamu hilo, ndipo tutakapofahamu uharamu uliokatazwa. Katika hadithi zinapatikana dalili zinazoshuhudia kwamba Wayahudi na Wakristo walikuwa wakiyafanya makaburi ya Mitume wao kuwa ni kibla chao, na wanaacha kuelekea kibla inayowapasa kuielekea. Na zaidi ya hapo, walikuwa wakiwaabudu Manabii wao karibu na makaburi yao badala ya kumwabudu Mwenyezi Mungu Mmoja, au walikuwa wakiwafanya Manabii wao kuwa ni washirika wa Mwenyezi Mungu katika ibada. Basi ikiwa maana iliyoko katika hadithi hizo ni: Msiyafanye makaburi ya watu wema kuwa ni kibla chenu, au msiwafanye watu wema kuwa washirika wa Mwenyezi Mungu katika ibada, basi haiwezekani kabisa kuzitolea ushahidi kwa namna yoyote ile kuharamisha kujenga kwenye makaburi yao, kwani wanaozuru hawayafanyi makaburi hayo kuwa ni kibla chao wala

hawawaabudu wala kuwafanya washirika wa Mwenyezi Mungu katika ibada. Bali lililopo ni kwamba wote ni waumini wanaomwamini Mwenyezi Mungu na kumpwekesha na katika sala zao wanaelekea kwenye Al-Kaaba tukufu. Na lengo la kujenga msikiti kwenye makaburi hayo ni kupata tu baraka iliyopo kwenye ardhi hiyo ambayo imehifadhi miili yao mitukufu. Na muhimu sasa ni kuthibitisha kwamba lengo la hadithi hizo kukataza kuyafanya makaburi kuwa misikiti ni lile tulilolitaja. Hebu angalia dalili zinazojulisha hilo:

1. Hadithi iliyotajwa katika Sahih Muslim ni hadithi namba 4 nayo itafafanua hadithi nyingine. Wakati Mama Ummu Habiba na Ummu Salama, ambao wote ni wakeze Mtume **[s.a.w.w]**, waliposema kwamba wameona picha za Nabii katika moja ya Kanisa la Ethiopia Mtume **[s.a.w.w]** alisema: "**Hakika watu hao anapokuwepo miongoni mwao mtu mcha Mungu kisha akafa, hujenga kwenye kaburi lake msikiti na kuchora picha hizo**." Lengo la kuweka picha za wachamungu hao karibu na makaburi yao ilikuwa ni kwa ajili ya kuzisujudia na kusujudia makaburi, kiasi cha kuwa kaburi na picha inakuwa ndiyo kibla chao, au vikawa kama sanamu zinazoabudiwa na kusujudiwa. Hakika maana hii tuliyoitaja katika hadithi hii inakubaliana na mwenendo walionao Wakristo katika kumwabudia Masihi Mwana wa Mariamu, na kuweka picha na sanamu zake na za Bibi Mariamu [a.s]. Kwa maana hii tuliyokwisha ieleza, haiwezekani kutolea ushahidi hadithi hizi kuharamisha kujenga misikiti kwenye makaburi ya wacha mungu au karibu yake kama kutakuwa hakuna kitu kinachopelekea kuabudiwa kama ilivyo kwa Wakristo.

2. Anasimulia Ahmad ibn Hanbal katika Musnad yake, na Malik ibn Anas naye katika "Muwataa" ukamilifu wa hadithi hii, nayo ni kwamba Mtume **[s.a.w.w]** amesema baada ya kukataza kuyafanya makaburi kuwa misikiti: "**Ewe Mwenyezi Mungu usilifanye kaburi langu kuwa sanamu litaloabudiwa**".[1] Maneno haya yanajulisha kwamba watu hao walikuwa wakiyafanya makaburi na picha zilizokuwa kwenye makaburi hayo kuwa ni kibla cha kukielekea na wakiabudu masanamu kinyume cha Mwenyezi Mungu.

3. Mazingatio katika hadithi ya pili ya Bibi Aisha yanaongeza ufafanuzi wa ukweli huu, kwani yeye Bibi Aisha baada ya kupokea toka kwa Mtume **[s.a.w.w]** anasema: "**Lau si hivyo wangelidhihirisha kaburi lake Mtume, lakini mimi nachelea kuwa litafanywa kuwa msikiti**.

Tunajuiuliza: Kusimamisha ukuta pembeni ya kaburi kunazuia kitu gani? Ukweli ni kwamba ukuta unazuia kuswali juu ya kaburi lenyewe na kufanywa kuwa sanamu linaloabudiwa na kwa mukhtasari lisije kuwa kibla likaelekewa. Ama kuswali karibu ya kaburi bila ya kuliabudia kaburi au kulifanya kibla kwa ajili ya ibada hakuna kizuizi, sawa sawa kuna kizuizi kinachozuia kuliona kaburi au hapana na vile vile kaburi liwe limetokeza kwenye ardhi au hapana. Na hiyo ni kwa sababu Waislamu tangu karne kumi na nne zilizopita, wanaswaii karibu na kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** wakielekea kibla wakati huo wa kuswali na wanamwabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa hiyo kuwepo kizuizi hakuzuii yote haya.

1. Musnad Ahmad, juz. 3 uk 248.

Kifupi cha maelezo ni kwamba ukamilifu wa hadithi ya pili ambayo ina maneno ya Bibi Aisha unaiweka wazi maana ya hadithi, kwani Bibi Aisha anataja sababu ambayo iliyozuia kudhihiri kwa kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** ili kuepusha kufanywa msikiti, na kwa ajili hiyo ulijengwa ukuta pembeni ya kaburi tukufu la Mtume **[s.a.w.w]**. Kizuizi hiki kinazuia mambo mawili:

1. Ni kuzuia lisije likageuzwa kaburi hilo na kuwa sanamu na watu wakasimama kuliabudia, hivyo basi ikiwa kuna kizuizi haitawezekana kulionana halitafanywa sanamu kwa ajili ya ibada.

2. Ni kuzuia lisifanywe kuwa ndiyo kibla, kwani kulifanya kuwa ni kibla kutategemea kule kuonekana kwake. Iwapo mtu atasema: "Mbona Al-Kaaba ni kibla cha Waislamu wakati Waislamu wengi hawaioni Al-Kaaba wakati wa ibada? Jawabu lake ni kuwa: Haifai kulinganisha kaburi na Al-Kaaba kwa sababu AI-Kaaba ndiyo kibla cha Waislamu wote ulimwenguni. Na wala kibla hicho siyo kwa ajili ya ibada peke yake bali ni kwa ajili ya ibada na mengineyo kama vile kuchinja, kuzika na mfano wa hayo. Kwa hiyo Al-Kaaba ni kibla katika kila hali wala haina uhusiano wa kuonwa au kutokuonwa. Ama kule kulifanya kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** kuwa ni kibla jambo hilolinawezekana kwa wale waliomo katika Msikiti wake na wanaswali humo, hivyo kudhihiri kwa kaburi lake kunaweza kupelekea urahisi wa kulifanya kuwa kibla kwa mujibu wa fikra ya Bibi Aisha katika hadithi, kama vile alivyoona kwamba kulisawazisha na ardhi hakuna hatari hii.

3. Katika dalili zinazojulisha kwamba katazo la Mtume **[s.a.w.w]** ni kule kuyaabudu makaburi, ni kwamba wafasiri wengi waliosherehesha Sahih Bukhari na Sahih Muslim, wamefasiri hadithi hiyo kama tulivyoifasiri, na waliielewa kama tulivyoielewa sisi. Kwa mfano: Anasema AI-Qastalani katika kitabu kiitwacho Irshaadus Saari: "Hakika mwanzoni watu walitengeneza picha za wachamungu na Mawalii na Mitume, ili wajiliwaze kwa picha hizo na wakumbuke matendo yao mema, wapate kujitahidi kama walivyojitahidi wale, na wakawa wanamwabudu Mwenyezi Mungu kwenye makaburi yao, kisha walifuatia baadaye watu ambao hawakujua lengo la wazazi wao, na shetani naye akawashawishi kuwa wazazi wao walikuwa wakiziabudu picha hizi, ndiyo maana Mtume **[s.a.w.w]** akatahadhari jambo hili. " Anaendelea kusema: - "Baidhawi amesema: "Wayahudi na Wakristo walipokuwa wakisujudia makaburi ya Mitume wao ili kuwatukuza, na wakayafanya kuwa ndiyo kibla cha kuyaelekea wakati wa sala na wakayafanya kuwa masanamu, Waislamu wamekatazwa kufanya namna hiyo. Ama kule kujenga msikiti karibu ya kaburi la mtu mwema na kukusudia kupata baraka na siyo kumwabudu au kumwelekea kama kibla, jambo hili haliingii katika maonyo yaliyotajwa ndani ya hadithi."[1] Naye Ibn Hajar katika Fathul-Bari Juz. 3 uk. 208 amesema:

"Makatazo yako kwenye mambo yanayopelekea matendo waliyokuwa wakiyafanya Ahlul-kitab; ama kinyume cha hivyo hakuna ubaya". Na huyu AI-Qastalani siyo peke yake aliyesherehesha namna hii, bali pia As-Sindi aliyetoa Sherehe ya As-Sunan An-Nasai anasema: "Waliyafanya makaburi ya Mitume wao kuwa Misikiti" maana yake ni: Waliyafanya kuwa kibla

---

1. Ir-Shadus-Sari, Fi Sharhi Sahih Al-Bukhari.

wakati wa sala, au walijenga misikiti juu yake na wakawa wanasali humu, na inaonyesha kuwa huenda ukaraha huu unapelekea kule kuliabudu kaburi lenyewe." Anasema tena: "Mtume **[s.a.w.w]** anauonya umma wake wasije lifanya kaburi lake kama walivyofanya Wayahudi na Wakristo kwenye makaburi ya Mitume wao pale walipoyafanya kuwa ni misikiti, iwe ni kwa kusujudu au kuyafanya kuwa ni kibla cha kuelekea wakati wa sala". Naye An-Nawawi anasema katika Sherehe ya Sahih Muslim:

"Wamesema wanachuoni: Mtume amekataza kulifanya kaburi lake na kaburi la mwingine yeyote kuwa ni msikiti kwa kuchelea kuvuka mpaka wa kumtukuza na kufanya watu wapotee, jambo ambalo huenda likapelekea watu kukufuru, kama ilivyotokea kwa nyumati zilizopita. Na Masahaba na Tabiina walipotaka kuuongeza Msikiti wa Mtume **[s.a.w.w]** kutokana na ongezeko la Waislamu, uliongezeka mpaka nyumba za wakeze Mtume zikaingia katika msikiti kikiwemo chumba cha Bibi Aisha ambacho ndimo alimozikwa Mtume **[s.a.w.w]** na Masahaba wake wawili, basi walilijengea kaburi ukuta mrefu kulizunguka lisiwe linaonekana katika msikiti na watu wa kawaida (wasio na ujuzi wa kutosha) wasije wakaliabudia Na kwa ajili hii Bibi Aisha amesema katika ile hadithi "Lau si kuogopea hilo jambo wangelidhihirisha kaburi la Mtume, isipokuwa paliogopewa kuwa litafanywa msikiti". Yuko mshereheshaji mwingine anasema:

"Hakika hadithi ya Aisha inafungamana na Msikiti wa Mtume kabla haujaongezwa; ama baada ya kuongezwa na chumba che kuingizwa msikitini, chumba hicho kilijengwa kwa umbile la pembe tatu ili isiwezekane kwa yeyote kuswali juu ya kaburi.... Wayahudi na Wakristo walikuwa wakiwaabudu Mitume wao karibu na makaburi yao au wakiwashirikisha na Mwenyezi Mungu katika ibada". Mimi nasema: Pamoja na qarina zote hizi na vile walivyofahamu washereheshaji wa hadithi ni lazima pawe na maelezo kuhusu hadithi hii, na haiwezekani kupata matokeo kinyume chake au fatwa isiyokuwa hiyo. Tukizifumbia macho qarina hizi, tunaweza kutatua tatizo kama ifuatavyo:

**Kwanza**: Hadithi yenyewe ilivyokuja inalenga kuwa: "Kama msikiti wenyewe utakuwa umejengwa juu ya kaburi". Kwa maana hiyo haina uhusiano wowote na maziyara matukufu, kwa kuwa misikiti yote iko karibu na makaburi hayo wala siyo juu yake, kwa namna ambayo kila kimoja kiko mbali na mwenziwe. Kwa hiyo yale maziyara yanakuwa ni kwa ajili ya kuzuru na kutawas-sal kwa Mwenyezi Mungu kupitia kwa huyo Walii mwema, na ule msikiti uliyo karibu yake nikwa ajili ya kuswali na ibada nyinginezo.

Baada ya haya, basi vipi itawezekana kusema kwamba ni haramu kujenga Msikiti karibu na kaburi au ni karaha? Wakati ambapo kwa macho yetu tunauona Msikiti wa Mtume **[s.a.w.w]** uko karibu na kaburi lake tukufu? Iwapo Masahaba ni kama nyota na ni wajibu kuwafuata, basi ni kwa nini hawafuatwi katika jambo hili? Bila shaka wao (Masahaba) ndiyo walioongeza ndani ya msikiti wa Mtume nyongeza nyingi kiasi kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** limekuwa katikati ya msikiti, baada ya kuwa msikiti ulikuwa upande wa mashariki mwa kaburi hilo tukufu, na kwa sababu ya hizo nyongeza nyingi, upande wa magharibi nao ukaingia ndani ya msikiti.

Basi ikiwa kujenga msikiti karibu na makaburi ya watu wema ni haramu, ni kwa nini Waislamu waliziweka nyongeza hizi katika kila upande wa msikiti? Basi Je, lIe maana ya kuwafuata Salafa na Salafiyyah wanayoilingania Mawahabi iko katika kuwafuata kwenye maudhui moja tu na kuziacha zingine? Kwa hali hii tunafahamu kwamba maneno ya Ibnul-Qayyim anaposema kuwa "Kaburi na msikiti havikutani mahali pamoja" yanakhalifu mwenendo wa Waislamu waliopita hapo kabla; wala maneno yake hayana msingi wo wote wa kusihi.

**Pili**: Tunaweza kufahamu kutoka katika hadithi hizi (iwapo tutazikadiria kuwa ni sahihi) na kwamba Mtume **[s.a.w.w]** amekataza kujenga msikiti juu ya makaburi ya wachamungu au karibu yake. Lakini haipatikani dalili ya yakini inayothibitisha kwamba katazo hili ni katazo la kuharamisha, bali inawezekana kuwa ni Nahyi Tanzihi (karaha), na ndiyo maana Bukhari amezitaja hadithi hizi kwenye kitabu chake chini ya anuani isemayo "Babu Ma-yukhrahu Minittikhadhil-Masajid Alal-Qubur," (Mlango wa, ni karaha kujenga misikiti juu ya makaburi).[1] Na jambo hilo pia linashuhudia kwamba katazo limeambatanishwa na laana kwa wanawake wanaozuru makaburi".[2] Kilichothibiti ni kwamba kuzuru makaburi kwa wanawake ni makruhu kutokana na baadhi ya mambo fulani na wala siyo haramu.

Iwapo Mtume **[s.a.w.w]** anawalaani wanawake wanaozuru makaburi basi laana hiyo haijulishi kuwa jambo hilo ni haramu, kwani kutokana na mambo mengi ya karaha imekuja laana kwa mwenye kuyatenda katika hadithi nyingi, na lengo la laana hiyo, ni kuonyesha ukaraha mkubwa wa jambo hilo na kwamba (kulitenda) hi kujiweka mbali na Rehma za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa mfano, imekuja katika hadithi: "Mwenyezi Mungu amewalaani watu watatu; Mwenye kula chakula chake cha safari peke yake, na mwenye kulala ndani ya nyumba peke yake, na mwenye kusafiri jangwani peke yake".

Na inafahamika kwamba mambo haya matatu siyo haramu. Na hatimaye, tunasisitiza kwamba kujenga misikiti kwenye makaburi ilikuwa ni Sunna inayotendeka tangu mwanzo wa kuja Uislamu. As-Samhudi anasema katika hadithi ambayo ametaja kifo cha Bibi Fatma binti Asad "Mama wa Imam Ali [a.s]." "Alipofishwa (Bibi Fatma Binti Asad), Mtume **[s.a.w.w]** alitoka na akaamuru lichimbwe kaburi, likachimbwa mahala penye msikiti ambao leo unaitwa "Qabr Fatimah."[3] Anachokusudia As-Samhudi hapa ni kwamba "Mahali lilipokuwa kaburi la Bibi Fatma bint Asad paligeuzwa na kuwa msikiti". Anasema tena As-Samhudi:

"Hakika Mus'ab ibn Umair na Abdallah ibn Jahshi wamezikwa ndani ya msikiti ambao ulijengwa juu ya kaburi la Hamza".[4] Msikiti huo ulikuwepo mpaka pale uvamizi wa Kiwahabi ulipoivamia ardhi hii tukufu na kuubomoa msikiti huu na misikiti mingine pamoja na kumbukumbu nyingi kwa sululu za wakoloni wa Kiingereza.

---

1. Sahih Bukhari, juz. 2, uk. 111.
2. Sunan An-Nasai, juz. 3, uk 77, chapa ya Misri.
3. Wafaul-Wafa, juz. 3, uk 897.
4. Wafaul-Wafa, juz. 3, uk. 922-936.

6

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## KUZURU MAKABURI KWA MUJIBU WA QUR'AN NA SUNNA

Wanachuoni wa Kiislamu na wataalamu wa sheria ya Kiislamu wametoa fatwa inayoruhusu kuzuru makaburi, hasa yale ya Manabii na watu wema. Fatwa hii wameitoa hali ya kuwa wanategemea aya nyingi za Qur'an na hadithi za Mtume [s] zinazohusu jambo hiti. Zaidi ya Fatwa inayoruhusu jambo hili, wanachuoni hao wametoa Fatwa kusisitiza kufanywa ziyara kuwa ni jambo bora na pia ni mustahab. Ama Mawahabi, kama inavyodhihiri ni kwamba hawaharamishi asili ya kuyazuru, bali wanaharamisha kukusudia safari ya kuzuru makaburi ya watu wema. Kwa hiyo basi utafiti wetu juu ya jambo la kuzuru makaburi utakuwa katika sehemu mbili.

1. Ziyara.
2. Safari kwa ajili ya ziyara.

### KUZURU MAKABURI

Katika mambo yasiyo na shaka ndani yake ni kuwa, kuzuru makaburi huwa kuna jumuisha kupatikana athari muhimu za tabia njema na mafunzo mengine mema. Tunaonyesha kwa ufupi kama ifuatavyo: Kushuhudia uwanja uliotulizana kimya, ambao chini yake kuna idadi kubwa ya watu waliopata kuishi katika dunia hii kisha wakafariki, wakiwemo masikini na matajiri, wanyonge na wenye nguvu, kipindi hicho wakiwa hawana wanachokimiliki isipokuwa sanda, hali hii huutingisha moyo na roho ya mtu na kumpunguzia furaha na tamaa ya dunia na starehe zake. Lau mtu atauangalia uwanja huu wa makaburi kwa jicho Ia mazingatio, hakika atabadili mwenendo wake katika hii dunia na kuweka mazingatio yake akhera, na atakuwa akijiwaidhi mwenyewe kwa kusema: "Hakika maisha ya dunia ni ya muda na yatatoweka tu, na kwamba kipindi cha maisha ninayoishi kina mwisho na matokeo yake nitazikwa kaburini na kukandamizwa na rundo la udongo, na huko akhera kuna malipo ima mema au mabaya.

Kwa hiyo ataona kuwa maisha haya ya dunia haifai kwa mtu kusumbuka kutafuta mali na heshima na cheo kwa kumdhulumu huyu au yule, kitu ambacho kitamfanya achume dhambi na mambo maovu. Mtazamo wa makini kwenye uwanja hun uliotulia kimya, hulainisha moyo hata kama ulikuwa mgumu, na humfanya mtu asikie hata kama alikuwa kiziwi, na kuyafungua macho hata kama yalikuwa hayaoni, na zaidi ya hapo humfanya mtu asahihishe tabia yake na maisha yake na ajihisi kuwa analo jukumu kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mutukufu na watu.

1. Mtukufu Mtume **[s.a.w.w]** anasema: "Zuruni makaburi kwani yanakukumbusheni akhera".[1] Pamoja na ukweli kwamba Masala ya kuzuru makaburi hayahitaji kutolewa dalili na hoja juu yakusihi kwake na umuhimu

1. Sahih Ibn Majah, juz. 1 uk 113., Babu majaa fi ziyaratil-qubur.

wake, sisi tunalazimika kuyazungumzia kwa wale wenye shaka (ili tuwaondolee shaka yao).

## QUR'AN NA KUZURU MAKABURI

Mwenyezi Mungu anamkataza Mtume **[s.a.w.w]** kuswalia jeneza Ia mnafiki na kusimama kwenye kaburi lake anasema: "Wala usinisalie kamwe mmoja wao yeyote yule akifa, wala usisimame kaburini kwake hakika hao wamemkufuru Mwenyezi Mungu na mjumbe wake na wakafa hali ni mafasiki. Qur'an, 9:84. Aya hii tukufu inalenga kuvunja heshima (dhati) ya mnafiki na inatoa onyo mbele ya wanafiki wenziwe na wenye mfano kama huo. Kukatazwa kwa mambo mawili haya (kumsalia mnafiki na kusimama kaburini kwake) maana yake na maf-humu yake ni kwamba asiye mnafiki anastahiki kufanyiwa mambo haya mawili. Sasa tunalazimika tuangalie nini maana ya kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema: "Wala Taqum Ala Qabrih", (yaani wala usisimame kaburini kwake). Je, maana yake ni kuwa, kule kusimama kwenye kaburi ambako haifai kwa mnafiki, na kwa muumini inafaa, ni katika kipindi kile cha mazishi tu au maana yake inaenea tangu wakati wa kuzika na hata baada ya wakati huo? Jawabu ni kwamba: Baadhi ya wafasiri wameichunguza aya hii kwa uchunguzi au mtazamo finyu na wakatumia ile kauli ya kwanza, yaani ni ule tu wakati wa kuzika.

Lakini wengine kama vile Al-Baidhawi na wengineo wanaitazama kwa mtazamo mpana na wakasema: "Hakika katazo lililoko katika "Usisimame kaburini kwake", linaanzia tangu kuzika mpaka kumfanyia ziyara". Mtazamo wenye mazingatio unatupeleka kwenye maana hii tulioyoitaja hivi punde, maana ambayo ni pana. Hali hii inakuja kutokana na aya yenyewe kushikamana na sentensi mbili: Ya Kwanza: "La Tusali Ala Ahadinmin-hum Mata Abadan, Usimsalie kamwe mmoja wao yeyote yule akifa." Hakika tamko 'Ahadan" kwa sababu limefuata nafyi hufidisha umumu na Istighraqi kwa afradi zote na kadhalika. Tamko 'Abadan" linapokuja katika mtiririko wa kukanusha huwa linafidisha "Al-umumu Wal-istighraq Lijamiil-afrad" na tamko "Ahadan" huwa linafidisha "Al-istighraquz-zamani", yaani linaenea wakati wote.) Kwa hiyo maana ya aya itakuwa, "Usimsalie kamwe mmoja wao ye yote miongoni mwa wanafiki wakati wowote ule".

Baada ya kufahamu matamko mawili haya pia tunafahamu wazi kabisa kwamba, lengo la kukatazwa kumsalia maiti mnafiki halihusu sala ya maiti wakati wa mazishi tu, kwa sababu sala ya maiti haisaliwi mara kwa mara siku baada ya siku, bali maana ya sala katika aya hii kinachokusudiwa ni dua yoyote na kumuombea rehma, iwe ni wakati wa kuzika au baadaye. Lau ingekuwa imekusudiwa wakati wa mazishi tu, basi palikuwa hakuna haja ya kuwepo tamko "Abadan". Iwapo kuna mtu atasema: Tamko abadan ni kwa ajili ya kusisitiza kuenea afradi zote "Taukidil-istighraqil-afradi na siyo kwa ajili ya kusisitiza wakati. Jawabu lake ni hili ifuatalo:

1. Tamko "Ahadin" (yeyote) lilifidisha kuwakusanya na kuwaenea wanafiki wote (Basi hapakuwa na haja ya kuongeza Abadan).

2. Tamko "Abadan" katika lugha ya Kiarabu hutumiwa ili kuenea nyakati zote kama ilivyo katika kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema:

"Wala tankihuu Az-wajahu Min Baadihi Abadan", yaani: Wala musiwaoe wake zake baada yake kamwe". Qur an, 33:53.

Kwa hiyo basi matokeo yanakuwa kwamba, kilichokusudiwa ni kukataza kumrehemu mnafiki na kumuombea msamaha, sawa sawa kwa kumsalia au kwa jingine. Ya Pili: "La Taqum Ala Qabrih" - (usisimame kaburini kwake). Maf-humu ya jumla hii itakuwa, "Wala Taqum Ala Qabrihi Abadan" yaani, kamwe usisimame kaburini kwake". Na hii ni kwa kuwa jumla hii inaat-fia (inafuatia) ile jumla iliyotangulia "La Tusali Ala Ahadinmin-hum Mata Abadan." Kwa hiyo kila kilichothibiti kwenye kile kinachofuatwa yaani "Abadan" ambayo ni "Qayd" basi pia kitathibiti kwa hiki kinachofuata vile vile. Katika hali hii basi, haiwezekani kusema kwamba: "Makusudio ya kusimama kwenye kaburi ni wakati wa kuzika tu kwa sababu ya kutowezekana kukaririka kisimamo cha kuzika, kama tulivyoeleza kuhusu swala ya maiti. Na tamko Abadan lililokadiriwa kwenye hii jumla ya pili linafidisha uwezekano wa kukaririka tendo hili la kusimama kwenye kaburi. Hivyo basi inajulisha kwamba kusimama kwenye kaburi la mnafiki hakuhusu wakati wa mazishi tu bali wakati wote.

Na kama kuna msemaji atasema kuwa tamko "Abadan" lililokadiriwa katika jumia ya pili maana yake hi kuenea afradi zote. Sisi tutasema: "Maelezo ya hilo yamekwisha tangulia, na kwamba tamko "Ahadin" ndilo linalohusu istighraqi ya afradi zote wala siyo tamko "Abadan" ambalo ni istighraqi ya nyakati zote. Kwa hiyo maana ya aya tukufu itakuwa ni kwamba, Mwenyezi Mungu anamkataza Mtume **[s.a.w.w]** kumtakia Magh-fira na kumrehemu mnafiki, sawa sawa kwa kumswalia au kumuombea dua, na pia anamkataza kusimama kwenye kaburi la mnafiki, uwe ni wakati wa mazishi au wakati mwingine. Na Maf-humu yake ni kwamba, mambo haya mawili yanajuzu kufanyiwa "Muumini". Na kwa maelezo haya inathibiti kuwa inajuzu kuzuru kaburi la Muumini na inajuzu kuisomea Qur'an roho yake hata kama ni baada ya mamia ya miaka.

Kwa hiyo maelezo haya ni kwa munasaba wa Mar-hala ya kwanza nayo ni asili ya kuzuru makaburi kwa upande wa Qur'an inavyosema. Ama kwa munasaba huu wa ziyara kwa upande wa hadithi za Mtume **[s.a.w.w]** hebu tazama ufafanuzi wake kama ifuatavyo:

## HADITHI TUKUFU ZA MTUME [s.a.w.w] NA KUZURU MAKABURI

Kinachoeleweka katika hadithi tukufu za Mtume **[s.a.w.w]** ambazo wamezipokea hao wenye sihah na sunan ni kwamba: Mtume **[s.a.w.w]** alikataza kuyazuru makaburi kwa muda fulani na kwa sababu maalum, kisha baadaye aliondoa katazo hilo na akasisistiza kuyazuru: Na huenda sababu ya kukataza kwa muda ilikuwa ni kwamba, maiti hao walikuwa ni washirikina na waabudu sanamu, wakati ambapo Uislamu ulikuwa umekata kila aina ya mahusiano na shirki pamoja na washirikina, ndipo Mtume **[s.a.w.w]** akakataza kuwazuru wafu (kwenye makaburi yao). Na inatiwa nguvu fikra hii na kauli ya Mtume **[s.a.w.w]** wakati alipokuwa anazuru makaburi husema, "nyumba ya watu walioamini" kama tutakavyoeleza baadaye. Pia huenda sababu ya kukataza ikawa ni jambo jingine, nalo ni kwamba, Waislamu walikuwa bado ni wageni katika Uislamu, kwa hiyo walikuwa wakiomboleza wafu wao kwa maombolezo batili yanayoweza kuwatoa katika sehemu fulani ya sheria.

Na pale Uislamu ulipokuwa umeimarika katika mioyo ya Waislamu na kuzizoweya sheria na hukmu za Uislamu, hapo ndipo Mtume **[s.a.w.w]** kwa amri ya Mwenyezi Mungu akalibatilisha lile katazo la kuzuru makaburi kwa kuwa kuzuru makaburi kuna kumbukumbu na matokeo mema, na ndiyo maana wamepokea wenye sihah na sunan kwamba, Mtume **[s.a.w.w]** amesema: "Nilikuwa nimekukatazeni kuyazuru makaburi, basi sasa yazuruni kwani yanafanya musiipende (sana) dunia na yanakumbusha akhera".[1] Na kwamba msingi huu basi Mtume **[s.a.w.w]** mwenyewe alikuwa akilizuru kaburi la mama yake Bibi Amina binti Wahabi [r.a] na akiwaamuru watu kuyazuru makaburi kwani kuyazuru kunamkumbusha mtu akhera. Naye Muslim amepokea katika Sahih yake:

3. Mtume **[s.a.w.w]** alilizuru kaburi la mama yake, kisha akalia na waliokuwa karibu yake nao wakalia, kisha akasema; **Nimemuomba Mola wangu ruhusa ya kuzuru kaburi lake (Bibi Amina binti Wahabi) na ameniruhusu, basi nanyi yazuruni makaburi kwani yatakukumbusheni kifo**.[2] Naye Bibi Aisha amesema:

4. "**Hakika mjumbe wa Mwenyezi Mungu ameruhusu kuyazuru makaburi**".[3]

5. Na amesema tena Bibi Aisha kwamba, Mtume **[s.a.w.w]** amesema: "Ameniamuru Mola wangu niende Baqii nikawaombee msamaha." Mimi nikasema, "Basi nitasemaje ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu"? Mtume akasema; "Sema, As-salaamu Ala Ah-lid-diyari Minal-Muuminina Wal-Muslimina Yar-hamullahu Al-Mustaqdimina Minna WaI-Mustaakhirina, Wainna Insha-alIahu Bikumu Lahiquuna". Maana Yake: Amani iwafikie watu wa makazi haya miongoni mwa Waumini na Waislamu, Mwenyezi Mungu awarehemu waliokwisha tangulia miongoni mwetu na hao watakaokuja baadaye, nasi apendapo Mwenyezi Mungu tutakutana nanyi.[4] Na imekuja katika hadithi zingine zilizotaja maneno ambayo Mtume **[s.a.w.w]** alikuwa akiyasema wakati anapozuru makaburi. Maneno inengine ni haya:

6. As-salaam-Alaikum Dara Qaumimuuminina Wainnaa wa Iyyakum Mutawaaiduna Ghadan Wamuwakiluna, Wainna lnsha-allahu Bikum Laahiquuna Allahummagh-fir Li-ahlil-baqiil-gharqad.[5] Maana Yake: Amani ikufikieni enyi watu wa makazi haya ya waumini, sisi na ninyi tutakutana kesho na tutapata riziki pamoja toka kwa Mwenyezi Mungu nasi kwenu tutafika, Ewe Mwenyezi Mungu wasamehe watu wa Baqiiul-gharqad. Na imekuja katika hadithi nyingine iliyotaja maneno hayo kama ifuatavyo: "As-salaam Alaikum Ah-lad-diyari Minal-Muumina WalMuslimina, Wainna Insha-allahu Bikum Lahiquna, Antum Lana Far-tun Wanahnu Lakum

---

1. Sunan Ibn Majah, juz. 1, uk 114 Chapa ya India mlango wa kuzuru makaburi, Sahihi Tirmidhi milango ya Janaiz, juz ya 3, uk. 274.
2. Sunan Abi Dawood, juz. 2 Kitabul-Janaiz uk. 195 Chapa ya Misri, Sahihi Muslim, juz. 3, uk. 65 Babu Istiidhanin-Nabiyy Rabbahu Azza Wajalla Fi Ziyarati Qabri ummih, Sahihi Ibn Majah Juz. 1. uk. 114.
3. Sahih Ibn Majah juz. 1 uk. 114.
4. (1) Sahih Muslim juz. 2 uk. 63, Babu maa yuqalu inda dukhulil Qubur (2) Sunan An-Nasai juz. 3, uk. 76.
5. Sunan an-Nasai, juz. 4, uk. 76-77.

Tabaun As-Alullahal-afiyata Lana Walakum."[1] Maana Yake: Amani ikufikieni enyi wenye makazi haya mkiwa ni miongoni mwa Waumini na Waislamu nasi apendapo Mwenyezi Mungu tutafika huko mliko ninyi, ninyi mmetutangulia nasi tutakukuteni, namuomba Mwenyezi Mungu atupe afya nanyi pia akupeni afya. Na katika hadithi nyingine ya tatu:

As-salaamu Alaykum Dara Qaumi Muuminina Wainnaa Insha-allahu Bikum Lahiquna.[2] Maana Yake: Amani ikufildeni enyi wenye makazi nikiwa miongoni niwa waumini nasi apendapo Mwenyezi Mungu tutafika huko niliko. Na kutokana na hadithi ya Bibi Aisha inafidisha kwamba Mtume **[s.a.w.w]** alikuwa akitoka kila sika mwishoni mwa usiku na kwenda Baqii kisha husema: "As-salaamu Alaikum Dara Qaumimuuminina Waatakum Matuuaduna Waghadan Muwajaluna, Wainna Insha-allahu Bikum Lahiquna, Allahummaghfir Liah-li Baqiil-gharqad."[3] Maana Yake: Amani ikufikieni enyi wenye makazi mukiwa miongoni mwa waumini na akupeni Mwenyezi Mungu uliyokuahidini na kesho akupeni ahyokuwekeeni nasi apendapo Mwenyezi Mungu takukutana nanyi. Na katika hadithi nyingine inafidisha kwamba Mtume **[s.a.w.w]** alikuwa akizuru makaburi yeye pamoja na kundi miongoni mwa Masahaba wake, na akiwafundisha namna ya kuzuru makaburi.

Mtume alikuwa akiwafundisha Masahaba wake wanapotoka kwenda makaburini, basi msemaji wao alikuwa akisema: "As-salaamu Alaa Ah-lid-diyar, au husema: As-salamu alaikum Ah-lad-diyar Minal-Muumina Wal-muslimina wainnaa Insha-allahu Lahiquna, As-alullaha Lana Walakumul-afiyah." Maana Yake: Amani iwe kwenu watu wa makazi haya au Amani iwe kwenu enyi watu wa makazi miongoni mwa waumini na Waislamu, namuomba Mwenyezi Mungu atupe afya nanyi akupeni afya.[4]

## WANAWAKE NA KUZURU MAKABURI

Jambo la mwisho ambalo inapasa tulizungumzie, ni la wanawake kuzuru makaburi. Kuna mapokezi katika baadhi ya hadithi kwamba Mtume **[s.a.w.w]** amewakataza wanawake kuzuru makaburi: "Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amewalaani wanawake wanaozuru makaburi".[5] Pamoja na kuwepo hadithi hii kuna haja ya kufahamu kwamba, kuharamishwa wanawake kuzuni makaburi kwa hoja ya hadithi hii siyo sahihi kutokana na sababu nyingi tu.

**Ya Kwanza**: Wanachuoni wengi wanazingatia kuwa, kukatazwa huku ni (kwa karaha siyo kwa kuharamisha) na karaha kwenye jambo hili limekuja kutokana na sababu maalum zinazohusika na wakati ule. Mwandishi wa kitabu kiitwacho "Mif-tahul-hajat Fii Shar-hi Sahihi Ibn Majah" anaashiria sababu hizo na anasema: "Wametofautiana (wanachuoni) katika karaha (ya kuzuru makaburi) je ni karaha Tahriim au ni karaha Tanzih? Wengi wao wameruhusu (wanawake wazuru makaburi) kama hakutakuwa na fitna.[6]

---

1. Sunan an-Nasai, juz. 4, uk. 76-77.
2. Sunan Abi Dawood, juz. 2 uk 196.
3. Sahih Muslim juz. 3, Uk. 63 Babu Ma Yuqalu inda Dukhulil Qabri.
4. Sahih Muslim juz. 3, uk. 11, Babu Ma yuqalu inda Dukhulil-qabri.
5. Sahih Ibn Majah, Kitabul-Janaiz juz. 1 uk. 478, Chapa ya kwanza ya Misri.
6. Hawashii Sahih Ibn Majah juz. 1, uk. 114 chapa ya India.

**Ya Pili**: Hapo kabla imetangulia hadithi ya Bibi Aisha kwamba, Mtume **[s.a.w.w]** ameruhusu kuzuru makaburi. Rejea hadithi namba 4. Lau ruhusa hii ingewahusu wanaume peke yao, basi ingekuwa lazima kwa Bibi Aisha kulitaja jambo hilo hasa kwa kuwa yeye mwenyewe ni mwanamke, na pia lilikuwa ni jambo Ia kawaida kwa wanawake kuwepo katika msikiti wa Mtume **[s.a.w.w]** na kila aliyekuwa akisikia hotuba ya Mtume, alikuwa akifahamu kuwa kila hukmu (inayotolewa na Mtume) inamuhusu isipokuwa kama Mtume atabainisha wazi kutowahusisha wengine.

**Ya Tatu**: Pia imetangulia hadithi hapo kabla ya kuwa, Mtume **[s.a.w.w]** alimfundisha Bibi Aisha maneno yanayopaswa kusemwa wakati wa kuzuru makaburi, naye Bibi Aisha alikuwa akiyazuru makaburi baada ya Mtume **[s.a.w.w]** kufariki. Rejea hadithi namba 5.

**Ya Nne**: At-Tirmidhi anapokea hadithi kuwa; Abdur-Rahman bin Abubakr (nduguye Bibi Aisha) alipokufa huko Al-junta, waliubeba mwili wake hadi Makka na wakamzika hapo hapo, Bibi Aisha alipokuja Makka kutoka Madina alitoka kwenda kuzuru kaburi la nduguye na akasoma beti mbili za mashairi kuomboleza kifo cha nduguye.[1]

Aliyesherehesha Sahih At-Tirmidhi Al-Hafidh Ibnul-Arabi aliyezaliwa mwaka 435 Hijiriya na kufariki mwaka 543 anasema: "Iliyo sahihi ni kwamba, Mtume **[s.a.w.w]** aliwaruhusu wanaume na wanawake wayazuru makaburi, na yule asemaye kuwa ni karaha (wanawake kuzuru makaburi) hiyo ni kwa sababu ya woga walionao na uchache wao katika kusubiri au ni kwa kukosa kwao wanawake kuvaa hijabu."

**Ya Tano**: Bukhari anapokea kutoka kwa Anas kwamba yeye Anas amesema: "Siku moja Mtume **[s.a.w.w]** alipita akamkuta mwanamke analia kwenye kaburi, Mtume akamwambia mche Mungu na uwe na subira. Yule mwanamke akasema niondokee hapa hakika wewe hukufikiwa na msiba wangu, (na wala mwanamke huyu hakumtambua Mtume **[s.a.w.w]**. Baadaye yule mama akaambiwa, "Huyo ndiye Nabii", basi akaja nyumbani kwa Mtume akasema; "**Nilikuwa sikukufahamu". Mtume akasema; "Hakika subira iliyotimia iko mwanzoni wa msiba unapokupata**".[2] Kama kuzuru makaburi itakuwa ni haramu, Mtume angemkataza mwanamke yule kuzuru makaburi, lakini utaona kwamba Mtume anamuusia mwanamke yule kumcha Mungu na kusubiri wakati wa msiba, wala hamkatazi kuzuru makaburi.

**Ya Sita**: Bibi Fatma az-Zahraa ambaye ni Binti ya Mtume **[s.a.w.w]** alikuwa akitoka kila wiki mara moja au zaidi kwenda kulizuru kaburi la Bwana Hamza ambaye ni Ami yake Mtume **[s.a.w.w]**, na akiswali kaburini hapo na kulia.[3]

**Ya Saba**: Al-Qurtubi anasema: "Mtume **[s.a.w.w]** hakumlaani kila mwanamke anayezuru makaburi, bali amemlaani mwanamke ambaye anazuru makaburi mara kwa mara mfululizo, na dalili ya kuthibitisha hilo ni kauli ya Mtume aliyoitumia "Zuwwaratul-Quburi" na tamko Zuwwaaru ni tamko Ia Mubalagha na linajulisha kukaririka mara kwa mara". Na huenda

1. Sahih At-Tirmidhi Kitabul-Janaiz juz. 4, uk. 27.
2. Sahih Bukhari Kitabul-Janaiz juz. 2, uk. 79, Babu Ziyaratil-qubur.
3. Mustadrak As-sahihain lil-hakim juz. 1, uk. 277. Wafaul-Wafa juz. 2, uk. 112.

sababu ya kulaaniwa wanawake wanaozuru makaburi mara kwa mara mfululizo ni kwamba, wingi huo wa ziyara unapelekea kupoteza haki ya mume na pia kumsababishia mwanamke huyo kuwa ni mwenye kudhihirisha mapambo yake jambo ambalo limekatazwa, na atakuwa (pengine) ni mwenye kulia kwa sauti ya juu. Lakini iwapo ziyara ya wanawake makaburini itakuwa haina mambo yaliyoharamishwa hakuna ubaya ndani yake kabisa, kwani kukumbuka mauti na akhera ni katika mambo ambayo wanaume na wanawake wanayahitajia wote sawa kwa sawa.

**Ya Nane**: Kuzuru makaburi licha ya kupelekea (kumfanya mtu) kiipa nyongo dunia na starehe zake, pia kunamnufaisha maiti aliyelala chini ya rundo la udongo, kwani kwa kawaida ziyara makaburini inaambatana na kusomwa Suratul-Fatiha na kuizawaidia roho ya maiti (aliyekusudiwa). Na zawadi hii ndiyo zawadi bora aitoayo mtu aliye hai kuipa roho ya marehemu. Anasimulia Ibn Majah kwamba imepokewa kwa Mtume **[s.a.w.w]** amesema: "**Wasomeeni Surat Ya'asini maiti wenu**".[1] Basi iko wapi tofuati kati ya mwanamume na mwanamke katika jambo hili ili ziyara ya mmoja wao iwe inafaa na ya mwingine ni haramu, kama visingekuwepo vitu maalum vilivyoharamishwa ambavyo vimetajwa hapo juu? Na sasa baada ya kuthibitisha kwamba inajuzu kuzuru makaburi, umefika wakati wa kuzungumzia athari nzuri na matokeo mazuri ya kuzuru malazi (makaburi) ya mawalii wa Mwenyezi Mungu. Hayo tutayaleta katika sehemu inayofuata.

lliyochapishwa pamoja na sherehe ya Ibn Al Arabi Al Maliki. Tirmidhi anasema baada ya kuinakili hadithi hii kutoka kwa Buraidah "Hadithiya Buraidah ni Sahihi na inatumika kwa wanachuoni, na wala hawaoni ubaya wowote kuyazuru makaburi, na hiyo ndiyo kauli ya Ibn Al-Mubarak na Shafii na Ishaq." Na kuhusiana na sehemu hii ni bora kuzirejea zifuatazo:

(1.) Sahih Muslim, Juz 3, Babu is-Tiidhanin-Nabi Rabbahu azza wajalla Fi Ziyarat Qabri ummih, uk. 65.

(2.)Sahih Abu Dawood. Juz. 2, Kitabul-Janaiz Babu Ziyaratil-Qubur uk. 195.

(3.) Sahih Muslim, juz. 4, Kitabul-Janaiz Babu Ziyaratil-Qubur, uk. 73.

Nasema kwamba, sababu wanayoitaja kwa Mtume **[s.a.w.w]** kuomba ruhusa ya yeye kuzuru kaburi la mama yake ni (kama wanavyodai) kwamba, mama yake Mtume alikuwa mushriki lakini ukweli usio na shaka ni kwamba mama yake Mtume **[s.a.w.w]** alikuwa kama walivyokuwa babuzake Mtume **[s.a.w.w]** yaani alikuwa miongoni mwa watu wa Tauhid na Imani, kwa ajili hii mtazamo huu na tafsiri hii inakhalifu kabisa misingi ya aqida ya Kiislamu na inawezekana ikawa na tafsiri nyingine.

1. Sahih Ibn Majah, hadithi ya 1448.

7

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## MATOKEO MAZURI YANAYOPATIKANA KUTOKANA NA KUWAZURU WATU MUHIMU WA KIDINI

Makaburi yanayopata hadhi ya kutunzwa na kuheshimiwa na watu wanaomuamini Mwenyezi Mungu katika ulimwengu - hasa Waislamu ni yale ambayo mara nyingi yanakuwa ni makaburi ya watu ambao wamebeba ujumbe wa amani na kuufikisha kama ilivyotakiwa ufike. Watu hawa wamegawanyika sehemu tatu:

1. Manabii: Ambao ndiyo viongozi wa dini, walibeba mabegani mwao ujumbe kutoka mbinguni, walizitoa nafsi zao na mali zao pamoja na wanavyovipenda kwa ajili ya kufikisha ujumbe huo, na wakavumilia aina mbali mbali za taabu na matatizo ili wapate kuwaongoa watu.

2. Wanachuoni na wanafikra: Ambao ni kama mshumaa unaowangazia wengine wakati wenyewe unateketea.

Watu hawa waliishi maisha ya kichamungu na kujinyima na wakaupatia ulimwengu maelezo yenye thamani na uchambuzi mzuri, katika nyanja za elimu, fikra, tabia na elimu za maumbile na ufunuo kutoka mbinguni na elimu za ulimwengu, viumbe na mengineyo.

3. Mujahidina (wapiganaji Jihadi): Hawa ni wale wenye kupigania mabadiliko ambao walihuzunishwa na hali ya maisha ya jamii kutokana na dhulma na ubaguzi wa rangi na kabila na hawakuivumilia hali hiyo, wakapigana dhidi ya dhulma na ukandamizaji na wakadai heshima na haki za binadamu zilindwe, na wakajenga ngome ya uadilifu kwa kutoa damu zao zenye thamani kubwa. Mapinduzi yoyote au mabadiliko ya jamii hayalinganishwi na kitu chochote isipokuwa kwa kutoa kitu cha thamani ili mafaniko yapatikane. Na thamani ya mapinduzi inayoweza kubomoa tawala za madhalimu na kuwasonga koo, ni kutoa damu tukufu ambayo wapiganaji mashujaa hujitolea muhanga kwa damu hiyo ili kurejesha haki na uhuru kwenye nchi za Kiislamu.

Kwa hiyo watu huwa wanazuru makaburi ya watu wa aina hizi, na hutokwa machozi wawapo makaburini na huwa wanakumbuka ushujaa wao na kujitoa kwao muhanga, pia huziliwaza roho za mashujaa hao kwa kusoma Qur'an kisha kuwazawadia thawabu za visomo hivyo. Kadhalika huimba Qasida ambazo hutaja sifa zao na utukufu wao na kiwango cha daraja zao tukufu. Hakika kuzuru makaburi ya watu hawa muhimu ni moja katika aina ya kuwashukuru na kuwatukuza kwa kujitolea kwao na pia kujulisha kizazi kilichopo kuwa, hayo ndiyo malipo ya wale ambao hupita njia ya haki na uongofu na ubora, na ndiyo malipo ya wale wanaopigana na kulinda misingi ya itikadi (Uislamu).

Malipo yao ni kudumu kwa utajo wao, utajo ambao ni mwema na sifa nzuri hata kama ni muda mrefu umepita toka kufariki kwao. Mpaka hapa tumefahamu umuhimu wa kuhuyisha utajo wa watu hawa muhimu wa dini, na kwa msingi huu inapasa kufanya juhudi ili kuendelea kuzifanya kumbukumbu zao kuwa hai na kuzihifadhi na kusimamisha sherehe kubwa za kukumbuka siku za kuzaliwa kwao na kuvaa mavazi ya kuonyesha msiba na kufanya hafla za kuomboleza na kukumbuka kufa kwao, pia kufanya

vikao na mikusanyiko mikubwa na kutoa hotuba za kuwatambulisha watu hao watukufu na itikadi zao zilizopelekea wao wajitoe muhanga. Kadhalika kuyaheshimu malazi yao (makaburi) na kujiepusha na kila linalotia dosari heshima yao, kwani kuyaheshimu makaburi yao ndiko kuheshimu ujumbe wao na itikadi zao.

Kinyume cha hivyo ni kuyadharau na kuyapuuza makaburi yao, na itakuwa ndiyo kuudharau ujumbe wao na ni kuwadharau wao wenyewe. Katika siku zetu hizi, mtu anapoingia katika makaburi ya Baqii ili akazuru makaburi ya watu wa kizazi cha Mtume **[s.a.w.w]** na makaburi ya viongozi wa Kiislamu na watetezi wa dini na Masahaba, atayaona makaburi hayo yako katika hali inayohuzunisha kutokana na dharau yaliyofanyiwa, jambo ambalo linatetemesha nafsi na kuifanya ishangazwe na uovu wa kikundi cha Mawahabi ambao wanadai kuwa wao ndiyo watetezi wa Uislamu. Ajabu ni kwamba, kwa upande mmoja Mawahabi huwataja masahaba kwa wema na kuwasifu katika majukwaa ya hotuba zao, lakini kwa upande wa pili wanayaacha makaburi ya Masahaba bila ya heshima yoyote, na katika hali ya kusikitisha katika kuyadharau na kuyapuuza makaburi hayo, Mawahabi hawayajali kabisa hata kama wanyama wataingia na kuharibu sehemu ya makaburi ya Masahaba. Zawadi ya pekee ambayo Mawahabi huwapatia mahujaji na wanaozuru (makaburi ya Baqii) ni kuwaita kuwa ni washirikina na tendo lao la kuyazuru makaburi hayo ni tendo la shirki.

Mawahabi wanawaambia Waislamu maneno (haya machafu) kwa sababu tu Waislamu hao wanawaheshimu viongozi wa dini, na wanawatukuza Mawalii wa Mwenyezi Mungu. Hali hii inaonyesha kwamba, Mawahabi wanaficha mioyoni mwao chuki na kero waliyonayo dhidi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu na viongozi wa dini yake. Na sasa umefika wakati wa kuzungumzia ziyara ya kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** kwa mujibu wa mtazamo wa dalili za Kiislamu.

## KUZURU KABURI LA MTUKUFU MTUME

Katika maelezo yafuatayo tutatoa baadhi ya aya za Qur'an na hadithi tukufu za Mtume **[s.a.w.w]** ambazo zinahimiza kulizuru kaburi lake. Na tunataraji kuwa msomaji atapata maelekezo zaidi na kufahamu.

## USHAHIDI WA QUR'AN

Qur'an tukufu inawaamrisha wenye madhambi wafike mbele ya mjumbe wa Mwenyezi Mungu na wamuombe awaombee msamaha kwa Mwenyezi Mungu, kwani dua au maombi ya Mtume yatakubaliwa kwa ajili yao. Mwenyezi Mungu anasema:

وَلَوْ أَنَّهُمْ إِذ ظَّلَمُوا أَنفُسَهُمْ جَاءُوكَ فَاسْتَغْفَرُوا اللَّـهَ وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ الرَّسُولُ لَوَجَدُوا اللَّـهَ تَوَّابًا رَّحِيمًا ﴿٦٤﴾

"Na lau wangelikuja kwako walipojidhulumu nafsi zao wakaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu, na Mtume pia akawaombea msamaha, bila shaka wangelinikuta Mwenyezi Mungu ni mwenye kupokea toba tena mwenye kurehemu. (Qur'an, 4:64).

Lau aya hii ingekuwa ndiyo pekee katika mada hii, basi tungelisema kuwa inahusika tu katika zama za uhai wa Mtume **[s.a.w.w]** na ni kwa kipindi kile tu cha yeye kuwepo miongoni mwa watu. Lakini sisi

tunachukua hukmu ya jumla inayoenea, ambayo haimuwekei Mtume mpaka wa mwisho kwa maisha yake ya dunia. Hukmu hiyo iko katika maelezo yafuatayo:

**Kwanza**: Qur'an inabainisha kuwa, Manabii, Mawalii na baadhi ya watu wengine wako hai katika Bar-zakh (uhai baada ya kufa) na inawazingatia kuwa wanaona na wanasikia katika huo ulimwengu wa Barzakh.

Tutazionyesha hizo aya zinazobainisha jambo hili katika sehemu ya kuzungumzia kutawasal kwa roho tukufu.

**Pili**: Hadithi tukufu zinabainisha kwamba, Malaika humfikishia Mtume **[s.a.w.w]** salamu za yeyote anayemsalimia. Imekuja hadithi katika Sihah: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: "**Hapana yeyote atakayenisalimia, isipokuwa Mwenyezi Mungu hunirudishia roho yangu mpaka nami nimrudishie salamu**".[1] Na amesema Mtume **[s.a.w.w]**: "**Niswaliyeni, kwani swala zenu zinanifikia (kutoka) popote mlipo**."[2]

**Tatu**: Waislamu wamefahamu tangu siku hizo kwamba maana ya aya tuliyotangulia kuitaja inaendelea kutumika na wala haikomi kwa kufariki Mtume **[s.a.w.w]**, kiasi kwamba kuna baadhi ya mabedui (kwa mujibu wa fikra zao nzuri) walikuwa wakilikusudia kaburi Ia Mtume na wanalizuru na wanaisoma aya hii kaburini kwa Mtume na kumuomba awatakie msamaha.

Ametaja Taqiyyud-din As-Subaki katika kitabu kiitwacho "Shifaus-siqami" na pia As-Samhudi katika kitabu kiitwacho "Wafa-ul Wafa" mifano mbali mbali ya Waislamu kuzuru kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** na kusoma kwao aya hii mbele ya kaburi lake tukufu. Tunataja baadhi ya mifano kama ifuatavyo: Amepokea Sufyan bin Anbar kutoka kwa Al-Utbi, na wawili hawa ni Masheikh wa Imamu Shafii na ni wallimu wake, kwamba yeye amesema, "Nilikuwa nimekaa kwenye kaburi la mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]**, mara akaja bedui mmoja akasema: "As-Salaamu Alaika ya Rasulallah, nimemsikia Mwenyezi Mungu akisema: "Na lau wangelikuja kwako walipojidhulumu nafsi zao wakaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu na Mtume pia akawaombea msamaha, bila shaka wangelimkuta Mwenyezi Mungu ni mwenye kupokea toba tena mwenye kurehemu". Nami nimekujia mwenye kutaka msamaha kutokana na dhambi zangu mwenye kutaka Shafaa kwako (uniombee) kwa Mola wangu". Kisha bedui yule akalia, na akawa anasema:

"Ewe mbora wa waliozikwa ardhini, kwa uzuri wako ardhi na mimea (iliyopo hapa) vimependeza, nafsi yangu iwe fidia ya kaburi ulilomo, ndani yake kuna utakatifa na kuna kila ukarimu na ubora". Kisha bedui yule akaomba msamaha na akaenda zake.[3] Naye Abu Said As-Sam-ani anapokea kutoka kwa Imam Ali bin Abi Talib [a.s] kwamba, bedui mmoja alikuja Madina baada ya siku tatu tangu Mtume **[s.a.w.w]** azikwe, akajitupa kwenye kaburi tukufu la Mtume akajipaka udongo wa kaburi kichwani mwake na akasema: "Ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ulisema nasi

1. Sunan Abi Dawuud, juz. 1, Kitabul-Haj Babu Ziyaratil-Qubur, uk. 470-471.
2. At-Tajul-Jamiu Lil-Usuli Fiahadithir-Rasuli, kilichoandikwa na Sheikh Mansur Ali Nasif, juz. 2, uk. 189.
3.(1) Wafa-ul Wafa, juz. 4, uk. 1361. (2) Ad-durarus-Saniyyah cha Ahmad Dah-lan uk. 21.

tukaisikia kauli yako, umepokea kwa Mwenyezi Mungu mambo ambayo tumeyapokea kwako na katika aliyokuteremshia Mwenyezi Mungu ni "Na lau wangelikuja kwako walipojidhulumu nafsi zao.... nami nimedhulumu nafsi yangu na nimekuja ili unitakie msamaha kwa Mola wangu"[1] Yote haya yanajulisha cheo kikubwa alichokitoa Mwenyezi Mungu kwa Mtume **[s.a.w.w]** kama ilivyobainisha aya hii kwamba cheo hicho siyo makhsusi katika uhai wake tu, bali inatia mkazo kuwa kinathibiti hata baada ya kufa vile vile.

Kwa ujumla Waislamu wanazizingatia aya zote zilizoshuka kwa ajili ya kumtukuza Mtume **[s.a.w.w]** kwamba, zinakusanya kipindi cha uhai wake na baada ya kufa, na hapana yeyote anayezihusisha katika wakati wa uhai wake tu. Na katika historia imekuja kwamba: Alipouawa Imam Hasan bin Ali [a.s] na mwili wake Mtukufu ukaletwa ndani ya msikiti wa Mtume **[s.a.w.w]**, Banu Ummayya walidhani kwamba Banu Hashim wanataka kumzika karibu na kaburi la Babu yake, wakaeneza fitna na makelele ili asizikwe karibu na Babu yake. Imam Husein [a.s] akasoma kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo: "Enyi mulioamini, musipaze sauti zenu kuliko sauti ya Mtume. Qur'an, 49:2.

Hakuna mtu yeyote aliyempinga Imam Husein [a.s] eti kuwa aya hii inahusu zama za uhai wa Mtume **[s.a.w.w]**, hata hao Banu Ummayya hawakuthubutu. Na leo hii utawaona Mawahabi wameiandika aya hii na kuiweka kwenye ukuta unaokabiliana na kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** hali ya kuwa wanakusudia kuzuwiya watu wasipaze sauti zao mahala hapo. Na kwa mtiririko huu tunaweza kutoa maana pana zaidi ya aya hii, nayo ni kwamba, ni juu ya Waislamu wa leo kusimama mbele ya kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** na wamuombe Mtume awatakie msamaha kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo kumzuru Mtume **[s.a.w.w]** hakuna maana isipokuwa kufanya yale ambayo yamo katika aya hii na zinginezo. Aya hii inajulisha maudhui mbili nazo ni:

1. Mtu anawajibika kusimama kwenye kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** baada ya kufa kwake na kumuomba Mtume amtakie msamaha kwa Mwenyezi Mungu.

Tutafafauna maudhui haya wakati wa uchambuzi kuhusu kutawassal kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu, Insha-Allahau Taala.

2. Aya hii inashuhudia kuweko ruhusa ya kuzuru kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** kwani ukweli wa ziyara huwa hauna maana isipokuwa mwenye kuzuru afike pale alipo anayemzuru. Basi ikiwa kusimama mbele ya kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** na kumuomba atutakie msamaha kwa Mwenyezi Mungu ni jambo linalojuzu, bila shaka yatathibiti mambo mawili:

1. Tutakuwa tumemuomba atuombee msamaha kwa Mwenyezi Mungu.
2. Tumefika mbele yake na tumemsemesha.

Na maana ya ziyara hakuna isipokuwa mambo haya mawili.

## DALILI NYINGINE

Ij-mai ya Waislamu juu ya hukmu fulani miongoni mwa hukmu za kisheria katika zama mbali mbali, huwa inazingatiwa kuwa ni dalili iliyo

---

1. Al-Jauharul-munadham cha Ibn Hajar; Na ameitaja As-Samhudi katika Wafa-ul Wafa, juz. 2, uk. 612, na katika Ad-durarus-saniyya cha Dah-lan, uk. 21.

wazi kabisa ya kusihi kwa hukmu hiyo na kuthibiti kwake. Na ziyara kwenye kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** ni miongoni mwa mambo haya na unadhihiri ukweli wa mambo iwapo tutarejea vitabu vya hadithi, Fiqhi, Akhlaq na Historia na hasa sehemu zinazohusu ibada ya Hija katika vitabu hivyo. Ameutaja ubora wa kuzuru kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** Al-Marhum Al-Allama AI-Amini kutoka katika rejea arobaini na mbili zikiwa ni miongoni mwa rejea muhimu za elimu za Kiislamu. Ndani ya kitabu chake kiitwacho Al-Ghadir kwenye juzuu ya tano ukurasa wa 106 mpaka ukurasa wa 129, amezitaja nassi na ibara zinazohusu maudhi hii kwa undani sana. Miongoni mwa vitabu ambavyo tumevitegemea kutolea ushahidi kuhusu mada hii ni kama ifuatavyo:

1. Shifaus-siqami fi Ziyarati Khairil-Anami, kilichoandikwa na Taqiyyud-din As-Subaki as-Shafii, aliyefariki mwaka 706 A.H. Ndani ya Kitabu chake hiki ametaja mkusanyiko wa maneno ya wanachuoni walioboresha ziyara ya kuzuru makaburi na kuisisitiza sana.

2. Wafa-ul Wafa, kilichoandikwa na As-Samhudi aliyefariki mwaka 911 A.H., naye ametaja katika kitabu chake maneno ya wanachuoni katika kuboresha na kupendekeza ziyara.

3. Al-Fiqhu Alal-madhahibil-ar-baa, kilichotungwa na wanachuoni wanne wa Madhehebu manne, na wamekusanya ndani ya kitabu hicho Fatwa za Maimamu wa Madhehebu manne mashuhuri kwa Masunni. Wanachuoni hawa wanasema: "Kulizuru kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** ni sunna iliyo bora kuliko Sunna zote kwani hadithi nyingi zimekuja juu ya jambo hili".[1] Sasa umefika wakati wa kutaja baadhi ya hadithi zilizopokelewa na wanahadithi kuhusu kuzuru kaburi Ia Mtume **[s.a.w.w]**

## HADITHI TUKUFU JUU YA KUZURU KABURI LA MTUME [s.a.w.w]

Hadithi tukufu ambazo wanachuoni wa hadithi wamezipokea kuhusu kumzuru Mtume **[s.a.w.w]** ni nyingi mno kiasi kufikia daraja ya Mutawatir, kwa hiyo hatuoni sababu ya kuzihakiki katika Sanadi zake wala wapokezi wake. Mahafidh kutoka Madh-hebu zote za Kiislamu wameziandika katika vitabu vyao na Sihahi zao, na hadithi zote kwa ujumla zinajulisha kwamba, kulizuru kaburi la Mtume ilikuwa ni sunna iliyothibiti kwa wanachuoni hao wa hadithi. Na lau tungetaka kuzitaja zote ingechukuwa nafasi kubwa, kwa hiyo tunatosheka kutaja baadhi yake kama ifuatavyo:

1. Imepokewa toka kwa Abdallah bin Omar kwamba: Mtume **[s.a.w.w]** amesema: "**Ye yote mwenye kuzuru kaburi langu, yamemuwajibikia maombezi yangu**". Hadithi hii imekuja katika kitabu cha Al-fiqhi Alal-madhahibil-ar-baa, Juz. 1 uk. 590.

Wanachuoni wa madhehebu manne wametoa fatwa kwa mujibu wa hadithi hii. Ili kufahamu rejea zilizotumika, rejea kitabu kiitwacho Wafa-ul Wafa, Juz. 4 uk. 1336. Katika mambo yasiyo na shaka ni kwamba, hadithi wanayoipokea mahafidh na maulamaa tangu nusu ya karne ya pili Hijiriya mpaka leo haiwezekani kuwa ni uzushi na eti haina msingi. Sheikh Taqiyyud-din As-Subaki, ameandika uchunguzi wa hadithi hii na Sanadi zake na wapokezi wake katika kitabu chake Shifaus-siqami na

1. Al-Fiqhu Alal-madhahibil-ar-baa, juz. 1, uk. 590.

akathibitisha kuwa ni hadithi sahihi. (Na kitabu hiki ni kitabu bora mno kilichoandikwa na masunni dhidi ya Ibn Taymiyyah kuhusu kuharamisha kwake Safari ya kwenda kuzuru kaburi la Mtume **[s.a.w.w]**.

2. Amesema Mtume **[s.a.w.w]**: "**Ye yote atakayenijia kwa lengo la kunizuru na ikawa hakuna kingine kilichomfikisha kwangu ila kunizuru mimi tu, basi nitakuwa na wajibu wa kuwa muombezi wake siku ya Qiyama**". Hadithi hii imetajwa na mahafidh na wanachuoni wahadithi kumi na sita ndani ya vitabu vyao. Naye Taqiyyud-din As-Subaki ameizungumzia hadithi hii katika kitabu chake tulichokwisha kitaja juu ya sanadi zake na wapokezi wake, na vile vile As-Samhudi ameitaja katika kitabu chake Wafa-ul Wafa Juz. 4, uk. 1340.
3. Amesema Mtume **[s.a.w.w]** "**Mwenye kuhiji nyumba tukufu (Al-Kaaba) na asinizuru, basi mtu huyo amenidhulumu**". Hadithi hii wameipokea Masheikh na Mahafidh wa hadithi tisa, na As-Samhudi amewataja kwa ufafanuzi katika kitabu chake Juz. 4, uk. 1342.
4. Mtume **[s.a.w.w]** amesema "**Mwenye kuhiji kisha akalizuru kaburi langu baada ya kufa kwangu, atakuwa kama amenizuru katika zama za uhai wangu**". Wameipokea hadithi hii watu kumi na tano miongoni mwa wanahadithi na mahafidhi mashuhuri. Sheikh Taqiyyud-din As-Subaki katika kitabu chake amezungumzia Sanadi za hadithi hii, kama ambavyo As-Samhudi ameitaja katika kitabu chake Juz. 4, uk. 1340.
5. Mtume **[s.a.w.w]** amesema: "Mwenye kuzuru kaburi langu au mwenye kunizuru, nitakuwa muombezi wake". Hadithi hii imepokewa na wana hadithi na mahafidhi kumi na watatu, As-Samhudi amewataja ndani ya kitabu chake Juz. 4, uk. 1347. 6. Amesema Mtume **[s.a.w.w]**: "**Mwenye kunizuru baada ya kufa kwangu ni kama amemzuru wakati wa uhai wangu**". Hii ilikuwa ni mifano ya hadithi nyingi ambazo zimepokelewa kutoka kwa Mtume **[s.a.w.w]** zinazowataka watu na kuwahimiza kulizuru kaburi tukufu la Mtume **(s.a.w.w)**. Mar-hum Sheikh Al-Amini katika kitabu chake kiitwacho "Al-Ghadir" amekusanya hadithi ishirini na mbili juu ya maudhui hii. As-Samhudi katika kitabu chake, yeye ametaja hadithi kumi na saba na amezungumzia sanadi zake na wapokezi wake kiasi kwamba hakuna Ia kuongeza.[1] Ikiwa Mtume **[s.a.w.w]** amewataka watu walizuru kaburi lake tukufu, basi bila shaka ni kutokana na matokeo na athari na faida za kimaada na kimaana zinazoambatana na kumzuru yeye na kuwazuru watu wengine mashuhuri wa kidini. Kwa hakika, kutokana na kuzuru kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** Waislamu hupata fursa ya kukifahamu kituo cha Uislamu na pia kuyafahamu matukio yaliyopata kutokea na yanayotokea kwa kipindi hicho na kutoka huko huwa wanajipatia elimu na maarifa ya Kiislamu ambayo huyachukua na kuyasambaza kila pembe ya dunia.

## DALILI ZA MAWAHABI KATIKA KUHARAMISHA SAFARI ZA KUZURU MAKABURI

1. Wafa-ul Wafa, juz. 4, uk. 1336.

Kinachojitokeza kwa Mawahabi ni kwamba, asili ya kufanya ziyara wanaruhusu, lakini wanaharamisha kufanya safari kwa nia ya ziyara. Muhammad Abdul-Wahabi anasema katika risala yake ya pili miongoni mwa risala za "Hadiyatus-saniyyah" kama ifuatavyo: "Inasuniwa kumzuru Mtume **[s.a.w.w]**, isipokuwa haiwezi kufungwa safari ila kwa (nia ya) kuzuru msikiti na kuswali ndani yake". Na dalili wanayoshikilia katika kuharamisha ziyara ni ile hadithi iliyotajwa katika Sihahi zao kutoka kwa Abu Huraira!! Kwamba Mtume **[s.a.w.w]** amesema, "Haifungwi safari isipokuwa kwa Misikiti mitatu: Msikiti wangu huu na Masjidil-haram (Makka) na Masjidil-Aqsaa (Baitul-Muqadas). Na imepokewa tena hadithi hii kwa namna nyingine kama ifuatavyo: "Hakika hufanywa safari kwenda kwenye Misikiti mitatu: Msikiti wa Al-Kaaba, na msikiti wangu na msikiti wa Il-Yaa. Vile vile imepokewa kwa namna ya tatu nayo ni hii: "Hufungwa safari kwenda kwenye Misikiti mitatu..."

Hadithi zote hizi tatu amezileta Muslim ndani ya Sahih yake.[1] Hapana shaka yoyote kwamba hadithi hii imo katika Sihahi lakini sasa hivi sisi hatuko katika uwanja wa kuijadili hadithi hii, hasa kwa kuwa katika sanadi hii yako Bwana Abu Huraira (ambaye hali yake inaeleweka kwa wanachuoni) bali makusudio yetu ni kutazama hadithi hii inamaanisha nini. Basi hebu na tukadirie kwamba Nassi ya hadithi hii iko kama ifuatavyo: "Haifungwi safari ila ya kwenda kwenye Misikiti mitatu...." Ukweli unaothibiti ni kwamba harfu ya "Il-la" ni "Adatustith-Nai" kwa hiyo hapana budi awepo "Mustathna minhu" na ni wajibu afahamike. Na kwa kuwa hapa katika Nassi hayupo, basi hapana budi kumkadiria kuwa yupo katika maneno haya.

Na kabla ya kuonyesha dalili zinazopatikana inawezekana kumkadiria Mustath-na Min-hu kwa namna mbili:

1. Haifungwi safari kwenda kwenye Msikiti miongoni mwa Misikiti isipokuwa Misikiti Mitatu...

2. Haifungwi safari kwenda sehemu miongoni mwa sehemu yoyote isipokuwa kwenye misikiti mitatu... Kuifahamu hadithi hii na kuichunguza maana yake kutategemea moja ya makadirio haya mawili. Basi iwapo tutachagua makadirio ya kwanza, maana ya hadithi itakuwa kutokufungwa safari kwenda msikiti wowote isipokuwa misikiti ile mitatu, wala haitakusudia kutoruhusu kufungwa safari kwenda sehemu yoyote hata kama sehemu hiyo siyo msikiti. Kwa hiyo katazo lililopo hapa halimhusu yule anayefunga safari kwa ajili ya kuwazuru Manabii, Maimamu Watukufu na wachamungu, kwani mahala panapofanyiwa uchambuzi ni ufungwaji wa safari za kuzuru misikiti kwa kuwa misikiti iliyovuliwa ni mitatu. Ama anayefunga safari kuyazuru maziyara matukufu hatahusika na katazo hili wala haingii katika maudhui hii. Maelezo haya ni kwa mujibu wa makadirio ya kwanza.

Tukija kwenye makadirio ya pili ni lazima zihusike safari za aina zote za kidini isipokuwa safari za kwenda sehemu hizo tatu zilizotajwa, sawa sawa

---

1. (1) Sahihi Muslim Kitabul-hajj Babu latu Shaddu Rihal, Juz. 4 uk. 126 (2) Abu Dawuud katika Sunan yake, juz. 1, uk. 469, Kifabul-hajji. 3) Sunan An-nasai, juz. 2, uk. 37-38, kilichochapishwa pamoja na Sharh As-Suyuti.

kama safari hizo zitakuwa ni kwa ajili ya kuzuru msikiti au kuzuru sehemu nyinginezo. Lakini qarina na dalili zinaelekeza kwamba makadirio ya mwanzo ndiyo sahihi kama tutakubali kwamba sanadi ya hadithi hii ni sahihi. Ama qarina zinazoonyesha kusihi kwa makadirio ya kwanza ni kama ifuatavyo: Kwanza: Misikiti iliyovuliwa ni mitatu na hiyo Istith-nai ni Muttasil kama inavyoonekana wazi, basi hapana budi mustathnaminhu awe ni misikiti na wala siyo mahala. Kama mtu atasema: "Majaa Il-la Zaidun" yaani "hakuja isipokuwa Zaidi" basi "Mustath-na Min-hu" katika sentensi hii atakuwa ni mtu au watu na wala haliwezi kuwa ni tamko la ujumla kwa mfano kitu. Pili: Lau kama lengo lingekuwa ni kuzuwiya safari zote basi Istith-nai ya misikiti mitatu tu haitosihi kwani mtu hukusudia safari katika msimu wa hija na akafanya safari kwenda "Arafa" na "Mash-ari na Mina".

Kwa hiyo kama safari za dini zisizokuwa za misikiti mitatu zingekuwa haramu, basi ni kwa nini zinafanywa katika sehemu hizi tulizozitaja? Tatu: Qur'an Tukufu na hadithi tukufu vinaashiria kuwepo kwa safari zingine za kidini na kumekuja msukumo wa kuhimiza na kusisitiza kuhusu safari hizo, kama vile safari kwa ajili ya kupigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, kutafuta elimu na kuunganisha udugu, kuwazuru wazazi na mfano wa hayo. Na miongoni mwa hayo yapo ambayo Mwenyezi Mungu ameyazungumzia aliposema:

وَمَا كَانَ الْمُؤْمِنُونَ لِيَنفِرُوا كَافَّةً فَلَوْلَا نَفَرَ مِن كُلِّ فِرْقَةٍ مِّنْهُمْ طَائِفَةٌ لِّيَتَفَقَّهُوا فِي الدِّينِ
وَلِيُنذِرُوا قَوْمَهُمْ إِذَا رَجَعُوا إِلَيْهِمْ لَعَلَّهُمْ يَحْذَرُونَ ﴿١٢٢﴾

"Kwa nini halitoki kundi katika kila Taifa miongoni mwao liende likajifundishe vyema dini na kisha wakaja kuowaonya wenzao (waliosalia) ili wapate kujihadharisha". Qur'an, 9:122.

Na kwa sababu ya aya hii wafasiri wakubwa na wahakiki wa hadithi wameifasiri hadithi hii kama tulivyoonyesha sisi.

Kwa mfano: Ghazali anasema katika kitabu chake Ih-yaau Ulumid-din: Sehemu ya Pili: Nayo ni kuwa, asafiri kwa ajili ya ibada ima ya Hija au Jihadi ..... na inaingia katika jumla ya hayo, kuzuru makaburi ya Manabii [a.s], na kuzuru makaburi ya Masahaba na Tabiina na wanachuoni na Mawalii na kila ambaye (watu) hutabaruku kwake zama za uhai wake, basi watatabaruku kwa kumzuru baada ya kufa kwake." "Na inajuzu kufunga safari kwa lengo hili na wala halizuwiliki hili kutokana na kauli ya Mtume **[s.a.w.w]** aliposema: "Haifungwi safari isipokuwa kwenda kwenye misikiti mitatu, musikiti wangu huu na masjidil-haram na masjidil-Aqsa: Kwa sababu hadithi hii inahusu misikiti tu kwani misikiti yote ni sawa sawa katika ubora isipokuwa misikiti mitatu na hakuna tofauti baina ya kuzuru makaburi ya Mitume, Mawalii na wanachuoni katika asili ya ubora japo katika daraja kuna tofauti kubwa kutegemea vyeo vyao mbele ya Mwenyezi Mungu.[1] Kwa hiyo kilichokatazwa katika hadithi ni kufungwa safari kwenda kwenye Misikiti yoyote isiyokuwa hiyo mitatu, na haihusiki safari ya kuzuru au kwa malengo mengine ya dini.

---

1. (1) Ih-yau Ulumid-din cha Ghazali Kitabu adabu safari chapa ya daru maarifa Beirut, juz. 2, uk. 247. (2) Al fatawal-Kubra, juz. 2, uk. 24.

Na kwa kumalizia, hapana budi tuonyeshe kwamba Mtume **[s.a.w.w]** wakati aliposema "Haifungwi safari isipokuwa kwenda kwenye Misikiti mitatu", alikuwa hana maana kwamba kufunga safari kwenda kwenye Misikiti mingine ni haramu, bali maana yake ilikuwani kwamba haistahiki mtu kufunga safari na kupambana na mashaka ya safari kwa ajili ya kuzuru Misikiti hiyo kwani Misikiti hiyo haitofautiani katika ubora kwa tofauti kubwa, sawa sawa kama Msikiti uko mjini an kijijini au schemu fulani hapana tofauti kubwa, na kwa ajili hiyo hapana kinachomlazimisha mtu kuifungia safari Misikiti hiyo. Ama akifunga safari kwa ajili ya Misikiti yoyote basi tendo la mtu huyo haliwi ni haramu wala lenye kwenda kinyume cha sunna tukufu, hilo linajulishwa na kile walichokipokea As-habus-sihah Wassunan: "Mtume **[s.a.w.w]** alikuwa akienda kwenye msikiti wa Qubaa hali akiwa kwenye kipando au kwa miguu, basi (akifika) huswali rakaa mbili msikitini.[1] Sisi tunawajibika kujiuliza ni vipi itawezekana kuwa haramu kufunga safari na kukata masafa marefu kwa ajili ya kusimamisha sala katika moja ya nyumba miongoni mwa nyumba za Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu? Ikiwa kuswali msikitini ni Mustahabu basi kilichodhahiri ni kuwa kitangulizi cha Mustahabu ni Mustahabu vile vile.

---

1. (1) Sahih Muslim, juz. 4, uk. 127 (2)Sahih Bukhari, juz. 2, uk. 76 (3) As-Sunan cha Nasai kilichochapishwa pamoja na Shar-h Suyuti, juz. 2, uk. 37.

8

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## KUSWALI NA KUOMBA DUA KWENYE MAKABURI YA MAWALII

Miongoni mwa mambo ambayo Mawahabi wanayapigia kelele katika vitabu vyao na sehemu nyingine ni kuswali na kuomba dua kwenye makaburi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu, pia kuwasha taa katika sehemu hizo. Muanzilishi wa Uwahabi anasema katika moja ya risala zake iitwayo "Ziyaratul-Qubur" kama ifuatavyo: "Hakuna Imamu yeyote miongoni mwa Maimamu waliyotangulia aliyetaja kwamba, kuswali makaburini na kwenye maziyara ni jambo la Sunna, na wala kuswali na kuomba katika sehemu hizo kuwa ni bora, bali Maimamu wote wameafikiana kuwa, kuswali misikitini na majumbani ndiyo bora kuliko kuswali kwenye makaburi ya Mawalii na Wachamungu".[1] Na vile vile yamekuja maelezo yanayonasibishwa kuwa ni jawabu lililotolewa na wanachuoni wa Madina kama ifuatavyo: "Ama kukielekea chumba alichozikwa Mtume wakati wa kuomba dua, kilicho bora ni kulizuwia tendo hili, kama inavyoeleweka katika vitabu vya Madhehebu vinavyotegemewa, kwani upande uliyo bora kuelekewa ni upande wa Qibla". Jambo hili limevuka mpaka, kutoka kwenye kiwango cha wao Mawahabi kulizuwiya, mpaka kwenye kiwango cha kuwa ni shirki, kiasi kwamba leo hii wanalizingatia kuwa ni shirki na kila alitendaye kuwa ni mushriki. Bila shaka ni kwamba, kuswali kwa ajili ya huyo mwenye kaburi na kumuabudia au kumfanya yeye ndiyo Qibla katika swala itakuwa ni shiriki moja kwa moja.

Lakini ifahamike kwamba, hapa duniani hakuna Muislamu anayefanya namna hii kwenye makaburi ya Mitume na Mawalii, na hakuna anayemuabudia aliyezikwa hapo au kumuelekea katika sala. Kwa hiyo basi fikra hii ya kuwepo shirki ni uzushi na ni tuhuma zinazopandikizwa na Mawahabi. Hakika lengo la Waislamu kuswali na kuomba dua kwenye makaburi ya Mawalii ni kutaka kupata baraka za sehemu hizo ambazo zimehifadhi vipenzi miongoni mwa vipenzi ya Mwenyezi Mungu. Waislamu wanaitakidi kuwa mahali hapo pana daraja kubwa kwa sababu pameuhifadhi mwili wa mtu mtakatifu miongoni mwa watu watakatifu wa Mwenyezi Mungu. Hivyo basi, kuswali na kuomba dua sehemu hiyo kunampa thawabu nyingi mwenye kutenda hayo. Kuna swali ambalo niwajibu lijibiwe nalo ni hili: Je, kuwazika Mawalii wa Mwenyezi Mungu katika sehemu fulani huwa kunaifanya sehemu hiyo ipate aina fulani ya heshima au hapana? Iwapo itathibiti kuwa "ndiyo" kwa mujibu wa dalili za Qur'an na hadithi, basi kuswali na kuomba dua kwenye makaburi ya viongozi wa Uislamu ni jambo mustahabu na linazo thawabu nyingi.

Hata kama pengine lisithibiti jambo hili (kama tulivyotangulia kusema) haiwezekani kuharamisha kuswali na kuomba dua mahali hapo bali patajaaliwa kuwa ni kama sehemu nyingine tu ambazo inafaa kuswali na kuomba dua japokuwa hapana aina yoyote ya ubora. Hebu tuyaelekeze

1. Ziyaratul-Qubur uk. 159-160.

mazungumzo yetu kwenye maudhui yenyewe ambayo ni Je, maziyara na kaburi ya Mawalii yanaoutukufu na heshima maalum? Na Je kuna ushahidi ndani ya Qur'an na hadithi kuhusu jambo hili. Jawabu liko kama ifaatavyo:

1. Kisa cha As-Habul-Kahfi ambacho tumetangulia kueleza kwamba, waumini na watu wa tauhidi walisema kuhusu namna ya kuyafanya mazishi ya hao As-Habul-Kahfi. "Tuwajangee msikiti juu yao"[1] Hapa utaona kuwa, lengo lililowafanya waumini hao kujenga msikiti mahali walipozikwa As-Habul-Kahfi si jingine bali ni kwa ajili wapate kutekeleza faradhi zao ndani ya msikiti huo.[2] Waumini hao walikuwa wakifikiri kuwa: Mahali hapa pamekuwa patukufu na panaheshimika kwa sababu panahifadhi miili ya watu miongoni mwa waja wa Mwenyezi Mungu waliowachamungu, kwa hiyo hapana budi kutabaruku napo kwa kupafanya kuwa ni msikiti kwa ajili ya swala na ibada za Mwenyezi Mungu ili kupata thawabu nyingi zaidi.

Qur'an inalitaja jambo hili lililofanywa na Waumini hao bila ya kuwakemea wala kuwakosoa bali imenyamaza kabisa. Na lau tendo lao hili lingekuwa liko kinyume cha sheria au ni miongoni mwa mambo ya upuuzi yasiyofaa, Qur'an isingewanyamazia, bali ingewakemea kama ilivyo kawaida ya Qur'an kutokunyamazia itikadi batili.

2. Qur'an tukufu inawaamuru mahujaji wa nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu waswali kwenye "Maqam Ibrahim [a.s] nalo ni jiwe ambalo Nabii Ibrahim [a.s] alisimama juu yake alipokuwa akijenga Al-Kaaba. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema "**Pafanye mahali alipokuwa akisimama Ibrahim pawe pa kusalia**". Qur 'an, 2:125.

Yeyote anayeisoma aya hii atafahamu wazi kabisa kwamba swala iliwajibika mahala hapo siyo kwa jingine bali ni kwa sababu ya Maqam Ibrahimu (jiwe aliposimama Nabii Ibrahim) na kwamba lilejiwe ndilo lilisababisha mahala hapo papate utukufu na heshima hiyo. Na utawaona Waislamu kwa mamilioni wanapafanya kuwa ni mahali pa kusalia na kuomba dua. Kama mambo yako namna hii kuhusu mahali tu aliposimama Nabii Ibrahimu, je haitapasa hali iwe ni kama hiyo kuhusu sehemu walizolala watu wa Mwenyezi Mungu na viongozi wa Uislamu? Je, haitakuwa swala inayoswaliwa katika makaburi yao ni bora kuliko swala inayoswaliwa sehemu nyinginezo? Ni kweli kwamba aya hii imeshuka kuhusu kusimama kwa Nabii Ibrahimu mahala pale, lakini je hivi haiwezekani tukatoa kutokana na aya hii hukmu inayoenea?

Khalifa Mansoor Al-Abbasi (Ad-Dawaaniqi) alimuuliza Imam Malik Bin Anas (Imam wa Madhehebu ya Malik) walipokuwa ndani ya Msikiti wa Mtume **[s.a.w.w]** akasema: "Ewe baba Abdillahi nielekee Qibla ndiyo niombe au nimuelekee Mtume wa Mwenyezi Mungu?" Malik akasema: "Kwa nini wampa kisogo Mtume hali ya kuwa yeye ni wasila wako na ndiye wasila wa baba yako Adam [a.s] siku ya Kiyama? Iliyopo muelekee na umuombe, Mwenyezi Mungu atakukubalia maombi yako."[3] Mazungumzo

---

1. Qur'an. 18:21.
2. Tafsiri Al-Kas-Shaaf anasema Az-Zamakhshari wakati akifasiri aya hizo: "Waislamu wanaswali katika Msikiti huo na kupata baraka za mahali hapo." Al-Nishapuri naye anasema hivi hivi: Waislamu wanaswali katika msikiti huo na kupata baraka za mahali hapo.
3. Wafa-ul Wafai, juz. 4, uk. 1376.

haya yanatufahamisha kwamba dua kwenye kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** ilikuwa haina mushkeli wowote, pia kwamba suali la Mansur kumuuliza Malik ilikuwa ni kutaka kupata nguvu ya kufanya maombi kwa kuelekea Qibla au kwenye kaburi la Mtume **[s.a.w.w]**, naye Imam Malik anatoa fatwa kwamba kuelekea kaburi Ia Mtume **[s.a.w.w]** katika dua ni kama kuelekea Qibla.

3. Lau tutayarejea maelezo ya safari ya Miiraji, ukweli ungelijitokeza wazi wazi kwa namna nyingi zaidi. Kuna maelezo yasemayo kwamba Mtume **[s.a.w.w]** katika safari hiyo alishuka "Madina" na kwenye "Mlima wa Sinai" na Baiti Allaham" na aliswali katika sehemu hizo.

Jibril alimwambia Mtume **[s.a.w.w]**: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu unazifahamu sehemu ulizoswali? Hakika umeswali katika "Taiibah". Na hapo ndipo utapohamia, na umeswali kwenye "Mlima Sinai" mahali ambapo Mwenyezi Mungu alimsemesha Mussa na pia umeswali katika Bait Allaham (Bait-lehem)" mahali alipozaliwa Issa [a.s]."[1] Hadithi hii inafahamisha kwamba, inapendekezwa kuswali katika sehemu ambazo zimeguswa na Manabii, na kwamba sehemu hizo zimepata heshima na utukufu kwa sababu ya Nabii huyo.

4. Bibi Hajir "Mama wa Ismail bin Ibrahim" alifikia daraja ya juu mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa sababu ya subira na kuvumilia taabu katika njia ya Mwenezi Mungu mambo ambayo yalisababisha Mwenyezi Mungu apafanye mahali alipokanyaga Mama huyu, kuwa ni mahali pa ibada na akawajibisha Mahujaji wa nyumba yake tukufu waende kama alivyokwenda Bibi Hajir baina va Milima miwili ya "Safaa na Marwaa", jambo ambalo Ibn Al-Qayyim ambaye ni mwanafunzi wa Ibn Taimiyya analikubali.[2] Sisi tunajiuliza, ikiwa uvumilivu wa Bibi Hajir kuyavumilia matatizo na taabu katika njia ya Mwenyezi Mungu kumesababisha kupapatia utukufu mahala zilipo kanyaga nyayo zake, na Mwenyezi Mungu akawajibisha kwa Waisiamu kuwa wamuabudu yeye Mwenyezi Mungu katika sehemu hiyo kwa kuenda baina ya Safaa na Marwaa, basi ni kwa nini kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** lisiwe ni lenye baraka na utukufu wakati Mtume **[s.a.w.w]** alivumilia aina nyingi za matatizo na misiba na kero kwa ajili ya kuitengeneza jamii na kuiongoza?

5. Iwapo kuswali makaburini ni haramu katika sheria ya Kiislamu, basi ni kwa nini Bibi Aisha aliishi umri wake wote huku akiswali katika nyumba yake ambayo ndani yake mna kaburi la Mtume **[s.a.w.w]**? Kama tutakubali kwamba hadithi ifuatayo ni sahihi yaani Mtume amesema: "Mwenyezi Mungu awalaani Mayahudi na Wakristo, wameyafanya makaburi ya Mitume wao kuwa ni Misikiti".[3] Basi maana yake ni kwamba wao walikuwa wakiwaabudu Mitume wao na wakisujudu juu ya makaburi ya Manabii hao au kuyafanya makaburi hayo kuwa ndiyo kibla yao.

Na mambo haya mawili ni kinyume cha sheria tukufu ya Kiislamu. Lakini Mawahabi huitumia hadithi hii kuharamisha kuswali kwenye makaburi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu. Basi lau dalili ya hadithi hii

---

1. Al-Khasaisul-Kubra cha As-Suyuti.
2. Kitabu-Jalail-Af-Haami. Fis-salat Was-Salaam Ala Khairil-Anam cha Ibnul-Qayyim, uk. 228.
3. Sunan An-Nasai, juz. 4, uk. 96. Chapa ya Beirut.

ingekuwa sahihi, ni kwa nini basi Bibi Aisha ambaye ni mpokezi wa hadithi hii alimaliza karibu muda wa miaka hamsini ya umri wake akiswali na kufanya ibada ndani ya chumba ambacho amezikwa Mtume **[s.a.w.w]**.

6. Lau kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** lisingekuwa na heshima na utukufu, ni kwa nini basi Abubakar na Omar walikazania wazikwe karibu na kaburi la Mtume **[s.a.w.w]**? Hivyo basi hadithi hii inauhusiano gani na mwenendo wa Waislamu unaoruhusu kuswali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kwa kuelekea Qibla lakini karibu ya kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** ili kupata ubora na thawabu nyingi?

7. Bibi Fatm az-Zah-Raa [a.s] alikuwa akizuru kaburi Ia Ammi yake Hamza kila siku ya ljumaa au kila wiki mara mbili, na alikuwa akilia na kuswali kwenye kaburi lake.

Al-Baihaqi anasema: Fatma [r.a] alikuwa akilizuru kaburi la Ammi yake Hamza kila ljumaa na kisha huswali hapo na kulia."[1] Bibi Fatma huyu ndiye yule ambaye zimepokelewa kwa Mtume hadithi sahihi zisemazo kwamba: "Radhi ya Fatma ndiyo radhi ya Mwenyezi Mungu na mjumbe wake, na ghadhabu ya Fatma ndiyo ghadhabu ya Mwenyezi Mungu na mjumbe wake."[2] Ewe msomaji mpendwa, dalili zote hizi ukiongeza na mwenendo wa Waislamu wa kuswali na kuomba dua katika sehemu walizozikwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu, na wapenzi wake vinatia nguvu kuwa, kuswali na kuomba dua kwenye makaburi haya kuna thawabu nyingi na ubora mkubwa, na kwamba lengo ni kupata baraka zilizopo katika sehemu hizo na ni kutekeleza faradhi mahala hapo kwa kutaraji kukubaliwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Lau tutakadiria kwamba hakuna dalili katika Qur'an na hadithi inayoonyesha ubora na heshima ya sehemu hizo na pia kwamba hakuna ubora wowote kuswali na kuomba dua mahala hapo, hata hivyo ni kwa nini iwe haramu kuswalia katika sehemu hizo? Na ni kwa nini basi sehemu hizi haziingii ndani ya kanuni ya Kiislamu yenye kuenea, ambayo inaizingatia ardhi yote kuwa ni mahali pa kufanyia ibada ya Mwenyezi Mungu kama alivyosema Mtume **[s.a.w.w]**: "Ardhi yote imefanywa kuwa ni msikiti na ni safi kwa ajili yangu."[3]

## KUWASHA TAA MAKABURINI

Kuwasha taa kwenye makaburi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu, jambo ambalo mawahabi wanadai kuwa ni haramu, halina umuhimu mkubwa kwa kuwa dalili pekee waitumiayo ni ile hadithi aliyoitaja An-Nasai kutoka kwa Ibn Abbas kwamba, "Mtume **[s.a.w.w]** amewalaani wanawake wanaozuru makaburi na wanaoyafanya kuwa ni misikiti na wale wanaayawasha taa".[4][108] Hadithi hii na nyinginezo mfano wa hii zinahusika tu kama kuwasha taa huko kutakuwa ni kupoteza na kufuja mali au kutasababisha kujifananisha kwa baadhi ya nyumati na mataifa na dini batili, kama alivyolionyesha jambo hilo Al-Allamah as-Sindi katika sherehe ya hadithi hii aliposema: "Na katazo hilo ni kwa kuwa (kuwasha taa) husababisha

1. (1). As-Sunan Lil-Baihaqi, juz. 4, uk. 78. (2). Mustadrak As-Sahihain Lil-Hakim, juz. 1, uk 377.
2. Sahihi Bukhari, juz. 5, Babu Manaqib Qarabat Rasulillahi uk. 21.
3. Sahih Bukhari, juz. 1, uk. 91, Musnad ibn Hanbal, juz. 2, uk. 222 na vinginevyo.
4. Sunan An-Nasai, juz. 3, uk. 77.

kupoteza mali bila manufaa".[1] Ama kama lengo litakuwa ni kuwasha taa kwa ajili ya kusoma Qur'an, kuomba, kunyenyekea kwa Mwenyezi Mungu, kuswali na mengineyo katika mambo mustahabbu na wajibu pamoja na manufaa yanayo kubalika kisheria, basi haya yote hayana matatizo kabisa, "Saidianeni katika mema na uchamungu". (Qur'an, 5:2). Basi vipi itakuwa haramu? Ilivyo ndivyo ni kwamba, kuwasha taa makaburini ni jambo mustahabbu kisheria na linapendeza kiakili.

## KUTAWAS-SAL KWA MAWALII WA MWENYEZI MUNGU

Mas-ala ya kutawasal Kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu na wapenzi wake ni mas-ala yanayofahamika miongoni mwa Waislamu ulimwenguni kote, na zimekuja hadithi nyingi kuruhusu jambo hili na kulipendekeza. Kwa hiyo kutawas-sal siyo jambo geni bali ni jambo Ia kidini lililofahamika miongoni mwa Waislamu tangu mwanzoni mwa kuja Uislamu mpaka leo hii, na wala humkuti Muislamu anayelipinga. Kwa muda wote wa karne kumi na nne tangu kuja Uislamu, hapana yeyote aliyelipinga jambo hili isipokuwa Ibn Taymiyyah na wanafunzi wake katika karne ya nane Hijiriya. Na baada ya karne mbili akaja Muhammad bin Abdil-Wahab, ambaye yeye wakati mwingine akaona kuwa kutawas-sal kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu ni Bid'a na wakati mwingine akaona kuwa eti ni kuwaabudu Mawalii hao. Hapana shaka yoyote kwamba kumuabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu ni shiriki na ni haramu. Sisi sasa hivi hapa hatufanyi uchunguzi juu ya neon Ibada na uhakika wake ingawa jambo hili ni muhimu sana, lakini tutalizungumzia kwa ufafanuzi katika mahali pake maalum, kwa kuwa sasa hivi tunashughulika na kutawas-sal kwa Mawalii. Hivyo basi tunasema: Fahamu (ewe msomaji) kwamba, kutawas-sal kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu kuna namna mbili:

1. Kutawas-sal kwa Mawalii wao wenyewe nafsi zao kama vile tukisema:

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nintawas-sal kwako kwa Mtume wako Muhammad **[s.a.w.w]** nikubalie haja yangu".

2. Kutawas-sal kwa cheo cha Mawalii na utukufu waliyonao mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kama vile tukisema: "Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninatawas-sal kwako kwa utukufu wa Muhammad na heshima yake na haki yake unikubalie haja yamgu." Kwa upande wa Mawahabi, wao wanaziharamisha namna zote mbili, wakati ambapo hadithi tukufu za Mtume **[s.a.w.w]** na sera ya Waislamu vinashuhudia kinyume cha madai ya Kiwahabi na pia vinatilia mkazo kuwa namna zote mbili zinafaa. Hivi sasa tunataja baadhi ya hadithi hizo moja baada ya nyingine, kisha tutaleta maelezo juu ya sera ya Waislamu, na hapo ndipo itakapoyeyuka na kupotea kauli ya mwenye kuharamisha tawas-sul na kuwa eti ni Bid'a.

## HADITHI TUKUFU ZA MTUME [s.a.w.w]

Hadithi zinazojulisha kuwa kutawa-sal kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu kunafaa ni nyingi mno, na zinapatikana katika vitabu vya Historia na hadithi. Katika maelezo yafuatayo tunataja sehemu yake tu:

---

1. As-Sunan An-Nasai. juz. 3, uk. 77, chapa ya Misri. Na juz. 4, uk. 95, chapa ya Beirut, Sharh Jamiu Saghir, juz. 2, uk. 198.

## HADITHI YA KWANZA

Imepokewa toka kwa Uthman bin Hunaif kwamba amesema: "Mtu mmoja kipofu alikuja kwa Mtume **[s.a.w.w]** akasema: "Niombee kwa Mwenyezi Mungu aniponye (upofu)". Mtume akamwambia, "Ukipenda nitaomba na ukipenda uvumilie na ndiyo bora". Yule mtu akamwambia Mtume: "Muombe Mwenyezi Mungu (aniponye"). Basi Mtume **[s.a.w.w]** akamuamuru kipofu yule atawadhe vizuri na aswali rakaa mbili na aombe kwa kutumia Dua hii. "**Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nakuomba na ninaelekea kwako kupitia kwa Mtume wako Mtume wa Rehma, Ewe Muhammad hakika mimi naelekea kwa Mola wangu kupitia kwako katika haja yangu ili ikubaliwe, ewe Mwenyezi Mungu mfanye Muhammad kuwa muombezi wangu**." Ibn Hunaif anasema:"Basi Wallahi, tulikuwa hatujatawanyika tukiendelea kuzungumza mpaka aliingia kwetu kama kwamba hakuwa na ugonjwa (upofu)".

## MAELEZO JUU YA SANAD YA HADITHI HII

Hakuna ubishi katika kusihi kwa Sanad ya hadithi hii, kwani hata huyo Imam wa Mawahabi "Ibn Taimiyyah" ameihesabu kuwa ni hadithi sahihi na akasema kuwa, makusudio ya "Abu Jaafar" jina linalopatikana katika Sanad ya Hadithi hi ni 'Abu Jaafar Al-Khatmi" na huyu Bwana ni mpokezi anayetegemewa. Imekuja katika Musnad ya Imam Ahmad (Abu Jaafar Al-Khatmi). Amma ndani ya Sunan Ibn Majah imekuja (Abu Jaafar) tu. Mwandishi wa Kiwahabi katika zama hizi aitwaye Ar-Rifai ambaye wakati wote anajaribu kuzifanya dhaifu hadithi zinazohusu Tawas-sul anasema kuhusu hadithi hii tuliyoitaja hapo kabla: "Hapana shaka kwamba hadithi hii ni sahihi na ni mashuhuri na imethibiti bila wasiwasi wala mashaka (kwamba) macho ya kipofu yule yalirudi (akawa anaona) kwa sababu ya Dua ya Mtume **[s.a.w.w]**."[1] Na anasema tena:

"Hadithi hii wameileta An-Nasai na Al-Baihaqi, At-Tabran na At-Tirmidhi na AI-Hakim wao wametaja "Allhumma Shaf-Fihu Fihi" badala ya "Allahumma Shaf-Fihu Fiy-ya."[2] Mufti wa Makka Zaini Dahlan anasema: "Bukhari na Ibn Majah na Al-Hakim (ndani ya Mustadrak yake) pamoja na Jalalud-Dinis-Suyuti (katika Jaami' yake) wameitaja hadithi hii na Sanad zake ni sahihi. Na sisi tunaitaja hadithi hii kutoka katika rejea zifuatazo:

1. Sunan Ibn Majah, Juzuu ya kwanza, uk. 441 ikiwa ni hadithi na 1385, kimehakikiwa na Muhammad Fuad Abdul-Baqii, toleo la Dar-Ihyail-Kutubil-Arabiyya. Naye Ibn Majah anaeleza kutoka kwa Abu Is-Haqa kwamba yeye amesema: "Hadithi hii ni sahihi." Kisha akasema:

"Na ameipokea Tirmidhi katika kitabu "Abuwa-bul-ad-iyya" akasema, Hadithi hii ni ya kweli na ni sahihi gharib.

2. Musnad Ahmad bin Hanbal, Juzuu ya nne uk. 138, "kutoka kwa Athuman bin Hunaif" chapa ya "Maktabul-islami, Muasasah dari-Saadir/Beirut, na ameipokea hadithi hii kwa njia tutu.

3. Mustad-ra kus-sahihain ya Al-Hakim An-Nishapuri, Juzuu ya kwanza, uk. 313, chapa ya Haidar-abad/India. Amesema baada ya kuitaja hadithi hi:

---

1. At-Tawas-sul Ilaa Haqiqatit-Tawas-sul, uk. 158.
2. At-Tawas-sul Ilaa Haqiqatit-Tawas-sul, uk. 158.

"Hadithi hii ni sahihi kwa sharti ya Bukhari na Muslim lakini hawakuiandika"

. 4. Al-Jamius-Saghiru cha As-Suyuti, uk. 59, kutoka kwa Tirmidhi na Al-Hakim.

5. Tal-khisul-Mustad-rak cha Adh-dhahabi-alivefariki mwaka 748 A.H., kilichochapishwa katika Hashiya ya AI-Mustad-rak.

6. At-Tajul-Jamii, Juzuu ya kwanza, uk. 286, nacho ni kitabu kilichokusanya hadithi zilizomo katika sihahi tano isipokuwa sahih ya Ibn Majah. Baada ya haya hakuna haja ya majadiliano kuhusu Sanad ya Hadithi hii au kuitia dosari.

Ama maelekezo yake na mafunzo yaliyomo, lau utamuonyesha hadithi hii mtu anayefahamu vyema lugha ya Kiarabu tena mwenye akili safi na akajiepusha na chuki za Kiwahabi na kuchanganya kwao mambo kuhusu tawa-suli kisha umuulize: "Ni kitu gani Mtume **[s.a.w.w]** alimuamuru kipofu yule akifanye wakati akiomba dua ile"?

Kwa haraka tu jibu lake litakuwa: "Mtume **[s.a.w.w]** alimfundisha namna atakayo tawas-sal kwa Mwenyezi Mungu kupitia kwa Mtume wake Mtume wa Rehma na namna Mwenyezi Mungu atakavyokubali maombi yake". Maana hii ndiyo inayofahamika moja kwa moja kutokana na maneno yaliyomo katika hadithi iliyotajwa. Ndani ya maelezo yafuatayo tunaigawa hadithi hii katika mafungu ili kuongeza ufafanuzi.

### FUNGU LA KWANZA

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba na ninaelekea kwako kupitia kwa Mtume wako." Neno "Mtume wako"linauhusiano na maneno mawili yaliyokuja kabla ya neno hili. Maneno hayo ni: "Ninakuomba na ninaelekea kwako". Kwa maneno yaliyo wazi tutasema kama ifuatavyo: Kipofu yule anamuomba Mwenyezi Mungu kupitia kwa Mtume **[s.a.w.w]** kama ambavyo anaelekea kwa Mwenyezi Mungu kwa kupitia heshima na utukufu wa Mtume **[s.a.w.w]** na wasila wake.

Kinachokusudiwa kwa neno "Mtume" siyo dua yake bali ni ile dhati yake tukufu. Ama anayesema kwamba neno dua limekadiriwa kabla ya neno Mtume na maana ya (As-aluka Binabiyyika) ni ninakuomba kwa dua ya Mtume wako, basi kusema hivyo ni madai bila ya dalili na ni kinyume cha maana iliyo dhahiri. Na sababu ya madai hayo yaliyo kinyume na dalili ni kuwa, yeye haitakidi kutawasal kwa dhati ya Mtume **[s.a.w.w]** ndiyo maana akalazimika na akakadiria kusema kwamba neno dua hapa limekadiriwa ili tu kwa njia hii apate kuitakasa itikadi yake ya kupinga kutawasal kwa Mtume mwenyewe.

### FUNGU LA PILl

"Muhammad Nabii wa Rehma". Ili iweze kufahamika vyema kwamba makusudio katika Dua hiyo, ni kumuomba Mwenyezi Mungu kupitia kwa Mtume na dhati yake na heshima yake, basi imekuja jumla baada ya neno "Mtume wako" isemayo "Muhammad Nabii wa Rehma", ili ifafanue lengo wazi wazi.

### FUNGU LA TATU

Sentensi isemayo "Ewe Muhammad, hakika mimi naelekea kwa Mwenyezi Mungu kupitia kwako", inajulisha kwamba kipofu yule

alimfanya Mtume mwenyewe kuwa ndiyo wasila wa maombi yake, siyo dua ya Mtume **[s.a.w.w]** yaani yeye alitawassal kwa dhati ya Mtume siyo kwa dua ya Mtume.

### FUNGU LA NNE

Na aliposema: "Mfanye Muhammad awe muombezi wangu", alikuwa na maana ya kusema kuwa: "Ewe Mola mfanye Muhammad **[s.a.w.w]** awe ndiye muombezi wangu na ukubali uombezi wake kwangu, katika haki yangu." Ewe msomaji mpenzi bila shaka imekudhihirikia kwamba nukta muhimu katika dua yote ni dhati ya Mtume **[s.a.w.w]** na shakhsiyya yake tukufu, na katika dua hii hakuna utajo wa dua ya Mtume asilan. Na kila atayedai kuwa kipofu yule alitawassal kwa dua ya Mtume na wala hakutawassal kwa dhati ya Mtume wala shakhsiyya yake, huyu atakuwa amejifanya kutoyaelewa maneno ya hadithi hii yaliyo wazi na amejifanya kutoifahamu hadithi hii. Nawe msomaji lau utaifanyia mazingatio kauli ya muombaji aliposema: "Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nakuomba na ninaelekea kwako kupitia kwa Mtume wako, Mtume wa Rehma" na aliposema tena muombaji huyo: "Ewe Muhammad hakika mimi naelekea kwa Mola wangu kupitia kwako", itakudhihirikia wazi wazi kwamba, lengo linalokusudiwa ni nafsi ya Mtume awe ndiyo wasila kupitishia maombi ya muombaji.

Na lau lengo ingekuwa ni dua ya Mtume ndiyo wasila ingelazimika kusema: "Ewe Mwenyezi Mungu nakuomba kwa (kupitia) dua ya Mtume". Baada ya haya tuliyoyaeleza hivi punde hakuna mush-keli unaobakia miongoni mwa mish-keli aliyoitaja yule mwandishi wa Kiwahabi katika Kitabu kiitwacho "At-Tawas-Sul Ilaaz HaqiqatitTawas-sul". Mish-keli hiyo tumeitaja pamoja na majibu yake ndani ya kitabu chetu kiitwacho "At-Tawas-sul" kuanzia ukurasa wa 147 mpaka 153 na unaweza kurejea ukaona.

### HADITHI YA PILI KUTAWAS-SAL KWA HAKI YA WAOMBAJI

Amepokea Atiya Al-aufi kutoka kwa Abu Said Al-Khudri kwamba Mtume **[s.a.w.w]** amesema: "Yeyote atakayetoka nyumbani mwake kwenda kuswali akasema: Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nakuomba kwa haki ya wanaokuomba, na ninakuomba kwa haki ya mwendo wangu huu kwani mimi sikutoka kwa maringo na majivuno, wala kujionyesha wala kutaka sifa, nimetoka kwa kuogopa ghadhabu zako na kutafata radhi zako, basi ninakuomba unilinde kutokana na moto na unisamehe madhambi yangu, kwani hapana anayesamehe madhambi isipokuwa wewe.[1] (Atakayesema hivi) Mwenyezi Mungu atamuelekea mtu huyo kwa dhati yake na watamtakia msamaha malaika sabini elfu." Hadithi hii iko wazi mno katika maana yake na inajulisha kwamba mtu anayo ruhusa ya kutawas-sal kwa heshima ya Mawalii na daraja walizonazo na cheo chao mbele ya Mwenyezi Mungu. Basi na awafanye Mawalii hawa kuwa ndiyo wenye kukaa kati na kuwa waombezi, ili haja zake zikubaliwe na dua zake zipokelewe.

### HADITHI YA TATU KUTAWAS-SAL KWA HAKI YA MTUME MTUKUFU [s.a.w.w]

---

1. Sunan Ibn Majah, juz. 1, uk. 256. Hadith namba 778.

Nabii Adam **[a.a.w.w]** yalipomtokea mambo ambayo ilivyokuwa ni bora yasimtokee, naye akarejea kwa Mwenyezi Mungu kutokana na hayo yaliyomtokea, alipokea maneno kutoka kwa Mola wake kama Qur'an Tukufu inavyoonyesha:

﴿فَتَلَقَّىٰ آدَمُ مِن رَّبِّهِ كَلِمَاتٍ فَتَابَ عَلَيْهِ ۚ إِنَّهُ هُوَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿٣٧﴾

"Kisha Adam akapokea maneno kutoka kwa Mola wake, na Mola wake akakubali toba yake hakika yeye ni mwingi wa kupokea (toba) na ni mwingi wa huruma."[1] Qur'an, 2:37.

Wafasiri wa Qur'an na wataalam wa hadithi wamefafanua na kutoa rai zao na mtazamo wao kuhusu aya hii na maana yake, na wamefanya hivyo kutokana na kutegemea kwao baadhi ya hadithi ili kupata maana ya aya hii. Yafuatayo ni maelezo ambayo ndani yake tutataja hadithi hizo ili tuone matokeo ambayo tunaweza kuyapata baada ya kuzitaja hizo hadithi.

At-Tabrani katika Al-muujamus-Saghir na Al-Hakim katika Mustadrak yake, na Abunuaim Al-Isfahani katika Hil-yatulAuliyai, Baidhawi naye katika Dalailun-nubuwat, na Ibn Asakir Ad-Dimishqi katika Tarikh yake, As-Suyuti naye ndani ya Tafsirud-duril Manthur, Al-A'lusiy yeye katika Tafsiri Ruhul-maan wote hawa wametoa mapokezi kutoka kwa Umar bin Al-Khatab naye kutoka kwa Mtume **[s.a.w.w]** kwamba Mtume amesema: "Wakati Adam alipokosea lile alilolikosea, alinyanyua kichwa chake juu akasema, Nakuomba (Ewe Mwenyezi Mungu) kwa haki ya Muhammad unisamehe, Mwenyezi Mungu akampelekea wahi Adam (akamwambia) huyu Muhammad ni nani? Adam akasema:

Limetukuka Jina Lako (Ewe Mwenyezi Mungu), wakati nilipokuwa nimeumbwa nilinyanyua kichwa changu, kuiangalia arshi yako, basi niliona maandishi (yasemayo) hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na Muhammad ni mjumbe wa Allah nikasema, bila shaka hapana kiumbe Mtukufu mbele yako kuliko yule ambaye umeliweka jina lake pamoja na jina lako, Mwenyezi Mungu akampelekea Adam wahi (akamwambia) huyo ndiyo Nabii wa mwisho katika kizazi chako, na lau si yeye nisingekuumba wewe."[2] Akinakili toka kwa At-Tabrani na Abunuaim na AI-Bayhaqi na matni ya hadithi imenakiliwa kutoka kwa Ad-durul-Manthoor.

## MAONI YETU JUU YA HADITHI HII

Kinyume cha mazowea tuliyonayo kuwatambulisha watu hao au nafsi hizo. Qur'an inazungumzia nafsi au watu kwa kutumia neno "AL-KALIMAH" kinyume cha matumizi yetu ya kawaida kuhusti neno hili. Kwa mfano Mwenyezi Mungu anasema:

(a) "Mwenyezi Mungu anakupa bishara njema ya Yahya mwenye kumsadikisha neno atokaye kwa Mwenyezi Mungu. Qur'an, 3:39

(b) Kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo: "Ewe Mariam, Mwenyezi Mungu anakupa bishara njema ya neno atokaye kwake jina lake ni Masih Isa mwana wa Mariam". Qur'an, 3:45.

---

1. Maelezo: Imethibiti kwamba, lile katazo lililoko katika kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo: 'Msiukurubie mti huu" ni katazo la kutoa muongozo na

2.(1) Mustadrakus-Sahihain, juz. 2, uk. 615. (2) Ruhul-Maani, juz. 1, uk. 217. (3) Ad-durul-Manthoor, juz. 1, uk. 59.

(c) "Hakika Masih Isa mwana wa Mariam ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu na ni neno lake." Qur'an, 4:171

(d) Kauli ya Mwenyezi Mungu: "Waambie lau kama bahari ingekuwa ndiyo wino kwa (kuandikia) maneno ya Mola wangu, basi bahari ingekwisha." Qur'an, 18:109.

(e) Kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo: "Na bahari hii (ikafanywa wino) na bahari nyingine saba (zikaongezwa), maneno ya Mwenyezi Mungu yasingelikwisha." Qur'an, 31:27. Tukiziangalia aya hizi inawezekana kabisa kusema kwamba: Makusudio ya "Kalimaat" yaani katika ile aya isemayo "Akapokea Adam kutoka kwa Mola wake maneno" makusudio yake ni dhati tukufu yenye heshima ambayo kwayo Nabii Adam alitawas-sal kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Na katika hadithi iliyotangulia utaliona jina la Muhammad **[s.a.w.w]** tu ndiyo lililotajwa. Ama katika hadithi zilizoko katika madheheb ya haki (Shia) utaona hadithi hii imepokewa kwa sura inayokubaliana na aya tukufu ya Qur'an, pia utaikuta imepokewa kwa namna mbili. Wakati mwingine neno "Kalimaat" limefasiriwa kwa maana ya majina ya watukufu watano [a.s], na wakati mwingine limefasiriwa kwa sura zao zenye nuru. Hebu itazame hadithi ifuatayo: "Hakika Adam aliona kwenye arshi pameandikwa majina matukufu yenye heshima akauliza, majina hayo (ni ya kina nani)? Akaambiwa, haya ni majina ya viumbe watukufu mno kwa daraja mbele ya Mwenyezi Mungu, kuliko viumbe wote na majina hayo ni, Muhammad, Ali, Fatma, Hasan na Husein. Basi Adam [a.s] akatawas-sal kwa Mola wake kupitia kwao ili kukubaliwa toba yake na kunyanyuliwa daraja yake.[1] Na baadhi ya hadithi zinajulisha kwamba Adam [a.s] aliona Sura za nuru za watukufu watano, basi akatawas-sal kwazo baada ya kuziona. (Kwa ufafanuzi zaidi tazama Tafsir AI-Burhan, juz. 1, uk. 87, Hadith na 13, 15, na 16.)

2. Na tunaporejea vitabu vya historia na hadithi inatudhihirikia kwamba, Qadhiya ya Adam kutawas-sal kwa Mtume Muhammad **[s.a.w.w]** lilikuwa ni jambo mashuhuri miongoni mwa watu, ndiyo manna utamkuta Imam Malik bin Anas (Imam wa Madhehebu ya Malik) anasema kumwambia Mansur Ad-Dawaniq katika Msikiti wa Mtume **[s.a.w.w]** : "Mtume ni wasila wako na ni wasila wa Baba yako Adam". Nao washairi wa Kiislamu wameuonyesha ukweli huu katika mashairi yao. Mmoja wa washairi hao anasema: "Kwa Mtume **[s.a.w.w]** Mwenyezi Mungu alikubali maombi ya Adam na aliokolewa Nuhu ndani ya Safina."[2] Mwingine naye anasema: Ni watu ambao kwao lilisameheka kosa la Adam, nao ndiyo wasila na nyota zing'aazo.[3]

---

1. (1) Maj-maul-bayan Juz. 1 uk 89 Chapa ya Lebanon (2) Tafsirul-bur-han Juz. 1, uk 86-88 hadithi namba 2, 5, 11, 12, 14 na 27.
2. Kashful-irtiyab, uk. 307. Ameinakili kutoka katika Mawahib, na shairi hili ni la Ibn Jabir.
3. Kashful-irtiyab, uk. 308. Na Shairi hili ni la Al-wasiti.

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## HADITHI YA NNE MTUME KUTAWAS-SAL KWA HAKI YAKE NAHAKI YA MANABII WALIOMTANGULIA

"Alipofariki Bibi Fatma binti Asad, Mtume alinigia mahala alipofia Mama huyo, akakaa upande wa kichwa chake akasema: "Mwenyezi Mungu akurehemu ewe mama yangu baada ya mama yangu. Kisha Mtume akamwita Usama bin Zaid, na Abu Ayyubul-Ansari na Omar bin AI-Khatab na kijana fulani mweusi ili wakachimbe kaburi. Wakachimba kaburi hilo, na walipofikia kuchimba mwanandani, Mtume **[s.a.w.w]** akaichimba mwanandani hiyo yeye mwenyewe kwa mkono wake na kuutoa mchanga. Alipomaliza, akaingia kwenye mwanadani kisha akalala ndani yake na akasema:

"Mwenyezi Mungu ndiye anayehuisha na kufisha, na yeye yu hai wala hatokufa. Ewe Mwenyezi Mungu msamehe mama yangu Fatma binti Asad na uyapanue makazi yake kwa haki ya Mtume wako na Manabii ambao wamepita kabla yangu". Mtungaji wa kitabu kiitwacho "Khulasatul-kalam" amesema: Hadithi hii imepokewa na, Tabrani katika kitabu kiitwacho, Almuujamul-Kabir na Almuujamul-Ausat, na ameipokea Ibn Hiban na Al-Hakim na wamesema kuwa ni hadithi sahihi.[1] Naye Sayyid Ahmad Zaini Dah-lan ameandika katika kitabu kiitwacho "Ad-Durarus-Saniyya Fiir-radd Alal-Wahabiyya" kama ifuatavyo: "Amepokea Ibn Abi Shaiba kutoka kwa Jabir (kama tulivyoitaja hadithi hii, na vile vile ameipokea hivyo hivyo Abdul-Bari kutoka kwa lbn Abbas, na ameipokea Abu Nuaim katika kitabu "Hil-yatul-auliyai" kutoka kwa Anas, na yote haya ameyataja Alhafidh Jalalud-dinis-Suyuti katika kitabu "Al-jamiul-Kabir"[2] Ama sisi tumetaja hadithi hii kutoka kwenye rejea mbili, moja inaambatana na maudhui haya tunayozungumzia ambayo yanahusu dua, na ya pili haihusiani na maudhui haya. Rejea hizo ni:

(1) Hil-yatul-auliyai ya Abu Nuaim AI-Isfahani, juzuu ya tatu, uk. 121.

(2) Wafaul Wafa ya As-Samhudi, juzuu ya tatu, uk. 899.

### HADITHI YA TANO, KUTAWAS-SAL KWA MTUME MWENYEWE

Wanachuoni wengi wa hadithi wamepokea kwamba, bedui mmoja aliingia kwa Mtume **[s.a.w.w]** akasema: Kwa hakika tumekujia hali ya kuwa wanyama na wanaadamu wote hawana hata sauti kwa ajili ya njaa." Kisha akasema Ushairi huu: "Tumekujia (Ewe Mtume) hali ya kuwa maziwa ya mwanamke kijana yanatoka damu (badala ya maziwa, kwa sababu ya njaa) na kwa hakika mama mwenye mtoto naye hamjali mwanawe na hatuna cho chote kinacholiwa na watu isipokuwa hanzal (matunda machungu) na Il-hizi,[3]. Na wala hatuna pengine pa kukimbilia isipokuwa kwako. Basi watu

1. Kashful-irtijab, uk. 312 amenakili toka Khulasatul-kalaam.
2. Ad-durarus-Saniyya,uk. 8.
3. Il-hizi ni kitu ywalichokuwa wakikitumia katika miaka ya njaa na kilikuwa kikitengenezwa kutokana na mcanganyiko wa damu na manyoya ya ngamia

wakimbilie wapi? Hakuna, isipokuwa waende kwa Mtume". Basi Mtume **[s.a.w.w]** alisimama huku nguo zake zinakokota chini mpaka akapanda kwenye Mimbar na kunyanyua mikono yake akasema, ewe Mwenyezi Mungu tupe mvua nyingi kabla Mtume hajateremsha mikono yake, basi mbingu ilinyesha mvua, kisha Mtume akasema: "Mwenyezi Mungu amlishe Abu Talib huko peponi. Lau angekuwa hai angelifurahi sana basi nani atatusomea maneno yake?" Akasimama Ali bin Abi Talib [a.s] akasema, ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu kama kwamba unakusudia maneno yake haya yafuatayo: "Na mwenye nuru ambaye huombwa mvua kwa uso wake yeye ndiye tegemeo la mayatima na yeye ndiyo mlinzi wa wajane. Wanamzunguka wenye matatizo miongoni mwa kizazi cha Hashim, basi kwake yeye wao wanapata neema nyingi na raha". Mtume **[s.a.w.w]** akasema "Naam".

Imam Ali [a.s] alisoma beti nyingi za Qasida ile na huku Mtume anamuombea Magh-fira Abu Talib hali yeye akiwa kasimama kwenye Mimbar. Baadaye mtu mmoja miongoni mwa Bani Kinanah akawa anasoma Qasida akasema, "(Ewe Mwenyezi Mungu) unastahiki shukurani, na shukurani hizi zatoka kwa mwenye kushukuru. Kwa hakika tumepata mvua kupitia kwenye uso wa Mtume mwenyewe". Mimi nasema, "Rejea zilizotaja Qadhia hii ni nyingi mno, nasi tumeitaja Qadhia hii kutokana na rejea zifuatazo:

(1) Umdatul-qarii fii shar-hil Bukhari, juzuu ya saba, uk. 31 utunzi wa Badru-din Mahmud bin Ahmad Al-ain aliyefariki mwaka 855 A.H, chapa ya Idaratut-Taba-atil-Muniriyya.

(2) Shar-hu Nah-jul-Balaghah cha Ibn Abil-Hadid, juz. 14, uk. 80.

(3) As-siratul-Halabiyya, juz. ya 3, uk 263.

(4) Al-hujat Ala dhahib ila tak-fiiri Abi-Talib, utunzi wa Shamsuddin Abi Ali Fakhar bin Maad aliyefariki mwaka 630,chapa ya Najaf katika Maktaba ya Alawiyya, uk 79.

(5) Siratu Zaini Dah-lan, kilichochapishwa katika Hamish Sirat Al-halab-iyyah, juzuu 1, uk. 81.

## HADITHI YA SITA VILE VILE INAHUSU KUTAWAS-SAL KWA MTUME

Imepokewa kwamba, Sawad bin Qarib alimsomea Mtume **[s.a.w.w]** Qasida yake ambayo ndani yake alitawas-sal kwake Mtume **[s.a.w.w]** akasema: "Nashuhudia kwamba hapana Mola isipokuwa Allah, na kwamba wewe ndiwe mwenye kuaminiwa kuhusu mambo ya kila asiyekuwepo. Nawe ndiye uliye karibu mno kama wasila kwa Mwenyezi Mungu kuliko Mitume wengine ewe mwana wa watukufu walio wema. Tuamrishe (tutende) yale yanayokufikia ewe mbora wa Mitume, japo yatukuwa mazito, na uwe muombezi wangu siku ambayo maombezi yeyote hatamnufaisha Sawad bin Qarib japo kwa sehemu ndogo.[1] Ewe msomaji mpenzi, mpaka sasa tumetaja kiasi cha kutosha cha hadithi zilizopokelewa kuhusu Tawas-

---

kishahukikaanga kwa moto na kukila. Taz: Annihayah fi Gharibi-lhadith cha Ibn Athir al-Jazari chapa ya Beirut, juz. 3, uk 293.

1. Ad-duraru Saiyyah, uk. 27 utunzi wa Zaini Dah-lan, At-tawas-sul Ilahaqiqati-tawas-sul, uk 300.

sul, na tumetegemea vitabu vya hadithi na historia vya Kisunni. Ama kutawas-sal kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu, kwa mujibu wa mapokezi ya watu wa nyumba ya Mtume **[s.a.w.w]** katika vitabu vya kishia jambo hili liko wazi mno na limethibiti barabara kiasi ambacho limekuja kwa njia ya dua vile vile. Sote tunawajibika kujiuliza: "Je tunalazimika kuchukua maarifa ya Kiislamu na hukumu za sheria kutoka kwa "Ibn Taimiyyah" na "Muhammad Ibn Abdul Wahab" na wengineo mfano wa watu kama hawa, au tuchukue maarifa ya Kiislamu na hukumu za sheria toka kwa watu wa kizazi cha Mtume **[s.a.w.w]** ambao Mtume amewataja katika hadithi "Thaqalan" (vizito viwili) kwamba wao ndio kile kizito kidogo cha pili na kwamba wao ni sawa na Qur'an? Kwa hakika kila Muislamu mwenye akili safi ataamua na kuona ulazima wa kuchukua mafunzo hayo toka kwa watu wa kizazi cha Mtume **[s.a.w.w]** ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na kuwatakasa mno.

## MIFANO VA DUA ZA TAWAS-SUL

Ama dua ambazo zimekuja na ndani yake kuna kutawas-sal kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu, na zimetapakaa katika Sahifatul-Alawiyyah[1], na dua ya Arafah[2], na Sahifatus-Sajjadiyyah[3] na vitabu vinginevyo ni nyingi mno, tunataja mifano ya dua hizo kama ifuatavyo:

1. Imam Ali [a.s] katika dua yake anasema: Kwa haki ya Muhammad na Aali Muhammad iliyo juu yako, (Ewe Mwenyezi Mungu) na kwa haki yako tukutu juu yao (nakuomba) uwape rehma kwa sababu wewe ndiwe unayestahiki na unipe mimi kilicho bora mno ya vile ulivyowapa waombaji miongoni mwa waja wako waliopita katika waumini na unipe kilicho bora mno ya vile utakavyowapa waja wako waliosalia miongoni mwa waumini.
2. Na anasema bwana wa mashahidi AI-Imam Husein bin Ali [a.s] katika dua yake ya Arafah: "Ewe Mwenyezi Mungu tunaelekea kwako jioni hii ambayo umeifaradhisha na kuitukuza kwa haki ya Muhammad Mtume wako, mjumbe wako na mteule wako katika viumbe vyako". " Na anasema Al-Imam Zaynul-Abidiina katika dua yake inayohusu kuandama kwa Mwezi wa Ramadhan: "Ewe Mwenyezi Mungu nakuomba kwa haki ya Mwezi huu na kwa haki ya wale wataofanya Ibada ndani yake tangu mwanzo hadi mwisho, miongoni mwa Malaika uliyemkurubisha au Nabii uliyemtuma, an mja mwema uliyempenda".[4]

## MWENENDO WA WAISLAMU KATIKA TAWAS-SUL

Sera ya Waislamu katika zama za uhai wa Mtume **[s.a.w.w]** na baada ya kufa kwake inakubaliana na kutawas-sal kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu na kuomba uombezi kupitia vyeo vyao na heshima zao mbele ya Mwenyezi Mungu. Ifuatayo ni mifano ya sera hiyo ya Waislamu.

1. Ibn Al-Athir mwana historia mashuhuri aliyefariki mwaka 630 anaandika hivi: "Omar bin Al-Khatab aliomba mvua kupina kwa Abbas

---

1. Ni mkusanyiko unaokusanuya baadhi ya dua za Imam Ali, Amirul-Muuminina [a.s] alizikusanya Sheikh Abdulla As-Samahiji.
2. Ni dua ya Imam Husein [a.s] katika Arafaat siku ya Arafah.
3. Ni baadhi ya dua za Imam Zaynul Abidiina.
4. Sahifatus-Sajjadiyah dua namba 44.

katika mwaka wa ukame ulipozidi, basi Mwenyezi Mungu akawateremshia mvua na kwa dua hiyo ardhi ikaota mimea, Omar akasema: "Wallahi huu ni wasila kwa Mwenyezi Mungu na hii ni daraja mbele yake". Naye Hassan alisema: "Imamu aliomba baada ya ukame kutufikia mfululizo. Basi Mawingu yakanyesha kwa kipaji cha Abbas. Ni Ammi ya Mtume na ndugu wa mzazi wake ambaye amemrithisha Mtume heshima hiyo, watu wengine hawakuipata. Kwake yeye Mola ameihuyisha ardhi na sasa imekuwa ya kijani kibichi kila sehemu baada ya kuwa kame". Na baada ya watu kuwa wamepata mvua hii wakawa wanajipangusia kwa Abbas na kumwambia, pongezi ewe uliyezinywesha maji haram mbiIi (Maka na Madina).[1] Kufanya mazingatio kwenye tukio hili la kihistoria ambalo sehemu yake fulani ameitaja pia Bukhari katika sahihi yake, kunatia nguvu kusema kwamba miongoni mwa aina za wasila ni kutawas-sal kwa watu wenye vyeo na heshima mbele ya Mwenyezi Mungu, na ni kitu ambacho matokeo yake ni kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu na pia kumtukuza muombaji na yule mwenye kutawas-sal.

Je, ni maelezo gani yaliyo wazi kuliko kauli ya Omar aliposema "Wallahi huu ndiyo wasila kwa Mwenyezi Mungu na daraja mbele yake".

2. Al-Qastalimy aliyefariki mwaka 923 A.H. anasema: "Hakika Omar alipoomba mvua kwa wasila wa Abbas alisema, "Enyi watu hakika Mtume alikuwa akimuona Abbas kuwa ana haki kwake kama ile aionayo mtoto kwa mzazi wake, basi mfuateni Mtume kwa amii yake na mumfanye Abbas kuwa ni wasila kwa Mwenyezi Mungu". Katika maelezo haya kuna ufafanuzi wa kusihi tawas-sul, na kwa maelezo haya pia inavunjika kabisa kauli ya mwenye kuzuwiya Tawasul kwa watu walio hai na wafu na pia inavunjika kauli ya anayezuwiya kutawas-sal kwa mtu asiye Mtume."[2]

3. Hapo kabla tumetaja kwamba "Mansur Al-Ab-basi Ad-dawaniqi" alimuuliza Malik bin Anas, Imam wa Madhehebu ya Malik, namna ya kumzuru Mtume **[s.a.w.w]** na namna ya kutawas-sal kwake..... naye akamwambia Malik:

"Ewe Abu Abdillah nielekee Qibla niombe au nimuelekee mjumbe wa Mwenyezi Mungu?" Malik akasema: "Kwa nini unampa kisogo Mtume wakati yeye ndiyo wasila wako na wasila wa baba yako Adam kwa Mwenyezi Mungu siku ya Kiyama? Ilivyo sawa muelekee na umuombe akuombee na Mwenyezi Mungu atakubali maombi yako, kwani Mwenyezi Mungu anasema: Na lau wao wakizidhulumu nafsi zao...[3]

4. Beti hizi mbili zifuatazo amezitaja lbn Hajar Al-Haithami kutoka katika shairi la Imam Shafii - Imam wa Madhehebu ya Kishafii. "Kizazi cha Mtume, wao ni njia yanga na wao ni wasila wangu kwa Mwenyezi Mungu, kwao wao kesho nataraji kupewa kitabu changu kwa mkono wa kulia."[4] Baada ya maelezo yote yaliyotangulia miongoni mwa dalili na hoja na ushahidi inawezekana kusema kwamba Manabii na watu mashuhuri wa dini wao ndio ule wasila alioukusudia Mwenyezi Mungu aliposema: "Enyi

1. Usudul-ghabah fii maarifat-S-Sahaba, juz. 3, uk 111, chapa ya Misri.
2. Kitabul-Mawahibil-laduniyyah: Chapa ya Misri.
3. Wafaul Wafa, juz. 2, uk. 1376.
4. As-sawaiqul-muh-riqah cha Ibn Hajar, uk. 178.

mlioamini, mcheni Mwenyezi Mungu na mtafute wasila kwake." Qur'an, 5:35.

Na kwa hakika Mwenyezi Mungu ameamuru kuwafanya wao kuwa ni wasila wa kumfikia yeye Mwenyezi Mungu. Na hapana shaka kwamba, wasila haukuishia kwenye kutekeleza mambo ya faradhi na kujiepusha na mambo ya haramu peke yake, bali unakwenda mbele zaidi na kukusanya matendo ya Sunna ambayo ndani yake mna kutawas-sal kwa Mawalii. Je, yawezekana kusema kwamba wanachuoni na wahakiki walikosea kuifahamu maana ya "wasila"? Pamoja na kufahamika kuwa wao ndio marejeo katika hukmu za sheria nao ndio walohifadhi hadithi na ni miongoni mwa wasomi wa Kiislamu ambao huashiriwa kwa kutolewa mifano yao? Hakika watu wanaojitokeza kukosoa ukweli huu na dalili hizi na wakawa wanatafiti huku na huko kujaribu kugeuza kila hadithi na dalili, wao wanafanana na hakimu ambaye hukimbilia kuhukumu bila ya kuwa na ushahidi anaoutegemea. Bukhari anapokea hadithi katika Sahihi yake isemayo:

"**Hakika Omar bin Khatab alikuwa kila wanapopatwa na ukame huomba mvua kwa Abbas bin Abdil-Muttalib (r.a.) na kisha husema, "Ewe Mwenyezi Mungu tulikuwa tukitawas-sal kwako kupitia kwa Mtume wetu na ukitupa mvua, basi sasa tunatawas-sal kwako kwa ammi ya Mtume wetu basi tupe mvua." Bukhar anasema, "Basi hupewa Mvua.**"[1] Hakuna majadiliano juu ya kusihi kwa hadithi hii kiasi kwamba hata huyo Ar-rifai ambaye ni mwandishi wa Kiwahabi anayepinga hadithi mutawatiri za kutawas-sal kwa njia yoyote ile, lakini amekiri kwamba hadithi hii imesihi akasema: "Hakika hadithi hii ni sahihi na kama ruhusa hii itakuwa imesihi kisheria, basi sisi tutakuwa miongoni mwa watu wa kwanza kuikubali na kutenda kwa mujibu wa hadithi hiyo". Kutokana na kufahamika maelezo waliyoyataja yaliyopokelewa toka kwa Omar bin Khatab kuhusu kutawas-sal kwa Abbas na kwamba yeye aliapa kwa Mwenyezi Mungu akasema, "Wallahi huu ndiyo wasila kwa Mwenyezi Mungu na daraja mbele yake", inadhihiri katika hadithi hii kuwa ukweli wa wasila ni kutawas-sal kwa Abbas yeye mwenyewe an ni kwa heshima yake na jaha yake mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na siyo kutawas-sal kwa dua ya Abbas.

Kwa hali hii, amepokea Muhammad Bin Nuuman Al-Maliki aliyefariki mwaka 683 A.H. ndani ya kitabu chake kiitwacho "Misbahud-dhalami fil-mustaghiithina bikhairil-anam" namna ya kutawas-sal alikotawas-sal Omar kwa Abbas akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu tunakuomba mvua kupitia kwa ammi ya Mtume wako, na tunataka kwako msaada kupitia kwake kwa ndevu zake nyeupe, basi wakapewa mvua" na kwa matokeo haya Abbas bin Ut-ba bin Abi-Lahab anasema: "Kupitia kwa ammi yangu Mwenyezi Mungu aliinywesha Hijazi na watu wake, wakati Omar alipoomba kupitia kwenye ndevu zake nyeupe".[2] Naye Hassan alisema: "Mvua ilinyesha kwa kipaji cha Abbas". Na amesema Ibn Hajar Al-Al-as-qalani, "Abbas aliomba

1. Sahih Bukhari, babu salatul-istiqai, juz. 2, uk. 32.
2. Wafa-ul Wafa, juz. 3, uk. 375. Amenakili toka katika Mis-bahud-Halam.

kwa Mwenyezi Mungu kwa kusema....Watu walikuelekea kupitia kwangu kutokana na daraja yangu kwa Mtume wako".

Ewe msomaji mpendwa; imekudhihirikia wazi kwamba kutawas-sal hapa tunakokuelezea hapa kulikuwa ni kutawas-sal kwa dhati ya Abbas na heshima yake. Wanachuoni wa fani ya Balagha wamesema: "Taaliqul-hukmi Bil-was-fi Mush-irun bil-illiyyat." Maana yake: "Hukumu inapolazimiana na sifa huwa inajulisha kwamba sababu ya kupatikana hukumu hiyo ni sifa ile. Kwa mfano Qur'an tukufu inasema: "Na ni juu ya mtu ambaye kwa sababu yake amezaliwa mtoto (yaani baba) rizki ya hao kina mama". Qur'an, 2:233.

Maana yake ni kwamba mwanamke aliyemzalia mume mtoto, basi ni wajibu kwa mume kusimamia matumizi ya mwanamke huyo. Hukumu iliyopo hapa ni ule wajibu wa kutoa matumizi, na sifa ni yule mtoto aliyezaliwa na mwanamke. Hebu tazama mfano mwingine: "Kama mzazi atamwambia mwanawe "Muheshimu mwanachuoni" hakuna sababu nyingine isipokuwa ni elumi yake na ubora alionao. Kwa msingi huu tulioueleza sasa hivi unaikuta kauli ya Omar anaposema: "Sisi tunatawas-sal kwako kupitia kwa ammi ya Mtume wako".

Ndani ya kauli hii kunabainika sababu ya katawas-sal kwa Abbas kinyume na mtu mwingine, na hiyo ni kwa sababu ya kuwa kwake ni ammi ya Mtume **[s.a.w.w]**. Naye Abbas mwenyewe alisema: "Kwa heshima niliyo nayo kwa Mtume wako". Kwa ufupi baada ya yote yaliyotangulia inawezekana kusema kwa yakini kamili kwamba, "Bila shaka Waislamu toka hapo mwanzo wa kuja Uislamu walikuwa wakitawas-sal kupitia kwa watu wema na watukufu".

## 6. USHAIRI WA SAFIYYAH AKIOMBOLEZA KIFO CHA MTUME [s.a.w.w]

Bibi Safiyyah binti Abdil-Muttalib (Shangazi ya Mtume) alisoma Qasida baada ya kufariki Mtume **[s.a.w.w]** kuomboleza kifo chake, na sehemu ya Qasida hiyo ni hii ifuatayo:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wewe ndiyo matumaini yetu, uIikuwa mwema wetu na wala hukuwa mnyanyasaji, na ulikuwa mwema mpole ewe Mtume wetu, basi leo na akulilie yeyote mwenye kulia".[1] Kitika kipande hiki cha shairi ambacho kilisomwa mbele ya masikio ya Masahaba, nao wanahistoria wakakisajili tunapata faida ya mambo mawili: Kwanza: Kuzisemesha roho na hasa kumsemesha Mtume baada ya kufa ni jambo lililokuwa linafaa na likitumika tangu hapo mwanzo, na bibi Safiyyah anaposema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu" kusema hivi haikuwa ni usemi wa kipuuzi na mchezo tu, au ni shirki kama wanavyodai Mawahabi wapotovu. Pili: Bibi Safiyyah aliposema, "Wewe ndiyo matumaini yetu" inajulisha kwamba Bwana Mtume **[s.a.w.w]** ndiye matarajio na matumaini ya jamii ya Kiislamu katika nyakati zote na kila hali na wala hauwezi kukatika au kumalizika uhusiano wake na jamii hiyo hata baada ya kufariki kwake.

---

1. (1) Dhakhairul-uqbaa cha Al-hafidh Al-Muhibbu At-Tabari, uk. 252. (2) Maj-mauz-zawaid, juz. 9, uk. 36.

## BAADHI YA MAANDIKO YALIYOANDIKWA KUHUSU TAWAS-SUL

Inafaa tuashirie baadhi ya vitabu vinavyotegemewa vilivyoandikwa na wanachuoni wa Kisunni kuhusu kutawas-sal kwa Mtume Mtukufu **[s.a.w.w]**, na pia kuvirjea vitabu hivi kutayaweka wazi maoni ya wanachuoni wa Kiislamu juu ya kutawas-sal kwa Manabii na Mawalii, na kutia nguvu kwamba kutawas-sal tangu hapo mwanzo lilikuwa ni jambo linalotendeka na ni sunna iliyokuwa ikifuatwa na Waislamu sika zote kinyume cha wanavyodai Mawahabi.

1. Kitabu kiitwacho, Al-Wafau fii Fadhailil-Mustafa, cha lbn Al-Jauzi aliyefariki mwaka 597 A.H. Yeye alitenga mlango maalumu katika kitabu chake hiki utakaozungumzia kutawas-sal kwa Mtume **[s.a.w.w]** na mlango mwingine uliohusu kuomba uponyo kwenye kaburi lake tukufu.

2. Mis-bahud-dhalami fil-mustaghithina Bikhairil-anam, kilichotungwa na Muhammad bin Nuuman Al-Maliki, aliyefariki mwaka 673 A.H., na As-Samhudi amenakili nakala nyingi kuweka kwenye kitabu chake kiitwacho Wafaul Wafa kutoka ndani ya kitabu hiki cha Muhammad bin Nuuman Al-Maliki Babul-tawas-sul Binnabi **[s.a.w.w]**.

3. Al-Bayan Wal-Ikhtisar cha ibn Dawud Al-Maliki As-Shadhili. Ndani ya kitabu hiki ametaja khabari za wanachuoni na watu wema kutawas-sal kwa Mtume **[s.a.w.w]** nyakati walizokuwa wakipatwa na matatizo.

4. Shifaus-siqami cha Taqiyuddin as-Subaki aliyefariki mwaka 756 A.H., yeye amezungumzia vizuri kutawas-sal kwa Mtume kwa njia ya Tah-liiili kuanzia uk. 120 mpaka 133.

5. Wafaul Wafai liakhbari Daril-Mustafa cha As-sayyid Nurudin As-Samhudi aliyefariki mwaka 911 A.H. Yeye ameitafiti tawas-sul kwa upana sana ndani ya juzuu ya pili kutoka uk. 413 mpaka 419.

6. Al-Mawahibal-laduniyyah cha Abul-abbas AI-Qastalani aliyefariki mwaka 932 A.H.

7. Shar-hul-mawahibil-laduniyyah cha Az-Zirqani Al-Maliki Al-Misri aliyefariki mwaka 1122 A.H., ndani ya Juzuu ya Nane uk. 317 amezungumzia tawas-sul.

8. Sul-hul-ikh-wan cha Al-Khalidi Al-Bagh-dadi aliyefariki mwaka 1299, pia anayo risala maulum inayozungumzia ruhusa ya kutawas-sal kwa Mtume **[s.a.w.w]**, akimpinga katika risala hiyo Al-Alusi, na risala hiyo ilichapishwa mwaka 1306 A.H.

9. Kanzul-matalib cha AI-Adawi AI-Hamzawi aliyefariki mwaka 1303 A.H.

10. Fur-qanul-Qur-an cha Al-Azzami As-Shafi al-Qudhai kitabu hiki kilichapishwa pamoja na kitabu kiitwacho Al-as-mau Wassifat cha Al-Baihaqi chenye kurasa 140.

Ewe msomaji mpendwa kuvirejea vitabu hivi na hasa vile vilivyozungumzia tawas-sul kwa ufafanuzi (kitabu Sul-hul-Ikhwan na Fur-qanul-Qur'an viko katika mstari wa mbele) kunaithibitisha sera ya Waislamu katika zama zote na nchi zote kuwa wao hutawas-sal kwa Mtume **[s.a.w.w]** na kunadhihirisha kupotea kwa Ibn Taimiyyah na wanafunzi wake na ubovu wa maoni yao na itikadi yao mbovu.

**Mwisho**: Kwa kumalizia sehemu hii tunasema: Qur'an tukufu imeweka wazi kuwa kutawas-sal kupitia kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu ni jambo linalofaa, bali inahimiza kutawas-sal pale iliposema: "Enyi mlioamini mcheni Mwenyezi Mungu na mtafute wasila kwake na piganeni katika njia yake ili mpate kufanikiwa". Qur'an, 5:35. Aya hii inahimiza kutafuta wasila katika nyanja zote kwa jumla. Swali linakuja, "Wasila ni kita gani?" Jawabu: Aya tukufu ya Qur'an haikutaja wasila kuwa ni kitu gani. Bila shaka kutekeleza faradhi za dini ni miongoni mwa (wasila) za mafanikio na uokovu, lakini hapana shaka vile vile kwamba wasila hauishii kwenye mambo hayo peke yake, bali kufuatana na mwenendo wa Waislamu kwa muda mrefu katika historia, miongoni mwa wasila ni kutawas-sal kupitia kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu na wacha Mungu na kwamba wasila huu ni miongoni mwa mafanikio na kukubaliwa mahitajio na matumaini.

Jambo hili liko wazi ndani ya maelezo tuliyoyaeleza katika maneno ya Imam wa Kimalik alipozungumza na Mansuri AI-Abbasi. Na kutawa-sal kwa Omar bin Khataab kwa Abbas ili wapate mvua na mengineyo. "Hakika haya ni mawaidha atakaye na ashike njia aende kwao Mola wake".

siyo katazo Ia kuharamisha litokalo kwa Mola. Na katazo la muongozo liko katika mahala pa nasaha na mawaidha, na kulikhalifu katazo hili hakuwajibishi adhabu, wala haliondoshi isma kwa namna yoyote ile. Basi huwajibisha Taathira kwenye dhati ya kitendo, k.m., Lau tabibu atamkataza mgonjwa wa mafua kutumia vitu vichachu, kisha mgonjwa akakhalifu, basi tendo lake la kukhalifu litaakisi athari ya kimaumbile ambayo ni kuzidi kwa mafua na ugonjwa. Na ndani ya Qur'an Tukufu ziko aya nyingi zinazojulisha kwamba, katazo alilokatazwa Adam kuukurubia mti ule lilikuwa ni katazo la kutoa muongozo na hapana athari kwa kukhalifu katazo hili isipokuwa ni matokeo ya kimaumbile kwa kukhalifu huko. Unaweza kurejea aya ya 118 na 119 katika Surah Taha.

10

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## KUWAWEKEA NADHIRI WATU WALIOKUFA

Kabla ya kueleza chochote, tunataja kwanza "Taarifu" ya "Nadhiri". Maana ya nadhiri ni mtu kuilazimisha nafsi yake kutenda kitu maalum iwapo makusudio yake yatatimia au haja yake ikikubaliwa, na atasema wakati awekapo nadhiri, kwa mfano: "Ni wajibu juu yangu iwapo nitapasi mtihani nitahitimisha Qur'an kwa ajili ya Mwenyezi Mungu." Hii ndiyo nadhiri ya kisheria, na ni lazima iwekwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu. Ikiwa muweka nadhiri atasema: "Nimeweka nadhiri kwa ajili ya mtu fulani, basi usemi wake huo utachukuliwa kuwa ni "majazi", na maana yake itakuwa "Nimeweka nadhiri kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na thawabu za nadhiri hii ni kwa ajili ya Fulani."

### THAWABU ZA NADHIRI

Thawabu za nadhiri zimegawanyika mafungu matatu:

1. Thawabu zake ziwe kwa mwenye kuweka nadhiri
2. Thawabu zake ziwe kwa mtu mwingine aliye hai
3. Thawabu zake ziwe kwa mtu mwingine aliye kufa.

Kwa hiyo muweka nadhiri anaweza kuzihusisha thawabu za nadhiri yake kwake mwenyewe au kwa mtu mwingine aliye hai mmoja au zaidi au kwa mtu aliye kufa mmoja au zaidi. Mafungu yote haya matatu yanafaa na ni lazima kwa yule anayeweka nadhiri kuitimiza nadhiri yake pindi atakapokuwa ametimiziwa haja yake. Mwenyezi Mungu Mtukufu amemsifu Imam Ali, Bibi Fatma, Hasan na Husein [a.s] (kwa kutekeleza nadhiri) aliposema: "Wanatimiza nadhiri." Qur'an, 76:7 Ewe msomaji, nadhiri ni suna maarufu kwa Waislamu wote ulimwenguni kote, na hasa katika miji ambayo kuna makaburi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu na waja wake wema.

Na ilizoweleka kwa muda mrefu miongoni mwa Waislamu kuweka nadhiri kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kuzitoa zawadi thawabu zake kwa mmoja wa Mawalii wa Mwenyezi Mungu na waja wake wema, mpaka lilipokuja lile gonjwa baya la kansa (fitna na unafiki wa Ibn Taimiyya) akadai kuwa nadhiri ni haramu na kuwashambulia Waislamu hasa Mashia ambao nadhiri imezoweleka kwao zaidi ya Waislamu wengine kutokana na kuweko kwa makaburi mengi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu katika miji yao, basi kwa hilo (Ibn Taimiyya) akawatuhumu kuwa wanafanya shirki na upotevu na akasema: "Yeyote mwenye kuweka nadhiri ya kitu chochote kwa ajili ya Mtume au mwingine miongoni mwa Manabii na Mawalii katika watu waliokufa, au akachinja kichinjo, basi atakuwa kama washirikina ambao huchinja kwa ajili ya masanamu yao na kuyawekea nadhiri masanamu hayo, basi mtu huyo atakuwa anaabudu kisichokuwa Mwenyezi Mungu kwa hiyo atakuwa ni kafiri."[1] Baadaye tena akaja Muhammad ibn Abdul-Wahab baada ya kupita karne tatu hivi, akaanza kuipiga kelele kama za huyo aliyemtangulia na kuhuisha bid'a na uzuishi wake. Kwa bahati

1. Fur-qanul-Qur'an cha Al-Azzami uk. 132 (amemnukuu Ibn Taimiyya).

mbaya sana wawili hawa hawakufahamu au walijifanya hawafahamu kwamba, kipimo cha ujumla ni makusudio na nia ya moyoni kwani "matendo ni kwa niya".

Na kama itahukumiwa kuwa, eti kiasi cha matendo yanavyoonekana ndiyo dalili ya nia ilivyo basi matendo mengi ya Ibada za Hija yanafanana na matendo ya wale waabuduo sanamu kwa yanavyoonekana, kwani wao walikuwa wakitufu kuzunguuka masanamu yao na wakiyabusu, nasi tunatufu kuzunguuka Al-Kaaba tukufu na tunaibusu Hajarul-as-wad, na tunachinja na kufanya Taqarub huko Mina siku ya Idi Al-adh-haa. Basi je tumekufuru na tumemshirikisha Mwenyezi Mungu katika kutekeleza Ibada hizi?!!! Kwa hiyo, kipimo ni nia ya moyoni na wala haifai kabisa kuhukumu na kutoa fatwa kwa kiasi cha matendo kama yanavyoonekana. Kwa hiyo kila anayeweka nadhiri kwa mmoja wa Mawalii wa Mwenyezi Mungu, hakuna anachokikusudia moyoni mwake isipokuwa ni nadhiri kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kuzitoa zawadi thawabu za nadhiri hiyo kwa Walii huyo na wala siyo kinyume chake. Na kwa bahati nzuri ni kwamba, wanachuoni na wanafikra wa Kishia na Kisunni wameupinga uzushi na upotevu wa Ibn Taimiyyah na waliyo kama yeye. Hebu msikilize Al-Khalidi akimpinga Ibn Taimiyyah anasema:

"Hakika mas-ala ya nadhiri yatatazamwa kwa mujibu wa nia ya mwenye kuweka nadhiri na kwamba matendo yanategemea nia ya mtendaji, basi kama mwenye nadhiri atamkusudia maiti mwenyewe kuwa ndiyo anamuwekea nadhiri na kujikurubisha kwa maiti huyo, nadhiri hiyo haitafaa kabisa. Na ikiwa nia yake ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukfu na kuwanufaisha walio hai kwa namna fulani, na thawabu zake apate yule aliyemuwekea nadhiri hiyo sawa sawa akibainisha aina ya manufaa hayo au asibainishe, na kukawa kuna kitu kitakachoendelea kutumika katika mazingira ya watu au ndugu wa maiti au mfano wa hayo, basi katika hali hii ni lazima nadhiri hiyo itimizwe."[1] Kisha akaeleza mambo waliyoyaweka wazi wanachuoni wa zama zake na waliokuwa karibu ya zama zake juu ya mas-ala haya. Naye Al-Azzami katika kitabu chake kiitwacho "Fur-qanul-Qur'an amesema: "Na yoyote atakayefahamu hali ya wanaofanya jambo hilo (nadhiri) miongoni mwa Waislamu, atawakuta katika kuchinja wanakochinja na nadhiri waziwekazo hawawakusudii maiti miongoni mwa Manabii na Mitume isipokuwa wanachokusudia ni kutoa sadaka kwa niaba yao na thawabu ziwaendee wao, nao wanafahamu kwamba Ij-mai ya Masunni imekubaliana kwamba sadaka itolewayo na watu walio hai, huwanufaisha waliokufa na inawafikia, na hadithi zilizotaja jambo hili ni sahihi tena mashuhuri."

Miongoni mwa hadithi hizo ni ile iliyosihi na kupokelewa toka kwa Sa'ad, kwamba yeye alimuuliza Mtume **[s.a.w.w]** akasema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hakika mama yangu amefariki na ninafahamu kwamba lau angeishi zaidi ya hapa angetoa sadaka, basi je kama nitatoa sadaka kwa niaba yake itamnufaisha?" Mtume **[s.a.w.w]** akasema: "Ndiyo". Sa'ad akauliza: "Ni sadaka ipi yenye manufaa makubwa zidi ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?" Mtume **[s.a.w.w]** akasema "Maji". Basi Sa'ad

---

1. Sul-hul-ikh-wan cha Al-Khalidi, uk. 102 na kuendelea.

akachimba kisima na akasema: "Kisima hiki (thawabu zake) ni kwa ajili ya mama wa Sa'ad".[1] Amekosea sana Muhammad Ibn Abdul-Wahab pale alipodai kwamba, Muislamu atakaposema "Sadaka hii Linnabi (kwa ajili ya Mtume) au Lil- Walii (kwa ajili ya Walii)" eti lamu iliyopo hapa ni ile ile lamu iliyopo kwenye kauli yetu tusemapo "Nadhartu Lillah" yaani nimeweka nadhiri kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na maana yake ni kuonyesha lengo Ia nadhiri. Lakini maoni haya si sahihi kwa sababu kama sadaka hii itatumika kwa maslahi ya Nabii wakati wa uhai wake na baada ya kifo chake (basi nadhiri itakuwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, lakini matumizi yake ni kwa ajili ya maslahi ya Nabii). Na kwa muelekeo huu anasema Al-Azzami baada ya kukitaja kisa cha Sa'ad: "Lamu iliyoko kwenye "Hadhihi Liumi Sa'ad" ni lamu inayoonyesha upande ilikoelekezwa thawabu ya sadaka hii, wala haionyeshi kwamba mama wa Sa'ad ni mwenye kuabudiwa na mwanawe, na maana hii ndiyo inayokusudiwa na Waislamu, hivyo wao ni wafuasi wa Sa'ad na wala siyo wenye kuabudu sanamu. Na lamu hiyo ni kama iliyoko katika kauli yake Mwenyezi Mungu aliposema: "In-namas-sadaqatu Lil-fiqarai" yaani sadaka ni kwa ajili ya mafakiri (wenye kuhitajia), na siyo kama lamu iliyoko kwenye kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema "Rabbi Innii Nadhartu Laka Mafii Bat-ni Muhar-ran" yaani, "Mola wangu nimeweka nadhiri kwako aliyemo tumboni mwangu awe wa kukutumikia"- Qur'an, 3;35. Aukauli ya msemaji asemapo, "Salaitu Lillahi wa Nadhartu Lillahi", yaani nimeswali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na nimeweka nadhiri kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Atakapochinja mchinjaji kwa ajili ya Nabii au Walii au akaweka nadhiri ya kitu kwa ajili yake, hapo huwa hakusudii ila kumtolea sadaka hiyo na kumpa thawabu za sadaka hiyo. Na hapo itakuwa ni zawadi toka kwa walio hai kuwapa waliokufa jambo ambalo linakubalika kisheria na lina thawabu. Mas-ala haya yanadhri yameelezwa kwa urefu katika vitabu vya Fiq-hi na vile vilivyoandikwa kumpinga Bwana huyo (Ibn Taimiyya) na wale wote wanaomfuata".[2] Bila shaka ewe msomaji imekudhihirikia kwamba inafaa kuweka nadhiri kwa ajili ya manabii na Mawalii bila ya kuwepo mchanganyiko wa shirki katika suala hili, hupata thawabu kwa tendo hilo anayeweka nadhiri iwapo nadhiri hiyo ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na kile kinachowekewa nadhiri kikachinjwa kwa jina Ia Mwenyezi Mungu. Mtu asemapo nimechinja kwa ajili ya Mtume haina maana kuwa kachinja kwa ajili yake bali ana maana ya zile thawabu za kuchinja ndiyo za Mtume, ni sawa na kusema nimemchinja kuwa ajili ya mgeni ambayo itamaanisha manufaa ya kilichochinjwa yatamrejea mgeni, kwani yeye ndiye sababu ya kupatikana kichinjo hicho. Kuliweka wazi zaidi jambo hili tunataja hadithi iliyopokelewa kwa Thabiti bin Adh-haak amesema: "Mtu fulani aliweka nadhiri katika zama za Mtume **[s.a.w.w]** kuchinja ngamia mahala paitwapo "Buwanah" baadaye alikuja kwa Mtume **[s.a.w.w]** akamweleza, Mtume **[s.a.w.w]** akasema: Je, hapo Buwanah kulikuwa na sanamu anayeabudiwa miongoni mwa masanamu ya Kijahiliya?" Wakasema: "Hapana". Mtume **[s.a.w.w]** akauliza, "Je, kulikuwepo na sikukuu miongoni mwa sikukuu

1. Fur-qanul-Qur'an, uk. 133.
2. Fur-qanul-Qur'an, uk. 133.

zao?" Wakasema: "Hapana". Mtume **[s.a.w.w]** akamwambia muulizaji, "Timiza nadhiri yako, kwani nadhiri haitimizwi katika kumuasi Mwenyezi Mungu, wala kitu asichokimiliki mwanadamu".[1] Na imepokewa tena kama ifuatavyo:

Kuna mwanamke fulani alifika kwa Mtume **[s.a.w.w]** akasema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu mimi niliweka nadhiri kuchinja mahala fulani ambapo watu wa zama za Jahiliyya walikuwa wakichinja..." Mtume **[s.a.w.w]** akasema, Je, hapo kulikuwepo na wathan (kitu chochote kinachoabudiwa)? Yule mama akasema: "Hapana". Mtume **[s.a.w.w]** akamwambia: "Timiza nadhiri yako"[2] Na imepokewa toka kwa Maimuna binti Kardam kwamba, baba yake alimwambia Mtume **[s.a.w.w]**: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu mimi nimeweka nadhiri, iwapo atazaliwa kwangu mtoto wa kiume, nitachinja kiasi cha mbuzi fulani kwenye kilele cha Buwanah". Anasema mpokeaji aliyepokea toka kwa Maimuna, sikumbuki isipokuwa yeye alisema hamsini. Basi Mtume **[s.a.w.w]** akasema, "Je, kuna chochote katika wathan?" Akajibu, "Hapana". Mtume **[s.a.w.w]** akasema: "Tekeleza nadhiri yako uliyoiweka kwa ajili ya Mwenyezi Mungu".[3] Bila shaka ewe msomaji umeona jinsi ambavyo Mtume **[s.a.w.w]** amekariri suali la kuwepo masanamu mahali pa kuchinjia? Hii ni dalili kwamba nadhiri iliyo haramu ni ile ya kukusudia masanamu, kitu ambacho ilikuwa ndiyo desturi ya watu wa Jahiliyya kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu,... "Na kilichochinjwa mahali panapofanyiwa Ibada ya masanamu... hilo kwenu ni dhambi". Qur'an, 5:3

Na kila atakayetazama kwa makini hali za watu wanaozuru sehemu tukufu na makaburi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu, atafahamu vizuri kwamba watu hao huweka nadhiri kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na radhi yake na huchinja vichinjo vyao kwa jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa nia ya kumnufaisha mwenye kaburi kwa thawabu za nadhiri hiyo na kuwanufaisha mafakiri kwa nyama ya hicho kilichochinjwa. Kwa kumalizia sehemu hii tunataja neno la Al-Khalidi alilolisema baada ya kutaja yale aliyoyapokea Abu Dawud katika Sunan yake. Amesema Al-Khalidi: "Ama Makhawarij kutolea kwao dalili hadithi hii kuwa eti haifai kuweka nadhiri mahala walipozikwa manabii na watu wema kwa madai kwamba manabii hao na watu hao wema ni masanamu (Tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana na kauli kama hizi) na nisherehe miongoni mwa sherehe za Kijahiliya, madai yao yote ni miongoni mwa upotevu wao na uzushi wao na ujeuri wao dhidi ya manabii wa Mwenyezi Mungu na Mawalii wake kiasi cha kuwaita kuwa ni masanamu, na kwa kweli inaonyesha wazi dharau kubwa hasa kwa Mitume [a.s]. Hakika yeyote atakayewadharau japo iwe kwa kinaya atakufuru na toba yake haikubaliwi katika baadhi ya kauli za Maulamaa. Na watu hawa (makhawariji) ambao Mwenyezi Mungu amewatenga kwa sababu ya ujinga wao wanasema eti kutawas-sal kwa Mitume ni kuwaabudu na wanawaita ni masanamu, hawawaidhiki

1. Sunan Abu Dawud, juz. 2, uk 80.
2. Sunan Abu Dawud, juz. 2, uk. 81.
3. Sunan Abu Dawud, juz. 2, uk. 81.

(hawasikii) watu hawa kwa ujinga wao na upotevu walio nao. Mwenyezi Mungu ndiye mjuzi zaidi.[1]

## KUADHIMISHA KUZALIWA KWA MAWALII WA MWENYEZI MUNGU NA KUFA KWAO

Je, kuadhimisha uzawa na vifo vya Mawalii wa Mwenyezi Mungu ni Bid'a? Hakika Mawahabi wao wanadai kuwa, kufanya maadhimisho hayo ni haramu.... kwa madai yao haya, wanaonyesha wazi chuki na uadui walionao dhidi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu na viongozi wa Uislamu, hasa pale wanapozuwia kufanyika mikusanyiko ya kusherekekea kuzaliwa kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu na ile ya kuomboleza vifo vyao. Wahabi mmoja ambaye ni Rais wa kikundi cha "AnsarusSunnatil-Muhammadiya" aitwaye "Muhammad Hamid Faqii", katika hashiya yake juu ya kitabu kiitwacho AI-Fat-hul-majid anasema: "Kumbukumbu zilizojaa katika Miji (ya Kiislamu) kwa nia ya kuwakumbuka Mawalii (wa Mwenyezi Mungu) yote hayo ni miongoni mwa aina za kuwafanyia ibada Mawalii hao na kuwatukuza".[2] Ukweli ulivyo ni kwamba, sababu ya msingi ya upotovu wa Kiwahabi katika mambo haya ni kuwa, wao Mawahabi mpaka sasa hawajaifahamu maana ya "Tauhidi, shiriki na ibada". Na kwa sababu hii basi, wao wanachukulia kila aina ya kuwaheshimu Mawalii wa Mwenyezi Mungu kuwa ni kuwafanyia ibada na ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu. Kwa hakika utaona kwamba, mtunzi huyo wa Kiwahabi amefanya mambo bila kuwa na muelekeo hali ambayo imemfanya achanganye baina ya maneno mawili "Ibada" na "Kutukuza".

Yeye ameyataja maneno haya kuwa kila moja lina maana sawa na ya lile lingine, akidhani kwamba maana ya maneno haya mawili ni moja. Ama kwa upande wetu sisi, baadaye tutazungumzia neno "Ibada" na maf-humu yake katika mlango ujao, na tutatoa uthibitisho kwamba, siyo kabisa kila wanapotukuzwa na kuheshimiwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu, basi hiyo iwe ni kuwafanyia ibada. Sasa hivi hebu mazungumzo tuyaelekeze upande wa ruhusa ya kuyaheshimu (Maadhimisho ya) uzawa na kufa kwa Mawalii hao kwa mujibu wa muongozo wa Qur'an tukufu. Katika mambo ambayo hayana shaka ndani yake ni kuwa, Qur'an Tukufu imewataja Manabii wengi kwa maneno ya kuwasifa na kuwatukuza na kuwaheshimu. Kwa mfano:

1. Qur'an inasema kumhusu Nabii Zakariyya na Yahya na wengine kama ifuatavyo: "Bila shaka wao (Manabii) walikuwa wepesi wa kufanya mema, na wakituomba kwa shauku na khofu na walikuwa wakitunyenyekea". Qur'an, 21:90. Basi iwapo kutafanywa Mah-fali ya kuwatukuza manabii hawa, kisha akasimama mzungumzaji akazungumzia habari zao kama zilivyokuja katika Qu'ran kwa maneno ya kuwasifu na akawataja kva utukufu na heshima...basi je, kufanya hivyo atakuwa kafanya kosa? Ilivyo sawa ni kwamba atakuwa ameifuata Qur'an!

2. Qur'an inasema tena kuhusu watu wa nyumba ya Mtume **[s.a.w.w]**:

"Na huwalisha chakula katika mahaba yake, masikini, mayatima na wafungwa... Qur'an, 76:8.

---

1. Sul-hul-ikh-wan cha AI-khalidi, uk. 109.
2. Al-Fat-hul-majid, uk. 154.

Sasa basi, iwapo watakusanyika wafuasi wa Amirul Muuminina Ali bin Abi Talib [a.s] katika kumbukumbu ya siku tukufu aliyozaliwa, na kisha mzungumzaji wao (kwenye mkusanyiko huo) akasema "Kwa hakika Imam huyu yeye ni miongoni mwa hao watu waliotoa chakula chao kumpa masikini, yatima na mfungwa). Je! Hi itakuwa na maana kwamba wamemuabudia? Kwa hiyo basi, hali ni hiyo hiyo katika munasaba wa (maadhimisho ya kumbukumbu ya) kuzaliwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]**. Tunapofanya sherehe kubwa siku ya kuzaliwa kwa Mtume **[s.a.w.w]** na tukazizungumzia aya za Qur'an ambazo zimemsifu Mtume **[s.a.w.w]** au tukazitafsiri aya hizo kutoka katika lugha ya Kiarabu na kuziweka katika lugha nyingine - kutegemeana na hafla yenyewe ilivyo, au tukataja maana ya aya hizo katika mfumo wa kishairi au mfano wake, basi ni kwa nini kwa kitendo hiki tuwe ni waasi wa dini ya Mwenyezi Mungu? Kwa hakika Mawahabi, wao ni maadui wa heshima na utukufu wa Manabii, na Mawalii na uadui wao wanauvalisha vazi la (kutetea) dini na wanasema: "Hakika kuwatukuza na kuwaheshimu Manabii na Mawalii ni Bid'a", ili wawazuwiye Waislamu kufanya maadhimisho haya. Ewe msomaji mpendwa: Hakika maudhui wanayoipinga na kuikemea Mawahabi kwa kupitia madai yao batili, ni ile ya kufanya hafla kwa ajili ya kumbukumbu za Mawalii wa Mwenyezi Mungu. Mawahabi wanadai kwamba, kwa kuwa sherehe hizo zinafanywa kwa Jina Ia Uislamu, basi hapana budi Uislamu uzikubali kwa N-nass maalum au ya jumla vinginevyo zitakuwa ni bid'a na ni haramu.

Jawabu la madai haya liko wazi mno, kwani aya nyingi za Qur'an zinazotufanya tuone umuhimu wa kumheshimu na kumtukuza Mtume **[s.a.w.w]** zinatosha kuruhusu na kwamba mahfali hizi na maadhimisho haya, hayafanywi isipokuwa ni kwa ajili tu ya kuwaheshimu Manabii na Mawalii (wa Mwenyezi Mungu). Basi lengo la maadhimisho haya na mahfali hizi ambazo Mataifa yote ulimwenguni yanaziadhimisha, siyo jingine bali ni kuwapa heshima na daraja watu mashuhuri, kadhalika maadhimisho haya siku zote yamekuwa yakifanywa na Mataifa yote ya Kiislamu ukiondoa tu kikundi hiki kipotofu cha kutoka Najdi (Mawahabi). Lau ingekuwa kitendo hiki ni bid'a na ni jambo jipya linalokwenda kinyume na sheria ya Kiislamu, basi wanachuoni wa Kiislamu katika nchi zote za Kiislamu wao wenyewe wasingefanya mahfali haya wala wasingeshiriki kutoa hotuba na kusoma visomo mbali mbali ambavyo huzidisha mazingatio na furaha kwenye mahfali hizo.

## QUR'AN NA KUWATUKUZA MANABII NA MAWALII

Hivi sasa tunataja baadhi ya ushahidi kutoka katika Qur'an unaoruhusu kuwatukuza Manabii na Mawalii kama ifuatavyo:

Aya ya Kwanza: Qur'an inawaunga mkono watu walionitukuza Mtume **[s.a.w.w]** na inasema: "Basi wale ambao wamemuamini yeye Mtume **[s.a.w.w]** na wakamheshimu na kumsaidia na wakaifuata nuru iliyoteremshwa pamoja na (Qur'an) hao ndiyo wenye kufaulu.[1] Kwa hakika maneno yaliyokuja katika aya hii ni haya yafuatayo:

1. Amanu Bih.. Waliomuamini

1. Qur'an, 7:157.

2. Az-Zaruhu.... Wamemheshimu
3. Nasaruhu.... Wamemsaidia
4. It-tabaun-nura... Wameifuata nuru.

Je, hivi kuna yeyote awezaye kusema kuwa maneno haya na sifa hizi zinahusika tu (kutumika) katika zama zile (alizoishi) Mtume **[s.a.w.w]**? Kamwe haiwezekani kabisa!!! (Kudai namna hiyo). Ilipokuwa hakuna kabisa uwezekano huo, basi neno "Az-zaruhu" ambalo maana yake ni kutukuza na kuheshimu,[1] litakuwa linaenea katika zama za uhai wa Mtume **[s.a.w.w]** na baada ya kufa kwake. Basi Mwenyezi Mungu anataka kipenzi chake mteule (Mtume Muhammad **[s.a.w.w]**) awe ni mwenye kutukuzwa na kuheshimiwa siku zote. Sisi tunajiuliza: Je, kufanya mahfali siku ya kuzaliwa Mtume **[s.a.w.w]** na siku aliyotangaza utume wake na kusoma khutba na Qasida siyo utekelezaji ulio wazi wa kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema "Az-zaruhu" yaani wamemheshimu? Ni ajabu kwamba Mawahabi hawa wanawapa heshima kubwa zaidi viongozi wao na watawala wao, na sisi tunapofanya chini ya heshima hiyo kwa Mtume **[s.a.w.w]** au kwa mimbari yake au Mihrabu yake wao hudai kuwa ni bida'a na ni shirki.

Kwa hakika Mawahabi kwa itikadi yao hii kavu (isiyo hai) wanaharibu heshima ya Uislamu mbele ya mtazamo wa ulimwengu kwa jumla, na wanasababisha Uislamu ueleweke kuwa ni dini isiyokuwa na hisia za kiutu na haina maono ya kiuanadamu na ina upungufu wa kila aina katika kuheshimu na kutukuza na inapinga kuwaheshimu wakubwa zake na viongozi wake. Mawahabi wanaufanya Uislamu uonekane kuwa na upungufu wa kila aina katika (suala zima la) kuwaheshimu na kuwatukuza viongozi wake na kwamba Uislamu unapinga mambo hayo. Na kwa sababu hii basi Mawahabi wanawafanya watu wawe na chuki na Uislamu na kuwaacha wakiupinga na kuuchukia. Yote haya wayafanyayo ni kinyume kabisa na Uislamu ambao, Mwenyezi Mungu ameufanya kuwa ni dini nyepesi yenye ukarimu inayokubaliana na maumbile ya watu, na inakwenda sambamba na huruma za kiutu, na pia kwa uzuri wake inawavutia watu mbali mbali kuikubali.

Aya ya Pili: Kikundi cha Mawahabi ambacho kinapinga kila namna ya maombolezo na kuwalilia mashahidi waliouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu, kinasemaje juu ya mambo yaliyompata Nabii Yaqub [a.s]? Lau Nabii huyu Mtukufu angekuwa hai anaishi miongoni mwa watu wa "Najdi" na wafuasi wa Muhammad bin Abdul-Wahabi, wangelimhukumu vipi Nabii huyu?

Kwa hakika Nabii Yaqub [a.s], alikuwa akilia usiku na mchana kwa kutengana na mwanawe Yusuf [a.s]., na alikuwa akiomboleza na kutaka kujua habari zake na kutaja jina lake mpaka "Macho yake yakawa meupe kutokana na huzuni naye alikuwa amejawa na huzuni."[2] Nabii Yaqub alikuwa akikabiliwa na kila aina ya misiba na macho kuwa meupe na huzuni ya moyo na machungu ya kutengana na mwanawe, lakini hakumsahau mwanawe, bali alikuwa akizidi kuwa na hamu kwa mwanawe kila muda wa kukutana naye ulivyokaribia, kiasi cha kuweza kunusa harufu ya Yusuf [a.s]

1. Kitabu Mufradatil-Qur'an cha Ar-Raghib katika mada ya Az-Zara.
2. Qur'an, 12:84.

kutoka masafa ya mbali. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema akimnukuu Nabii Yaqub [a.s]: "Hakika mimi nahisi harufu ya Yusuf, lau msingekuwa mnaitakidi kuwa nimeharibikiwa na akili (ningenisadiki)".[1] Basi yatakuwaje mapenzi haya na kudhihirisha uhusiano wenye nguvu katika uhai wa huyu mwenye kupendwa (Yusuf [a.s] kuwa ni tendo linalofaa na linaafikiana na Tauhidi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu - lakini mapenzi hayo hayo na tangazo la uhusiano huo huo ugeuke kuwa bid'a, tena haramu baada ya kufa kwake?!!! Inavyoeleweka ni kwamba, kutengana na mtu umpendaye kwa kufariki kwake, ni jambo linalouacha moyo ukiungua kwa majonzi na huzuni na machungu mengi kuliko kutengana naye hali akiwa yu hai.

Basi leo iwapo waumini watakusanyika (ambao wanafanana na Yaqub [a.s] katika kuhuzunika kwake) wakaomboleza kifo cha Walii fulani miongoni mwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu (kama vile Maimamu watukufu ambao kutokana na matatizo yaliyowapata wanafanana na Yusuf bali misiba yao ni mikubwa kuliko ule wa Yusuf) wakafanya kumbukumbu za Walii huyo mwema, kwa hotuba na Qasida, pia wakairejea sera yake na tabia zake tukufu na mambo yake mengine mazuri, kisha wakalia machozi ya mapenzi na huruma juu yake... Je, maana ya matendo yao haya ni kwamba watakuwa wamemuabudu Walii huyo?!!! (Kuitakidi kuwa wamemuabudu Walii huyo) ni uchache wa kufikiri na uchambuzi wa mambo pia ni uchache wa maarifa na kufahamu!!!) Aya Ya Tatu: Mwenyezi Mungu anasema: "Waambie sikutakeni malipo yoyote (juu ya kuwaleteeni Uislamu) isipokuwa muwapende Al-Qurbaa".[2] Miongoni mwa mambo yasiyo na shaka ndani yake ni kwamba, kuwapenda Al-Qurbaa ni moja ya mambo ya faradhi kidini, faradhi ambayo Qur'an imelitolea ushahidi wa wazi mno jambo hili. Sasa basi, iwapo mtu atataka kuutekeleza wajibu huu (wa kuwapenda Al-Qurbaa) baada ya kupita karne kumi na nne, basi atafanya nini katika hali kama hii?!!! Je, siyo kwamba anachotakiwa ni kufurahi kwa yale yaliyowafurahisha na ahuzunike kwa yale yaliyowahuzunisha?!!!

**TAN-BIH**

Zimekuja hadithi nyingi kutoka kwa Mtume **[s.a.w.w]** kwamba, maana ya Al-Qur-baa ni watu wa nyumba ya Mtume **[s.a.w.w]**. Basi iwapo mtu ataadhimisha hafla maalum kwa ajili ya mmoja wa watu hao watukufu, akamsifu Mtukufu huyo na kuyaeleza maisha yake yaliyoambatana na mema na sifa zake njema, pia namna alivyojitolea (katika dini) na akaeleza matatizo na misiba iliyompata Mtukufu huyo... basi je atakuwa kafanya kitendo cha haramu? Au atakuwa amehuisha utajo wa Mtukufu huyo na kumtekelezea yale Mawadda (mapenzi) yaliyowajibishwa (katika aya iliyotajwa hapo kabla)? Na lau mtu yeyote katika kuzidisha upendo kwa hao Al-qurbaa atamtafuta yeyote mwenye nasaba na hao Al-qurbaa na akaja kuzuru makaburi yao, na akasimamisha visomo kwenye makaburi hayo. Je, watu wenye akili na utambuzi wa dini hawataona kuwa mtu huyo anatekeleza faradhi ya kuwapenda Al-Qur-baa? Labda Mawahabi watuambie kuwa: "Ni wajibu kuyaficha moyoni na kutoyadhihirisha kwa

---

1. Qur'an, 12:94.
2. Qur'an 42:23.

namna yoyote ile mapenzi (kwa Al-Qurbaa)...." Inafaa kusema, zama alizoishi Mtume **[s.a.w.w]** na baada yake, zilikuwa na mabadiliko ya itikadi na fikra, basi zama hizi zinashuhudia kukubaliwa kwa Uislamu na mataifa mbali mbali na watu wa aina tofauti, na ndiyo maana Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema: "Na utawaona watu wanaingia katika dini ya Mwenyezi Mungu makundi kwa makundi".[1]

Uislamu ulikuwa ukiwalea wote wanaosilimu na kutosheka na shahada mbili tu hapo mwanzoni, na wao walikuwa wakibakia katika utamaduni wao na desturi zao. Na wala Mtume **[s.a.w.w]** na waliokuja baada yake hawakuweka usimamizi juu ya ada ya watu hao na desturi zao na wala hawakuyataka makabila yote kuwa na desturi moja ya kiutamaduni (bali Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliwaacha wakaendelea na desturi na mila hizo ambazo haziendi kinyume na sheria ya Mwenyezi Mungu.) Kwa hakika kuwaheshimu watu wakubwa na kufanya mikutanao ya maombolezo ya kutaja vifo vyao, na kukusanyika kwenye makaburi yao, pia kudhihirisha upendo kwa ajili yao, yote hayo yalikuwa na bado yanaendelea kuwa ni mambo yanayotendeka katika mataifa yote ulimwenguni. Na katika zama zetu za leo, utawaona watu wa Mataifa ya Mashariki na Magharibi wanasimama muda wa saa nyingi wakisubiri kwenda kuzuru miili iliyohifadhiwa ya viongozi wao na pia makaburi ya viongozi wao waliopita hapo zamani, na huwa wanababujikwa na machozi kutokana na hisia za kujiona kuwa karibu na miili ya viongozi hao, kisha tendo hili wanalizingatia kuwa ni moja katika namna za kuwaheshimu na kuwatakuza. Haijapata kupokewa habari kwamba Mtume **[s.a.w.w]** alikuwa akichunguza mila na desturi za watu kwanza ndipo awakubalie kusilimu, bali alikuwa akitosheka kwa shahada mbili walizokuwa wakizitoa. Basi lau mila na desturi hizi za (kuheshimu uzawa na kuomboleza vifo vya viongozi wao) zingekuwa haramu na ni aina ya kuwaabudu watu hao bila shaka Mtume **[s.a.w.w]** angeliwapa sharti ya wao kujitenga na kila aina ya mila na desturi walizonazo ndipo waingie katika Uislamu, lakini Mtume **[s.a.w.w]** hakufanya hivyo.

Aya ya Nne: Nabii Isa [a.s] alimuomba Mola wake amteremshie chakula kutoka mbinguni na aifanye siku ya kushuka chakula hicho kuwa ni sikukuu kwake yeye Nabii Isa [a.s] na wafuasi wake.

Ikimnukuu Nabii Isa [a.s], Qur'an Tukufu inasema: "Ewe Mola wetu tuteremshie chakula kutoka mbinguni kiwe ni sikukuu kwa ajili ya wa mwanzo wetu (nao ni sisi) na wa mwisho wetu na kiwe ni ishara itokayo kwako na uturuzuku kwani wewe ndiye mbora wa wanaoruzuku".[2] Basi je ndugu msomaji, unafikiria kwamba dhati ya Mtume Muhammad **[s.a.w.w]** ilikuwa na daraja ya chini kuliko kile chakula ambacho Nabii Isa [a.s] aliifanya siku ya kushuka kwake kuwa ni sikukuu? Ikiwa siku hiyo imefanywa kuwa ni sikukuu kwa sababu ya kuwa chakula hicho ni alama na ishara za Mwenyezi Mungu na muujiza uliotoka mbinguni, basi je hakuwa Nabii wa Uislamu ni alama na ishara kubwa itokayo kwa Mwenyezi Mungu na ni muujiza wa milele? Basi ole wao na wameangamia wale wanaokubali

1. Qur'an, 11 0:3.
2. Qur'an, 5.114.

kuifanya sikukuu siku kiliposhuka chakula hicho toka mbinguni (ambacho hakikuwa na athari isipokuwa kushibisha matumbo yenye njaa) lakini watu hao hao wanaipuuza siku iliyoshuka Qur'an kwa Mtume **[s.a.w.w]**, na pia wanaipuuza siku tukufu aliyotumwa Mtume **[s.a.w.w]** na zaidi ya kupuuza kwao wanaona kuwa kuadhimisha siku hiyo ni uzushi na ni haramu.

Aya ya Tano: Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na tumeutukuza utajo wako".[1] Hakika kufanya vikao na maadhimisho, ni miongoni mwa kutukuza utajo (wa Mtume **[s.a.w.w]**) na Waislamu wanapoadhimisha uzawa wa Mtume **[s.a.w.w]** na siku ya kumbukumbu ya kupewa kwake utume pamoja na maadhimisho mengine ya kidini hakuna kitu kingine wanachokikusudia isipokuwa kutukuza utajo wa Mtume **[s.a.w.w]** na watu watukufu wa nyumbani kwake. (Amani ya Mwenyezi Mungu iwashukie). Basi je ni kwa nini hatufuati muongozo wa Qur'an? Je, Qur'an siyo muongozo wetu na kigizo chetu tunachotakiwa kufuata? Kwa hiyo basi, haifai kabisa kwa mtu yeyote kusema kwamba: "Kuutukuza utajo wa Mtume **[s.a.w.w]** ni jambo linalomhusu Mwenyezi Mungu tu na kwamba mwingine hahusiki". Kwani kusema namna hii ni kama kusema kwamba kumsaidia Mtume **[s.a.w.w]** kunamhusu Mwenyezi Mungu peke yake wala haifai kwa yeyote miongoni mwa Waislamu kumsaidia Mtume **[s.a.w.w]** kwa sababu Mwenyezi Mungu amesema: "Na akusaidie Mwenyezi Mungu kwa msaada wenye nguvu." Qur'an, 68:3

Kwa hakika lengo la aya kama hizi ni kuwataka Waislamu wamsaidie Mtume **[s.a.w.w]** na kudumisha utajo wa (sifa zake) na kulihuusha jina lake na sera zake.

## MANENO NA MATENDO VA MAWAHABI YANAPINGANA

Ajabu waliyonayo Mawahabi ni kama ifuatavyo: Ni vipi wanaharamisha hafla ya utajo na uzawa mtukufu wa Mtume **[s.a.w.w]**, Mtume ambaye ndiye aliyewapa wanaadamu wote zawadi kubwa kuliko zote tena ya kudumu (nayo ni Uislamu) na tena Mawahabi kwao wao wanaona kumheshimu Mtume **[s.a.w.w]** na kuadhimisha uzawa wake ni shirki, lakini wao hao hao ndiyo wanaofanya maadhimisho makubwa kwa ajili ya watu wao na viongozi wao, na wanatoa mamilioni ya Riali (pesa za Kisaudia) ili kufanya maadhimisho haya na ili kuonyesha heshima kwa utumishi wa hao viongozi wao? Hebu litazame toleo la 102 la jarida la Al-Faisal, (Jarida ambalo uchapishwaji wake ni wa hali ya juu na wa pekee nchini Saudi Arabia) limekusanya kwa urefu maelezo yanayohusu maadhimisho (yao) makubwa ambayo yalifanywa na utawala wa mabavu wa Wasaudiyya kuadhimisha kurejea kwa "Amiri Sul-taan" kutoka katika safari ya anga ndani ya rocket iitwayo "Discovery".

Toleo hili pia limekusanya picha nyingi zinazoonyesha gharama kubwa zilizotumika katika sherehe hizo na limechapisha hotuba na nyimbo zilizoimbwa katika sherehe hizo, isitoshe (limechapisha) sifa zilizosomwa kwenye maadhimisho hayo kuwasifu wafalme wa kizazi cha Saudi kwa jumla na kwa amiri kwake pekee, sifa ambazo zilikuwa ni za kuvuka mipaka mno. Ewe msomaji, nakuapia kwa Mwenyezi Mungu kwamba, hivi kweli Amiri (wa Kisaudiya) ambaye hakufanya chochote katika safari hiyo

1. Qur'an, 94:4.

isipokuwa aliwafuata wageni wa kimagharibi kwenda hiyo safari ya anga za juu ambayo iliandaliwa na Wamarekani, anastahiki kuheshimiwa na kutukuzwa na kutolewa mali nyingi na kupiga mizinga bila faida yoyote?

Na eti asistahiki heshima na utukufu huo Mtume **[s.a.w.w]** ambaye amewakusanya watu katika ukamilifu wa kiroho na amewatoa watu kwenye giza na kuwapelekea kwenye nuru na akawaonyesha ubora wa utu wao na akawaepusha na kila aina za unyonge na upotevu. Hivi kweli haistahiki kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** kudumishwa utajo Mtukufu wa kuzaliwa kwake na kutajwa katika kuadhimisha uzao huo, sifa zake na kazi zake alizozifanya, ikiwemo utumishi wake kwa umma wake na jihadi alizopigana na ukarimu wa Mtume **[s.a.w.w]** na mengineyo, ili tu kizazi kijacho kifahamu kuwepo na kuendelea kwa matendo na kazi za Nabii huyu Mtukufu? Pia kizazi hicho kijacho kiweze kufahamu namna mbali mbali za matatizo yaliyomkuta Bwana Mtume **[s.a.w.w]** na jinsi alivyoyakabili akiwa na lengo la kuwaongoa watu. Na hayafanywi maadhimisho haya na heshima hizi pamoja na kueneza msimamo bora wa Mtume **[s.a.w.w]** isipokuwa ni kwa lengo Ia kuhimiza kumuiga na kumfuata Mtume **[s.a.w.w]** na kuhifadhi kumbukumbu zake.

Basi ni kwa nini isifae kumsifu Mtume **[s.a.w.w]** na kusomwa qasida zinazohusu ubora na utukufu wake, ila eti ifae kukisifu kizazi cha Wasaudiya na maamiri waovu ambao si chochote bali ni madhara na balaa kwa jamii na umma? Ni kwa kiasi gani basi maneno na matendo ya Mawahabi yanapingana? Kwa nini Mawahabi wanazuwia kufanyika kwa maadhimisho ya kuzaliwa Mtume Mtukufu kwa hoja ya kuwa eti jambo hili halikuja katika sheria ya Kiislamu, lakim wao hao hao wanafanya sherehe kubwa kwa ajili ya watu wao wa Kisiasa? Mwenyezi Mungu anasema:

وَإِذَا لَقُوا الَّذِينَ آمَنُوا قَالُوا آمَنَّا وَإِذَا خَلَوْا إِلَىٰ شَيَاطِينِهِمْ قَالُوا إِنَّا مَعَكُمْ إِنَّمَا نَحْنُ مُسْتَهْزِئُونَ
﴿١٤﴾ اللَّـهُ يَسْتَهْزِئُ بِهِمْ وَيَمُدُّهُمْ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١٥﴾

"Wanapokutana na walioamini husema: "Tumeamini' na wanapokuwa peke yao kwa mashetani wao husema: "Hakika sisi tu pamoja nanyi tunawacheza shere tu, Mwenyezi Mungu atawalipa shere yao na kuwaacha katika upotofu wao wakitangatanga ovyo". (Qur'an, 2:14-15).

Bila shaka waislamu tangu hapo zamani wamekuwa wakifanya sherehe za kuzaliwa Mtume **[s.a.w.w]**: Anasema "Ad-diyar Bakri" "Waislamu wanaendelea kufanya sherehe katika mwezi aliozaliwa Mtume **[s.a.w.w]** na kupika vyakula pamoja na kutoa sadaka katika siku za mwezi huo, pia hufurahi na wanafanya kheri nyingi na kusoma Maulidi ya Mtume **[s.a.w.w]** na huonekana mambo mengi mazuri kwao kutokana na ukarimu wa (Mwezi huu).[1]

1. Tarikh Al-Khamis, juz. 1, uk 223.

11

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## KUTABARUKU KWA ATHARI ZA MAWALLI WA MWENYEZI MUNGU NA KUOMBA UPONYO

Mawahabi wanaitikadi kwamba kutaka baraka kwenye Athari za Mawalii wa Mwenyezi Mungu ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu. Mawahabi pia wanamuona kuwa ni mshirkina mtu ambaye ataibusu mihrabu ya Mtume **[s.a.w.w]** na mimbari yake, japo hatafanya hivyo kwa nia ya ibada, isipokuwa ni kwa ajili tu ya mapenzi yake kwa Mtume **[s.a.w.w]** ndiyo maana katabaruku na kutaka uponyo kwenye Athari zake. Kukataza kutabaruku kwa athari za Mtume **[s.a.w.w]** na kulibusu kaburi lake na mimbari yake tukufu ni katika mambo ambayo Mawahabi wametilia nguvu kuyapinga dhidi ya Waislamu, na wamekuwa wakitumia makundi ya askari wa kigaidi waliopewa jina la waamrishaji mema na kukataza maovu, na wamewasambaza (askari) hao katika Msikiti wa Mtume **[s.a.w.w]** ili wazuwiye kulibusu kaburi lake tukufu na mimbari yake tukufu, pamoja na mihrab ya Msikiti wa Mtume **[s.a.w.w]**. Mawahabi hawa wanawahujumu mahujaji hapo Madina kwa kila aina ya mateso na kuwazuwiya kutabaruku na kulibusu kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** na utawaona kila mara wameshika fimbo, na mikononi mwao mna nyaya ngumu tayari kumshambulia kila Hujaj atakayethubutu kutabaruku au kulibusu kaburi la Mtume **[s.a.w.w]**. Na kutokana na hali hii basi, mara kwa mara wamekuwa wakimwaga damu za mahujaji wasio na makosa na kuudhalilisha utu wao katika Msikiti wa Mtume **[s.a.w.w]**, kwa madai kwamba kutabaruku na kulibusu kaburi ni kumuabudu huyo aliyezikwa hapo.

Kwa hakika watu hawa hawaujuwi Uislamu, na wamekosea kufahamu maana ya Ibada na Maf-humu yake, na kwa sababu hii basi wamepotea njia na wanatangatanga ndani ya upotevu. Wamekuwa wanaona eti kila anapoheshimiwa mtu aliyekwisha kufa ni kumuabudu mtu huyo, pamoja na kufahamu kwamba kubusu kaburi tukufu na kutabaruku kwa athari za Utume siyo kwa ajili nyingine isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu, kwa kuwa Waislami hawamtukuzi Mtume Mtukufu wala hawatabaruku kwa athari zake ila ni kwa kuwa yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na ni Nabii wake mteule ambaye Mwenyezi Mungu amemtukuza kuliko Manabii wote na viumbe wote. Basi na ifahamike kwamba kila wanapoheshimiwa na kutukuzwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu tendo hilo (kwa asili) ni kumtukuza Mwenyezi Mungu. Na hauthibitiki ukweli wa Tauhidi ila pale kila kitu kitakapotendwa kiwe ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na katika njia yake, na hapo ndipo itakapokuwa kila kitu kinaanzia kwa Mwenyezi Mungu na kila kitu kinaishia kwake.

Tutazungumzia maana ya Ibada katika sehemu ifuatayo kwa undani, ama sasa hivi utafiti wetu utahusu kutabaruku kwa athari za Mawalii, na utafiti huu tutalazimika kuulekeza kwenye kipimo cha Qur'an na Sunna ya Mtume **[s.a.w.w]** ili haki iweze kubainika.

## MTAZAMO WA QUR'AN JUU YA KUTABARUKU

Katika Qur'an tunatosheka na aya moja tu, nayo ni ile inayomnukuu Nabii Yusuf [a.s] akisema: "Nendeni na kanzu yangu hii mukaiweke usoni kwa baba yangu (macho yake yatarudi) ataona". Qur'an, 12.93. Nabii Yusuf aliituma kanzu yake kwenda kwa baba yake na akawaambia ndugu zake "Nendeni na kanzu yangu hii na muiweke usoni kwa baba yangu ili macho yake yarudi apate kuona. Mwenyezi Mungu anasema: "Na alipokuja mtoaji habari njema, aliiweka kanzu ile usoni kwake na macho yalirudi akaona". Qur'an, 12:96. Aya hii iko wazi kutoa ruhusa ya kutabaruku kwa athari za Manabii na Mawalii kiasi kwamba hata Nabii anatabaruku kwa Nabii mwenziwe kama hivi Nabii Yaqub [a.s] anatabaruku kwa kanzu ya Nabii Yusuf [a.s].

Na ni wazi kabisa kwamba kuponya kunatoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na yeye ndiye mtendaji halisi, isipokuwa kutabaruku kwa kanzu ya Nabii kumekuwa ni wasila wa kuponya kama tunavyotumia dawa kuwa ni wasila wa kupona kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ewe msomaji ingekuwaje kama kutabaruku kwa Nabii Yaqub kwa kanzu ya mwanawe Yusuf kungelitokea mbele ya watu wa Najdi na wafuasi wa Muhammad Ibn Abdul-Wahab, wangelihukumu namna gani jambo hili? Je, wangehukumu kuwa ni kafiri au mshirikina au mwenye dhambi? Wakati yeye ni Nabii na ni maasum? Kutabaruku kwa Waislamu kwenye kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** na makaburi ya watu wa nyumba yake na pia athari zao hakuna tofauti na kutabaruku alikotabaruku Nabii Yaqub [a.s] kwa kanzu ya mwanawe Yusuf [a.s].

## KUTABARUKU NA SERA YA WAISLAMU

Mtazamo wa haraka katika sera ya Waislamu kuanzia kwa Masahaba mpaka leo, unatuonyesha wazi sunna inayofuatwa kuhusu kutabaruku kwa Mtume **[s.a.w.w]** yeye mwenyewe na athari zake tukufu katika kpindi chote cha historia ya Uislamu. Na katika maelezo yafuatayo tutaeleza mifano michache inayohusu kutabaruku:

1. Bibi Fatma Az-Zahra ambaye ndiye mwanamke bora ulimwenguni na ni binti ya Mtume **[s.a.w.w]**, alifika kwenye kaburi la baba yake na akachukua gao Ia udongo wa kaburi akawa anaunusa na kulia huku akisema: "Mtu aliyenusa udongo wa kaburi la Ahmad, halaumiwi iwapo hatanusa mafuta mazuri ya ghaliya." Yamenipata milele masaibu ambayo lau yangeliupata mchana ungegeuka na kuwa usiku. Wameitaja Qadhiya hii wanahistoria wengi miongoni mwao ni As-Samhudi.[1] Kwa hakika kitendo hiki cha Bibi Fatma Az-Zahra ambaye ni maasum kinajulisha kwamba kutabaruku kwenye kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** ni jambo linalofaa na pia kutabaruku kwa udongo wa kaburi lake.

2. Bilal ambaye alikuwa ni muadhini wa Mtume **[s.a.w.w]** alipata kuishi Shamu katika kipindi cha utawala wa Omar Ibn Khattab. Siku moja alimuona Mtume **[s.a.w.w]** katika ndoto anamwambia:

"Ewe Bilal mbona umenitupa kiasi hiki, je haujakufikia wakati wa kunizuru ewe Bilal?" Basi Bilal alizindukana usingizini akiwa na huzuni na

1. (1) Wafaul-wafa cha As-samhudi, juz. 2, uk. 444 (2) Sul-hul-ikh-wan cha Al-Khalidi, uk. 57 na wengine.

khofu nyingi na alipanda kipando chake kuelekea Madina na akafika kwenye kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** akawa analia pale kaburini huku anausugua uso wake kwenye kaburi, mara Hasan [a.s] na Husein [a.s] wakafika, Bilal akawakumbatia na kuwabusu....[1]

3. Ibn Hajar anasema: "Kila mtoto aliyezaliwa katika zama za uhai wa Mtume **[s.a.w.w]** huhukumiwa kwamba alimuona Mtume **[s.a.w.w]**, na hii ni kwa sababu Ansar wote walikuwa wakiwaleta watoto wao kwa Mtume **[s.a.w.w]** kwa ajili ya Tahnik[2] na kupata baraka kiasi kwamba imesemwa kuwa: Wakati Makka ilipotekwa na (Waislamu), watu wa Makka wakawa wanakuja kwa Mtume **[s.a.w.w]** wakiwa na watoto wao ili awaguse vichwa vyao na awaombee baraka".[3] Na kuhusu jambo la kutabaruku, mwandishi wa kitabu kiitwacho, "Tabar-rukus Sahabah" amesema: "Hapana shaka kwamba athari za Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (ambaye ni) mbora kuliko viumbe wote na mbora kuliko mitume wote, kuwepo kwake ni jambo lenye kuthibiti na ni mashuhuri mno. Basi kwa hiyo athari hizo ndiyo bora kutabaruku kwazo, na idadi kubwa ya Masahaba wameziona na wakaafikiana kutabaruku kwazo na kuzipa umuhimu wa kuzikusanya nao Masahaba ndiyo watu waongofu na ni kiigizo kizuri, kwani walitabaruku kwa nywele zake na maji aliyotawadhia na jasho lake na nguo zake na pia kuugusa mwili wake na mengineyo yanayofahamika katika athari zake tukufu ambazo zimesihi khabari zake toka kwa watu wema.[4] Yanatosheleza maelezo aliyoyataja Muslim katika Sahih yake kuhusu kutabaruku aliposema: "Hakika Mtume **[s.a.w.w]** alikuwa akiletewa watoto naye huwafanyia tahnik.[5]

4. Masahaba walikuwa wakitabaruku kwa maji ya udhu aliyotawadha na aliyokoga Mtume **[s.a.w.w]**: Bukhari amopokea hadithi isemayo: "Mtume **[s.a.w.w]** alitutokea katika kipindi cha jua kali, akaletewa maji ya kutawadha na akatawadha, basi watu wakawa wanachukua maji ya udhu atawadhayo Mtume **[s.a.w.w]** wanajipangusia".[6] Kuhusu jambo hilo kuna riwaya nyingi zilizojaa katika vitabu vya hadithi.

5. Masahaba walikuwa wakitabaruku kwa nywele za Mtume **[s.a.w.w]** kama alivyopokea Anas kwamba: "Mtume **[s.a.w.w]** aliponyoa kichwa chake, Abu Tal-ha alikuwa ni mtu wa kwanza kuchukuwa nywele za Mtume **[s.a.w.w]**.[7] Anas anaposema "Abu Tal-ha ndiyo mtu wa kwanza kuchukua nywele za Mtume **[s.a.w.w]**" inaonyesha wazi kuwa Masahaba walishindana katika kutabaruku kwa nywele za Mtume **[s.a.w.w]** lakini Abu Tal-ha alikuwa wa kwanza kuzichukua. Na imepokewa tena kwamba: "Mtume **[s.a.w.w]** alifika Mina akaenda kwenye Jamrah akalipiga, kisha akaenda kwenye makazi yake hapo Mina, kisha akamwambia kinyozi, "ninyowe," na

---

1. Usudul-ghabah cha Ibnil Athir, juz. 1, uk. 28.
2. Tahnik: Maana yake ni kuweka asali kwenye dole gumba na kumrambisha mtoto ndani ya kinywa sehemu ya juu.
3. Al-Isabah, juz. 3, uk. 63.
4. Tabar-rukus Sahabah, uk. 5.
5. Sahih Muslim, juz. 3, uk 1691.
6. Sahih Bukhari, juz. 1, uk. 59, Fat-hul-bari, juz. 1, uk. 256.
7. Sahih Bukhari, juz. 1, uk. 54.

akaashiria upande wa kulia kisha kushoto kisha akaendelea kuwapa watu (nywele zake)".[1]

6. Masahaba vile vile walikuwa wakitabaruku kwa chombo alichokuwa amenyewea Mtume **[s.a.w.w]**: Abu Bar-da amesema: "Abdullah bin Salaam aliniambia, "Je, nisikunyweshe kwenye chombo alichonywea Mtume?"[2] Riwaya hii inaonyesha kwamba, Abdallah bin Salaam alikuwa amekihifadhi chombo hicho kwa kuwa kilikuwa kimepata baraka kwa sababu mjumbe wa Mwenyezi Mungu alinywea chombo hicho.

7. Pia Masahaba walikuwa wakitabaruku kwa mikono yake Mitukufu: "Imepokewa toka kwa Abu Juhaifah amesema, "Mtume alitoka katika siku yenye joto kali akaenda mpaka Bat-haa akatawadha kisha akaswali Adhuhuri rakaa mbili na Al-asr rakaa mbili.... watu wakasimama wakaishika mikono yake wakawa wanajipangusia nyuso zao. Anasema Abu Juhaifah, "Nikauchukua mkono wake nikauweka usoni kwangu, basi niliuona ubaridi mno kuliko theluji na una harufu nzuri kuliko miski".[3]

8. Pia wakitabaruku kwenye mimbari yake tukufu:

Imepokewa toka kwa Ibrahim bin Abdur-Rahman bin Abdil-Qari kwamba yeye alimuona Ibn Omar ameweka mkono wake kwenye Mimbar mahala ambapo Mtume **[s.a.w.w]** alikuwa akikaa, kisha akauweka nikono wake usoni kwake.[4]

9. Vile vile walikuwa wakitaka uponyo kwenye kaburi lake tukufu: Imepokewa toka kwa Imam Ali [a.s] kwamba yeye amesema, "Kuna bedui alikuja kwetu baada ya kuwa tumemzika Mtume **[s.a.w.w]** kiasi cha siku tatu zimepita, akajitupa kwenye kaburi Ia Mtume **[s.a.w.w]**, akajipaka kichwani udongo wa kaburi Ia Mtume **[s.a.w.w]** na akasema, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ulisema tukasikia usemi wako na uliyapokea toka kwa Mwenyezi Mungu, nasi tulipokea toka kwako na miongoni mwa yale ulioteremshiwa na Mwenyezi Mungu ilikuwa, lau wao watazidhulumu nafsi zao wangekujia... nami nimedhulumu (nafsi yangu) na nimekujia unitakie msamaha". Basi palisemwa kutoka kaburini "Hakika umesamehewa."[5] Kwa kifupi, iwapo mtu atavirjea vitabu vya historia (As-sihah na As-Sunan na Masanid) ataona ni jinsi gani Masahaba na Tabiina walivyokuwa wakitabaruku kwa kila kitu ambacho kinamafungamano na Mtume **[s.a.w.w]**, na walikuwa wakitaka kuponywa kwenye kaburi lake kwa kuweka mashavu yao juu ya kaburi na kuunusa udongo wa mahali hapo na kulia kwenye kaburi la Mtume **[s.a.w.w]**.

Zaidi ya hapo, walikuwa pia wakitabaruku kwa fimbo ya Mtume **[s.a.w.w]** na mavazi yake na kuswali sehemu alizokuwa akiswali au alimopita. Na masimulizi yanayozungumzia jambo la kutabaruku ni mengi mno na haiwezekani kwa mtu mwenye akili kusema eti masimulizi haya ni ya kutungwa tu. Basi yatakuwaje ni ya kutunga wakati Bukhari na Muslim pamoja na wanachuoni wengine wa hadithi wameyapokea? Isitoshe hali hii, bali wanachuoni wawili wakubwa wamesimamia ukusanyaji wa riwaya hizi

1. Sahih Muslim, juz. 3, uk. 947.
2. (1) Sahih Bukhari, juz. 7, uk. 147 (2) Fat-hul Bari, juz. 10, uk. 85.
3. Sahih Bukhari, juz. 4, uk. 188.
4. AI-tabaqatul-kubra, juz. 1, sehemu ya pili, uk. 13.
5. Kanzul-Ummal, juz. 2, uk. 248, Wafaul Wafa, juz. 2, uk. 1361.

na kuzifafanua pamoja na kutaja rejea zake. Wa kwanza ni, Al-Ustadh Sheikh Muhammad Tahir Makki katika kitabu chake kiitwacho "Tabar-rukus-Sahabah Bia'thari Rasulillah". Wa pili ni, Al-Ustadh Sheikh Ali Ahmadi katika kitabu chake madhubuti kiitwacho "At-Tabar-ruk". Yeye amefafanua kwa undani habari zote zilizokuja kuhusu Tabar-ruk; na kitabu hiki kinahesabiwa kuwa bora cha zama hizi. Basi watasemaje Mawahabi juu ya hadithi hizi ambazo ni mutawatiri kimatamko na kimaana? Na ni upi msimamo wao kutokana na ukweli huu ulio wazi?

Basi ni za nini kelele hizi wazipigazo dhidi ya kutabaruku kwenye kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** jambo ambalo Masahaba na Tabiina wamekuwa wakilifanya bila ubaya wowote wala kulipinga au kuliharamisha, wakati hatuoni popote kwamba Mtume au Masahaba wake waliharamisha jambo hili. Na ni kwa nini Mawahabi hawawaachi Waislamu walibusu kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** na wapate baraka zake na waonyeshe hisiya zao na mapenzi yao kwa Mtume **[s.a.w.w]**? Je, Mawahabi hawajuwi kuwa, kukataza kutabaruku kwenye kaburi la Mtume na athari zake ilikuwa tabia na kazi ya Bani Ummayya hasa Mar-wani aliyelaaniwa na Mtume **[s.a.w.w]**? Hebu soma mapokezi aliyoyapokea Al-Hakim ndani ya Mustad-rak yake kutoka kwa Dawuud bin Salih amesema: "Sika moja Mar-wan alikuja akamkuta mtu ameweka uso wake juu ya kaburi (la Mtume **[s.a.w.w]**) akamshika shingoni kisha akamwambia, "Je unafahamu unachokifanya"? Kumbe mtu yule alikuwa Abu Ayyubul-Ansari, akamjibu, "Ndiyo mimi sikulijia jiwe hapa nimemjia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu". Nimemsikia mjumbe wa Mwenyezi **[s.a.w.w]** akisema: "Msiililie dini (msiihuzunikie) kama watawala wake ni watu wanaostahiki lakini ililieni dini watakapoitawalia wasiostahiki".[1] Mar-hum Sheikh Al-Amini amesema:

"Hadithi hii inatufahamisha kwamba kuzuwiya kutawas-sal kwenye makaburi matakatifu ni miongoni mwa Bid'a za Banu Ummayya na upotevu wao tangu zama za Masahaba na hakuna hata sikio moja kabisa lililopata kumsikia Sahaba akipinga tawas-sul hiyo isipokuwa Mar-wan mdhalimu aliyetokana na kizazi cha Umayya". Ni kweli "Ng'ombe huilinda pua yake kwa pembe zake". Ni kweli pia kwamba "Kwa kisingizio cha kumtafuta njiwa, muwindaji hula tende (za shamba la mitende aliloingia). Ukweli ulivyo ni kwamba Banu Ummayya na hasa Mar-wan, wanayo chuki dhidi ya Mtume **[s.a.w.w]** tangu siku ile Mtume **[s.a.w.w]** alipokuwa hakubakisha heshima yoyote ya Banu Ummayya, ila aliivunja wala cheo chochote ila alikiharibu na wala nguzo yao yoyote isipokuwa aliivunja na hayo yametokea kutokana na maneno makali ya Mtume **[s.a.w.w]** kuhusu Bani Ummayya ile siku ya Badri alipowapiga. Mtume **[s.a.w.w]** hasemi lolote kwa matamanio ya nafsi yake ila ni wahyi aliyopewa (aliyemfundisha Bwana Mtume ndiye mwenye nguvu zote) kwani imepokewa hadithi sahihi kuwa Mtume **[s.a.w.w]** amesema, "Itakapofika idadi ya Banu Ummayya watu arobaini watawafanya waja wa Mwenyezi Mungu kuwa ni watumwa, na mali ya Mwenyezi Mungu wataipora na kuifanya knwa ni mali yao na watakitumia vibaya kitabu cha Mwenyezi Mungu".[2]

1. Mustad-rak Al-Hakim, juz. 4, uk. 515.
2. Al-Ghadir, juz. 5 uk. 129-130.

Umeona jibu la Abu Ayyubul-Ansari kwa Mar-wan pale alipomuuliza unafanya nini? Akawa amejibu, sikujia jiwe bali nimemjia mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Hapa tunamuona Abu Ayyubul-Ansari anaeleza kwamba: "Makusudio ya kutawas-sal na kutabaruku ni kwa Mtume **[s.a.w.w]** ambaye tunaitakidi kuwa hapana tofauti baina ya kuwa yu hai au amekufa katika suala hili, lakini udongo na jiwe havina umuhimu wowote, isipokuwa udongo na jiwe vilivyopo kwenye kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** vimepata heshima na utukufu kwa sababu ya Mtume **[s.a.w.w]**. Ewe msomaji mpendwa, Bukhari ambaye kitabu chake kinazingatiwa na Masunni kuwa ndiyo kitabu sahihi mno kuliko vingine, yeye ameweka mlango aliouita "Babu Ma-dhukira Min Dir-in-nabi wa asahu wa Saifahu wa qadahahu wa khatamahu wa mas-ta-amalal-khulafan baadahu. Yaani mlango unaozungumzia habari za deraya ya Mtume, panga lake na fimbo yake, kikombe chake, pete yake na vitu walivyovitumia makhalifa waliokuja baada yake katika vitu ambavyo havikugawanywa na nywele zake, na viatu vyake na vyombo vyake ambavyo Masahaba wa Mtume na wengineo walikuwa wakitabaruku kwa vitu hivyo baada ya kufa Mtume **[s.a.w.w]**.[1]

Kama Mawahabi watazifuatilia hadithi hizi nyingi zaidi ya mia hawatakuwa na njia isipokuwa kukubali ukweli na kukiri iwapo tu watakuwa miongoni mwa wale wanaosikiliza maneno na kufuata yaliyo bora, vinginevyo: "Siku ya Hukumu imewekewa wakati maalum".

### TAUHIDI KATIKA IBADA

Msingi wa wito wa Manabii [a.s] siku zote umekuwa ni kulingania kumuabudu Mwenyezi Mungu peke yake na siyo kumuabudu mwingine peke yake, au kumshirikisha na Mwenyezi Mungu. Na msingi wa hukmu za mbinguni tangu mwanzo wa kutumwa ujumbe wa Manabii ilikuwa ni kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kukata mizizi ya shirki. Ukweli halisi ulivyo ni kwamba, lengo la kutumwa kwa Manabii ni kulingania (watu) kwenye ibada ya Mwenyezi Mungu peke yake, na kupiga vita ushirikina wa aina zote na khususan kupinga shirki katika ibada. Qur'an Tukufu inaashiria ukweli huu wazi wazi na inasema:

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّـهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ ﴿٣٦﴾

"Na bila shaka tulimpeleka Mjumbe kwa kila umma (akawambie umma wake) muabuduni Mwenyezi Mungu na muyaepuke masanamu. (Qur'an, 16:36)

وَمَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَـٰهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ ﴿٢٥﴾

Na hatukumtuma kabla yako Mjumbe yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hakuna apasiwaye kuabudiwa ila mimi, basi niabuduni." (Qur'an, 21:25) Qur'an imeizingatia ibada ya Mwenyezi Mungu kuwa ni jambo linalokusanya na kushirikisha sheria zote za mbinguni na inasema:

قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْا إِلَىٰ كَلِمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَّا نَعْبُدَ إِلَّا اللَّـهَ وَلَا نُشْرِكَ بِهِ شَيْئًا ﴿٦٤﴾

1. Sahih Bukhari, juz. 4, uk. 82, kilichochapishwa mwaka 1314 A.H.

"Waambie, Enyi mliopewa Kitabu cha Mwenyezi Mungu njooni katika neno lililo sawa baina yetu na baina yenu, ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu na wala tusimshirikishe na chochote." (Qur 'an, 3:64)

Tauhidi katika ibada ni msingi imara kwa Waislamu wote, na hapana yeyote aipingaye Tauhidi au kuwa na tofauti ndani yake miongoni mwa vikundi vyote vya Kiislamu, ijapokuwa Mutazilah mtazamo wao juu ya Tauhid ya matendo ya Mwenyezi Mungu unatofauti, na vile vile Ashaira nao wanayo tofauti juu ya Tauhid katika sifa za Mwenyezi Mungu, lakini madhehebu zote za Kiislamu zinaafikiana kuhusu Tauhid ndani ya ibada na hakuna nafasi ya kupinga hilo. Kama kutakuwa na khitilafu, basi ikhtilafu hiyo haiko katika msingi wa Tauhidi ya ibada bali iko katika Misdaaq za Tauhidi ya Ibada. Hii inamaanisha kwamba, baadhi ya Waislamu wanaona kuwa baadhi ya matendo ni ibada na Waislamu wengine wanaona kuwa (matendo hayo) ni Takrima na Taadhima tu na siyo ibada. Na kwa mujibu wa Istilahi ya Elimu ya "Mantik" Tofauti kama hii iko ndani ya 'As-Sughraa" ambayo ni Je, kitendo hiki ni ibada au hapana? Wakati ambapo hakuna tofauti katika 'Al-Kubraa" ambayo ni je, inafaa kumuabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu au hapana? Na hii wameafikiana (Waislamu wote) kwamba haijuzu kumuabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu.

Kwa maneno mengine (Tunaweza kusema) tofauti iliyopo inatokana na Mawahabi kuyazingatia matendo fulani kuwa ni ibada wakati ambapo wasiokuwa wao miongoni mwa Waislamu ulimwenguni kote hawayazingatii kamwe matendo hayo kuwa ni ibada. Hapana budi tuifafanue maana ya "Ibada" kwa mujibu wa lugha na vile vile kwa mjibu wa Qur'an, na hapo ndipo yatakapofahamika matawi ambayo ndani yake imekuja tofauti kuyahusu mwenyewe kwa dhati yake, na ndipo utakapotudhihirikia uhakika na ukweli wa ibada.

## TAARIFU KAMILI YA MAANA YA IBADA

Bila shaka maana na Maf-humu ya Ibada iko wazi katika lugha ya Kiarabu, na lau tutakwa hatuwezi kuiarifisha "Ibada" kwa Taarifu ya kimantik kwa kutumia neon moja, basi ni kama mbingu na ardhi ambazo zina maana mbili zilizowazi, wakati ambapo wengi katika sisi hawawezi kutoa taarifu kamili kwa kutumia neon moja lakini hali hii haizuwii kujengeka maana ya ardhi na mbingu katika akili zetu tunapoyasikia matamko hayo. Bila shaka basi, maana ya Ibada ni kama maana ya ardhi na mbingu ambayo inafahamika kwetu sote, pamoja na kutokuweza kuziarifisha mbingu na ardhi kwa taarifu ya kimantiki: Kwa hiyo basi "Ibada" na "Kutukuza" na "Kuheshimu" na "Kukirimu" ni matamko mbali mbali yenye matawi yanayofahamika, na kuyachambua ni jambo rahisi tena jepesi.

Kwa hakika mtu ambaye anampenda yeyote yule kwa mapenzi ya kweli kabisa, utamuona akibusu kutaza nyumba ya mpenzi wake na kunusa mavazi yake na kuyakumbatia kifuani, na atapokufa (mpenzi wake huyu) atalibusu kaburi lake na udongo wa kaburi hilo.... Pamoja na matendo yote haya, hapana yeyote atakayeona kuwa matendo yake huyu mwenye kupenda ni ibada amfanyiayo yule mpenzi wake. Hali hii ni kama ile ya watu kukimbilia kwena kuona miili ya viongozi iliyomo ndani ya majeneza, au kuona kumbukumbu zao na majumba walioyokuwa wakiishi na kusimama

dakika chache kuonyesha huzuni kwa ajili ya rohozao yote haya hayazingatiwi kuwa ni ibada katika Taifa lolote miongoni mwa mataifa ulimwenguni, japokuwa mapenzi yao na unyenyekevu wao kwa wato hao uko katika kiwango cha unyenyekevu wa waumini kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hivyo basi, watu wenye maarifa na wachambuzi wa mambo ndiyo ambao wanaweza kupambanua baina ya kuheshimu na ibada. Ewe msomaji mtukufu iwapo tutataka kutoa taarifu ya ibada kimantik, basi ibada itakuwa na taarifu za aina tatu na zote hizi zitalenga maana moja. Ama Mawahabi wao wamechagua Taarifu mbili nyingine na wakazitegemea, lakini zinaupungufu hazikukamilika. Katika maelezo yafuatayo tunazileta hizo Taarifu zao ili tuzijadili.

## TAARIFU MBILI PUNGUFU KUHUSU IBADA

Ibada ni kunyenyekea na kudhalilika. Ndani ya vitabu vya lugha Taarifu ya ibada imekuja kwa maana ya kunyenyekea na kudhalilika. Na maana hii imekuja katika Qur'an tukufu lakini Taarifu hii ya Ibada haitoi maana ya ibada kwa undani, na hiyo ni kwa sababu zifuatazo: Ikiwa ibada inakubaliana katika maana na kuwa ni kunyenyekea na kudhalilika, basi haitawezekana kwa mtu yeyote kumzingatia kuwa anampwekesha Mwenyezi Mungu, kwani mtu kwa maumbile yake humnyenyekea Mwalimu wake na mtoto naye huwanyenyekea wazazi wake wawili na kila mpenzi kwa ampendaye. Bila shaka Qur'an Takufu inamuamuru mtu adhalilike kwa wazazi wawili inasema:

وَاخْفِضْ لَهُمَا جَنَاحَ الذُّلِّ مِنَ الرَّحْمَةِ وَقُل رَّبِّ ارْحَمْهُمَا كَمَا رَبَّيَانِي صَغِيرًا ﴿٢٤﴾

"Na wainamishie Bawa Ia udhalili kwa kuwaonea huruma na useme, Mola wangu wahurumie (wazazi) wangu kama walivyonihurumia mimi nilipokuwa mdogo". (Qur'an, 17:24)

Basi iwapo unyenyekevu na udhalili maana yake ni kumfanyia ibada uliyemdhalilikia, basi italazimu kumhukumu ukafiri yeyote anayelea wazazi wake wawili na kinyume chake itakuwa ni lazima kumhukumu kuwa ni mtu wa Tauhidi yule anayewatelekeza wazazi wake na kutowafanyia wema. B: Ibada ni ukomo wa kunyenyekea. Baadhi ya wafasiri walijaribu kuitengeneza na kuirekesbisha Taarifu ya ibada ya kilugha pale walipogundua kuwa inaupungufu wakasema:

"Ibada ni ukomo wa kunyenyekea kwa yule ambaye utukufu wake na ukamilifu wake unafahamika." Taarifu hii inashirikiana na ile ya kwanza katika upungufu na utata. Mwenyezi Mungu anawaamuru Malaika wamsujudie Adam anasema:

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ أَبَىٰ وَاسْتَكْبَرَ وَكَانَ مِنَ الْكَافِرِينَ ﴿٣٤﴾

"Na kumbuka tulipowaambia Malaika, msujudieni Adam, wakasujudu wote isipokuwa Iblisi". Qur'an, 2:34

Bila shaka kusujudu ndiyo ukomo wa kadhalilika na kunyenyekea kwa yule unayemsujudia, basi ikiwa maana ya ibada ni ukomo wa kunyenyekea italazimu kuwakufurisha Malaika waliotekeleza amri ya Mwenyezi Mungu, na Iblisi kwa kupinga kwake amri ya Mwenyezi Mungu atakuwa ndiyo mwenye imani. Hakika ndugu wa Nabii Yusuf na wazazi wake Nabii Yusuf wote walimsujudia Yusuf kama asemavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَرَفَعَ أَبَوَيْهِ عَلَى الْعَرْشِ وَخَرُّوا لَهُ سُجَّدًا ۖ وَقَالَ يَا أَبَتِ هَٰذَا تَأْوِيلُ رُؤْيَايَ مِن قَبْلُ قَدْ جَعَلَهَا رَبِّي حَقًّا ﴿١٠٠﴾

"Na waliporomoka wote kumsujudia, (Naye Yusuf) akasema: Ewe Baba yangu hii ndiyo Tafsiri ya ndoto yangu ya zamani bila shaka Mwenyezi Mungu ameithibitisha". Qur'an, 12:100

Ndoto aliyoiashiria Nabii Yusuf katika Aya hii, hi ile iliyoko katika kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema:

إِذْ قَالَ يُوسُفُ لِأَبِيهِ يَا أَبَتِ إِنِّي رَأَيْتُ أَحَدَ عَشَرَ كَوْكَبًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ رَأَيْتُهُمْ لِي سَاجِدِينَ ﴿٤﴾

"(Kumbuka) Yusuf aliopomwambia Baba yake, Ewe baba yangu hakika nimeona (ndotoni) nyota kumi na moja na jua na mwezi vinanisujudia" (Qur'an, 12:4)

Ni hakika (isiyopingika) kwamba Waislamu wote kwa kufuata mwendo wa Mtume **[s.a.w.w]** huwa wanalibusu "Hajarul-As-wad". Jiwe jensi lililoko kwenye kona ya Kaaba Tukufu na pia hutaka baraka kwenye jiwe hilo. Kitendo kile kile hufanywa na waabuduo sanamu kwenye masanamu yao jambo ambalo moja kwa moja ni shirki, lakini tendo la Waislamu kwenye Hajarul-As-wad ni tendo la Tauhidi bila shaka yoyote. Kwa hiyo, maana ya ibada siyo ukomo wa kunyenyekea na kudhalilika ingawaje (kunyenyekea na kudhalilika) hakika ni miongoni mwa nguzo za Ibada lakini siyo kwamba hizo ndiyo nguzo pekee za ibada. Hivyo basi, hapana budi pasemwe kuwa, Ibada maana yake ni kunyenyekea na kudhalilika kunakoambatanishwa na itikadi maalum, kitu ambacho kitaifanya ibada iwe imeundika katika misingi miwili.

1. Kunyenyekea na kudhalilika.
2. Itikadi maalum.

Na hii itikadi maalum ndiyo ambayo inaweka msimamo wa kufafanua Qadhiya ya ibada, kwani kunyenyekea japo si sana, ikiwa kutaambatanishwa na itikadi maalum, basi itakuwa ibada. Kwa hakika "Itikadi Maalum" ndiyo inayokivalisha kitendo vazi Ia Ibada, na bila itikadi hiyo maalum ibada haithibitiki japo itadhihirika katika hali ya Ibada.

Na sasa baada ya kuwa tumethibitisha ubatili wa Taarifu mbili ambazo Mawahabi wamezitegemea, na umedhihiri upungufu wake na udhaifu wake, umefika wakati wa kuzungumzia zile Taarifu tatu. Sasa suali ni je, ni nini hiyo "Itikadi maalum" ambayo inaitenganisha ibada na visivyokuwa ibada? Jawabu lake: Kwa hakika ukweli na usahihi, hapa ndipo mahali pa uchambuzi na uhakiki, na jawabu lake litaonekana ndani ya Taarifu tatu zifuatazo:

Taarifu ya Kwanza: Ibada ni kunyenyekea kimatendo au kimatamko, ambako kunatoka ndani ya itikadi ya mtu kwa ajili ya Uluhiyyah (Uungu). Nini maana ya Uluhiyyah nukta hii ni muhimu sana kwa hiyo ni lazima kuieleza.

Jibu: "Uluhiyyah" ni tamko litakanalo na neno "Al-Ilahu" na hilo neno "Al-Ilahu" ndiyo Allah kwa tamko la nakira, (naye ndiyo muumba mtukufu). Na ilivyokuwa neno "Al-llahu" hupata likafasiriwa kwa maana ya mwenye kuabudiwa, basi tafsiri hiyo hiyo ni tafsiri ya kulazimiana, yaani

Uluhiyyah unalazimu kuabudiwa siyo kwamba Ilahu maana yake ni mwenye kuabudiwa.

Bila shaka watu wanaoitakidi Ilahu vile vile wanaitakidi kuwepo ulazima wa kumuabudia, sawa sawa ikiwa ni Ilahu wa haki kama alivyo Mwenyezi Mungu au akawa siyo wa haki kama illvyo miungu isiyokuwa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo neno Al-Ilahu hufasiriwa kwa maana ya chenye kuabudiwa kutokana na hali hii tu basi. Dalili iliyowazi kuhusu taarifu hii ni Aya za Qur'an zilizokuja kuzungumzia nyanja hii. Katika mazingatio ndani ya aya hizo inatudhihirikia kwamba "Ibada" na matendo na maneno yanayotokana na Itikadi za Uungu, na kwamba Itikadi hii inapokosekana, basi maana ya Ibada haithibitiki, na ndiyo maana utaiona Qur'an wakati inapoamuru ibada ya Mwenyezi Mungu, basi haraka sana hutoa maelekezo kwamba, hapana mungu asiyekuwa Mwenyezi Mungu. Kwa mfano isema:

"Enyi watu wangu, muabuduni Mwenyezi Mungu ninyi hamna Mungu ila yeye." Madhumuni ya aya hii yamekuja katika sehemu tisa ndani ya Qur'an au zaidi, nawe msomaji mpendwa unaweza kuzirjea aya hizi katika Surat A'araf aya ya 65, 73 na 58. Pia Surat Huud aya ya 5, 61 na 84, vile vile Surat Anbiyyah aya ya 25, kadhalika Surat Muuminnuna aya ya 23 na 32 na Surat Taha aya ya 14. Ibada zote hizi zinajulisha kwamba, ibada ni kule kunyenyekea na kudhalilika kunakotokana na itikadi ya kuitakidi Uluhiyyah na bila itikadi hii tendo hilo halitaitwa Ibada. Hebu angalia aya zaidi zinazojulisha makusudio hayo. Anasema Mwenyezi Mungu:

إِنَّهُمْ كَانُوا إِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا إِلَـٰهَ إِلَّا اللَّـهُ يَسْتَكْبِرُونَ ﴿٣٥﴾

"Hakika wao walipokuwa wakiambiwa, hapana Mungu (Mwingine) ila Mwenyezi Mungu wao Hupinga." Qur'an, 37:35

Ni kwa nini walikuwa wakipinga? Ni kwa sababu wanaitakidi waungu wasio Mwenyezi Mungu na wanawaabudu. Na anasema Mwenyezi Mungu:

أَمْ لَهُمْ إِلَـٰهٌ غَيْرُ اللَّـهِ ۚ سُبْحَانَ اللَّـهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٤٣﴾

"Au wanaye Mungu mwingine asiye Mwenyezi Mungu, ametakasika Mwenyezi Mungu kutokana na hao washirikina hao wanaowashirikisha." Qur'an, 52:43.

Qur'an inawazingatia watu hawa kuwa ni washirikina kwa kuwa wanaitakidi uungu kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Anasema tena Mwenyezi Mungu:

الَّذِينَ يَجْعَلُونَ مَعَ اللَّـهِ إِلَـٰهًا آخَرَ ۚ فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ ﴿٩٦﴾

"Wale ambao wanafanya pamoja na Mwenyezi Mungu; Mungu Mwingine basi hivi karibuni watajua." Qur'an , 15:96

وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّـهِ إِلَـٰهًا آخَرَ ﴿٦٨﴾

"Na wale ambao hawamuombi mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu..... (Qur'an, 25:68).

Na miongoni mwa aya zinazojulisha kwamba maombi ya Washirikina yalikuwa yakiambatana na itikadi ya uungu kwa masanamu yao ni hizi zifuatazo:

وَاتَّخَذُوا مِن دُونِ اللَّـهِ آلِهَةً لِّيَكُونُوا لَهُمْ عِزًّا ﴿٨١﴾

"Waliwafanya waungu wengine badala ya Mwenyezi Mungu ili wawe wenye nguvu." Qur'an, 19:81.

"Je, ninyi mnashuhudia kwamba kuna waungu wengine pamoja na Mwenyezi Mungu." Qur'an, 6:19

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ آزَرَ أَتَتَّخِذُ أَصْنَامًا آلِهَةً إِنِّي أَرَاكَ وَقَوْمَكَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٧٤﴾

"Na (kumbukeni) Ibrahimu alipomwambia Baba yake Azar. 'Unawafanya Masanamu kuwa ni waungu.'" Qur'an, 6:74

Mazingatio katika aya zinazozungumzia shirki yawatu wanaoabudu sanamu yatatudhihirishia ukweli huu, nao ni kuwa ushirikina wa watu hawa umekuja kwa sababu ya kuitakidi kwao uungu wa masanamu yao waliyokuwa wakiyaabudu, na kwamba masanamu hayo ni miungu wadogo ambao Mungu mkubwa amewapa baadhi ya mambo yanayomstahiki, basi (masanamu hayo) yameumbwa na wakati huo huo yanaabudiwa. Na kwa ajili hii basi walikuwa wakiikataa Tauhidi. Qur'an inasema:

ذَٰلِكُم بِأَنَّهُ إِذَا دُعِيَ اللَّـهُ وَحْدَهُ كَفَرْتُمْ وَإِن يُشْرَكْ بِهِ تُؤْمِنُوا فَالْحُكْمُ لِلَّـهِ الْعَلِيِّ الْكَبِيرِ ﴿١٢﴾

"Hii ni kwa sababu mlikuwa akitajwa Mwenyezi Mungu peke yake mnakanusha, na akishirikishwa mnaamini, basi (leo) hukumu ni yake Mwenyezi Mungu Mtukufu aliye mkuu." Qur'an, 40:12

Na kwa ajili hii mfasiri mkubwa mar-hum Ayatullah Sheikh Muhammad Jawad Al-Balaghi ametoa Taarifu nzuri ya "Ibada" katika tafsiri yake madhubuti iitwayo Aalaur-Rahman anasema: "Ibada: Ni hisia ya unyenyekevu wanayoifanya kwa ajili ya yule wanayemfikiria kuwa ni Mungu wake ili atimize haki yake makususi ya uungu.[1]

Bila shaka marehemu Al-Balaghi ametoa mtazamo wake wa kielimu kutokana na ufahamu wa kimaumbile juu ya neno "Ibada" katika msingi wa tamko, ndipo ilipokuja Taarifu hii inayokubaliana na aya za Qur'an. Taarifu ya Pili ya Ibada: Hakika Ibada ni kunyenyekea mbele ya yule ambaye (Mwenye kunyenyekea) humzingatia kuwa ndiyo Rabbi (Mola). Na tunaweza kuiarifisha ibada kama ifuatavyo; Ibada ni kunyenyekea kimatendo au kimaneno kwa yule anayeitakidiwa kuwa Mola basi kuabudiwa kunalazimiana na kuwa Mola na ikiwa mtu atajiona yeye mwenyewe kuwa ni mja kwa yule anayemuitakidi kuwa ni Mola wake kwa kuumba; sawa sawa Mola huyo akiwa ni kwa hakika au hapana, na akamnyenyekea pamoja na itikadi hii basi atakuwa amemuabudia. Na katika Qur'an Tukufu kuna aya zinazofahamisha kuwa ibada ni miongoni mwa mambo ya umola yaani "Ar-rububiyyah". Hebu ziangalie baadhi ya hizo aya:

وَقَالَ الْمَسِيحُ يَا بَنِي إِسْرَائِيلَ اعْبُدُوا اللَّـهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ ﴿٧٢﴾

"Naye Masihi alisema, Enyi wana wa Israeli, mwabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu na Mola wenu". Qur'an, 5:72

إِنَّ اللَّـهَ رَبِّي وَرَبُّكُمْ فَاعْبُدُوهُ هَـٰذَا صِرَاطٌ مُّسْتَقِيمٌ ﴿٥١﴾

1. Tafsiri Alaul-Qur'an, juz. 1, uk 57.

"Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mola wangu na ni Mola wenu. Basi muabuduni hii ndiyo njia iliyonyooka" Qur'an 3.51

Na aya nyinginezo zaidi ya hizi. Na kuna aya nyingine zinazoizingatia Ibada kuwa ni miongoni mwa mambo ya muumba kama ilivyo katika kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema:

ذَٰلِكُمُ اللَّـهُ رَبُّكُمْ لَا إِلَـٰهَ إِلَّا هُوَ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ فَاعْبُدُوهُ ﴿١٠٢﴾

"Huyo ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu, hakuna anayeabudiwa kwa haki ila yeye muumba wa kila kitu, basi muabuduni." Qur'an 6:102

Ni maana ya neno (Ar-Rabbu)? Neno Rabbu hutumika katika lugha ya Kiarabu kwa yule aliyetegemezewa uangalizi wa kitu fulani na yakaachwa mikononi mwake matokeo au ukomo wa kitu hicho. Basi iwapo neno hili litatumika kwa mtu anayemiliki nyumba na au anayemiliki ngamia au mlezi wa mtoto na mkulima na wengineo, basi hiyo ni kwa sababu wanamiliki kuendesha kitu hicho na kusimamia majukumu yake. Nasi tunapomzingatia Mwenyezi Mungu kuwa ni "Ar- Rabbu" ni kwa sababu mambo yetu na mwisho wetu kama vile mauti, uhai, rizki, afya na uwekaji wa sheria pia msamaha na mambo mengineyo, yote yako mikononi mwake Mwenyezi Mungu Mtukufu. Sasa basi Iau kuna mtu ataitakidi kwamba, moja katika mambo haya au yote, Mwenyezi Mungu amempa mtu fulani (Ayasimamie), basi maana ya itikadi hii ni kwamba kumzingatia huyo mtu kuwa ni "Rabbu" na kumuamini Rabbi huyu na kumnyenyekea itakuwa ni kumuabudia. Kwa maneno mengine tunasema, "Bila shaka ibada inatokana na hisiya za mtu kujiona kuwa yeye ni mja (mtumwa) na hii ndiyo hakika ya ubudiyah, ni ni mtu kuizingatia nafsi yake kuwa amemilikiwa na yuko juu yake aliyemmiliki, kuwepo kwake na kifo chake na uhai na rizki yake na mengineyo. Au kwa uchache akamfanya huyo aliye juu yake kuwa ni mwenye kumiliki uwezo wa kusamehe:

(1) Mwenyezi Mungu Anasema: Nani anayesamehe madhambi isipokuwa ni Mwenyezi Mungu; 3:135

(2) Mwenyezi Mungu Anasema: Waambie Shafaa ni ya Mwenyezi Mungu; Az-zumar: 44

(3) Mwenyezi Mungu Anasema: Waliwafanya Makasisi wao na watawa wao kuwa ni Mola badala ya Mwenyezi Mungu, 9:31 Na Shafaa, na kumuwekea Kanuni (za maisha yake) na wajibu mwingineo, basi kwa ajili hiyo atakuwa amemfanya kuwa ni "RABBU" mlezi wake. Kwa hiyo yeyote ambaye atakayeamini na kuitakidi katika nafsi yake (kama tulivyoeleza hapo kabla) na akaifasiri itikadi hiyo kwa maneno na matendo, basi hapana shaka kwamba anamuabudu huyo aliyemzingatia kuwa ni "Rabbu".

### TAARIFU YA TATU YA IBADA

Hapa tunaweza kutoa Taarifu hii ya tatu ya ibada inayopatikana kutokana na maumbile na nguvu ya nafsi. Tunasema: "Ibada ni kumnyenyekea yule ambaye tunamzingatia kuwa Mungu na ndiyo asili ya matendo ya kiungu". Hapana shaka kwamba matendo ambayo yanahusiana na ulimwengu, kama vile kusimamia uendeshaji wa ulimwengu na kuhuisha na kufisha na kugawa rizki baina ya viumbe na kusamehe madhambi yote haya yanamuhusu Mwenyezi Mungu Mtukufu. Nawe (msomaji) lau utazizingatia vyema aya za Qur'an zinazozungumzia maelezo tuliyotangulia kuyataja,

katika Aya ya 35 Surat Al- Qasa, Aya ya 60 mpaka Aya ya 64 Surat An-Namli Aya ya 5 na ya 6 Sura Az-Zummar. Utaona kwamba Qur'an inasisitiza kwa nguvu sana kuwa matendo haya yanamuhusu Mwenyezi Mungu tu na wala hayamuhusu mwingine asiyekuwa yeye. Hii ni kwa upande mmoja, ama kwa upande wa pili: Sote tunafahamu kwamba ulimwengu wa viumbe ni ulimwengu uliopangwa vyema kabisa, na hakiwezi kutokea kitu isipokuwa sababu ya kutokea kwake itarejea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Qur'an Tukufu inaonyesha (ukweli) wa jambo hili. Mwenyezi Mungu anasema:

وَهُوَ الَّذِي يُحْيِي وَيُمِيتُ وَلَهُ اخْتِلَافُ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٨٠﴾

"Na ni yeye (Mwenyezi Mungu) ndiye anayehuisha na kufisha, na mabadiliko ya usiku na mchana yamo katika milki yake." Qur'an, 23:80.

Katika mahala pengine Mwenyezi Mungu anasema kwamba miongoni mwa Malaika wapo wanaosimamia utoaji wa Roho. Nayo ni kauli yake isemayo:

حَتَّىٰ إِذَا جَاءَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ تَوَفَّتْهُ رُسُلُنَا وَهُمْ لَا يُفَرِّطُونَ ﴿٦١﴾

"Hata pale mmoja wenu anapofikiwa na mauti wajumbe wetu humfisha." Qur'an, 6:61

Kwa kuijengea hali hii, inawezekana kuzikusanya aya hizi mbili na tukasema kama ifuatavyo: "Bila shaka hizi sababu zinazosababisha pia matendo ya ulimwenguni, kama yatakuwa ni ya kimaumbile ya kawaida au kimaana kama vile Malaika, basi iwe iwavyo yanathibitika kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu naye ndiye mtendaji halisi." Kwa maneno mengine ni kwamba, kitendo cha watendaji hawa wawili (Mwenyezi Mungu na Malaika) ni kitendo kimoja tu na si vitendo viwili lakini mtendaji wa kwanza anafanya kwa uwe wake na yule wa pili anamfuatia yule wa kwanza (kutekeleza maamrisho yake).

Maana hii ni miongoni mwa maarifa ya juu katika Qur'an ambayo hufahamika kwa kuzirejea aya za Qur'an zinazozungumzia matendo ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Sasa basi ikiwa mtu ataitakidi kwamba Mwenyezi Mungu amewapa baadhi ya viumbe wake kama vile, Malaika na Mawalii matendo yake ya kuruzuku, na kuhuisha na yasiyokuwa hayo, na akaammi pia kuwa viumbe hao ndiyo wanaoendesha mambo ya ulimwengu na kuyasimamia mambo yake na akaona kuwa Mwenyezi Mungu hahusiki tena kwenye matendo hayo kiasi kwamba itikadi hiyo ikampelekea kuwanyenyekea viumbe hawa, basi hapana shaka yoyote kwamba unyenyekevu wake huu ni ibada na tendo hili ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa maneno mengine tunasema: "Lau mtu ataitakidi kwamba Mwenyezi Mungu ameukabidhi ustahiki wa kutekeleza matendo kwa Malaika na Mawalii, na Mwenyezi Mungu akawa amebaki hana ustahiki wote wote (katika matendo hayo) na hao Malaika na Mawalii wanayafanya matendo hayo bila kumtegemea Mwenyezi Mungu na bila idhini yake, basi mtu huyu aliyeitakidi itikadi hii, hakika amemfanyia Mwenyezi Mungu mshirika na amemfananisha (Na viumbe vyake). Hapana shaka kwamba itikadi kama hii ndiyo kuishirikisha dhati ya Mwenyezi

Mungu na kutawas-sal na kunyenyekea kunakotokana na itikadi hii ni ibada kama ilivyokuja katika Qur'an Tukufu.

Anasema Mwenyezi Mungu:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَتَّخِذُ مِن دُونِ اللَّـهِ أَندَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ اللَّـهِ ﴿١٦٥﴾

"Na miongoni mwa watu wako wanaofanya waungu badala ya Mwenyezi Mungu, na wanawapenda kama (anavyostahiki) kupendwa Mwenyezi Mungu". Qur'an, 2:165

Kwa hakika chochote chenye kuwa na kuwepo hakiwezi kuwa mfano wa Mwenyezi Mungu au mshiriki isipokuwa kitakapokuwa na uwezo wa kuuendesha ulimwengu kwa matakwa yake binafsi bila ya matakwa ya Mwenyezi Mungu lakini hakuna yeyote mwenye uweza huo. Bali kila kilichopo ni chenye kunyenyekea mbele ya matakwa ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kitake au kisitake basi kwa hiyo hakiwezi kuwa mshirika wa Mwenyezi Mungu bali kitakuwa kitiifu kwake kutenda kama atakavyo yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ukweli halisi in kuwa, washirikina walikuwa wakiitakidi kwamba, masanamu yao waliyokuwa wakiyaabudu yanajitegemea katika kunendesha ulimwengu huu na pia katika mambo ya uungu.

Na katika zama za Jahiliya (kabla kuja Uislamu) kulikuwa na ushirikina wa namna mbali mbali na ushirikina wa daraja ya chini kabisa ilikuwa ni itikadi ya Mayahudi na Wakristo kwamba mapadri na Makasisi wao wanayo madaraka ya uwekaji wa kanuni na sheria kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

وَعَلَّمَ آدَمَ الْأَسْمَاءَ كُلَّهَا ثُمَّ عَرَضَهُمْ عَلَى الْمَلَائِكَةِ فَقَالَ أَنبِئُونِي بِأَسْمَاءِ هَـٰؤُلَاءِ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ ﴿٣١﴾

"Waliwafanya wanachuoni wao na watawa wao kuwa ni waungu wao kinyume cha Mwenyezi Mungu". Qur 'an, 2:31

Kadhalika washirikina walikuwa wakiitakidi kwamba, ustahiki wa Shafaa na Maghfira (mambo ambayo yanamstahiki Mwenyezi Mungu tu) vimekabidhiwa kwa Masanamu yao wanayoyaabudu, na masanamu hayo yanafanya mambo hayo yenyewe kikamilifu kwa kujitegemea katika ustahiki huo. Na kwa ajili hii utaona aya nyingi za Qur'an zinazozungumzia Shafaa zinasisitiza kwamba Shafaa haithibitiki ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu asemavyo ndani ya Qur'an:

مَن ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِندَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ ﴿٢٥٥﴾

"Na ni nani huyo awezaye kushufaiya (kuombea) mbele ya Mwenyezi Mungu isipokuwa kwa idhini yake." Qur 'an, 2:255

Na lau washirikina wangekuwa wanaitakidi kwamba, masanamu yao waliyokuwa wakiyaabudu yanauwezo wa kushufaiya kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, basi usingeona Qur'an inakanusha moja kwa moja Shafaa bila ya idhini ya Mwenyezi Mungu. Baadhi ya wanafalsafa wa Kiyunani walikuwa wamejenga ndani ya fikra zao Miungu wengi kwa kila jambo miongoni mwa mambo ya ulimwenguni. (Kwa mfano) mvua ina Mungu wake, mimea ina mungu wake, mtu ana Mungu wake na mambo mengine (kila moja lina mungu wake). Na walikuwa wakidai kwamba utendaji wa kuendesha mambo ya ulimwengu ambao unamuhusu Mwenyezi

Mungu peke yake, umekabidhiwa kwa miungu hawa. Na katika zama za Jahiliya, baadhi ya Waarabu walikuwa wakiabudu Malaika na nyota zitembeazo na zile zisizotembea hali ya kuwa wakidhani kwamba usimamizi wa mambo ya ulimwengu na watu umekabidhiwa kwa vitu hivyo, navyo ndivyo vinavyotenda kikamilifu kwa kujitegemea na hiyari kamili, na kuwa Mwenyezi Mungu ameuzuliwa na hana uwezo wowote juu ya mambo haya kabisa (ametakasika Mwenyezi Mungu na fikra hizi sana sana).[1]

Na kwa hiyo basi kila aina ya unyenyekevu utaofanywa kwa Malaika na nyota utazingatiwa kuwa ni ibada kwa kuwa unatokana na itikadi hii yenye makosa. Kuna baadhi ya Waarabu wengine wa zama za Jahiliyyah, hawakuyaitakidi masanamu yaliyochongwa kwa miti na madini kuwa ni Miungu na kwamba ndiyo yaliyowaumba wala kusimamia mambo ya ulimwengu na watu, bali wao walikuwa wakiyaamini kuwa yanao uwezo wa kuwaombea na walikuwa wakisema: "Masanamu haya ni waombezi wetu mbele ya Mwenyezi Mungu".[2] Na kwa msingi wa mtazamo huu batili, walikuwa wakiyaabudu Masanamu haya kwa lengo la kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu na walikuwa wakisema wamasema:

مَا نَعْبُدُهُمْ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى اللَّـهِ زُلْفَىٰ ﴿٣﴾

"Sisi hatuyaabudu (Masanamu) isipokuwa kwa ajili ya kutukurubisha kwa Mwenyezi Mungu." Qur 'an, 39:3

Kwa kifupi tunasema: "Bila shaka tendo lolote litokanalo na itikadi hii na likajulisha kufuata na kunyenyekea basi ni ibada, na kinyume chake ni kuwa tendo lolote ambalo halikutegemezewa itikadi kama hii haliwezi kuzingatiwa kuwa ni ibada wala shirki."

Lau mtu atanyenyekea mbele ya mtu na akamuheshimu na kumtukuza bila ya kuamini itikadi kama hii, basi tendo hili halitachukuliwa kuwa ni shirki wala ibada hata kama tendo hilo litakakadiriwa kuwa ni haramu.

Kwa mfano: Haitazingatiwa kuwa ni ibada sijda ya mpenzi kwa mpenzi wake, wala mwenye kuamriwa kumsujudia aliyemuamuru na mke kumsujudia mume pamoja na kwamba Sijda kumsujudia asiye Mwenyezi Mungu ni haramu kisheria, kwani Sijda ni Makhsusi kwa Mwenyezi Mungu peke yake wala hairuhisiwi kwa yeyote yule kafanyiwa japo itakuwa ni kwa sura ya dhahiri isiyokuwa na itikaadi isipokuwa kama Mwenyezi Mungu ataamuru kufanywa kwa sijida hiyo (kwa asiye Mwenyezi Mungu).

1. Al-Milal Wanihal cha Shahirstani, juz. 2, chapa ya Misri uk. 244-247.
2. Qur'an, 10:18.

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## NATIJA YA UTAFITI

Mpaka hapa kwa namna fulani tunaweza kufafanua uhakika wa Ibada na sasa ni lazima tueleze kwa kifupi matokeo ya utafiti huu na tunasema: Lau mtu atawanyenyekea watu wengine bila ya kumzingatia mmoja wapo kuwa ni Mungu au Rabbu au kuwa ni asili inayojitegemea kwa kutenda matendo ya Mwenyezi Mungu, bali amewaheshimu tu kwa kuwa wao ni:

عِبَادٌ مُّكْرَمُونَ ﴿٢٦﴾ لَا يَسْبِقُونَهُ بِالْقَوْلِ وَهُم بِأَمْرِهِ يَعْمَلُونَ ﴿٢٧﴾

"Waja waliotukuzwa hawamtangulii Mwenyezi Mungu kwa neno (Lake asemalo) nao wanatenda amri zake" - Qur'an, 21:26.

Basi mtu huyo tendo lake hili la kunyenyekea haliwi ila kuwaheshimu na kuwatukuza, wala hakuna uhusiano wowote wa tendo hili na ibada kamwe. Bila shaka Mwenyezi Mungu amewataja baadhi ya waja wake kwa utajo mwema na amewasifu kwa namna inayoamsha raghba (hamu) ya kila mtu awatukuze na kuwaheshimu. Miongoni mwa utajo huo ni kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema:

إِنَّ اللَّـهَ اصْطَفَىٰ آدَمَ وَنُوحًا وَآلَ إِبْرَاهِيمَ وَآلَ عِمْرَانَ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿٣٣﴾

"Bila shaka Mwenyezi Mungu alimchagua Adam na Nuh na kizazi cha Ibrahim na kizazi cha lmran juu ya walimwengu wote." Qur'an, 3:33.

Vile vile Qur'an inabainisha kwamba Mwenyezi Mungu alimchagua Nabii Ibrahim kwa ajili ya Uimamu anasema:

قَالَ إِنِّي جَاعِلُكَ لِلنَّاسِ إِمَامًا ﴿١٢٤﴾

"(Mwenyezi Mungu) akasema bila shaka ninakufanya uwe lmamu kwa ajili ya watu. Qur'an, 2:124

Pia Mwenyezi Mungu katika Qur'an amewataja kwa utajo mwema Manabii Nuh, Ibrahim, Dawood, Seleiman, Musa, Isa na Muhammad, (Rehma za Mwenyezi Mungu ziwashukie wote). Na amewasifu kwa sifa tukufu kiasi kwamba kila sifa moja peke yake inatosha kuuvuta moyo na kuleta mapenzi ndani ya nafsi za watu. Na utaiona Qur'an Tukufu inatangaza ubora wa kizazi cha Mtume Muhammad **[s.a.w.w]** katika aya nyingi. Miongoni mwa aya hizo ni hizi zifuatazo:

إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّـهُ لِيُذْهِبَ عَنكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا ﴿٣٣﴾

"Bila shaka Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu Enyi watu wa nyumba (ya Mtume) na akutakaseni sana sana." Qur'an, 33:33

قُل لَّا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِلَّا الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَىٰ ﴿٢٣﴾

"Waambie sikutakeni malipo yoyote juu ya utume wangu isipokuwa muwapende Al-Qurbaa". Qur'an 42:23

Na huwalisha chakula katika mahaba ya Mwenyezi Mungu, masikini, yatima na mateka hali ya kuwa wenyewe wanakipenda (chakula hicho) (nao husema moyoni mwao) tunakulisheni kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu (tu) hatutaki kwenu malipo wala shukurani, hakika sisi tunaiogopa kwa Mola wetu hiyo siku yenye shida na taabu, basi Mwenyezi Mungu atawalinda na shari ya siku hiyo na kuwakutanisha na neema na furaha na

atawalipa mabustani ya pepo na (nguo) za hariri kwa sababu ya kusubiri (kwao)... mpaka mwisho wa Surat hii ya 76.[1] Basi lan watu wangesimama upande wa Mawalii hawa watukufu kwa matendo ambayo yanakubalika ikiwa ni pamoja na kuwatukuza na kuwaheshimu, sawa sawa katika zama za uhai wa Mawalii hao au baada ya kufa kwao, bila ya kuwaitakidi kuwa wao ni miungu na ni vyanzo vinavyojitegemea kwa matendo yanayomstahiki Mwenyezi Mungu, basi hapana mtu yeyote ambaye angeyaona matendo haya kuwa ni ibada wala anayeyasimamia asingeonekana kuwa ni mshirikina, bali kinyume chake angewaona kuwa ni watu wenyc mafanikio wanaoheshimu Mawalii wa Mwenyezi Mungu na kudumisha utajo wao na kuwafanya Mawalii hao kuwa ni kiigizo (chema) kwa watu hao.

Bila shaka kuwatukuza Mawalii wa Mwenyezi Mungu ni kutukuza vitambulisho vya Mwenyezi Mungu kama ilivyokwisha onyeshwa hapo kabla, na kwamba Uislamu unavitukuza vitambulisho vya Mwenyezi Mungu. Mtume **[s.a.w.w]** alikuwa akilishika na kulibusu "Hajarul-Aswad" pamoja na yeye kufahamu wazi kwamba hilo ni jiwe tu. Na sisi pia tunamfuata Mtume **[s.a.w.w]** kwa tendo lake hilo, tunalibusu Hajarul Aswad na tunatufu nyumba ya Mwenyezi Mungu ambayo si kitu ila mkusanyiko wa mawe na udongo, na tunakimbia baina ya Safa na Marwah na si kitu ila vilima viwili. Hii ni (kana kwamba) tunatenda matendo yale yale yaliyokuwa yakitendwa na waabuduo sanamu kwa masamu yao, lakini hapana kabisa mtu yeyote ambaye imepata kumpitia katika fikra zake kwamba sisi tunaabudu udongo na mawe. Basi Je, ni kwa nini? Ni kwa sababu mawe hayo hayadhuru wala kunufaisha.

Ama tungetekeleza Ibada hizi hali ya kuwa tunaitakidi kuwa mawe haya na vilima hivi ni miungu na ndiyo chanzo cha athari za uungu, basi tungekuwa miongoni mwa wanaoabudu sanamu. Na kwa msingi huu, bila shaka kuubusu mkono wa Nabii au Imam au Mwalimu au wazazi wawili na pia kuibusu Qur'an na vitabu vya dini kama vile "Nahjul-Balagha" na kubusu Zariha na kila kile chenyc kuhusiana na waja wema wa Mwenyezi Mungu, hakuna kinachokusudiwa ila ni heshima na kuwatukuza, na kawatukuza wao si kitu kingine ila kumtukuza Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ndani ya Qur'an imekuja (Habari) ya Malaika kumsujudia Adam [a.s] na pia ndugu wa Nabii Yusuf kumsujudia Yusuf [a.s], lakini hapana yeyote iliyempitia katika akili (yake) kwamba kusujudu (kwao hawa) ilikuwa ni kumuabudia Adam au Yusuf na hiyo ni kwa sababu hao waliomsujudia Adam na Yusuf hawakuwaitakidi wawili hao kuwa ni miungu na hawakuwazingatia kuwa wao ndiyo asili ya matendo ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, bali jambo hilo lilikuwa ni heshima na utukufu na siyo ibada kama inavyoonekana.

Bila shaka Mawahabi wakati wanapokutana na aya hizi, wanagongana nazo, kwani utawaona wanachunguza huku na huko ili kuzikwepa na kuzificha na husema; "hakika kusujudu kwa watu hao ilikuwa ni amri ya Mwenyezi Mungu kwa hiyo haiwezi kuzingatiwa kuwa ni ibada." Ni sawa kwamba yote hayo na hata kusujudu kwa ndugu wa Yusuf [a.s] kulikuwa ni kwa amri ya Mwenyezi Mungu au radhi yake, lakini kitu ambacho

1. Qur'an, 76:8-12.

Mawahabi wanajisahaulisha na kujifanya hawakijuwi ni ule ukweli wa tendo lenyewe Ia Sajdah siyo ibada na ndiyo maana Mwenyezi Mungu akaliamrisha. Na lau Sajdah ingekuwa ni ibada kwa anayesujudiwa, Mwenyezi Mungu asingeliamrisha kabisa, kwani amri haiwezi kuitoa ibada kwenye uhakika wake na wala haiwezi kuifanya shiriki kuwa Tauhidi. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿قُلْ إِنَّ اللَّـهَ لَا يَأْمُرُ بِالْفَحْشَاءِ أَتَقُولُونَ عَلَى اللَّـهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢٨﴾

"Waambie, bila shaka Mwenyezi Mungu haamrishi maovu, Je, Mwasema juu ya Mwenyezi Mungu mambo msiyoyajua?" Qur'an, 7:28.

Kifupi ni kuwa, uhakika wa tendo lolote lazima uwe siyo wa kiibada kabla haijatolewa amwi kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuliamrisha tendo hilo ili (itakapotoka amri) ipate kuihusisha ibada (kwenye tendo hilo) na wala hakuna namna yoyote ya amri itakayokuja kulitengua tendo hilo kutoka kwenye hukmu ya Ibada.

Bila shaka kujitakasa ambako Mawahabi wanategemea, kitu ambacho muda mrefu tumekuwa tukisikia toka kwa Masheikhe zao huko Maka na Madina, kunajulisha ukaidi walionao juu ya kufahamu maarifa ya Qur'an na kukosa kwao kuelewa kuwa "Ibada" inao uhakika wa pekee unaojitegemea na hupata ikatokeza amri kuamrisha ibada na wakati mwingine katazo kukataza. Hii ina maana kwamba, kitu ambacho kwa dhati yake ni ibada, Mwenyezi Mungu hukiamrisha au kukikataza, kama vile Sala na Saumu ambazo Mwenyezi Mungu amewaamrisha watu "Mukalafu" kazitekeleza na amemkataza (kufanya ibada hizo) mwanamke mwenye hedhi, ati kama vile kufunga siku ya Idi al-Fitri na Adh-haa ambazo Mwenyezi Mungu amewakataza watu wote "Wasifunge". Basi kama kusujudu kwa Malaika kumsujudia Adam [a.s] na ndugu wa Yusuf [a.s] na wazazi wake wawili kumsujudia Yusufu [a.s] ni kuwafanyia Ibada, basi ile amri ya kuamrishwa kwao kusujudu, hakuitoi sijda katika uhakika wa kuwa ni ibada bali hapana budi tuseme kuwa kuitakidi Uungu ndiko kutakakokiharamisha kitendo hicho na kukifanya kuwa ni ibada, au kuitakidi kuwa yule anayenyenyekewa ndiyo asili (chanzo) cha matendo ya Mwenyezi Mungu. Vipi tutapata msimamo?

Ewe msomaji mpendwa inapasa ufahamu kuwa, kuondosha tofauti iliyopo kati ya Waislamu na Mawahabi ndani ya mambo mengi (wanayohitalifiana) inategemea kupata ufumbuzi wa maana ya ibada. Ikiwa haikubainishwa maana ya ibada kwa taarifu ya kimantiki, na ikawa hakuna maelewano na uadilifu katika pande mbili, basi hakuna faida ya kutafiti na kujadiliana. Kwa maelezo haya basi, hana budi mtu mwenye kutafuta ukweli afanye kila njia ya kuchunguza maudhui hii kwa undani na asihadaike na taarifu za kilugha zilizopungufu kuweza kutatua na kufafanua. Rejea iliyo bora atakayoirejea ni aya za Qur'an, hiyo ndiyo dalili inayoongoza (kufahamu) maudhui hii na kila maudhui. Na miongoni mwa mambo yanayohuzunisha ni kwamba, waandishi na watunzi wa Kiwahabi na walioandika kuwajibu Mawahabi, wamefanya utafiti na uchunguzi kwa urefu katika nukta zingine na wala hawakuitilia maanani nukta hii muhimu (ya Ibada) kwa kuisherehesha na kuithibitisha. Basi Mawahabi wanasema, "Matendo mengi muyafanyayo Enyi Waislamu kumhusu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** na Maimamu wa nyumba yake ni kumuabudia,

na hali hiyo inalazimu kumshirikisha Mwenyezi Mungu katika ibada." Kwa hiyo basi inabidi Waislamu walete ufafanuzi na maelezo ya kina kuhusu ibada ili kuiondoa dalili yao ya upuuzi. Kwa hakika Mawahabi wanayaona mambo mengi wayatendayo Waislamu kwa maiti kuwa ni kumuabudia. Kwa mfano:

1). Kuomba Shafaa kwa Mtume **[s.a.w.w]** na watu wema.

2). Kuomba uponyo kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu.

3). Kuomba kutekelezewa haja toka kwa viongozi wa Dini.

4). Kumheshimu na kumtukuza mwenye kaburi.

5). Kutaka msaada kwa Mtume **[s.a.w.w]** na wengineo.

Basi wao (Mawahabi) wanasema, "Hakika Shafaa ni katika matendo ya Mwenyezi Mungu na vile vile kuponya ni kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kuomba mojawapo ya mawili haya kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu kunapelekea kumuabudu huyo (aombwaye).

### NI KIPI KITENDO CHA MWENYEZI MUNGU?

Katika kitabu hiki kidogo tunatanguliza uchunguzi juu ya matendo ya Mwenyezi Mungu na maana yake ili maudhui hii ipate kufahamika na tunasema: "Ikiwa ambaye anasimamaia Shafaa na kuponya kwa uwezo wake mwenyewe na kwa kutaka kwake hali ya kujitegemea bila ya kuipata haki ya Shafaa kutoka kwa yeyote yule na bila ya kutegemea uwezo wa aliye juu zaidi kuliko yeye kiuwezo) basi haya ni miongoni mwa matendo ya Mwenyezi Mungu yanayomuhusu peke yake. Na kuomba Shafaa kwa yeyote yule hali ya kaitakidi (kama tulivyosema hivi punde) maana yake ni kuamini Urabbi na Uungu wa huyo anayeombwa. Ama ikiwa kuomba Shafaa na uponyo kumesalimika kutokana na itikadi hii, na mtu akaomba Shafaa kwa mtu anayemuitakidi kuwa ni mja wa Mwenyezi Mungu, pia anatenda kwa msaada na uwezo wa Mwenyezi Mungu na idhini yake, basi Shafaa hii na uponyo huu havilazimiani na itikadi ya Uungu na siyo kuomba tendo la Mwenyezi Mungu kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu." Qur'an Tukufu inasema ikimnukuu Nabii Isa [a.s]:

وَأُبْرِئُ الْأَكْمَهَ وَالْأَبْرَصَ وَأُحْيِي الْمَوْتَىٰ بِإِذْنِ اللَّـهِ ﴿٤٩﴾

"Na ninaponya vipofu na wenye mbaranga, na ninafufua wafu kwa idhini ya Mwenyezi Mungu". Qur'an, 3:49

Na ufafanuzi kama huu unakuja pia ndani ya munasaba wa kuomba kukidhiwa haja toka kwa mmoja wa Mawalii wa Mwenyezi Mungu au kumuomba msaada. Basi kutaka kukidhiwa haja na Walii huyo kuna namna mbili:

1). Kumuomba mja pamoja na kuitakidi kuwa anao uwezo wa kujitegemea Mwenyewe, hii itakuwa ni Ibada.

2). Kumuomba mja hali ya kuitakidi kuwa yeye ni mja wa Mwenyezi Mungu na nguvu zake zinatoka kwa Mwenyezi mungu, basi hali hii haihusiani kabisa na ibada. Kwa Hakika ufafanuzi huu siyo tu ndiyo ukomo wa kutenganisha baina ya ibada na kisichokuwa ibada kwa munasaba wa matendo haya, bali ni kanuni ya ujumla inayotenganisha baina ya Shirki na Tauhidi katika kila vinavyo athiri na sababu. Bila shaka kuitakidi athari (matokeo) ya 'Asprini' (kwa mfano) katika kutuliza maumivu, na kuitakidi kuwa ikiwa athari hiyo inatokana na uwezo wake wa kujitegemea na

kwamba hakuna mafungamano na uwezo uliyo juu zaidi ambaye ni Mwenyezi Mungu, basi maana yake ni kuitakidi Uungu wa hiyo 'Asprini'. Ama kuitakidi kwamba Mwenyezi Mungu ndiye aliyeyaweka matokeo haya na athari hii ndani ya Asprini na pia dawa hii si lolote ila ni sababu ya kutuliza maumivu na vile vile haiwezi kutuliza maumivu isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, bila shaka itikadi ya namna hii inatokana na Tauhidi yenyewe khasa, kwani hapana mwenye kuathiri ila yeye Mwenyezi Mungu.

Na kwa sababu hii tumesema kwamba "Kuondosha tofauti mbali mbali kunaegemezewa kwenye ufafanuzi wa maana ya Ibada na kuitakasa Tauhidi kutokana na shirki na matendo ya Mwenyezi Mungu kutokana na mengineyo na kuutakasa uungu kutokana na Ubudiyyah. Na hapo kabla imeonyeshwa kuwa Waarabu wa zama za Jahiliyya walikuwa wakiitakidi itikadi hii yenye makosa, kwamba Masanamu (hayo hayo) ndiyo yaliyokuwa yanaendesha baadhi ya mambo ulimwenguni kwa kujitegemea na yalikuwa yakimiliki Shafaa na mambo mengineyo. Itikadi hii ndiyo iliyowafanya wawe washirikina. Kwa hiyo, iwapo utataka ufafanuzi wa kielimu juu ya maudhui hii rejea vitabu hvi viwili vifuatavyo vilivyoandikwa na Mwandishi wa kitabu hiki.

1). Maalimut-Tauhidi Fil-Qur-'anil-Karim.

2). At-Tauhidu Was-Shirku Fil-Qur-anil-Karim.

### MANENO YA AL-QUDHAI AL-MISRI

Baada ya kuwa nimeyahariri (maelezo yaliyotangulia) na kubainisha ufafanuzi wa ibada niliyaangalia kwa makini maneno ya mmoja wa wachunguzi miongoni mwa wanachuoni wa chuo cha Az-har, yaani Ustadh Sheikh Salamah Al-Qudhai Al-Izami As-Shafii ambaye ndiye Mwandishi wa kitabu kiitwacho "Fur-Qanul Qur'an Baina Sifatil-Khaliq Wa Sifatil-Ak-Waan.[1] Yeye amesema: Mwenyezi Mungu aing'arishe hoja yake: (Sasa tutazame maana ya Ibada kisheria, na ninataraji mahala hapa patatoa uzinduzi uliyo bora, kwa hakika kosa lililomo ni kuteleza kukubwa na ni kosa kubwa ambalo zilimwagwa damu (za watu) zisizoidadi ya kudhibitiwa

1. Ni miongoni mwa vitabu bora vilivyotungwa katika zama za hivi karibuni, na mtunzi huyu pamoja na mwenziwe aitwaye Al- Ustadhi Muhammad Zahid AI-Kauthari AI-Misri ambaye ni mwanachuoni wa hadithi na muhakiki, ni miongoni mwa Wanachouni ambao walisimama kupinga uzushi wa Kiyahudi unaomshabihisha Mwenyezi Mungu Mtukufu na kumfanyia mwili na upande na mahali. Kwa hakika uzushi huu ulianza kupata nguvu mwanzoni mwa Qarne ya nane kutoka mkononi mwa Sheikh wa Bid'a na upotofu aliyekuwa akiitwa: "Ahmad Abdil-Halim Ibn Taimiyyah AI-Harrani na baada yake kupitia mkononi mwa mwanafunzi wake lbn Al-Qayyim, na baada ya wawili hao, kupitia kwa yule aliyekunywa makombo yao yaani Sheikh Muhammad Ibn Abdil-Wahab. Basi huyo mwanachuoni wa mwanzo alisimama akatunga Kitabu chake kiitwacho, "Fur-Qanul-Qur'ani akapinga uzushi huu (wa Ibn Taimiyyah na wenzake) na mwingineo miongoni mwake ikiwa ni kuzuwia (watu) kutawassal na kuomba msaada na kutaka shafaa kwa yule ambaye Mwenyezi Mungu amemjaalia kuwa mwenye kusaidia kwa idhini yake na mwenye kushufaiya kwa amri yake Mwenyezi Mungu, kama ambavyo yule mwanachuoni wa pili alisimama kwa kusambaza kitabu kiitwacho "Al-Asmau Was-sifatu" cha Al-Hafidh Abubakr Al-Bayhaqi ikiwa ni pamoja na kukihakiki na kukiwekea ufafanuzi wa utangulizi wenye manufaa, na vitabu hivi viwili vilichapishwa Misri Mwaka 1358 A.H. katika mjaladi mmoja. Basi Mwenyezi Mungu awalipe juhudi zao najuhudi za msambazaji wa vitabu vya haki. Ameen.

na heshima za watu zilizovunjwa hazina hesabu, na jamii zikatenganishwa mahala ambapo Mwenyezi Mungu ameamuru ziunganishwe Mwenyezi Mungu atulinde kutokana na makosa na fitna hasa hasa fitna za Shubuhati - basi fahamu kwamba wao yaani Mawahabi waliifasiri ibada kuwa ni "Kufanya unyenyekevu ulio katika daraja ya juu sana", na wakakusudia ndani ya tafsiri hiyo maana ya kilugha tu. Ama maana ya kisheria inatoa maana iliyo finyu kuliko hii (ya kilugha) kama itakavyodhihiri kwa mchunguzi mwenye kuvumilia katika utafiti iwapo ataangalia kila mahali ambapo neno ibada limekuja katika sheria, kwani maana yake ni "kufanya unyenyekevu wa hali ya juu kwa moyo kwa kuitakidi Uungu wa anayenyenyenyekewa, au kwa mwili pamoja na itikadi hiyo.

Basi ikiwa itikadi hii itakuwa haipo, unyenyekevu wa dhahiri alioufanya (Mwenye kunyenyekea) hauwezi kuwa ni ibada kisheria, ikiwa kanyenyekea sana au kidogo na kwa namna yoyote hata kama ni kusujudu na hata kama hakuamini Rububiya kwa yule anayemnyenyekea lakini akaamini kuwa anazo khususiyah fulani za Rububiyah, basi hii pia itakuwa ni ibada. Kwa mfano kama ataitakidi kwamba huyo mwenye kunyenyekewa anajitegemea katika kunufaisha au kudhuru na kama vile kupitisha matakwa yake japokuwa kwa njia ya Shafaa kumshufaia huyo mwenye kumuabudia mbele ya Mola ambaye ni mkuu kuliko huyu mwenye kuabudiwa. Kwa hakika washirikana walikufuru kwa sababu ya kuyasujudia masanamu yao na kuyaomba na mambo mengineyo miongoni mwa aina za unyenyekevu kwa sababu ya sharti hii kwani washirikina waliitakidi umola wa hayo wanayoyanyenyekea au wakayahusisha na khususiyyat za Rububiyah kama utakavyokujia ufafanuzi wake. Na haiwezekani kusema kwamba kumsujudia asiyekuwa Mwenyezi Mungu bila itikadi hii ni ibada kisheria ukiachilia mbali aina zingine za unyenyekevu ambazo ni duni kuliko Sijda. Na kama tutasema, Sijda hii ni Ibada itakuwa ni kufru, na chochote kilicho kufru hakitofautiani kutokana na tofauti ya sheria wala amri ya Mwenyezi Mungu kwa kitu hicho wala Mwenyezi haamrishi kitu kama hicho: "Waambie Mwenyezi Mungu haamrishi mambo mabaya" Qur'an, 7:28

"Na wala haridhii kufru kwa waja wake." Qur'an, 39:7

Na haya yako wazi (yanaeleweka) kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Na (sasa) hebu msikilize Mwenyezi Mungu Mtukufu alipowaambia Malaika:

"Msujudieni Adam, wakasujudu wote isipokuwa Ibilisi alikataa na akapinga" Qur'an, 2:34 Na alisema Iblisi: "Mimi ni bora kuliko yeye": Qur'an,7:12

"Na alisema tena: Je, Nimsujudie Uliyemuumba kwa Udongo?" Qur 'an, 17:61

Na kusema kwamba Adam alikuwa ndiyo Qibla (cha Malaika walipamuriwa kumsujudia) ni usemi ambao haukubaliwi na ukweli na pia uchunguzi (wa jambo hili) katika kuifahamu aya inavyopasa kuifahamu unapinga kauli hiyo. Na kama fahamu zako zitashindwa kulifahamu jambo hili, basi huyu hapa Nabii Yaqub na mkewe na watoto wao kumi na mmoja ambao Mwenyezi Mungu amesema kuhusu wao,

"Wakaporomoka kumsujudia". Hapa inamaana walimsujudia Yusuf [a.s]. Qur'an, 12:100.

Mwanachuoni Al-Hafidh Ibn Kathir amesema katika Tafsiri ya aya hii, "Walimsujudia (Yusuf) wazazi wake wawili na ndugu zake na walikuwa watu kumi na moja, na tendo lao hili lilikuwa ni desturi inayokubalika kufanywa katika sheria zao wanapomsalimia mkubwa humsujudia. Na desturi hii ilikuwa imeruhusiwa tangu kwa Nabii Adam [a.s] hadi kwenye sheria ya Nabii Isa [a.s], kisha iliharamishwa katika mila hii ya Kiislamu na kuifanya Sijda ni makhsusi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na haya ndiyo madhumuni ya kauli ya Qatada (juu ya Qadhiya hii na wengineo). Na kuna mapokezi katika hadithi kwamba: "Muadhi alifika Shamu akawakuta watu wa huko wakiwasujudia Maaskofu wao, naye aliporudi (Madina) akamsujudia Mtume **[s.a.w.w]**, Mtume akasema "Nini hiki (ukifanyacho) Ewe Muadhi"?

Muadhi akasema: "Mimi nimewaona (Huko Shamu) wanawasujudia Maaskofu wao, nawe unastahiki mno mimi nikusujudie." Mtume akasema: Lau ningekuwa mwenye kumuamrisha yeyote kumsujudia mwingine, basi ningemuamuru mke amsujudie mumewe kutokana na haki kubwa aliyonayo kwake." Na katika hadithi nyingine inasemwa kwamba: "Salmaan alikutana na Mtume **[s.a.w.w]** katika baadhi ya njia za Madina, na huyu Salmaan alikuwa kasilimu hivi karibuni, basi akamsujudia Mtume **[s.a.w.w]**, Mtume akasema, "Ewe Salmaan usinisujudie bali msujudie (Mwenyezi Mungu) aliye hai ambaye hatakufa". Lengo katika maelezo haya ni kuonyesha kuwa (Desturi ya kusujudia wakubwa) ilikuwa ikiruhusiwa katika sheria zao, (mwisho wa kauli ya Ibn Kathir).

Naye Imam Abu Jaafar (At-Tabari) katika tafsiri yake amesema mfano wa maelezo haya. Bila shaka umekwisha fahamu kwamba (Kitendo) kilicho cha kufru hakitofautiani kwa kutofautiani sheria, wala Mwenyezi Mungu hakiamrishi kuwa kitendwe wakati fulani miongoni mwa nyakati, basi kusujudu kwa Malaika kumsujudia Adam wala sijda aliyosujudiwa Yusuf [a.s] hazikuwa ni kufru kwa kuwa waliosujudu hawakuwa wameitakidi itikadi ya mambo ambayo yanamuhusu Mwenyezi Mungu peke yake wakati walipowasujudia hao waliosujudiwa, bali Malaika waliposujudu (kumsujudia Adam) kwao ilikuwa ni ibada kwa kuwa Mwenyezi Mungu ndiye aliyewaamuru kufanya hivyo waliomsujudia Yusuf kwao ilikuwa ni maamkizi yaliyoruhusiwa, na ruhusa hiyo ilifutwa katika sheria yetu (ya Kiislamu). Na wanachuoni wamehukumu kuwa, ni kufuru kwa yeyote mwenye kusujudia jua, au mwezi au sanamu, kwa kuwa kufanya hivyo ni alama za kufru ambayo ni kupinga mafunzo ya msingi katika dini kama ambavyo wamehukumu kuwa, mwenye kutamka shahada mbili ni muumini kwa hivyo ndizo dalili za imani, na imani ni kitu cha moyoni. Wamehukumu hivi sio kwa kuwa eti kile kitendo cha kwanza yaani kusujudia mwezi na jua kwa dhati yake ndiyo kufru na kile cha pili (kutamka shahada mbili) ndiyo imani.

Ikiwa kuna uzito wa kufahamu maelezo haya ambayo siyo mazito kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu, hebu iangalie nafsi yako mwenyewe, huenda heshima na adabu uliyonayo kwa baba yako ikakuzuwia kukaa au kulala mbele yake, hivyo ukawa umesimama au kuketi kiasi saa moja au zaidi, na (kufanya hivi) haitakuwa ni ibada uliyomfanyia. Kwa nini basi? Hii ni kwa sababu tendo lako hili halikuambatana na itikadi ya mambo ambayo ni

maalum kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Na utaposimama kiasi cha kusoma Sura Al-Fatihah, na ukakaa kiasi cha kusoma Tashahudi kwa kiasi cha dakika moja au mbili hivi, na ikahesabiwa kuwa umefanya ibada kwa huyo uliyemsalia. Siri ya kuwa matendo haya ni ibada, ni kule kunyenyekea kwako kulikofanyika ndani ya kisimamo chako na kukaa kwako kulikoambatana na itikadi ya Uungu wa yule uliyemnyenyekea ambaye ni Mwenyezi Mungu.

Na (kwa mfano) unamwita kiongozi wako katika kazi au amiri wako ili akusaidie dhidi ya mtu aliyekudhulumu, au akusaidie kutokana na shida iliyokufika na hali wewe hukuitakidi kuwa huyo umwitaye ana uwezo wake wa kujitegemea kuleta manufaa au kuondosha madhara lakini tu Mwenyezi Mungu amemfanya awe ndiyo sababu ya kupitishia mambo ya kawaida mikononi mwake kwa yale ayapendayo yeye Mwenyezi Mungu. (Basi kuomba kwako msaada kwa kiongozi wako au amiri wako) haiwezi kuwa ni ibada kwa yule uliyemuomba kama tulivyokwisha eleza. Lakini iwapo utamwita (akusaidie) hali ya kuwa unaitakidi kwamba yeye ndiye anayenufaisha kwa dhati yake au kudhuru au kupitisha maamuzi bila kupingwa kwa ombi hilo, itakuwa wewe ni mwenye kumuabudia yeye, na kwa ibada hii umemshirikisha Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kuwa umeitakidi ndani ya tendo hilo mambo yanayomuhusu Mwenyezi Mungu, kwani bila shaka kujitegemea kwa dhati, kuleta manufaa au kuondoa madhara na kupitisha maamuzi bila kipingamizi ni katika matendo makhususi ya Mwenyezi Mungu.

Na washirkina walikufuru kwa kuyasujudia masanamu na mfano wake kwa sababu ya kuyaitakidi masanamu hayo kuwa na uwezo wa dhati wa kujitegemea kunufaisha au kudhuru na kupitisha maamuzi bila kuyatenganisha na Mwenyezi Mungu japo kwa njia ya uombezi mbele yake kwani wao wanamuitakidi Mwenyezi Mungu kuwa ndiyo Mungu mkubwa na vile wanavyo viabudia ni waungu chini ya Uungu wa Mwenyezi Mungu, na kwa sababu ya uungu walionao imebidi wapitishe maamuzi wao na Mwenyezi Mungu bila kipingamizi. Aya nyingi za Qur'an zinajulisha kama tulivyoeleza na kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

أَمَّنْ هَـٰذَا الَّذِي هُوَ جُندٌ لَّكُمْ يَنصُرُكُم مِّن دُونِ الرَّحْمَـٰنِ إِنِ الْكَافِرُونَ إِلَّا فِي غُرُورٍ ﴿٢٠﴾

"Ni nani huyu ambaye ni mlinzi wenu atakayekusaidieni pasipo (Mwenyezi Mungu) mwingi wa Rehma, hawako makafiri ila katika kudanganyika". Qur'an, 67:20

Na kauli yake nyingine aliposema:

أَمْ لَهُمْ آلِهَةٌ تَمْنَعُهُم مِّن دُونِنَا لَا يَسْتَطِيعُونَ نَصْرَ أَنفُسِهِمْ وَلَا هُم مِّنَّا يُصْحَبُونَ ﴿٤٣﴾

"Je, wanao Miungu wanaowalinda badala yetu, hawawezi kujisaidia wenyewe na wala hawatahifadhiwa katokana nasi." Qur'an, 21:43

Na Istif-hami iliyoko katika aya hizi mbili ni ya makemeo kwanjia yakuwalaumu katokana na yale waliyoitakidi. Pia Mwenyezi Mungu amesimulia habari za watu wa Nabii Huud [a.s] walipomwambia: "Hatusemi ila ni kuwa baadhi ya Miungu yetu imekwisha kukutia katika balaa". Qur'an, 11:54 Naye Nabii Huud alipowaambia:

"Basi nyote nifanyieni hila (kunidhuru) na musinicheleweshe". Qur'an, 11:55-56.

Nyingine ni kauli yake Mwenyezi Mungu atakayosema kuwalaumu washirikina siku ya Qiyama kutokana na itikadi walizoziitakidi kwa masanamu ikiwa ni pamoja na kuamini kuwa yana uwezo wa kunufaisha na kupitisha maamuzi kama yapendavyo:

وَقِيلَ لَهُمْ أَيْنَ مَا كُنتُمْ تَعْبُدُونَ ﴿٩٢﴾ مِن دُونِ اللَّـهِ هَلْ يَنصُرُونَكُمْ أَوْ يَنتَصِرُونَ ﴿٩٣﴾

"Wako wapi mliokuwa mkiwaabudu, badala ya Mwenyezi Mungu, Je, wanaweza kukusaidieni au kujisaidia wenyewe? Qur'an, 26:92-93.

Nao washirkina watasema hali wakiwa motoni wakizozana na kuwaambia hao waliowaitakidi kuwa ni Miungu na wanazo khususiya za kiungu:

تَاللَّـهِ إِن كُنَّا لَفِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٩٧﴾ إِذْ نُسَوِّيكُم بِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٩٨﴾

"Wallahi bila shaka tulikuwa katika upotofu uliodhahiri, tulipokufanyeni sawa na Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu wote". Qur'an, 26:97-98.

Hebu angalia kulinganisha walikokiri (washirikina) kiasi kwamba muongo anasema kweli na muovu naye anajuta wakati majuto yake hayamsaidii kita. Bila shaka kulinganisha kulikotajwa ikiwa ni kwa ajili ya kuthibitisha kitu katika sifa za Uungu, basi hilo ndilo lengo na kutokana na hali hii ndipo unapatikana ushirikina wao na kufru yao, kwani sifa za Mwenyezi Mungu zinawajibisha upweke kwa maana ya kutokuwa na mfano wake kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kama ilivyotangulia kuelezwa. Na kama kulinganisha huko ni katika kustahiki kwake ibada, basi italazimu kuitakidi ushirika katika yale ambayo ndani yake kuna ustahiki wa ibada, na huo ustahiki ni sifa za Uungu au baadhi ya sifa hizo, na ikiwa (kulinganisha) ni katika nafsi ya ibada yenyewe basi kitendo hicho hakifanywi na mtu mwenye akili ila kwa yule anayeitakidi kustahiki huyo mwenye kuabudiwa kama vile anavyostahiki Mola wa ulimwengu. Basi ni vipi itakanushwa itikadi yao ya Uungu kwa miungu yao hali ya kuwa waliifanya kuwa niwashirika wa Mwenyezi Mungu na wakaipenda kwa mapenzi anayostahiki kupendwa Mwenyezi Mungu kama alivyosema yeye Mwenyezi Munga akieleza habari zao:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَتَّخِذُ مِن دُونِ اللَّـهِ أَندَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ اللَّـهِ ﴿١٦٥﴾

"Na miongoni mwa watu kuna wanaowafanya miungu wasiokuwa Mwenyezi Mungu, wanawapenda kwa mapenzi anayostahiki kupendwa Mwenyezi Mungu". Qur'an, 2:165.

Na neno "Andaad" lililotumika kwenye Aya hiyo hapo juu ni uwingi wa "Nidd" na maana yake ni kama walivyosema wataalam wa tafsiri na lugha. Ama kauli ya Mwenyezi Mungu akiwazungumzia washirikina akasema:

وَلَئِن سَأَلْتَهُم مَّنْ خَلَقَهُمْ لَيَقُولُنَّ اللَّـهُ فَأَنَّىٰ يُؤْفَكُونَ ﴿٨٧﴾

"Na ukiwauliza ni nani aliyewaumba, bila shaka watasema, ni Mwenyezi Mungu". Qur'an, 43:87.

Kauli hii na nyinginezo mfano wa hii maana yake siyo kwamba wao (washirikina) hawauthibitishi uungu wa miungu yao na yale mambo maalum yanayohusu uungu, bali maana yake ni kwamba, wanapohojiwa hukiri kutokana na ukweli ambao Mwenyezi Mungu ameziumbia nafsi (kumtambua). Lakini ni kwa kiasi gani wao hurejea haraka katika itikadi zao

za waungu wa uongo kwa miungu yao, hurudi na katumbukia humo kama alivyosema Mwenyezi Mungu katika aya nyingine.

يَعْرِفُونَ نِعْمَتَ اللَّـهِ ثُمَّ يُنكِرُونَهَا وَأَكْثَرُهُمُ الْكَافِرُونَ ﴿٨٣﴾

"Wanazijua neema za Mwenyezi Mungu kisha wanazikanusha na wengi wao ni makafiri". Qur'an, 16:83.

Na kauli nyingine ya Mwenyezi Mungu akizungumzia kikundi miongoni mwao: "Kila wakirudishwa katika fitna, huangushwa humo". Qur'an, 4:91

Kurudishwa katika fitna na kuangushwa humo siyo jambo la ajabu kutokea kwa wale walioyafanya matamanio yao kuwa miungu yao, nawe msomaji utawaona hao wenye matamanio hayo iwapo utamjadili katika Bid'a zake, atakusikiliza kwa makini na atakinaika (atatosheka) wakati wa majadiliano na atakiri kuwa amekwenda kinyume cha haki na ataonyesha dalili za uadilifu (katika majadiliano na matokeo yake). Kinapomalizika kikao cha mjadala hurudi kule kwenye mazoea ya matamanio na kurudia Bid'a yake kama kwamba hapakuwa na mjadala baina yako na yeye (isipokawa waliorehemewa na Mwenyezi Mungu). Na hali kama hii tumeiona mara nyingi kwa wale tuliokutana nao miongoni mwa wanaofuata matamanio. Tunamuomba Mwenyezi Mungu kwa fadhila zake atupe mafanikio. Pamoja na yote haya, lau itakubalika kwamba (washirikina) hawakuitakidi kwa miungu yao kuwa na uwezo wa kuumba, kuruzuku wala kuendesha mambo, lakini wanaitakidi ndani ya miungu hiyo mambo yasiyokuwa hayo ambayo yanahusu mas-ala ya uungu nao ni wajibu wa kupitisha maamuzi wayatakayo. Basi wao wanaona kuwa shafaa ya masanamu hayo inakubaliwa moja kwa moja hairudishwi na haitegemei idhini ya Mwenyezi Mungu. "Ametakasika sana Mwenyezi Mungu na yale wayasemayo wajinga." Kwa ajili hiyo Mwenyezi Mungu amesema katika Qur'an akijibu madai yao haya:

مَن ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِندَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ ﴿٢٥٥﴾

"Ni nani huyo awezaye kuombea mbele yake (Mwenyezi Mungu) bila idhiniyake? Qur'an, 2:255

Amesema Qadhi Nasirudin Al-Baidawi katika tafsiri ya aya hiyo, "Ni ubainifu wa utukufu wa mambo yake, na hiyo ni kwa sababu hakuna anayeungana naye au kumkurubia awezaye kutoa akitakacho iwe kwa shafaa au kunyenyekea, basi itakuwaje iwezekane kwa njia ya kumpinga": Hivyo basi iangalie kauli ya Baidawi aliposema; "Awezaye kutoa akitakacho ikiwa ni kwa Shafaa" utakuta ni dhahiri kuwa inahusu wajibu wa matakwa yake yakubalike kwanza kwa Mwenyezi Mungu na wajibu wa kupitisha maamuzi ni miongoni mwa mambo yanayohusu uungu kama inavyofahamika. Na aina hii ya Shafaa ni Shafaa ya shirki ambayo Qur'an imeibatilisha, kwani kuiamini Shafaa ya aina hii ni kufru kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

"Au ndiyo wamejifanyia waombezi kinyume cha Mwenyezi Mungu?" Qur'an, 39:43 Na kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

قُلْ مَن ذَا الَّذِي يَعْصِمُكُم مِّنَ اللَّـهِ إِنْ أَرَادَ بِكُمْ سُوءًا أَوْ أَرَادَ بِكُمْ ...﴿١٧﴾

"Waambie, ni nani ambaye anaweza kukulindeni kutokana na Mwenyezi Mungu kama akikutakieni ubaya au (nani anayeweza kuzuwiya Rehma yake) kama akikutakieni Rehma?" Qur'an, 33:27.

Ama Shafaa ambayo wanaiitakidi watu wa Tauhidi na ndiyo iliyoletwa na Qur'an na Sunna, yenyewe iko mbali na itikadi ya Shafaa inayoitakidiwa na washirikina kama ulivyo umbali wa imani na kufru na umbali wa mwangaza na kiza. Na Shafaa ya watu wa Tauhidi ni maombi ya mwenye kushufaiya kumuombea mwenye kushufaiwa, na Mwenyezi Mungu kwa fadhila zake humkubalia amtakaye na hiyo ndiyo maana ya Istith-nai katika kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema: "Isipokuwa kwa idnini yake". Na maana ya idhini hapa ni kuridhia kama alivyosema kwenye aya nyingine: "Wala hawamuombei yeyote ila yule aliyeridhiwa (na Mwenyezi Mungu). Qur'an, 21:28. Na nyingine tena:

وَكَم مِّن مَّلَكٍ فِي السَّمَاوَاتِ لَا تُغْنِي شَفَاعَتُهُمْ شَيْئًا إِلَّا مِن بَعْدِ أَن يَأْذَنَ اللَّـهُ لِمَن يَشَاءُ وَيَرْضَىٰ ﴿٢٦﴾

"Na wako Malaika wangapi mbinguni ambao uombezi wao hautafaa chochote isipokuwa baada ya Mwenyezi Mungu kutoa idhini kwa amtakaye na kumridhia". Qur'an, 53:26.

Na kwa maelezo haya inakubainikia tofauti baina ya yale iliyoyathibitisha Qur'an katika Shafaa na yale iliyoyakanusha (ambayo hayana idhini yake na radhi yake.) Mwenyezi Mungu ni mkubwa, hakifanyiki kitu katika ufalme wake ila yeye atake. Ama Shafaa kwa idhini yake na radhi yake inayotokana na waja wake wema walio wateule kuwaombea wenye kuasi katika watu wa Tauhidi inafaa, na limethibiti hilo kwa njia ya mutawatir wala hapana kizuizi ndani yake na kuitakidi hivyo ni katika mambo ya dini, kwani jambo hili liko katika mlango wa Dua, naye Mwenyezi Mungu huwakubalia waaminio na wakatenda mema na huwazidishia fadhila zake. Tunataraji itakuwa imeeleweka kwako msomaji (Insha-Allah) nini maana ya ibada kisheria, na wakati huo huo utakuwa umefahamu kuwa siyo ibada ya asiyekuwa Mwenyezi Mungu pale Mwislamu anapotaka wasila kwa Mwenyezi Mungu.[1] Basi haya yalikuwa ndiyo maneno yaliyoandikwa na Al Allamah Al-Qudhai, nasi tumeyaleta kutokana na faida nyingi zilizomo, na bila shaka tumeifafanua hali yake, ni juu yako ewe msomaji muadilifu kufanya uchunguzi.

1. Fur-qanul-Qur'an, uk. 111-115.

13

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## KUOMBA MSAADA KWA MAWALII WA MWENYEZI MUNGU KATIKA UHAI WAO

Bila shaka kuomba kitu chochote katoka kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu kuna namna nyingi, nasi tutazionyesha katika mpango ufuatao:

1. Kumuomba mtu aliye hai atusaidie katika ujenzi wa nyumba au kunywesha maji.

2. Kumuomba mtu aliye hai atuombee kwa Mwenyezi Mungu atusamehe.

Namna hizi mbili zinashirikiana kwa kuwa jambo litakiwalo ni la kawaida kimaumbile, na huyo aombwaye anao uwezo wa kulifanya, lakini namna hizi zinatofautiana kwa kuwa ile ya kwanza imefungamana na mambo ya kidunia, na ile ya pili inamafungamano na akhera.

3. Kumuomba mtu aliye hai atufanyie kazi bila ya kutumia sababu za kimaada, kwa mfano kumuomba amponye mgonjwa bila ya dawa, au kumuomba kukirejesha kitu kilichopotea bila kukitafuta, au kumuomba kalipa deni bila ya kufanya kazi ili kaipata mali (ya kulipia deni).

Kwa maelezo mengine, tunamuomba kufanya kazi kwa njia ya muujiza au karama[1].

4. Kumuomba mtu aliyekufa atuombee kwa Mwenyezi Mungu, na ombi letu kwa mtu huyo litatokana na itikadi yetu kwamba yeye yu hai katika ulimwengu wa Akhera na anaruzukiwa huko.

5. Kumuomba mtu atake msaada kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu (uwezo ambao Mwenyezi Mungu amempa) kumponyesha mgonjwa wetu au aturejeshee kitu chetu kilichopotea au jambo jingine lolote lile. Namna hizi mbili ni kama ile ya pili na ya tatu, lakini tofauti baina yao ni kwamba, kule maombi ni kwa mtu aliye hai katika ulimwengu wa kimaada, na hapa maombi yetu ni kwa mtu aliyekufa kidhahiri lakini kihakika yu hai. Na kwa msingi huu basi, hatuwezi kumuomba mtu aliyekufa atusaidie katika mambo ya kimaada kwa kupitia sababu za kimaada, na hiyo ni kwa sababu ya kutokuwepo utendaji wa kimaada wa maiti katika ulimwengu huu kwa kuwa yeye amekwisha ondoka duniani. Ewe msomaji mpendwa, hizi ni sehemu tano za namna ya kuomba msaada, tatu miongoni mwake zinamuhusu mtu aliye hai ndani ya ulimwengu huu wa kimaada, na mbili zinahusika na mtu aliye katika ulimwengu wa akhera.

Sisi sasa hivi tutazungumzia zile namna tatu za mwanzo na "tunaakhirisha mazungumzo ya kuwaomba msaada Mawalii wa Mwenyezi Mungu walio hai katika ulimwengu wa akhera, jambo hilo tutalizungumzia

---

1."Muujiza" ni tamko linalotumika juu ya kitu ambacho kinatoka kwa Maasumu (kama vile Nabii na Imam) ambacho ni miongoni mwa mambo yaliyo kinyume na mazoea ili kuthibitisha utume wake au Uimamu wake.

"Karama" ni tamko linalotumika juu ya kitu ambacho hutoka kwa wasiyokuwa Manabii au Maimamu miongoni mwa mawalii wema wa Mwenyezi Mungu, kama tendo lililokuja katika Qur'an Tukufu kuhusu haki ya Bibi Maryam, bila ya yeye kutumia sababu za kimaumbile.

katika mlango ujao apendapo Mwenyezi Mungu. Na sasa hebu zingatia uchunguzi ndani ya zile namna tatu: Namna ya Kwanza: Bila shaka kuomba msaada kwa watu walio hai ndani ya mambo ya kawaida ambayo yanazo sababu za kimaumbile ni jambo linaloweka msingi wa utamaduni wa binadamu, kwani maisha ya wanadamu duniani kote yamesimama katika msingi wa kusaidiana na kushirikiana na watu wenye akili ulimwenguni wanasaidiana na kushirikiana katika mambo ya maisha. Kwa hiyo, hukumu ya msaada wa aina hii inaeleweka wazi mno kiasi kwamba hapana yeyote aliyeikanusha wala kuipinga.

Na kwa kuwa utafiti wetu umetegemea muongozo wa Qur'an na hadithi, basi bila shaka tutayatatua mas'ala haya ndani ya msingi wa Qur'an, na tunatosheka na aya moja tu. Wakati Dhul-Qar-nain alipotaka kujenga ngome dhidi ya mashambulizi ya "Yaajuju" na 'Maajuju" aliwaelekea wakazi wa sehemu hiyo akawaambia:

"Nisaidieni kwa nguvu (zenu wafanyakazi) nitaweka baina yenu na baina yao kizuwizi kilicho imara." Qur'an, 18:94 Namna ya Pili: Kuomba msaada kwa mtu aliye hai (ndani ya ulimwengu huu wa kimaada) ili aombe maombi ya kheri na kutaka msamaha kwa Mwenyezi Mungu, ni katika mambo ya lazima tena yako wazi wala hapana tofauti katika mambo haya baina ya watu wawili. Qur'an Tukufu inasisitiza jambo hilo mahala pengi na tukitazama haraka haraka katika aya tukufu inatuthibitishia kwamba Manabii walikuwa na kawaida ya kuwaombea watu wao mambo ya kheri na uongofu na mafanikio, au kwamba watu wenyewe walikuwa wakiwaomba manabii wao wawaombee mambo mema na maghfira. Aya za Qur'an ni nyingi mno nazo zimegawanyika (katika vigawo) nasi tunazitaja kwa tarakimu kama ifuatavyo:

1. Mwenyezi Mungu anamuamini Mtume wake Muhammad **[s.a.w.w]** awatakie maghfira umati wake anasema: "Basi wasamehe na uwaombee msamaha (kwa Mwenyezi Mungu) na upime maoni yao katika mambo". Qur'an, 3:159.

2. "Peana nao ahadi na uwatakie maghfira kwa Mwenyezi Mungu bila shaka Mwenyezi Mungu ni mwingi wa maghfira mwingi wa Rehma". Qur'an, 3:159.

3. "Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe na kuwatakasa kwa sadaka hiyo na uwaombee, hakika maombi yako juu yao kutawapa utulivu, na Mwenyezi Mungu ni mwenye kusikia, mwenye kujua." Qur'an, 9:103.

Na ndani ya aya hii ya mwisho Mwenyezi Mungu anamuamuru Nabii wake Muhammad **[s.a.w.w]** awaombee waumini na kwamba maombi yake yataleta utulivu ndani ya nyoyo zao. Na wakati mwingine Manabii walikuwa wakiwaahidi wenye madhambi na waasi kuwa watawaombea maghfira katika wakati unaokubalika. Kwa mfano Mwenyezi Mungu anasema: "Ila katika usemi wake Ibrahimu kumwambia baba yake, "Bila shaka nitakuombea msamaha". Qur'an, 60:4.

"Nitakuombea msamaha kwa Mola wangu bila shaka yeye ananihurumia sana". Qur'an, 19:47.

Na haikuwa kwa Ibrahim kutaka maghfira kwa ajili ya baba yake, ila ni kwa sababu ya ahadi aliyompa. Qur'an, 9:144.

Aya hizi tukufu zinajulisha kwamba Manabii walikuwa wakiwabashiria wenye dhambi kuwaombea msamaha, hata Nabii Ibrahim [a.s] alimuahidi "Aazar" kumuombea msamaha, lakini Ibrahim [a.s] alipomuona "Aazar" anaendelea kuabudu masanamu alibadilisha ahadi yake, kwani miongoni mwa sharti za kukubaliwa maombi ni lazima anayeombewa awe anamuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu.

5. Mwenyezi Mungu amewaamuru waumini wenye madhambi waende kwa Mtume **[s.a.w.w]** na waombe awaombee msamaha, kwani Mwenyezi Mungu atawasamehe kwa baraka ya Mtume kuwaombea msamaha. Mwenyezi Mungu anasema:

وَلَوْ أَنَّهُمْ إِذ ظَّلَمُوا أَنفُسَهُمْ جَاءُوكَ فَاسْتَغْفَرُوا اللَّـهَ وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ الرَّسُولُ لَوَجَدُوا اللَّـهَ تَوَّابًا رَّحِيمًا ﴿٦٤﴾

"Na lau wangelikuja kwako walipojidhulumu nafsi zao wakaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu, mjumbe wa Mwenyezi Mungu naye akawaombea msamaha, bila shaka wangemkuta Mwenyezi Mungu ni mwenye kupokea toba na mwenye kurehemu. Qur'an, 4:64.

Ni aya gani basi iliyo wazi kuliko hii ambayo Mwenyezi Mungu anawaamuru wenye dhambi (katika umma huu) waende kwa Mtume **[s.a.w.w]** na wamuombe awaombee msamaha? Bila shaka kwenda kwa Mtume **[s.a.w.w]** na kumuomba kuombea msamaha kuna faida mbili: Ya Kwanza: Jambo hili humfanya mtu kuwa na roho ya utiifu na kumfuata Mtume **[s.a.w.w]** na hii itakuja kutokana na kuelekea na kuufahamu utukufu wa Mtume **[s.a.w.w]** na heshima yake mbele ya Mwenyezi Mungu kiasi kwamba kumtaka Mtume aombe msamaha kunaleta maghfira ya Mwenyezi Mungu. Na kwa ujumla kufika mbele ya Mtume **[s.a.w.w]** na kumuomba aombee maghfira kunawajibisha unyenyekevu kwa Mtume na humuandaa mtu kinafsi awe tayari kufuata kauli ya Mwenyezi mungu isemayo: "Mtiini Mwenyezi Mungu na mumtii Mtume." Qur'an, 4:59.

Ya Pili: Jambo hili linajulisha wazi wazi daraja ya Mtume **[s.a.w.w]** mbele ya umma, na kuwabainishia kwamba, matokeo ya kimaada kama ambavyo yenyewe yanategemea sababu za kimaumbile, vile vile matokeo ya kiroho, kwa mfano maghfira ya Mwenyezi Mungu yanakuja kwa kupitia sababu maalum, kama vile dua ya Mtume na Mawalii wa Mwenyezi Mungu kumuombea mtu. Kama lilivyojua, ndiyo asili ya mwanga, nguvu na joto na ikawa neema zinawashukia waja wa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya jua, basi neema za Mwenyezi Mungu na kheri zake zinawashukia waja wa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya jua la utume linalong'ara na kuwaenea kwa kheri na rehma.

Bila shaka ulimwengu huu ni ulimwengu wa sababu na visababishaji na neema za kimaada na kiroho zinakuja kwa kupitia sababu zinazozihusu.

4. Kuna baadhi ya aya za Qur'an Tukufu zinafahamisha kwamba, kuna Waislamu ambao walikuwa wakifika kwa Mtume **[s.a.w.w]** mara kwa mara na kumuomba awaombee dua na maghfira, na Waislamu hao hao walipowataka wanafiki waende kwa Mtume **[s.a.w.w]** na wamuombe awaombee dua na maghfira, walikataa kama asemavyo Mwenyezi Mungu.

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا يَسْتَغْفِرْ لَكُمْ رَسُولُ اللَّـهِ لَوَّوْا رُءُوسَهُمْ وَرَأَيْتَهُمْ يَصُدُّونَ وَهُم مُّسْتَكْبِرُونَ ﴿٥﴾

"Na wanapoambiwa njooni ili mjumbe wa Mwenyezi Mungu akuombeeni msamaha, hugeuza vichwa vyao na utawaona wanajizuwia na kujiona wakubwa. Qur'an, 63:5.

5. Na kuna baadhi ya aya za Qur'an zinazoshuhudia kwamba, watu kutokana na maumbile yao matukufu walikuwa wakifahamu ya kuwa, dua ya Mtume inayo athari ya pekee kwao, na kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu hukubali maombi yao bila ya shaka, na kwa ajili hii basi walikuwa wakimuomba awaombee dua na msamaha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Bila shaka watu kwa maumbile yao yaliyosalimika walikuwa wakijua kwamba neema na rehma za Mwenyezi Mungu huzidi kwa kupitia maombi ya Manabii kama ambavyo uongofu wa watu hukamilika kwa kupitia kwa Manabii. Na kwa ajili hii basi, wakawa wanawakusudia na kuwaomba wawaombee msamaha, kama ilivyokuja katika Qur'an tukufu jun ya kisa cha ndugu wa Nabii Yusufu [a.s] baada ya kulitambua kosa lao na mahusiano yao mabaya kwa ndugu yao Yusuf [a.s] Mwenyezi Mungu anasema:

قَالُوا يَا أَبَانَا اسْتَغْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا إِنَّا كُنَّا خَاطِئِينَ ﴿٩٧﴾ قَالَ سَوْفَ أَسْتَغْفِرُ لَكُمْ رَبِّي إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٩٨﴾

"Wakasema, Ewe Baba yetu tuombee msamaha kwa dhambi zetu, bila shaka sisi tulikuwa wenye makosa, akasema (Baba yao) nitakuombeeni msamaha kwa Mola wangu, hakika yeye ndiye mwenye kusamehe na mwingi wa kurehemu." Qur'an, 12:97-98.

6. Ziko aya nyingine ambazo Mwenyezi Mungu anamtahadharisha Mtume **[s.a.w.w]** kuwaombea dua na msamaha wanafiki ambao wanaendelea kuabudia masanamu, na hii ni kwa sababu ibada yao hiyo siyo ibada ya Mwenyezi Mungu, hivyo basi inazuwiya wao kupata msamaha wa Mwenyezi Mungu hata kama Mtume atawaombea msamaha. Kuzuwiwa kukubaliwa msamaha kwa watu hao ni jambo linalojulisha kwamba, maombi ya Mtume kuwaombea msamaha (watu) yanakubaliwa isipokuwa kwa wale wanaoendelea na ibada ya masanamu (maombi yao) hayawezi kukubaliwa (japo Mtume ndiye atakayeomba), kwa kuwa ibada ya masanamu inazuwiya kukubalika kwa maombi. Kwa hiyo mfano wa maombi ya Nabii kwa watu hao ni kama maji yanayotiririka juu ya ardhi ngumu isiyoweza kupenya maji ndani yake. Mwenyezi Mungu anasema:

إِن تَسْتَغْفِرْ لَهُمْ سَبْعِينَ مَرَّةً فَلَن يَغْفِرَ اللَّـهُ لَهُمْ ﴿٨٠﴾

"Hata ukiwaombea msamaha mara sabini Mwenyezi Mungu hatawasamehe" Qur'an, 9:80.

سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ أَسْتَغْفَرْتَ لَهُمْ أَمْ لَمْ تَسْتَغْفِرْ لَهُمْ لَن يَغْفِرَ اللَّـهُ لَهُمْ ﴿٦﴾

"Ni sawa kwao ukiwaombea msamaha au usiwaombee msamaha, Mwenyezi Mungu hatawasamehe". Qur'an, 63:6.

وَلَمَّا وَقَعَ عَلَيْهِمُ الرِّجْزُ قَالُوا يَا مُوسَى ادْعُ لَنَا رَبَّكَ بِمَا عَهِدَ عِندَكَ لَئِن كَشَفْتَ عَنَّا الرِّجْزَ لَنُؤْمِنَنَّ لَكَ وَلَنُرْسِلَنَّ مَعَكَ بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿١٣٤﴾

"Ilipowaangukia adhabu walisema: Ewe Musa tuombee kwa Mola wako kwa yale aliyokuahidi, kama utatuondolea adhabu bila shaka tutakuamini na kwa yakini tutawapeleka wana wa Israel pamoja nawe." Qur'an, 7:134.

Bila shaka katika aya (hii iliyotangulia) watu wenye madhambi walimtaka Nabii Musa [a.s] awaombee. Na ile sentensi isemayo; "Kwa yale aliyokuahidi Mola wako" inajulisha kwamba watu hao walikuwa wakifahamu kuwa Mwenyezi Mungu anayoahadi aliyomuahidi Musa [a.s]. Ama kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema; "Tuombee kwa Mola wako" ina mielekeo namna mbili:

Mwelekeo wa Kwanza: Kuomba kwao kuondolewa adhabu kuwe ni kwa njia ya muujiza, na hii ni kwa sababu ya imani yao juu ya uwezo wa Nabii Musa [a.s] kwa kusaidiwa na uwezo wa Mwenyezi Mungu juu ya jambo hilo. Pamoja na kusihi kwa muelekeo huu, aya hii inaingia ndani ya ile namna ya tatu ya uchunguzi tuliokwishataja, nayo ni kule kumuomba msaada mtu aliye hai kusimamia kazi ambayo ni ya kimuujiza unaokuwa kinyume na sababu za maumbile ya kawaida, na hapo baadaye utakuja uchunguzi wake Insha-Allah Ta'ala. Mwelekeo wa Pili: Ni kutaka kuomba kuondolewa adhabu wala siyo kwa muujiza unaokhalifu mazoweya. Mwelekeo huu wa pili uko dhahiri kwa sababu Maf-humu ya sentensi isemayo "Tuombee kwa Mola wako" inafahamisha kuwa ni kiasi cha kuwa waombewe ili kuondolewa adhabu. Naam.... katika aya hii hakuna ishara inayoonyesha kuwa Mwenyezi Mungu hatakubali maombi ya Musa [a.s] kuwaombea washirikina na waabudu sanamu, bali ishara hiyo imetangulia katika aya zingine.

7. Kuna baadhi ya aya za Qur'an ambazo zinafahamisha kuwa, wapo baadhi ya waumini ambao walikuwa wakiwaombea msamaha baadhi ya waumini wenzao kama ilivyo katika kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

وَالَّذِينَ جَاءُوا مِن بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ ﴿١٠﴾

"Na wale waliokuja baada yao wanasema, Mola wetu tusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia katika imani". Qur'an, 59:10.

8. Zaidi ya waumini hao wanaowaombea msamaha (waumini wenzao) Malaika wanaochukua Ar-shi nao wanawatakia maghfira waumini kama ilivyo kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema:

الَّذِينَ يَحْمِلُونَ الْعَرْشَ وَمَنْ حَوْلَهُ يُسَبِّحُونَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَيُؤْمِنُونَ بِهِ وَيَسْتَغْفِرُونَ لِلَّذِينَ آمَنُوا

رَبَّنَا وَسِعْتَ كُلَّ شَيْءٍ رَّحْمَةً وَعِلْمًا فَاغْفِرْ لِلَّذِينَ تَابُوا وَاتَّبَعُوا سَبِيلَكَ وَقِهِمْ عَذَابَ الْجَحِيمِ ﴿٧﴾

"(Malaika) wanaoichukua arshi na wale wanaoizunguka wanamtukuza Mola wao na kumsifu na wanamuamini na wanawaombea msamaha walioamini, (na wanasema) Mola wetu umekienea kila kitu kwa Rehma na Elimu, basi wasamehe waliotubu na wakaifuata njia yako na waepushe na adhabu ya moto." Qur'an, 40:7.

Kwa msingi huu basi, ni uzuri ulioje kwetu sisi kuwafuata hawa katika mwendo huu unaoridhiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu ili tuwaombee msamaha wenye madhambi. Mpaka hapa umekamilika utafiti wa ile namna ya kwanza na ya pili, na sasa hebu angalia namna ya tatu. Namna ya Tatu: Namna ya Tatu ni kuomba msaada kwa mtu aliye hai mwenye uwezo wa kafanya muujiza na kuikhalifu ada (mazowea) ili afanye jambo fulani kwa

njia hiyo ya muujiza bila kutegemea sababu za maumbile ya kawaida kama vile kumponyesha mgonjwa na kupasua chemchemi ya maji mahala pakavu na mfano wa hayo. Baadhi ya waandishi wakubwa, wanaiona aina hii ya msaada kuwa inaingia katika ile namna ya pili na wanasema: "Makasudio ya muujiza ni mtu kumuomba Mola wake amponye mgonjwa wake au kumlipia deni lake na mengineyo, kwani vitendo hivi vinamuhusu Mwenyezi Mungu peke yake na hayawi maombi ya Nabii au Imam isipokuwa ni wasila tu kwa Mwenyezi Mungu. Na kwa ajili hii basi kuvinasibisha vitendo hivi kwa Nabii au lmam ni katika mlango wa majazi na siyo hakika."[1] Lakini ndani ya Qur'an ziko aya zinazojulisha wazi wazi kuwa kuomba haja hizi kwa Manabii na Mawalii ni jambo sahihi na siyo majazi, kwani sisi tunapomuomba Maasum yeye mwenyewe (mwenye uwezo wa kufanya muujiza) amponye mgonjwa ambaye kuna uzito wa kupona kwake, basi jambo hilo (la kumponyesha) litathibitika kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na nguvu zake. Ni sawa sawa kwamba, Qur'an inakizingatia kitendo cha kuponya ni miongoni mwa mambo makhsusi ya Mwenyezi Mungu. Anasema Mwenyezi Mungu: "Na ninapokuwa mgonjwa Yeye ndiye aniponyeshaye." Qur'an, 26:80.

Lakini katika kipindi hicho hicho Qur'an inauhusisha uponyeshaji kwenye Qur'an yenyewe na vile vile asali na inasema:

وَنُنَزِّلُ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ وَلَا يَزِيدُ الظَّالِمِينَ إِلَّا خَسَارًا ﴿٨٢﴾

"Na tunateremsha katika Qur'an mambo ambayo ni uponyo na rehma kwa walioamini." Qur'an, 17:82.

يَخْرُجُ مِن بُطُونِهَا شَرَابٌ مُّخْتَلِفٌ أَلْوَانُهُ فِيهِ شِفَاءٌ لِّلنَّاسِ ﴿٦٩﴾

"Kinatoka katika matumbo yao (nyuki) kinywaji chenye rangi mbali mbali ndani yake kinauponyo kwa watu" Qur'an, 16:69.

يَا أَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَتْكُم مَّوْعِظَةٌ مِّن رَّبِّكُمْ وَشِفَاءٌ لِّمَا فِي الصُّدُورِ ﴿٥٧﴾

"Bila shaka yamekufikieni mawaidha kutoka kwa Mola wenu na ni uponyo wa yale yaliyomo katika nyoyo." Quran, 10:57.

Suali lililopo sasa hivi ni Je, namna gani tunaweza kuleta muafaka baina ya aya hizi? Jawabu: Mtazamo wa sawa ili kuziweka pamoja aya hizi, yaani zile zilinazohusisha uponyo kwa Mwenyezi Mungu na zile zinazouthibitisha uponyo kwenye asali na Qur'an na Mawaidha ya Mwenyezi Mungu ni kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye mtendaji pekee wa mambo kwa kujitegememea kwa dhati yake mwenyewe katika kila kitu, wakati ambapo asali na Qur'an na mawaidha ya Mwenyezi Mungu, vyote hivi vinaathiri katika vitu kwa idhini ya Mwenyezi Mungu na kutaka kwake. Bila shaka mtazamo wa Uislamu juu ya ulimwengu na maisha unayazingatia mambo yote na watendaji wote kuwa ni wenye kufuata utashi wa Mwenyezi Mungu na uwezo wao wa kutenda, umo ndani ya idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na pia sababu zote na illa zote kamwe hazijitegemei japo kidogo katika athari zake pasina tofauti baina ya sababu za kimaumbile na zile za kiroho.

1. Kash-Ful-Irtiyabi, uk 274.

Na kwa msingi huu basi, hapana kizuwizi chochote kwa mujibu wa Qur'an na akili kuwa, Mwenyezi Mungu ambaye ameweka uponyo ndani ya asali na dawa za mimea na zile za kemikali, hakuna kizuwizi cha kuwapa uwezo kama huo Manabii na Maimamu [a.s]. Hebu watazame watu wanaokaa Riyadha[1] ni vipi wanaweza kufanya baadhi ya mambo ya ajabu, basi kuna kizuwizi gani kwa Mwenyezi Mungu kuwapa Manabii na Maimamu uwezo wa kuponyesha na kuwafanya waweze kutenda mambo yanayoishangaza akili na yenye kukhalifu sababu za kimaumbile ya kimaada? Bila shaka uwezo wa Manabii na Maimamu [a.s] juu ya kuponyesha maradhi na kutenda matendo ya kipekee haupingi kuwa Mwenyezi Mungu ndiye sababu halisi na ya msingi wa matendo hayo, lakini tu amewapa uwezo huo ili kuutumia katika ulimwengu kwa idhini yake kila inapohitajika na kwa maslahi.

Na ukweli ulivyo ni kwamba, ndani ya Qur'an Tukufu kuna aya nyingi zinazofafanua wazi kwamba, watu walikuwa wakiwafuata Manabii na wasiokuwa Manabii vile vile ili wafanye mambo ya kipekee yaliyo kinyume na mazoweya na maumbile. Hebu soma baadhi ya aya hizo:

وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ إِذِ اسْتَسْقَاهُ قَوْمُهُ أَنِ اضْرِب بِّعَصَاكَ الْحَجَرَ ﴿١٦٠﴾

"Na tulimfunulia wahyi Musa pale watu wake walipomuomba maji (tukamwambia) lipige jiwe kwa fimbo yako". - Qur'an, 7:160.

Dhahiri ya aya hii inajulisha kwamba wana wa Israil walimtaka Nabii Musa [a.s] baada ya kupatwa na ukame na maji yakakosekana, awape maji kwa njia ya muujiza na siyo kwa njia za kawaida. Na utaona wazi ndani ya aya kwamba, wana wa Israel hawakumtaka Musa [a.s] amuombe Mwenyezi Mungu wapate maji, bali walimtaka awape maji mara moja na bila kutumia sababu za kimaada na ndipo Mwenyezi Mungu alipomuamuru alipige jiwe kwa fimbo yake ili yatoke maji katika jiwe hilo kwa njia ya muujiza. Mwenyezi Mungu Anasema: "Basi mara ghafla zikabubujika chemchem kumi na mbili." - Qur'an, 2:60.

Aya nyingine iliyo wazi zaidi kuliko hii ni ile inayozungumzia kisa cha Nabii Suleiman [a.s] wakati alipowataka waliokuwa wamehudhuria mbele yake wamletee kiti cha "Bal-Qiis" bila kujali ugumu na vizuwizi vilivyokuwepo njiani (kwani Nabii Suleiman [a.s] alikuwa akiishi Jordan na kiti cha Bal-Qiis kilikuwa Yemen).

Mwenyezi Mungu anasema, akiisimulia kauli ya Suleiman kwa waliokuwa mbele yake:

قَالَ يَا أَيُّهَا الْمَلَأُ أَيُّكُمْ يَأْتِينِي بِعَرْشِهَا قَبْلَ أَن يَأْتُونِي مُسْلِمِينَ ﴿٣٨﴾

"Ni nani atakayeniletea kiti chake cha enzi kabla hawajaja kwangu bali yakuwa wamekwisha kusilimu". Qur'an, 27:38.

Bila shaka lengo la Suleiman [a.s] lilikuwa ni kukileta kiti cha Bal-Qiis kwa njia isiyo ya kawaida, na hilo lilitimia kwa vitendo kutokana na kutumika njia isiyo ya kawaida kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

1. Mwenye kukaa Riyadha ni yule ambaye hufanya mazoezi magumu ya kiroho ili kuiwezesha roho kufanya mambo yo ajabu, hasa hasa mambo hayo kuwa ni ya kishetani na sio ya kiungu. kwa hiyo huwa yanaondoka mambo hayo anapoacha mazoezi hayo.

قَالَ الَّذِي عِندَهُ عِلْمٌ مِّنَ الْكِتَابِ أَنَا آتِيكَ بِهِ قَبْلَ أَن يَرْتَدَّ إِلَيْكَ طَرْفُكَ فَلَمَّا رَآهُ مُسْتَقِرًّا عِندَهُ ﴿٤٠﴾

"Akasema yule ambaye anayo elumi kutoka katika kitabu, mimi nitakuletea kabla ya kupepesa jicho lako (kufumba na kufumbua) basi alikiona kimewekwa mbele yake". Qur'an, 27:40.

Bila shaka kiini cha maudhui ni ule mtazamo wa baadhi ya watu kwamba, matendo ya kawaida ndiyo yanayomstahikia mtu na matendo ya kipekee ambayo kwa kawaida watu hawayawezi, hayo yanamuhusu Mwenyezi Mungu peke yake, na mtazamo huu ni wa kimakosa kwa sababu kipimo cha kutenganisha baina ya matendo ya Mwenyezi Mungu na yale ya asiyekuwa yeye ni kwamba Mwenyezi Mungu anafanya kwa kujitegemea na wengine wanafanya si kwa kujitegemea. Matendo ya kiungu ni yale ambayo mtendaji mwenyewe (yaani Mwenyezi Mungu) huyatenda bila ya mwingine yeyote kuingilia kati na bila msaada wa nguvu ya wengine.

Na kwa maneno mengine tunaweza kusema kuwa, matendo ya kiungu ni yale ambayo mtendaji anakuwa ni mwenye kujitegemea kikamilifu kuyatenda na wala hamhitajii mwingine kabisa kuyatekeleza. Ama matendo yasiyo ya kiungu, sawa sawa yakiwa ni matendo madogo madogo na ya kawaida tu, au yakawa magumu na yasiyo ya kawaida ni yale ambayo mtendaji wake hawi mwenye kujitegemea katika kuyafanya, bali yanakamilika utendaji wake chini ya kivuli cha uwezo kinachojitegemea na nguvu kutoka kwake, nao ni uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa msingi huu basi, hapana kizuwizi kwa Mwenyezi Mungu kuwapa uwezo Mawalii wake wa kufanya matendo yaliyo kinyume na mazowea na maumbile na ambayo kwa kawaida watu wanashindwa kuyafanya. Mwenyezi Mungu anasema kumwambia Nabii Isa [a.s]:

وَتُبْرِئُ الْأَكْمَهَ وَالْأَبْرَصَ بِإِذْنِي وَإِذْ تُخْرِجُ الْمَوْتَىٰ بِإِذْنِي ﴿١١٠﴾

"Unaponyesha vipofu na wenye mbaranga kwa idhini yangu na ulipowatoa wafu (makaburini mwao) kwa idhini yangu...." Qur'an, 5:110.

Basi ni kwa kiasi gani aya hii imefafanua dalili ya maudhui haya? Bila shaka mkusanyiko wa aya hizi unajulisha kwamba, Mawalii wa Mwenyezi Mungu walikuwa na uwezo huu na kwamba maombi ya watu kwa Mawalii ili wawafanyie mambo ya kimiujiza lilikuwa ni jambo lililokuwa likifanyika na kufahamika. Ewe msomaji mpendwa, kwa hakika mpaka sasa tumezizungumzia zile namna tatu za kuomba msaada kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu katika zama za uhai wao kwa mujibu wa Qur'an Tukufu na bila shaka umefahamu kwamba Qur'an imeeleza kusihi kwa namna hizo na imesisitizia katika aya nyingi. Ama kuzungumzia zile namna mbili za mwisho ambazo zinahusiana na kuomba msaada kwa roho takatifu tutakuletea katika mlango ufuatao Insha-Allahu Taala.

Mwenye kukaa Riyadha ni yule ambaye hufanya mazoezi magumu ya kiroho ili kuiwezesha roho kufanya mambo yo ajabu, hasa hasa mambo hayo kuwa ni ya kishetani na sio ya kiungu. kwa hiyo huwa yanaondoka mambo hayo anapoacha mazoezi hayo.

14

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## KUOMBA MSAADA KWA KUPITIA ROHO ZA MAWALII WA MWENYEZI MUNGU

Mas-ala ya kuomba msaada kwa kupitia roho za Mawalii wa Mwenyezi Mungu baada ya kufa kwao na kutoweka katika maisha haya ya kimaada, ni jambo muhumi mno kulifanyia uchunguzi, na hakuna tofauti baina ya kuwa huko kutaka msaada ni kwa namna ya dua au kwa kuomba. Sababu ya umuhimu wa jambo hili kuliko yale yaliyotangulia ni kuwa, leo hii Waislamu hawako katika mahdhar (ushuhuda) wa Nabii au Imam ili wakamuombe msaada ana kwa ana, kwa sababu hiyo basi, Waislamu wanaomba msaada kupitia roho za Mawalii hao watukufu. Mpaka hapa yaonekana umuhimu wa kuyafanyia uchunguzi mkubwa mas-ala haya kuliko yale yaliyotangulia.

Ewe msomaji mtukufu, uchunguzi wa maudhui hii utazungumzia mambo manne, na wakati wa kuelezea na kuichambua maudhui hii, bila shaka kufaa kwa mas-ala ya kuomba msaada kupitia kwa roho tukufu za Mawalii kutaeleweka vizuri. Mambo hayo manne ni haya yafuatayo:

1) Roho huwa zinabaki hai baada ya mtu kufa.

2) Ukweli halisi wa mtu ni roho yake.

3) Kuwasiliana na ulimwengu wa roho ni jambo linalowezekana.

4) Hadithi sahihi zilizopokewa na wanachuoni wa hadithi zinazungumzia kusihi mas-ala ya kuomba msaada kupitia kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu na kwamba, sera ya Waislamu imekuwa hivyo toka hapo kabla. Na ufuatao ndiyo ufafanuzi wa mambo hayo manne:

### MTU ANAPOKUFA HAINA MAANA KUWANDIYO AMETOWEKA KABISA

Aya nyingi za Qur'an zinajulisha wazi kwamba kufa siyo mwisho wa uhai, bali kufa ni moja ya kituo cha kuhamia kuelekea kwenye maisha mapya, na pia kufa kunamuingiza mtu kwenye ulimwengu mpya ulio bora kuliko ulimwengu huu wa kimaada. Kila anayeitakidi kwamba kufa ndiyo kutoweka kabisa, na ndiyo mtu huwa habakishi athari yoyote isipokuwa mwili usio na roho, mwili ambao hatimaye baada ya muda fulani hugeuka na kuwa udongo, mwenye itikadi hii huwa anafuata falsafa ya kimaada ambayo inapinga kuwepo kwa vitu visivyo vya kimaada, naye anafuata bila kujua anachokifanya. Watu wenye nadharia hii, hawauoni uhai isipokuwa ni matokeo ya kimaada yenye silsila ya utendaji wa kikemia na kifizikia unaopatikana ndani ya ubongo na mishipa ya fahamu. Na pindi mwili utakapokosa joto lake na chembe hai nazo zikakoma kufanya kazi basi uhai wa mtu nao hukoma vile vile na kugeuka kuwa mwili mkavu. Nadharia hii inakwenda mbele zaidi na kusema, eti roho ni matokeo ya vitu fulani vya kimaada na misingi yake, na inapokosekana misingi hiyo na athari zake, basi roho nayo hupotea na kuharibika kufuatia kuharibika kwa hivyo vitu vya kimaada. Kwa sababu hii basi watu hawa hawaitakidi kuwepo kwa ulimwengu mwingine ambao ni wa kiroho.

Hakika nadharia hii inategemea falsafa ya kimaada ambayo inamuona mtu kuwa ni kama mashine iliyounganishwa vipande vipande na sehemu tofauti tofauti, na kwamba utendaji wa baadhi ya viungu kuvifanyisha kazi viungo vingine ndiko kunakozalisha uwezo wa kufikiri na kufahamu ndani ya ubongo, na pindi viungo hivi vikisimama kutenda kazi, basi athari za kufikiri hukosekana na uhai nao hutoweka moja kwa moja. Wanafalsafa wakubwa na wanachuoni wa dini wanaipinga kabisa nadharia ya kimaada kuhusu roho, na wanasema kwamba, ni kweli mtu katika mwili wake anayo nidhamu ya kimaada inayotawala katika mwili wake na utendaji unaotegemeana na silsila ya viungo, lakini zaidi ya haya yote yeye anachokitu cha asili kinachoitwa roho. Na kitu hiki (yaani roho) kuna kipindi inakuwa pamoja na mwili kisha roho hutengana na mwili na kupaa ikaenda kwenye ulimwengu uitwao "Bar-zakh" ili iungane na mwili latifu. (Mwili latifu ni kitu chenye urefu, upana na kina lakini hakionekanai kama hewa). Kuizungumzia roho "ili kuifahamu" baada ya kufa inataka kitabu maalum kitakachohusika na suala la roho tu, na wala haiwezekani kuitafiti kwa upana ndani ya kurasa hizi chache, na hii ni kwa sababu aya za Qur'an na hoja za kifalsafa na majaribio ya wataalamu wa roho wamebainisha kubakia kwa roho ya mtu baada ya kufa.

Hapa tunataja baadhi ya aya za Qur'an Tukufu zinazothibitisha kubakia kwa roho baada ya kufa.

### QUR'AN NA KUBAKIA KWA ROHO

Aya za Qur'an zinafahamisha wazi kabisa kwamba roho huwa inabaki baada ya kiwiliwili kufa, na tunazitaja aya chache ili kufupisha maelezo.

وَلَا تَقُولُوا لِمَن يُقْتَلُ فِي سَبِيلِ اللَّـهِ أَمْوَاتٌ بَلْ أَحْيَاءٌ وَلَـٰكِن لَّا تَشْعُرُونَ ﴿١٥٤﴾

(1) Na wala msiseme kuwa, wale waliouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu ni wafu, bali wao wa hai lakini ninyi hamtambui. Qur'an, 2:154.

وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّـهِ أَمْوَاتًا بَلْ أَحْيَاءٌ عِندَ رَبِّهِمْ يُرْزَقُونَ ﴿١٦٩﴾ فَرِحِينَ بِمَا آتَاهُمُ اللَّـهُ مِن فَضْلِهِ وَيَسْتَبْشِرُونَ بِالَّذِينَ لَمْ يَلْحَقُوا بِهِم مِّنْ خَلْفِهِمْ ...﴿١٧٠﴾ يَسْتَبْشِرُونَ بِنِعْمَةٍ مِّنَ اللَّـهِ وَفَضْلٍ ...﴿١٧١﴾

(2) Wala usidhani wale waliouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni wafu, bali wao wa hai wanaruzukiwa mbele ya Mola wao. Wanafurahia yale aliyowapa Mwenyezi Mungu kwa fadhila zake na wanawashangilia wale ambao hawajajiunga nao.... Wanashangilia neema na fadhila za Mwenyezi Mungu. Qur'an, 3:169, 170, 171.

إِنِّي آمَنتُ بِرَبِّكُمْ فَاسْمَعُونِ ﴿٢٥﴾ قِيلَ ادْخُلِ الْجَنَّةَ قَالَ يَا لَيْتَ قَوْمِي يَعْلَمُونَ ﴿٢٦﴾ بِمَا غَفَرَ لِي رَبِّي وَجَعَلَنِي مِنَ الْمُكْرَمِينَ ﴿٢٧﴾

(3) Bila shaka mimi nimemuamini Mola wenu, basi nisikilizeni. (Hawakusikiliza bali walimuuwa), akaambiwa ingia peponi, akasema laiti watu wangu wangejua. Jinsi Mola wangu alivyonisamehe na akanijaalia miongoni mwa walioheshimiwa. Qur'an, 36:25-27.

Makusudio ya Pepo aliyoamrishwa aingie ndani yake ni pepo ya barzakh[1] siyo ile ya akhera kutokana na kauli ya Mwenyezi Mungu pale aliposema "laiti watu wangu wangejua jinsi Mola wangu alivyonisamehe na akanijaalia miongoni mwa walioheshimiwa".

Bila shaka kutamani kwake kwamba watu wake wangefahamu cheo alichokipata, hakuna maana ya kuwa cheo hicho alichopata ni cha huko akhera kwa sababu huko akhera siri zote zitadhihirishwa wazi mbele ya macho ya watu na wala hapatafichikana hali za watu fulani kuwaficha wengine. Bali matarajio haya yanalingana na uhai wa dunia hii ambayo watu wanaishi bila ya kufahamu mambo ya barzakh na yanayotendeka huko na haya yanathibika katika aya hii tukufu. Zaidi ya hapo aya nyingine inayofuatia baada ya aya iliyotajwa, inaonyesha kwamba Qaumu ya mtu yule mwema aliyeingia Peponi, walikufa baada yake kutokana na ukelele mkali kutoka mbinguni na Mwenyezi Mungu anasema:

وَمَا أَنزَلْنَا عَلَىٰ قَوْمِهِ مِن بَعْدِهِ مِن جُندٍ مِّنَ السَّمَاءِ وَمَا كُنَّا مُنزِلِينَ ﴿٢٨﴾ إِن كَانَتْ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً فَإِذَا هُمْ خَامِدُونَ ﴿٢٩﴾

(4) "Na hatukuwateremshia watu wake jeshi kutoka mbinguni (kuwaangamiza) baada yake, wala hatukuwa ni wenye kuteremsha majeshi toka mbinguni, bali ulikuwa ni ukelele mmoja tu na mara moja wakazimika (wakafa)." Qur 'an, 36:28-29.

Ndani ya aya hizi mbili kinachofahamika ni kwamba, wale Qaumu ya yule mtu aliyeingia peponi walikuwa wakiishi hapa duniani kisha ghafla yaliwafikia mauti, kwa hiyo pepo iliyotajwa hapo si nyingine ila ni ile ya barzakh.

النَّارُ يُعْرَضُونَ عَلَيْهَا غُدُوًّا وَعَشِيًّا ۖ وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ أَدْخِلُوا آلَ فِرْعَوْنَ أَشَدَّ الْعَذَابِ ﴿٤٦﴾

(5) Adhabu za motoni wanadhihirishiwa asubuhi na jioni, na siku kitakapotokea Kiyama kutasemwa, 'Waingizeni watu wa Fir-aun katika adhabu kali zaidi". Qur 'an, 40:46.

Kufuatana na maana iliyomo katika aya hizi inatudhihirikia kwamba, watu wa Firaun wako hai katika ulimwengu wa barzakh; kwa kuwa wanadhihirishiwa adhabu za moto asubuhi na jioni mpaka siku ya kiyama, na kiyama kitakaposimama, wataingizwa kwenye adhabu kali zaidi ya Jahannam. Basi lau si kauli ya Mwenyezi Munga aliposema "Na siku kitakapotokea kiyama" makusudio ya aya hii yasingedhihiri, lakini sasa inathibitisha kwamba maneno kabla ya siku ya kiyama yanarejea kwenye ulimwengu wa Bar-zakh. Zaidi ya hayo ni kule kutamka kwa "asubuhi na jioni" kunaonyesha kwamba adhabu hiyo siyo ya sika ya kiyama kwa kuwa siku hiyo hakuna asubuhi wala jioni. Msomaji mtukufu, maelezo yaliyotangulia yalikuwa ni uchunguzi kwa kifupi kuthibitisha kuwepo kwa uhai baada ya kufa na sasa tuzungumzie jambo la pili.

## UHAKIKA WA MTU NI ROHO YAKE

Mtu kwa mara ya kwanza hufikiria kwamba ameungamana kwa roho na mwili vikiwa pamoja, lakini ukweli halisi wa mtu ni ile roho yake inayopatikana katika mwili wake. Sasa hivi sisi hatufanyi uchunguzi wa

1. Barzakh ni ulimwengu ambao uko kati ya dunia na siku ya Kiyama.

maudhui haya kafuatana na mtazamo wa falsafa ya Kiislamu na ile ya Kiyunani, isipokuwa lengo letu ni kuyafahamu maudhui haya kwa mujibu wa kitabu cha Mwenyezi Mungu ambacho hakina shaka ndani yake. Bila shaka tukifanya mazingatio kwenye aya zinazomzungumzia mtu, kutatudhihirishia wazi kabisa kwamba ukweli halisi wa mtu ni ile roho yake. Hebu soma aya hii ifuatayo:

﴿قُلْ يَتَوَفَّاكُم مَّلَكُ الْمَوْتِ الَّذِي وُكِّلَ بِكُمْ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ تُرْجَعُونَ ﴿١١﴾

Waambie; "Atakufisheni Malaika wa mauti aliyewakilishwa kwenu kisha mtarejeshwa kwa Mola wenu". Qur'an, 32:11.

Ilivyo sahihi ni kwamba neno "tawafaa" halina maana ya kufisha inavyodhaniwa na watu bali maana yake ni kuchukua, kwa ajili hiyo basi kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema "yatawafaakum" maana yake ni "anakuchukuweni".[1] Kwani roho ni sehemu moja ya dhati ya mtu, na sehemu ya pili ni kiwiliwili chake, basi ibara hii itakuwa ni "Majaz"; kwani Malaika wa mauti huwa anachukua sehemu moja ambayo ni roho tu, na ama ile sehemu ya pili ambayo ni kile kiwiliwili hukiacha na kikabakia duniani kisha huzikwa kaburini wala Malaika wa mauti huwa hajishughulishi nacho.

Msomaji mpendwa, aya zinazozungumzia roho na mahala pake katika utu ni nyingi mao, sisi tumetaja moja tu kama mfano. Na jambo Ia mwanzo tulililoashiria yaani "kubaikia kwa roho baada ya mauti" maelezo yetu yaliyotangulia yanaonyesha wazi kuwa roho ndiyo mtu mwenyewe halisi na ndiyo asili ya kukamilika kwake kinafsi na kiroho kama ambavyo mwili unachukua nafasi ya vazi ambalo huifunika roho. Qur'an Tukufu haizingatii mauti kuwa ndiyo kutoweka kwa mtu na kuwa eti ndiyo mwisho wa uhai wake, bali inasisitiza "hasa kwa mashahidi na watu wema" na hata kwa watu wenye dhambi pia kwamba, wanao uhai mwingine kabla ya siku ya Kiyama na kwamba uhai huo ima utakuwa ni wa furaha na kushangilia au utakuwa ni wa adhabu kali. Na kama itakuwa kwamba uhakika wa mtu umo katika mwili wake, hapana shaka mwili wake huo baada ya kufa na kazikwa utaoza na kugeuka kuwa udongo n.k. Iwapo haii itakawa namna hivi basi utakuwa wapi huo ulimwengu wa barzakh?

## MAWASILIANO NA ULIMWENGU

Je, inawezekana kuwasiliana na ulimwengu wa kiroho? Jawabu linasema kuwa: Ndiyo bila shaka upo uwezekano huo, nasi tutatoa dalili kwa mujibu wa Qur'an tukufu na pia dalili za kielimu. Kuthibitika kubakia kwa roho isiyokuwa ndani ya mwili, hakatoshelezi kukubalisha kufaa kuomba msaada kupitia kwenye roho hiyo mpaka uthibiti uwezekano wa kuwepo mawasiliano baina ya roho hiyo na ulimwengu wa duniani. Ndani ya Qur'an kuna aya nyingi zinathibitisha kwamba, mtu kuwasiliana na ulimwengu wa kiroho ni jambo linalowezekana, isitoshe jambo hili limethibitika kwa vitendo kwa mfano:

### 1). NABII SALEHE [a.s] ALIZISEMESHA ROHO ZA WATU WA QAUMU YAKE

Mwenyezi Mungu anasema:

---

1. Tafsir Alaaur-Rahman cha Mar-hum al-Allammah al-Balaghi uk. 34, kwa ufafanuzi kuhusu neon "Tawafaa".

فَعَقَرُوا النَّاقَةَ وَعَتَوْا عَنْ أَمْرِ رَبِّهِمْ وَقَالُوا يَا صَالِحُ ائْتِنَا بِمَا تَعِدُنَا إِن كُنتَ مِنَ الْمُرْسَلِينَ
﴿٧٧﴾ فَأَخَذَتْهُمُ الرَّجْفَةُ فَأَصْبَحُوا فِي دَارِهِمْ جَاثِمِينَ ﴿٧٨﴾ فَتَوَلَّىٰ عَنْهُمْ وَقَالَ يَا قَوْمِ لَقَدْ
أَبْلَغْتُكُمْ رِسَالَةَ رَبِّي وَنَصَحْتُ لَكُمْ وَلَٰكِن لَّا تُحِبُّونَ النَّاصِحِينَ ﴿٧٩﴾

"Wakamchinja yule ngamia na wakaiasi amri ya Mola wao na wakasema: Ewe Saleh tuletee hayo unayotuahidi ikiwa wewe ni miongoni mwa Mitume. Mtetemeko wa ardhi ukawanyakuwa (roho zao) na wakawa wamekufa humo katika nyumba zao. Basi akawaacha na huku anasema: Enyi kaumu yangu nilikufikishieni ujumbe wa Mola wangu na nikakupeni nasaha lakini ninyi hamuwapendi wenye kutoa nasaha". Qur'an, 7:77, 78, 79.

Ziangalie aya hizi kwa makini: Aya ya kwanza inaashria kwamba watu wa Nabii Saleh walipokuwa hai duniani walimtaka awaletee adhabu ya Mwenyezi Mungu iliyoahidiwa. Aya ya pili inaashiria kushuka kwa adhabu juu yao na kufa kwao wote. Aya ya tutu inaashiria usemi wa Nabii SaIeh [a.s] aliousema baada ya watu wake kufa, akawahuzunikia kwa matokeo hayo ya kutisha waliyoyachagua wenyewe akawaambia: "Enyi watu wangu nilikufikishieni ujumbe wa Mola wangu na nikakunasihini lakini ninyi hamuwapendi wanaotoa nasaha". Na dalili inayoonyesha kwamba khitabu (usemi) hii ilitoka kwa Nabii Saleh baada ya watu wake kufa ni kama ifuatavyo: a) Mpango na mfumo wa aya kama zilivyopangika zaonyesha wazi jambo hilo. b) Herufi ya "FAA" katika neno "FATAWALAA" ambalo linajulisha kuwepo utaratibu "yaani baada ya hiki kinakuja hiki" na tamko "FATAWALAA" limekuja baada ya kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo "Wakawa wamekufa humo katika nyumba zao", kitu ambacho kinajulisha kwamba Khitabu ya Nabii Saleh [a.s] kwa watu wake ilikuja baada ya kuwashukia adhabu. Pia inafahamika kutokana na kauli yake Mwenyezi Mungu kwamba, watu hao walikuwa wamekithiri katika ujeuri na uovu kiasi kwamba hata baada ya kufa kwao roho zao zilikuwa bado zikipinga mawaidha na nasaha. Na inafahamika katika kauli yake aliposema: "Lakini ninyi hamuwapendi wanatoa nasaha".

## 2) NABII SHUAIBU [a.s] ALIZISEMESHA ROHO ZA WATU WAKE

Soma aya hizi:

فَأَخَذَتْهُمُ الرَّجْفَةُ فَأَصْبَحُوا فِي دَارِهِمْ جَاثِمِينَ ﴿٩١﴾ الَّذِينَ كَذَّبُوا شُعَيْبًا كَأَن لَّمْ يَغْنَوْا فِيهَا
الَّذِينَ كَذَّبُوا شُعَيْبًا كَانُوا هُمُ الْخَاسِرِينَ ﴿٩٢﴾ فَتَوَلَّىٰ عَنْهُمْ وَقَالَ يَا قَوْمِ لَقَدْ أَبْلَغْتُكُمْ رِسَالَاتِ
رَبِّي وَنَصَحْتُ لَكُمْ فَكَيْفَ آسَىٰ عَلَىٰ قَوْمٍ كَافِرِينَ ﴿٩٣﴾

"Basi mtetemeko wa ardhi uliwatoa roho zao wakawa hawajimudu (wamekufa) katika nyumba zao. Wale waliompinga Shuaib wakawa kama kwamba hawakuwako, (mahala hapo) waliompinga Shuaib ndiyo waliokula khasara. Basi akawaacha akaenda zake na akasema: Enyi watu wangu nimekufikishieni ujumbe wa Mola wangu na nimekupeni nasaha; basi ni vipi nihuzunike kwa watu waliokufuru". Qur'an, 7:91, 92, 93.

Kutolea ushahidi aya hizi ni sawa na zile aya zilizotangulia kutokana na mafungamano yaliyopo kwa Nabii Saleh [a.s].

## 3) MTUME MUHAMMAD [s.a.w.w] PAMOJA NA MANABII WENGINE

Mwenyezi Mungu anasema:

وَاسْأَلْ مَنْ أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ مِن رُّسُلِنَا أَجَعَلْنَا مِن دُونِ الرَّحْمَـٰنِ آلِهَةً يُعْبَدُونَ ﴿٤٥﴾

"Na waulize Mitume wetu tulio watuma kabla yako: Je! Tulifanya miungu mingine iabudiwe badala ya Rah'mani?" Qur'an, 43:45.

Hakika dhahiri aya hii inajulisha kwamba, upo uwezekano wa Mtume **[s.a.w.w]** (Ambaye anaishi katika ulimwengu huu) kuwasiliana na Manabii wanaoishi kwenye ulimwengu mwingine ili apate kuwathibitishia washirikina ya kwamba, Manabii wote na katika kila zama walikuwa wakilingania kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kumuabudu.

## 4) SALAMU ZA QUR'AN KWA MANABII

Qur'an Tukufu inawatolea salamu Manabii mahala pengi, na wala hapana shaka kwamba salamu hii siyo salamu ya juu juu isiyo na uhakika bali ni salamu na maamkizi ya hakika ambayo Qur'an inayaelekeza kwa Manabii na Mitume wa Mwenyezi Mungu. Siyo uadilifu iwapo mtu atajaribu kuzifasiri aya za Qur'an kwa tafsiri ya juu juu bila ya undani wake, basi atakuwa amezigeuza aya za Qur'an na kuwa matamko matupu yasiyo na maana. Kwa hakika watu wasioamini Mwenyezi Mungu, ambao hawaamini kuwepo kwa roho, huwatolea salamu viongozi wao kwa kutumia ibara zisizo na maana. Ama kwa upande wetu sisi Waislamu, tunanufaika kutokana na itikadi sahihi kuhusu suala la roho, na haifai kuzifasiri maana za maneno ya Qur'an kuhusu roho kwa tafsiri ya juu juu kwa sababu mafuhum ya Qur'an inategemea hakika na misingi ya ukweli. Basi hatuwezi kusema kwamba, maamkizi yaliyomo katika Qur'an ambayo tunayasema usiku na mchana ni maamkizi ambayo hayana hakika wala maana sawa sawa na maamkizi ya watu wasioamini. Hebu itazame Qur'an namna inavyowatolea salamu Manabii:

1. "Salamu zimshukie Nuhu katika walimwengu".
2. "Salamu zimshukie Ibrahim"
3. "Salamu zimshukie Musa na Harun"
4. "Salamu ziwashukie kizazi cha Yasin" 5. "Salamu ziwashukie Mitume". Quran, 37:79, 109, 120, 130, 181.

## MAAMKIZI KWA MTUME [s.a.w.w] MWISHONI MWA SWALA

Waislamu wote ulimwenguni, bila kujali tofauti za Madhhebu yao katika furui za dini humsalimia Mtume **[s.a.w.w]** ndani ya swala zao mwishoni na huwa wanasema: "Salamu zikushukie Ewe Nabii, na Rehma na Baraka za Mwenyezi Mungu". Imam Shafii na wengineo wametoa Fat-wa kuwa ni wajibu kuitoa salamu hiyo baada ya 'TASHAHUD", na wengine nao wametoa Fat-wa wakasema kuwa ni Sunna, lakini wote wameafikiana kuwa Mtume **[s.a.w.w]** amewafundisha salaam hiyo. Pamoja na tofauti hii katika salamu hiyo na kwamba Sunna ya Mtume huwa inathibiti katika uhai wake na baada ya kufa kwake.[1] Suala ambalo sasa hivi tunalazimika kujiuliza ni hili lifuatalo: "Ikiwa maungamano na mawasiliano yetu na Mtume **[s.a.w.w]**

---

1. Rejea Kitabu Tadhikirati lfuquhai Juz. 1 na Kitabul-Khilafi cha Sheikh Tusi Juz. 1 uk. 47 ili upate kufahamu kauli za Madh-hab na wanachuoni kuhusu jambo hili.

yalikatika baada ya kufa kwake basi kuna maana gani kumsemesha na kumsalimia kila siku (katika Sala zetu)?" Imepokewa kutoka kwa Mtume **[s.a.w.w]** kwamba yeye amesema: "Yeyote mwenye kunitakia Rehma kwenye kaburi langu nitamsikia, na yeyote atakayenitakia rehma kutoka mbali, nitafikishiwa salamu yake".[1] Tumezungumza kwa ufafanuzi kuhusu maudhui ya kuwepo maungamano na roho zilizoko katika huo ulimwengu mwingine ndani ya kitabu maalum, na humo tumetaja aya nyingi kulihusu jambo hilo, hapa tunatosheka na aya hizi ili kufupisha maelezo. Kwa kumaliza inafaa kutambulisha kwamba, tumeleta dalili za kutoa salamu wakati wa 'Tashahud' tulipokuwa tukizitafiti zile aya tulizozitaja hapo kabla na hii ni kwa sababu jambo hili limethibiti bila ya shaka yoyote.

Sasa hivi hebu angalia mifano iliyomo katika tarekh (Historia) inayozungumzia uwezekano wa kuzisemesha roho (za watu waliokufa).

1. Imepokewa kutoka kwa Mtume **[s.a.w.w]** kwamba yeye alisimama kwenye kisima cha Badri na akawasemesha washirikina ambao waliuawa na miili yao ikatoswa kisimani humo: "Ninyi mlikuwa ni majirani wabaya kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, mlimtoa nyumbani mwake na mkamfukuza, kisha mkaungana dhidi yake mkampiga vita, basi mimi nimeyapata aliyoniahidi Mola wangu". Basi mtu mmoja akamwambia Mtume **[s.a.w.w]** "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu namna gani unavisemesha vichwa vilivyooza?" Mtume **[s.a.w.w]** akasema: "Wallahi wewe siyo msikivu kuliko wao, na hapana (kizuwizi) baina yao na kuadhibiwa kwao na Malaika kwa mijeledi ya chuma ila inwageuzie uso wangu hivi".[2]

2. Na imepokewa kwamba Imam Ali bin Abi Talib [a] alipanda mnyama wake baada ya kumalizika vita vya Jamal huko Basra, kisha akawa anapita katikati ya watu waliouawa mpaka akapita mahali alipokuwa kaangukia Kaab bin Suur ambaye alikuwa Qadhi wa Basra tangu zama za Omar bin Khatab na Uthman, na ilipotokea fitna huko Basra, Bwana huyu na watu wake na mwanawe walitaka kupigana dhidi ya Imam Ali [a.s] ambaye alikuwa Khalifa wa Mtume na Imam wa zama zake na wote wakauawa.

Imam Ali [a.s] alipofika hapo alipolala Bwana huyu akasimama akawaambia watu waliokuwa karibu naye: "Mkalisheni Kaab bin Suur". Wakamkalisha huku watu wawili wamemshikilia. Imam Ali [a.s] akasema: "Ewe Kaab bin Suur hakika mimi nimeyakuta aliyoniahidi Mola wanga kuwa ni ya kweli, basi je wewe umeyakuta aliyokuahidi Mola wako kuwa ni ya kweli?" Kisha Imam Ali [a.s] akasema: "Mlazeni". Akaenda mbele kidogo akafika mahali alipokuwa ameangukia Tal-ha bin Abdallah akasema: "Mkalisheni Tal-ha". Wakamkalisha na akasema tena Imam Ali [a.s] "Ewe Talha hakika mimi nimeyakuta aliyoniahidi Mola wangu kuwa ni ya kweli, basi je wewe umeyakuta aliyokuahidi Mola wangu kuwa ni ya kweli?" Kisha akawaambia; "Mlazeni Tal-ha". Mtu mmoja akamwambia Imam Ali [a.s] "Ewe Amirul Muuminina yanafaida gani maneno yako uliyowaambia maiti hawa wawili hali wao hawakusikii?" Imam Ali [a.s] akasema: "Ewe

1. Kitabu Haqul-yaqin cha Sayyid Abdullah Shubbar,Juz. 2 uk. 73.
2. Sahihi Bukhari Juz. 5, Babu Qat-li Abi Jah-li, uk. 76, na 77. Pia Sirat lbn Hisham, Juz. 2 uk. 292, Haqul-yaqin cha Sayyid Abdullah Shubbar Juz. 2, uk. 73.

mtu, Wameyasikia maneno yangu kama vile watu wa kisima (cha Badri) walivyoyasikia maneno ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu".[1]

## MATOKEO YA UCHUNGUZI

Yafuatayo ni maelezo kwa kifupi juu ya uchunguzi wa maudhui hii:

1. Tumethibitisha ndani ya ile maudhui ya kwanza kwamba kifo siyo mwisho wa uhai, wala haimaanishi kuwa ndiyo kutoweka kwa mtu, bali kifo ni njia apitayo mtu kuelekea ulimwengu mwingine.

2. Tumethibitisha ndani ya maudhui hii ya pili kwamba, uhakika wa mtu ni roho yake, na kwamba mwili si chochote bali ni vazi linaloifunika roho. Na kubakia kwa roho maana yake ni kubakia kwa utu wa mtu na ukamilifu wa maana halisi ya mtu, ukiondoa uwezo wa kimatendo ambao hutoweka kwa kutoweka mwili. Na kwa msingi huu, iwapo nafsi ya mtu na roho yake itakuwa inao uwezo wa kuomba na kufanya mambo ya muujiza wakati wa uhai wake (duniani) basi roho yake vile vile inao uwezo wa kuyatenda matendo yote hayo baada ya kufa kwake kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.

3. Na katika maudhui ya tatu tumethibitisha kuwepo uwezekano wa maungamano na ulimwengu mwingine, isitoshe tumethibitisha kuwepo maungamano hayo duniani na kwamba roho zilizoko huko zinauwezo wa kusikia maneno yetu tunapozisemesha, na wala hakuna tofauti kati ya roho za watu wema na waovu katika kusikia maneno kama ambavyo tumeeleza matukio ya aina hiyo katika Qur'an na historia. Baada ya kuyafahamu mambo haya matatu inathibiti kwamba Mawali wa Mwenyezi Mungu wanasikia maneno yetu tunapowasemesha, na pindi Mwenyezi Mungu anapowapa idhini ya kutujibu basi huwa wanaturudishia majibu. Swali lililopo hapa sasa hivi ni: Je, inafaa kwa mujibu wa sheria kuzisemesha roho za Mawalii wa Mwenyezi Mungu na kuziomba msaada? Insha-Allah jawabu litakujia katika jambo la nne lifuatalo.

## WAISLAMU NA KUZIOMBA MSAADA ROHO TAKATIFU

Ibnu Taimiyya na wafuasi wake walifanya pupa kutoa hukmu pale walipopinga wakasema, "Masahaba na Tabiina hawakumuomba msaada Mtume **[s.a.w.w]** ". Watu hawa (Ibn Taimiyya na wafuasi wake) wanasema, "Hapana mtu yeyote miongoni mwa salafu wa umma huu waliotangulia katika zama za Masahaba wala zile za Tabiina wala wale waliofuatia baada ya Tabiina waliokuwa wa kiswali na kuomba dua kwenye makaburi ya Manabii au kuwaomba Manabii hao wala hawakuomba msaada wao wanapokuwa hawapo, wala kwenye makaburi yao.[2] Huenda mtu asiyefahamu historia ya Masahaba na Tabiina akahadaika kwa maneno haya na akayaona kuwa ni ya kweli na sahihi. Lakini iwapo ataiangalia historia kwa makini na akasoma juu ya Masahaba na wengineo kutawas-sal kwa Mtume **[s.a.w.w]** na kumuomba kwao msaada, utamthibitikia uongo wa madai haya. Hebu tazama mifano ifuatayo:

1. Watu walipatwa na ukame katika zama za Omar bin Al-Khatab, mtu mmoja akaenda kwenye kaburi Ia Mtume **[s.a.w.w]** na akasema, "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, waombee umati wako kwa Mwenyezi

---

1. Haq-qul-yaqin cha Sayyid Abdullah Shubbar, juz. 2, uk. 73.
2. Risalatul-hadiyatis-saniyya, uk. 162, Chapa ya AI-manar Misri.

Mungu wapate mvua, kwani wemekwisha angamia, basi Mtume alimjia mtu huyo usingizini akamwambia, nenda kwa Omar mwambie watapata mvua".[1]

Baada ya kutaja kisa hiki As-samhudi anasema: "Mahali penye ushahidi ni pale Mtume alipoombwa awaombee watu wake mvua hali akiwa katika ulimwengu wa Bar-zakh, na Mtume kumuomba Mola wake akiwa katika hali hiyo siyo jambo lisilowezekana, na imekuja katika hadithi kwamba Mtume anafahamu ombi Ia anayemuomba basi hakuna kizuiwizi kumuomba awaombee mvua na mengineyo kama alivyokuwa akifanya zama za uhai wake duniani.[2]

2 As-samhudi amepokea vile vile kutoka kwa Al-hafidh Abu Abdillahi Muhammad bin Musa bin Nuuman kwa Sanad inayoishia kwa Imam Ali [a.s]: "Hakika bedui mmoja alikuja Madina baada ya siku tata tangu kuzikwa Mtume **[s.a.w.w]**, akajitupa kwenye kaburi la Mtume na akajipaka udongo wa kaburi hilo kichwani na akasema, ewe Mtume ulisema tukasikia maneno yako na ulipokea toka kwa Mola wako nasi tukapokea toka kwako, na miongoni mwa yaliyoteremshwa kwako ni "Na lau wangekujia walipojidhulumu nafsi zao wakaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu na Mtume naye akawaombea msamaha bila shaka wangemkuta Mwenyezi Mungu ni mwenye kupokea toba na mwenye kurehemu", nami nimeidhulumu nafsi yangu, na nimekujia (Ewe Mtume) uniombee msamaha".[3] Ewe msomaji mtukufu, As-Samhudi anataja katika kitabu chake kiitwacho Wafaul-wafai ndani ya mlango wa nane, matukio mengi na yote yanajulisha kwamba kumuomba msaada Mtume **[s.a.w.w]** ulikuwa ni mwenendo unaoendelea kwa Waislamu kiasi amesema huyu Samhudi kwamba, Imam Muhammad bin Nuuman ameandika kitabu juu ya maudhui haya kiitwacho: Misbahudhalami fil-mustaghithina Bikhairil-anam".

3. Muhammad bin Al-munkadir anasema: "Mtu mmoja aliwekeza kwa baba yangu Dinari thamanini, kisha akaenda kwenye Jihadi na akamwambia baba yangu, iwapo utakuwa na haja nazo basi zitumie mpaka nitakaporudi, baadaye watu walipatwa taabu ya kupanda thamani ya vitu baba yangu akazitoa Dinari zile na yule mtu aliporudi alitaka apewe Dinari zake. Baba yangu akamwambia njoo kesho, (baba yangu) alilala msikitini, akawa mara analikumbatia kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** na wakati mwingine kwenye mimbari ya Mtume **[s.a.w.w]** mpaka karibu ya kupambazuka, hali akiomba msaada kwenye kaburi Ia Mtume **[s.a.w.w]**. Wakati akiwa katika hali hiyo ghafla alitokea mtu katika giza akasema chukua ewe Abu Muhammad, basi baba yangu akanyoosha mkono na akapokea mfuko ambao ndani yake ulikuwa na dinari themanini". "Kulipokucha yule mtu alikuja na akampa dinari zake".[4]

4. Anasema Abubakar Al-muqri: "Nilikuwa mimi na At-tabrani na Abus-shaikh katika msikiti wa mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** na tulikuwa katika hali fulani na njaa ilikuwa imetuathiri, siku hiyo tukaimaliza na ulipofika wakati wa I'sha nilikwenda kwenye kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** nikasema, Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (nahisi) njaa.... Basi alikuja

---

1. Wafaul-wafai, Juz. 2, uk. 1371.
2. Wafaul-wafai, Juz. 2, uk. 1371.
3. Wafaul-wafai, Juz. 4, uk. 1361.
4. Wafaul-wafai, Juz. 4, uk. 1380.

mlangoni sharifu akagonga na tukamfungulia, kumbe alikuwa pamoja na vijana wawili ambao kila mmoja wao ana kikapu ndani yake mna vita vingi tukakaa tukala na tukadhani kwamba vilivyobaki vitachukuliwa na mmoja wa vijana hao, lakini aliondoka na kutuachia hivyo vilivyobakia. Tulipomaliza kula akasema yule Sharifu, Je, Nyie watu mmemlalamikia mjumbe wa Mwenyezi Mungu? Kwani mimi nimemuona Mtume **[s.a.w.w]** usingizini akaniamuru nikuleteeni chochote".[1]

5. lbn Jal-laad anasema: "Niliingia Madina mji wa Mtume **[s.a.w.w]** hali ya kuwa nina njaa, basi nikaenda kwenye kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** nikasema mgeni wako, (baada ya muda) nikasinzia na nikamuona Mtume **[s.a.w.w]** akinipa mkate nikaula nusu yake, nilipozinduka nikaiona ile nusu nyingine iko mkononi mwangu."[2] Sasa hivi hatujadili matukio haya yaliyotajwa na kubainisha usahihi wake au makosa yake, bali tunachozungumzia ni kuwa, matukio yote haya kwa ujumla yanashuhudia kwamba kumuomba msaada Mtume **[s.a.w.w]** ni jambo ambalo lilikuwa likitendeka miongoni mwa Waislamu. Na lau lingekuwa ni uzushi na ni haramu au ni shiriki au ni kufuru hata hao wazushi wa hadithi wasingelisema kwa kuchelea kuharibu heshima zao miongoni mwa watu. Na kutokana na ukweli wa jambo hili sisi tumeandika kitabu makhususi kuhusu jambo hili kiitwacho: "Isalatur-ruuh" na humo tumezungumza kwa upana kila kinachofungamana na maudhui haya, na tumeleta hadithi na mapokezi mengi, na yote yanajulisha juu ya kusihi kuomba mahitaji kupitia kwenye roho tukufu na pia kusihi kuomba kutekelezwa kwa jambo ambao likokinyume na maumbile ya kawaida. Na kwa kukamilisha mlango huu tunaleta uzindushi kwenye mambo yafuatayo:

1. Kuwaomba msaada Mawalii wa Mwenyezi Mungu kamwe siyo kuwaabudu, na hasa baada ya kuwa tumeieleza kwa upana maana ya neno Ibada, na linavyotumika neno lenyewe na kwamba kuitakidi uungu (katika kutenda) ndiyo jambo ambalo hulipa picha ya Ibada tendo linalotendwa. Na jambo lililo wazi ni kwamba mtu anaye tawa-sal kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu huwa hana itikadi kwamba Mawalii hao ni Miungu na wala haitakidi kwamba wao ndio wanaosimamia mambo ya ulimwengu na wala kutenda matendo ya Mwenyezi Mungu kwa uhuru bila kumtegemea Mwenyezi Mungu bali anawafahamu tu kuwa wao ni waja watukufu walio wema mbele ya Mwenyezi Mungu wasiotenda japo dhambi ndogo au maasi.

2. Mambo manne yaliyotajwa hapo kabla yamethibitisha tena kwa hoja na dalili kwamba, Mawalii wa Mwenyezi Mungu wanao uwezo wa kukidhi haja ya mwenye kutawas-sal kwa kuwa wao wako hai mbele ya Mwenyezi Mungu, na kwamba kila kinachotoka kwao huwa ni kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa hiyo basi wao ndio thibitisho la kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema "Na hamtataka (kitu kiwe) mpaka Mwenyezi Mungu atake (kiwe kitakuwa). Kwa mfano: Nabii Isa **[a.a.w.w]** ambaye katika zama za uhai wake na maisha ya duniani alikuwa akimuomba Mwenyezi Mungu amjaalie kheri mtu amtakaye, au kuwaponya vipofu na wenye mbaranga kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, vile vile Nabii Isa [a.s]

---

1. Wafaul-wafai, Juz. 4, uk. 1380.
2. Wafaul-wafai, Juz. 4, uk. 1381.

anao uwezo wa kufanya hivyo baada ya kuhamia kwenye ulimwengu wa Bar-zakh kwa kuwa roho yake inaendelea kubakia, nayo ndiyo hakika yake yeye Nabii Isa [a.s].

3. Kuheshimu na kunyenyekea mbele ya makaburi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu ni kumheshimu Mwenyezi Mungu, japokuwa dhahiri inaonekana kuwa ni kumheshimu walii aliyezikwa hapo, lakini lau tutaufungua moyo wa huyu mwenye kutoa heshima na unyenyekevu huo tungemuona anamnyenyekea Mwenyezi Mungu kupitia kwa Walii huyo mwema, na kwamba yeye anaomba maombi yake kwa Mwenyezi Mungu kupitia kwa Walii huyu. Kwa hiyo basi, kutawas-sal kwa kupitia sababu ndiyo huko huko kutawas-sal kwa aliyesababisha sababu hizo ziwepo naye ni Mwenyezi Mungu Mtukufu. Jambo hili liko wazi kwa watu wenye kuchunguza na kufahamu.

Nawe msomaji lau utamuuliza huyu anayetawas-sal kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu kwamba ni jambo gani limemfanya atawas-sal kwa Walii? Haraka sana atakujibu kuwa "Walii huyo ni wasila (njia) ya kumfikisha kwa Mwenyezi Mungu kama alivyosema Mwenyezi Mungu, "Enyi mlioamini mcheni Mwenyezi Mungu na mutafute wasila wa kukufikisheni kwake, na mupiganie katika njia yake ili mupate kufaulu".[1] Hali ni ile ile mtu anapotawas-sal kwa Mwenyezi Mungu kupitia kwenye Sala, Saumu, Ibada na mengineyo ya wema, ndiyo hivyo hivyo anavyotawas-sal kwa Mwenyezi Mungu kupitia kwa Mawalii wema waliotukuzwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Kwa ufupi, muumini anaitakidi katika nafsi yake kuwa, kutawas-sal kwake kupitia kwa Mtume **[s.a.w.w]** na wengineo miongoni mwa maasumina na watu wema huwa kunamfanya huyo anayefanyiwa tawasuli hiyo kumuomba Mwenyezi Mungu akubali maombi ya yule aliyetawas-sal, sawa sawa kama tawasuli hiyo itakuwa ni kutaka kusamehewa madhambi au kulipa deni, kuponya maradhi, au kupata maisha mazuri na mengineyo.

1. Qur'an, 5:35.

15

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## KUTAKA UOMBEZI TOKA KWA MAWALII WA MWENYEZI MUNGU

Neno "Shafaa" ni maarufu miongoni mwetu sote, nalo tunalitamka mara nyingi katika ndimi zetu katika nyakati na muhala munamo husika. Kwa mfano: Yanapofanyika mazungumzo kumhusu mtu fulani aliyetenda kosa fulani na mahakama imemhukumu kifo au kufungwa au namna nyingine, kisha akatokea mtu akaingilia kati na kumuokoa tokana na hukumu aliyohukumiwa, basi huwa tunasema mtu fulani kamuombea (kanishufaia) fulani.

### MAANA YA SHAFAA (KUSHUFAIA)

Neno Shafaa linatokana na shaf'a kwa maana ya jozi ambalo kinyume chake ni witiri na sababu zilizofanya neno "Shafaa" litumike kwa maana ya kile kitendo cha kuombea na "Shafii" kwa maana ya yule mwenye kuombea ni kwamba, juhudi na bidii zifanywazo na huyu mwenye kuombea zinaoana na juhudi na bidii nyingine za kutaka kujiokoa zinazofanywa na yule anayeombewa, na ndipo yule mwenye kutenda makosa au mwenye kutuhumiwa hupata kuokoka kutokana na kuangamia. Uombezi wa Mawalii wa Mwenyezi Mungu kuwaombea watu wenye madhambi kunakuja kutokana na ukaribu wao hao Mawalii kwa Mwenyezi Mungu, pia daraja yao na heshima yao mbele yake Mwenyezi Mungu. Basi wao huombea watu wenye dhambi kwa idhini ya Mwenyezi Mungu ndani ya masharti maalum ili Mwenyezi Mungu apate kuwasamehe au kuwapokelea maombi yao. Kwa maelezo mengine ni kwamba "Shafaa" ni msaada wa Mawalii wa Mwenyezi Mungu kwa idhini yake kuwasaidia watu ambao hawakukata maungamano yao ya kidini kwa Mwenyezi Mungu na Mawalii wake, pamoja na kwamba wao ni wenye dhambi.

Taarifu hii ya "Shafaa" imetoa maana ya kina ambayo inapasa kuizingatia muda wote, na kwa maelezo ya namna ya tatu ni kwamba, Shafaa ni msaada wa mtu mwenye daraja ya juu kwa ajili ya mtu wa daraja ya chini, kwa sharti ya kuwepo maandalizi kupokea Shafaa kwa ajili ya ukamilifu wa mafanikio yake na kupanda kwenye daraja ya juu, na kumbadili kuwa mtu mwema mtakatifu. Baada ya taarifu hizi nyingi tunasema: "Historia inathibitisha kwamba, Waislamu tangu zama za Mtume **[s.a.w.w]** na baada yake, walikuwa wanaomba "Shafaa" toka kwa Mawalii wema wa Mwenyezi Mungu, sawa sawa Mawalii hao wawe hai au baada ya kufa kwao, na wala hakuna mwanachuoni yeyote wa Kiislamu aliyeifahamu "Shafaa" kuwa inapingana na misingi ya Uislamu, mpaka alipokuja Ibn Taimiyya katika karne ya nane Hijiriya akiwa na mawazo potofu akayapinga mambo mengi miongoni mwa misingi ya Uislamu na mwenendo wa Waislamu. Na baada ya kupita karne tatu tangu yeye Ibn Taimiyya kuzusha fikra hizo alikuja Muhammad bin Abdul-Wahab kutoka Najdi, yeye aliinyanyua juu bendera ya upinzani dhidi ya Waislamu na akazusha fitna na utengano baina yao, pia akaupa uhai uzushi wa Ibn Taimiyya kwa nguvu kuliko hata alivyokuwa Ibn Taimiyya mwenyewe.

Mawahabi wanaitakidi kusihi kiva "Shafaa" katika misingi yake, lakini tofauti iliyo baina yao na Waislamu ni kwamba wao Mawahabi wanaharamisha kuomba "Shafaa" kutoka kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu hapa duniani, na wao wanaeleza itikadi yao hii kwa maelezo machafu yanayoonyesha dharau kwa Manabii na Mawalii kiasi ambacho inatia woga kuyataja hayo wayasemayo Mawahabi. Miongoni mwa maneno wayasemayo ni kwamba "Mtume wa Uislamu yeye na Manabii wengine na Mawalii na Malaika, wanayo haki ya kushufaia huko Akhera tu, lakini kuomba Shafaa ni lazima iwe kwa Mwenyezi Mungu na sio kwao na isemwe kama ifuatavyo: "Ewe Mwenyezi Mungu mfanye Mtume wetu Muhammad **[s.a.w.w]** awe muombezi siku ya Qiyama, au Ewe Mwenyezi Mungu wafanye waja wako wema wawe waombezi wetu au Malaika wako au mfano kama huu miongoni mwa mambo ambayo huombwa kwa Mwenyezi Mungu na siyo kwao Mitume na Mawalii na Malaika hapo haiwezi kusemwa: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu au Ewe Walii wa Mwenyezi Mungu nakuomba "Shafaa" au kitu kingine miongoni mwa mambo ambayo hakuna ayawezaye isipokuwa Mwenyezi Mungu, basi iwapo utaomba "Shafaa" katika siku zao za kuwa katika Bar-zakh basi tendo hilo litakuwa ni miongoni mwa shirki".[1] Kwa hali hii unawaona Mawahabi wanavyowatuhumu Waislamu eti kuwa wanafanya shirki kwa kuomba "Shafaa" toka kwa Mtume **[s.a.w.w]** na Mawalii wa Mwenyezi Mungu hapa duniani na huko Akhera. Sisi kabla ya kuingia katika majadiliano dhidi ya hoja na dalili za Mawahabi kwanza tunaanza kuyachunguza mas-ala hayo ya "Shafaa" kwa mujibu wa Qur'an Tukufu na Sunna pia sera ya Waislamu kisha tuzilete hizo dalili za Mawahabi na tuzichunguze na kuzijadili.

## DALILI ZINAZORUHUSU KUOMBA SHAFAA HAPA DUNIANI

Dalili yetu inayoruhusu kuomba Shafaa hapa duniani imefungamana na mambo mawili, na yatakapothibiti mambo hayo, maudhui ya Shafaa itakuwa imekaa wazi kikamilifu. Mambo hayo mawili ni haya yafuatayo:

1. Kuomba Shafaa ni kuomba dua.
2. Kuomba dua toka kwa watu wachamungu ni jambo Mustahabbu katika Uislamu. Sasa hebu angalia uchambuzi wa mambo haya mawili kama ifuatavyo:

## 1). KUOMBA SHAFAA NI KUOMBA DUA

Uombezi wa Mtume **[s.a.w.w]** na waombezi wengine miongoni mwa watu wema si kitu kingine, bali ni maombi yao kwa Mwenyezi Mungu, kwani wao daraja yao na heshima yao ni kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa sababu ya daraja yao huwa wananyenyekea mbele ya Mwenyezi Mungu kwa dua na kuwatakia maghfira (msamaha) watu wenye dhambi, naye Mwenyezi Mungu huyakubali maombi yao na kuieneza huruma yake kwa waja wake hao wenye kufanya maasi na kuwasamehe na kuyakosha madhambi yao. Kuomba dua kutoka kwa ndugu muumini Muislamu yeyote ni jambo zuri linalopendekezwa (katika Uislamu) na hapana mtu mwenye shaka juu ya ubora wa jambo hili miongoni mwa wanachuoni wa Kiislamu na Madhehebu mbali mbali hata hao Mawahabi

---

1. AI-hadiyatus-saiyya Risala ya pili, uk. 42.

wenyewe, basi itakuwaje hali ya dua ya Mtume na Mawalii wema? Bila shaka haiwezekani kusema kwamba Shafaa maana yake ni ile dua ya siku ya kisimamo cha Kiyama, lakini kinachowezekana kusemwa ni kwamba, katika maana zilizo wazi kuhusu Shafaa ni dua na pia kwamba yeyote anayemsemesha mmoja miongoni mwa Mawalii akasema, "Ewe mwenye cheo mbele ya Mwenyezi Mungu tuombee kwa Mwenyezi Mungu", huwa hakusudii ila maana ya dua.

Amepokea Nidhamud-dini An-Nishapuri, kuhusu tafsir ya kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Surat an-Nisa aya ya 85 isemayo: "Yeyote atakayeombea maombezi mabaya atakuwa na sehemu katika mabaya hayo." Yeye Nidhamud-din amepokea toka kwa Muqatil amesema: "Shafaa kwa Mwenyezi Mungu maana yake ni kumuombea Muislamu". Na pia imepokelewa kwa Mtume **[s.a.w.w]** kwamba, anayemuombea nduguye Muislamu hali ya kuwa hayupo, maombi yake hukubaliwa, nao Malaika husema (kumuambia aliyeomba) nawe upate mfano wa hayo uliyomuombea nduguyo. Hakika huyu Ibn Taimiyya yeye ni miongoni mwa wale ambao wanaofahamu wazi kwamba, kuomba dua kwa mtu aliye hai (akuombee) ni jambo sahihi, na kwa msingi huu basi kutaka Shafaa hakumuhusu Mtume na Mawalii wa Mwenyezi Mungu peke yao, bali pia inafaa jambo hilo kwa kila muumini mwenye daraja tukufu mbele ya Mwenyezi Mungu.

Al-Imam Fakhrudin Razi, ni miongoni mwa wale wanaoifasiri maana ya "Shafaa" kuwa ni dua na ni Kutawas-sal kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Amesema Fakhrudin Razi katika kufasiri kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

وَيَسْتَغْفِرُونَ لِلَّذِينَ آمَنُوا رَبَّنَا وَسِعْتَ كُلَّ شَيْءٍ رَّحْمَةً ﴿٧﴾

"Na wanawaombea msamaha wale walioamini (kwa kusema), Ewe Mola wetu umekienea kila kitu kwa Rehema." - Qur'an, 40:7.

akasema kama ifuatavyo: "Aya hii inajulisha kuwepo kwa Shafaa toka kwa Malaika kuwaombea waja wenye dhambi.... Na litakapothibiti jambo hili katika haki ya Malaika (kuwaombea wenye dhambi) basi hali itakuwa ni hiyo hiyo katika haki ya Manabii kuwaombea wenye (dhambi) kutokana na kukubaliana Ijmai kwamba hakuna tofauti yoyote kati ya Malaika na Manabii katika jambo hili.

Na amesema vile vile kwamba: Kadhalika Mwenyezi Mungu amemwambia Mtume Muhammad **[s.a.w.w]** "Omba msamaha kwa makosa yako na uwatakie msamaha waumini wanaume na waumini wanawake", (Mwenyezi Mungu) akamuamuru Mtume kwanza aombe msamaha kwa ajili ya nafsi yake mwenyewe kisha awaombee msamaha wengine." Pia Mwenyezi Mungu anasimulia habari za Nuhu [a.s] kwamba, yeye Nuhu alisema: "Ewe Mola wangu nisamehe mimi na wazazi wangu na umsamehe yeyote atakayeingia nyumbani mwangu hali ya kuwa ameamini na uwasamehe waumini wanaume na waumini wanawake".[1] Ufafanuzi huu wa Fakhrur-razi unashuhudia kwamba yeye anaona maana ya Shafaa kuwa ni maombi ya mwenye kumshufaiya mwenye dhambi na kuomba Shafaa ni kuomba dua kwa huyo mwenye kushufaia.

1. Tafsir Fakhrur-Razi, Juz. 7, uk 33-34.

Pia imekuja katika hadithi nyingi za Mtume **[s.a.w.w]** kwamba, dua ya Mwislamu kumuombea nduguye Mwislamu ni kumshufaia. Imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas naye kapokea toka kwa Mtume **[s.a.w.w]** kwamba, Mtume amesema: "Hapana mtu yeyote Muislamu atakayekufa kisha wakasimama kusalia Jeneza lake watu arobaini wasiomshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote isipokuwa Mwenyezi Mungu atakubali uombezi wao kwa mtu huyo".[1] Kwa hakika imekuja katika hadithi hii matumizi ya maneno Shafaahumullahu fihi kwa ajili ya wale wanaomuombea ndugu yao mwislamu ili kuonyesha maana ya Shafaa kuwa ni dua. Kwa mujibu wa hadithi, lau mtu atawausia (katika uhai wake) watu arobaini miongoni mwa marafiki zake, wasimame kusalia Jeneza lake atakapokufa na wamuombee, basi mtu huyo atakuwa amewaomba watu hao "Shafaa" na atakuwa ameandaa uombezi wa waja wa Mwenyezi Mungu kumuombea nafsi yake. Naye Bukhari katika Sahih yake ametenga mlango maalum akauita "Watu watakapoomba Shafaa kwa Imam awaombee mvua basi asiwakatalie". Na ametenga mlango mwingine pia ambao ameuita "Pindi washirikina watakapoomba Shafaa kwa Waislamu wakati wa ukame".[2] Na hadithi zote ambazo Bukhari amezitaja katika milango yote miwili zinajulisha kwamba kuomba "Shafaa" ni kuomba dua na wala haifai kuifasiri Shafaa kwa maana nyingine ila hiyo.

Mpaka hapa tumemaliza kutoa dalili ya Shafaa katika sehemu ya kwanza, na imethibiti kwamba, kuomba Shafaa ni kuomba dua wala siyo kinyume chake. Na sasa hivi tunaanza uchunguzi wa maudhui ya pili ambayo ni kwamba, "kumuomba dua Muumini (akuombee) ni jambo mustahabu basi vipi kuomba dua kwa Mitume na Mawalii wa Mwenyezi Mungu?

## 2). QUR'AN NA KUOMBA DUA TOKA KWA WATU WEMA

Aya nyingi za Qur'an zinashuhudia kwamba Mtume **[s.a.w.w]** anapowaombea msamaha kwa Mwenyezi Mungu baadhi ya waja wake ni jambo lenye manufaa sana. Mwenyezi Mungu anasema:

وَاسْتَغْفِرْ لِذَنبِكَ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ ﴿١٩﴾

1. "Omba msamaha kwa makosa yako na uwaombee waumini wa kiume na waumini wa kike". Qur'an, 47:19.

وَصَلِّ عَلَيْهِمْ إِنَّ صَلَاتَكَ سَكَنٌ لَّهُمْ ﴿١٠٣﴾

2. "Na uwaombee dua, hakika kuwaombea kwako dua kutawapa utulivu (wafanikiwe). Qur'an, 9:103

Iwapo dua ya Mtume **[s.a.w.w]** aombapo inaleta matokeo haya mazuri kwa yule anayeombewa, basi kuna kizuwizi gani kwa mtu kuomba kwa Mtume amuombee mtu huyo hali ya kuwa tunajua kwamba kuomba dua ni kuomba Shafaa kwa Mtume. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema:

وَلَوْ أَنَّهُمْ إِذ ظَّلَمُوا أَنفُسَهُمْ جَاءُوكَ فَاسْتَغْفَرُوا اللَّـهَ وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ الرَّسُولُ لَوَجَدُوا اللَّـهَ تَوَّابًا رَّحِيمًا ﴿٦٤﴾

---

1. Sahih Muslim, Juz. 3, uk. 53.
2. Sahih Bukhari, Juz.1.

"Na lau wangelikujia walipojidhulumu nafsi zao wakaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu na Mtume naye akawaombea msamaha, bila shaka wangemkuta Mwenyezi Mungu ni mwenye kupokea toba na mwenye kurehemu". Qur'an, 4:64.

Maana ya kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema, "Wangelikujia" ina maana ya kumjia Mtume **[s.a.w.w]** na kumtaka awaombee dua na msamaha, lau kama si maombezi ya Mtume kwao hao watu, basi kuja kwao kusingekuwa na maana ila upuuzi na mchezo tu. Kwa hakika kufika kwao mbele ya Mtume **[s.a.w.w]** na kuomba kwake dua awaombee msamaha ni dalili ya kuathirika nafsi zao na kupatikana mabadiliko yanayoandaa njia inayofaa ya kukubaliwa dua. Qur'an inawanakili watoto wa Yaqub [a.s] ya kwamba, wao walimuomba baba yao awaombee msamaha kwa Mwenyezi Mungu, naye akaitikia maombi yao na akatekeleza ahadi yake. Mwenyezi Mungu anasema:

قَالُوا يَا أَبَانَا اسْتَغْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا إِنَّا كُنَّا خَاطِئِينَ ﴿٩٧﴾ قَالَ سَوْفَ أَسْتَغْفِرُ لَكُمْ رَبِّي ...﴿٩٨﴾

"Wakasema, Ee baba yetu tuombee msamaha kwa makosa yetu, hakika sisi tulikosea, akasema nitakuombeeni msamaha kwa Mola wangu..." Qur 'an, 12:97-98.

Aya zote hizi zinajulisha kwamba kuomba dua kwa Manabii na watu wema jambo ambalo ndiyo kuomba Shafaa halipingani na hukumu za kisheria, kanuni na mizani ya Kiislamu. Ewe msomaji Mtukufu, ziko hadithi nyingi zinazohusu kuomba dua kwa waja wema na Mawalii, lakini tumeziacha ili kufupisha maelezo.

### 3).HADITHI ZA MTUME NA SERA YA MASAHABA

Tirmidhi amepokea ndani ya Sahih yake kutoka kwa Anas kwamba amesema: "Nilimuomba Mtume **[s.a.w.w]** aniombee siku ya Qiyama akasema, mimi nitafanya, mimi nikasema, basi nitakuona wapi siku hiyo? Akasema: kwenye Sirat.[1] Hadithi nyingine ni ile ambayo Sawad bin Qarib alipokuja kwa Mtume **[s.a.w.w]** akimtaka amshufaiye akasema katika beti za kishairi alizoziimba: "Uwe wewe Mtume ndiyo muombezi wangu katika siku ile (ambayo) hakuna mwenye kuombea atakayemnufaisha Sawad bin Qarib japo kidogo.[2]

Na yapo maelezo yaliyokuja katika historia kwamba, kuna mtu mmoja aliyekuwa akiitwa "Tub-baa", na aliishi miaka zaidi ya Elfu moja kabla ya kudhihiri Mtume **[s.a.w.w]**., pia habari za kudhihiri kwa Nabii wa zama za mwisho kutoka Makka zilikwisha kumfikia, basi aliandika maandiko akayatoa kwa baadhi ya jamaa zake ili wamfikishie Mtume **[s.a.w.w]**., ndani ya maandishi hayo alieleza imani yake na Uislamu wake na kwamba yeye ni katika umati wa mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]**. Akasema katika maandiko hayo: "Iwapo sitakuwahi (Ewe Muhammad) basi niombee siku ya Qiyama usinisahau". Bwana huyu alifariki, lakini maandiko yake yakawa yanapokewa toka kwa mtu hadi kwa mwingine mpaka alipodhihiri Mtume **[s.a.w.w]**. Na yalipomfikia maandishi haya mikononi mwake, Mtume

1. Sunan Tirmidhi Juz. 4, uk. 42, Babu Maajaafi Shaan Sirat.
2. Ad-durarus-Saniyyah cha Zaini dahlan Uk. 29.

**[s.a.w.w]** alisema, "Karibu ewe ndugu mwema" mara tatu".[1] Basi iwapo kuomba Shafaa ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu, Mtume asingemwita yule "Tub-baa" kuwa ni 'Ndugu mwema" na wala asingesema mara tatu "karibu". Hizi ni baadhi ya hadithi ambazo zinathibitisha kuruhusu kuomba dua na uponyo toka kwa Mtume **[s.a.w.w]** zama za uhai wake.

### 4). KUOMBA SHAFAA BAADA YA KUFA

Zipo riwaya nyingi zinazofahamisha kwamba Masahaba walikuwa wakiomba Shafaa kwa Mtume **[s.a.w.w]** baada ya kufa kwake. Hebu tazama baadhi ya mifano ifuatayo:

1. Ibn Abbas amesema: "Pindi Amiril-Mu'minina Ali [a.s] alipomaliza kumkosha Mtume **[s.a.w.w]** alisema; "**Baba na mama yangu wawe fidia kwako unapendeza ukiwa mzima au umekufa.... tukumbuke mbele ya Mola wako.**"[2]

2. Na imepokelewa kwamba, alipofariki Mtume **[s.a.w.w]**, Abu Bakr alimfunua Mtume usoni kisha akaumbusu na akasema: "Baba na mama yangu wawe fidia kwako unapendeza ukiwa mzima au umekufa, tukumbuke mbele ya Mola wako".[3]

Riwaya mbili hizi na nyingine kama hizi zinajulisha kwamba, hakuna tofauti baina ya kuomba Shafaa kwa muombezi katika hai wake, na baada ya kufa kwake, na Masahaba walikuwa wakiomba dua kwa Mtume **[s.a.w.w]** baada ya kufariki kwake. Ikiwa kuomba dua kwa Mtume **[s.a.w.w]** baada ya kufa kwake ni jambo sahihi basi kuomba Shafaa ambayo ni aina za dua itakuwa ni sahihi pia. Kwa ufupi, kwa kutegemea aya na riwaya pamoja na sera ya Waislamu kwa karne nyingi zilizopita kuomba Shafaa ni jambo litakalozingatiwa kuwa ni sahihi moja kwa moja wala hakuna nafasi ya kufanyia shaka jambo hili kabisa.[4]

## DALILI ZA MAWAHABI ZA KUHARAMISHA KUOMBA SHAFAA

Tumetaja ndani ya mlango uliopita dalili zinazoruhusu kuomba Shafaa, zikiwemo hadithi mbali mbali na aya za Qur'an. Sasa hivi umefika wakati wa kutaja dalili za Mawahabi ambazo wanadai kwamba zinaharamisha Shafaa, zikiwemo hadithi mbali mbali na aya za Qur'an. Huu ndiyo ule wakati muafaka wa kutaja zile dalili za Mawahabi ambazo wanadai kwamba zinaharamisha Shafaa na kuzijadili (ili Mwenyezi Mungu aithibitishe haki kwa maneno yake). Mawahabi wametolea ushahidi mambo kadhaa katika kuharamisha Shafaa, nasi tunayataja kama ifuatavyo:

### 1) WANASEMA: "KUOMBA SHAFAA NI KUMSHIRIKISHA MWENYEZI MUNGU"

Wanachokikusudia Mawahabi katika shirki ni ile shirki ndani ya Ibada, kiasi wanadai kwamba kuomba kwa huyo anayeshufaiya ni kumuabudu. Katika mlango uliopita tumeeleza kwa upana maana ya Ibada na tumetaja kwamba, ombi Ia mtu kuomba Shafaa litakuwa Ibada tu ikiwa litatolewa na

---

1. (1) Al-Maqib cha Ibn Shah-rashuu Juz. 1, uk. 16 (2) Biharul-an-war, juz.15, uk 224.
2. Nah-jul-Balagha Khut-ba Na. 230.
3. Kash-ful-ir-tiyab uk 65, akinakili kutoka Khulasatul-kalaam.
4. Tumeandika kitabu maalum juu ya Shafaa na tumetaja ndani yake hadithi mia moja, arobaini na nne katika hizo zinatoka katika vitabu vya Kisunni, na zilizobaki zinatoka katika vitabu vya Kishia, ili kufahamu zaidi rejea kitabu hicho.

muombaji haliya kuwa anaitakidi kuwa huyo mwenye kuombwa Shafaa ni Mola au ni Mungu au yeye ndiye asili ya kupatikana matendo ya Mwenyezi Mungu, na kwamba muombeaji huyo ndiyo msimamizi halisi wa mambo ya ulimwengu na anasimamia yote ambayo (kwa asili na ukweli) yanarejea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu (kuwa ndiyo muumba wa mambo hayo).

Hakika (ilivyo ni kwamba) mtu anayeomba Shafaa kwa waombeaji ambao Mwenyezi Mungu amewapa idhini ya kuombea, huwa anaitakidi kuwa wao ni waja wa Mwenyezi Mungu waliokaribu naye na ni watukufu na wenye heshima mbele ya Mwenyezi Mungu.

Hapana itikadi ya kuwa wao ni Miungu au eti wao ndio asili ya matendo ya Mwenyezi Mungu, na hakuna itikadi ya kuwa eti uombezi huo au msamaha wa Mwenyezi Mungu umetegemezewa kwao moja kwa moja bila ya kuhitajia idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hakuna kabisa itikadi za aina hiyo, kwani waombeaji hao wema huwa wanaombea kwa idhini ya Mwenyezi Mungu kumuombea anayestahiki hiyo Shafaa na hii ni kwa sababu ya kuwepo maungamano yao ya kiroho ambayo hayakatiki. Ukweli unaojitokeza ni kwamba, lau kama kuomba shafaa kwa mtu aliyekufa maana yake itakuwa ni kumuabudu, basi kuomba Shafaa kwa mtu aliye hai pia itakuwa ni kumuabudu.

Katika mlango uliotangulia tumetaja kwamba Qur'an inawataka Waislamu waende kwa Mtume **[s.a.w.w]** na wamuombe awaombee msamaha kwa Mwenyezi Mungu, hivyo basi ombi hili kwa Mtume **[s.a.w.w]** ni kuomba Shafaa katika zama za uhai wake na haiwezekani tendo hili la kumuomba Mtume Shafaa liwe ni shirki katika wakati fulani na wakati mwingine liwe ni tendo la tauhidi ya Mwenyezi Mungu. Kama ambavyo tumetaja pia katika mlango wa kuomba msaada kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu kwamba, "Iwapo kuomba Shafaa kwa Walii mwema, hakutakuwa kwa kumuitakidia Uungu Walii huyo, basi Shafaa hiyo haitazingatiwa kuwa ni shiriki kabisa. Kwa mfano Mwenyezi Mungu anasema: "Peke yako tu tunakuomba msaada". Qur'an, 1:5.

Hapa ina maana kwamba msaada ni jambo linalomuhusu yeye Mwenyezi Mungu peke yake. Baadaye Mwenyezi Mungu anasema: "Tafuteni msaada kwa kusubiri na kuswali". Qur'an, 2:45.

Basi je mtu anaweza kusema kwamba kutafuta msaada kwa kusubiri ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu? Moja kwa moja jibu lake ni hapana, kwani kutaka msaada kulikoharamishwa ni kule kutakakoambatanishwa na itikadi ya uungu wa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, jambo ambalo hakuna anayeliamini miongoni mwa Waislamu.

### 2) WASHIRIKINA NA UOMBEZI WA MASANAMU

Baada ya kuibatilisha dalili ya kwanza ya Mawahabi inayoharamisha kuomba Shafaa kwa Mawalii, sasa ni wakati mwingine na kuibatilisha dalili ya pili ambayo ni: "Mwenyezi Mungu aliwazingatia wanaoabudu masanamu kuwa ni washirikina kwa kuwa wao walikuwa wakiomba Shafaa kwa masanamu yao, na walikuwa wakilia mbele ya masanamu hayo na kuyaomba uwakala kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَيَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّـهِ مَا لَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنفَعُهُمْ وَيَقُولُونَ هَـٰؤُلَاءِ شُفَعَاؤُنَا عِندَ اللَّـهِ ﴿١٨﴾

"Wanaabudu visivyokuwa Mwenyezi Mungu, vitu ambavyo haviwezi kuwadhuru wala kuwanufaisha, na (walipoulizwa kwa nini wanaviabudu) husema hawa ni waombezi wetu mbele ya Mwenyezi Mungu". Qur'an, 10:18.

Na kwa msingi huu basi, kumuomba Shafaa asiyekuwa Mwenyezi Mungu kwa ujumla kutafahamika kuwa ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu na ni kumuabudu muombezi huyo.

### JAWABU LA MADAI HAYO

**Kwanza**: Katika aya hii hakuna kabisa dalili yoyote iliyopo wanayoidhani Mawahabi kuwa inawaunga, kwani Qur'an kwa mujibu wa aya hii inapowaona watu hao kuwa ni washirikina siyo kwa ajili ya kuomba Shafaa kwa masanamu bali ni kwa sababu ya wao kuyaabudu Ibada ambayo imewapelekea wayaombe Shafaa vile vile. Na kama ingekuwa kile kiasi cha kutaka Shafaa kwa masanamu ni kuyaabudu jambo ambalo lingewajibisha shirki, kusingekuwa na haja yoyote kwa Mwenyezi Mungu kusema "na wanasema kuwa hawa ni waombezi wetu" bali kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo "Wanayaabudu" ingetosha kuwahusisha watu hao na ushirikina, lakini kuongezeka kwa sentensi ile ya pili baada ya ile ya kwanza ni dalili ya kwamba vitu hivyo viwili ni tofauti na pia kwamba maudhui ya kuabudia masanamu ni tofauti na maudhui ya kutaka Shafaa kwa hayo masanamu. Kwa hakika kuyaabudu Masanamu ni dalili ya kumshirikisha Mwenyezi Mungu Mtukufu, ama kuomba Shafaa kwa jiwe au ubao ni dalili ya ujinga na kukosa akili, pia ni kutokuwa na busara.

Zaidi ya hapo aya hii tuliyoitaja hapo kabla haijulishi kwamba kutaka Shafaa kwa masanamu ni kuyaabudu, basi vipi itawezekana kuzingatia kuwa kuomba Shafaa kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu ni dalili ya kuwaabudu Mawalii hao? Kwa hiyo aya hii haina mafungamano kabisa na maudhui ya Shafaa. Pili: Hebu tukadirie (kama mjadala) kwamba sababu ya shirki kwa watu hao waliotajwa ndani ya aya ni kule kuomba kwao Shafaa kwa masanamu, lakini ieleweke pia kwamba baina ya hao washirikina kuomba kwao Shafaa kwa masanamu na Waislamu kuomba Shafaa kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu, kuna tofauti kubwa na kuna utengano mfano wa masafa yaliyopo baina ya mbingu na ardhi, hasa kwa kuwa washirikina hao walikuwa wakiamini kuwa, masanamu hayo yanaimiliki hiyo Shafaa na msamaha kama kwamba Mwenyezi Mungu hahusiki kabisa katika mambo hayo mawili, na waliyaona hayo masanamu ndiyo yenye uamuzi wote wa kusamehe na kushufaiya.

Basi ukweli uko wazi kusema kwamba kuomba Shafaa kwa namna hii itakuwa ni kuyaabudu masanamu hayo kwa kuwa Shafaa hii imeambatanishwa na itikadi ya uungu kwa masanamu hayo na vile vile yenyewe kufanywa ndiyo chimbuko la matendo ambayo ni ya Mwenyezi Mungu katika hali ya kuendesha ulimwengu. Kwa hiyo basi Mwislamu huwa anaomba Shafaa na dua kwa huyo mwenye kushufaiya hali ya kumuitakidi kwamba yeye ni mja aliyekurubishwa kwa Mwenyezi Mungu na ni mja mwenye heshima na utukufu aliyepewa ruhusa ya kuombea toka kwa Mwenyezi Mungu. Ewe msomaji, hivi kudai kwamba hakuna tofauti baina ya Shafaa hizi mbili (iliyofanywa na washirikina kwa masanamu yao na ile ifanywayo na Waislamu kwa Mitume na Mawalii) ni kupingana na

akili na mantiki na ni kuacha uadilifu? Je, huoni tofauti iliyopo kati ya mambo haya mawili kama unavyoweza kuona tofauti baina ya kiza Ia usika na mwangaza wa mchana?

## 3).KUTAKA HAJA KWA ASIYEKUWA MWENYEZI MUNGU NI HARAMU

Baada ya kuivunja dalili ya pili ya Mawahabi inayoharamisha kuomba Shafaa kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu, sasa inakuja dalili yao ya tutu. Nayo ni ile inayokataza kumuomba na kumtaka haja asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na kudai kwamba kuomba Shafaa kwa Mawalii ni namna ya kutaka haja, basi jambo hili ni haramu kwani Qur'an inaeleza wazi wazi kama ifuatavyo: Mwenyezi Mungu amesema, "Msimuombe yeyote pamoja na Mwenyezi Mungu". Qur'an, 72:18.

Kuikusanya kauli inayoharamisha kumuomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu na kauli inayothibitisha kupatikana uombezi wa Mawalii nikumuomba Mwenyezi Mungu awaamuru Mawalii wake wamuombee mwanadamu. Na dalili ya kwamba kumuomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu ni kumuabudu huyo anayeombwa ni kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ ﴿٦٠﴾

"Niombeni nitakubali maombi yenu, hakika wale wajivunao kufanya Ibada yangu wataingia Jahanamu wadhalilike." Qur'an, 40:60.

Pindi tukiifanyia mazingatio aya hii tutaiona imeanza kwa tamko la 'Ad-dawat" kwa maana ya maombi, na imemalizikia kwa tamko la "Ibada". Basi hali hii inatuonyesha kwamba, Maf-humu ya maneno haya mawili ni moja. Imepokewa kwa Mtume **[s.a.w.w]** amesema: "**Dua ndiyo kiini cha Ibada**".[1] Jawabu Letu: Kwanza Tunasema: Siyo kweli kwamba makusudio ya kuharamisha kumuomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu katika aya iliyotajwa ni kuharamisha maombi kwa ujumla, lakini makusudio yaliyopo kwenye aya hiyo ni kuharamisha "kumuabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu". Ushahidi wa jambo hili uko mwanzoni mwa aya aliposema Mwenyezi Mungu, "Na kwa hakika misikiti yote ni ya Mwenyezi Mungu basi msimuombe (msimuabudu) yeyote pamoja na Mwenyezi Mungu".

Kwa hiyo basi mkusanyiko uliomo katika aya unajulisha kwamba dua iliyoharamishwa ni ile inayochanganywa na Ibada na kuitakidi uungu wa huyo anayeombwa na pia kuitakidi uwezo wake wa kuamua katika mambo ya viumbe na ulimwengu. Ukweli ulivyo ni kwamba, itikadi kama hii haipo miongoni mwa Waislamu ambao huomba Shafaa kwa mawalii wa Mwenyezi Mungu.

**Pili**: Kwa hakika kinachoharamishwa ndani ya aya hiyo nakukatazwa ni kumuabudu Mwenyezi Mungu pamoja na mwingine na kumfanya huyo kuwa yeye ni sawa na Mwenyezi Mungu katika dua (Ibada), kama inavyojulisha sentensi iliyoko kwenye aya isemayo "pamoja na Mwenyezi Mungu" yaani sawa naye. Basi iko haja ifahamike kwamba, mtu anapomuomba Mtume **[s.a.w.w]**. anyenyekee kwa Mwenyezi Mungu kumuombea mtu huyo ili shida yake itatuliwe au asamehewe makosa yake

1. Safinatul-bihar mada inayohusu dua.

haina maana kwamba mtu huyu atakuwa amemuomba (yaani amemuabudu) Mwenyezi Mungu pamoja na mwingine bali maombi haya ukweli wake ni kumuomba yeye Mwenyezi Mungu peke yake.

Na ikiwa ziko baadhi ya aya za Qur'an zinazofahamisha kuwa, kutaka haja kwa masanamu ni ushirikina, hiyo ni kwa sababu watu hao walikuwa wakiamini masanamu hayo kuwa ni Miungu wadogo wenye kumiliki kikamilifu maamuzi ya matendo ya Mwenyezi Mungu yote au sehemu yake, na ndiyo maana utaiona Qur'an inaikosoa fikra hii potofu. Qur'an inasema:

وَالَّذِينَ تَدْعُونَ مِن دُونِهِ لَا يَسْتَطِيعُونَ نَصْرَكُمْ وَلَا أَنفُسَهُمْ يَنصُرُونَ ﴿١٩٧﴾

"Na wale muwaombao kinyume cha Mwenyezi Mungu hawawezi kukusaidieni wala kujisaidia wenyewe nafsi zao"- Qur'an, 7:197.

Pia Qur'an inasema:

إِنَّ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّـهِ عِبَادٌ أَمْثَالُكُمْ ﴿١٩٤﴾

"Bila shaka hao muwaombao kinyume cha Mwenyezi Mungu ni viumbe kama ninyi". Qur'an, 7:194.

Kwa kufupisha maelezo ni kwamba, washirikina walikuwa wakiamini kuwa masanamu hayo ni miungu wadogo na kwamba matendo ya Mwenyezi Mungu yameegemezwa kwao moja kwa moja, lakini kuomba Shafaa na dua kwa mtu ambaye Mwenyezi Mungu amempa cheo hiki na haki hii hatuamini kwamba wao ni Miungu wadogo au matendo ya Mwenyezi Mungu yameegezwa kwao, basi kuna tofauti kubwa baina ya itikadi ya washirikina na itikadi ya utukufu wa walii mwema na mwenye heshima mbele ya Mwenyezi Mungu na kutaka kwake msaada mbele ya Mwenyezi Mungu. Je, Mawahabi hawana uadilifu wala hawatazami vitu kama vilivyo? Je, hawana akili kabisa?

**Tatu**: Kwa hakika neno 'Ad-dawah" lina maana pana kiasi kwamba wakati mwingine hutumika kimajazi kwa maana ya "Ibada" kama ambavyo (Mawahabi) walivyolitolea ushahidi katika aya ya 60 sura ya 7 tuliokwisha itaja hapo kabla, na pia katika hadithi ambayo tumeitaja huko nyuma. Lakini tunajua wazi kwamba matumizi haya ya kimajazi hayatoshi kuwa ni ushahidi wa kufasiri maana ya dua kuwa ni ibada kila wakati, au ushahidi wa madai kwamba kuomba haja kwa yeyote ni ushirikina.

## 4). SHAFAA NI HAKI INAYOMUHUSU MWENYEZI MUNGU TU

Ewe msomaji mpendwa, tumeibatilisha dalili ya tatu ya Mawahabi na sasa tunaitaja dalili yao ya nne ambayo ni kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

أَمِ اتَّخَذُوا مِن دُونِ اللَّـهِ شُفَعَاءَ ۚ قُلْ أَوَلَوْ كَانُوا لَا يَمْلِكُونَ شَيْئًا وَلَا يَعْقِلُونَ ﴿٤٣﴾ قُل لِّلَّـهِ الشَّفَاعَةُ جَمِيعًا ۖ لَّهُ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ ثُمَّ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٤٤﴾

"Au ndiyo wamejifanyia waombezi mbele ya Mwenyezi Mungu, waambie: Ijapokuwa hawana mamlaka juu ya kitu chochote wala hawatambui lolote? Waambie uombezi wote uko katika milki ya Mwenyezi Mungu". Qur'an, 39:43-44.

Makusudio ya kutolea ushahidi aya hii, ni kubainisha kwamba Shafaa ni jambo linalomuhusu Mwenyezi Mungu tu, kwa hiyo basi kuna maana gani kutaka Shafaa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu? Jawabu Lake: Mwenyezi

Mungu aliposema kwamba "Uombezi wote uko katika milki ya Mwenyezi Mungu" siyo maana yake kwamba Shafaa ni jambo linalo muhusu yeye Mwenyezi Mungu na hakuna mwingine mwenye haki ya kuombea. Na hii ni kwa sababu, hapana shaka kabisa kwamba, Mwenyezi Mungu hamuombei mtu fulani kwa (Mola) mwingine, bali maana iliyokusudiwa hapo ni kuwa, yeye Mwenyezi Mungu ndiye mwenye asili ya mamlaka ya Shafaa wala siyo masanamu, na hiyo ni kwa kuwa muombezi (mwenye kushufaiya) ni lazima kwanza awe na akili na utambuzi, na aweze huko kuombea kwa upande wa pili, kitu ambacho masanamu yamekosa sifa hizi mbili: Na kwa ajili hii Mwenyezi Mungu amesema:

**Kwanza**: "Waambie japokuwa hawana mamlaka juu ya kitu cho chote"?

**Pili**: "Wala hawatambui lolote?" Kwa hiyo aya inasisitiza kuwa, Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiyo mwenye mamlaka ya Shafaa siyo masanamu, na pia kwamba Mwenyezi Mungu humpa jambo hili (la Shafaa) mtu ambaye zimetimia sifa zinazostahiki kuwaombea waja wa Mwenyezi Mungu. Hivyo basi aya hii haina uhusiano na maudhui tunayoyazungumzia, hasa inapozingatiwa kwamba Waislamu wanaamini kuwa, Mwenyezi Mungu peke yake ndiye mwenye mamlaka ya Shafaa na wala siyo Mawalii wake, kadhalika Waislamu wanaamini kwamba yeyote ambaye Mwenyezi Mungu amempa ruhusa ya kuombea, basi anao uwezo wa kuombea kinyume cha mtu ambaye hakupewa ruhusa hiyo. Hali hii ya kushufaiya ndiyo ile ile ambayo Waislamu wanayoitakidi kwa kutegemea aya za Qur'an na hadithi kwamba, Mwenyezi Mungu amempa idhini Mtume **[s.a.w.w]** yeye na watu wa nyumba yake [a.s] ya kuombea, nasi kwa sababu hiyo basi tunaomba Shafaa yao. Kwa hiyo Ewe msomaji imekudhihirikia kutokuwepo uhusiano baina ya aya hizo na uchunguzi huu na kutokuwepo uhusiano bania ya hadithi waliyoitaja na uchunguzi huu.

### 5). UPUUZI WA KUTAKA SHAFAA KWA MAITI

Dalili ya mwisho ya Mawahabi juu ya kuharamisha Shafaa kwa Mawalii inasema kwamba: "Kuomba Shafaa kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu katika maisha haya (ya duniani) ni sawa na kuomba haja kwa maiti asiyesikia". Mawahabi wametolea ushahidi madai yao haya kwa aya mbili zifuatazo: **Kwanza**:

﴿إِنَّكَ لَا تُسْمِعُ الْمَوْتَىٰ وَلَا تُسْمِعُ الصُّمَّ الدُّعَاءَ إِذَا وَلَّوْا مُدْبِرِينَ ﴿٨٠﴾

"Kwa hakika huwezi kuwasikilizisha wafu mwito, wala kuwasikilizisha viziwi wanapogeuka wanakwenda zao". Qur'an, 27:80.

Makusudio ya kutolea ushahidi wa aya hii ni kwamba, Qur'an Tukufu imewafananisha washirikina na maiti na aya hii inamwambia Mtume **[s.a.w.w]** kwamba yeye hawezi kuwafahamisha washirikina hawa kwani wao nikama maiti hawasikii, kwa hiyo lau maiti wangekuwa wanao uwezo wa kusema na kusikia basi isingefaa washirikina kufananishwa na maiti. **Pili**:

﴿إِنَّ اللَّـهَ يُسْمِعُ مَن يَشَاءُ ۖ وَمَا أَنتَ بِمُسْمِعٍ مَّن فِي الْقُبُورِ ﴿٢٢﴾

"Bila shaka Mwenyezi Mungu humsikilizisha amtakaye na wewe huwezi kuwasikilizisha waliomo makaburini". Qur'an, 35:22.

Kutolea ushahidi aya hii ni sawa na ushahidi uliotolewa katika aya iliyotangulia kwa kutokuwepo uwezekano kwa maiti kusikia na kusema.

Kwa hiyo basi kuwaomba (maiti) Shafaa ni kama kukiomba Shafaa kitu kisicho uhai, kama vile mawe n.k.

**Jawabu Letu**: Bila shaka Mawahabi wamelifanya suala la shirki kuwa ndiyo ngao yao kila wanapoyakosoa madhehebu mbali mbali ya Kiislamu na kuwatuhumu Waislamu kwa ukafiri nyuma ya pazia la kutetea Tauhidi ya Mwenyezi Mungu na kuihusisha kwake Ibada. Lakini Mawahabi walipotolea ushahidi aya hizi wamebadilisha usulubu wao wakang'ang'ania usemi wao kuwa "kuomba Shafaa kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu ni jambo la upuuzi wala halina faida, kwa kuwa Mawalii hao wamekwisha kufa". Mawahabi hawa ambao Qur'an hawaifahamu vilivyo, wamejisahaulisha na kupuuza hata zile hoja za kiakili na sheria ambazo zinathibitisha kuwa hai kwa Mawalii hata baada ya kufa. Wanafalsafa wa Kiislamu wamethibitisha kwamba, baada ya roho kujitenga na mwili na kutoutegemea, yenyewe hubakia milele na kuishi maisha yanayohusiana na roho na ufahamu wa kiroho. Wanafalsafa wanaomuitakidi Mwenyezi Mungu wametaja dalili kumi za kiakili kuhusu jambo hili, kiasi kwamba hazikuacha nafasi ya mashaka na wasi wasi ndani yake kwa kila mtu muadilifu na mwenye akili. Zaidi ya hizo dalili za kiakili, Qur'an ambayo ni kitabu cha Mwenyezi Mungu imetangaza wazi wazi kuwepo kwa uhai baada ya kufa, pia ziko hadithi nyingi za Mtukufu Mtume **[s.a.w.w]** kuhusu jambo hili. Ili kuthibitisha unaweza kurejea katika Qur'an aya zifuatazo:

1) Aya 169-170 Sura ya 32) " 41 " 4.3) " 45 " 33.4) " 100 " " 23.5). " 46 " " 40.

Zote hizi zinathibitisha juu ya kuwepo uhai baada ya kifo. Basi ina hali gani hoja yenu dhaifu enyi Mawahabi? Na Je, zinamaanisha nini basi aya hizo mbili? Jawabu Lake: Bila shaka aya hizo mbili zinamaanisha kwamba, miili iliyolala makaburini haina uwezo wowote wakufahamu kitu, jambo ambalo linakubalika moja kwa moja, kwani mwili unapotengana na roho kinachobakia ni kitu (kiwiliwili) kisicho na fahamu wala akili. Lakini lazima ieleweke kwamba nukta muhimu tunayozungumzia hapa ni kwamba, wale ambao sisi tunawasemesha na kuwaomba Shafaa kama ambavyo Qur'an inasisitiza "siyo kiwiliwili kilichozikwa katika udongo bali ni roho takatifu zilizo hai ndani ya miili ya Bar-zakh katika ulimwengu wa Bar-zakh." Hivyo basi, ilivyokuwa hakuna uwezekano wa miili iliyozikwa ardhini kufahamu cho chote, hali hii haimaanishi kwamba roho takatifu za miili hiyo ambazo ni hai na zinaruzukiwa huko kwenye ulimwengu wa Bar-zakh eti nazo haziwezi kufahamu kitu. Na ifahamike pia kwamba, salamu, maamkizi na ziyara (zifanywazo na Waislamu kwa Mawalii) ni kwa ajili ya roho zenye nuru zinazobakia milele na ndizo zinazoombwa Shafaa. Na pengine utajiuliza, ni kwa nini Waislamu wanayazuru Makaburi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu? Jawabu: Ni kwa sababu ya mambo yafuatayo:

1. Zimekuja hadithi mutawatiri za Mtukufu Mtume **[s.a.w.w]** zinazohimiza kuzuru makaburi ya Mawalii, na katika mstari wa mbele wa hao katika umuhimu, ni Mtume **[s.a.w.w]** na watu wa nyumba yake watakatifu (amani ya Mwenyezi Mungu iwashukie), na kuna thawabu nyingi na radhi za Mwenyezi Mungu katika ziyara za makaburi hayo, nasi hapo kabla tumetaja baadhi ya hadithi zilizohimiza kuhyazuru wakati tulipokuwa tukizungumzia kuhusu kumzuru Mtume **[s.a.w.w]**.

2. Kuyazuru makaburi yao huwa kunaijenga hali ya kuwepo kwao (miongoni mwetu) na kuziandaa nafsi zetu kuwasiliana na roho zao tukufu, na hali zao za kiroho na wakati tunapowatolea salamu huwa tunajihisi kama kwamba tunaongea nao hali ya kuwa wanatusikiliza, kama ilivyokuja katika moja ya ziyara iliyowekwa na hao maasumin. "Nashuhudia kwamba wewe unashuhudia kisimamo changu na unayasikia maneno yangu, na kwamba wewe ni hai mbele ya Mola wako unaruzukiwa, basi muombe Mola wako ambaye ndiye Mola wangu anikubalie haja yangu.[1]

Kadhalika yemekuja mapokezi yasemayo: "Ewe Mwenyezi Mungu...Mimi nafahamu pia kwamba, Mtume wako na Makhalifa wako [a.s] wako hai mbele yako wanaruzukiwa, wanakiona kisimamo changu na wanasikia maneno yangu na wanajibu salamu yangu na wewe Mola wangu umeweka kizuwizi kwangu mimi kutoyasikia maneno yao (lakini) umefungua mlango wa fahamu zangu ili nipate utamu wa kuwazungumzisha".

3. Kuna hadithi tukufu chungu uzima zinazobainisha kwamba miili ya Manabii na Mawalii na wengineo pia hubakia katika udongo hali ya kuhifadhika bila ya kuharibika kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Jambo hili linayo masimulizi mengi na matukio mengi ambayo nafasi hairuhusu kuyaeleza. Tunatosheka kuashiria tukio lililotajwa na wanahistoria kwamba, Waislamu walichimba mifereji ya maji katika ardhi ya Uhdi huko Madina, miaka hamsini baada ya tukio la vita vya Uhdi. Walipokuwa wakichimba wakafukua miili iliyovuja damu ikiwa mizima kabisa kama kwamba imezikwa sasa hivi, kiasi hata sanda zake hazijaharibika. Habari za tukio hili zilipofika mjini Madina, watu walitoka mbio wakiwemo Masahaba na wengineo hata kina mama pia walitoka kwenda kushuhudia na waliitambua miili ya maiti hao kwa majina yao na majina ya wazazi wao na kwamba miili hiyo ilikuwa ya mashahidi wa Uhdi.

Miili hiyo ilibakia katika hali ya usalama ikazishinda zama na mchanga (kutoiharibu) kwa idhini ya Mwenyezi Mungu muweza. Ikiwa miili ya mashahidi hawa imeweza kubakia katika hali hii, basi vipi mwili wa Mtume **[s.a.w.w]** na Maimamu watukufu wa kizazi cha Mtume? Hapana shaka miili yao itabakia katika hifadhi dhidi ya kila aina ya uharibufu hasa kwa kuwa miili hiyo inao utukufu mkubwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Vile vile sehemu ambayo umezikwa mwili wa mmoja wa Mawalii wa Mwenyezi Mungu, inapata utukufu kwa ajili ya Walii huyo, hivyo basi kufika mahali hapo patukufu huwa panamsababishia mtu kupata rehma na baraka za Mwenyezi Mungu. Mpaka hapa ewe msomaji, imekudhihirikia kwamba, dalili wazitumiazo Mawahabi kuharamisha kuomba Shafaa kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu ni dalili dhaifu, na ukweli ni ule ambao Waislamu wanautenda kwa kufuata Qur'an na hadithi tukufu za Mtume **[s.a.w.w]**.

---

1. Kitabu Ud-datid-daai, cha Ibn Fahd AI-hilli, imepokewa toka kwa Imam Jaafar As-Saadiq [a.s].

16

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## KUITAKIDI UWEZO WA GHAIB WA MAWALII WA MWENYEZI MUNGU

Je, kuitakidi kwamba Mawalii wa Mwenyezi Mungu wanao uwezo wa ghaib ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu? Bila shaka hakuna wasi wasi kwamba, mtu hawezi kuomba haja yake kwa yeyote yule ila atakapokuwa na uhakika wa uwezo wa huyo amuombaye kuwa atamtimizia haja yake na kutekeleza ombi lake. Uwezo huu umegawika sehemu mbili:

1. Uwezo wa kimaada unaoonekana kama vile kumuomba maji mtu fulani kisha akakujazia maji hayo kwenye chombo na akakupatia.

2. Uwezo wa ghaib uliojitenga na mazingira ya maada ulio nje ya matendo ya kimaumbile, kwa mfano mtu akaamini kwamba, Imam Ali bin Talib [a.s] anao uwezo wa kuung'oa mlango wa Khaibar, ambao kwa kawaida mtu hawezi kuung'oa bali yeye Imam Ali [a.s] anaweza kwa kutumia nguvu ya ghaibu ambayo iko juu kuliko uwezo wa watu. Au mtu akaamini kwamba Nabii Isa [a.s] kwa maombi yake ya kumponya mgonjwa ambaye ugonjwa wake umeshindikana kupona, lakini Nabii Isa anamponya mgonjwa huyo bila kutumia dawa yoyote au kufanya operesheni. Kama umeifahamu mifano hii, basi fahamu pia kwamba kuamini uwezo wa ghaibu ikiwa uliotegemezewa kwenye uwezo wa Mwenyezi Mungu na idhini yake na kutaka kwake, ni sawa na kuitakidi uwezo ulioko katika maumbile ya mazingira ya kimaada na wala siyo kumshirikisha Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwani yeye Mwenyezi Mungu ndiye muweza wa kumpa mtu uwezo wa mazingira ya kimaada na ndiye anayempa mwingine uwezo wa ghaibu. Na katika kuamini jambo hili inatakiwa pasiwe na imani kwamba, kiumbe aliyepewa uwezo huu yeye hahitajii msaada na uwezo wa Mwenyezi Mungu.

### MAONI YA KIWAHABI

Wawahabi wanaitakidi kwamba, lau mtu atamuomba haja fulani mmoja wa Mawalii wa Mwenyezi Mungu, awe hai Walii huyo au aliyekwisha fariki, kwa mfano, akamuomba amponye maradhi yake au amrejeshee kitu chake kilichopotea, na au kumlipia deni lake na mengineyo, basi mtu huyo atakuwa ameamini kuwepo uwezo wa siri kwa huyo aliyemuomba kiasi cha kuwa anaweza kwa uwezo huo kukiuka kanuni za kimaumbile zitumkazo katika ulimwengu huu. Na kwa ajili ya kuitakidi uwezo huu kuwa anao mwingine asiyekuwa Mwenyezi Mungu, basi itakuwa ni kuamini uungu wa huyo asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na kumuomba pamoja na itikadi hii ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa kufafanua ni kwamba: Kwa maoni ya Kiwahabi; lau mtu yuko jangwani na ana kiu ya maji, kisha akamuomba mtumishi wake ampe maji, ombi hili halikiuki kanuni za kimaumbile na linafaa na siyo shiriki. Ama ikiwa mtu ataomba ombi kama hili hili kumuomba Mtume au Imam ambaye amezikwa au anayeishi sehemu nyingine katika mji mwingine au akawa hayupo machoni mwake, basi ombi hilo ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kuwa ameitakidi kwamba Nabii huyo au Imam huyo anaweza kumtatulia shida ya

maji kinyume na mfumo wa kanuni na sababu za kimaumbile, yaani kumpa uwezo wa siri. Na itikadi hii ni kuitakidi uungu kwa huyo anayeombwa ikiwa ni Nabii au Imam. Maoni haya ya Kiwahabi ameyafafanua zaidi mwandishi wa Kiwahabi aitwaye "Abul-aala Al-maududi" akasema: "Bila shaka sifa ambayo kwayo mtu humuomba Mola na kumtaka msaada na kumnyenyekea lazima itakuwa ni ile sifa ya kuwa kwake yeye Mola ndiye mwenye kumiliki uwezo wa kusimamia kanuni za maumbile".

### MAONI YETU JUU YAMANENO HAYA

Bila shaka kosa alilolifanya Maududi na wengineo kama yeye ni kwamba, yeye ameona kuwa kuamini kuwepo uwezo wa siri kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu ni kumshirikiisha Mwenyezi Mungu moja kwa moja, na hakutofautisha au hakutaka kutofautisha baina ya kuamini uwezo huo wa siri unaotoka kwa Mwenyezi Mungu na kumtegemea yeye na ule uwezo ambao haumuhitajii Mwenyezi Mungu, wakati ambapo ushirikina ni hii itikadi ya pili siyo ile ya kwanza (yaani uwezo wa kutokumuhitajia Mwenyezi Mungu). Nayo Qur'an Tukufu inataja wazi wazi majina ya watu ambao walikuwa nao uwezo wa siri, na matakwa yao yalikuwa yakienda kinyume na kanuni za kawaida na kuzibadilisha nyendo zake. Hebu angalia baadhi ya majina ya watu ambao Qur'an imewataja:

### 1). UWEZO WA SIRI WA NABII YUSUF [a.s]

Nabii Yusuf [a.s] aliwaambia nduguze:

اذْهَبُوا بِقَمِيصِي هَـٰذَا فَأَلْقُوهُ عَلَىٰ وَجْهِ أَبِي يَأْتِ بَصِيرًا وَأْتُونِي بِأَهْلِكُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٩٣﴾

"Nendeni na kanzu yangu hii na muiweke usoni mwa baba yangu, yeye atafunuka macho aone; basi alipokuja mtoaji wa habari ujema akaiweka (kanzu ya Yusuf) usoni mwake mara aliona". Qur'an, 12:93 na 96.

Dhahiri ya aya inayoonyesha kwamba Nabii Yaaqub [a.s] macho yake yalirudi (akaona) kikamilifu kutokana na uwezo wa siri alioutumila Nabii Yusuf [a.s] ili kuyarejesha macho hayo. Ukweli ulivyo ni kwamba kurejea kwa macho ya Nabii Yaaqub [a.s] hakukutokana na Mwenyezi Mungu kwa sura ya moja kwa moja, bali liliwezekana jambo hilo kwa idhini yake Mwenyezi Mungu lakini kupitia kwa Nabii Yusuf [a.s]. Kwa hiyo basi, Nabii Yusuf [a.s] yeye alikuwa ndiye sababu ya kurudi macho ya baba yake kikamilifu, na lau si hivyo basi asingewaamuru nduguze waende na kanzu yake na kuiweka usoni mwa baba yake bali angemuomba Mwenyezi Mungu tu ili jambo hilo litimie. Hii bila shaka ndiyo nguvu ya siri iliyotoka kwa Nabil Yusuf [a.s] mmoja wa Mawalii wa Mwenyezi Mungu, na alibadilisha mwenendo wa kawaida kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na hapana yeyote awezaye kutenda hivi isipokuwa yule tu aliyepewa na Mwenyezi Mungu uwezo huo wa siri.

### 2). UWEZO WA SIRI WA NABII MUSA [a.s]

Mwenyezi Mungu alimpa Nabii Musa [a.s] uwezo wa siri pale alipolipiga jiwe kwa fimbo yake na zikapasuka chemchem kumi na mbili kufuatia idadi ya makabila ya wana wa Israil kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

فَقُلْنَا اضْرِب بِّعَصَاكَ الْحَجَرَ فَانفَجَرَتْ مِنْهُ اثْنَتَا عَشْرَةَ عَيْنًا ﴿٦٠﴾

"Tulimwambia (Musa) lipige jiwe kwa fimbo yako, basi (alipopiga) zilipasuka chemchem kumi na mbili". Qur'an, 2:60.

Nabii Musa [a.s] pia alitumia uwezo wake wa siri kwa mara nyingine pale alipoipiga bahari kwa fimbo yake ili afungue njia kumi na mbili zilizo kavu ndani ya bahari wapate kupita wana wa Israel na waivuke bahari hiyo, (baada ya kuipiga) maji yalijikusanya kama milima pembeni ya njia hizi bila ya kurukia japo tone dogo la maji njiani!!! Mwenyezi Mungu anasema:

فَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ أَنِ اضْرِب بِّعَصَاكَ الْبَحْرَ فَانفَلَقَ فَكَانَ كُلُّ فِرْقٍ كَالطَّوْدِ الْعَظِيمِ ﴿٦٣﴾

"Basi mara tulimpelekea Musa ufunuo (Wahyi) tukamwambia, ipige bahari kwa fimbo yako, (alipopiga) ikatengana na kila sehemu ikawa kama mlima mkubwa". Qur'an, 26:63.

Ndani ya sehemu mbili hizi haiwezekani kabisa kujifanya hatujuwi nafasi ya Nabii Musa [a.s] katika kupasua chemchem na kufungua njia ndani ya bahari, na kufaidika kwa nguvu yake ya siri, yote haya yalithibitika kwa idhini ya Mwenyezi Mungu na kutaka kwake.

### 3). UWEZO WA SIRI WA NABII SULEIMAN [a.s]

Ni mara nyingi Nabii Suleiman [a.s] alikuwa akinufaika kwa uwezo wa siri, na ameielezea zawadi hiyo tukufu ya Mwenyezi Mungu ambayo amepewa kwa kauli yake mwenyewe kama ilivyo ndani ya Qur'an Tukufu. "Na tumepewa kutokana na kila kitu". Qur'an, 27:16.

Ufafanuzi wa maelezo ya zawadi na uwezo aliopewa Nabii Suleiman [a.s] umo ndaji ya sura ya An-namli kuanzia aya ya 16 hadi aya ya 44, na sura Sabai aya ya 12, pia sura Anbiyaa aya ya 81 na sura Saad kuanzia aya ya 36 hadi aya ya 40. Bila shaka kufanya mazingatio katika aya hizi kutatudhihirishia wazi zawadi hizi tukufu na uwezo wa siri ambao Mwenyezi Mungu amempa mja wake na Nabii wake Suleiman [a.s]. Na kabla hujaifungua Qur'an ili kuzisoma aya zilizoashiriwa, hapa tunakutajia baadhi ya aya hizo ili ikukalie wazi hali ya utukufu wa uwezo huo wa siri, na uone kwa macho yako kwamba Qur'an Tukufu inavyouthibitisha uwezo huo wa siri kwa baadhi ya waja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Nabii Suleiman [a.s] alikuwa na mamlaka juu ya majini na ndege, pia alikuwa akifahamu semi za ndege na lugha za wadudu. Mwenyezi Mungu anasema:

وَوَرِثَ سُلَيْمَانُ دَاوُودَ وَقَالَ يَا أَيُّهَا النَّاسُ عُلِّمْنَا مَنطِقَ الطَّيْرِ وَأُوتِينَا مِن كُلِّ شَيْءٍ إِنَّ هَٰذَا لَهُوَ الْفَضْلُ الْمُبِينُ ﴿١٦﴾ وَحُشِرَ لِسُلَيْمَانَ جُنُودُهُ مِنَ الْجِنِّ وَالْإِنسِ وَالطَّيْرِ فَهُمْ يُوزَعُونَ ﴿١٧﴾ حَتَّىٰ إِذَا أَتَوْا عَلَىٰ وَادِ النَّمْلِ قَالَتْ نَمْلَةٌ يَا أَيُّهَا النَّمْلُ ادْخُلُوا مَسَاكِنَكُمْ لَا يَحْطِمَنَّكُمْ سُلَيْمَانُ وَجُنُودُهُ وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿١٨﴾ فَتَبَسَّمَ ضَاحِكًا مِّن قَوْلِهَا وَقَالَ رَبِّ أَوْزِعْنِي أَنْ أَشْكُرَ نِعْمَتَكَ الَّتِي أَنْعَمْتَ عَلَيَّ وَعَلَىٰ وَالِدَيَّ ...﴿١٩﴾

"Na Suleiman alimrithi Daudi na akasema, Enyi watu tumefundishwa (hata kutambua) semi za ndege na tumepewa kutokana na kila kitu, hakika huu ni ukarimu wa Mwenyezi Mungu uliyo wazi, na alikusanyiwa Suleiman majeshi yake miongoni mwa majini na watu na ndege nayo yakapangwa makundi makundi, hata walipofika katika bonde la wadudu "chungu" alisema mdudu chungu (kuwaambia wenziwe) ingieni majumbani mwenu asikupondeni Suleiman na majeshi yake hali ya kuwa hawana khabari, basi (Suleiman) akatabasamu akilichekelea neno lake (yule chungu) na akasema

Ee Mola wangu, nipe nguvu nikushukuru neema yako uliyonineemesha mimi na wazazi wangu...." Qur'an,27:16, 17, 18, 19 na kuendelea.

Ewe msomaji mtukufu lau utaisoma Qur'an juu ya kisa cha ndege "Hud-Hud" ambaye Nabii Suleiman [a.s] alimtuma kwa Malkia wa Sabai apeleke barua kutoka kwake kwenda kwa Malkia huyo, utakupata mshangao kutokana na nguvu hiyo ya siri aliyokuwa nayo Nabii Suleiman [a.s]. Kwa hiyo tunataraji utafanya mazingatio katika aya ya 20 mpaka ya arobaini na nne ndani ya Surat An-namli ili upate nguvu ya kuyakanusha na kuyabatilisha madhhebu ya Kiwahabi yanayopingana na Qur'an. Isitoshe zaidi ya hayo ni kwamba Nabii Suleiman [a.s] kwa mujibu wa ufafanuzi wa Qur'an alikuwa na mamlaka juu ya upepo ambao ulikuwa ukivuma apendavyo kwa amri yake. Mwenyezi Mungu anasema:

وَلِسُلَيْمَانَ الرِّيحَ عَاصِفَةً تَجْرِي بِأَمْرِهِ إِلَى الْأَرْضِ الَّتِي بَارَكْنَا فِيهَا ۚ وَكُنَّا بِكُلِّ شَيْءٍ عَالِمِينَ ﴿٨١﴾

"Na kwa Suleiman (tukaupa utii) upepo wa nguvu ukavuma kwa amri yake katika ardhi ambayo tumeibarikia nasi ndio tunaokijua kila kitu". Qur'an, 21:81.

Yeyote mwenye kuweka mazingatio kwenye aya hii "unavuma kwa amri yake", ambayo ni kauli ya Mwenyezi Mungu, (ataona) inajulisha uwezo wa siri wa Nabii Suleiman [a.s] juu ya upepo na kuuhukumu kwake katika njia zake na nyendo zake.

### 4). NABII ISA [a.s] NA UWEZO WA SIRI

Tunaweza kuufahamisha uwezo wa siri wa Nabii Isa [a.s] kwa kupitia mazingatio tunayoweza kuyapata katika aya za Qur'an zinazomzungumzia Nabii Isa [a.s] na uwezo huo. Miongoni mwa aya hizo ni kauli ya Mwenyezi Mungu akimnakili Nabii Isa [a.s]:

أَنِّي أَخْلُقُ لَكُم مِّنَ الطِّينِ كَهَيْئَةِ الطَّيْرِ فَأَنفُخُ فِيهِ فَيَكُونُ طَيْرًا بِإِذْنِ اللَّـهِ ۖ وَأُبْرِئُ الْأَكْمَهَ وَالْأَبْرَصَ وَأُحْيِي الْمَوْتَىٰ بِإِذْنِ اللَّـهِ ۖ وَأُنَبِّئُكُم بِمَا تَأْكُلُونَ وَمَا تَدَّخِرُونَ فِي بُيُوتِكُمْ ۚ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً لَّكُمْ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ ﴿٤٩﴾

"Bila shaka mimi nakuumbieni kutokana na udongo kama sura ya ndege, kisha nampulizia na mara anakuwa ndege kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na ninawaponyesha vipofu na wenye mbaranga, ninawafufua (baadhi ya) waliokufa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu na nitakwambieni mtakavyovila na mtakavyoweka akiba katika nyumba zenu, bila shaka katika haya imo hoja kwenu ikiwa ninyi ni watu wa kuamini". Qur'an, 3:49.

Katika aya hii neno "kwa idhini ya Mwenyezi Mungu" limerudiwa mara mbili ili kutia mkazo kwamba matumizi ya uwezo wa siri ambao Mawalii wa Mwenyezi Mungu huutumia, huwa yanatokana na uwezo wa Mwenyezi Mungu na kutaka kwake. Ndiyo maana unamuona Nabii Isa [a.s] katika aya hii anauzingatia uwezo wake wote kuwa umo ndani ya udhibiti wa idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Basi hali ni kama hii hii kwa Manabii wa Mwenyezi Mungu na Mawalii. Mwenyezi Munga anasema:

وَمَا كَانَ لِرَسُولٍ أَن يَأْتِيَ بِآيَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّـهِ ﴿٣٨﴾

"Na haiyumkiniki kwa Mtume kuleta muujiza isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu". Qur'an, 13:38.

Pamoja na hayo, utamuona Nabii Isa [a.s] anayanasibisha matendo yake yote ya uwezo huo wa siri kwenye nafsi yake tukufu anasema, "Naumba" "Napuliza" "Naponya" "Nafufua" 'Nakwambieni" yote ameyatamka kwa dhamiri ya msemaji mmoja. Kwa hiyo basi, Manabii Yusuf, Musa, Isa na Suleiman [a] siyo wao peke yao ambao walikuwa na uwezo wa siri, bali wako Manabii wengi ambao walikuwa na bado wanaminiliki uwezo huo, na kulitafiti jambo hili kwa upana kunahitaji kitabu makhsusi kuzungumzia jambo hili, nasi tumelizingumzia kwa upana katika kitabu kiitwacho "Al-qudratul-maanawiyya Lil-anbiyaa" na kimechapishwa mara nyingi.

5). UWEZO WA SIRI WA MALAIKA

Bila shaka Malaika nao pia wananufaika kuta uwezo wa siri. Hii hapa Qur'an inamsifu Malaika Jibril kwa kusema, "Mwenye nguvu sana". Qur'an, 53:5.

Na inawasifu baadhi ya Malaika inasema: "Wakazitengenezea mambo yake" Qur'an, 79:5. Na aya nyingine zaidi ya hizo mbili ambazo zimeeleza wazi wazi au zinaashiria kwamba, Malaika wanasimamia uendeshaji wa mambo ya ulimwengu ikiwa ni pamoja na kutoa roho na kuwalinda watu na kuandika matendo (ya watu) "waandishi watukufu" na kuangamiza nyumati zenye maovu na mengineyo miongoni mwa majukumu ya ulimwengu huu. Bila shaka kwa kiIa mwenye kuifahamu vyema Qur'an japo kidogo anafahamu kwamba Malaika wanao uwezo wa siri na kwamba wanautumia kimuujiza kwa idhini ya Mwenyezi Mungu na nguvu zake. Basi lau kuamini nguvu hizo za siri kungelazimiana kuamini uungu (wa mwenye nguvu hizo) basi Mitume wote na Malaika wangekuwa ni waungu kinyume cha Mwenyezi Mungu, jambo ambalo haliwezekani kabisa.

## BASI NINI UFUMBUZI WAKE NA NI IPI KAULI ILIYO SAWA

Hakika tumekwisha taja kuwa ufumbuzi na kauli ya sawa, ni kutenganisha baina ya uwezo wa kujitegemea na ule wa kupewa. Kuamini kuwa uwezo wa kujitegemea kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu Mtukufu, wakati ambapo kuamini uwezo wa kupewa (na Mwenyezi Mungu) katika nyanja yoyote ile, hiyo ndiyo Tauhidi yenyewe. Mpaka hapa ewe msomaji, imekubainikia kwamba, kuamini kuwepo uwezo wa siri kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu haiwezi kuwa ni shirki, bali hiyo ndiyo Tauhidi (kumpwekesha Mwenyezi Mungu) hasa, lakini kwa sharti kwamba mtu aitakidi uwezo huo umetegemezewa kwa Mwenyezi Mungu ambao ni uwezo wa milele, na katika hali kama hii imekubainikia vile vile kwamba, maana ya Tauhidi siyo kuviegemezea vitendo vya kimaumbile kwa mtu na vile vya siri kuviegemezea kwa Mwenyezi Mungu, bali Tauhidi halisi ni kuviegemeza vitendo vyote kwa Mwenyezi Mungu na inafahamika kuwa nguvu na uwezo vyote vinaanzia na kumalizikia kwake Mwenyezi Mungu. Na sasa ndiyo umefika ule wakati wa kuzungumzia ile nguzo ya pili katika mlango huu, nayo ni ile inayozungumzia kufaa kuwaomba Mawalii wa Mwenyezi Mungu mambo ya siri yasiyowezekana (katika maumbile yetu ya kawaida).

## KUWAOMBA MAWALII MATENDO YA GHAIBU

Je, inafaa kumuomba mmoja wa Mawalii wa Mwenyezi Mungu matendo ya muujiza? Na je, ombi kama hilo ni ushirikina? Kwa kuanza tunasema: "Kila tukio linayo sababu yake", kini ambacho hakuna khitilafu yoyote ulimwengu mzima, hivyo basi kila kitu hakiwezi kuwa ila ni kwa sababu, kwani maisha tunayoishi ni maisha ya sababu na visababishwaji, zaidi ya hapo ni kwamba hakipatikani chenye kupatikana ulimwenguni kote ila kutakuwa na sababu yake. Vile vile miujiza ya Manabii na karama za Mawalii haziwezi kutokea pasina sababu, isipokuwa sababu zake siyo za kimaumbile, bali zimefichikana na ziko nje ya maada na ziko juu ya kiwango (chetu) cha maarifa. Kwa mfano, ilipogeuka fimnbo ya Nabii Musa na kuwa nyoka, au Nabii Isa alipokuwa akifufua wafu naye Mtume **[s.a.w.w]** mwezi uliposuka kwa ajili yake na zilifanya Tasbihi tembe za mchanga mkononi mwake na miujiza mingineyo ya Manabii, yote hii haikutoka bila ya sababu yoyote, lakini sababu iliyosababisha kutokea kwake kama tulivyokwisha sema siyo sababu ya kimaumbile tunayoweza kuidiriki (kuiona) kwa macho yetu lakini siyo kwamba yote haya yamefanyika bila sababu, bali sababu yake iko nje ya maada.

Baada ya maelezo haya mafupi, sasa tuzungumzie maudhui inayohusika, nayo ni ile ya kuwaomba Mawalii wa Mwenyezi Mungu matendo ambayo ni ya kimiujiza yaliyo kinyume na maumbile ya kawaida. Bila shaka Mawahabi wapotofu na kwa upotevu wao wanapoteza (umma) wanadai kwamba, kuomba (kwa Mawalii) matendo ambayo yako kinyume na maumbile ni kumshirkisha Mwenyezi Mungu, lakini kuomba mambo ya kawaida katika maumbile (yetu) siyo ushirikina. Basi Je, nini maoni ya Uislamu juu ya madai haya? Jawabu: Qur'an hii tukufu ndiyo muongozo bora ambao tutapata kwayo uamuzi kwani utaiona Qur'an mahala pengi tu imeweka wazi jambo hili kwa kuwataka Manabii na wengineo wasimamie mambo yaliyo nje ya kanuni za kawaida ya maumbile. Kwa mfano: Watu wa Nabii Musa [a.s] walimuomba awape maji na mvua na awaokoe kutokana na ukame ambao ulikuwa ukiwasumbua, na hapo ikatoka amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuitikia maombi yao akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ إِذِ اسْتَسْقَاهُ قَوْمُهُ أَنِ اضْرِب بِّعَصَاكَ الْحَجَرَ ﴿١٦٠﴾

"Na tukampelekea wahyi Musa, pale watu wake walipomuomba maji (tukamwambia) lipige jiwe kwa fimbo yako." Qur 'an, 7:160.

Iwapo mtu atasema "Hapana kizuwizi kumuomba muujiza mtu aliye hai, basi utafiti ufanywe juu ya kumuomba maiti". Je, Inafaa? Jawabu litakuwa: Bila shaka uhai na kifo haviibadili hakika ya Tauhidi na shirki, kiasi kwamba kitu kiwe ni Tauhidi wakati wa uhai na kiwe ni shirki katika hali ya ufu, au kinyume cha hivi, bali hakika ya Tauhidi inabaki pale pale katika hali zote". Naam,..... inawezekana kukawa na athari Fulani kwa uhai na mauti katika (kupatikana) faida ya maombi au kukosekana, kitu ambacho hakiathiri ukweli wa Tauhidi na shirki.

## NABII SULEIMAN [a.s] ANAOMBA (KULETEWA) KITI CHA BIL-QIIS

Qur'an Tukufu inatusimulia kwamba Nabii Suleiman [a.s] aliwaomba waliokuwa wamehudhuria mbele yake kwamba, mmoja wao amletee kiti cha enzi cha Bil-qiis kwa kutumia uwezo wa ghaibu na kinyume cha maumbile. Nabii Suleiman [a.s] akawaambia kama ilivyo ndani ya Qur'an: "Nani kati yenu atakayeniletea kiti chake cha enzi kabla hawajaja kwangu hali ya kuwa wamekwisha silimu? Mjasiri mmoja miongoni mwa majini akasema, mimi nitakuletea kabla hujainuka mahali pako hapo, na bila shaka ninazo nguvu za (kutenda) hayo na nimuaminifu. Akasema yule aliyekuwa na elimu kutoka katika kitabu; "Mimi nitakuletea kabla ya kupepesa jicho lako," basi alipokiona kimewekwa mbele yake, (Nabii Suleiman) alisema "Haya yote ni kwa fadhila za Mola wangu". Qur'an, 27:38-40.

Ikiwa madh-hebu ya Mawahabi yatasihi kuharamisha kumuomba yeyote asiyekuwa Mwenyezi Mungu kutenda matendo yanayokwenda kinyume na kawaida ya maumbile, basi Nabii Suleiman [a.s] atakuwa alifanya kufru na ushirikina kuwaomba waliohudhuria mbele yake wamletee kiti cha enzi cha Bil-qiis!!! Vile vile kumuomba muujiza mtu aliyedai Utume katika zama zozote na mahala popote itakuwa ni tendo la ukafiri na ushirikina. Lakini tunajua kwamba watu walikuwa wakimuomba muujiza kila aliyedai Utume akiwa mkweli au muongo ili iwe ni dalili ya kuthibitisha ukweli wa madai yake na kama kweli anayo mawasiliano na ulimwengu wa juu. Yote haya hawakumuomba Mwenyezi Mungu ambaye ndiye aliyemtuma bali walikuwa wakisema:

"Kama umekuja na alama (muujiza) basi ilete iwapo wewe ni miongoni mwa wasemao kweli". Qur'an, 7:106.

Na hii ndiyo kawaida ya mataifa yote na nyumati zote ulimwenguni, kwani kila walipotaka kupambanua baina ya Nabii wa kweli na muongo mwenye kujipachika Unabii walikuwa wakimuomba muujiza utakaojulisha uwezo wake wa ghaibu, nao Manabii katika kutekeleza wajibu wao walikuwa wakiwaita watu waje kushuhudia miujiza yao inayojulisha ukweli wao. Bila shaka Qur'an Tukufu imesajili baadhi ya matukio ambayo yalipita baina yao Manabii na nyumati (zao) kuhusu maudhui hii, bila ya kuwakosoa waombaji wa mijuza kwa Manabii, jambo ambalo linajulisha kwamba Qur'an inakubaliana na maombi haya. Hebu natutaje mfano mmoja kwamba: Lau umati fulani unaotafuta ilipo haki utamwijia Nabii Isa [a.s] na kumwambia, "Kama wewe ni mkweli kwa madai yako ya Unabii basi hebu mponye kipofu huyu na umrudishie macho yake na mponye huyu mwenye mbaranga, umati huu hauwezi kuzingatiwa kuwa umefanya shirki bali utahesabiwa kuwa ni miongoni mwa nyumati bora ambao unatafuta ukweli na kwa ajili hiyo utasifiwa.

Na sasa tena, lau tutakadiria kifo cha Nabii Isa [a.s] na kisha umati wake ukaiomba roho yake tukufu, imponye kipofu na mwenye mbaranga, basi ni kwa nini umati huu uonekane kuwa umefanya shirki pamoja na kufahamu kwamba mauti na uhai wa Nabii huyu havina athari yoyote katika Tauhidi na shirki? (Ili kuifahamu miujiza ya Nabii Isa [a.s] rejea aya ya 49 Sura ya 3 na aya ya 100 na 101 Sura ya 5.

### KHULASA YA MAELEZO

Kwa kufupisha maelezo, Qur'an Tukufu inabainisha majina ya baadhi ya Mawalii aliowachagua Mwenyezi Mungu na akawapa uwezo huo wa siri ili

watekeleze matendo ambayo yamefichikana yaliyo kinyume na maumbile ya kawaida, nao Mawalii hawa walikuwa wakitumia uwezo huu katika nyakati zinazofaa kama ambavyo kulikuwa na watu ambao walikuwa wakienda kwa Mawalii hao na kuwaomba kuwasaidia kwa uwezo huu. Kwa hiyo basi ewe msomaji imekudhihirikia kwamba, aya nyingi za Qur'an ziko wazi kabisa katika kuyapinga madhehebu ya Kiwahabi na zinavunja rai yao hiyo ya pekee. Lau Mawahabi watasema, "Kuomba muujiza Mawalii ni shirki." Sisi tutasema, "Kwa nini basi Nabii Suleiman [a.s] na wengineo aliomba matendo yaliyo kinyume cha maumbile kwa wengine"? Na iwapo watasema: "Bila shaka kuwaomba haja fulani Mawalii wa Mwenyezi Mungu kwa njia ya muujiza kunalazimu kuitakidi uwezo wao wa ghaibu". Sisi tutasema, "Kuamini uwezo wa ghaibu kuna namna mbili, ya kwanza itakuwa ndiyo Tauhidi yenyewe, na ile ya pili itakuwa inalazimu kupatikana shirki". Na iwapo watasema: "Hakika kuomba karama kutoka kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu katika zama za uhai inafaa, lakini kuziomba hizo karama kwa Walii aliyekwisha fariki haifai".

Sisi tutasema, "Hakika mauti na uhai vyote viwili siyo msingi wa Tauhidi na shirki wala hivi haviwezi kubatilisha ukweli wa kimojawapo." Na iwapo wao watasema, "Hakika kuomba uponyo kwa mgonjwa na kuondosha deni kwa njia isiyo ya kawaida ni kuomba kwa asiye Mwenyezi Mungu afanye tendo la Mwenyezi Mungu". Sisi tunasema, "bilashaka sharti ya kupatikana shirki ni kuitakidi uungu kwa yule unayemuomba au kuamini kuwa yeye ndiyo mfanyaji wa matendo ya Mwenyezi Mungu, kwa kujitegemea na kwamba kuomba matendo yasiyo ya kawaida kimaumbile maana yake siyo kuomba matendo ya Mwenyezi Mungu kutoka kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, kwani kipimo cha matendo ya Mwenyezi Mungu hakipimwi kwa kuwa matendo hayo yako nje ya kanuni za kimaumbile ili ombi hili liwe ni ombi Ia kuomba kitendo kinachostahiki kutendwa na Mwenyezi Mungu ambacho ameombwa mja akitende. Sivyo kabisa, bali kipimo cha matendo ya Mwenyezi Mungu ni kuwa mtendaji ni mwenye kujitegemea kule kufanya matendo hayo na kuyatekeleza. Ama ikiwa mtendaji anafanya kitendo fulani kwa kutegemea uwezo wa Mwenyezi Mungu basi kumuomba yeye hakuwi na maana ya kumuomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu kutenda tendo la Mwenyezi Mungu. Na wala hapana tofauti katika uombaji ikiwa tendo hilo ni miongoni mwa matendo ya kawaida au ni yale yaliyo kinyume na kawaida. Majibu kama haya pia yatakuwa sawa sawa kuhusu kuomba uponyo kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu kwani kuna baadhi ya watu ambao wanapinga jambo hili kwa kutolea ushahidi aya ya Qur'an isemayo: "Na ninapoumwa yeye ndiye aniponyaye". Qur'an aya ya 80 Surat As-shuaraa.

Wanasema; "Basi vipi itafaa kusema ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu niponye"? Na mengineyo katika matendo yaliyo kinyume na ada kawaida)? Jawabu lake: Bila shaka wale wanaoitakidi itikadi hii kwa bahati mbaya hawakutenganisha baina ya matendo ya kiungu na yale ya kiutu, na ndiyo maana wanaona kwamba kila kitendo ambacho kina kwenda kinyume na njia za kawaida kiutendaji, basi hicho ni miongoni mwa matendo ya Mwenyezi Mungu na kitendo kinachopita katika utendaji wakawaida, basi hicho ni miongoni mwa matendo ya watu. Bila shaka watu hawa

hawakufahamu au wanajifanya kutokufahamu kipimo kinachotenganisha kati ya matendo ya Mwenyezi Mungu na yale yasiyo yake. Kama ingekuwa kila kitendo kilicho kinyume cha maumbile kinazingatiwa kuwa ni miongoni mwa matendo ya Mwenyezi Mungu, basi matendo yanayofanywa na watawa wa huko India yangekuwa ni matendo ya kiuungu na wote hao wanaoyatenda wangekuwa ni "Miungu". Tumekwisha taja zaidi ya mara moja kwamba, kipimo katika matendo ya Mwenyezi Mungu nikule "kujitegemea katika utendaji" na kutokutegemea aina ya uwezo mwingine wowote ule, wakati ambapo matendo yatendwayo na watu ni kinyume cha hivyo. Kwa hakika mtu (siku zote) anamtegemea Mwenyezi Mungu na hutaka msaada kwa uwezo wake katika kila jambo sawa sawa likiwa ni Ia kimaumbile (yetu) au lililovuka mipaka ya kimaumbile, na watu wengi hupata uwezo (huo) na kuutumia kufikia malengo yao wayatakayo. Basi je, kuomba jambo fulani kwa watu hawa ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu?

Kwa hakika kuenda kinyume cha Tauhidi kumo udani ya itikadi iliyoambatanishwa na ombi (la mtu), basi iwapo muombaji aombapo kitu kwa mmojawapo wa Mawalii wa Mwenyezi Mungu hali ya kuwa anaamini kwamba Walii huyo ni mwenye kujitegemea (katika matendo yake) basi atakuwa kamfanya Walii huyo kuwa ni mtu anayejitosheleza kwa dhati yake, na maana ya kujitosheleza ni kwamba atakuwa amemzingatia Walii huyo kuwa ni mtu asiyemuhitajia Mwenyezi Mungu kwa lolote, na hii ndiyo shirki kwa kuwa hakuna anayejitosheleza kwa dhati yake isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake. Na hapo kale wengi wa washirikina katika zama za jahiliya na mwanzo wa kuja Uislamu walikuwa wakiitakidi itikadi hii kuhusu Malaika na nyota, na kwamba Mwenyezi Mungu ameviumba viumbe hivi na akaviegemezea uwezo wa kuendesha ulimwengu na kuuangalia kwa muegemezo wa viumbe hivyo kujitegemea kikamilifu na au kwa uchache, washirkina waliamini kuwa viumbe hivyo vinamiliki shafaa (uombezi) na kuutumia uwezo huo wa shafaa wapendavyo.

## SHIRKI NA JINSI WASEMAVYO MUUTAZILA

Ama kundi Ia Muutazila wao wanamuona mtu katika hali ya kuwepo kwake kuwa yeye ni kiumbe wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, lakini Muutazila hao hao kwa wakati huo huo wanamuona mtu kuwa ni mwenye kujitegemea katika kutoa athari kwenye vitu na kutekeleza matendo. Lau hawa Muutazila wangefanya mazingatio kidogo katika kauli yao hii wangeona kuwa kuna aina fulani yashirki iliyofichikana, lakini wao wameghafilika nayo. Bila shaka shirki hii iliyojificha haifikii ule ushirikina wa washirikina (hao) na tofauti iliyopo katika shirki mbili hizi ni kwamba washirikina wanadai kuwa masanamu yao yanajitegemea kiuwezo katika kuendesha mambo ya ulimwengu na matendo yanayomstahikia Mwenyezi Mungu Mtukufu. Nao Muutazila wandai kuwa mtu anao uwezo wa kujitegemea katika matendo yake. Al-mustalahat Al-arbaa, uk. 18.

17

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## KUMUAPA MWENYEZI MUNGU KWA HAKI YA MAWALII

Miongoni mwa nukta wanazotofautiana Waislamu na Mawahabi ni kwamba, Mawahabi wanadai kuwa, ni haramu kumuapa Mwenyezi Mungu kwa haki ya Mawalii, na pia kuapia kisichokuwa Mwenyezi Mungu. Wakati mwingine Mawahabi wanaona kuwa viapo hivi viwili ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu katika Ibada. Katika maelezo yafuatayo tutaisherehesha kwa urefu maudhui hii ili kupata hukmu sahihi ya kisheria.

### KUMUAPA MWENYEZI MUNGU KWA HAKI YA MAWALII

Bila shaka Qur'an inawasifu baadhi ya waja wa Mwenyezi Munga inaposema:

الصَّابِرِينَ وَالصَّادِقِينَ وَالْقَانِتِينَ وَالْمُنفِقِينَ وَالْمُسْتَغْفِرِينَ بِالْأَسْحَارِ ﴿١٧﴾

"Wafanyao subira na wasemao kweli na watifu na watoao sadaka na wale wanaoomba msamaha saa zilizo kabla ya alfajiri". Qur'an, 3:17.

Basi lau mtu atasimama katikati ya usiku akasali kwa ajili ya Mola wake rakaa nyingi, kisha akanyenyekea kwa Mwenyezi Mungu huko akisema: "Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nakuomba kwa haki ya wanaokutaka msamaha wakati wa karibu ya al-fajiri, unisamehe dhambi zangu". Itakuwaje basi kauli yake hii tuione kuwa ni shirki katika Ibada? Bila shaka shirki katika Ibada maana yake ni "Kumuabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu, au ni kumzingatia asiyekuwa Mwenyezi Mungu kuwa ni Mungu na ndiyo chanzo cha matendo ya Kiungu". Ama mahala hapa (tunapopazungumzia) yule mtu anayeswali anamuelekea Mwenyezi Mungu na haombi chochote (kwa mwingine) isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu. Basi iwapo tendo hili ni haramu, hapana budi kuwe kuna sababu nyingine isiyokuwa shirki.

Sisi hapa (nia yetu) tunataka kuwaelekeza Mawahabi wafahamu kwamba, Qur'an Tukufu imetaja kipimo na kanuni ili kufafanua na kupambanua baina ya mshirkina katika Ibada na yule mwenye Tauhidi, na kwa kipimo hiki imeweka kizuwizi mbele ya kila tafsiri itayofasiriwa kwa maoni (binafsi) juu ya maana ya "mshirikina." Kipimo hiki ni kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

وَإِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَحْدَهُ اشْمَأَزَّتْ قُلُوبُ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ وَإِذَا ذُكِرَ الَّذِينَ مِن دُونِهِ إِذَا هُمْ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿٤٥﴾

"Na anapotajwa Mwenyezi Mungu peke yake, nyoyo za wale wasioamini Akhera huchukia, na wanapotajwa wale wasiokuwa Mwenyezi Mungu basi wao hufurahi". Qur'an, 39:45.

Na katika aya nyingine Qur'an inawataja waovu ambao ni wale wafanyao shirki inasema:

إِنَّهُمْ كَانُوا إِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا إِلَٰهَ إِلَّا اللَّهُ يَسْتَكْبِرُونَ ﴿٣٥﴾ وَيَقُولُونَ أَئِنَّا لَتَارِكُو آلِهَتِنَا لِشَاعِرٍ مَّجْنُونٍ ﴿٣٦﴾ بَلْ جَاءَ بِالْحَقِّ وَصَدَّقَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٣٧﴾

"Bila shaka wao walipokuwa wakiambiwa "Hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, walikuwa wakipinga na husema je, sisi tuiache Miungu yetu kwa ajili ya huyu mtunga mashairi mwendawazimu." Qur'an, 37:35-36.

Kwa hiyo basi kwa mujibu wa aya mbili hizi mushrik (mwenye kumshirikisha Mwenyezi Mungu) ni yule ambaye huchukia moyo wake atajwapo Mwenyezi Mungu peke yake, na hufurahi watajwapo Miungu batili, au hupinga upweke wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Baada ya kipimo hiki cha Qur'an tunajiuliza, "Hivi yule mtu asimamaye katikati ya usiku na akamaliza saa nyingi akifanya Ibada na kuomba na akaswali mbele ya Mwenyezi Mungu kwa ikhlasi na unyenyekevu na akamuapa Mwenyezi Mungu kwa haki ya Mawalii wake wema na akamuomba Mwenyezi Mungu kupitia kwa waja wake wema..... hivi kweli mtu huyu atakuwa mushrik kwa amali yake hii?! Basi ni kwa namna gani amepinga utajo wa Mwenyezi Mungu na ni vipi amekataa kukiri upweke wa Mwenyezi Mungu Mtukufu (hata aitwe ni mushrik)?!!! Ni kwa nini basi waandishi wa Kiwahabi wanategemea misingi ya kabuni na dalili dhaifu kuliko hata nyumba ya buibui, kisha wanawatuhumu Waislamu kuwa wanafanya shirki halafu wao wakajiona kuwa peke yao ndiyo taifa teule la Mwenyezi Mungu?! Vipi itafaa wawazingatie asilima 99% ya Waislamu kawa ni washirikina na wao wawaone Mawahabi toka Najdi kuwa ndiyo peke yao ni watu wa Tauhidi pamoja na kuyazingatia (maelezo) ya kipimo cha Qur'an? Na je, Mwenyezi Mungu amewapa uwakala Mawahabi wa kuifasiri maana ya shirki kama wapendavyo na waamue kwamba kundi hili ni washirikina wa kundi hili ni la watu wa Tauhidi? Ukweli ulivyo ni kwamba, "Mwenyezi Mungu ameweka kifuniko kwenye nyoyo zao basi wao hawafahamu (kitu)".

## AMIRUL-MU'MINIINA (ALI [a.s] NA KUMUAPA MWENYEZI MUNGU KWA HAKI YA MAWALII

Tunaangalia kumuapa Mwenyezi Mungu kama ilivyo katika dua za Mawalii wake watukufu. Kwa mfano: Amirul-Mu'miniina Imam Ali [a.s] anasema katika maombi yake baada ya Sala ya usiku: "Ewe Mwenyezi Mungu mimi ninakuomba kwa heshima ya yule aliyejilinda kwako kutokana na adhabu yako na akazitumainia nguvu zako na akajikinga kwa kivuli chako na akashikamana na kamba yako na hakutegemea ila kwako".[1] Na anasema tena Imam Ali [a.s] katika dua aliyomfundisha Sahaba wake mmoja. "Na kwa haki ya wanaokuomba na wale wanaonyenyekea kwako na wanajilinda kwako na wanaodhalilika mbele yako na kwa haki ya kila mja mwenye kukuabudia katika kila sehemu ya nchi kavu au baharini au mbugani au mlimani, nakuomba maombi ya mtu mwenye shida mno...[2] Hivi kuna kitu gani kingine kisichokuwa kumpwekesha Mwenyezi Mungu ndani ya maombi haya yanayoihimiza roho na kuipeleka kwenye Ibada na kudhalilika mbele ya Mwenyezi Mungu.... Je, kuna matokeo mengine yasiyokuwa ya kuimarisha kumpwekesha Mwenyezi Mungu na (kuonyesha kuwa) hakuna mlinzi ila yeye, na kudhihirisha upendo kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu na wapenzi wake, jambo ambalo linaonyesha kuwa ni

1. As-sahifatul-alawiyya, uk. 370.
2. Al-sahifatul-alawiyya, uk. 51.

kumuelekea Mwenyezi Mungu katika wakati ule ule?" Na kwa mantiki hii basi, tuhuma ya ukafiri na shirki inayotangazwa na Mawahabi (juu ya jambo hili) kuliko kitu kingine chochote ni lazima ikome.

Na inafaa kuyasoma maudhui haya kwa njia ya mantiki na dalili. Kwa ajili hii ndiyo maana utawaona baadhi ya Mawahabi waadilifu japo kidogo wametatua suala la "kumuapa Mwenyezi Mungu kwa haki ya Mawalii", na wanasema kwamba jambo hili ni haramu au makruhu, kinyume cha huyu 'As-san-ani" Wahabi aliyekosa uadilifu ambaye ameyasoza mas-ala haya kwenye shirki. Na sasa basi baada ya kubainika msingi wa mazungumzo ni lazima kusoma maudhui ndani ya eneo la uharamu na karaha na kisha kubainisha dalili iliyo wazi juu ya kusihi kwa jambo hili na kufaa kwake. Kwa hiyo tunasema:

## KUTHIBITI KWA KIAPO HIKI NDANI YA UISLAMU

Qadhiya ya kumuapa Mwenyezi Mungu kwa haki ya Mawalii imekuja katika hadithi nyingi mutawatiri baadhi yake zimepokewa kwa Mtume **[s.a.w.w]** na nyingine zimepokewa toka kwa Maimamu wa nyumba ya Mtume **[s.a.w.w]**. Na kwa mujibu wa hadithi hizi haiwezekani kabisa kusema kwamba ni haramu au karaha kumuapa Mwenyezi Mungu kwa haki ya Mawalii. Hebu tazama mifano ya hadithi hizo:

1. Hapo kabla imetangulia ishara kwamba, Mtume **[s.a.w.w]** alimfundisha kipofu aliyekuja kwa Mtume akimuomba Mtume **[s.a.w.w]** amuombee Mwenyezi Mungu ili macho yake yarudi. Mtume alimfundisha kipofu yule aseme! "Ewe Mwenyezi Mungu nakuomba na ninaelekea kwako kwa haki ya Mtume wako Muhammad Mtume wa Rehma".[1]

2. Abu Said Al-khudri amepokea toka kwa Mtume **[s.a.w.w]** dua hii ifuatayo: "**Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba kwa haki yawanaokuomba na ninakuomba kwa haki ya mwendo wangu huu**".[2]

3. Naye Nabii Adam [a.s] alitubia kwa Mwenyezi Mungu akasema:

"Nakuomba kuta haki ya Muhammad unisamehe".[3]

4. Baada ya Mtume **[s.a.w.w]** kwisha kumzika Bibi Fatma binti Asad ambaye ni mama wa Imam Ali [a.s], Mtume alimuombea dua mama huyu akasema: "Msamehe mama yangu Fatma binti Asad na uyakunjue makazi yake kwa haki ya Mtume wako na Manabii waliopita kabla yangu.[4] Dua hizi japokuwa hazina lile tamko lenyewe la kiapo, lakini madhumuni yake ni kiapo kwa kuwepo herufi ya "BAA" ambayo ni ya kiapo katika hadithi zote, kwani muombaji asemapo **ALLAHUMMA INNII AS-ALUKA BIHAQQIS-SAILIINA ALAIKA**" maana yake ni, ninakuapa kwa haki yao.

5. Bwana wa mashahidi Imam Hussein bin Ali [a.s] anasema alipokuwa akiomba: "Ewe Mwenyezi Mungu nakuomba kwa haki ya maneno yako, na kwa mafungamano ya enzi yako, na kwa haki ya wakaazi wa mbingu zako

---

1. (1) Sunan lbn Majah Juz. 1, uk. 261. (2) Musnad Ahmad Juz. 3, hadithi ya 21.
2. (1) Sunan Ibn Majah,Juz.1, uk 441 (2) Mustad'rak sahihain, Juz. 1, Uk 313. (3)Musnad Ahmad Juz. 4, uk. 138 n.k.
3.(1) Sunan Ibn Majah, Juz. 1, uk 441. (2) Mustadrak sahihain, Juz. 1, uk. 313 (3)Musnad Ahmad, Juz. 4, uk. 138 n.k.
4. Al-fusulul-muhimmah, uk. 31 cha Ibn Sab-baagh al-Maliki aliyefariki mwaka 855 A.H.

na ardhi yako na Manabii wako na Mitume wako, unikubalie (maombi yangu) kwani nimefikwa na jambo zito, basi nakuomba umpe rehma Muhammad na kizazi cha Muhammad na uyawepesishe mambo yangu". Na utakapoiangalia Sahifatu as-Sajadiyah iliyopokelewa toka kwa Imam wa nne katika Maimamu wa nyumba ya Mtume aitwaye Imam Zainul-abidina [a.s] humo utaona viapo vingi sana, na hii ndiyo dalili iliyo bora mno inayoonyesha kusihi kwa aina hii ya kutawassal..... Hebu angalia mifano ifuatayo:

6. Imam Zainul-abidina [a.s] anasema ndani ya dua yake siku ya Arafa "(Ewe Mola) kwa haki ya yule uliyemchagua miongoni mwa viumbe wako, na kwa haki ya yule uliyemteua kwa ajili yako, na kwa haki yake uliyemchagua kutoka miongoni mwa viumbe wako, na uliyemteua kwa ajili ya shani yako, na kwa haki ya yule ambaye umeunganisha kumtii yeye ndiyo kukutii wewe na ni yule ambaye umeunganisha kufanyiwa yeye uadui ni kufanyiwa wewe uadui.[1].

7. Na wakati Imam Jaafar as-Saadiq alipozuru kaburi Ia Imam Ali [a.s] ambaye ni babu yake, mwishoni mwa ziyara yake aliomba akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu nikubalie maombi yangu na upokee sifa ninazokutukuza, na unikutanishe na Mawalii wangu, kwa haki ya Muhammad na Ali na Fatma na Hasan na Husein."[2] Ewe msomaji Mtukufu, aina ya dua kama hizi zilizoshikamana na kumuapa Mwenyezi Mungu kwa haki ya Mawalii wake zimekuja kwa wingi mno kutoka kwa Maimamu wa nyumba ya Mtume **[s.a.w.w]**, wenye ismah, na wala nafasi haitoshi kutaja zaidi ya tulizotangulia kuzitaja. Na dua zote hizi zinajulisha juu ya ruhusa ya kumuapa Mwenyezi Mungu kwa haki ya Mawalii wake wema

## DALILI ZA MAWAHABI JUU YA KUHARAMISHA

Mawahabi wametaja baadhi ya dalili za kuharamisha kumuapa Mwenyezi Mungu kwa haki ya Mawalii wake. Dalili hizo ni dhaifu hazifai kutolea hoja wala kutiliwa maanani. Na sasa tunazitaja sambamba na kuzijibu katika maelezo yafuatayo: Dalili ya Kwanza: Mawahabi wanasema: "Wanachuoni wa Kiislamu wameafikiana kwamba, kumuapa Mwenyezi Mungu kwa haki za viumbe wake ni haramu."[3] Jawabu Lake: Maana ya Ijmau ni kuafikiana wanachuoni wa Kiislamu katika zama moja au zama zote juu ya hukumu fulani miongoni mwa hukmu za kisheria. Hii ndiyo Ij-mai, nayo ni hoja ya kisheria kwa Masunni kwa sababu kuafikiana kwa wanachuoni juu ya hukumu fulani ni hoja kwao na ni hoja ya kisheria kwa Mashia kwa kuwa inadhihirisha kuwafikiana na maoni ya Imam aliye Maasum ambaye huwa anaishi miongoni mwa watu, ima akawa haonekani machoni pao au akawa yu waonekana. Sasa hivi hebu tuone je, Ij-mai ya wanachuoni ilithibiti kuharamisha mas-ala haya au hapana? Sisi kwa sasa tunayaacha kwanza maoni ya wanachuoni wa Kishia na yale ya wanachuoni wa Kisunni kuhusu mas-ala haya, na tunatosheka na kutaja fat-wa za Maimamu wa madhehebu manne kisha tunajiuliza; je maimamu wa madh-hebu manne wanayofat-wa inayoharamisha jambo hili?.

1. Al-Sahifatus Sajadiyah, dua ya 47.
2. Ziyaratu Aminil-lahi Al-maarufah.
3. Kashful-ir-tiyabi, uk. 32, imenakiliwa toka 'Al-hadiyyatus-saniyyah".

Iwapo walitoa fat-wa kuharamisha, basi tunachokitaraji ni watutajie Nassi ya fat-wa hiyo pamoja na kitabu ambacho fat-wa hiyo imo pia nambari ya ukurasa ilipo. Bila shaka vitabu vya Fiqhi na hadithi vya wanachuoni wa Kisunni havikulizungumzia kabisa jambo hili ili tuweze kuufahamu mtazamo wao katika qadhiya hii. Kwa hiyo basi iko wapi hiyo Ij-mai na maafikiano anayoyadai mtunzi wa kitabu kiitwacho "Al-hadiyatus-saniyyah"?!! Hapana shaka kwamba mtu pekee ambaye mtunzi huyu alinakili kutoka kwake uharamu wa jambo hili ni mtu "Maj-hul" asiyefahamika hali yake, asiye na utajo wowote anayeitwa "Al-izzu bin Abdis-salaam", basi je vitabu vyote vya wanachuoni wa Kiislamu vimo ndani ya maandiko yaliyomo katika kitabu kiitwacho Al-hadiyatus-saniyyah? Na je, wanachuoni wote wa Kiislamu wamo ndani ya huyu Al-izzu bin Abdus-salaam? Ukweli ulivyo ni kwamba yeye mwenyewe mtunzi wa kitabu hiki "Al-hadiyyatus-saniyyah" amesema ndani ya kitabu hiki kwamba, Abu Hanifa na mwanafunzi wake aliyekuwa akiitwa Abu Yusuf wametoa fat-wa kwamba ni karaha kuapa kwa haki ya viumbe lakini hawakuharamisha.

Baada ya hapo, je ina nafasi gani fat-wa ya mtu fulani mbele ya hadithi sahihi zilizopokelewa toka kwa Mtume **[s.a.w.w]** na Maimamu watukufu toka katika kizazi cha Mtume **[s.a.w.w]** ambao wanachuoni wa Kisunni wamekubaliana kuwa (Maimamu hao ndiyo kile kizito kidogo baada ya Qur'an na maneno yao ni hoja ya kisheria). Hadithi ya vizito viwili ni Mutawatiri toka kwa mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** na wameitaja wana sihahi na sunan na wanahadithi na wanahistoria, na hawezi kuipinga isipokuwa mjinga na hadithi yenyewe ni hii: Amesema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]**: "Hakika ninakuachieni vizito viwili, Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Kizazi changu watu wa nyumba yangu, ambavyo nikishikamana navyo hamtapotea baada yangu milele; na kwamba viwili hivyo havitaachana mpaka vinifikie kwenye haudh, basi angalieni ni vipi mtanifuata katika viwili hivyo." Zaidi ya hapo maelezo aliyoyataja mtunzi huyo toka kwa Abu Hanifa hayakuthibiti. Kwa kifupi tunasema, "Hakuna dalili yoyote ile ya Ij-mai juu ya mas-ala haya moja kwa moja."

Dalili Ya Pili: Baada ya kuibatilisha dalili ya kwanza ya Mawahabi na kubainisha kutokusihi kwa dalili hiyo, sasa tunataja dalili yao ya pili nayo ni kauli ya mmoja wao anasema: "Kwa hakika kuomba kwa haki ya viumbe haifai, kwani viumbe hawana haki juu ya Muumba."[1] Jawabu Lake: Bila shaka kutoa ushahidi kama huu ni ijtihadi dhidi "Nassi" iliyo wazi, basi lau viumbe wasingekuwa na haki yoyote katika dhimma ya Muumba mtukufu, ni kwa nini basi Nabii Adam [a.s] na Mtume Muhammad **[s.a.w.w]** walimuapa Mwenyezi Mungu kwa haki hizi (za viumbe) na walimuomba Mwenyezi Mungu kwa sababu ya haki hizi kama ilivyokuja katika hadithi zilizotangulia?!! Zaidi ya hapo, wanasemaje watu hawa (Mawahabi) juu ya aya za Qur'an ambazo zinathibitisha haki za waja wema wa Mwenyezi

1. Kashful-ir-tiyabi akinakili kwa al-Qaduuri.

Mungu juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu."[1] Pia watasemaje jun ya hadithi tukufu zinazothibitisha haki hizo? Soma aya zifuatazo:

1. "Na ni haki juu yetu kuwanusuru wenye kuamini" Qur'an, 30:47.

2. "Hii ndiyo ahadi na haki juu ya Mwenyezi Mungu ndani ya Taurati na Injili". Qur'an, 9:111.

3. "Namna hii, ni haki juu yetu kuwaokoa walioamini". Qur'an, 10:103.

4. "Kukubali toba ni juu ya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya wale wanaofanya uovu kwa ujinga". Qur'an, 4:17. Kwa kuongezea juu ya aya zilizotangulia kuna hadithi nyingi zinazohusu jambo hili, na hebu ona mifano ifuatayo:

1) "Ni haki juu ya Mwenyezi Mungu kumsaidia aliyeowa kwa kutaka kujizuwiya na mambo aliyoyaharamisha Mwenyezi Mungu".[2]

2) Mtume **[s.a.w.w]** amesema: "**Watu wa aina tatu ni haki juu ya Mwenyezi Mungu kuwasaidia, mpiganaji katika njia ya Mwenyezi Mungu, na Mtumwa mwenye kutaka kujikomboa, na mwenye kuoawa kwa kutaka kujizuwiya kutenda maovu**".[3]

3) "Je, unafahamu ni ipi haki ya waja waliyonayo juu ya Mwenyezi Mungu"?[4]Naam,.... inaeleweka wazi kwamba hakuna yeyote ambaye kwa dhati yake anayo haki juu ya Mwenyezi Mungu, hata kama atamuabudu Mwenyezi Mungu kwa muda wa karne nyingi hali ya kumkhofu na kumnyenyekea Mwenyezi Mungu, kwani kila alichonacho mja, kimetoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, hakuna alichokitoa mja yeye mwenyewe kwa nafsi yake katika njia ya Mwenyezi Mungu eti ili astahiki kwa dhati yake kupewa thawabu. Basi tunauliza, nini maana ya "haki". Jawabu: Hakika makusudio ya haki katika Ibara hizi, ni malipo, na daraja ambavyo Mwenyezi Mungu huwapa waja wake wanapomtii na kumfuata yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu, na haya yote ni ziyada na ubora na umuhimu autoao Mwenyezi Mungu (kwa waja wake), na hii inaonyesha upole (huruma) na utukufu wake. Basi haki hii ambayo kwayo tunamuapa Mwenyezi Mungu ni haki aliyoiweka yeye Mwenyezi Mungu juu yake siyo kwamba mja anayo haki juu ya Mwenyezi Mungu, na maana hii imeelekezwa katika baadhi ya hadithi tukufu za Mtume **[s.a.w.w]**. Na hii ni kama karadha anayowakopa Mwenyezi Mungu waja wake aliposema, "Nani atakayemkopesha Mwenyezi Mungu kopesho zuri." Qur'an, 2:245.

Kwa hakika utendaji huu wa Mola na kutoa haki kwa waja wake unatokana na huruma yake Mwenyezi Mungu na uangalizi wake mkubwa kwa waja wake wema kiasi cha kujiona dhati yake tukufu kuwa ni yenye kudaiwa na waja wake na anawaona waja wake kuwa ndiyo wenye haki juu yake. Na ndani ya hali hii (iliyopo baina ya Mwenyezi Mungu na waja wake) inahamasisha na kutia nguvu ya kumtii Mwenyezi Mungu jambo ambalo liko wazi.

---

1. Mawahabi wanatumia rai zao na maoni yao kupinga aya za Qur'an na hadithi za Mtume [s.a.w.w].
2. Al-Jamius-saghiru cha Suyutiyy, Juz. 2, uk. 33.
3. Sunan ibn Majah, Juz. 2, uk. 84.
4. An-nihayah cha Ibn Athir katika Maddah (Haq).

## KUMUAPIA ASIYEKUWA MWENYEZI MUNGU MTUKUFU

Kuapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu ni miongoni mwa mambo ambayo Mawahabi wana uchungu nayo sana na ni katika mas-ala ambayo wao wanayakemea na kuyapigia kelele kwa kutumia kalamu zao potofu. Mwandishi wa Kiwahabi aitwaye As-San-Ani, yeye kwa mawazo yake anaona kuwa kumuapia asiyekuwa Mwenyezi Mungu ni shirki!![1] Vile vile mtunzi wa Kitabu kiitwacho 'Al-Hadiyyatus-Saniyya, yeye kwa mawazo yake anaona kuwa (kumuapia asiyekuwa Mwenyezi Mungu) ni shirki ndogo.[2]

## DALILI ZINAZORUHUSU KUMUAPIA ASIYEKUWA MWENYEZI MUNGU

Dalili Ya Kwanza: Bila shaka Qur'an ndicho kile kizito kikubwa na ndicho kiongozi cha juu na ndiyo kiigizo hai kwa kila Muislamu. Ndani yake utaona viapo vingi katika mahali pengi vya kumuapia asiyekuwa Mwenyezi Mungu kiasi kwamba kuvitaja kwa uchambuzi kutapelekea kurefusha uchambuzi wa maudhui hii. Kwa mfano: Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Surat As-Shamsi peke yake ameapa kwa vitu vinane vikiwa ni miongoni mwa viumbe vyake. Vitu hivyo ni: Jua, Mwanga wa Jua, Mwezi, Mchana, Usiku, Mbingu, Ardhi na nafsi ya mtu. Qur'an, 91:1-7. Kama ambavyo Mwenyezi Mungu katika Surat "An-Naziat" ameapia vitu vitatu, na akaapa kwa vitu viwili katika Surat "Al-Mursalat" na pia vimekuja viapo kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu katika Surat "At-Tariq", "Al-Qalam" "Al-Asr", na "Al-Balad". Qur'an, 79:1-3 na 77:1-3. Hebu angalia mifano ya aya za kiapo cha kumuapia asiyekuwa Mwenyezi Mungu ndani ya Sura zingine (zaidi ya tulizozitaja hapo juu). "Naapa kwa (Miti Ya) Tini na Zaituni, na kwa Mlima Sinai, na kwa Mji huu wenye Amani". Qur'an, 95.1-3.

"Naapa kwa usiku ufunikapo, na kwa mchana uangazapo". Qur'an, 96:1-2. "Naapa kwa Al-Fajri, na kwa masiku kumi, na kwa Shafaa na Witri na kwa usiku unapopita". Qur'an, 89:1-4.

وَالطُّورِ ﴿١﴾ وَكِتَابٍ مَّسْطُورٍ ﴿٢﴾ فِي رَقٍّ مَّنشُورٍ ﴿٣﴾ وَالْبَيْتِ الْمَعْمُورِ ﴿٤﴾ وَالسَّقْفِ الْمَرْفُوعِ ﴿٥﴾ وَالْبَحْرِ الْمَسْجُورِ ﴿٦﴾

"Naapa kwa Mlima, na kwa Kitabu kilichoandikwa katika karatasi ya ngozi kikakunjuliwa, na kwa nyumba inayozuriwa, na kwa sakafu (mbingu) iliyonyanyuliwa, na kwa bahari zilizojazwa (maji). Qur'an, 52:1-6.

لَعَمْرُكَ إِنَّهُمْ لَفِي سَكْرَتِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿٧٢﴾

"Naapa kwa uhai wako, bila shaka wao wako katika upofu wanahangaika". Qur'an, 15:72.

Basi ni vipi itafaa kuhukumu kwamba kuapia kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu ni shirki na ni haramu, hali ya kuwa kuna aya nyingi za Qur'an zimelitaja jambo hilo?

Ikiwa mtu atasema, "Kiapo hiki kinamuhusu Mwenyezi Mungu peke yake".

---

1. Tat-Hirul-Iitiqad cha As-Sanani, uk. 14.
2. Al-Hadiyyatus-Saniyyah, uk. 25.

Jawabu: Sivyo kabisa, bila shaka Qur'an ni Kitabu cha muongozo kwa watu, na watu wanakichukulia kuwa ni kiigizo cha kufuata, basi lau ingekuwa aina hii ya kiapo ni haramu kwa waja wa Mwenyezi Mungu, Qur'an ingelazimika kuhadharisha kwamba kiapo hiki ni miongoni mwa mambo yanayomuhusu Mwenyezi Mungu. Na ilipokuwa tahadhari hii haikutajwa, basi imekuwa ni dalili ya kutokuhusika kwa kiapo hiki kwa Mwenyezi Mungu peke yake. Wako baadhi ya watu miongoni mwa wale wasiojua malengo ya Qur'an wanasema kwamba "Inawezekana kuwa jambo litokalo kwa Mwenyezi Mungu likawa zuri, na jambo hilo hilo likafanywa na mwingine likawa baya". Jawabu la madai haya liko wazi, kwani kuapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu lau ingekuwa ni shirki na ni kumshabihisha kwa Mwenyezi Mungu asiyekuwa Mwenyezi Mungu, basi ni kwa nini shirki hii hii (ndogo au kubwa) imetoka kwake Mwenyezi Mungu? Je, Hivi inasihi kwa Mwenyezi Mungu yeye mwenyewe kujiwekea mshirika na akamkataza mwingine kufanya shirki kama hii? Dalili Ya Pili: Mtume **[s.a.w.w]** aliapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu katika mahala pengi. Miongoni mwake ni:

1. Muslim katika Sahihi yake amepokea (hadithi ifuatayo). Kuna mtu fulani alikuja kwa Mtume **[s.a.w.w]** akasema, "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ni sadaka gani yenye malipo makubwa"? Mtume akasema, "Amma naapa kwa baba yako, wewe ni lazima utapewa khabari yake nayo ni kwamba wewe unatoa sadaka wakati wewe ni mzima na unaipenda mali, unaogopa ufakiri na unatarajia kuendelea kuishi."[1]

2. Muslim amepokea tena (hadithi ifuatayo): "Kuna mtu fulani kutoka Najdi, alikuja kwa mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** akitaka kuufahamu Uislamu, Mtume **[s.a.w.w]** akasema: "Ni Kusali Sala tano kila siku." Yule mtu akasema; Je, kuna wajibu juu yangu zaidi ya Sala tano? Mtume akasema: Hapana, isipokuwa ukitaka kufanya Sunna na ufunge mwezi wa Ramadhani". Yule mtu akasema: Ninawajibu mwingine juu yangu zaidi ya huu? Mtume akasema: "Hapana, isipokuwa ukifunga Sunna na Mtume akamtajia mtu huyo Zaka". Yule mtu akasema: "Kuna wajibu juu yangu zaidi ya huu"? Mtume akasema: "Hapana, isipokuwa ukitaka kufanya Sunna". Yule mtu aliondoka huku akisema, "Namuapa Mwenyezi Mungu sintazidisha zaidi ya hivi (nilivyofundishwa) wala sintapunguza." Mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** akasema, "Naapa kwa Baba yake, kama anasema kweli, basi amefaulu". Au alisema, "Naapa kwa Baba yake, kama anasema kweli ataingia Peponi."[2]

3. Hadithi hii (Tuliyoitaja) imekuja pia katika Musnad ya Ahmad bin Hanbal na mwishoni mwa hadithi hii katika Musnad ya Ahmad imekuja kwamba Mtume **[s.a.w.w]**. alimwambia yule mtu, "Naapa kwa maisha yangu, ikiwa utaamrisha mema na kukataza maovu ni bora kuliko kukaa kimya".[3] Na kuna hadithi nyingine ambazo nafasi ya kitabu haitoshelezi kuzitaja.[4] Naye Amirul-Mu'miniina Ali Ibn Abi Talib [a.s] ambaye

---

1. Sahihi Muslim, Juz. 3, Kitabul-zakat.
2. Sahih Muslim, Juz. 1, babu Mahuwal-Islam, uk.32.
3. Musnad Ahmad, Juz. 5, uk. 225.
4. Musnad Ahmad, Juz. 5, uk. 212, Sunan Ibn Majah, Juz. 4, uk. 995 na Juz. 1, uk. 255 ili kupata maelezo kwa urefu zaidi.

anazingatiwa kuwa ni mfano ulio wazi wa malezi ya Kiislamu na uongozi mtukufu, aliapia nafsi yake tukufu zaidi ya mara moja katika khutba zake na barua zake na maneno yake.[1] Vile vile Bwana Abubakr bin Abi Qahafah aliapa kwa baba wa mtu aliyekuwa akizungumza naye.[2]

## KUAPA KWA ASIYEKUWA MWENYEZI MUNGU KATIKA MADHEHEBU MANNE

Kabla hatujaleta dalili za Mawahabi zinazoharamisha kuapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, ni bora tukaleta fat-wa za Maimamu wa madhehebu manne kuhusu mas-ala haya. Kwa ufafanuzi zaidi unaweza kurejea kitabu kiitwacho "Al-Fiq-hu Alal-Madhahibil-Ar-Baa", mlango wa kiapo Juz. 1, uk. 75 Chapa ya Misri. Ama Madh-hebu ya Kihanafi, wao wanasema kwamba, "Kuapia baba na uhai kama vile mtu akasema, "Naapa kwa baba yako, au akasema, naapa kwa uhai wako" na mfano wa viapo hivi, jambo hili ni karaha (makruhu). Nao Mashafii wao wanasema kwamba; "Kuapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, ikiwa si kwa itikadi ya shirki, basi jambo hili ni makruhu." Ama madhehebu ya Kimaliki, wao wanasema, "Bila shaka kuapia vitu vitukufu na vyenye heshima, kama Nabii na Al-Kaaba, kuna kauli mbili, haramu na karaha." Lakini iliyo mashuhuri baina yao (wenye Madhehebu ya Malik) ni haramu.

Na kwa upande wa Madh-hebu ya Hanbal wao wanasema kwamba, kuapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu na sifa zake ni haramu hata kama kiapo hicho kitakuwa ni kuapia Manabii au mmoja wa Mawalii wa Mwenyezi Mungu. Hizi ndizo fat-wa za Maimamu wa madh-hebu manne. Nasi sasa hivi hatuko katika msimamo wa kujadiliana na wale wasemao kuwa ni Haramu (kuapa kwa asiye Mwenyezi Mungu). (Tunachoweza kusema) ni kwamba fat-wa zao ni jitihada yao dhidi ya nassi ya Qur'an na Sunna ya Mtume **[s.a.w.w]** na sera ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kadhalika wanachuoni wa madhehebu haya wameufunga mlango wa Ijtihadi kwao wao kwa hiyo wakajikuta wamelazimika kufuata maoni ya wale Maimamu wanne peke yao. Sisi hatuyaamini maneno waliyonasibishiwa Maimamu hao juu ya mas-ala haya, kwani AI-Qastalani amesema kuwa, "Imam Malik bin Anas alikuwa akisema kuwa ni karaha kuapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu".[3]

Pia kuwanasibishia Madh-hebu ya Hanbal kuwa wanasema ni haramu haikuthibiti vile vile kwa sababu, Ibn Qud-damah anaeleza katika kitabu kiitwacho "Al-Mughni" alichokiandika ili kuihuisha Fiqhi ya Kihanbal anasema, "Ahmad bin Hanbal ametoa fat-wa kuwa inafaa kuapia kwa Mtume **[s.a.w.w]**, na kwamba kiapo kinathibiti kwa kuwa Mtume ni moja ya nguzo mbili za shahada. Na amesema Ahmad bin Hanbal: "Lau (Mtu) ataapa kwa kumuapia Mtume, kiapo chake kitathibiti na kama hatatekeleza kiapo chake basi itamlazimu kutoa kafara". Pamoja na kauli zilizo tangulia, haiwezi kuthibitika moja kwa moja kuwa Maimamu wa madhehebu haya

1. Nah-Jul-Balagha Hashiya ya Muhammad Abdoh, Khutba Na. 22, 25, 56, 85, 161, 168, 182, 187, na Barua Na. 6, 9 na 54.
2. Kitabul-Muwataa cha Malik Bin Anas Imam wa Madh-hebu ya Malik chenye Sherehe ya Zir-Qani, Juz. 4, uk. 159.
3. Ir-Shadis-Saari, Juz. 9, uk. 358.

manne wametoa Fat-wa kuharamisha kuapia kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ewe msomaji mpendwa, baada ya kuzichunguza fat-wa za Maimamu wa madh-hebu manne, sasa tunahamia kwenye kutaja hadithi mbili ambazo Mawahabi wamezishikilia katika kuharamisha kuapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu. Na kwa kutumia hadithi hizo, Mawahabi wamemwaga damu ya watu wasiyokuwa na makosa na kuwashambulia mimilioni ya Waislamu kwa kuwakufurisha. Kwa hakika Mawahabi waliushambulia mara mbili mji mtakatifu wa Karbala, moja ya mashambulizi hayo lilikuwa mwaka 1216 A.H. na jingine mwaka 1259 A.H., na hawakumhurumia mdogo wala mkubwa kiasi kwamba waliwauwa Waislamu elfu sita katika muda wa siku tatu tu, na walipora kila kitu cha thamani kubwa kichokuwa katika Haram Tukufu ya Imam Husein, na tendo lao hili ni la kufuata nyayo za matendo yaliyofanywa na majeshi ya Yazid Ibn Muawiyah wakati yalipoushambulia mji wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]**. Lakini ni kwa nini? Ni kwa nini basi kufanya mashambulizi haya yenye chuki?

Sababu yake ni kuwa, Waislamu hawa walikuwa wakimuapa Mwenyezi Mungu kwa haki ya watoto wa Mtume **[s.a.w.w]** na wakiwapenda.

Hadithi ya Kwanza: Hakika mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimsikia Omar akisema, "Namuapa baba yangu". Mtume akamwambia, "Hakika Mwenyezi Mungu anakukatazeni kuapa kwa baba zenu, basi kama kuna yeyote mwenye kuapa na amuape Mwenyezi Mungu au anyamaze (asiape)".[1]

**Jawabu**: Kwanza, huenda katazo la kuwaapa wazazi (wao) lilikuja kwa sababu wazee hao wengi wao walikuwa ni washirikina waliokuwa wakiabudu masanamu, kwa hiyo hawana ubora wala utukufu kiasi cha kuweza yeyote yule kuwaapia. Na bila shaka kuna hadithi imekuja kutoka kwa Mtume **[s.a.w.w]** kwamba: "Musiapie kwa wazee wenu wala kwa masanamu".[2] Na imepokelewa vile vile kwamba: "Musiapie kwa Baba zenu wala mama zenu wala kwa miungu."[3]

Pili: Makusudio ya katazo la kuapa kwa baba, (Mtume alipokataza kuapa kwa baba makusudio yake) ilikuwa ni kile kiapo ambacho kinatumika katika hukumu ya kesi ili kuondoa kutokuelewana na uhasama kwani wanachuoni wa Uislamu wanaafikiana kwamba, kiapo ambacho kinatumika kwa ajili ya kuondosha kutoelewana na ugomvi ni kuapa kwa Mwenyezi Mungu na sifa zake, ama kiapo kingine hiki hakiingii mahala hapa. Pamoja na kuwepo kwa Qarina hizi zilizowazi..... Basi vipi itawezekana kusema kwamba Mtume **[s.a.w.w]** alikataza kuapia kwa vitu vitakatifu kama vile Al-Kaaba na Qur'an na Mawalii wa Mwenyezi Mungu hali ya kuwa tunafahamu kwamba katazo lilikuwa linahusu mahali maalum na Mtume mwenyewe alikuwa akiapia vitu visivyokuwa Mwenyezi Mungu? Hadithi ya Pili: Ibn Omar aliijiwa na mtu mmoja akamwambia, "Je, Niapie Al-Kaaba"? Ibnu Omar akamwambia yule mtu, "Hapana (usiapie Al-Kaaba) lakini apa kwa Mola wa al-Kaaba, kwani Omar alikuwa akiapa kwa baba

1. Sunan Ibn Majah Juz. 1, uk. 277, na Sunan Atir-midhi, Juz. 4 uk. 109 n.k.
2. Sunan An-Nasai Juz. 7, uk. 7, Sunan Ibn Majah, Juz. 1, uk. 278.
3. Sunan An-Nasai Juz. 7, uk. 9.

yake na Mtume akamwambia, usiapie kwa baba yako kwani yeyote mwenye kuapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu bila shaka atakuwa amefanya shirki".[1]

Jibu La Kwanza: Bila shaka hadithi hii imefungamana na mambo matatu:

1. Mtu aliyekuja kwa Ibn Omar akasema niape kwa al-Kaaba? Akamjibu kwa kusema, hapana, lakini apa kwa Mola wa Al-Kaaba.

2. Omar bin Khatab alikuwa akiapa kwa baba yake, Mtume **[s.a.w.w]** akamkataza kufanya hivyo.

3. Mtume **[s.a.w.w]**. alibaimsha ubaya wa kufanya hivyo kuta kusema "Yeyote atayeapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu atakuwa kafanya shirki".

Kiapo chenye uhakika katika hadithi hiyo kama yalivyokuja maneno ya Mtume **[s.a.w.w]** ni kuwa, iwapo kinachoapiwa siyo katika vitu vitakatifu kama vile kafiri na sanamu.

Lakini Ibn Omar alifanya Ij-tihadi kwa kusema kuwa, kauli ya Mtume isemayo "Yeyote mwenye kuapa kwa asiye Mwenyezi Mungu atakuwa kafanya shirki" ambayo aliisema kutokana na kuapiwa kwa mshirkina ambaye ni Khattab mzazi wa Omar, Ibn Omar alijitahidi (kutoa maoni yake) kuwa eti kauli hiyo ya Mtume inakusanya pia kuapa kwa vitu vitakatifu, kama vile al-Kaaba, hali ya kuwa anafahamu kuwa maneno ya Mtume **[s.a.w.w]** yalikuja kutokana na kiapo cha kumuapia mshirkina kama tulivyofafanua wakati tukiichambua ile hadithi iliyotangulia. Kwa hiyo basi maneno ya Mtume **[s.a.w.w]** yalikuwa katika kanuni maalumu aliyoiweka kwamba, ikiwa kinachoapiwa ni kitu kisichokuwa kitakatifu. Lakini Ibn Omar alifanya Ij-tihadi akayafanya maneno ya Mtume kuwa yanakusanya zaidi ya maana hiyo. Na Ij-tihad yake hiyo ni hoja juu yake mwenyewe na siyo juu ya mwingine.

Bila shaka hapo kabla tumefafanua ya kwamba, Mtume **[s.a.w.w]** alikuwa akiapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu mara nyingi tu. Basi inapasa tuichukue kauli yake isemayo; "Yeyote mwenye kuapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu atakuwa kafanya shirki" iwe kwa maana ya kuapia kwa mshirikina na mfano wake, na siyo kwa maana ya kuapia vitu vitukufu kama vile Qur'an na al Kaaba na Mtume. Na hii itakuja kutokana na dalili kwamba Mtume aliweka kanuni hii wakati Omar alipoapa kwa baba yake ambaye ni mshirikina. Ibn Omar alipoieneza hadithi hii na kuingiza kuapa kwa asiyekuwa mshirikina hiyo in ij-tihadi yake mwenyewe bila ya dalili. (Pengine) utauliza: Ni kwa nini Mtume **[s.a.w.w]** aliona kuwa kuapia kwa mshirikina ni shirki? Jawabu Lake: Ni kwamba, kuapa kwa mshirikina ni miongoni mwa aina za kumpa nguvu mshirkina na kumtukuza na kuithibitisha dini yake na itikadi yake potofu.

Kwa kifupi sisi tunaikubali asili ya hadithi lakini hatukubali Ij-tihad ya Ibn Omar kutokana na yeye kwenda kinyume na Sunna ya Mtume **[s.a.w.w]** na sera ya Masahaba. Kanuni iliyotajwa ndani ya hadithi ya Mtume Mtukufu **[s.a.w.w]** inahusu kile alichokiapia Omar, wala haikusanyi kamwe vitu vitukufu vya Kiislamu. Na ama kuapia Al-Kaaba na Qur'an na Manabii

1. As-Sunanul-Kubraa cha Al-Baihaqi Juz. 10, uk. 29, na hadithi kama hii iko katika Musnad Ahmad bin Hanbal, Juz. 2, uk. 69.

na Mawalii mahala pasipokuwa na kesi na hukumu zake jambo hilo liko nje ya kanuni hiyo ya ujumla, na siyo shirki wala haramu. Jawabu la Pili: Hapa kuna Jawabu jingine lililo wazi zaidi kuliko lile la kwanza, nalo ni lifuatalo): Bila shaka kauli ya Mtume **[s.a.w.w]** aliposema: "Yeyote atakayeapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu basi atakuwa kafanya shiriki". Inaashira kiapo maalum tu nacho ni kuapia masanamu kama vile lata na uzza (miungu iliyokuwa ikiabudiwa na Maquraishi) wala hakimuingizi mtu mshirikina licha ya vitu vitukufu. Jawabu hili, linaungwa mkono na hadithi aliyoipokea An-Nasai ndani ya Sunan yake kwamba, Mtume **[s.a.w.w]** amesema: "Yeyote atakayeapa akasema katika kiapo chake, Naapa kwa Lata na Uzza, basi mtu huyu na (Atoe Shahada) aseme; "La illaha Ila-llahu."[1] Pia hadithi aliyoipokea ndani ya kitabu hicho hicho kwamba Mtume **[s.a.w.w]** amesema: "Msiape kwa baba zenu wala mama zenu wala kwa miungu". Bila shaka hadithi ya kwanza inajulisha kuwa, itikadi za Kijahiliya zilikuwa zimeacha mabaki yake katika baadhi ya nafsi za watu, basi wakawa huapia Masanamu yao waliyokuwa wakiyaabudu kinyume cha Mwenyezi Mungu, ndipo Mtume **[s.a.w.w]** akawaamuru kusema "La illaha ila llahu" ili kuondosha mabaki hayo ya itikadi za Kijahiliyya.

Na yale mapokezi yaliyopokelewa na Imam wa Mahanbali yanafahamisha kuwa kauli yake Mtume **[s.a.w.w]** isemayo, "Yeyote atakayeapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu basi atakuwa kafanya shirki". Hadithi iko peke yake tu. Baadaye akaja huyu Ibn Omar akaingiza Ij-tihadi yake binafsi kwamba, kiapo (kilichotajwa katika hadithi) kinakusanya kiapo cha kumuapia baba na vitu vitakatifu. Lakini (kwa mujibu wa hadithi hiyo) kuapia kwa wazazi na vitu vitakatifu havikuwemo ndani ya hadithi hiyo, na aliyeviingiza humo ni Ibn Omar. Ile hadithi aliyoipokea Imam wa Madh-hebu ya Hanbal ni hii ifuatayo: Imepokewa kutoka kwa Ibn Omar amesema, Baba yangu alikuwa akiapa, Mtume akamkataza akasema; "Yeyote atakayeapa kwa asiye Mwenyezi Mungu basi atakuwa kafanya shirki". Bila shaka unaiona hadithi ya Mtume **[s.a.w.w]** imepwekeka kutokana na maneno ya Ibn Omar na haikuja na Waw ya Atfu au Fau ya Tafrigh, bali amesema; "Fanahahun-Nabiyyu" (Yaani Mtume akamkataza) akasema: ...... Jambo ambalo linajulisha kwamba hadithi hii ilitoka katika wakati mwingine na haikuwa na nyongeza yoyote.

Ewe msomaji mpendwa mukhtasari wa maelezo yaliyomo ndani ya mlango huu tulioeleza uko kama ifuatavyo:

1. Kuapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu hapana kizuwizi chochote kishera, na kiapo hicho kimeanzia kwake Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani ya Qur'an Tukufu na Mtume wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** na pia Khalifa wa Mtume Amirul-Mu'minina Ali [a.s] na Waislamu.

2. Kuapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu si sahihi (Lakini hutusemi haijuzu), si sahihi katika hukumu na kesi, bali ni lazima kumuapa Mwenyezi Mungu au kuapa kwa moja ya sifa zake ambazo ndizo dhati yake tukufu, na hili limethibiti kwa dalili maalum wala halina uhusiano katika uchunguzi huu. Bila shaka hadithi mbili ambazo Mawahabi wapotofu wamezitolea

1. Sunan An-Nasai Juz. 7, uk 8.

dalili juu ya kuharamisha kuapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, hazina uhusiano na kile ambacho sisi tunakizungumzia yaani kuapa kwa vitu vitukufu vya Kiislamu kama Qur'an, al-Kaaba, Manabii, Maimamu na Mawalii, bali hadithi hizo zinahusu kuapia mambo yasiyokuwa matukufu kama vile wazazi washirikina na masanamu yaliyokuwa yakiabudiwa zama za jahiliya. Namna hi kwa maelezo haya kile kifuniko cha Uislamu walichokivunja Mawahabi wapotovu kinaondoka, kifuniko ambacho hukivalisha ule mtazamo wao wa kipekee na fikra zao potofu. Sifa zote njema Anastahiki Mwenyezi Mungu.

18

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## KUWAOMBA MSAADA MAWALII WA MWENYEZI MUNGU

Je, inafaa kuwaita Mawalii wa Mwenyezi Mungu kuwaomba msaada wakati wa shida na matatizo? Mas-ala haya ni miongoni mwa Mas-ala ambayo kuna tofauti ndani yake baina ya Waislamu na Mawahabi. Kuwaomba msaada Manabii na Mawalii wa Mwenyezi Mungu, na pia kuwaita kwa majina yao wakati wa shida, matatizo na mambo ya hatari ni sunna iliyojengeka miongoni mwa Waislamu. Basi, ni sawa sawa kuwaomba msaada huo kwenye makaburi yao matukufu au sehemu nyingine yoyote ile na wala hawaoni ubaya wowote katika kuomba msaada wa aina hii wala siyo shirki na wala si kinyume cha dini. Wakati Mawahabi wanalipinga jambo hili kwa bidii zote, Waislamu hawaoni ubaya wa kulitenda wala siyo shirki ndani ya uombaji huu wala siyo kinyume cha dini. Mawahabi hawa kila wafanyapo upinzani wao dhidi ya mas-ala haya wanatumia baadhi ya aya za Qur'an ambazo kamwe hazina uhusiano wowote na mas-ala haya, isipokuwa lengo lao ni kuuchanganya uovu wao huo na haki. Aya wazitumiazo ni kama hii ifuatayo: Mwenyezi Mungu amesema:

وَأَنَّ الْمَسَاجِدَ لِلَّـهِ فَلَا تَدْعُوا مَعَ اللَّـهِ أَحَدًا ﴿١٨﴾

"Na kwa hakika misikiti ni ya Mwenyezi Mungu, basi msimuabudu yeyote pamoja na Mwenyezi Mungu". Qur'an, 72:18.

Ewe msomaji mpendwa, ili uweze kuzifahamu aya za Qur'an ambazo Mawahabi wanazitolea ushahidi kutilia nguvu maoni yao ya kipekee, tunazileta hapa aya hizo kwa ajili ya kufanya utafiti na uchunguzi ili uweze kufahamu tafsiri yake sahihi "Insha-Allah". Na kwa hiyo basi sisi tunawajibu kwa Qur'an hii hii ambayo wao wanadai kuwa ndiyo wanayoitolea ushahidi kabla ya kitu kingine chochote. Baadhi ya aya hizo tunazitaja kama ifuatavyo:

لَهُ دَعْوَةُ الْحَقِّ وَالَّذِينَ يَدْعُونَ مِن دُونِهِ لَا يَسْتَجِيبُونَ لَهُم بِشَيْءٍ ﴿١٤﴾

"Kwake ndiko yaliko (maitikio ya) maombi ya haki, na wale wawaombao asiyekuwa yeye hawatawaitikia kwa chochote". Qur'an, 13:14.

وَالَّذِينَ تَدْعُونَ مِن دُونِهِ لَا يَسْتَطِيعُونَ نَصْرَكُمْ وَلَا أَنفُسَهُمْ يَنصُرُونَ ﴿١٩٧﴾

"Na wale mnaowaita badala yake, hawawezi kukusaidieni wala hawawezi kujisaidia nafsi zao". Qur'an, 7:197

وَالَّذِينَ تَدْعُونَ مِن دُونِهِ مَا يَمْلِكُونَ مِن قِطْمِيرٍ ﴿١٣﴾

"Na wale mnaowaita kinyume chake, hawamiliki japo utando wa kokwa ya tende." Qur'an, 35:13

إِنَّ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّـهِ عِبَادٌ أَمْثَالُكُمْ ﴿١٩٤﴾

"Na wale mnaowaita kinyume cha Mwenyezi Mungu (wao) ni waja kama ninyi". Qur'an, 7:194.

قُلِ ادْعُوا الَّذِينَ زَعَمْتُم مِّن دُونِهِ فَلَا يَمْلِكُونَ كَشْفَ الضُّرِّ عَنكُمْ وَلَا تَحْوِيلًا ﴿٥٦﴾

"Waambie, waiteni wale mnaodai (kuwa ni Miungu) kinyume chake (Mwenyezi Mungu) hawawezi kukuondoleeni matatizo wala kubadilisha (chochote). Qur'an, 17:56

﴿أُولَـٰئِكَ الَّذِينَ يَدْعُونَ يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمُ الْوَسِيلَةَ ﴿٥٧﴾

"Hao wanaowaita wao (wenyewe) wanatafuta (njia) ya ukaribiano na Mola wao". Qur'an, 17:57

﴿وَلَا تَدْعُ مِن دُونِ اللَّـهِ مَا لَا يَنفَعُكَ وَلَا يَضُرُّكَ ﴿١٠٦﴾

"Wala usikiite (chochote) kinyume cha Mwenyezi Mungu, ambacho hakikunufaishi wala kukudhuru". Qur'an, 10:106

﴿إِن تَدْعُوهُمْ لَا يَسْمَعُوا دُعَاءَكُمْ ﴿١٤﴾

"Kama mkiwaomba (masanamu hao) hawasikii wito wenu: Qur'an, 35:14

﴿وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن يَدْعُو مِن دُونِ اللَّـهِ مَن لَّا يَسْتَجِيبُ لَهُ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ ﴿٥﴾

"Ni nani mpotevu mkubwa kuliko yule anayemuomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu, ambaye hatamjibu mpaka siku ya Qiyama?" Qur'an, 46:5

Kwa kutumia aya hizi, Mawahabi wanazitolea ushahidi kuharamisha kuomba msaada kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu na pia kuwaita baada ya kufa kwao, na (wanasema) kwamba, kufanya hivyo ni kuwaabudia Mawalii hao na ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu. Wanasema Mawahabi, "Kama mtu atasema kwenye kaburi la Mtume **[s.a.w.w]** au akawa sehemu nyingine akasema, "Ewe Muhammad". Basi atakuwa amemuabudu (Mtume) kwa wito huu alio mwita na dua hii. Wahabi aitwaye As-San-Ani anasema: "Bila shaka Mwenyezi Mungu ameiita dua kuwa ni ibada pale aliposema, "Niombeni nitakuitikieni, kwa hakika wale wanaopinga ibada yangu...." Basi yeyote atakayeliita jina la Mtume fulani au Mcha mungu fulani kwa kutaka kitu fulani (kwa Nabii au Mchamungu huyo) au akasema (Ewe Nabii) niombee kwa Mwenyezi Mungu katika shida yangu au akasema, nakuomba uniombee kwa Mwenyezi Mungu katika shida yangu, au akasema, (Ewe Nabii) nilipie deni langu, niponye ugonjwa wangu na mengineyo mfano wa haya, basi atakuwa amemuomba Nabii huyo au Mchamungu huyo wakati dua ni Ibada, na zaidi ya hapo (dua) ndiyo roho ya ibada, hivyo amemuabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu na amekuwa mshirikina, kwani tauhidi haitimii isipokuwa kwa kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika uungu kwa kuitakidi kuwa hakuna muumba wala mwenye kutoa riziki isipokuwa yeye, na pia kumpwekesha katika ibada kwa kutokumuabudu asiyekuwa yeye japo kwa baadhi ya ibada, na wale waabuduo sanamu walikuwa washirikina kwa kutompwekesha Mwenyezi Mungu katika ibada."[1]

Jibu Lake: Miongoni mwa mambo yasiyokuwa na shaka ndani yake ni kwamba, tamko "Dua" katika lugha ya Kiarabu maana yake ni wito, na huenda pia likatumika kwa maana ya ibada, isipokuwa tu haiwezekani kwa namna yoyote ile matamko ya dua na ibada kuwa na maana moja.

---

1. Kashful-Irtiyabi: uk. 274, ikiwa ni makala toka ndani ya kitabu Tanzihul-iitikad cha As-San-Ani.

Haiwezekani kusema kuwa "Kila dua ni Ibada" kutokana na sababu zifuatazo:

1. Bila shaka Qur'an imelitumia tamko la dua mahala pengi na haiwekani kusema kuwa makusudio yake yalikuwa ni ibada, kwa mfano: Mwenyezi Mungu anasema:

قَالَ رَبِّ إِنِّي دَعَوْتُ قَوْمِي لَيْلًا وَنَهَارًا ﴿٥﴾

"(Nuhu) akasema, Ee Mola wangu hakika nimewalingania (yaani Daawtu) watu wangu usiku na mchana". Qur'an: Nuh: Aya ya 5

Hivi kweli inakubalika kusema kwamba Nabii Nuh [a.s] kwa maneno yake hayo alikusudia kwamba yeye amewaabudu watu wake usika na mchana? Hebu soma kauli ya Mwenyezi Mungu akimnukuu Ibilisi atapokuwa akiwaambia wenye dhambi siku ya Qiyama:

وَمَا كَانَ لِيَ عَلَيْكُم مِّن سُلْطَانٍ إِلَّا أَن دَعَوْتُكُمْ فَاسْتَجَبْتُمْ لِي ﴿٢٢﴾

"Wala sikuwa na mamlaka juu yenu (ya kukulazimisheni mnifuate) isipokuwa nilikwiteni (yaani Daawtukum) nanyi mkaniitikia". Qur'an, 14:22 Je, kuna yeyote atakayepelekea (mawazo yake) kwamba, maana ya wito (yaani dua) wa shetani kwa watu wenye dhambi unamaanisha kuwa shetani aliwaabudu wata hao? Pamoja na hali hii tunafahamu kwamba, kama ibada ikithibitika basi ibada hiyo itatoka kwa watu hao wenye madhambi kumuabudia shetani na siyo shetani kuwaabudia wao. Ndani ya aya hizi mbili na zingine zinazofanana na hizi, tamko "Aad-Daawah" limekuja siyo kwa maana ya ibada, kwa ajili hiyo basi haiwezekani kusema kuwa dua na ibada ni matamko mawili yenye maana moja, wala haiwezekani kusema kwamba yeyote mwenye kumuita mmoja wa Manabii au Mawalii basi atakuwa kamuabudia na amemshirikisha Mwenyezi Mungu hapana sivyo kabisa, kwani mwito na dua yana maana pana zaidi kuliko ibada na mengineyo.

2. Maana ya dua katika aya walizotolea ushahidi Mawahabi haina mama ya wito tu, bali ni wito ambao uko katika maana ya ibada, kwa kuwa aya zote hizi zilishuka kuwahusu wafanyao ibada ya masanamu, ambao walikuwa wakiyaitakidi masanamu yao kuwa ni mungu wadogo waliopewa jukumu Ia (kusimamia) baadhi ya mambo ya ulimwengu, na miungu hao wanaouwezo wa kuendesha (mambo ya ulimwengu).

Zaidi ya hapo ni kwamba, dua na mwito kwa masanamu haya sawa sawa kama yatakuwa ni miungu wakubwa au wadogo, kuitakidi kuwa yanamiliki uwezo wa kushufaiya na maghfira ni kuyaabudu na ni shirki. Dalili iliyo wazi mno juu ya kwamba waabudu sanamu walikuwa wakiyaita masanamu yao kwa kuitakidi kuwa hayo ni miungu ni hii kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

فَمَا أَغْنَتْ عَنْهُمْ آلِهَتُهُمُ الَّتِي يَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّـهِ مِن شَيْءٍ ﴿١٠١﴾

"Haikuwafaa kitu miungu waliyokuwa wakiita kinyume cha Mwenyezi Mungu". Qur'an, 11:101.

Kwa hiyo basi aya zilizotajwa (Na Mawahabi) hazina kabisa uhusiano kati yake na mas-ala haya, kwa kuwa mas-ala haya yanachunguza juu ya uwezekano wa mtu kumuomba msaada mtu mwingine bila ya kumuitakidi kuwa ni mungu wala kumuitakidi kuwa na uwezo wa kujitegemea na

kumiliki uendeshaji wa mambo ya ulimwengu wala dunia wala akhera isipokuwa (anaombwa msaada huo hali ya) kuzingatiwa kuwa ni mja mwema mwenye cheo mbele ya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Utume au Uimamu, na Mwenyezi Mungu ameahidi kukubali maombi ya mja huyu mwema kwa amuombeaye kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

وَلَوْ أَنَّهُمْ إِذ ظَّلَمُوا أَنفُسَهُمْ جَاءُوكَ فَاسْتَغْفَرُوا اللَّـهَ وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ الرَّسُولُ لَوَجَدُوا اللَّـهَ تَوَّابًا رَّحِيمًا ﴿٦٤﴾

"Lau wao waliopojidhulumu nafsi zao wangekujia na wakamuomba Mwenyezi Mungu msamaha, na Mtume naye akawaombea msamaha, wangemkuta Mwenyezi Mungu ni mwenye kukubali toba Mwenye huruma". Qur'an, 4:64.

3. Bila shaka aya zilizotolewa na Mawahabi kama ushahidi zinaonyesha kuwa Makusudio ya neno "Dua" yanamaanisha maana ya "Ibada" nasiyo kinyume cha hivyo. Hebu fanya mazingatio ya kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema:

وَقَالَ رَبُّكُمُ ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ ۚ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ ﴿٦٠﴾

"Na Mola wenu anasema, niombeni nitakujibuni, kwa hakika wale wanaojivuna kufanya ibada yangu, bila shaka wataingia motoni wadhalilike." Qur'an, 40:60.

Bila shaka Mwenyezi Mungu amelitaja jambo la "Ud-uuni" kisha akalifuatisha tamko la Ibada yangu, "ibaadati" jambo ambalo linajulisha wazi kwamba, makusudio ya "Niombeni (Ud-uuni)" katika aya hii ni ibada ya Mwenyezi Mungu na (kunatakiwa) kuacha ibada isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu, na hii inaonyesha kuwa washirikina walikuwa wakijivuna kufanya dua na ibada ya Mwenyezi Mungu Mtukufu." Mjukuu wa Mtume **[s.a.w.w]**, al-Imam Zainul-Abidin [a.s] anasema katika moja ya dua zake: "**Dua ya (kukuomba) wewe umeiita kuwa ni ibada, na kuiacha umekuita ni kujivuna na umeonya kwa kuiacha (kutasababisha) kuingia motoni katika hali ya kudhalilika.**"[1][233] Katika Qur'an kuna aya mbili zilizokuja zikiwa na maana moja, mojawapo limetumika tamko 'Al-Ibadah" na ya pili limetumika tamko 'Ad-Daawa". Aya ya kwanza Mwenyezi Mungu Anasema:

قُلْ أَتَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّـهِ مَا لَا يَمْلِكُ لَكُمْ ضَرًّا وَلَا نَفْعًا ﴿٧٦﴾

"Waambie, Mnawabudu wasiokuwa Mwenyezi Mungu ambao hawamiliki dhara wala manufaa"? Qur'an, 5:76

Ya pili kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

قُلْ أَنَدْعُو مِن دُونِ اللَّـهِ مَا لَا يَنفَعُنَا وَلَا يَضُرُّنَا ﴿٧١﴾

"Waambie, Je, tumuombe asiyekuwa Mwenyezi Mungu, ambaye hatatunufaisha wala kutudhuru"? Qur'an, 6:71. Pia Mwenyezi Mungu Anasema:

وَالَّذِينَ تَدْعُونَ مِن دُونِهِ مَا يَمْلِكُونَ مِن قِطْمِيرٍ ﴿١٣﴾

1. As-Sahifatus-Sajjadiyyah, dua ya 45.

"Na wale muwaombao hawamilki japo utando wa kokwa ya tende". Qur'an, 35:13

Ndani ya aya hii imekuja kwa tamko "Mnaomba," yaani "Tad 'uuna" na humo mna dalili iliyo wazi kabisa kwamba, ombi hili 'Ad Daawah" ni la kuwaomba masanamu, na hiyo ndiyo iliyokuwa itikadi ya washirikina, wakiitakidi kuwa masanamu ni Miungu inayodhuru na kunufaisha kinyume cha Mwenyezi Mungu na ndiyo maana Mwenyezi Mungu akawakosoa kwa kuwaambia kuwa (Masanamu) hayo "Hayamiliki japo utando wa kokwa ya tende." Maana kama hii imekuja katika aya inayofanana kwa tamko la "Ta'abuduna" kama ilivyo kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema:

﴿إِنَّ الَّذِينَ تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّـهِ لَا يَمْلِكُونَ لَكُمْ رِزْقًا ﴿١٧﴾

"Bila shaka hao mnaowaabudu kinyume cha Mwenyezi Mungu hawana mamlaka ya riziki zenu". Qur'an, 29:17.

Na ndani ya aya nyingine yamekuja maneno mawili yenye kulingana kwa maana moja. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿قُلْ إِنِّي نُهِيتُ أَنْ أَعْبُدَ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّـهِ ﴿٥٦﴾

"Waambie, Mimi nimekatazwa kuwaabudu wale mnaowaita kinyume cha Mwenyezi Mungu". Qur'an, 6:56.

Na karibu na maana ya aya hii ni aya ya 66 Sura ya 40.

Ewe msomaji mpendwa nakutarajia kuwa utairejea al-Mujamul-Mufahras Li alfaadhil-Qur'an il-Karim katika madda ya "Abada, ameabudu" na "Daa, ameomba" ili upate kuona kwa macho yako ni namna gani tamko la ibada lilivyokuja katika aya fulani na pia tamko la "Ad daawat" na "Ad duaa" yalivyokuja katika aya nyingine. Utaona kuwa matamko hayo katika namna hizo mbili yamekuja kwa maana na madhumuni ya namna moja yaani ibada, jambo ambalo ni dalili iliyo wazi kuonyesha kuwa makusudio ya "Ad Daawat" na "Ad Duaa" katika aya hizi ni ibada na kwamba aya hizi hazihusiki na mwito peke yake. Basi utakapozifanyia mazingatio aya ambazo zimeambatana na tamko "Ad Duaa" na "Ad Daawat" kwa maana ya ibada, utaona kuwa aya hizo zinazungumzia mapambano kati ya imani na kufru, na pia baina ya ibada ya Mwenyezi Mungu, Tauhidi, imani ya uungu wake dhidi ya ibada ya masanamu na itikadi za (kuyapa) uwezo wa kumiliki riziki, maghfira, shafaa, kunufaisha na kudhuru.

Hivyo basi, Mawahabi kutoa ushahidi kwa aya hizi ili kuharamisha kuwaita Manabii na Mawalii na kutaka kwao msaada, ni jambo linalopelekea kushangaza na kustaajabisha hasa inapoonekana kuwa aya walizotolea ushahidi hazina uhusiano wowote na mas-ala haya. Kifupi tu, kwa yale yaliyothibiti ndani ya utafiti huu ni kuwa: Kauli yako utaposema, "Yaa Ali" hali ya kuwa unakusudia kumsemesha Khalifa wa Mtume [s] au ukasema, "Ya Husain" au "Ya Zahraa" au ukataja jina jingine la mmoja miongoni mwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu waliotakasika hakuna tatizo kabisa kwa kusema hivyo, bali ni namna ya kuomba msaada kwao, Mwenyezi Mungu awateremshie Rehma wote. Basi jambo hili ni zuri linalofaa kufanywa, na humsaidia mtu kujinasua toka kwenye matatizo na shida na kumuokoa kutokana na maangamizi na kisha kumpa faraja.

## HIJJA - MSIMU WA IBADA NA NI MKUTANO WA KISIASA

Mwenyezi Mungu ameifanya al-Kaaba kuwa ni nyumba tukufu na ni wasila wa kusimamisha amani miongoni mwa watu, na akaifanya Hijja kuwa ni msimu wa ibada na ni fursa ya Waislamu kutoka kila upande kukutana na kufahamiana, na pia wafahamishane mambo muhimu ya Dini yao na kuzichunguza hali zao. Basi mambo haya baada ya Ibada ni miongoni mwa uthibitisho dhahiri wa kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema:

"Na ili washuhudie manufaa yao" Qur'an, 22:28. Basi ni manufaa yepi makubwa baada ya ibada kuliko Waislamu kukutana mahala pamoja ambapo wameacha kila hisia ya dhati na jamii na mipaka ya kitaifa na kimataifa na rangi, bali Waislamu wote hufunikwa na kivuli cha Dini na kupambwa na hisiya za upendo pia moyo wa udugu wa kweli? Na ni masala gani muhimu kuliko Waislamu kufahamishana hatari na matatizo yaliyowazunguka, na wakaeleweshana namna ya kuyatatua kwa pamoja na kwa nguvu moja na azma ya pamoja ili kuyaondoa au kupunguza uzito wake?

Na Je, Ni tatizo gani kubwa zaidi linalowakandamiza Waislamu leo hii kuliko tatizo la ukoloni wenye aina tofauti ambao umezikalia nchi za Waislamu kijeshi, au kuzitawala kisiasa au kizipiga vita kitaaluma na kisha kuupora uchumi wa Waislamu na kueneza fitna miongoni mwao na kuwauwa watoto wao na kuwaharibu (kitabia) vijana wa Kiislamu, na, na, na, na......!!! Je, siyo kwamba Hijja ndiyo mahali bora pa kutangazia uchungu wa Waislamu wote dhidi ya ukoloni huu mbaya unaongozwa na Amerika na Urusi? Na kama Waislamu wenye kudhulumiwa na kutawaliwa katika nchi zao hawawezi kutangaza uchungu wao na chuki yao dhidi ya wakoloni wakiwa ndani ya kitovu cha nchi zao kwa kuwa tu kuna serikali zinazotumiwa kuwaziba vinywa na kunyamazisha sauti zao, basi Hijja haiwi ndiyo fursa inayofaa mno kutangaza uchungu wao na chuki zao bega kwa bega, Waislamu wote wakiwa katika ibada unyenyekevu na kutubia (kwa Mwenyezi Mungu)? Je, kuwapinga mabeberu ambao kuwatii hukmu zao na kukubaliana nao na pia kuwategemea ni miongoni mwa shirki katika twa'a ya Mwenyezi Mungu? Je, kuwapinga mabeberu siyo miongoni mwa aina dhahiri mno za tauhidi ambayo Mwenyezi Mungu ameifanya Hijja iwe ndiyo kielelezo chake na uthibitisho wa ukweli wake?

Na kwa hakika leo hii Waislamu wameutambua ukweli huu pamoja na kukua kwa harakati za Kiislamu na kuongezeka kwa jamii ya Kiislamu. Waislamu wamekwisha tambua kwamba Hijja ndipo mahali panapofaa na ni fursa inayofaa kuwaunganisha Waislamu na kuwazindua, kisha kawatambulisha ukweli wa matukio ya kusikitisha ambayo yanatendwa na maadui wa Uislamu, (ambao ni) Amerika, Urusi, Ufaransa, Uingereza na wengineo miongoni mwa tawala za kikoloni na kibeberu. Kwa hakika Waislamu wamekwisha fahamu kwamba, Hijja ndiyo fursa nzuri ya kutangaza uchungu wa Waislamu bega kwa bega kutokana na ukoloni muovu pamoja na kufanya ibada na kutubu kwa kufuata kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema:

"Ili washuhudie manufaa yao na wamtaje Mwenyezi Mungu". Qur'an, 22:28 Kauli hii (ya Mwenyezi Mungu) inaashiria falsafa ya Hijja inayochanganya ibada na siyasa na malengo yake ya kidunia na akhera. Na

kwa ajili hii ndiyo maana kumekuweko mshikamano mkubwa wa kisiasa ambao Waislamu wameuanzisha katika siku za Hijja kwa miaka kadhaa wakiongozwa na Waislamu wa Iran.

Lakini kwa huzuni kubwa tunakuta baadhi ya watu wanaodai kuwa na elimu na wanakalia vyeo vya uenezaji wa Uislamu, wanapinga kwa nguvu harakati hizi tukufu, na wanapinga hatua hizi zenye athari (nzuri) ambazo hazilengi ila kuwakomboa wenye kunyimwa na kudhulumiwa (haki zao) (pia harakati hizi zinalenga) kuutokomeza ukoloni na utumwa. (Watu hao wapingao wanapinga) hali ya kuwa kila sika wanasikia habari za mauaji na uchinjaji wa mamilioni ya vijana wa umma wa Kiislamu huko India, Palestina, Lebanon na Afghanistan, Eritrea na katika mipaka ya Iraq na Iran na kwingineko. Na mauaji hayo moja kwa moja yanatokana na sababu zinazosababishwa na ukoloni. Watu hawa badala ya kuunganisha sauti zao na sauti za Waislamu wengine wanaopinga matendo ya ukoloni ambao kwa uovu wake unapokonya haki za Uislamu na Waislamu, tunawakuta wananyanyua sauti zao upande wa ukoloni dhidi ya Waislamu, na wanapinga chuki na hasira za Waislamu dhidi ya ukoloni mamboleo wa Kimarekani, Urusi, Uingereza na Ufaransa ambao mikono yao imelowana kwa damu ya Waislamu na majumba yao yamejengwa kwa mafuvu ya watoto wa Kiislamu. Cha ajabu zaidi kuliko hili, ni kule kushikilia kwao kuharamisha hatua hizi tukufu (za kupinga wakokoni kwenye Hijja) kwa kutumia kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema;

"Hapana kusema maneno machafu wala kufanya vitendo vichafu wala asibishane katika Hijja." Qur'an, 2:197

Huyo ni Sheikh Abdallah al-Khayyat ambaye ni Imam na ni Khatibu wa msikiti Mtukufu wa Maka. Yeye ameona kuwa, kuyaeleza matatizo ya kisiasa ya Waislamu katika msimu wa Hijja ni kutoka nje ya lengo la Hijja, na akatoa dalili ya madai yake kwa kutumia kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema:

فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ الْحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِي الْحَجِّ ﴿١٩٧﴾

"Basi yeyote aliyekusudia kufanya Hijja, asiseme maneno machafu wala kufanya vitendo vichafu, wala asibishane katika hiyo Hijja." Qur'an, 2:197.

Na akasema tena Sheikh Khayyat, "Na kama alivyoikusudia Mtume **[s.a.w.w]** Ibada ya Hijja pale aliposema, "Yeyote mwenye kuhiji na akawa hakusema maneno machafu wala hakutenda matendo machafu hurejea kama siku aliyozaliwa na mama yake". Anaendelea kusema Sheikh Abdallah al-Khayyat, "Ama wito wa Iran ya Khomein ambao anataka kuigeuza Hijja kuwa ni matangazo ya kisiasa na maandamano ya kudai (haki) na kupinga Serikali, mambo hayo hayakubaliki namna yafanyikavyo na pia madhumuni yake, kwani yanapingana na mafunzo ya Dini yetu tukufu na yanatoka nje ya maana yake na misingi yake bora, kwa kuwa yanavunja moja ya nguzo miongoni mwa nguzo (za Dini)."

"Ndani yake mna uvunjaji wa heshima ya vitu vitukufu vya Mwenyezi Mungu na kuna kiburi dhidi ya mambo matukufu ya Mwenyezi Mungu na pia kwenda kinyume cha mwelekeo alioelekeza Mwenyezi Mungu." "Anaendelea kusema: "Bila shaka mwito wa Iran ya Khomein unaeneza fitna na kubomoa umoja na kubadilisha upendo kuwa chuki na kuzigeuza sehemu takatifu kuwa nyanja za kutangaza mambo ya siasa na kueneza

miito isiyokuwa na maana. Hapana Muislamu yeyote ulimwenguni isipokuwa anapinga wito huu, kwani ndani yake kuna mambo yanayopinga Uislamu na kuvunja heshima ya alama za Kiislamu. Na Hijja haiwezekani kuwa isipokuwa ni mkutano wa kiroho na ni mkusanyiko wa kila mwaka ambao Waislamu toka kila shemu za mbali hukusanyika".[1] Bila shaka yaliyomo ndani ya khutba hii (iliyotangulia) ndiyo maneno ambayo tunayasikia (kila mara) kutoka kwa watu wanaoajiriwa na Suudiya, kila mwaka tunayasikia, na katika kila hotuba na kila muhutubiaji (anayasema), basi wao hawakiuki zaidi ya kusoma aya hiyohiyo na kufuata vile alivyosoma khatibu huyo maneno ambayo ni matupu.

Na sisi hapa hatutamkabili Sheikh isipokuwa kwa njia aliyotuamuru Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema, "Jadiliana nao kwa njia iliyo njema", hivyo basi tunaifafanua maana ya aya hiyo na kuiweka wazi ili makusudio yake yaeleweke na watu wote wajue kwamba maandamano ya kisiasa na kutangaza kujitenga na makafiri na kuyatokomeza matendo yao yanayoupinga Uislamu na Waislamu, na kuwaita Waislamu kwenye umoja ambao ndiyo nguzo ya maandamano aliyoyaamrisha Imam Khomeini siyo uthibitisho wa mabishano yaliyotajwa katika aya hiyo. Hebu iangalie tafsiri ya aya hiyo na ufafanuzi wa makusudio yaliyomo. Amesema Mwenyezi Mungu,

لْحَجُّ أَشْهُرٌ مَّعْلُومَاتٌ فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ الْحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِي الْحَجِّ ﴿١٩٧﴾

"Hijja ni miezi maalum, basi yeyote anayekusudia kufanya Hijja katika miezi hiyo, asiseme maneno machafu wala asifanye matendo machafu na wala asibishane katika Hijja". Qur'an, 2:197.

1. Bila shaka kukaririka kwa tamko la "Hijja" mara tatu katika aya hii, imeweka neno dhahiri badala ya dhamiri, hata hivyo hapa ni ufupisho kwani makusudio ya Hijja ya kwanza ni kutaja "wakati wa kufanya Hijja" na ile ya pili ina maana ya "tendo lenyewe la Hijja" na ile ya tatu inakusudia wakati na mahala pa kufanyia Hijja", na Iau siyo kudhihirisha (tamko la) Hijja ingekuwa hapana budi kuleta "It-Nab Ghair lazim" (Ufafanuzi usiyo wa lazima). Amesema ndani ya tafsiri aI-Manar ya Rashid Ridhaa: "Bila shaka miongoni mwa "Balaghatul-Iijaz" katika aya hii ni kule kuweka dhahiri mahala pa kuweka dhamiri kwa kuitaja Hijja mara tutu, ya kwanza ikiwa na maana ya kipindi cha Hijja kama wasemavyo "Baridi ni miezi miwili", na ya pili maana yake ni ile Hijja yenyewe ambayo ni Ibada, na ya tutu makusanya kipindi cha kutekeleza na mahala pake ambapo ni ardhi tukufu ya msikiti wa Maka nasehemu zinazofuatia kama vile Arafa".[2]

2. Makusudio ya kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema: "Yeyote anayekusudia kufanya Hijja katika miezi hiyo" Yami ameilazimisha nafsi yake kuanza Hijja kwa nia ya makusuduio ya ndani (ya moyo) na kuhirimia kwa kutenda dhahiri na kuitikia kwa kutamka labbaika.[3]

3. Iliyo Mash-huri ni kwamba maana ya neno "Ar-Rafathu" ni "kuingilia", imepokewa kwa Abdallah bin Omar na Tauus na Atwa'a na

1. Jarida la Rabitat al-Alami al-Islami la mwaka wa kumi na moja toleo la kumi na mbili.
2. Al-Manar, Juz. 2, uk. 228.
3. Tafsiri Al- Qurtubi, Juz. 2, uk. 406.

wengineo kuwa, "Ar-Rafathu" ni kutusemesha mwanamke kwa maneno machafu au uchafu kwa jumla, na imesemwa vinginevyo pia.[1]

4. Na wamelifasiri neno "Fusuuq" kuwa ni maasi yote, amesema Ibn Zaidi na Malik "Al-Fusuuq" ni kuchinja kwa ajili ya masanamu, na Adhahak amesema "Al-Fusuuq" ni kuitana (kuaibishana) kwa majina mabaya, na amesema Ibn Omar, "Al-Fusuuq" ni "Kutukana". Na kauli ya mwanzo ndiyo sahihi zaidi kwani inakusanya kauli zote. Na imepokewa kwa Mtume **[s.a.w.w]** kwamba amesema, "Atakayehiji ikawa hakusema maneno machafu wala kufanya matendo mabaya hurejea kama siku aliyozaliwa na mama yake". "Na Hijja iliyotekelezwa vyema haina malipo isipokuwa pepo". Amepokea hadithi hizi Muslim na wengineo.

5. "Jidala" katika maana ya kilugha ni mabishano, uhasama na ugomvi. Na uhasama umeitwa kuwa ni mjadala kwa kuwa kila mmoja hutaka kumgeuza mwenziwe kutoka kwenye rai yake. La muhimu mahala hapa ni kuifasiri kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo kuwa, "Na asibishane katika Hijja" na pia kubainisha makusudio yake. (Kauli hii ya Mwenyezi Mungu) kwa watu wanaoajiriwa na Suudiya wanaifanya kuwa ndiyo dalili ya kuharamisha maandamano na utoaji wa hotuba za kisiasa na miito ya umoja na kudhihirisha kujitenga na makafiri na wanafiki.

Wala hakiwezi kubainika kiwango cha dalili ya aya hii kama waionavyo watu hawa, isipokuwa ni kunakili maoni ya uwezekano wa namna ya kuifasiri aya hii kama yalivyotajwa na wafasiri wakubwa kama ifuatavyo:

A. Maoni aliyoyataja Qadhi al-Baidhawi na ar-Razi naye ameegama kwa Baidhawi, kwa kuichukulia kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo: "La Rafatha Wala Fusuqa Fil-Hajji Wala Jidalafil Haji" kuwa ni "Khabar" maelezo ambayo maana yake ni kwamba, "Hijja haiwezi kuthibiti (ikitendwa) pamoja na mojawapo ya mipaka hii, bali itaharibika kwa kuwa ni kama kufanya kinyume chake, na mambo hayo yanazuwia kusihi kwa Hijja. Kwa hiyo basi matamko hayo matatu ni lazima yachukulike kuwa ni yenye kuharibu Hijja na muradi wake ni vitendo vinavyoharibu Hijja na yanawajibisha kulipa Qadha mwakani iwapo Hijja hii ilikuwa ni wajibu.

Basi "Ar-Rafathu" hufasirika kwa maana ya "Kuingilia" na "Al-Fusuqu" kwa maana ya "Kuzini" kwa sababu vitendo hivi vinaharibu Hijja, na jidala huchukuliwa kwa maana ya kuitilia Hijja juu ya kuwa kwake ni wajibu na kusihi kwake kisheria na kuwa kwake ni tendo linalokubaliana na akili.[2] Kwa kifupi, bila shaka kilicho dhahiri ni kule kuwepo kinyume kati ya mambo haya na Hijja ambayo Mwenyezi Mungu ameamuru mwanzoni na kwa msingi huo basi, kama ambavyo haiwezekani kuchukulia neno "Fusuqu" katika maana ya lugha kwani siyo kila "Fusuqu" huharibu Hijja kama vile uongo na kuteta, vile vile haiwezekani kuchukulia neno "Jidala" katika maana ya kila ubishi kwani siyo kila ubishi unaharibu Hijja, bali muradi wake ni mabishano maalum ambayo hayawezi kukusanyika pamoja na Hijja kama vile kutia shaka uwajibu wa Hijja na kusihi kwake kisheria na kuona kuwa ni upuuzi kule kutufu jiwe, udongo na ubao - al-Kaaba.

---

1.(1) Tafsiri aI-Kashaaf ya Zama Ukhshari, Juz. 1, uk. 264. (2) Tafsiri Qur-Tubi, Juz. 2, uk. 406.

2. Mafatihul-Ghaib, Juz. 2, uk. 175, Naye pia amenakili kwa Qadhi al-Baidhawi.

Maana hii ndiyo aliyoichagua Qadhi (al-Baidhawi) na akaiunga mkono Ar-Razi katika tafsiri yake, na (maana hii) ndiyo chaguo la wanachuoni wengi ndani ya sentensi nyingi (zilizokuja namna hii) kama vile: "La Salata ila Bifatihatil-Kitabi" Yaani, hakuna Sala ila kwa (kusoma) "Suratil-Fatiha". Au "La Salata ila Bitahurin" Yaani, hakuna Sala ila kwa Tahara." Na makusudio yake ni kukanusha kusihi (kwa Sala) bila ya vitu hivyo viwili, na kwamba kuthibiti kwa Sala kumetegemea vitu hivyo, kama ambavyo makusudio ya aya ile vile vile ni kukanusha kusihi kwa Hijja (ikitendwa) pamoja na mambo hayo matatu. Basi iwapo uwezekano huo utasihi, haitafaa kuitolea dalili kwa namna waionayo hawa (wanaofadhiliwa na Suudiya) kwa kuharamisha kila majadiliano ikiwa ni pamoja na maandamano, kwani makusudio ya aya ni kubainisha uharamu wa majadiliano ambayo hayaafikiani na kusihi kwa Hijja, na makusidio (ya aya) siyokubainisha uharamu wa kila mjadala japokuwa unaafikiana na usahihi wa Hijja. Hata kama tukikubali kwamba Jidala na maandamano juu ya kuyakadiria ni haramu lakini haiharibu Hijja.

B. Kutenganisha kati ya mambo haya matatu kwa kuyachukulia yale mawili ya mwanzo kuwa ni katazo, japokuwa itakuwa ni kwa kulihalifu dhahiri ya tamko yaani "La Tar-Fathuu Wala Tufsiquu" (msitoe maneno machafu wala vitendo vichafu) na kulichukulia lile jambo la tatu kuwa ni "Khabari" yaani, hapana mjadala wala kwenda kinyume ndani ya wakati wa Hija na sehemu ya (kufanyikia) Hijja, kwa msingi huu basi, makusudio itakuwa, "Hapana mjadala wala kwenda kinyume ndani ya kipindi cha Hijja na mahali panapofanyikia Hijja, na maana hii ndiyo ambayo ameishikilia Ibn Jariri at-Tabari ndani ya Tafsiri yake.[1] Na ameitaja pia Az-Zamakh-Shari:[2] Na wote wawili wametoa ushahidi kwa namna mbili: Ya Kwanza: Kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** amesema: "Yeyote atakaye Hiji kwa ajili ya Mwenyezi Mungu akawa hakusema maneno machafu wala kufanya matendo mabaya hurejea katika hali yake kama siku aliyozaliwa na mama yake". Na wala (Mtume) hakusema "Wala hakufanya mjadala". Kwa msingi huu kuna dalili kwamba yale mambo mawili ya mwanzo yana maana ya makatazo ya kusema machafu na kutenda mabaya, wala hakuna katazo kwa lile la tatu, vinginevyo lingefuatishwa kwa hayo mawili kwa namna ya katazo, isipokuwa (hili la tutu) lina maana ya kutoa khabari na kukanusha kuwepo mjadala na kubishana katika kipindi cha Hijja na mahali pa Hijja.

Kwa hiyo kutokana na pande hizi mbili (yaani mahala na wakati) inajulikana wazi kuwa hapastahiki kutiliwa mashaka wala wasi wasi. Ya Pili: Hakika Maquraishi walikuwa wakiwakhalifu Waarabu wengine, wao husimama Mash-Aril-Haram na Waarabu wengine husimama Arafah, na walikuwa mwaka mwingine wakiiwahisha Hijja na mwaka mwingine wakiichelewsha na hiyo ndiyo "An-Nasii". Basi Hijja ikarejeshwa kwenye wakati mmoja na Wuquuf ikarudishwa Arafah, basi Mwenyezi Mungu Mtukufu akaeleza kwamba "Hakika tofauti imeondoka katika Hijja" na Mwenyezi Mungu akaieleza "An-Nasii" kuwa ni kuzidi katika kufru,

1. Tafsir at-Tabari, Juz. 2, uk. 162.
2. Tafsir al-Kash-Shaaf, Juz. 1, uk. 264.

inawapotosha waliokufuru wanahalalisha mwaka fulani na wanaiharamisha mwaka mwingine. Naam, Hijja ilirejea kwenye wakati wake na mahala pake katika Hijja ya kuaga, Mtume **[s.a.w.w]** alisema, "Bila shaka wakati umerejea kama ulivyokuwa siku iliyoumbwa mbingu na ardhi". Naye Qurtubi amesema maana yake ni kuwa, "Suala Ia Hijja limerejea kama lilivyokuwa, yaani limerejea kwenye siku yake na wakati wake".

Na amesema Mtume **[s.a.w.w]** alipohiji yakuwa "**Chukueni Ibada zenu kutoka kwangu**" akabainisha visimamo vya Hijja na mahala pake.[1] Basi kama tukikubali maana hii kauli ya Mwenyezi Mungu haitakuwa na mafungamano yoyote na maoni ya huyu khatibu al-Khayyat, kwani kauli hiyo haina maana ya katazo ili iwe Taklifu II-zami inayokusanya aina yoyote ya mjadala, isipokuwa hiyo ni jumla Khabariyah na hii khabari inaeleza mambo ya kimaumbile. Kwa hakika baada ya matendo ya Mtume **[s.a.w.w]** na kuweka kwake mipaka ya visimamo na Mash-Ari na kuithibitisha katika mwezi maalum, Hijja imekuwa kama jua la mchana, basi haiwezi kukurubiwa na shaka kuhusu wakati wake na mahali pake, basi maneno haya yana uhusiano gani wa kuharamisha mjadala na kuharamisha maandamano ya kisiasa hata kama tutasema kwamba maandamano ya kisiasa yanaingia katika maana ya mjadala. Amesema Ibn Jariri: Kauli zinazostaajabisha mno kwangu mimi kuhusu jambo hilo, iwapo litakuwa kama nilivyoeleza kwamba, kisomo cha atakayesoma, "Falaa Rafathun Wala Fusuqun Wala Jidala FilHaj" kwa kuitia Raf-u Rafathu na Fusuqu na kuzitia Tan-win zote hizo mbili, na kuitia Fataha jidala bila ya Tan-wini, kisomo ambacho ni cha watu wa Basra na watu wengi wa Maka akiwemo Abdallah bin Kathiri, na Ibn Amri bin Al-Ula.[2] Na bila shaka yamerufaishwa matamko mawili ya mwanzo na likanasibishwa la tatu kwa kuyachukulia yale matamko mawili ya mwanzo kwa maana ya makatazo, na ikawa kama kwamba pamesemwa kwa mkazo pasiwepo maneno machafu na wala matendo mabaya, na la tatu kwa maana ya kueleza kukanushwa kwa mjadala ikawa kama kwamba pamesemwa, hapana shaka wala kutofautiana katika Hijja, yaani ndani ya kipindi chake na mahali pake. Ya Tatu: Ni kauli iliyoteuliwa na wafasiri wengi, nayo ni kuichukua nafyi (kanusho) na kulipeleka kwenye makatazo, na lengo liwe ni kukataza mambo yote matatu, na katika kipindi hiki (ifanywapo namna hii) ndipo anapokanganyika mtoaji wa dalili, kwa kuwa dhahiri ya aya inakataza mjadala wowote ule ikiwa ni pamoja na maandamano ya kisiasa.

Lakini ni lazima kwa mtu anayetaka kupata ukweli atulizane kidogo ili yambainike mambo mawili:

1. Jidala, inagawika kwenye haramu, mubaha na mustahabbu sasa basi kilichokatazwa ni jidala (mjadala) wa aina yeyote au ni ule unaohusu sehemu ya kwanza (yaani mjadala ulio haramu) na kama mjadala huo utakuwa haramu katika nyakati zingine basi haipingiki kuwa ni haramu katika Hijja vile vile na inakuwa mkazo zaidi uharamu wake katika Hijja.

2. Bila shaka maandamano ya kisiasa na kutoa hotuba na kuwazindua Waislamu kutokana na kujisahau kwao, na kudhihirisha kujitenga na

1. Tafsir Qurtubi Juz. 2, uk. 410.
2. Tafsir Ibn Jariri Juz. 2, uk. 161.

maadui zao wa mashariki na magharibi, Je, hayo ni katika aina za "Jidala" na ndiyo milango yake au hayana kabisa mahusiano nayo? Hebu angalia ufafanuzi wa mambo mawili: Bila shaka makusudio ya "Jidala" Ni kubishana ambako ni lazima kuepukwa katika Hijja na kwingineko, lakini katika Hijja ndiyo muhimu zaidi kuepuka. Amesema Zamakhshari: "Wala Jidala, Yaani hapana mabishano na marafiki na watumishi wa wenye kuajiriwa, na imeamuriwa kujiepusha na ubishani na ni wajibu kujiepusha nao kwa hali yoyote ile, kwani katika Hijja ni kubaya nino (kubishana) kama vile kuvaa nguo ya hariri katika Sala na kujitingisha tingisha wakati wa kusoma Qur'an."[1].

Na amesema ndani ya Tafsir Al-Manaar kwamba, "Al-Jidalu, ni kubishana na kukhasimiana (kugombana) basi yote haya yaliyokatazwa yanakuwa ni mafunzo ya ulimi (namna ya kuzungumza) na ni wajibu kwa mtu anapokuwa katika ibada na mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, awe mwenye ukamilifu wa adabu na mazingira bora".[2] Al-Jas-Sas amesema: Al-Jidal ni Mabishano, na Ibn Abbas amesema, Al-Jidal ni kumjadili mwenzio mpaka ukamkasirisha, kisha akasema, hakika aliyehirimia amekatazwa kutukana na kubishana katika miezi ya Hijja na katika miezi mingine, na amekatazwa matendo mabaya japokuwa matendo hayo ni haramu hata kabla ya kuhirimia, basi Mwenyezi Mungu ameyataja uharamu wake wakati wa kuhirimia ili kuonyesha ubaya zaidi kutokana na utukufu wa Ih-ram, na hasa kwa kuwa kufanya maasi katika hali ya kuwa ndani ya Ih-ram kuna adhabu kubwa zaidi kuliko katika wakati mwingine.[3] Na kinachoweka bayana zaidi ni kule kuikutanisha "Jidala" na "Fusuqu" kwani kunaonyesha kuwa, mambo haya mawili yanatokana na asili moja ya jinsi moja, basi haifai kukusanya jidala kwa ujumla, (yaani) Jidala Mubaha au Mustahabu katika sheria. Na ndani ya sheria ya Kiislamu kuna aina za majadiliano mbayo ni Mubaha na zaidi ya hapo kuna ambayo ni mustahabbu na aya ile haihusiki nayo. Ama Jidala (majadiliano) ambayo ni Mubah miongoni mwake ni yale yaliyokuja katika kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema:

قَدْ سَمِعَ اللَّـهُ قَوْلَ الَّتِي تُجَادِلُكَ فِي زَوْجِهَا وَتَشْتَكِي إِلَى اللَّـهِ وَاللَّـهُ يَسْمَعُ تَحَاوُرَكُمَا ۚ إِنَّ اللَّـهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿١﴾

"Bila shaka Mwenyezi Mungu amekwisha sikia kauli ya mwanamke ambaye anajadiliana nawe kuhusu mumewe, na anashitakia mbele ya Mwenyezi Mungu" Qur'an, 58:1.

Lau litawafika jambo kama hili katika Hijja haliwezi kuwa haramu si kwa msemaji wala kwa msikilizaji. Kinachojulisha hapa ni kwamba, makusudio ya Jidala ni majadiliano na mabishano yaliyokatazwa ambayo ni lazima kujiepusha nayo, nao wameyafasiri majadiliano ndani ya aya hiyo kuwa ni mambo yote yasiyotokana na mjadala na ubishi uliokatazwa. Amesema Ar-Razi: "Wafasiri wametaja namna nyingi kuhusu mahali hapa:

1. Mjadala unaohofiwa kuleta matusi na kukadhibishana na kupeana sifa ya ujinga.

1. Al-Kashaafa Juz. 1, uk. 263.
2. AI-Manaar, Juz. 2, uk. 227-228.
3. Ah-kamul-Qur'an ya Al-Jasas, Juz. 1, uk. 308.

2. Amesema Muhammad bin Kaab Al-Quradhi, "Hakika Maquraish walikuwa wakikusanyika Mina na kuambizana, "Hijja yetu imetimia" Na wengine husema, "Sisi yetu ndiyo iliyotimia", Basi Mwenyezi Mungu akawakataza kufanya hivyo".

3. Malik amesema katika Muwatta, "Jidala katika Hijja, (maana yake) ni kwamba Maquraishi walikuwa wakifanya wuqufu kwenye Mash-Aril-Haram katika Muzd-alifa Mahala paitwapo Qaza na wengine hufanya wuquf Arafa, na walikuwa wakibishana hawa husema "Sisi ni sahihi zaidi" Na hawa nao husema "Sisi ndiyo sahihi zaidi", Mwenyezi Mungu akasema:

لِّكُلِّ أُمَّةٍ جَعَلْنَا مَنسَكًا هُمْ نَاسِكُوهُ فَلَا يُنَازِعُنَّكَ فِي الْأَمْرِ وَادْعُ إِلَىٰ رَبِّكَ إِنَّكَ لَعَلَىٰ هُدًى مُّسْتَقِيمٍ ﴿٦٧﴾ وَإِن جَادَلُوكَ فَقُلِ اللَّـهُ أَعْلَمُ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿٦٨﴾

"Kila umma tumeujalia ibada wanayoishika, basi wasishindane nawe katika jambo hili, walinganie watu kwa Mola wako, bila shaka wewe uko katika uongofu ulio sawa kabisa, na kama wakiendelea kukujadili basi waambie Mwenyezi Mungu anayajua yote mnayoyatenda". Qur'an, 22:67-68

Malik amesema haya ndiyo majadiliano (yaliyoharamishwa katika aya hii).

4. Amesema Qasim bin Muhammad "Majadiliano katika Hijja ni wengine kusema, "Hijja nileo" na wengine weseme, "Hijja ni kesho" na hiyo ni kwa kuwa walikuwa wameamrishwa kuweka hesabu ya miezi kwa kuonekana mwezi.

5. Amesema Al-Qaffaal: "Katazo linaingia kutokana na mambo ambayo walimjadili Mtume **[s.a.w.w]** alipowaamuru kubadilisha Hijja na kufanya Umra tamatui wakaona vibaya kufanya hivyo, na wakasema, Je, tutakwenda Mina hali yakuwa tupu zetu zinadondosha manii? Mtume **[s.a.w.w]** akasema, kama ningelijuwa mwanzoni kitu nilichoamuriwa sasa hivi nisingeleta pamoja nami wanyama wa kuchinja, na ningelifanya umra tamatui, basi baada yake wakuacha mjadala.

6. Amesema Abdur-Rahman bin Zaid: "Mabishano yao katika Hijja ni kwa sababu ya kuhitilafiana kwao kuhusu nani kati yao ambaye Hijja inafanana nmo na Hijja ya Nabii Ibrahim [a.s]?

7. Wao walikuwa wakitofautiana katika miaka, wakaambiwa hapana kujadiliana kuhusu wakati wa Hijja kwani nyakati zimerejea kama ilivyokuwa wakati wa Ibrahim [a.s]. Basi huu ni mkusanyiko wa yale waliyoyasema wafasiri katika mlango huu.[1] Mifano hii inajulisha kuwa makusidio ya majadiliano ndani ya aya hiyo, ni majadiliano yaliyokatazwa sawa yakiwa yamekatazwa katazo Ia kuharamisha au katazo la karaha. Na imekuja katika kitabu kiitwacho Al-Fiqhi Alal Madhahibil-Arbaa, kwamba "Ni haramu kutoka katika taa (kumtii) Mwenyezi Mungu tendo lolote la haramu japo litakuwa tendo hilo limeharamishwa mahala pasipokuwa pa Hijja, isipokuwa kunatiwa mkazo zaidi katika tendo hilo wakati wa Hijja, na ni haramu kugombana na marafiki na watumishi na mfano wa hao kutokana na kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema, "Yeyote atakayekusudia Hijja,

1. Tafsir ya Imam Fakhrur-Razi, Juz. 1, uk. 175.

basi asiseme maneno machafu, wala asitende matendo mabaya wala asijadiliane katika Hijja", na Jidala (maana yake) ni kukhasimiana.[1]

Na kwa msingi huu basi, majadiliano ambayo ni Mubah na kupingana bila ya kuzusha ghadhabu kwa mwingine ni kama majadiliano yaliyokuja katika kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema, "Bila shaka Mwenyezi Mungu ameisikia kauli ya mwanamke anayejadiliana nawe kuhusu mumewe na anashitakia kwa Mwenyezi Mungu". Majadiliano hayo yako nje ya mtiririko wa aya hiyo, na lau yule mwanamke anayeshitakia angekuwa katika hali ya Ihram na angelipeleka mashitaka yake kwa Mtume **[s.a.w.w]** na kutaka haki yake toka kwa mumewe, hiyo isingehesabiwa kuwa ni majadiliano haramu na kugombana kuliko kuchukiwa bali itahesabiwa kuwa huyu anafuta haki kwa njia iliyo sahihi.

Wafasiri wamesimulia kwamba, kuna mwanamke wa Kiansari ambaye baada ya mumewe kumfanyia dhihari alikwenda kwa Mtume **[s.a.w.w]** akasema, "Hakika mume wangu aliniowa nikiwa bado kijana tena najitosha kwa mali na jamaa, alipokwisha kula mali yangu na kuumaliza ujana wangu na jamaa zangu kutawanyika na umri wangu kuwa mkubwa amenifanyia dhihari...." Na mengine aliyoyataja. Ikiwa Jidala iliyo Mubaha iko nje ya aya hiyo basi mjadala ambao ni mustahabbu unayo haki zaidi kutoka kuliko hii, na kwa nini isiwe hivyo wakati Mwenyezi Mungu amemuamuru Mtume wake katika kitabu chake kufanya mjadala uliyo Mandub. Lau wakati wa Hijja yatatolewa Mas-ala ya Kifiq-hi au Akida au Tafsiri na kila mmoja akatowa Maoni yake na mwingine akamjadili kwa njia nzuri, basi haitakuwa haramu jambo hilo, bali litakuwa ni kutekeleza kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema:

ادْعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحِكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ ۖ وَجَادِلْهُم بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ ﴿١٢٥﴾

"Waite watu katika njia ya Mola wako kwa hekima na Mawaidha mema na ujadiliane nao kwa namna iliyo nzuri". Qur'an, 16:125

Na lau utatokea uchambuzi katika mahema ya Arafah kuhusu Mas-ala ya Kifiqhi au Akida kisha mmoja wa Waislamu akashika msimamo wake maalum na kutetea itikadi yake kwa dalili na hoja, bila ya kuonyesha uhasama au ubishi au jeuri, hapana shaka kwamba jambo hilo linafaa, na wala halitahesabiwa kuwa ni kuingia kwenye mjadala uliokatazwa na aya hiyo. Maelezo yote yaliyotangulia ndiyo msimamo ulivyo kwa Ahli-Sunna, ama kwa upande wa msimamo wa watu wa nyumba ya Mtume **[s.a.w.w]** ambao wako sambamba na Qur'an na ni wenza wa Qur'an kwa mujibu wa kauli ya Mtume **[s.a.w.w]**, wao wanafasiri "Jidala" iliyotajwa katika aya kuwa ni kauli ya mtu atakaposema La Wallah, Wallah (Nime....) Na (akasema) Balaa Wallah..... Ikiwa ataapa viapo vitatu vya kweli mfululizo basi huyo amefanya "Jidala" na anawajibika achinje, na akiapa kiapo kimoja cha uongo (Pia) atakuwa kafanya "Jidala" na anawajibika kuchinja.[2]

Basi uko wapi uharamu wa kuharamisha kila aina ya "Jidala" wanaoudai watu hawa? Na kilicho haramu kwa mujibu wa riwaya zao ni mabishano "Jidala" Maalum kama ulivyokwisha fahamu (hapo kabla). Hebu tukadirie kwamba aya inakusanya majadiliano ya aina zote, yale yaliyo haramishwa

1. Al-Fiq-Hu Alal-Madhahibil-Ar-Baa, Juz. 1, uk. 524.
2. Nurut-Thaqalain, Juz. 1, uk. 162, pia tazama vitabu vya hadithi k.m. Al-Wasail n.k.

katika wakati usio wa Hijja na yale ya Mubaha na Mandubu yote hata kama tutakubali hivyo basi makusudio ni mjadala baina ya Haji na Haji mwingine. Ama mjadala wa Haji na watu walioko katika haram (ya Maka), na ama yale maandamano yanayofanywa na Mahuhjaji wa Kiislamu na kutangaza kujitenga kwao na makafiri na kukemea matendo yao ya uadui kwa Waislamu na Uislamu, na (ama) kuwaita Waislamu kwenye umoja miongoni mwao ili kuzikabili hatari na ushindani, yote hayo asilani hakuna cho chote cha mabishano. Hapana chochote katika mkusanyiko huo isipokuwa ni (kuonyesha) umoja wa Waislamu na hapana yeyote miongoni mwa makafiri na wanafiki anayekabiliana nao (wakati huo kwenye Hijja) mpaka (Eti) isababishe kuzuka kwa majadiliano kati ya pande mbili hizo.

Hebu angalia, hivi je, inahesabiwa kuwa kitendo alichokifanya Imam Ali [a.s] alipowasomea makafiri aya zilizoko katika Surat Al-Baraat katika msimu wa Hijja kwa amri ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (kitendo hicho kinaitwa) kuwa ni majadiliano? "Jidala Fil-Hajj"? Au ni tangazo la Mwenyezi Mungu na Mtume wake kujitenga na makafiri na washirikina? Na iko wapi basi tofauti kati ya misimamo hii miwili? Bila shaka maandamano wanayoyafanya Waislamu wanaokwenda Kuhiji wakati wa Hijja kwa amri ya Imam Khomeni "Mwenyezi Mungu amrehemu" si kwa maana nyingine ila ni kutekeleza kwa vitendo na kuyathibitisha maelekezo yaliyokuja katika kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema:

أَشِدَّاءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحَمَاءُ بَيْنَهُمْ ﴿٢٩﴾

"(Waislamu) ni wakakamavu dhidi ya makafiri na ni wenye kuhurumiana wao kwa wao". Qur'an, 48:29

Naam, bila shaka watawala wa Suudiya ndiyo wanaoleta mazingira ya Jidala iliyokatazwa kwa kuwa wao ndiyo wanaowazuwiya Waislamu kutangaza chuki zao dhidi ya makafiri, na kuonyesha chuki zao kwa matendo yao maovu. Kuwa wanawazuia Waislamu wasitekeleze wajibu wao wa Kiislamu, na wanawalazimisha Waislamu wasiwahoji (watawala hao) na kuwajadili, basi watawala wa Suudiya ndiyo mjadala na ndiyo sababu ya jidala (mabishano). Basi Iau ingetolewa fursa ya Mahujaji wote wakaafikiana juu ya umuhimu wa kushirikiana katika maandamano haya yanayopinga matendo ya makafiri na uovu wa Walahidi, haitakuwepo tofauti miongoni mwa Mahujaji (kuhusu jambo hili) isipokuwa kile wanachokichochea watawala wa kizazi cha Suud. Mwisho tunamuuliza Khayyaat: Yeye anasema katika Khutba yake kuwa "Hijja ni mkutano wa kila mwaka ambao Waislamu hukusanyika kutoka sehemu mbali mbali". Basi ikiwa Hijja ni kama adaivyo yeye, Je, ni Mas-ala gani miongoni mwa Mas-ala yanayopasa kutolewa katika mkutano huu?

Je, inapasa kuzungumza maneno madogo madogo kama vile ukaraha wa kula kitunguu maji na kitunguu thaum kwa mtu atakaye kuingia msikitini au kuzungumzia kukosha nyayo na viatu kutokana na udongo na jasho kama ambavyo tumekuwa tukisikia mara nyingi (maneno hayo) toka kwa Makhatibu wa msikiti mtukufu wa Makka katika siku za Hijja na katika Sala za Jamaa, kama kwamba hakuna mambo mengine ya Kiislamu (yanayopaswa kuzungumzwa) isipokuwa haya. Utakapo kubainikia ewe msomaji ubatili wa yale aliyoyasema Khayyat, na pia ubatili wa ushahidi wake, bali kutokuwepo kwa maungamano ya aya (aliyoitowa) na Qadhiya

hii (ya maandamano kwenye Hijja) basi inapasa tuwe na msimamo wa pamoja juu ya (kuifahamu) falsafa (Hekima) ya Hijja ya kweli kwa namna ya uchambuzi kwa mujibu wa aya za Qur'an na hadithi tukufu na pia matukio ya kihistoria na sera za waliotangulia. Na sasa hebu tazama maelezo haya yafuatayo kwa ujumla.

19

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## NINI LENGO LA HIJJA?

Kwanza Hijja ni Ibada: Hapana shaka kwamba jambo la kwanza ambalo Hijja inalilenga na ndiyo makusudio muhimu ya ibada zake, ni kuzidisha kumuelekeza mja kwa Mwenyezi Mungu na kumfanya kuwa mnyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu na kuimarisha uhusiano kwake na kuiingiza kwa ndani zaidi imani katika moyo wake na kuithibitisha itikadi ndani ya dhamiri yake juu ya upweke wa Mwenyezi Mungu. Kwa kifupi tunaweza kusema kwamba lengo muhimu la Hijja ni ibada na ni kwa kuanzia kuhirimia kwa ajili ya umra na kutufu al-Kaaba tukufu kisha kuswali na kwenda baina ya Safa na Marwa na kupunguza nywele, na kisha Ihramu ya pili ni kwa ajili ya Hijja na kusimama Arafah na kwenda Muz-dalifa na kusimama hapo, kisha kwenda Mina na kulala usiku kadhaa na kupiga Jamarat, kisha kuchinja ngamia au (ng'ombe, mbuzi au kondoo) halafu kunyoa kisha kutufu aI-Kaaba Tukufu na kumalizia kufanya Saayi baina ya Safa na Marwa pamoja na kufanya yanayoambatana nayo miongoni mwa dua na dhikri na kujizuwiya na yaliyoharamisha yanayohusika nayo, yote haya ni kwa ajili ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hiyo ni ibada iliyo katika ubora wa aina yake, na ni kuonyesha utumwa (mbele ya Mwenyezi Mungu) katika daraja iliyo juu ya ibada. Na kwa hakika ni (kuonyesha) unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu katika namna zilizo bora mno.

Ni ibada inayoonyesha udhalili (wa waja) mbele ya Mwenyezi Mungu kwa undani wa aina yake. Hivyo basi Hijja ni ibada inayokusanya kila misingi inayodhihirisha utumwa (mbele ya Mwenyezi Mungu, na (pia inadhihirisha) kila aina za unyenyekevu na utii kwa Mola Mtukufu, (miongoni mwake) ni kutosheka na dunia na kuyapuuza ma-tamanio na kujitolea kwa mali na kudhalilika na kufanya dhikri, na Tah-lili na Tasbihi, Tahmidi na Takbira na kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika kumtii na kumuomba msaada na kutoka kwenye uzio wa mapendekezo ya kimaada na kujisahaulisha kwa muda (furaha ya) mali mtoto mke na jamaa kwa ajili ya kuitumikia dini ya Mwenyezi Mungu na kwa ajili yake Mwenyezi Mungu na kwa amri ya Mwenyezi Mungu na kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kufuata hukmu ya Mwenyezi Mungu, na kutekeleza matakwa ya Mwenyezi Mungu, na kuitikia wito wa Mwenyezi Mungu pekee asiye na mshirika. Bila shaka Hijja ni ibada, lakini je, lengo la Hijja linaishia kwenye matendo haya matukufu ya ibada tu? (au kuna zaidi)? Na Je, hivi Hijja ilifaradhishwa kwa Waislamu wote wanaume na wanawake, wazee na vijana na kila aina ya rangi (za watu) na jinsi (zao) ili watekeleze maamrisho yanayofungamana na uhusiano (wao) na Mola wao tu bila wajibu huu mtukufu (wa Hijja) kuwa na lengo la (maisha) ya kijamii na bila mafungamano yoyote na masuala ya maisha yao na mambo yao?

Na Je, hivi hata tendo dogo la kiibada ndani ya Uislamu huwa halina lengo la kijamli kiasi kwamba ibada hii kubwa ya Hijja ikose lengo hilo (la kijamii)? Na faradhi hii kubwa yenye vigawanyo na misingi mingi na yenye muundo wa kijamii kama swala ya Ijumaa (Iwe haina lengo lolote ndani

yake)? Bila shaka aya za Qur'an na Sunna tukufu na sera za waliotangulia na kauli za wanachuoni zote zinaungana (kutambulisha) kwamba lengo la Hijja haliishii na kukoma katika hali ya kuwa ni jambo la ibada peke yake na unyenyekevu auonyeshao mja katika maisha yake ya kijamii, (Bali) makusudio yake ndiyo makusudio ya ibada zingine miongoni mwa faradhi za Kiislamu kama vile Swala, Saumu, Zaka, Jihadi na nyinginezo ambazo hazihusiani tu na mambo ya kuabudu peke yake, bali zinajumuisha malengo ya Kijamii na mambo ya kisiasa katika maisha ya Waislamu (kuanzia) mmoja mmoja na (hadi kufikia ngazi ya) Taifa. Na jambo hili (kwa maana iliyoelezwa) linaungwa mkono na akili iliyosalimika na kutiwa nguvu na fikra sahihi. Bila shaka Uislamu ni dini yenye kuenea (kila upande) yaani ina muongozo wa kiibada, kisiasa, kiuchumi na kijamii, nayo iko kinyume na Uyahudi na Ukristo wa leo na kanuni zilizowekwa na watu, na haukuwa Uislamu ila ni mkusanyiko uliopangika wa itikadi na kauni na mafunzo yanayohusu kila upande wa maisha, bali ni kila sehemu ya dini hii ni mchanganyiko uliyowekwa kimahesabu kutokana na malengo mbali mbali na ni mpango uliowekwa kwa usawa kwa mtu mmoja mmoja, jamii, ibada, siasa, uchumi, afya, dunia na akhera.

Zaidi ya hayo ibada katika fikra ya dini hii, mipaka yake inatanuka mpaka inakusanya maisha yote na kuyaenea matendo yote ya watu kama yatatendwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, haikomei kwenye mambo ya ibada yaliyo mashuhuri kama vile Sala, Zaka na Hijja, bali inakusanya kila tendo ambalo kwalo kuna mafanikio ya maisha na kufaulu kwa watu. Na kwa ajili hii Mtume Mtukufu **[s.a.w.w]** amesema kumwambia Abu Dharri: "Uwe na nia njema kwa kila kitu (ukitendacho) hata katika usingizi"[1] Kwa hiyo basi, Hijja kama tunavyoibainisha kutoka katika Qur'an na Sunna na sera za waliotangulia, na kauli za wanachuoni wahakiki, (lengo lake) halikomei kwenye kuwa yenyewe ni msimu wa ibada kwa utambuzi uliozoeleka kwa watu wengi bali kwa upande mwingine ni mkutano wa kisiasa wa ulimwengu na ni mkusanyiko wa kijamii kwa jumla unaowapa Waislamu wanaokuja kutoka kila pande za miji fursa ya kufahamiana, kuzoweyana, kukutana na kunufaishana wao kwa wao na kubadilishana mambo yao na kutatua matatizo yao ya kisiasa, kiuchumi na kijamii wakiwa mahala pa amani na utukufu na upendo. Na haya ndiyo tunayotaka kuyaonyesha na kuyatolea ushahidi katika kurasa hizi chache pamoja na kuwa tunakiri ya kwamba Mas-ala haya (ya Hijja, na kuyasoma malengo ya Hijja ya kiibada na kisiasa na kijamii ni (somo) pana mno kuliko hili somo (tutakalolieleza) kwa ufupi. Kwa hiyo basi tunataraji kawa yatakayokuja katika mlango huu ni dalili tu siyo zaidi, na ni wajibu wa Waislamu wote na mahujaji kwa upande wao wajaribu kufahamu mafunzo zaidi katika nyanja hii, nayo ni kwa kuifanyia mazingatio faradhi hii na ibada zake na kuzitilia maanani aya za Qur'an na hadithi Tukufu katika njia hii.

## MAKUSUDIO YA HIJJA KIJAMII NA KISIASA NDANI YA QUR'AN

1. Madinatul-Balagha Fi Khutabin-Nabi Wa Kutubihi Wamawaidhihi, Juz. 1, uk. 469.

Qur'an Tukufu imeitaja Hijja mahala pengi ya kuwa ndani yake mna mambo yenye manufaa kwa watu na inayo maslaha yao, pale Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema:

وَأَذِّن فِي النَّاسِ بِالْحَجِّ يَأْتُوكَ رِجَالًا وَعَلَىٰ كُلِّ ضَامِرٍ يَأْتِينَ مِن كُلِّ فَجٍّ عَمِيقٍ ﴿٢٧﴾ لِّيَشْهَدُوا
مَنَافِعَ لَهُمْ وَيَذْكُرُوا اسْمَ اللَّـهِ فِي أَيَّامٍ مَّعْلُومَاتٍ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُم مِّن بَهِيمَةِ الْأَنْعَامِ فَكُلُوا مِنْهَا
وَأَطْعِمُوا الْبَائِسَ الْفَقِيرَ ﴿٢٨﴾ ثُمَّ لْيَقْضُوا تَفَثَهُمْ وَلْيُوفُوا نُذُورَهُمْ وَلْيَطَّوَّفُوا بِالْبَيْتِ الْعَتِيقِ ﴿٢٩﴾
ذَٰلِكَ وَمَن يُعَظِّمْ حُرُمَاتِ اللَّـهِ فَهُوَ خَيْرٌ لَّهُ عِندَ رَبِّهِ وَأُحِلَّتْ لَكُمُ الْأَنْعَامُ إِلَّا مَا يُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ
فَاجْتَنِبُوا الرِّجْسَ مِنَ الْأَوْثَانِ وَاجْتَنِبُوا قَوْلَ الزُّورِ ﴿٣٠﴾ حُنَفَاءَ لِلَّـهِ غَيْرَ مُشْرِكِينَ بِهِ وَمَن يُشْرِكْ
بِاللَّـهِ فَكَأَنَّمَا خَرَّ مِنَ السَّمَاءِ فَتَخْطَفُهُ الطَّيْرُ أَوْ تَهْوِي بِهِ الرِّيحُ فِي مَكَانٍ سَحِيقٍ ﴿٣١﴾ ذَٰلِكَ وَمَن
يُعَظِّمْ شَعَائِرَ اللَّـهِ فَإِنَّهَا مِن تَقْوَى الْقُلُوبِ ﴿٣٢﴾ لَكُمْ فِيهَا مَنَافِعُ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ثُمَّ مَحِلُّهَا إِلَى
الْبَيْتِ الْعَتِيقِ ﴿٣٣﴾

"Watangazie watu habari ya Hijja, watakujia watu kwa miguu na (wengine) wakiwa juu ya mnyama aliyekonda kutokana na machovu ya njiani, wakija kutoka njia ya mbali, ili washuhudie manufaa yao na kulitaja jina Ia Mwenyezi Mungu katika siku zinazojulikana - Juu ya yale aliyowaruzuku, nao ni wanyama wenye miguu minne, na kuleni katika wanyama hao na mumlishe mwenye shida aliye fakiri. Kisha wajisafishe taka zao na watimize nadhiri zao na waizunguke nyumba ya kale (Al-Kaaba). Namna hii iwe, na anayevitukuza vitu vitakatifu vya Mwenyezi Mungu basi (kufanya) hivyo ni kheri yake Mwenyewe mbele ya Mola wake, na mumehalalishiwa wanyama isipokuwa wale mnaosomewa humu (katika Qur'an kuwa wasiliwe), basi jiepusheni na uchafu wa masanamu na jiepusheni na usemi wa uongo, Mkhalisike kwa Mwenyezi Mungu bila kumshirikisha na anayemshirikisha Mwenyezi Mungu ni kama kwamba ameporomoka kutoka mbinguni, kisha ndege wakamnyakua au upepo kumtupa mbali. Namna hivi, yeyote anayeziheshimu alama za (Dini ya) Mwenyezi, basi hilo ni jambo katika utawa wa nyoyo. Katika (wanyama) mnaowapeleka Makka kuchinjwa) mnayo (ruhusa kutumia) manufaa (yake) mpaka muda maalumu, kisha mahala pa kuchinjwa kwake ni (karibu na) ile nyumba kongwe". Qur'an, 22:27-33.

Kuna mambo matatu ya kuzingatia ndani ya aya ya pili miongoni mwa aya hizi: Kwanza: Manufaa yamewekwa upande wa kumtaja Mwenyezi Mungu na ndani yake inafahamisha kwamba Hijja inayo malengo mawili: Moja wapo ni la Kiibada na linachukua nafasi ya kumtaja Mwenyezi Mungu, lengo jingine siyo Ia kiibada kwa maana iliyozoweleka nalo linachukua mahala pa manufaa. Pili: Kuyatanguliza manufaa juu ya kumtaja Mwenyezi Mungu jambo linaloshika nafasi ya kiibada. Tatu: Kuyafanya manufaa yasiwe na ufupisho uliofungika bali yawe yenye kuingia katika nyanja nyingi, kwani Mwenyezi Mungu hakusema kuwa ni manufaa ya kiuchumi tu peke yake, jambo ambalo linafahamisha kwamba manufaa haya yanakusanya manufaa ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na mengineyo. Amesema Al-Mar-hum Al-Imam Sheikh Muhammad Shaltut ambaye alikuwa Sheikh wa Chuo Kikuu cha Az-Har, kuhusu tafsiri ya aya hii kama

ifuatavyo: "Manufaa ambayo Hijja imefanywa kuwa ndiyo njia ya kuyashuhudia na kuyapata - nayo ndiyo yaliyotajwa mwanzo kuhusu hekima za Hijja, ni manufaa ya ujumla bila ya sharti, hayakufungiwa kwa aina moja pasina aina nyingine, wala upande mmoja bila upande mwingine, nayo kwa ujumla wake yanakusanya kila kinachomnufaisha mtu mmoja na jamii na kutengeneza mambo yao, kwani kuitakasa nafsi na kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu ni manufaa na kushauriana kuweka mipango ya Elimu na Taaluma na kuungana kuimarisha Da'awa na kufanya juhudi kuutangaza Uislamu na hukmu zake bora ni manufaa, na kuandaa mikakati ili kuimarisha heshima ya Uislamu kutokana na ukandamizaji na unyonge ni manufaa, na hali kama hii manufaa yake ni mengi na yana aina nyingi kutegemeana na hali zinavyolazimu na nyakati zinavyotambulisha na mitazamo kati ya watu na watu"[1]

Na amesema tena: "Nayo Hijja kwa kuzingatia utukufu wake ndani ya Uislamu na lengo lake lililokusudiwa kwa mtu binafsi na jamii, bila shaka wanaikubali watu wa elimu na watu wanaohusika na mafunzo na taalauma pia wanaohusika na uendeshaji wa mambo na idara na wale wanaohusika na mali na uchumi na watu wa sheria na dini na wale wanaohusika na mambo ya vita na jihadi. Ukweli ni kwamba (ilipasa) wakaishuhudia watu wa aina mbali mbali wenye fikra na watatuzi wa matatizo (tofauti tofauti ya kijamii n.k.), wachunguzi na wenye juhudi (ya kutafuta amani) na wenye imani ya kweli na malengo ya kisiasa ambayo Waislamu wanawajibika kuyakusudia (yawe ni msimamo wao) katika maisha yao, inafaa waielekee Hijja watu wote hawa na Makka iko tayari kuwapokea na kuwaunganisha kwenye neno la Mwenyezi Mungu pembezoni mwa nyumba ya Mwenyezi Mungu, utawaona wakitambuana (kufahamiana huyu katoka wapi na ninani anafanya nini huko aliko) na wanashauriana na kusaidiana, hatimaye hurejea makwao hali ya kuwa ni umma mmoja (kitu kimoja) na nyoyo zilizoshikamana na mawazo na fikra za aina moja".[2]

Kwa hiyo ukweli ulivyo ni kwamba, aya hizi za Hijja zinaendelea mpaka zinamalizika na kuungana na kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

إِنَّ اللَّـهَ يُدَافِعُ عَنِ الَّذِينَ آمَنُوا ۗ إِنَّ اللَّـهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ خَوَّانٍ كَفُورٍ ﴿٣٨﴾ أُذِنَ لِلَّذِينَ يُقَاتَلُونَ بِأَنَّهُمْ ظُلِمُوا ۚ وَإِنَّ اللَّـهَ عَلَىٰ نَصْرِهِمْ لَقَدِيرٌ ﴿٣٩﴾ الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِن دِيَارِهِم بِغَيْرِ حَقٍّ إِلَّا أَن يَقُولُوا رَبُّنَا اللَّـهُ ۗ وَلَوْلَا دَفْعُ اللَّـهِ النَّاسَ بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لَّهُدِّمَتْ صَوَامِعُ وَبِيَعٌ وَصَلَوَاتٌ وَمَسَاجِدُ يُذْكَرُ فِيهَا اسْمُ اللَّـهِ كَثِيرًا ۗ وَلَيَنصُرَنَّ اللَّـهُ مَن يَنصُرُهُ ۗ إِنَّ اللَّـهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٤٠﴾

"Bila shaka Mwenyezi Mungu huwakinga wale walioamini, kwa hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila haini asiyeshukuru, wameruhusiwa (kupingana) wale wanaopigwa hiyo ni kwa sababu wamedhulumiwa, na kwa yakini Mwenyezi Mungu ni muweza wa kuwasaidia wale waliotolewa majumbani mwao pasipo haki ila kwa sababu wamesema kuwa, Mwenyezi Mungu ndiye Mola wetu, na kama Mwenyezi Mungu asingeliwakinga watu baadhi yao kwa wengine, bila shaka yangelivunjwa mahekalu na makanisa na nyumba nyingine za ibada na misikiti ambamo jina la Mwenyezi Mungu

1. Tafsir Tabari, Juz. 17, uk. 108.
2. Tafsir Tabari, Juz. 7, uk. 49.

hutajwa kwa wingi, na bila shaka Mwenyezi Mungu humsaidia yule anayesaidia Dini yake, hakika Mwenyezi Mungu nimwenye nguvu na ni mwenye kushinda". Qur'an, 22:38-40.

Mtiririko huu haukuja kwa bahati tu bila kutegemea, haiwezekani kwa aya za Qur'an zipangike kwa mpangilio huu bila ya kuwepo mahusiano baina yake. Bila shaka mshikamano na mfumo wa namna ya aya hizi zilivyokuja kwa aina hii, kunaonyesha kuwepo maungamano yenye nguvu kati ya Hijja na matendo ya kisiasa.

Nasi hatukusudii kusema kuwa Hijja igeuke na kuwa uwanja wa mapigano, lakini kinachofahamika ndani ya mtiririko huo ni kuwa Hijja iwe ni hatua ya maandalizi ya mwelekeo (huo). Kwa hakika kinachowezekana kukipata na kufaidika nacho katika mtiririko huu ambao umekusanya baina ya aya zinazohusu Hijja na Jihadi na kupinga dhulma, na kuwemo msaada wa Mwenyezi Mungu kwa wanaodhulumiwa inajulisha kwamba Hijja ni mahala bora pa Waislamu kujiandaa kiroho na kinafsi kukabilina na dhulma na wanaodhulumu, na kupinga ukandamizaji na wakandamizaji na pia kupinga ukoloni na wakoloni. Bila shaka Hijja ni fursa nuzuri kwa Waislamu wanaokusanyika huko kutoka miji mbali mbali, kuonyesha nguvu waliyonayo na umoja wao, na watangaze msimamo wao wa umoja kisiasa na wawatamkie maadui mafunzo ambayo hawatayasahau pamoja nakuwa tendo hili haliishii kwenye Hijja tu kwani upinzani dhidi ya dhulma na wanaodhulumu na kutangaza chuki zao dhidi ya maadui wa Mwenyezi Mungu ni jambo ambalo halina mipaka ya nyakati wala mahali. Ndiyo maana wafasiri wametafsiri "Manufaa" kuwa ni mambo yanayojumlisha mambo ya dunia na dini.

lbn Jaririt-Tabari, baada ya kunakili kwake kauli nyingi kuhusu tafsiri ya "manufaa" ameandika kama ifuatavyo: "Na kauli bora miongoni mwa kauli iliyo sawa, ni kauli ya yule aliyesema: Akikusudia hilo (yaani) "Ili washuhudie manufaa yao" ni miongoni mwa matendo anayoyaridhia Mwenyezi Mungu na biashara, na hiyo ni kwamba Mwenyezi Mungu ameyajumlisha manufaa yao yote yanayoshuhudiwa na kipindi cha Hijja na huiletea Makka katika siku za msimu huo manufaa ya dunia na akhera na hakuhusisha kitu fulani miongoni mwa manufaa yao kwa kupitia riwaya yoyote au akili, basi manufaa hayo ni ya jumla."[1] Kisha Qur'an imeieleza AI-Kaaba Tukufu kuwa imefanywa iwe ni Qiyam (Kisimamo) kwa ajili ya watu pale iliposema:

﴿جَعَلَ اللَّـهُ الْكَعْبَةَ الْبَيْتَ الْحَرَامَ قِيَامًا لِّلنَّاسِ ﴿٩٧﴾

"Mwenyezi Mungu ameifanya Al-Kaaba nyumbaTukufu kuwa ni kisimamo kwa ajili ya watu. Qur'an, 5:97.

Na ndani ya Qur'an tamko "Qiyam" limekuja kuhusu mahali pale pale Mwenyezi Mungu anaposema:

﴿وَلَا تُؤْتُوا السُّفَهَاءَ أَمْوَالَكُمُ الَّتِي جَعَلَ اللَّـهُ لَكُمْ قِيَامًا ﴿٥﴾

"Wala musiwape wapumbavu mali zenu ambazo Mwenyezi Mungu amezijaalia kuwa ni Qiyam kwenu. Qur'an, 4:5.

1. Tafsir Tabari, Juz. 17, uk. 108.

Na hii inafahamisha namna ya kufanana baina ya Hijja na mali, kama ambavyo uchumi na mali vinaendesha maisha ya watu na kulinda maslahi ya umma na Kiislamu. Basi hivyo hivyo Hijja nayo ndivyo ilivyo, na hii ikiwa na maana kwamba mkusanyiko wa mambo yaliyomo ndani ya Hijja hauishii kwenye ibada na kuabudu peke yake na kuneynyekea tu, bali unayo nafasi pana kiasi cha kujumlisha kila kitu chenye mafungamano na maslahi ya Waislamu miongoni mwa mambo yanayoendesha maisha yao na mazingira yao. Na kitu chochote kinachoendesha maisha yao (kitu hicho) ni bora kuliko matendo ya kisiasa ambayo yanalengo Ia kupinga ukoloni na utumwa na kunyonywa na kuthibitisha uhuru wao katika kila nyanja, na kuwazindua Waislamu kutokana na kuendelea kwa mambo yanayowazunguka ikiwemo njama na vitimbi na hatimaye kuwaelekeza kushika msimamo mmoja na kumpiga adui na kumzuia. Kisha ikiwa haifai kuwapa mali watu wapumbavu ambao hawajui jinsi ya kuitumia kwa kukosa kwao kuwa na upeo wa maarifa au upungufu wa akili zao, basi haifai kabisa kwa njia ambayo inastahiki mno kuachwa Hijja ikawa mikononi mwa watu wasiotambua utukufu wake na uzito wake na umuhimu wake katika maisha ya umma wa Kiislamu.

Hebu tazama waliyoyasema baadhi ya wafasiri kuhusu aya hii: Amesema Ibn Jaririt-Tabari: Mwenyezi Mungu anasema: "Mwenyezi Mungu ameifanya Al-Kaaba nyumbaTukufu kuwa ni yenye kuwatengenezea mambo yao watu ambao hawana cha kuwatengenezea mambo yao kutokana na kiongozi ambaye anamzuwia mwenye nguvu dhidi ya mnyonge na muovu miongoni mwao dhidi ya mwema na dhalim dhidi ya anayedhulumiwa na akaifanya kuwa ndiyo utambulisho wa dini yao na maslahi ya mambo yao.[1] Na ndani ya Tafsirul-Manar amesema kama ifuatavyo: "Bila shaka (Mwenyezi Mungu) ameifanya Kaaba kuwa ni kisimamo kwa watu kuhusu mambo ya dini yao na ni yenye kurekebisha nyendo zao, na ni yenye kuzitakasa nafsi zao kwa yale aliyoyafaradhisha kwao katika Hijja, ambayo ni miongoni mwa nguzo kubwa za dini, kwani hiyo ni ibada ya kiroho na kimali na kijamii".

Na amesema tena: "Hakika uwekaji wa Mwenyezi Mungu wa mambo haya (Yaani Ibada za Hijja) ni kuweka kulikohusisha maumbile na sheria kwa pamoja na uwekaji huu unajumlisha kusimamia na kuyathibitisha maslahi ya dini yao na dunia yao".[2] Na lau tutayafumbia macho yote hayo basi Je, ni kweli itawezekana kuifumbia macho sura ya Bara'ah ambayo inatangaza wazi msimamo wa kisiasa kuwahusu washirikina, ilishuka (Sura hii) ili isomwe ndani ya siku za Hijja nalo ni tendo la kisiasa bila ya shaka yoyote. Basi hebu na tuisikilize Qur'an Tukufu inasema:

بَرَاءَةٌ مِّنَ اللَّـهِ وَرَسُولِهِ إِلَى الَّذِينَ عَاهَدتُّم مِّنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١﴾ فَسِيحُوا فِي الْأَرْضِ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ
وَاعْلَمُوا أَنَّكُمْ غَيْرُ مُعْجِزِي اللَّـهِ وَأَنَّ اللَّـهَ مُخْزِي الْكَافِرِينَ ﴿٢﴾ وَأَذَانٌ مِّنَ اللَّـهِ وَرَسُولِهِ إِلَى
النَّاسِ يَوْمَ الْحَجِّ الْأَكْبَرِ أَنَّ اللَّـهَ بَرِيءٌ مِّنَ الْمُشْرِكِينَ وَرَسُولُهُ فَإِن تُبْتُمْ فَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَإِن
تَوَلَّيْتُمْ فَاعْلَمُوا أَنَّكُمْ غَيْرُ مُعْجِزِي اللَّـهِ وَبَشِّرِ الَّذِينَ كَفَرُوا بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٣﴾

1. Tafsir Tabari, Juz. 7, uk. 49.
2. Tafsir-ul-Manar cha Sayyid Rashid Rida, Juz. 7, uk 119.

"(Hili ni) tangazo la kujitoa katika dhima, litokalo kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kwa wale mlioahidiana nao miongoni mwa washirikina (Makafiri) - (waambieni) basi tembeeni katika nchi kwa miezi minne na mtambue kwamba ninyi hamuwezi kumshinda Mwenyezi Mungu, na kwamba Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuwadhalilisha makafiri. Na ni tangazo litokalo kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwenda kwa watu kuwajulisha siku ya Hijja kubwa kwamba, Mwenyezi Mungu yu mbali na washirikina na pia Mtume wake (yu mbali nao) basi kama mkitubu ndiyo kheri kwenu na mkikengeuka basi jueni kwamba ninyi hamuwezi kumshinda Mwenyezi Mungu, na wapashe waliokufuru habari ya adhabu iumizayo: Qur'an, 9:1-3. Na zinazofuatia.

Na Mtume Mtukufu **[s.a.w.w]** alimuamrisha Imam Ali [a.s] alifikishe onyo hili na tangazo hili kwa washirikina ndani ya siku za Hijja, basi Imam Ali akafanya hivyo na liii ni kwa ushahidi wa wana tafsiri wote na wanahistoria na wanahadithi wote. Ndani ya tafsiri ya Tabari kuna hadithi yenye Isnad kama ifuatavyo: "Ilipofika siku ya kuchinja (siku ya kumi mfunguo Tatu) Ali bin Abi Talib (r.a) alisimama akawatangazia watu kile alichoamuriwa na Mtume na Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** akasema: "Enyi watu nimeamuriwa mambo manne:

(1) Asiikurubie nyumba hii baada ya mwaka huu mshirikina yeyote.

(2) Na wala asitufu uchi yeyote.

(3) Na haitaingia peponi isipokuwa nafsi iliyosilimu.

(4) Na atimize ahadi yake kila aliye na ahadi. Katika Riwaya nynigine imesema: "Na yeyote aliye na ahadi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** basi na aitimize kwa muda wake.[1] Na ukipenda unaweza kusema kwamba kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema: "(Hili ni) tangazo la kujitoa katika dhimma, litokalo kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa wale mlioahidiana nao miongoni mwa washirikina". Na kauli yake aliposema: "Na ni tangazo litokalo kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwenda kwa watu kuwajulisha siku ya Hijja kubwa kwamba Mwenyezi Mungu yu mbali na washirikina na pia Mtume wake (yu mbali nao)", bila shaka kujitenga kulikotajwa ndani ya aya hizi mbili hakuhusiani tu na washirikina wa Kiquraishi au washirikina wa Bara Arabu peke yao bali kujitenga kulikokusudiwa ndani ya aya hizo mbili ni tangazo la Kiungu linalokusanya washirikina wa ulimwengu mzima, waliokuwepo katika zama zake Mtume **[s.a.w.w]** na baada ya hao mpaka siku ya Kiyama.

Qur'an Tukufu inafunza umma wa Kiislamu na kufafanua daraja yao ya kidini na inawalazimisha kujibari (kujitenga) na washirikina wote katika zama zote, na kwa sababu hiyo lau wageni wa Mwenyezi Mungu wote watajibari kutokana na walahidi na washirikina wanao wakandamiza, basi watakuwa wametekeleza wajibu wao kwa pamoja. Na huenda ikafikiriwa kwamba, kujibari na kuwapinga (washirikina) kulikokuja katika aya hizi, kunahusika na zama aliyoishi Mtume **[s.a.w.w]** wala haikuvuka baada ya hapo, kwa hakika hiyo ni kauli isiyo na dalili, nayo ni mfano wakauli ya watu waovu ambao wanataka kuuhusisha ujumbe wa Mtume **[s.a.w.w]** na mwongozo wa Qur'an Tukufu katika zama maalum pasina zama zingine.

1. Tafsir Tabari, Juz. 10, uk. 47.

Nami sifikiri kwamba Muislamu aliye huru atakuwa na shaka kwamba, wakomunisti na wanaowaunga ni wabaya mno kuliko washirikina ambao ufunuo wa Mwenyezi Mungu umewajibisha kujitenga nao, kama ambavyo sifikirii mtu mwenye insafu atakuwa na shaka kwamba shetani mkubwa (Amerika) ni mbaya mno na ni mwenye madhara mno kuliko washirikina. Kama ambavyo imekuja ndani ya vitabu ya pande mbili (Sunni na Shia) kwamba Hisham Ibn Abdil-Malik alihiji katika zama za Ukhalifa wa Baba yake na akatufu, kisha akataka aibusu "Hajar-al-Aswad, "lakini hakuweza kutokana na msongamano (wa watu) basi akatengenezewa mimbar na akakaa juu yake, mara akaja Ali bin Husein [a.s] akiwa amevaa Ihram, akiwa ni mwenye uso mzuri kuliko watu wote na mwenye harufu nzuri na kwenye paji lake la uso kuna athari ya Sijda inaonekana kama koti la kondoo, akaanza kutufu Al-Kaaba na anapofika kwenye Hajar al-Aswad watu humpisha ili aibusu kwa kumheshimu na kumtukuza, basi jambo hilo likamchukiza Hisham, na mtu mmoja katika watu wa Sham akamuuliza Hisham "Ni nani mtu huyu ambaye watu wamemuheshimu kwa heshima hii na wamempisha kwenye Hajar al-Aswad?

Hisham akasema: "Simjui", Alijibu hivyo ili tu watu wa Shamu wasije wakampenda Imam Ali bin Husein. Basi Farazdaq aliyekuwepo hapo akasema: "Lakini mimi namjua". Yule mtu wa Shamu akamwambia "Ni nani huyu Ewe Abu Faras"? Farazdaq akasoma Qasida, nasi tunataja hapa sehemu ya beti zake. "Huyu ndiyo yule ambaye Makka inatambua sauti ya nyayo zake, nayo Al-Kaaba na nje ya Makka na Haramu ya Makka zote zinamtambua. Huyu ni mwana wa mmbora wa waja wa Mwenyezi Mungu wote. Huyu ndiye mcha Mungu mtakasifu mwenye tahara na ni bendera ya uongofu. Huyu ndiye ambaye mzazi wake ni Ahmad mteule, Mola wangu amsalie mpaka siku ya Qiyama". (Aliendelea) mpaka akasema: "Babu yake ni miongoni mwa Quraishi katika nasaba yake ni Muhammad kisha Ali ambaye ni bendera ya viongozi mashahidi wake ni vita vya Badri na pango la mlima wa Uhdi na vita vya Khandaq na wote walijulikana siku ya Fat-hi Makka, na Khaybar na Hunayn zinamshuhudia na siku ya Quraydha".[1] Namna hivi ndivyo mshairi huyu mkubwa wa Kiislamu anavyomkabili khalifa huyo mjeuri kwanjia ya kaswida hii ya kishujaa na anamuarifisha Imam wa haki kutoka katika kizazi cha mtume katika mkabala wenye changamoto la kisiasa.

Jambo ambalo linajulisha kwamba jambo hili ni sheria (kufanyika) katika msimu wa Hijja na kujuzu kwake ni kutokana na kutopingwa na Mwislamu yeyote siyo zama hizo wala baada ya hapo. Na kwa maneno mengine tunaweza kusema kwamba, mshairi huyo analazimika kufanya munadhara huo wa kisiasa wenye nguvu iii amtambulishe Imam mbele ya mkusanyiko wa Mahujaji waliofika kwenye nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu, kwa kumzingatia kuwa ndiyo mrithi wa haki wa kizazi cha mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]**, na tukio hili linatupatia dalili iliyo wazi kwamba, tendo la kisiasa katika msimu wa Hijja linazingatiwa kwa mujibu

---

1. Al-Alhani, Juz. 21, uk. 376, Chapa ya Beirut, na Manaqib ya Ibn Shah-Rashud, Juz. 4, uk. 169, na Qadhiya hii imenakiliwa katika vitabu vingi vya Tarikh na vya Adab, kwa mfano, "Al-Bayan Wat-Tabyin, na Al-Iqdu al-Farid na Matalibus-Suul na Tadh-Kiratul-Khawas, na Nurul-Absar.

wa kanuni na sheria, na hiyo ni kwa sababu hakuna kizuwizi au uharamu wa kutekeleza matendo kama haya, sawa sawa ni katika siku hizo, au miaka iliyofuatia siku hizo.

## MALENGO YA HIJJA YA KIJAMII NA KISIASA KATIKA SUNNAH

Kwa hakika Sunna na sera tukufu ya Mtume na kitu kingine kinachoashiria kwamba, Mtume **[s.a.w.w]** alifanya matendo ya kisiasa katika Hijja, na zaidi ya hapo kuna hadithi zinazofidisha kwamba Hijja ni aina ya jihadi pale Mtume **[s.a.w.w]** aliposema: "**Jihadi iliyo bora ni Hijja**".[1] Na kauli yake Mtume **[s.a.w.w]** isemayo: "**Hijja ni Jihadi**" Na pia kauli yake Mtume **[s.a.w.w]**: "**Hijja ni Jihadi ya kila mnyonge**" Hadithi hizi mbili za mwisho zinapatikana katika: Sunan lbn Majah: Al-Manasik, na Sunan an-Nasai: Al-Haj, Na Musnad ya Ahmad bin Hanbal. Na kauli yake Mtume **[s.a.w.w]** alipokuwa akiwajibu wanawake walipomtaka waende katika Jihadi akasema: "**Jihadi yenu ni Hijja**" Na katika baadhi ya hadithi Mtume **[s.a.w.w]** amelinganisha Hijja na Jihadi kinyume cha faradhi zingine hakuzilinganisha nayo, aliposema: "**Mwenye kupigana katika njia ya Mwenyezi Mungu na mwenye kuhiji na mwenye kufanya umra niwageni wa Mwenyezi Mungu aliowaita**".[2]

Na hadithi hii inaonyesha kupatikana kwa maungamano na wajihi wa kufanana katika athari na malengo baina ya faradhi hizi mbili na ukitaka unaweza kusema: "Hakika hadithi hii inaonyesha kwamba Hijja si mujaradi wa ibada kwa maana inayoelekeweka, bali ni tendo linalofanana na jihadi yaani ni ibada na ni tendo Ia kisiasa, basi Hijja ni msimu wa tendo la kisiasa kama ambavyo ni msimu wa ibada na unyenyekevu na kumuelekea Mwenyezi Mungu kwa kumuabudu." Kisha ni kwamba, sera inatusimulia kuwa Mtume Mtukufu **[s.a.w.w]** alihutubu mahala pawili (yaani) Arafah na Mina na akatangaza katika hotuba yake misimamo na hukumu muhimu za Kiislamu, za kiuchumi, kisiasa na za kijamii, hapa tunataja sehemu ya hotuba hiyo: Katika Sunan At-Tirmidhi: Imepokewa toka kwa Jabir ndani ya mlango wa Hijja ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** amesema: Ilipofika siku ya Tarwiyyah (siku ya nane ya mfunguo Tatu) na wakaelekea Mina na wakasoma Tal-Biya ya Hijja, Mtume **[s.a.w.w]** pia alikusudia na akasali Mina Adhuhuri na Alasiri na Magharibi, na I'sha na Asubuhi, kisha akakaa kidogo mpaka jua likachomoza na akaamuru khema lake lililotengenezwa kwa manyoya lisimikwe Namirah, Mtume akaenda mpaka Arafat akakuta hema lake limesimikwa, akateremka mpaka jua likapanda juu, akaamuru ngamia wake aletwe, na akaletwa basi akapanda mpaka akafika

Bat-Nul-Wadi na akawahutubia watu akasema:

1) Bila shaka Damu yenu na mali zenu ni vitu vyenye heshima juu yenu, kama ilivyo na heshima siku yenu hii ya leo katika mwezi wenu katika mji wenu huu.

2) Fahamuni ya kwamba kila kitu katika mambo ya kijahiliya kiko chini ya nyayo zangu hizi (yaani vimebatilishwa).

---

1. Bukhar: Jihad.
2. Sunan lbn Majah: Al-Manasik na Sunan An-Nasai: Al-Haj na Jihad.

3) Na Damu za wakati wa Jahiliyah zimeondolewa, na damu ya kwanza ninayoiondoa ni ya Rabia Ibn Al-Harith (Ibn Ammi ya Mtume, alikuwa amepelekwa kulelewa katika Bani Saad watu wa kabila la Huzail wakamuua)

4) Na riba ya Jahiliyah imeondolewa na riba ya kwanza ninayoindoa ni riba ya Abbas Ibn Abdil-Muttalib, hii imeondolewa yote.

5) Hakika kila Muislamu ni ndugu wa Muislamu na kwamba Waislamu wote ni ndugu, basi hakiwi halali chochote kwa mtu kutoka kwa nduguye isipokuwa kile alichompa kwa moyo safi.

6) Vitu vitatu moyo wa Muislamu usifanye hadaa juu ya vitu hivyo: Kufanya ikhlasi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu katika matendo, kuwa na moyo safi kwa Maimamu wa haki na kushikamana na jamaa ya waumini.

7) Katika Uislamu watu wote ni sawa, watu wote wanatokana na Adam na Hawa hapana ubora kwa Muarabu juu ya asiyekuwa Muarabu isipokuwa kwa kumcha Mwenyezi Mungu.

8) Bila shaka Muislamu nduguye ni Muislamu, asimdanganye nduguye wala asimfanyie khiyana wala asimtete wala damu yake haiwi halali kwake wala kitu chake chochote hakiwi halali kwake isipokuwa kwa radhi ya nafsi yake.

9) Msije mkarudia kuwa makafiri wenye kupotea baada yangu, baadhi yenu wasiwakandamize wengine.

10) Kwa hakika ninyi mutaulizwa, basi aliyepo na amfikishie asiyekuwepo.

Kisha Mtume **[s.a.w.w]** aliwashuhudisha mara tatu mambo aliyoyabalighisha, nao masahaba wakashuhudia kwake juu ya hayo.[1] Na bila shaka mapokezi sahihi yaliyopokelewa kutoka kwa Mtume **[s.a.w.w]** miongoni mwa dua na dhikri zinazohusu Hijja, mambo ambayo yameshikamana na maana za kisiasa pamoja na maana za Tauhidi. Ni ushahidi bora juu ya kuwa Hijja ni msimu unaonasibu (unaostahiki) kwa Waislamu kudhihirisha msimamo wao kwa maadui wa Mwenyezi Mungu na Uislamu na pindi tutakapofahamu kuwa ni mustahabu kuzikariri dua hizi wakati wa ibada kwa mfano dua ifuatayo: "Lailaha-illa-llah Wahdahu la Sharika Lahu Lahul Mulku Walahul-Hamdu Yuhyi Wayumitu Wahuwa Ala kulli shain Qadir." Lailah illa-llah Wahdahu Wahdahu Anjaza Waadahu Wanasara Abdahu Wahazamal-Ah-Zaba Wahdah.[2] Haya ni pamoja na ishara zinazopatika katika Manasikul Haj. Kila ibada iliyomo ndani ya ibada hizi inaashiria kwenye jambo la kijamii na kisiasa na kiakhlaq (Muenendo) zaidi ya kuwa kwake ni ibada na ni kutii japokuwa hatuwezi kujua kwa ukamilifu kila mama zilizomo katika Ibada hizi. Wanachuoni wengi wa Kiislamu na wanafikra wa Kiislamu wameyaashiria mambo yanayoelekezwa na ibada hizi, miongoni mwake yamo mambo ya kiroho, kiuchumi, kijamii na kisiasa, nasi tunamfupishia msomaji mtukufu ili kufanya mukhtasari.

---

1. Khutba hizi mbili tulizozichanganya hapa zimekuja ndani ya Sahihi Muslim katika hadithi inayozungumzia Hija ya Mtume na pia zimekuja ndani ya Sunan ya Abu Dawood na Sira ya Ibn Hisham na vitabu vinginevyo.

2. Bukhar: Umrah, na Muslim: Al-Hajj, na Dawuud: Al-Manasik, na At-Tirmidhi Al-Hajj na Ibn Majah: Al-Manasiki, na Al-Muwattaa cha Malik: Al-Hajj, na Musnad Ahmad.

Kwa hiyo kuna zaidi ya mambo ambayo yanajulisha kuwa Mtume **[s.a.w.w]** aliyachanganya matendo ya kiibada na matendo ya kisiasa katika Hijja. Ndani ya Bukhari, imepokewa kwa Said bin Jubair kutoka kwa Ibn Abbas amesema: "Pindi Mtume **[s.a.w.w]** alipofika katika mwaka aliopewa amani (mwaka wa saba Hijiriya) akasema, ongezeni mwendo (katika Saayi)". Mtume alifanya hivyo iii awaonyeshe washirikina nguvu za Waislamu. Ibn AI-Athir amesema ndani ya An-Nihayah, Mtume aliwaamuru Masahaba wake kuongeza mwendo katika Tawafu wakati wa umrah ya Qadhaa (mwaka wa saba Hijiriya) ili kuwaonyesha washirikina nguvu za Waislamu, kwa sababu washirikina walikuwa wakisema, "Limewadhoofisha joto la Madina" na ni sunna katika baadhi ya tawafu tu. Na pindi Uislamu ulipoimarika na kupata nguvu, Umar akasema, "Kuna haja gani sasa hivi kuongeza mwendo, yaani kutufu kwa aina ile, au kuacha wazi mabega, na Mwenyezi Mungu amekwisha yasawazisha mambo ya Waislamu na ameifukuza kufru na makafiri".

Ibn al-Athir amesema tena: "Muradi wa Umar kusema, Ramalani, maana yake ni tawafu pekee iliyosuniwa kwa ajili ya kuwaonyesha makafiri". Na hii inaashiria kuwa inajuzu kuziunganisha ibada za Hijja kwenye makusudio ya kisiasa na malengo yake ya Jihadi, kwa mfano kuwakhofisha maadui kama vile kuwaogopesha maadui na kupinga matendo yao na kuziangamiza njama zao na kuiumbua mipango yao. Kisha Je, hivi Mtume **[s.a.w.w]** kuzichagua Suratut-Tauhid "Qul-Huwallahu Ahad" na Suratul-Kafiruna katika Sala ya kutufu na kuzipendekeza zisomwe na muislamu anayehiji wakati kuna Sura nyingine na aya nyingine ambazo zinazo maana na malengo ya kiakhlaq na mafunzo zaidi na kushuhudia kwamba Hijja ni mkusanyiko wa Kiislamu wa ulimwengu na kwamba mkutano huu ni wakati mzuri wa kutangaza msimamo uliyo wazi dhidi ya nguvu za kufru na ubeberu kama ambavyo inajulisha hivyo (kwa mapokezi yasemayo) kwamba Umar Ibn Khattab pindi akipiga Takbira na kulibusu jiwe alikuwa akisema: "Bismillahi Wallahu Akbaru ala Mahadana, Lailaha illa llahu la Sharika lahu Amaantu Billahi Wakafartu Bittaghuti"[1]

Maana ya maneno hayo: "Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu ni Mkubwa juu ya aliyotuongoza, hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu asiye na mshirika, nimemuamini Mwenyezi Mungu na nimeyakufuru mataghuti". Kisha ni kwamba Imam Jaafar bin Muhammad As-Sadiq [a.s] amesema katika kubainisha falsafa ya Hijja kama ifuatavyo: "Bila shaka Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaumba viumbe si kwa ajili yoyote isipokuwa alitaka na akafanya, akawaumba mpaka ulipofika muda fulani akawaamuru na kuwakataza, kuhusu mambo ambayo yatakuwa ni miongoni mwa mambo ya utiifu katika dini na maslahi yao miongoni mwa mambo ya dunia yao, basi akafanya ndani yake mkusanyiko wa (watu) kutoka mashariki mpaka magharibi ili wafahamiane.... Na ili athari za mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** zitambulike na habari zake nazo zijulikane zisije zikasahaulika, na lau kila watu wangelitegemea miji yao na yaliyomo basi wangeangamia na miji

1. Tarikh Makkah, Juz. 1, uk. 339 chapa ya Makkatul-Mukarramah ya mwaka 1385 A.H.

ingeharibika na mapato na faida vingeanguka na khabari zingepotea na wasingefahamu chochote, basi hiyo ndiyo sababu (ya kuweko kwa) Hijja".[1]

Na vile vile imepokewa toka kwake Imam Jaafar As-Sadiq [a.s] amesema: "Hapana uwanja wowote unaopendwa mbele ya Mwenyezi Mungu kuliko Mas-aa (Mahala pa Saayi baina ya Safa na Marwa) kwani mahala hapo hudhalilika kila mwenye nguvu.[2]

## MALENGO YA HIJJA YA KISIASA NA YA KIJAMII KATIKA SERA YA SALAFU

Bila shaka historia inatusimulia kwamba Salafus-Salih hawakufupizika na matendo ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu na ibada tu katika Hijja, bali munasaba huu wa Hijja waliutumia kwa ajili ya matendo ya kisiasa kuwa ni sehemu ya asili katika faradhi hii na siyo kitu chenye kuzidi juu yake au kilicho nje yake. Basi huyu hapa Imam Husein Ibn Ali ambaye ni mjukuu wa Mtume **[s.a.w.w]** anatoa hoja cihidi ya mtawala jeuri miongoni mwa watawala wa zama zake hapo Mina katika kipindi cha Hijja. Hakika Imam [a.s] aliwakusanya Bani Hashim wanaume na wanawake na wafuasi wao wenye kuhiji na wale wasiohiji na Ansari ambao ni wafuasi wake na watu wa nyumba yake, kisha hakumwacha yeyote miongoni mwa Masahaba wa mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** na watoto wao na (Tabiina) na Maansari waliokuwa mashuhuri kwa uchamungu na ibada. Basi wakakusanyika hapo Mina zaidi ya watu elfu moja na wengi wao walikuwa Tabiina na watoto wa Masahaba, na Imam Husein [a.s] akatoka kwenye hema lake akasimama kuhutubia, akamhimidi Mwenyezi Mungu na akamtukuza kisha akasema: "Amma baad, kwa hakika ujeuri huu tumefanyiwa sisi jambo ambalo nyote munalijua, mumeliona, mumelishuhudia na limekufikieni, nami kwa hakika nataka kuwaulizeni vitu fulani basi iwapo nitakuwa mkweli nisadikisheni, na nikiwa muongo, basi nikadhibisheni, sikilizeni usemi wangu na mufiche kauli yangu kisha murudi kwenye miji yenu na makabila yenu, yeyote mutayemuamini na mukawa na imani naye mwiteni (mumjulishe) yale muyajuayo kwani mimi naogopa haki hii itafutwa na kutoweka na Mwenyezi Mungu ndiyo mwenye kutimiza nuru yake japokuwa makafiri watachukia.[3]

Basi Imam Husein [a.s] hakukiacha chochote alichokiteremsha Mwenyezi Mungu ndani ya Qur'an kuhusu Ahlul Bait ila alikisema..... Na alisema: "Nakuombeni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, mukirudi msimulieni yeyote munayemuamini". Kisha alishuka na watu wakatawanyika. Naye Uthmani lbn Affan anaiandikia miji yote ya Kilslamu zama za ukhalifa wake barua ambayo ndani yake alisema kama ifuatavyo: "Hakika mimi ninawalazimisha magavana wangu wanifikie katika kila msimu (wa Hijja) na kwa hakika umma umepewa madaraka ya kuamrisha mema na kukataza maovu, basi hapana chochote kitakachodaiwa dhidi yangu au dhidi ya magavana wangu ila nitampa anayestahiki, na sina mimi wala magavana wangu haki upande wa raia isipokuwa imeachwa kwao, na kwa hakika watu wa Madina wameniletea mashitaka kwamba kuna watu wanashutumu na kupiga

---

1. Biharul An-War, Juz. 99, uk. 33 imenakiliwa toka Ilalis-Sharaii ya Saduq.
2. Biharul-An-War, Juz. 99, uk. 49.
3. Al-Ihtijaj cha Attabrasi, uk. 19 na kitabu cha Sulaim Ibn Qays uk. 183.

(wenzao) basi yeyote mwenye kudai chochote katika hayo na aje kwenye msimu (wa Hijja) achukue haki yake ikiwa ni kutoka kwangu au kwa magavana wangu au msamehe kwa hakika Mwenyezi Mungu anawalipa wenye kusamehe.[1]

Bali hata wasiokuwa Waislamu walipata fursa ya kuaridhi mashtaka yao kwa Khalifa katika Hijja, basi Khalifa husimama kuwapatanisha ndani ya kipindi cha Hijja na siyo baada ya kipindi hicho, basi sote tunakijua kisa cha mtoto wa Kimisri aliyefanya mashindano na mtoto wa Amri bin Aas (gavana wa Misri) na yule Mmisri akashinda, mtoto wa Amri akampiga yule mtoto wa Kimisri, basi baba wa mtoto wa Kimisri akaeleza mashtaka yake kwa Umar, Umar akamchukulia kisasi katika msimu wa Hijja mbele ya macho na masikio ya maelfu ya mahujaji kisha akamwambia Liwali Amri lbn Al-Aas mbele ya ushuhuda wa mkusanyiko mkubwa: "Ewe Amri ni lini mumewafanya watu kuwa watumwa na hali ya kuwa mama zao waliwazaa wakiwa huru".[2] Na hapa inafaa tuashirie mambo aliyoyaandika mwandishi wa Kiislamu wa zama hizi muheshimiwa Dr. Yusuf Al-Qar-dhawi katika kitabu chake muhimu kuitwacho, 'Al-lbadatu-fil-Islam", kuhusu lengo hili.

"Makhalifa walitambua umuhimu wa msimu huu wa kiulimwengu, wakaufanya kuwa ndiyo nafasi ya kukutana baina yao na wanachi wanaokuja kutoka masafa ya mbali, na baina yao na magavana wao kutoka katika miji, basi yeyote miongoni mwa watu mwenye kudhulumiwa au mwenye mashitaka na ayalete kwa Khalifa mwenyewe bila ya wasita wowote wala kizuwizi, na huko wananchi wamkabili gavana mbele ya Khalifa bila ya woga wala kificho, basi hapo husaidiwa mnyonge na haki kupewa aliyedhulumiwa na haki kurejeshwa kwa mwenyewe hata kama haki hii ni ya gavana au Khalifa." Basi iwapo Hijja ni msimu wa kuibainisha dhulma na malalamiko yatendwayo na watawala na wasimamizi wa Kiislamu, je, haiwi ni bora zaidi kujulisha ndani yake malalamiko kwa wakoloni na wafuasi wao na watumishi wao na kuwasaidia Waislamu dhidi yao? Na Je, inajuzu kumlalamikia mtawala Muislamu anapovuka mipaka yake lakini haijuzu kumlalamikia mkoloni dhalimu mvamizi aliyetoka nje na hali yakuwa anafanya maovu na mauaji?.

1. AI-Ibadah Fil-Islam cha Dr. Qar-Dhawi.
2. Rejea tuliyoitaja hapo nyuma, na vile vile kitabu kiitwacho, "Madha khasira Al-Alam Al-Islami cha Abul-Aala Al-Maududi akinakili kutoka Tarikh ya Ibn Al-Jauzi.

20

# UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI

## MALENGO YA HIJJA YA KISIASA NA KIJAMII KATIKA KAULI ZA WANACHUONI

Kwa hakika wanachuoni na wanafikra wengi wa Kiislamu wameandika umuhimu wa Hijja kisiasa na kijamii na wakazingatia kuwa ni msimu bora na fursa nzuri kwa Waislamu kuonyesha nguvu yao, mshikamano wao, muamko wao na umoja wao kwa kauli na matendo na kwa dhahiri na hisia. Basi huyu hapa Al-Allamah Muhammad Farid Waj-di anaiandika ndani ya Dairatul-Maarif yake Maddah ya Hijja anasema: "Amma hekima ya kufaradhishwa Hijja kwa Waislamu, hakuna nafasi ya kueleza katika kitabu hiki, lakini kitu ambacho ni wazi kuhusu Hijja ni kwamba lau wenye mamlaka ndani ya Waislamu wangetaka kuitumia Hijja katika kuleta umoja wa Kiislamu basi wangefaulu. Kwani hukusanyika kwa mamilioni ya watu katika uwanja mmoja kutoka miji mbali mbali ya ulimwengu na kuzielekeza nyoyo zao na masikio yao mahala hapo penye kukhofisha kwa kila linalotolewa kwani huwajibisha kuwaathiri wote kwa roho moja na hasa watakapolinganiwa mambo ambayo ndani yake mna kheri zao, basi pindi wataporudi kwenye nchi zao na wakatawanyika kwenye miji yao watayatangaza mambo waliyojifunza kwa ndugu zao, na watakuwa kwao ni kama wajumbe wa mkutano mkuu uliohusisha jinsi zote na zama zote, ambapo wajumbe wake hukutana kila mwaka mara moja, basi ni athari iliyoje unayoikadiria kwa tukio hilo tukufu katika maisha ya umma huu mkubwa, na ni matokeo gani bora unayoyatarajia kutokana nalo pindi umma huu utakapozindukana kutoka katika usingizi wake. Basi Hijja itakuwa miongoni mwa nyenzo zake kubwa, na unafahamu ya kwamba mataifa ya nje yanayozikalia baadhi ya nchi za Kiislamu yanawazuia raia zake kufanya Hijja, kwani mabadiliko ya maisha lau yataenea (yataingia) ndani ya mataifa hayo. Hakuna chochote kitakachoweza kuyazuwia, na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye amri siku zote.[1]

Na imekuja ndani ya kitabu kiitwacho: "Ad-Dinu Wal-Hajj Alal-Madhahibil-Arba" kama ifuatavyo: "Hijja ni njia ya mafahamiano, mshikamano, usawa na kuimarisha mahusiano na ushirikiano na maungamano baina ya mataifa ya Kiislamu. Basi nyoyo zao hushikamana na tamko lao kuwa moja na kutenda kitu kitakachotengeneza hali yao na kurekebisha dosari katika mambo yao". Na ameandika ustadhi mtukufu Muhammad Mubarak ambaye ni mshauri katika chuo kikuu ya Mfalme Abdul-Aziz, amesema (katika maandiko yake): "Madhumuni ya Ibada peke yake bila kuunganisha na kitu chote iko wazi katika Hajji lakini kaiunganisha pamoja na maana nzuri ya kijamii, kwani Hijja ni mkutano wa ulimwengu (ambao) hukusanyika washiriki katika uwanja mmoja kwa ajili ya ibada ya Mungu mmoja. Pamoja na hayo ibada hii siyo kwamba imejitenga na maisha (ya kila siku) bali imeshikana nayo kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya kitabu chake kitukufu:

---

1. Rejea tuliyoitaja hapo nyuma, na vile vile kitabu kiitwacho, "Madha khasira Al-Alam Al-Islami cha Abul-Aala Al-Maududi akinakili kutoka Tarikh ya Ibn Al-Jauzi.

لِّيَشْهَدُوا مَنَافِعَ لَهُمْ وَيَذْكُرُوا اسْمَ اللَّـهِ فِي أَيَّامٍ مَّعْلُومَاتٍ ﴿٢٨﴾

"Ili washuhudie manufaa yao na kutaja jina la Mwenyezi Mungu katika siku maalum" (Qur'an, 22:28).

basi kushuhudia manufaa yao ni maana pana, inawezekana kukusanya maslahi mbali mbali ya Waislamu".

Kwa hiyo iwapo tendo la kisiasa linajuzu ndani ya Hijja, kama ulivyokwisha tambua kutokana na Qur'an na Sunna na sera ya Salaf na kauli za wanachuoni watukufu bali Hijja ni fursa inayofaa kuwakhofisha maadui na kuwatisha na kuzitokomeza njama zao, basi ni adui gani aliyedhidi yenu kuliko Amerika ambayo inafanya njama dhidi ya Uislamu na Waislamu siku zote na inapora mali zao na kuiba Petroli yao? Na Je, Ni adui gani aliye dhidi yetu kuliko Israel ambayo imepora ardhi yetu na kuwafukuza wananchi wetu na ikawaua na inaendelea kuwaua watoto wa Kipalestina na kuhalalisha mauaji yao na kuvunja utu wao?

Na ni adui yupi aliye dhidi yetu kuliko Urusi ambayo inayoufanyia uadui Uislamu na Waislamu katika itikadi na katika kila kitu na inaikalia ardhi yetu ndani ya Afghanistan na kuwaua vijana wake na kuibomoa miji yake na inaendelea (kufanya hayo)? Na Je, ni adui gani aliye dhidi yetu kuliko Uingereza ambayo imeunda dola ya Israel na ikafanya njama na inaendelea kufanya njama dhidi yetu kwa mujibu wa chuki za jadi za vita ya msalaba. Na ni adui gani aliye dhidi yetu kuliko Ufaransa ambayo imeua malaki ya wanachi wetu Waislamu katika Algeria, na bado inaendeleza mauaji na njama huku na huko katika miji ya Waislamu?

Na ni kwa nini tunatofautisha baina ya Marekani na Urusi na wote hao mila yao ni moja katika kuipinga dini yetu na kufanya njama mbaya dhidi yetu na kuyaua mataifa yetu na kupora utajiri wake? Na ni kwa nini tunaiacha fursa ya Hijja Tukufu na mkusanyiko wa pekee wa mamilioni (ya Waislamu), mkusanyiko ambao unakusanya nchi 40 za Kiislamu upotee bure bila ya kuutumia kuwaamsha Waislamu na kuwafanya wajitolee kupinga maovu ya (watu wa) magharibi na mashariki dhidi yetu. Na Je, hivi sisi tunazijua hukmu za Hijja zaidi kuliko Mtume **[s.a.w.w]** na Salaf wema waliokuja baada yake ambao katika Hijja walikuwa wakichanganya baina ya ibada na matendo ya kisiasa? Na ni kwa nini hatutoi nafasi katika Makka, Madina, Arafat, na Mina kwa Wapalestina, Philipine, Iraq, Iran, Afghanistan, Africa, Lebanon na Eritrea na kwingineko wanakodhulumiwa wabainishe dhuluma (wanazotendewa) na wawaamshe Waislamu juu ya yale wanayokabiliana nayo miongoni mwa dhulma na ukandamizaji na mauaji na jinai za kikoloni na wafuasi wao na watumishi wao?

Na ni kwa nini hatutoi fursa katika Hijja ili wanafikra wa Kiislamu kutoka kila nchi na sehemu zote wajadili matatizo ya Waislamu na watafiti ufumbuzi wa pamoja wa taabu wanazozipata toka kwa mabeberu? Kwa nini watawala wa Makka na Madina hawatoi nafasi kufanyika mikutano ya Jumuiya ili kuwajulisha Waislamu undani wa ukoloni wa Kimarekani, Kirusi, Kiingereza, na Kifaransa na malengo yao ya kishetani na wafahamishe matendo wanayotenda wavamizi hawa kutoka nje, ikiwa ni pamoja na kupora na kuiba na kuua na ukandamizaji. Mpaka lini Hijja itatengwa na athari zake za kijamii na kisiasa chini ya mapendekezo ya watu kutoka nje? Na ni mpaka lini idadi hii kubwa ya Waislamu kutoka kila

sehemu ya ulimwengu (itaendelea) kukusanyika kisha kutawanyika bila ya ndugu huyu kumtambua nduguye na bila ya ndugu huyu kuyajua matatizo na matarajio ya nduguye? Na ni hadi lini (Tutaendelea) kuipoteza fursa hii kubwa ambayo Uislamu umeiandaa kwa ajili ya umma huu?

Na iwapo Hijja itatupita (tukakosa kuitumia) basi ni wapi pengine itakapowezekana kuupata mkusanyiko huu mkubwa na idadi kubwa, na kongamano hili la waumini lililojiandaa kutenda na kuitika wito wowote wa Kiislamu unaowataka kupigana jihadi na kuwahimiza kuwa na muamko? Na ni vipi watawala wa Hijazi wanakubali waipoteze fursa hii kubwa na wanawazuia Waislamu kunufaika nayo kama alivyoamrisha Mwenyezi Mungu (Na washuhudie manufaa yao)? Bali ni vipi Waislamu wenyewe wanaruhusu kuiacha fursa ya Hijja ipotee bure bila ya kuitumikisha katika njia ya mambo yao yanayowahusu na kutatua matatizo yao?

## UCHAMBUZI WA MWISHO

Hapa zimebakia sehemu mbili muhimu za uchunguzi tutazionyesha katika sehemu hii ya mwisho, nazo ni kama ifuatavyo:

A). Kumlilia maiti kabla ya kuzika au baada ya kuzika.

B). Kudhifia tamko la "Abdi" kwa mja. Basi huenda mtu asiyejua hukmu za sheria akadhani kuwa, sheria zimeyaharamisha mambo hayo, na sasa hivi tunabainisha hukmu zake kwa mujibu wa kitabu (Qur'an) na sunnah na tunasema: Kwanza: Kumlilia maiti: Jicho na moyo havilaumiwi pindi mtu anaposimama juu ya kaburi la Mtume wake na Maimamu wa nyumba ya Mtume [a.s] na Masahaba wema (r.a) (Jicho halilaumiwi) kutoa machozi (na moyo) kuhuzunika, ili kuonyesha kilichomo ndani (ya nafsi) katika upendo, kutawalisha, mapenzi, huruma na shauku, na kwa hakika jambo hili linafuatana na maumbile ya kibinaadamu na wala sheria ya Mwenyezi Mungu hailipingi. Amma maumbile (yalivyo) ni kwamba: Huzuni na kuathirika hulazimiana na huruma ya kiutu pindi mtu anapojaribiwa kwa msiba wa mtu ampendaye miongoni mwa wapenzi wake au mtoto wake na ndugu zake, na yeyote asiyekuwa na hisia hii huhesabiwa kuwa ni wa pekee katika maumbile ya kiutu, na wala simuoni yeyote ulimwenguni anayekanusha ukweli huu kwa nguvu zake zote.

Ama Sheria: Inatosha (kulieleza) hilo kufuatia kilio cha Mtume Mtume **[s.a.w.w]** na Masahaba na watu waliowafuatia kwa wema kuwalilia maiti wao. Basi huyu hapa mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** anamlilia mwanawe mpenzi "Ibrahim" na anasema: "Jicho linatoa machozi na moyo unahuzunika, na wala hatusemi (chochote) isipokuwa kile anachokiridhia Mola wetu, nasi kwako Ewe Ibrahim ni wenye kuhuzunika:[1] Wanasira na wanahistoria wamepokea kwamba wakati Ibrahim mtoto wa Mtume alipokuwa katika 'Sakratul-maut' Mtume **[s.a.w.w]** alikuja akamkuta migunni mwa mama yake, akamchukua na kumweka miguuni mwake akasema: "Ewe Ibrahim hakika sisi hatuwezi kukutosheleza kitu kwa Mwenyezi Mungu". Kisha macho yake yakatiririka machozi na akasema: "Hakika sisi kwako wewe ni wenye kuhuzunika Ewe Ibrahim, jicho linalia na moyo unahuzunika na wala hatusemi kitakachomchukiza Mola, na lau lisingekuwa ni jambo la haki na ahadi ya kweli basi tungelikuhuzunikia

1. Abu Dawood, Juz. 3, uk. 58, Sunan Ibn Majah, Juz 1, uk. 482.

huzuni kubwa mno kuliko hii". Na pindi Abdur-Rahman bin Auf alipomwambia Mtume kwamba; "Je, Hukutukataza kulia"?

Mtume alijibu kwa kusema: "Hapana, lakini nilichokataza ni sauti mbili za ujinga na sauti mbili zingine: Sauti wakati wa msiba, na kilio cha kishetani na sauti ya ngoma, na kilio changu hiki ni huruma, na asiyekuwa na huruma hahurumiwi".[1] Na kilio hiki cha Mtume **[s.a.w.w]** hakikuwa ni cha kwanza na cha mwisho wakati akijaribiwa kwa misiba ya wapenzi wake, bali alikuwa akamlilia mwanawe "Tahir" na husema: "Jicho linatoa machozi, na machozi hayazuiliki, na moyo unahuzunika na wala hatumuasi Mwenyezi Mungu"[2] Na Al-Allama AI-Amini ndani ya kitabu chake kikubwa kiitwacho 'Al-Ghadir," amekusanya mahali pengi ambapo Mtume **[s.a.w.w]** na Masahaba na Tabiina waliwalilia maiti wao na wapenzi wao pindi walipofariki na hapa tunanakili ibara ya mwanachuoni huyu mtafiti: Huyu hapa Mtume **[s.a.w.w]** wakati Hamza (r.a) alipouawa, kisha Safiyah binti Abdil-Muttalib R.A akaja akimtafuta Hamza, Maansari wakamzuia, basi Mtume **[s.a.w.w]** akasema "mwacheni". Akakaa mbele yake, ikawa Safiyah anapolia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu naye hulia, na anapozidisha kulia kwa uchungu, Mtume **[s.a.w.w]** naye hulia kwa uchungu. Naye Bibi Fatmah alipokuwa akilia Mtume **[s.a.w.w]** naye hulia na kusema: "Sintapata msiba kama wako kamwe".[3]

Na pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliporudi toka Uhdi, wanawake wa Kiansari waliwalilia mashahidi wao, basi sauti zao zikamfikia Mtume **[s.a.w.w]** akasema: "**Lakini Hamza hana wakumlilia**" Basi Maansari wakarudi na wakawaambia wanawake wao "Msimlilie yeyote mpaka muanze kumlilia Hamza", basi desturi hiyo kwa Maansari imebakia mpaka leo hawamlili mtu ila kwanza humlilia Hamza.[4] Na huyu (tena) ni Mtume **[s.a.w.w]** anawapa watu wa Madina habari ya shahada ya Jaafar na Zaid bin Harith na Abdallah bin Ruwah na hali macho yake yanatiririka machozi.[5]

Na hapa Mtume **[s.a.w.w]** alilizuru kaburi la mama yake na akalia na akawaliza waliokuwa pamoja naye. Pia Mtume **[s.a.w.w]** anambusu Uthman bin Madh-un akiwa ni maiti na machozi yake (Mtume) yanatiririka usoni.[6] Vile vile Mtume **[s.a.w.w]** anamlilia mtoto wa mmoja wa mabinti zake na Ubbadah Ibn Samit akamwambia "Nini hiki Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?" Mtume Akasema: "Ni huruma aliyoiweke Mwenyezi Mungu ndani ya wanaadamu, na kwa hakika Mwenyezi Mungu anawahurumia wenye huruma miongoni mwa waja wake".[7] Naye Bibi mkweli aliyetakasika, (Fatmah binti Muhammad **[s.a.w.w]** anamlilia baba yake na anasema: "Ewe baba yangu uko karibu mno na Mola wako, Ewe baba yangu

---

1. Siratul-Halabiya, Juz. 3, uk. 348.
2. Maj-Mauz-Zawaid ya Al-Haithami, Juz. 3, uk. 8.
3. Imtau ya Al-Maqrizi, uk. 154.
4. Majmauz-Zawaid, Juz. 6, uk. 120.
5. Sahih Bukhar, Kitabul-Manaqib Fii Alaamatin-Nubuwwah Al- Islam. (2) Sunan Al-Bayhqi, Juz. 4, uk. 70.
6. Sunan Abi Dawood, Juz. 2, uk. 63, Suna Ibn Majah, Juz. 1, uk. 445.
7. Sunan Abi Dawood, Juz. 2, uk. 58, Sunan Ibn Majah, Juz. 1, uk. 481.

umemwitika Mola aliyekuita, Ewe baba yangu tunakuomboleza kwa Jibril, Ewe baba yangu makazi yako ni pepo ya Firdaus".[1]

Na vile vile Bibi Fatmah [a.s] alisimama kwenye kaburi tukufu Ia Baba yake na akachukua gao la udongo wa kaburi akauweka (karibu na macho) na akalia na kusoma shairi akasema: "Ana lawama gain mtu atakayenusa udongo wa kaburi la Ahmad **[s.a.w.w]** iwapo hatanusa ghaliya[2] milele. Nimefikwa na msiba ambayo lau ungeufika mchana ungegeuka na kuwa usiku. Na huyu hapa Abu Bakr Ibn Abi Qahafah anamlilia mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** na kumuomboleza kwa kusema: "Ewe Jicho lia usichoke, ni haki kumlilia Bwana". Na amesema tena: "Wanamlilia yule ambaye mbingu inamlilia na ni yule ambaye ardhi imemlilia na watu wamehuzunika mno". Na anasema: "Ewe Jicho lia kwa machozi mengi yanayotiririka, na usichoke kutoa machozi kila wakati na kulia". Naye Arwi binti Abdul-Muttalib anamlilia Mtume **[s.a.w.w]** na kumuomboleza kwa kusema: "Fahamu Ewe Jicho! Ole wako nipoze kwa machozi yako muda wote nitaobakia, na unipe ushujaa. Fahamu Ewe jicho, Ole wako jitokeze kwenye nuru ya miji na unipoze."

Na Atikah binti Abdul-Muttalib anamuomboleza Mtume **[s.a.w.w]** na anasema: "Enyi macho yangu! lieni sana siku zote na mutoe machozi, mtiririshe machozi bila udhuru. Ewe Jicho lia kwa machozi yasiyokatika. Ewe Jicho lia kwa machozi sana kwa ajili ya Mtume mwenye nuru aliyechaguliwa kuliko viumbe wengine wa Mwenyezi Mungu". Naye Safiyah binti Abdul-Muttalib, anamlilia Mtume na kumuomboleza kwa kusema: "Ewe Fatma lia pamoja na wenzako wala usichoke mpaka nyota zichomoze, Mtume ni mwenye kuliliwa na anastahiki kuliliwa, Yeye ndiye Mtukufu na Bwana aliye mzuri". Na pia anasema: "Enyi macho yangu lieni kwa machozi mfululizo. Enyi macho yangu lieni na mtiririshe machozi kwa huzuni nyingi". Na huyu hapa Hind bint Al-Harith Ibn Abdil-Muttalib anamlilia Mtume na anasema: "Ewe Jicho lia kwa machozi na uyatirirshe kama yanavyoshuka maji ya mvua yakatiririka". Na Hind binti Athatha anamuomboleza Mtume anasema: "Ewe Jicho lia usichoke kwa hakika nimepata khabari ya mauti ya yule umpendaye (Mtume **[s.a.w.w]**". Na huyu hapa Atika binti Zaid anamuomboleza Mtume na anasema: "Na sasa vipando vyake vinatingisha moyo na kwa hakika alikuwa akivipanda yule ambaye ni pambo lake. Na vipando hivyo vimekuwa vinamlilia Bwana wake na macho yake yanatiririsha machozi".

Naye Ummu Ayman anamuomboleza Mtume kwa kusema: "Ewe Jicho langu lia kwa sababu huzuni yangu itakuwa Shifaa, basi lia sana kwa machozi mengi mpaka ifike hukumu ya Mwenyezi Mungu ya kheri". Na huyu hapa Shangazi ya Jabir bin Abdallah alikuja siku ya Uhdi akimlilia nduguye Abdallah Ibn Amr, na Jabir amesema: "Nikawa nalia na watu wakawa wananikataza na mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** hanikatazi, basi mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema: "Lieni kwa ajili yake hata musipolia, Wallah Malaika hawakuacha kumfunika kwa mbawa

---

1. Sahih Bukhar, Babu Maradhin-Nabi Wawafatih Musnad Abi Dawood, Juz. 2, uk. 197. "Sunan An-Nasai, Juz. 4, uk. 13, Mustadrak Al-Hakim, Juz. 3, uk.163, Tarikh AI-Khatib, Juz. 6, uk. 262.
2. Al-Ghadir, Juz. 5, uk. 147.

zao mpaka mumemzika."[1] Naam, imepokewa toka kwa Umar lbn Khattab na Abdallah Ibn Umar kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** amesema: "Hakika mauti huadhibiwa kwa kilio cha watu wake". Mimi nasema: Dhahiri ya hadithi hii iko kinyume na matendo ya Khalifa (mwenyewe) aliyotenda mahala pengi palipothibitishwa na historia. Miongoni mwake ni kwamba, yeye alimlilia Nuuman Ibn Muqrin Al-Muzani pindi ilipomfikia habari ya kifo chake, basi akatoka akawajulisha watu akiwa juu ya mimbar na akaweka mkono wake juu ya kichwa chake akalia.[2] Na miongoni mwake ni kulia kwake yeye na Abu Bakr wakimlilia Saad Ibn Muan mpaka Aisha akasema: "Naapa kwa yule ambaye nafsi ya Muhammad iko mikononi mwake hakika mimi nilikuwa na tambua sauti ya kilio cha Abu Bakr na sauti ya kilio cha Umar, wakati mimi nikiwa chumbani mwangu."[3]

Na miongoni mwake ni kilio chake juu ya nduguye Zayd Ibn Khattab, na huyu (Zayd) alifuatana na mtu fulani katika Bani Adiy Ibn Kaab, basi yule mtu akarudi Madina na alipomuona macho yake yakatiririka machozi akasema: "Wewe umemuacha Zayd hali ya kuwa ni maiti nawe umekuja kwangu".[4] Basi kulia kwa Khalifa ambako kumekaririka kunatuongoza kwamba, makusudio ya hadithi hata kama Sanadi yake itasihi yana maana nyingine, itakuwaje (hali hii)? Na dhahiri ya hadithi lau tutaiamini inakwenda kinyume cha Qur'an, na hapa nakusudia kauli yake Mwenyezi Mungu isemayo, "Wala hatabeba mbebaji mzigo wa mwingine". Qur'an, 35:18. Basi kuna maana gani ya kumuadhibu maiti kutokana na watu wengine kumlilia!! Shafii amesema: Na hadithi aliyoipokea Aisha toka kwa mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** (Itatajwa baadaye) inaaminika kwamba ni hadithi iliyosemwa na Mtume **[s.a.w.w]** (Kuliko hadithi zilizotajwa na Umar na Abdallah) na dalili yetu ni Qur'an na Sunnah. Na iwapo itasemwa iko wapi dalili ya Qur'an, patasemwa, ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo "Wala Hatabeba mbebaji mzigo wa mwingine" na ile isemayo: "Na kwamba hatapata mtu isipokuwa yale aliyoyafanya" Qur'an, 53:39.

Na kauli yake isemayo:

فَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ ﴿٧﴾ وَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ﴿٨﴾

"Basi anayefanya wema (hata) wa kiasi cha mdudu chungu atauona na anayefanya uovu (hata) wa kiasi cha mdudu chungu atauona". Qur'an, 99: 7-8.

Na kauli yake isemayo: "Ili kila nafsi ilipwe kwa yale iliyoyafanya" Qur'an, 20:15. Na iwapo itasemwa iko wapi dalili ya Sunnah? Patasemwa, "Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimwambia mtu fulani "Huyu ni mwanao"? Akasema "Ndiyo" "Hakika yeye hatafanya makosa kwa ajili yako, wala hutafanya makosa kwa ajili yake". Basi Mtume akamjulisha kama alivyomjulisha Mwenyezi Mungu kwamba kila kosa Ia mtu ni lake

1. Al-Istiab: Tarjuma ya Abdallah, Juz. 1, uk. 368, Al-Ghadir, Juz. 3, uk. 165-167.
2. AI-Istiab katika Tarjuma ya Nuuman, Juz. 1, uk. 297, Al-Iqd Al-Farid cha Ibn Abdi Rabih Al- Undulus, Juz. 3, uk. 235.
3. Tarikh Tabari, Juz. 2, Uk. 253.
4. Iq-dul-Far, Juz. 3, uk. 235.

mwenyewe kama ambavyo amali yake siyo ya mwingine wala dhidi yake.[1] Ufahamisho wa hadithi: Yote tuliyonakili yanatujulisha kwamba makusudio ya hadithi inayosema kwamba, "Hakika maiti anaadhibiwa kwa kumlilia walio hai" (Kama Sanadi yake itasihi) sicho kinachofahamika kutokana na dhahir yake, na hadithi ilikuwa na qarina kujulisha maana yake lakini zilianguka wakati wa kunakili. Na kwa ajili hiyo baadhi ya watu wamedhania kuwa ni haramu kumlilia maiti kwa kutegemea hadithi hii hali ya kuwa wameghafilika na lengo Ia hadithi na maana yake.

Amepokea Umrah, kwamba yeye alimsikia Aisha (r.a) wakati alipoambiwa kwamba Abdallah Ibn Umar anasema: Maiti huadhibiwa kwa ajili ya kilio cha walio hai, basi Aisha R.A. akasema: "Amma yeye hajasema uongo (kwa makusudi) lakini amekosea au amesahau, hakika mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipita kwenye mazishi ya Myahudi ambaye jamaa zake walikuwa wanamlilia akasema: "Hakika wao wanamlilia naye anaadhibiwa kaburini mwake."[2] Na imepokewa toka kwa Ur-wa naye toka kwa Abdallah bin Umar amesema: "Amesema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** hakika maiti huadhibiwa kwa ajili ya kilio cha watu wake juu yake basi Ur-wa akamtajia Aisha hadithi hii akasema hali akimkusudia Ibn Umari: "Kwa hakika Mtume **[s.a.w.w]** alipita kwenye kaburi la Myahudi akasema, hakika mwenye kaburi hili anaadhibiwa na hali ya kuwa watu wake wanamlilia kisha akasoma, "Na wala hatabeba mbebaji mzigo wa mwingine".[3] Huu ndiyo ufahamisho wa hadithi na maana yake na hawezi kutia shaka katika kusihi maana hii mtu mwenye utambuzi na maarifa ya Qur'an na hadithi. Na kuna Riwaya nyingine zinazojulisha kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** alimkemea Umar kutokana na kuwakataza kwake wanawake waliokuwa wakiwalilia maiti.

Imepokewa toka kwa Ibn Abbas amesema: "Alipofariki Zainab binti ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.w.t]** Mtume **[s.a.w.w]** alisema, mfuatishieni kwa Salaf wetu mwema (aliyetangulia) Uthman Ibn Madh-un, basi wanawake wakalia, Umar akawa anawapiga kwa fimbo yake, mjumbe wa Mwenyezi Mungu akaushika mkono wake akasema, tulia Ewe Umar, waache walie na Ole wenu! na maombolezo ya shetani". Hadi akasema. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikaa ukingoni mwa kaburi na Fatmah akiwa pembeni mwake analia, basi Mtume **[s.a.w.w]** akawa anayapangusa macho ya Fatmah kwa nguo yake kwa kumuonea huruma".[4] Na Al-Bayhaqi ameandika ndani ya Sunan Al-Kubra hadithi kama hiyo kuhusu kufariki kwa Ruqaiyyah binti ya mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Na mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** alisema: "Wacha Ewe Umar" Kisha akasema: "Ole wenu! na maomboleza ya shetani, kwani chochote kiwacho kutoka jichoni na moyoni ni miongoni mwa huruma na kiwacho kutoka ulimini na mkononi kinatokana na shetani".[5] Na katika Riwaya nyingine: Mjumbe wa

1. Ikhtilaful-Hadithi katika Hashiya ya kitabu Al-ummu cha Shafii, Juz. 7, uk. 267.
2. 1, uk. 96, Sahih Muslim Juz. 1, uk. 344, Sunan Nasai, Juz. 4, uk. 17, Sunan Bayhaqi, Juz. 4, uk. 72.
3. Sunan Abi Dawood, Juz. 2, uk. 59, Sunan Nasai, Juz. 2, uk. 17.
4. Sunan Abi Dawood, Juz. 2, uk. 59, Sunan Nasai, Juz. 2, uk. 17.
5. Musnad Ahmad, Juz. 1, uk. 235-237. Mustadrak ya Al-Hakim, Juz. 1, uk. 191. Na amesema Adhahabi ndani ya Tal-Khisul-Mustadrak: Sanad yake ni nzuri.

Mwenyezi Mungu akasema: "Ewe Umar waache kwani jicho linalia na moyo unapata huzuni na ni hivi punde tu msiba umetufika".[1] Hiki ndicho tulichokinakili kutoka katika riwaya nyingi, kitamjulisha msomaji Mtukufu hukmu ya Kiislamu katika Mas-ala ya kumlilia maiti sawa sawa maiti akiwa ni jamaa na ni kipenzi au akawa ni rafiki mpenzi, basi iwapo itajuzu kuwalilia hao basi kumlilia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** na watu wa nyumba yake waliotakasika na Masahaba wake wema ni awla kujuzu.

Kwa nini isiwe na hali yakuwa riwaya nyingi zimekuja kuhusu jambo hili kutoka kwa makundi mawili Shia na Sunni zinazohusu kumlilia Mtume **[s.a.w.w]** na misiba ya watu wa nyumba yake, hatukulenga kuzitaja kwa, kufupisha maelezo na atakae kufahamu arejee kitabu kiitwacho, "Siratuna Wa Sunnatuna Siratun-Nabiyyi Wa Sunnatuh" cha mwanachuoni mkubwa Sheikh Abdul-Husain Al-Amini (r.a) Japokuwa tuliyoyataja katika kurasa hizi yanaambatana na yale aliyoyahakiki mwanachoni huyo katika mlango huu (Mwenyezi Mungu amrehemu).

Pili: Kudhifia tamko la "Abdi" (lenye maana ya mja au mtumwa) kwa kiumbe: Kwa hakika imekuwa ni jambo mashuhuri kwa wapenzi wa Ahlul Bayt [a.s] kuwaita watoto wao (majina ya) "Abdur-Rasul" na "Abduali" na "Abdul-Husein".... na mfano kama huo, yaani kudhifia neno "Abdi" kwenye majina ya (Ahlul-Bayt) [a.s]. Na kuita majina (kwa namna hii) kumezusha wasi wasi ndani ya baadhi ya makundi na hasa Mawahabi, hali yakuwa wanadai kwamba kuita jina (namna) hii ni aina ya shirki na wala hakuafikiani na misingi ya Tauhidi. Na kuna kikao huko Syria kilichotukutanisha mimi na Sheikh Nasirudin Al-Abani ambaye ni msahihishaji na ni mhakiki na baadhi ya vitabu vya hadithi, basi niliiona kwake chuki kubwa kutamkwa jina la Abdul-Husein, na hali hiyo (Ilitokea) pale yalipokuja mazungumzo kumhusu Al-Allamah AI-Hujjah As-Sayyid Abdul-Husein Sharafud-din Al-Amili ambaye ndiye mwandishi wa Al-Murajaat (Mwenyezi Mungu aitakase roho yake).

Na kwa ajili ya kuondoa utata mbele ya ukweli, sisi tunasimama kutatua Mas-ala haya kwa mtazamo wa Qur'an na Sunna, na tunasema: "Ubudiyyah, hutumika na kukusudiwa kutokana nayo (maana zifuatazo):

**Kwanza**: Maana inayokabili uungu, nalo kwa maana hii linajulisha kwamba mtu huyo au watu wote ni milki ya Mwenyezi Mungu katika asili ya kuumbwa, na mwenye kumiliki ni yeye Mwenyezi Mungu, nawe unafahamu kwamba mtu ni mtumwa wa Mwenyezi Mungu na ndiye Bwana wake, na chanzo cha mambo haya mawili ni kuwa Mwenyezi Mungu ndiye aliyemuumba baada ya kuwa hakuwepo naye ndiye mwenye kumpa kila kitu kinachomuhusu. Kwa hiyo basi Ubudiyyah kwa maana hii ni asili ya kila kilichopo, na ni asili ya kila kitu na kamwe hakiepukani na maana hiyo inayokusudiwa na kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukafu isemayo:

إِن كُلُّ مَن فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ إِلَّا آتِي الرَّحْمَـٰنِ عَبْدًا ﴿٩٣﴾

1. As-Sunan Al-Kubra, Juz. 4, uk. 70.

"Hapana yeyote aliyeko mbinguni na ardhini ispokuwa atafika kwa (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa Rehma hali ya kuwa ni mtumwa "Abdi". Quran, 19:93.

Kama ambavyo kauli ya masihi (Isa bin Mariyam) [a.s] inavyoashiria akasema:

قَالَ إِنِّي عَبْدُ اللَّـهِ آتَانِيَ الْكِتَابَ وَجَعَلَنِي نَبِيًّا ﴿٣٠﴾

"Hakika mimi ni Abdullahi (Mtumwa wa Mwenyezi Mungu) amenipa kitabu na amenifanya kuwa ni Nabii". Qur'an, 19:30.

Na aya nyinginezo. Na Idhafa ya Abdi kwa maana hii haiwezekani ila kwa Mwenyezi Mungu tu.

**Pili**: Ubudiyyah hutumika na kukusudiwa kutokana nayo utiifu au maana inayokaribiana na hiyo, na kwa hakika wameifafanua maana hii waandishi wa kamusi za lugha. Amesema ndani ya "Lisanul-Arabi": At-Taabudu (Maana yake ni) At-Tanasuku (kufanya ibada.), Al-Ibada (maana yake) "At-Taa" (utufii). Na amesema ndani ya "Al- Qamusul-Muhit": "Wal-Abdiyah, Wal-Ubudiyyah, Wal-Ubudah, Wal Ibadah, (Maana yake ni) At-Taa (yaani utiifu)". Na kwa msingi huu basi, makusudio ya "Abdur-Rasuli, Abdu Ali na.... "Ni Mwenye kumtii Mtume na mwenye kumtii Ali. Na "Makusudio haya" yako wazi, basi kwa nini isiwe hivyo na Mwenyezi Mungu ametuamuru kuwatii wao akasema:

أَطِيعُوا اللَّـهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنكُمْ ﴿٥٩﴾

"Mtiini Mwenyezi Mungu na mumtii Mtume na wenye mamlaka miongoni mwenu". Qur'an, 4:59.

Basi Qur'an imetambulisha kuwa Mtume ni mwenye kutiiwa na Waislamu ni wenye kutii, na halaumiwi mtu kuidhihirisha maana hii kwa kuwaita wanawe na awapendao (kwa majina hayo). Naam, ndani ya hadithi ya Abu Hurairah (imesemwa) "Asiseme mmoja wenu kumwambia aliyemmiliki "Abdii" Wa "Amatti" Yaani mtumwa wangu na mjakazi wangu, na aseme kijana wangu" (Lakini) Ibnul Athir ndani ya kitabu chake kiitwacho, "An Nihayah" ameitolea dosari hadithi hii kwa kauli yake aliposema: "Hadithi hii ni kwa maana ya kupinga kuwafanyia ujeuri juu yao na kuwanasibishia utumwa kwa maana ile ya kwanza. Kwani mwenye kustahiki hilo ni Mwenyezi Mungu Mtukufu naye ndiyo mlezi wa waja wote".[1] Na hadithi hii kwa dhahiri yake inakwenda kinyume na Qur'an Tukufu, vipi itakuwa wakati yeye Mwenyezi Mungu ndiye aliyewanasibishia "Ubudiyyah" kwa watu wanaowamiliki. Akasema Mwenyezi Mungu:

وَأَنكِحُوا الْأَيَامَىٰ مِنكُمْ وَالصَّالِحِينَ مِنْ عِبَادِكُمْ وَإِمَائِكُمْ ۚ إِن يَكُونُوا فُقَرَاءَ يُغْنِهِمُ اللَّـهُ مِن فَضْلِهِ ۗ وَاللَّـهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٣٢﴾

"Waozeni wajane miongoni mwenu na waliowema katika watumwa wenu (Ibadikum) na wajakazi wenu (Imaikum) na wakiwa mafakiri Mwenyezi Mungu atawatajirisha katika fadhila zake na Mwenyezi Mungu ni mwenye wasaa mwenye kujua". Qur'an, 24:32.

1. An-Nihayah cha Ibnul-Athir, Juz. 3, uk. 170.

Utaona kwamba Mwenyezi Mungu anaunasibisha Ubudiyah (utumwa) na Imaiyah (Ujakazi) kwa wale wanaowamiliki, na lau ndani ya Taabiri (Hii) kungekuwa na kitu fulani (kinachoonyesha) kiburi kwa mtumwa, basi Mwenyezi Mungu asingelitumia Taabiri hii. Kisha ni kwamba msingi wa Shubha hii ni kuwa, wenye kuwa na mushkeli (wa jambo hili) hawatofautishi baina Ubudiyyah Tak-winiyyah Al-haqiqiyyah ambayo haiepukani na mtu tangu mwanzo wa kupatikana kwake mpaka kwenye siku zake za mwisho, na baina ya milki yenye kajitokeza (isiyokuwa ya asili) kwa mtu kufuatia hali na masharti (yanayohusika) basi hapo bwana huwa mtumwa na mtumwa huwa bwana na hakimu. Hii ndiyo Fiqh ya Kiislamu inayojulisha kuwafanya mateka wa vita wanaume na wanawake kuwa watumwa. Amesema Ibn Quddamah ndani ya Kitabu chake kiitwacho, "Al-Mugni": "Pindi Imam anapowateka mateka, basi anahiyarishwa, akiona kuwa (inafaa) kuwaua (atawaua), na akiona awasamehe bila ya badali (ya kiti chochote atawasamehe), na akiona atawaachia kwa (badali ya) mali atakayoichukua toka kwao (atawaachia) na akiona (inafaa) atakubali fidia. Na akiona kuwa inafaa kuwafanya watumwa ni bora, (basi atafanya analoona kuwa linafaa kati ya hayo)".

Kwa hiyo ndani ya vitabu vya Fiqhi kuna mlango mpana unaohusu hukmu za watumwa na wajakazi, hivyo wanazo hukmu maalum anazifahamu yule aliye mtaalamu wa Fiqhi ya Kiislamu. Basi hulitumia tamko Ia "Maula" kwa yule Bwana anayewamiliki watumwa kwa kuwateka (vitani) au kwa kuwanunua, kama ambavyo hulitumia tamko la "Abdi" na "Amah" (mtumwa na mjakazi) juu ya mateka ambao hakimu ameona kuwa inafaa kuwafanya mateka, na hapana mwanachuoni yeyote miongoni mwa Mafaqihi aliyeona ubaya wa kutumia jina hili mtumwa au mjakazi. Na miongoni mwa mambo yanayostaajabisha ni kauli ya Muhammad Abdul-Wahabi isemayo kuwa: "Yeyote mwenye kumwambia mtu fulani, Maulana au Sayyidina basi mtu huyo ni kafiri".[1][289] Wakati ambapo Qur'an Tukufu inalitumia tamko la Sayyid kwa mwingine asiyekuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mwenyezi Mungu amesema: "....Mwenye kusadikisha kwa neno litokalo kwa Mwenyezi Mungu na atakayaekuwa "Sayyid" (Bwana) na mtawa". Qur'an, 3:39.

Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na akairarua kanzu yake kwa nyuma na akawakuta Sayyid wake mlangoni". Qur'an, 12:25. Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na watasema Mola wetu hakika tuliwatii Masayyid wetu na wakubwa zetu basi wao wametupoteza njia". Qur'an, 33:67. Zaidi ya hayo kuna riwaya nyingi Mutawatiri (zimekuja) katika matumizi ya "Sayyid" kwa Mtume na kwa Hasan na Husein[2] [a.s] kiasi kwamba hapana yeyote mwenye kutia shaka katika kusihi kwake. Na kwa hakika Abubakr alimuomboleza Mtume Mtukufu kwa beti ambazo mwanzoni mwake (alisema:). "Ewe Jicho lia wala usichoke na haki ya kumlilia iko juu ya Sayyid, Mlilieni yule ambaye alikuwa mlinzi wetu kwenye mabalaa, na sasa amezikwa kaburini". Naam, Suyuti ameleta

1. Kashful-Irtiyabi cha Sayyid Muhsin al-Amin: Amenakili toka katika Khul-Satul-Kalam.

2. Kinachokusudiwa ni ile hadithi isemayo Hasan na Husain ni Masayyid wa vijana wa peponi.

(masimulizi) ndani ya Al-Jamius-Saghir toka kwa Daylami ndani ya Musnad ya Al-Fir-Dausi toka kwa Ali [a.s] kwamba: "As-Sayyid ni Mwenyezi Mungu". Kama alivyoleta (masimulizi) AI-Azizi ndani ya Sharhul-Jamii As-Saghir kutoka Musnad ya Abi Dawood kwamba, ulikuja ujumbe wa Bani Amir kwa Mtume **[s.a.w.w]** wakasema: "Wewe ni Sayyid wetu", Mtume akasema, "Sayyid ni Mwenyezi Mungu". Basi lau hadithi hizi mbili zitasihi itabidi zichukuliwe kwenye maana ya hakika ya "As-Sayyid" yaani "Mwenye kumiliki na muumba" kwani As-Sayyid kwa maana hii inamuhusu Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kwa nini isisihi wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alilitumia neno Sayyid kwa Saad Ibn Maadh R.A. Tabari amesimulia kama ifuatavyo: "Alipotokea Saad, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu **[s.a.w.w]** alisema: "Simameni kwa ajili ya Sayyid Yenu"[1] Makatazo haya yaliyokuja hapa kuhusu neno Sayyid yatachukuliwa kwa makusudio ya maana inayokanusha Tauhidi ya Mwenyezi Mungu pindi ikitumika kwa maana ya mwenye kumiliki na kuamba. Naapa kwamba, ukweli uko wazi hauhitaji maelezo marefu, itakuwaje hali hii wakati ambapo maneno ya Waarabu na Mtume na Masahaba na Tabiina na Maimamu wa nyumba ya Mtume na Mafaqihi wa umma, yamejaa kwa matumizi ya maneno haya kuhusu asiyekuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na hapana yeyote aliyeona ubaya wa kayatumia kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na waliyachunguza mas-ala haya kwa upana na mtazamo wa undani na hawakuwatia Waislamu katika dhiki na shida na walifahamu kwamba sheria ya Kiislamu ni nyepesi inafuata makusudio na malengo siyo dhahiri (yake) na matamko (yalivyo). Basi Mawahabi ni kama Makhawariji, waliyadhiki mambo juu ya nafsi zao na juu ya Waislamu kwa vitu ambavyo Mwenyezi Mungu hakuviwekea vikwazo na makundi mawili haya yanaafikiana katika Mas-ala mengi bega kwa bega.

Khitamuhu Misk: Ewe msomaji mpendwa, sasa hivi umefika wakati wakuhitimisha uchambuzi huu mpana kuhusu itikadi za Kiwahabi na misingi yake na malengo yake kwa neno fupi lenye manufaa kwa jamii ya Kiislamu kwa jumla, na kwa vijana wa Kiislamu wenye ghera kwa upande wao. Bila shaka Uislamu umejengwa juu ya maneno mawili: Kalimatul-Tauhid na Tauhid-ul-Kalimah, basi ni wajibu juu ya umma wa Kiislamu kuulinda umoja wa kalima na mshikamano wa udugu, kama ambavyo ni wajibu juu ya umma kuihifadhi Kalimatul-Tauhid kwani viwili hivyo ni matawi mawili yanayotokana na asili moja. Basi kama ambavyo Qur'an na Sunna vimehimiza juu ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu kwa dhati na kwa vitendo na ibada, basi ndivyo hivyo hivyo vimehimiza kushikamana na kamba ya Mwenyezi Mungu na vimekemea mafarakano:

﴿وَاعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّـهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا ﴿١٠٣

"Shikamaneno katika kamba ya Mwenyezi Mungu na wala musifarakane". Qur'an, 3:103.

Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na atakayemuasi Mtume baada ya kumdhihirikia uongofu na akafuata njia ya wasiokuwa waumini,

1. Tabari, Juz. 2, uk. 249.

tutamgeuza alikogeukia na tutamuingiza ndani ya Jahannam na hayo ni marejeo mabaya".

Qur'an, 4:115. Na amesema Imam Ali [a.s] "Basi shikamaneni na Jamaa kubwa kwani mkono (msaada) wa Mwenyezi Mungu uko pamoja na wengi, na Ole wenu na mafarakano kwani hakika wenye kukhalifa miongoni mwa watu ni (kundi la) shetani kama ambavyo wenye kujitenga miongoni mwa kondoo ni kwa ajili ya mbwa mwitu, basi fahamuni ya kwamba mwenye kulingania kwenye utengano huu muueni japokuwa atakuwa chini ya kilemba changu hiki."[1] Basi iwapo Tauhidul-Kalimah iko katika daraja hii ya juu, basi itakuwaje hali ya mtu anayevunja mshikamano wa Waislamu na kueneza ndani yao utengano na kubomoa umoja wao na kuyavuruga maafikiano yao kwa kupandikiza mbegu ya mashaka ndani ya mambo ambayo umma wa Kiislamu ulikuwa ukiafikiana kabla (hata) ya kuzaliwa (huyu) aliyepandikiza mashaka yaani Ibn Taymiyyah na aliyeimwagilia mbegu hiyo yaani Ibn Abdul-Wahab. Ewe msomaji mpendwa: Kwa hakika yote tuliyokueleza ndani ya kurasa hizi ni kwa mujibu wa Qur'an Tukufu na Sunna ya Mtume Mtukufu **[s.a.w.w]** na ni matokeo ya kile ambacho umma wa Kiislamu umekubaliana kwa karne zote. Basi lina thamani gani neno au maneno yanayopinga kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume wake **[s.a.w.w]** na kile ambacho umma umekubaliana?

Ni jambo zito kwa umma wa Kiislamu ukiongozwa na Wanachuoni wake na wanafikia wake kupatikana ndani ya Makka na mahala paliposhuka wahyi watu wanaoukufurisha umma wote wa Kisunni na Kishia na wala hawamvui miongoni mwao isipokuwa watu wachache toka miji ya Najd. Na kwa hakika wakubwa watukufu wa umma wa Kiislamu walikwishahadharisha hatari ya msimamo huo na madhara ya fikra za kishetani ambazo alizipandikiza Sheikh Ibn Taymiyyah mpaka Al-Hafidh Ibn Hajar amesema ndani ya kitabu chake kiitwacho, "Al-Fatawa AI-Hadithiyyah" kumuhusu Ibn Taymiyyah kama ifuatavyo: "Ibn Taimiyya ni mja ambaye Mwenyezi Mungu amemdhalilisha, na amemuacha apotee naakampofua na kumfanya kiziwi, na wameyabainisha mambo haya yakawa wazi Maimamu ambao walieleza ufisadi wa hali yake na uongo wa kauli zake, na mwenye kutaka (kujua) ni juu yake kutalii (kusoma) maneno ya Imam Al-Muj-Tahid Abul-Hasan As-Subaki ambaye Uimamu wake na utukufu wake na kufikia kwake daraja ya Ij-Tihadi kumekubaliwa na wote na pia asome maneno ya) mwanawe (aliyekuwa akiitwa) At-Taaj na Sheikh Al-Imam Al-Izz miongoni mwa jamaa na watu wa zama zao miongoni mwa Mashafii na Malik na Mahanafii, na huyu Ibn Taymiyyah hakuishia kuwapinga Masufi wa zama zake bali amewataaradhi watu kama vile Umar Ibn Khataab na Ali Ibn Abi Talib R.A. Kilichopo ni kwamba maneno yake hayana maana na ni yakutupwa njiani. Na inaitakidiwa kwamba yeye ni mzushi mpotovu mwenye kupotosha amevuka mpaka, Mwenyezi Mungu amlipe kwa mujibu wa uadilifu wake".[2]

Na tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie "Miongoni mwa wenye kusikiliza maneno na wakafuata mema yake". Rehma na Amani Zimshukie

1. Nahjul-Balagha Khutba Na. 123.
2. Al-Fatawa Al-Hadithiyyah, uk. 86.

Bwana wetu Muhammad Mwisho wa Mitume na Aali Zake wema waliotakasika na Sahaba Zake Wema Watukufu. Na Maombi yetu ya mwisho ni kuwa kila sifa njema zinamstahaki Mwenyezi Mungu Mola wa Walimwengu.

Jaafar Sub-Hani,
Qum Takatifu,
Siku ya Idi ya Ghadir,
18 Mfunguo Tatu 1406.

## SHARTI YA KUCHAPA

Sharti ya kuchapa au kusambaza ni kutaja rejeo hili. haki zote zimehifadhiwa na Taasisi ya Al-Hasanain Taasisi ya Imamu Husein (a.s)

Site ya Al-Imaamaini Al-Hassanaini (a.s) ya usambazaji wa utamaduni wa Kiislamu na mafunzo ya Kidini.

## MWISHO WA KITABU

## YALIYOMO

**1** ..................................... **UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
1 .................... KIMEANDIKWA NA SHEIKH JA'FAR SUBHANI
1 ..... KIMETAFSIRIWA NA MUSABBAH SHAABANI MAPINDA
1 ...................................................................... MUHTASARI
**3** ..................................... **UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
3 ............................ UTANGULIZI WA CHAPA YA KWANZA
3 ......................... KUHUSU MAWAHABI NA ITIKADI ZAO
MAWAHABI NA MSIMAMO WAO KWA UNDANI KATIKA
4 ........................................ QADHIYYAH ZA TAUHID
WANACHUONI WA KIWAHABI WANAJIPENDEKEZA KWA
6 ...................................................................... WATAWALA
6 ...... MAPINDUZI YA KIISLAMU NA HUJUMA ZA KIWAHABI
**8** ..................................... **UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
8 .................................. UTANGULIZI WA CHAPA YA PILl
HAJA YA KUWEKO MKUTANO WA KIISLAMU WA
8 .......... ULIMWENGU ILI KUIDURUSU TAUHIDI NA SHIRKI
12 ................ NENO "SHIRKI" LITAKUKUTA KILA UPANDE
13 ................... MAKOSA KATIKA VITABU VYA MASUNNI
14 ....................... UCHACHE WA KUFIKIRI KWA UNDANI
**18** .................................... **UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
18 .......................................... KIASI CHENYE MAKOSA
18 ..... MWITO WA KUFANYIKA KONGAMANO LA KIISLAMU
19 ........................................ LENGO LA KITABU HIKI
20 .. VIDOKEZO JUU YA MAISHA YA MUASISI WA UWAHABI
**27** .................................... **UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
27 ...................................... IBNU TAYMIYYAH NI NANI?
MAWAHABI NA QADHIA YA KUJENGEA MAKABURI YA
30 ...................................................................... MAWALII
A: MTAZAMO WA QUR'AN KATIKA KUJENGA JUU YA
32 ...................................................................... MAKABURI
1). KUJENGA JUU YA MAKABURI YA MAWALII NA
33 KUVIHESHIMU VITU VITUKUFU VYA MWENYEZI MUNGU
35 .................................. 2. KUWAPENDA AL-QURBAA
35 . 3. KUJENGEA MAKABURI KATIKA NYUMATI LILIZOPITA
36 ............................ 4. RUHUSA YA NYUMBA MAALUM
B: UMMA WA KIISLAMU NA KUJENGA JUU YA MAKABURI
38 ......................................................................

**40** .................................... **UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
KUMBUKUMBU ZA KIISLAMU NI DALILI YA KUENDELEZA
40 ................................................................ DINI
43 .................... JAWABU LA WANACHUONI WA MADINA
43 ................................ C. HADITHI YA ABUL-HAYYAJ
44 .............................................. KUIJADILI HADITHI
44 ................................ UFAFANUZI WA MAMBO HAYA
46 ....................................... MWELEKEO WA KWANZA
46 ................................................ MUELEKO WA PILI
48 ................ UWEZEKANO WA MAANA MBILI MWISHONI
49 .......................................... D. HADITHI YA JABIR
51 ................ DALILI ZA UDHAIFU NDANI YA HADITHI HII
**55** .................................... **UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
55 ................. KUTOLEA USHAHIDI HADITHI ZINGINE MBILI
56 . KUPINGANA KWA SERA YA WAISLAMU NA MAWAHABI
57 ............. KUZUA DALILI POTOFU KWA KUKWEPA KOSA
59 KUJENGA MSIKITI KARIBU NA MAKABURI MATAKATIFU
DALILI ZA MAWAHABI KATIKA KUHARAMISHA KUJENGA
61 ........ MISIKITI KARIBU YA MAKABURI YA WATU WEMA
61 ....................... KUZIHAKIKI MAANA ZA HADITHI HIZI
**67** .................................... **UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
67 .KUZURU MAKABURI KWA MUJIBU WA QUR'AN NA SUNNA
67 ............................................ KUZURU MAKABURI
68 .............................. QUR'AN NA KUZURU MAKABURI
HADITHI TUKUFU ZA MTUME [s.a.w.w] NA KUZURU
69 ....................................................... MAKABURI
71 ........................ WANAWAKE NA KUZURU MAKABURI
**74** .................................... **UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
MATOKEO MAZURI YANAYOPATIKANA KUTOKANA NA
74 ........................ KUWAZURU WATU MUHIMU WA KIDINI
75 ..................... KUZURU KABURI LA MTUKUFU MTUME
75 .......................................... USHAHIDI WA QUR'AN
77 ................................................ DALILI NYINGINE
HADITHI TUKUFU JUU YA KUZURU KABURI LA MTUME
78 ........................................................... [s.a.w.w]
DALILI ZA MAWAHABI KATIKA KUHARAMISHA SAFARI ZA
79 ............................................ KUZURU MAKABURI
**83** .................................... **UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**

KUSWALI NA KUOMBA DUA KWENYE MAKABURI YA
83 ........................................................... MAWALII
86 ................................ KUWASHA TAA MAKABURINI
87 .. KUTAWAS-SAL KWA MAWALII WA MWENYEZI MUNGU
87 ........................ HADITHI TUKUFU ZA MTUME [s.a.w.w]
88 .......................................... HADITHI YA KWANZA
88 ................. MAELEZO JUU YA SANAD YA HADITHI HII
89 ............................................ FUNGU LA KWANZA
89 ................................................... FUNGU LA PILl
89 ................................................ FUNGU LA TATU
90 .................................................. FUNGU LA NNE
HADITHI YA PILl KUTAWAS-SAL KWA HAKI YA WAOMBAJI
90 ..........................................................
HADITHI YA TATU KUTAWAS-SAL KWA HAKI YA MTUME
90 ............................................... MTUKUFU [s.a.w.w]
91 ........................... MAONI YETU JUU YA HADITHI HII
**93 ................................... UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
HADITHI YA NNE MTUME KUTAWAS-SAL KWA HAKI YAKE
93 .................... NAHAKI YA MANABII WALIOMTANGULIA
HADITHI YA TANO, KUTAWAS-SAL KWA MTUME
93 .................................................... MWENYEWE
HADITHI YA SITA VILE VILE INAHUSU KUTAWAS-SAL KWA
94 ........................................................... MTUME
95 .............................. MIFANO VA DUA ZA TAWAS-SUL
95 ........ MWENENDO WA WAISLAMU KATIKA TAWAS-SUL
6. USHAIRI WA SAFIYYAH AKIOMBOLEZA KIFO CHA
98 ................................................ MTUME [s.a.w.w]
BAADHI YA MAANDIKO YALIYOANDIKWA KUHUSU
99 ....................................................... TAWAS-SUL
**101 ................................ UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
101 ................ KUWAWEKEA NADHIRI WATU WALIOKUFA
101 ...................................... THAWABU ZA NADHIRI
KUADHIMISHA KUZALIWA KWA MAWALII WA MWENYEZI
105 .................................... MUNGU NA KUFA KWAO
106 ...... QUR'AN NA KUWATUKUZA MANABII NA MAWALII
110 MANENO NA MATENDO VA MAWAHABI YANAPINGANA
**112 ................................ UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
KUTABARUKU KWA ATHARI ZA MAWALLI WA MWENYEZI
112 ................................ MUNGU NA KUOMBA UPONYO

113 .......... MTAZAMO WA QUR'AN JUU YA KUTABARUKU
113 .................. KUTABARUKU NA SERA YA WAISLAMU
117 .................................... TAUHIDI KATIKA IBADA
118 .................. TAARIFU KAMILI YA MAANA YA IBADA
119 ............... TAARIFU MBILI PUNGUFU KUHUSU IBADA
123 ............................... TAARIFU YA TATU YA IBADA
**127 ................................ UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
127 ............................................ NATIJA YA UTAFITI
130 .............. NI KIPI KITENDO CHA MWENYEZI MUNGU?
131 ........................ MANENO YA AL-QUDHAI AL-MISRI
**138 ................................ UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
KUOMBA MSAADA KWA MAWALII WA MWENYEZI MUNGU
138 ............................................ KATIKA UHAI WAO
**146 ................................ UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
KUOMBA MSAADA KWA KUPITIA ROHO ZA MAWALII WA
146 ............................................ MWENYEZI MUNGU
MTU ANAPOKUFA HAINA MAANA KUWANDIYO
146 ....................................... AMETOWEKA KABISA
147 .......................... QUR'AN NA KUBAKIA KWA ROHO
148 ........................ UHAKIKA WA MTU NI ROHO YAKE
149 ........................... MAWASILIANO NA ULIMWENGU
1). NABII SALEHE [a.s] ALIZISEMESHA ROHO ZA WATU WA
149 ............................................... QAUMU YAKE
2) NABII SHUAIBU [a.s] ALIZISEMESHA ROHO ZA WATU
150 ........................................................... WAKE
3) MTUME MUHAMMAD [s.a.w.w] PAMOJA NA MANABII
151 ......................................................... WENGINE
151 .................... 4) SALAMU ZA QUR'AN KWA MANABII
MAAMKIZI KWA MTUME [s.a.w.w] MWISHONI MWA SWALA
151 ..............................................................
153 ................................ MATOKEO YA UCHUNGUZI
153 . WAISLAMU NA KUZIOMBA MSAADA ROHO TAKATIFU
**157 ................................ UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
KUTAKA UOMBEZI TOKA KWA MAWALII WA MWENYEZI
157 ............................................................ MUNGU
157 ......................... MAANA YA SHAFAA (KUSHUFAIA)
DALILI ZINAZORUHUSU KUOMBA SHAFAA HAPA DUNIANI
158 ..............................................................

158 .................... 1). KUOMBA SHAFAA NI KUOMBA DUA
160 2). QUR'AN NA KUOMBA DUA TOKA KWA WATU WEMA
161 ........ 3).HADITHI ZA MTUME NA SERA YA MASAHABA
162 .................... 4). KUOMBA SHAFAA BAADA YA KUFA
DALILI ZA MAWAHABI ZA KUHARAMISHA KUOMBA
162 ........................................................ SHAFAA
1) WANASEMA: "KUOMBA SHAFAA NI KUMSHIRIKISHA
162 .......................................... MWENYEZI MUNGU"
163 .......... 2) WASHIRIKINA NA UOMBEZI WA MASANAMU
164 ................................... JAWABU LA MADAI HAYO
3).KUTAKA HAJA KWA ASIYEKUWA MWENYEZI MUNGU NI
165 ...................................................... HARAMU
4). SHAFAA NI HAKI INAYOMUHUSU MWENYEZI MUNGU TU
166 ...........................................................
167 .............5). UPUUZI WA KUTAKA SHAFAA KWA MAITI
**170** .................................. **UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
KUITAKIDI UWEZO WA GHAIB WA MAWALII WA MWENYEZI
170 ............................................................ MUNGU
170 ......................................... MAONI YA KIWAHABI
171 .......................MAONI YETU JUU YAMANENO HAYA
171 ................... 1). UWEZO WA SIRI WA NABII YUSUF [a.s]
171 .................... 2). UWEZO WA SIRI WA NABII MUSA [a.s]
172 .............. 3). UWEZO WA SIRI WA NABII SULEIMAN [a.s]
173 ........................ 4). NABII ISA [a.s] NA UWEZO WA SIRI
BASI NINI UFUMBUZI WAKE NA NI IPI KAULI ILIYO SAWA
174 ...........................................................
175 ........... KUWAOMBA MAWALII MATENDO YA GHAIBU
NABII SULEIMAN [a.s] ANAOMBA (KULETEWA) KITI CHA BIL-
175 .............................................................. QIIS
176 ...................................... KHULASA YA MAELEZO
178 ...............SHIRKI NA JINSI WASEMAVYO MUUTAZILA
**179** .................................. **UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
179 . KUMUAPA MWENYEZI MUNGU KWA HAKI YA MAWALII
179KUMUAPA MWENYEZI MUNGU KWA HAKI YA MAWALII
AMIRUL-MU'MINIINA (ALI [a.s] NA KUMUAPA MWENYEZI
180 ............................ MUNGU KWA HAKI YA MAWALII
181 ........KUTHIBITI KWA KIAPO HIKI NDANI YA UISLAMU
182 .......... DALILI ZA MAWAHABI JUU YA KUHARAMISHA

185KUMUAPIA ASIYEKUWA MWENYEZI MUNGU MTUKUFU
DALILI ZINAZORUHUSU KUMUAPIA ASIYEKUWA
185 ........................................ MWENYEZI MUNGU
KUAPA KWA ASIYEKUWA MWENYEZI MUNGU KATIKA
187 ...................................... MADHEHEBU MANNE
**192** .................................. **UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
192 KUWAOMBA MSAADA MAWALII WA MWENYEZI MUNGU
197HIJJA - MSIMU WA IBADA NA NI MKUTANO WA KISIASA
**208** .................................. **UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
208 ........................................ NINI LENGO LA HIJJA?
MAKUSUDIO YA HIJJA KIJAMII NA KISIASA NDANI YA
209 ....................................................... QUR'AN
MALENGO YA HIJJA YA KIJAMII NA KISIASA KATIKA
216 ..................................................... SUNNAH
MALENGO YA HIJJA YA KISIASA NA YA KIJAMII KATIKA
219 ............................................. SERA YA SALAFU
**221** .................................. **UCHUNGUZI JUU YA UWAHABI**
MALENGO YA HIJJA YA KISIASA NA KIJAMII KATIKA KAULI
221 ................................................ ZA WANACHUONI
223 .................................. UCHAMBUZI WA MWISHO
233 ...................................... SHARTI YA KUCHAPA
233 ...................................... MWISHO WA KITABU
234 .................................................... YALIYOMO